# Maswali & Majibu

## kuhusu Sheria za Tanzania

FAyaz A. Bhojani
Gaudiosus Ishengoma

Toleo la 2

FB Attorneys

# MASWALI NA MAJIBU

## Sheria za Tanzania

Toleo la 2

FAyaz A. Bhojani (Wakili)
BCom (McGill), LLB (London), LLM (Berkeley)

Gaudiosus Ishengoma (Wakili)
LLB (UDSM)

Toleo la 2 liliandaliwa na kuchapishwa katika lugha ya Kiingereza (Questions and Answers on Tanzanian Law) mnamo mwaka 2019. Chapisho hili la Kiswahili linatokana na tafsiri ya Toleo hilo la Kiingereza iliyofanywa na Bw. Jaba Tumaini Shadrack (UDSM), na kuhaririwa na Dk. Laurean Mussa (UDSM) akisaidiana na Bw. Rwekamwa Andrea Rweikiza (Wakili, FB Attorneys).

Dar es Salaam • Tanzania

Q&A with FB Attorneys

Hairuhusiwi kunakili, kuhifadhi, kuchapisha kwa njia ya kielektroniki au mekaniki, kutoa vivuli (kudurufu), kurekodi au kubadili sehemu yeyote ya kitabu hiki kwa njia, namna au mfumo wowote bila idhini ya maandishi kutoka FB Attorneys. Maswali yoyote juu ya kitabu hiki yatumwe FB Attorneys kwenye barua pepe: info@fbattorneys.co.tz

**Angalizo:** Maelezo yaliyomo katika kitabu hiki yanalenga kutoa mtazamo wa jumla wa kisheria. Sio mbadala wa mshauri wako wa masuala ya kisheria. Ikiwa una changamoto za kisheria, tunakusihi sana uwasiliane na mwanasheria wako. Tafadhali kumbuka na zingatia kuwa, sheria ambazo ndio msingi wa majibu na hoja zetu hapa zinaweza kuwa zimebadilika kitambo.

Toleo la 2.
Kimechapishwa na Kusanifiwa katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
ISBN 978-9976-5241-2-3

Kwa mama yangu Zainul, na baba yangu Amir.
*FAyaz A. Bhojani*

Kwa binti yangu Highness Ikamikile.
*Gaudiosus Ishengoma*

# Dibaji

Karibu kwenye toleo la pili la 'Maswali & Majibu na FB Attorneys' (Maswali na Majibu Kuhusu Sheria za Tanzania).

Safu ya Maswali & Majibu na FB Attorneys ilichapishwa kwa mara ya kwanza mwaka 2009 katika gazeti la Daily News, na kuifanya kuwa safu ya kwanza ya maswali na majibu ya kisheria katika ukanda wa Afrika Mashariki. Kutokana na kupokelewa vyema na mrejesho chanya wa Toleo la 1, FB Attorneys tumeamua kuandaa Toleo la 2, ambalo linajumuisha maswali na majibu kutoka mwaka 2012 hadi 2014 juu ya Sheria za Tanzania na kimataifa. Kitabu hiki ni mwongozo muhimu kwa wasomaji wa kawaida, wanafunzi, walimu, wanasheria na umma kwa ujumla. Toleo la pili lina Sura 14 na linajumuisha mada za ziada kama vile Migogoro ya Biashara, Sheria ya Uhamiaji, Mali isiyohamishika, Sheria ya Madini, Uhalifu wa Kibiashara, Sheria ya Mazingira, Sheria ya Ushuru na Mamlaka ya Mapato Tanzania.

Kitabu kina lengo la kuwafikia wasomaji kutoka kila nyanja ya maisha na kuelimisha umma juu ya sheria na madhara ya kuvunja sheria. Sheria inaweza kuchanganya, kukatisha tamaa na wakati mwingine inaweza hata isiwe upande wako, lakini utaratibu ni kwamba inapaswa kufuatwa. Kitabu hiki kitakuelimisha juu ya sheria, haki zako na mambo yote unayopaswa kufanya au kutokufanya. Pamoja na kujibu maswali mazito juu ya sheria, kitabu hiki kina ucheshi ndani yake na hivyo kufanya safu/makala hizi zinazochapishwa kila wiki kuwa ni somo zuri la Jumatatu asubuhi huku ukiwa na kikombe cha kahawa pembeni.

Tunapenda kutoa shukrani zetu za dhati kwa Daily News, gazeti la Kiingereza linaloongoza nchini Tanzania, ambalo linachapisha safu ya Maswali & Majibu kila Jumatatu (www.dailynews.co.tz). Kumekuwa na ushirikiano bora kati ya Daily News na FB Attorneys.

Tunatumaini utafurahia kusoma kitabu hiki.

# FB Attorneys

FB Attorneys ni kampuni ya kisheria iliyopo jijini Dar es Salaam na yenye uzoefu limbikizi wa zaidi ya miaka sabini (70) katika ukanda wa Afrika Mashariki. Tunashughulikia masuala yote ya kisheria na tumebobea zaidi katika Mambo ya Mashirika na Biashara ikiwa ni pamoja na Madini, Mafuta na Gesi, Kodi, Kesi za Madai, Mabenki, Ushindani, Mali zisizohamishika, Sheria ya Haki Miliki na Sheria ya Ardhi, miongoni mwa mambo mengine mengi.

Tunaheshimiwa sana kwenye ukanda wetu na kimataifa. Sifa yetu imejengwa na umahiri wetu katika kushughulikia kwa mafanikio changamoto ngumu za kibiashara ambazo zinahitaji mbinu na ufanisi wa hali ya juu. Hutegemewa mara nyingi na wateja kama chaguo namba moja miongoni mwa makampuni ya kisheria katika kesi za madai, FB Attorneys hutoa ushauri wa kisheria wa kipekee katika masuala mbalimbali ya makampuni na ya kibiashara.

FB Attorneys tuna mahusiano ya muda mrefu na baadhi ya taasisi mashuhuri za kifedha, mashirika ya Serikali, asasi za kiraia, na sekta nyingine maarufu za umma na binafsi katika ukanda wa Afrika Mashariki.

FB Attorneys wanajivunia kuwa mwanachama wa LEX Africa ambao ni ushirika wa kampuni kubwa za kisheria barani Afrika ambazo zimekuwa zikitoa huduma bora kwa zaidi ya miaka 20. Ushirika huu ulianzishwa mnamo mwaka 1993 na kuwa ushirika wa kwanza wa kisheria unaolenga Afrika tu.

# Kuhusu Waandishi

FAyaz A. Bhojani, *Wakili.*
BCom (McGill), LLB (London), LLM (Berkeley)

FAyaz Bhojani ni Mbia Mwendeshaji wa kampuni mwenye miaka 20 ya ujuzi katika masuala ya sheria za kampuni na msimamiaji mwenza wa idara ya kesi. FAyaz ni mhitimu wa Shule maarufu ya Sheria ya Berkeley, katika Chuo Kikuu cha California, inayoheshimika sana duniani. Katika Shahada ya kwanza, FAyaz alisomea Sayansi ya Takwimu-Bima chini ya Taasisi ya Wataalam wa Takwimu-Bima (Society of Actuaries - SOA), na hivyo kumjengea ujuzi thabiti wa hisabati.

Baada ya kuwa mshauri katika baadhi ya makampuni makubwa ya kimataifa, FAyaz hutumia uzoefu huo wa kibiashara katika shughuli zake za kisheria na ameshiriki na kufanikisha majadiliano mbalimbali ya mikataba mikubwa ya kibiashara katika sekta ya uchimbaji (madini, mafuta na gesi). Utaalamu wake unajumuisha sekta muhimu za uchumi kama vile huduma za kifedha, mawasiliano, nishati, madini, kodi, ushindani wa kibiashara, na Uunganishaji na Ununuzi Mashirika. Anafahamika kwa uwezo wake wa kutatua masuala magumu/tata ya kibiashara na migogoro ambayo inahitaji umakini mkubwa. Ni mbia ambaye anasimamia na kushiriki katika majadiliano na kuandaa nyaraka za wateja, na mara zote huorodheshwa na Chamber & Partners, IFLR 1000 na Legal 500 miongoni mwa wanasheria nguli na mahiri nchini Tanzania.

Gaudiosus Ishengoma, *Wakili.*
LLB (UDSM)

Baada ya kufanya kazi kama Mwanasheria wa Serikali kwa miaka minane, Ishengoma anaongoza Idara ya Mashtaka Mahakamani na ana uzoefu mkubwa katika kusimamia migogoro nyeti na masuala yote ya usuluhishi. Katika kazi zake za kisheria kwa muda wa miaka ishirini na sita (26), amesimamia kesi ngumu na sehemu kubwa ya migogoro mbalimbali ya kibiashara katika nyanja kama vile ardhi, sekta ya uchimbaji (madini, mafuta na gesi), fedha/mabenki, mawasiliano, ushindani wa kibiashara na mikataba.

Amehusika katika kesi kubwa zilizofunguliwa Mahakama Kuu ya Tanzania (Kitengo cha Ardhi na Kitengo cha Biashara), na Mahakama ya Rufaa na kuwa na rekodi nzuri katika ufuatiliaji wa madeni ya benki. Ishengoma alifundishwa mbinu za uendeshaji mashtaka na Baraza la Uingereza (British Council) chini ya timu ya wataalamu kutoka Bunge la Mabwanyenye (House of Lords) na ana uzoefu mkubwa kuhusu masuala ya ushindani wa kibiashara, migogoro ya wanahisa/wabia, rufaa za kodi pia jinai ya kampuni (uhalifu wa kibiashara). Ameorodheshwa na Chamber & Partners, IFLR 1000 na Legal 500 miongoni mwa wanasheria nguli na mahiri nchini Tanzania.

# Yaliyomo


Migogoro ya Kibiashara dhidi ya Viongozi wa Serikali ..... 1

Watoto, Mahusiano, Sheria za Ndoa na Talaka ..... 15

Sheria za Biashara, Migogoro ya Kibiashara na Haki Miliki ..... 39

Haki za Walaji ..... 59

Sheria za Makampuni na Kibenki, Migogoro ya Wanahisa/Wabia ..... 89

Sheria za Madini, Biashara na Uwekezaji wa Kimataifa ..... 105

Migogoro baina ya Watu Binafsi ..... 117

Sheria za Ajira na Uhamiaji ..... 125

Sheria za Mazingira na Urithi wa Mali za Kale ..... 149

Wanasheria, Tafsiri ya Sheria na Taratibu za Kimahakama ..... 157

Utakatishaji Fedha na Jinai ya Kampuni ..... 185

Hati ya Uwakilishi, Kifo, Mirathi na Wosia ..... 197

Sheria za Majengo, Ardhi na Mipango Miji ..... 203

Sheria ya Kodi na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ..... 211

# Migogoro ya Kibiashara dhidi ya Viongozi wa Serikali

"

Kila siku, na nchini kote, wafanyabiashara huwa na muingiliano na maafisa wengi wa serikali. Ingawa muingiliano huo mara nyingi huwa ni wenye tija na kiungwana, siyo mara zote huwa hivyo. Wakati mwingine maafisa wa serikali hutumia madaraka yao vibaya na hivyo kukiuka sheria. Hakika, siyo maafisa wa serikali pekee, hata Mawaziri huweza kuvunja sheria.

Katika sura hii, tunatoa mifano kadhaa inayoonesha namna ambavyo maafisa wa serikali wanapitiliza na kuvunja sheria, na namna ambayo wafanyabiashara wanaweza kudai haki zao. Vilevile tunatoa mifano mahususi kuhusiana na idara ya uhamiaji ambapo maafisa wa serikali wanatekeleza majukumu yao kwa mujibu wa sheria ingawa hatua hizo huwa ni kero kwa wafanyabiashara.

Sura hii pia inajumuisha mifano ya wahalifu wanaojifanya ni maafisa wa serikali au hata polisi (vishoka/matapeli) ili kupata taarifa na kuingia mahala pa biashara. Tunawashauri wenye kampuni kuchukua tahadhari na kuwakabili "maafisa" wanaowatilia mashaka.

## Mamlaka ya maafisa uhamiaji

**Mimi ni mfanyabiashara Jijini Dar es Salaam ambaye nina wafanyakazi wa ndani na nje ya nchi. Kuna tukio lilitokea ambalo liliathiri sana hadhi yangu na biashara kwa ujumla. Maafisa Uhamiaji walivamia ofisi yangu mchana kweupe, wakaigeuza ofisi yangu juu chini, wakatuweka chini ya ulinzi, wakiwemo wateja wangu, huku wakizuia mtu yeyote kuingia wala kutoka. Hawakuwa na hati za upekuzi wala hawakutoa taarifa. Walinivamia kama wao ndiyo wamiliki wa ofisi na wakaondoka na nyaraka za siri. Wana mamlaka ya kufanya hivyo? Mamlaka ya Maafisa Uhamiaji ni yapi?**

*23 Januari 2012*

Sheria za uhamiaji Tanzania zinaeleza kazi na mamlaka ya maafisa uhamiaji kwa ujumla. Sheria ya Uhamiaji inasema maafisa uhamiaji wana mamlaka ya kuingia jengo lolote kwa muda unaofaa na kukagua jengo hilo bila kuwa na hati ya upekuzi. Wana mamlaka ya kuchukua nyaraka zinazohusiana na masuala ya uhamiaji ikiwemo kuzidai kutoka kwa mtu ambaye wanaemuona ni mhamiaji, na ndiyo maana inashauriwa wale wenye vibali vya kazi wabebe vibali vyao vilivyothibitishwa.

Maafisa Uhamiaji pia wana mamlaka ya kumkamata mtu ambaye hana nyaraka zinazompa uhalali wa kukaa Tanzania. Na kama wakimkamata wanatakiwa wampeleke kwa hakimu aliyepo kwenye Mahakama yoyote iliyo karibu haraka iwezekanavyo. Hata hivyo, kisheria hawatakiwi kutumia nguvu kubwa kufanikisha hilo. Labda kama kuna mtu ameumizwa kutokana na matumizi ya nguvu iliyopitiliza au amekamatwa bila kufikishwa Mahakamani haraka iwezekanavyo, au walikuja muda usio muafaka, vinginevyo sheria inawaruhusu kufanya hivyo walivyofanya walipokuja ofisini kwako.

Yote kwa yote, ni lazima watende kwa kuzingatia utu wa kila mtu. Kwa upande wako, inaonesha unalalamikia sana namna ambavyo walikushtukiza na walivyowafanyia wafanyakazi wako. Unaweza kutoa taarifa kwa Mkurugenzi wa Uhamiaji kuhusu kuvunjiwa heshima na yeye anaweza kulifanyia uchunguzi tukio hilo.

Sehemu ya mwisho ya swali lako ni kuhusu mamlaka ya jumla ya maafisa uhamiaji. Kwa ajili hiyo, Tunanakili baadhi ya vifungu muhimu vya sheria kwa ajili ya rejea yako. Sheria inatamka kwamba afisa uhamiaji yeyote anaweza (a) kumhoji au kukagua pasipoti ya mtu yeyote anayetaka kuingia au kuondoka nchini Tanzania au mtu yeyote ambaye ataona ana sababu za msingi za kuamini kuwa ni mhamiaji haramu, na pale anapokuwa na sababu za msingi za kuamini kwamba vifungu vya sheria hii au kanuni zilizotungwa chini ya sheria hii zinavunjwa, anaweza kumhoji au kukagua pasipoti ya mtu yeyote ambaye anaamini kwamba anaweza kutoa maelezo kuhusu uvunjifu huo; (b) kumtaka mtu yeyote aliyeingia au anayetaka kuingia au kuondoka Tanzania kujaza au kusaini fomu yoyote ya kukubali kufanyiwa uchunguzi wa kitabibu; (c) kumtaka muongoza meli, rubani, dereva wa gari moshi au gari anayeingia au kutoka nje ya Tanzania kutoa nakala mbili za majina zilizosainiwa naye, wakala wake au mtu yeyote aliyeruhusiwa kufanya hivyo kwa niaba yake majina ya watu wote wa kwenye meli, ndege, gari moshi au gari na kumpatia maelezo yoyote ya ziada kama yatahitajika (d) kama ana sababu za msingi kuhisi kwamba mtu yeyote anakiuka vifungu vya sheria hii au kanuni zake au uwepo wa mhamiaji haramu nchini Tanzania na kama anaona ili kuhakikisha haki inatendeka ni lazima mtu huyo akamatwe anaweza kumkamata mtu huyo bila hati ya ukamataji na kumpeleka kwa hakimu haraka iwezekanavyo (e) kumtaka mtu kutoa uthibitisho au ushahidi wa maandishi au wa mdomo ambao anaona

ni muhimu ili kuthibitisha maelezo yoyote ya maandishi au mdomo yaliyotolewa kwa ajili ya kuomba kibali, pasi ya kusafiria au ruhusa nyingine ambazo zinatolewa chini ya vifungu vya sheria hii (f) kuingia kwenye jengo lolote kwa muda unaofaa na kufanya upekuzi wa jambo linalohusiana na uhamiaji na (g) kumtaka mtu yeyote kumpatia waraka ambao mtu huyo amebeba.

Kwa ajili ya kutekeleza kazi zilizoainishwa kwenye sheria hii, afisa uhamiaji anaweza, bila kuwa na hati ya upekuzi, kusimamisha, kuingia na kukagua ndani ya ndege, treni, gari, chombo, meli, jengo, ardhi, ghala, kontena, boti yoyote iliyopo nchini.

Kwa maelezo hayo, unaweza kuona kuwa mamlaka ya maafisa uhamiaji ni makubwa. Hata hivyo, ni kawaida kwao kutumia vibaya mamlaka hayo. Kwa mfano, wanaweza tu kuchukua nyaraka zinazohusiana na uhamiaji na siyo vinginevyo.

Ni lazima uelewe kwamba Idara ya Uhamiaji ina kazi kubwa ya kuweka mlinganyo/usawa ili kuhakikisha kwamba Watanzania wanapata ajira zisizohitaji ubobevu na wataalamu kutoka nje. Nchi zote zina sera za namna hiyo ili kulinda ajira za watu wake. Lakini pia kuna makampuni ambayo hayafuati sheria ambapo husababisha makampuni ambayo yanafuata sheria kuvamiwa. Hata hivyo, tunakiri kuwa baadhi ya makampuni hayafanyi kazi kwa kufuata sheria.

## Mahakamani kwa kushindwa kulipa ushuru wa taka

**Ofisi yangu ipo katikati ya jiji la Dar es Salaam ambapo kwa miaka mingi nimekuwa nikilipa Shilingi 7,500 kwa mwezi kama ushuru wa kukusanya taka. Miezi michache iliyopita wazoa taka walinidai Shilingi 150,000. Nilikataa kulipa kiasi kilichoongezeka na wao walikataa kuchukua kiasi nilichokuwa nalipa awali. Kwa sasa nimeletewa wito wa kwenda Mahakamani. Nifanye nini?**

*6 Februari 2012*

Ingawa ushuru wa taka unaonekana kama siyo jambo kubwa, kutokulipa ushuru huo ni kosa la jinai. Viwango vya malipo ya ushuru wa kukusanya taka vimeainishwa kwenye Sheria Ndogo za Makusanyo na Utupaji Taka za mwaka 1994 ambapo Nyongeza "C" inahusu swali lako.

Chini ya sheri hizo, viwango vya malipo vimeainishwa kulingana na idadi ya waajiriwa ulionao. Kwa mfano, biashara yenye waajiriwa kati ya 76 hadi 100 inatakiwa kulipa Shilingi 150,000; hiyo Shilingi 7,500 ni kwa biashara yenye waajiriwa 6 hadi 10. Tunaamini una utetezi mzuri, kama idadi ya wafanyakazi wako haijaongezeka.

Katika hatua nyingine, kama tahadhari tu, unashauriwa kwenda Mahakamani na watu wawili ambao wanaweza kukuwekea dhamana kama itahitajika.

## Mhariri wa gazeti ameshtakiwa kwa uchochezi

**Ninafanya kazi kama Mhariri Msaidizi kwenye mojawapo ya magazeti Tanzania. Kutokana na uhariri fulani ambao uliichefua Serikali nimeshtakiwa kwa uchochezi Mahakamani. Ni kweli niliandika chapisho/makala husika lakini ninaamini nilichoandika na sielewi kwa nini nikamatwe kwa kutoa maoni yangu. Kwani wahariri si hawabanwi na kanuni ya kuzingatia 'ulali/ulinganifu wa habari' kwa kuwa nilikuwa tu natoa maoni yangu. Nifanye nini?**

*2 Aprili 2012*

Umeshtakiwa kwa mujibu wa Kanuni ya Adhabu, ambayo ni sheria ya jinai Tanzania. Kifungu cha 55 (1) cha Kanuni ya Adhabu kinaelezea nia ya kufanya uchochezi kuwa ni nia ya (a) kuleta chuki au kudharau au kuchochea hali ya kutopendwa kwa mamlaka

halali ya Jamhuri ya Muungano au Serikali yake; au (b) kuhamasisha wakazi wowote wa Jamhuri ya Muungano ili kuleta mageuzi, kwa njia isiyo halali, juu ya jambo lolote lililowekwa na sheria katika Jamhuri ya Muungano; au (c) kuleta chuki au kudharau au hamasa ovu ya kuwafanya watu watende kinyume na utawala wa sheria katika Jamhuri ya Muungano; au (d) kupandisha hali ya kutoridhika au kudharau baina ya wakazi wa Jamhuri ya Muungano; au (e) kukuza hisia za nia mbaya na chuki baina ya aina mbali mbali za watu wa Jamhuri ya Muungano.

Kifungu kidogo cha (2) cha Kanuni ya Adhabu kinaeleza kwamba kitendo, hotuba au tangazo halitahesabiwa kuwa ni la kichochezi kwa sababu tu linalenga katika (a) kuonesha kwamba Serikali imepotoka au imekosea katika mwenendo wake wowote; au (b) kuonyesha makosa au mapungufu katika Serikali au Katiba ya Jamhuri ya Muungano au kama ilivyowekwa na sheria, au katika usimamiaji utoaji wa haki kwa lengo la kurekebisha makosa hayo au upungufu huo; au (c) kuwashawishi wakati wowote wakazi wa Jamhuri ya Muungano kujaribu kwa njia ya halali kuleta mageuzi/mabadiliko ya jambo lolote katika Jamhuri ya Muungano kama ilivyowekwa na sheria; au (d) kuonyesha, kwa nia ya kuyaondoa, mambo yoyote yanayoleta au yenye mwelekeo wa kujenga hisia za nia mbaya na uadui baina ya aina mbalimbali za watu wa Jamhuri ya Muungano. Kifungu kidogo cha (3) kinasema katika kuamua endapo nia ya kitendo chochote kilifanywa au inayohusishwa na kitendo ilikuwa ya, maneno yoyote yatakayozungumzwa au nyaraka yoyote itakayoandikwa itahesabiwa kuwa ni ya uchochezi, na mtu yeyote atahesabiwa kuwa alinuia matokeo ambayo kwa hali ya kawaida yanatokana na kitendo chake kwa wakati na katika hali aliyoitenda mwenyewe.

Una imani isiyo sahihi kuwa uhariri unaweza kuandikwa tu vyovyote. Si hivyo. Maoni ya mhariri yanaweza kuwa ni ya uchochezi. Ni kweli Katiba inakupa uhuru wa kujieleza, lakini uhuru huo ni lazima uwe ndani ya mipaka. Mwanasheria wako anaweza kukuongoza zaidi.

## Taarifa katika tovuti za Serikali zimepitwa na wakati

**Mimi ni mshauri kutoka nje, nimegundua kuwa mara nyingi tarrifa zilizo katika tovuti za idara za Serikali, wizara na pia bunge ama hazijasahihishwa ama zina taarifa ambazo ni za zamani sana, hazihusiani na uhalisia na siyo sahihi. Nikupe mfano wa tovuti moja ambayo bado inasema Rais ni Benjamin Mkapa. Tovuti za Serikali bado zina majina ya wizara za zamani. Mbaya zaidi baadhi ya tovuti bado zina sheria za zamani na zingine hata hazifunguki. Je, hakuna sheria ya tovuti ambayo inaharamisha kuweka taarifa za zamani? Huu ni mwaka 2012, uzembe wa namna hiyo unapaswa kupingwa kwa kuwa kuhudumia tovuti hakuhitaji bajeti kubwa zaidi ya nia tu. Je, suala hili linawezaje kutatuliwa? Je, kama nilitumia taarifa za kwenye mojawapo ya tofauti hizi, ninaweza kuishtaki idara husika?**

*9 Julai 2012*

Kwa bahati mbaya hatujui sheria yoyote inayoweka kosa kama hilo. Hata hivyo, kanuni za utawala bora na hekima vinazilazimu idara, wizara, au wakala za serikali kuhuisha tovuti zao angalau kila siku au kila wiki. Kwa kuwa unaonekana kufahamu idadi ya tovuti hizo, ni vyema ukaziandikia kuwaeleza kuhusu upungufu huu.

Upande wa pili wa swali lako hatuwezi kulijibu bila kwanza kujua ulizitegemeaje taarifa hizo na vyanzo gani vingine ulikuwa navyo kabla ya kuzitegemea taarifa hizo. Hata hivyo, kwa kawaida dai lako haliwezi kufanikiwa ikiwa ulikuwa na uelewa kama ulivyoonesha kwamba tovuti hizo

hazijasahihishwa. Kama hivyo ndivyo, hatuamini kama unaweza kufanikiwa. Wanasheria wako wanaweza kukuongoza baada ya kuwaeleza kila kitu.

## Mfamasia mmoja sehemu mbili za kazi

**Mimi ni Mfamasia ninayeendesha maduka mawili ya dawa ambapo nimeweka sifa zangu. Nina wasaidizi sehemu zote mbili lakini muda mwingi nautumia kwenye duka kubwa. Wakaguzi walikuja kwenye duka dogo na hawakunikuta. Kwa sasa nimeshtakiwa na kamati ya nidhamu kwa utovu wa maadili ya kazi kwa kumruhusu mtu asiye na sifa kutoa huduma kinyume na Sheria ya Famasia. Je, nimevunja sheria? Niendeshaje biashara yangu?**

*17 Septemba 2012*

Swali lako linaashiria jibu. Kama Mfamasia unaelewa wazi kwamba huwezi kuonesha vyeti vyako kwenye duka moja la dawa na kufanya kazi kwenye duka jingine. Ni kweli kwamba hii ndiyo hali halisi mitaani kwa sasa lakini tumearifiwa kwamba tabia hii inashughulikiwa. Mfamasia ni mtaalam anayetoa dawa za matibabu. Matibabu yasiyo sahihi yanaweza kupelekea kifo. Unatakiwa kuzingatia kazi yako kwa umakini mkubwa na utii Sheria ya Famasia ambayo inakutaka ufanye kazi sehemu moja tu unayoweka cheti chako cha usajili. Tunakushauri uache kufanya kazi sehemu mbili na uheshimu sheria.

## Zabuni ya chini na bado si mshindi

**Niliingia kwenye mchakato wa zabuni kubwa ya ujenzi wa barabara. Uzabuni wangu ulikuwa ni wa chini na bado sikupewa kazi. Baada ya kufuatilia niliambiwa kwamba wenzangu walikuwa na uzabuni bora zaidi. Je, sikustahili kupewa kazi?**

*17 Desemba 2012*

Hivi sasa, zabuni zinasimamiwa na Sheria ya Manunuzi ya Umma ya 2004 ambayo pia ina kanuni zake. Taarifa muhimu sana kwako ni kwamba bei siyo kigezo pekee kinachoamua bali mambo mengine pia huzingatiwa.

Sheria ya Manunuzi ya Umma inaanzisha nadharia ya "bei ya makadirio ya chini" ambayo ina maana ya bei inayotolewa na muuzaji, mjenzi au mshauri ambayo itaonekana kuwa ni ya chini zaidi baada ya kuzingatia mambo mengine yote husika na baada ya mahesabu mengine kwa kuzingatia mambo hayo, isipokuwa kwamba mambo hayo ni lazima yawe yameelezwa kwenye nyaraka za zabuni.

Baadhi ya zabuni zina gharama za ufundi na gharama za kifedha ambapo asilimia fulani inatolewa kwenye maeneo yote mawili na wastani wake unaunda bei ya makadirio ya chini. Kama haujaridhika na kutokuchaguliwa, una haki ya kukata rufaa kwenda kwenye taasisi ya manunuzi na baadaye kwenye Mamlaka ya Rufaa za Zabuni ambayo hivi karibuni imebatilisha zabuni nyingi ambazo zimefanyika bila kufuata taratibu. Mwanasheria wako anaweza kuangalia njia hii na kukuongoza zaidi.

## Sheria ya ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi

**Nimesikia kuhusu Sheria ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi na kwamba makampuni binafsi yatakuwa yanawatoza wananchi fedha kwa matumizi ya miundo mbinu ya umma ikiwemo barabara. Inawezekanaje Serikali kuuza barabara zetu? Tafadhali nieleze kama nimeelewa vibaya.**

*24 Desemba 2012*

Sheria ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi itaisaidia Serikali na sekta binafsi kufanya kazi kwa pamoja kwa faida ya jamii

nzima. Serikali ya Tanzania inakusudia kufanya vitu vingi sana kwa ajili ya kuiendeleza nchi, yaani kujenga barabara, hospitali, vyuo n.k. Hata hivyo, siyo siri kwamba Serikali haina pesa za kutosha kugharamia miradi hiyo mingi kwa haraka. Sheria hii inakusudia kuzishirikisha sekta binafsi na makampuni yenye uwezo wa kifedha kujenga miundo mbinu hiyo na kurejesha faida pamoja na gharama zao za ujenzi kwa kipindi fulani na baadaye miundo mbinu hiyo inarudi na kuwa mali ya Serikali. Ni kweli itahusisha wanachi kulipa kiasi fulani cha pesa kwa ajili ya matumizi ya miundo mbinu hiyo lakini ni kwa maendeleo ya nchi. Sheria kama hizi zipo kwenye nchi nyingi ambapo sekta binafsi imekuwa mstari wa mbele kwenye miradi hiyo. Umeelewa vibaya Serikali haiuzi nchi bali inafanya kazi ili kuleta maendeleo ya haraka.

## Usajili wa waongoza watalii

**Nimekua kwenye kijiji kimoja kilichopo chini ya Mlima Kilimanjaro. Tangu enzi na enzi, familia yetu imekuwa ikijipatia kipato kwa shughuli za kuongoza watalii. Kwa kipindi chote hicho hatujawahi kuingiliwa na mtu yeyote na kazi hii tumeirithi kutoka vizazi vingi vilivyopita. Hivi karibuni, kaka yangu mkubwa alikamatwa kwa kuongoza watalii bila kusajiliwa. Tulifanikisha kuachiwa kwake kwa sababu tulikuwa tunajuana na mkubwa fulani. Ninashangaa kwa nini sheria inatulazimisha kujisajili. Tumefanya kazi hii kwa miaka mingi sasa na wengi wetu hatuna sifa za kufanya kazi nyingine. Je, sababu za kukamatwa kaka yangu zilikuwa ni sawa? Tafadhali nisaidie.**

*31 Desemba 2012*

Kwanza kabisa tunataka kukueleza kwamba kila mwongoza watalii anatakiwa kusajiliwa kwa mujibu wa maelekezo ya Sheria ya Utalii Na. 29 ya 2008. Mtu anayekiuka sheria hii anatenda kosa na akikutwa na hatia atawajibika kwa faini isiyopungua milioni moja au kifungo kisichozidi miezi sita au vyote kwa pamoja.

Sheria ya Utalii pia imeweka sifa ambazo ni lazima mtu awe nazo ili aweze kusajiliwa kama muongoza watalii. Sifa hizo ni pamoja na umri angalau miaka 21, elimu ya angalau kidato cha nne, uwe na cheti cha huduma ya kwanza, ujuzi wa kutosha wa eneo husika na uelewa wa kutosha wa kazi yenyewe pamoja na kuwa na sifa nyingine ambazo waziri wa utalii atazibainisha kwenye Gazeti la Serikali.

Kwa kuwa kaka yako anafanya kazi ya kuongoza watalii kwa kukiuka sheria, kukamatwa kwake kulikuwa ni halali. Suala kwamba kujuana kwenu na mkubwa fulani kulisaidia kuachiwa kwake kunaweza kusiwasaidie huko mbeleni kama mtaendelea kufanya kazi ya kuongoza watalii bila kusajiliwa.

Mwisho, hata kama tungewaonea huruma kiasi gani kwamba sheria haijazingatia uzoefu wenu wa toka enzi kwenye suala la kuongoza watalii, bado tunapendekeza kufuata masharti yaliyowekwa na Sheria ya Utalii kwa kuwa ni sheria na ni lazima tuifuate. Vinginevyo, unaweza kushawishi sheria ifanyiwe mabadiliko kwa kumwandikia barua waziri wa utalii ili mahitaji yako yaingizwe kwenye marekebisho ya sheria.

## Kukataa kutoa nyaraka za mapato kwa afisa kazi

**Mimi ni mwanamke mfanyabiashara, kwa sasa nimefungua ofisi zangu hapa jijini Mwanza. Biashara yangu kuu ni uingizaji na uuzaji bidhaa kutoka China. Nimeajiri Watanzania saba kama wasaidizi wangu. Hivi karibuni mtu ambaye alijitambulisha kama afisa kazi alikuja ofisini kwangu na kuomba vitabu na nyaraka mbalimbali. Alisema alikuja hapo ili kuhakikisha kwamba tunafuata sheria za kazi. Nilimpa nyaraka alizohitaji lakini nilikataa kumpa**

**vitabu vinavyoonesha mapato ya biashara. Alisema atanichukulia hatua za kisheria. Je, sheria inasemaje?**

*28 Januari 2013*

Chini ya Sheria ya Taasisi za Kazi, sheria namba 7 ya mwaka 2004, kwa madhumuni ya usimamizi wa sheria za kazi, afisa kazi anaweza, kwa muda wowote unaofaa kuingia eneo lolote akiwa na cheti/kitambulisho husika chenye kumhalalisha na kumtaka mtu yeyote mwenye udhibiti wa taarifa yoyote, kitabu, hati au kitu, kukitoa na kuelezea chochote kilichomo kwenye taarifa, kitabu, hati au kitu hicho. Mamlaka haya yametolewa chini ya Kifungu cha 45 cha Sheria ya Taasisi ya Kazi na kimeenda zaidi na kutamka kwamba anaweza kukamata, kutoa nakala ya taarifa yoyote, kitabu, nyaraka au kitu chochote halisia.

Hata hivyo kwa ufafanuzi, sheria ya Taasisi za Kazi imesisitiza kwamba taarifa yoyote, kitabu au hati, sampuli au kitu halisia kitatumika tu katika utekelezaji na usimamizi wa sheria ya kazi. Ikiwa madai ya afisa yalikuwa ya vitabu na taarifa ambazo hazihusiani na kazi, tunakubaliana kabisa na wewe kwamba ulikuwa sawa kukataa kutoa vitabu vya mapato kwa afisa kazi huyo. Hatuoni uhusiano wa vitabu vya mapato na utekelezaji na usimamizi wa sheria za ajira labda kama haujatuambia ukweli wote.

Hata kama ni kosa chini ya Sheria ya Taasisi za Kazi kukataa kutoa nyaraka inayotakiwa na afisa kazi, kifungu cha 49 cha sheria hiyo hiyo pia kinatamka kwamba haitakuwa kosa kukataa kujibu swali au kutoa taarifa yoyote, kitabu, nyaraka au kitu halisia ikiwa kuna sababu za kisheria za kutofanya hivyo. Hatuoni uwezekano wowote wa hatua za kisheria kuchukuliwa dhidi yako kwa sababu una sababu halali za kukataa kutoa vitabu vya mapato kwa afisa kazi. Mambo yangekuwa tofauti kama vitabu vingehitajika na viongozi wa Mamlaka ya Mapato ya Tanzania. Ikiwa una jina la afisa kazi, usione aibu kumripoti kwa Kamishna wa kazi. Wanasheria wako pia wanaweza kukuongoza zaidi.

## Maafisa wa Serikali wanachelewa wakati wote

**Nimekuja Tanzania mara tano katika miaka miwili iliyopita na kila wakati ninapokuja kuonana na Katibu Mkuu au Naibu Mawaziri tunajikuta tukisubiri kwa saa ili tuonane. Hawaombi msamaha na inanishangaza kwa nini hawawezi kusimamia muda wao vizuri. Upotevu huo wa muda unaipotezea nchi hii mamilioni ya Dola kila siku. Kama ikitokea mara moja au mbili inaweza kueleweka, lakini hili inaonekana kuwa ni hali ya kila siku. Hakuna afisa wa umma anaonekana kujali muda. Kampuni yetu imetumia maelfu ya Dola za ziada juu yangu kwa kuwa mara kwa mara nalazimika kuongeza muda wa kuendelea kukaa Tanzania. Hivi karibuni mmoja wetu alitakiwa kwenda Dodoma ili kukutana na Waziri fulani kufika kule akaambiwa na naibu wake kuwa usiku uliopita Waziri alikuwa amesafiri kurudi Dar kwa majukumu "ya kiofisi". Kutupigia simu tu ingetosha ili tuahirishe safari na hivyo kuokoa fedha tulizotumia kwenda Dodoma. Tafadhali niongoze juu ya nini cha kufanya. Je, hakuna mwongozo juu ya hili? Jinsi gani na ni nani anaweza kulitatua hili?**

*6 Mei 2013*

Idara ya Utumishi wa Umma ina kanuni zinazoitwa, Kanuni za Maadili ya Utendaji katika Utumishi wa Umma zilizotungwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma kwa mamlaka aliyopewa na Kifungu cha 34 cha Sheria ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2002 na Kanuni ya 65(1) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2003.

Kanuni hizi zinaeleza kwa uwazi mambo yafuatayo: kutoa huduma bora, kutumia

misingi ya haki badala ya upendeleo katika utoaji wa huduma, kutimiza wajibu kwa kufanya kazi kwa ufanisi kwa kiwango cha juu na kuzikamilisha katika muda unaotakiwa, isipokuwa kama imeruhusiwa vinginevyo, watumishi wa umma wanapaswa kuwa waaminifu na kutumia muda wao wa kazi kutekeleza wajibu wao. Hawaruhusiwi kutumia muda wa kazi kwa shughuli zao binafsi au kwa mapumziko isipokuwa kama wamepewa idhini ya kufanya hivyo.

Kutokana na maelezo hapo juu, unaweza kuona kwamba sheria inawataka maafisa wa Serikali kutekeleza majukumu yao kwa kiwango fulani na kuzingatia misingi ya haki. Hivyo kutokujali muda ni kuvunja sheria na unaweza ama kupeleka malalamiko rasmi kwa wakubwa zao ama kwa Waziri anayeshughulikia Menejimenti ya Utumishi wa Umma.

Tunakubaliana na wewe kwamba kutokujali muda au kutokusimamia muda ni tabia mbaya ambayo inafanywa na maafisa. Kimsingi, kwenye nchi nyingine kutunza muda kwao ni muhimu na hata uchelewaji wa dakika tano tu, mchelewaji hulazimika kuomba msamaha. Wanasheria wako wanaweza kukuongoza zaidi.

## Benki Kuu ya Tanzania kukataa jina letu

**Sisi ni benki yenye kusifika kimataifa na tumekuwa tukitumia jina letu ambalo pia lina neno "Central" ndani yake. Majadiliano yetu yasiyo rasmi na Benki Kuu yameonesha kwamba Benki hiyo haifurahii matumizi ya neno 'Central' kwa sababu wakati mwingine Benki Kuu ya Tanzania (BoT) inaitwa "Central Bank". Hata hivyo jina letu sio Benki Kuu lakini neno 'Central' lipo ndani yake na ni miongoni mwa maneno mengine. Tunawezaje kuishawishi Benki Kuu? Kwa nini Benki Kuu inakuwa kali sana kwenye suala hili?**

*10 Juni 2013*

Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania inatamka wazi kwamba isipokuwa kwa idhini ya maandishi ya Benki, hakuna benki itasajiliwa hapa nchini kwa masharti ya sheria yoyote, kwa jina ambalo linajumuisha maneno yoyote kati ya haya: "Central", "State", "Government" and "Reserve". Benki Kuu imefungwa na Sheria hii na hakuna uwezekano wa kuwakubalia kusajili benki yenye jina lililo na neno "Central" ndani yake. Benki Kuu siyo kali bali inajaribu kuhakikisha kwamba, miongoni mwa mambo mengine, hakuna mkanganyiko wa soko unatokea.

## Polisi bandia ofisini kwangu

**Sekretari wangu alinitaarifu kwamba kuna polisi wawili wamekuja kunihoji kuhusu tuhuma fulani. Nikiamini kuwa ni polisi kweli, niliwaruhusu kuingia na wakaanza kunitishia kuhusu kitu ambacho hata sikijui. Hata gari waliyokuja nayo ilikuwa na namba ya polisi. Sikujua kwamba watu hao walikuwa ni maafisa polisi ambao walifukuzwa kazi na sasa wanazunguka wakitapeli watu fedha kwa kujifanya kama bado wapo kazini. Je kuna sheria ya kuwaadhibu?**

*8 Julai 2013*

Chini ya Sheria ya Usalama wa Taifa hili ni kosa kubwa. Kifungu cha 6 cha Sheria hii kinatamka kwamba mtu yeyote ambaye, kwa malengo ya kuingia au kumsaidia mtu mwingine kuingia sehemu inayolindwa au kwa malengo mengine yanayohatarisha usalama au maslahi ya Jamhuri ya Muungano (a) bila mamlaka halali anatumia au anavaa sare za majeshi ya ulinzi au jeshi la polisi au sare nyingine rasmi ya Jamhuri ya Muungano au zinazofanana sana kiasi cha kuonekana kupotosha, au anajifanya kuwa ni mtu anayestahili kuvaa au kutumia sare hizo; (b) bila kibali halali anatumia gari ya Serikali au la ofisi yake, au gari yoyote ambayo kwa sababu

ya namba batili au sababu nyingine, au anajifanya kuwa ni mtu anayestahili kutumia gari hiyo anatenda kosa na akikutwa na hatia atawajibika kwa kifungo kisichozidi miaka 20. Nenda katoe taarifa polisi, kama hujafanya hivyo.

## Ubia na Wakala wa Serikali

**Tumeingia kwenye ubia na Wakala wa Serikali, ambao mtendaji wake mkuu yupo chini ya Wizara fulani. Ubia wetu upo kwenye changamoto za kifedha kutokana na kuongezeka kwa wazalishaji wa kigeni pamoja na kushuka kwa bei ya bidhaa tunazozalisha. Makadirio yetu ya faida hayajafikiwa na Waziri amesema kwamba anakusudia kuvunja ubia. Tumewekeza mamilioni ya Dola kwenye mradi na tumeshtushwa sana na kitisho hicho. Hata mtendaji mkuu wa Wakala ameguswa na anasema Waziri ana mamlaka mapana kisheria ya kutusitishia hata kama kuna kipengele kwenye mkataba wa ubia kinachotoa njia ya utatuzi wa mgogoro kwa njia ya usuluhishi. Tafadhali tuongoze kama kuna sheria hiyo ambayo inampa Waziri mamlaka makubwa namna hiyo.**

*29 Julai 2013*

Inakuwa ni vigumu sana kwetu kujibu swali hili bila kujua huo uwakala unaouzungumzia ni upi na ni Wizara gani ambayo Wakala ipo. Wakala zote za Serikali zinaanzishwa chini ya sheria fulani ambayo ndiyo huanisha mamlaka ya wakala na wakati mwingine mamlaka ya Wizara husika. Hivyo tunajibu swali hili kwa ujumla na tunashauri utafute ushauri maalum.

Kwa kuanzia, mkataba wa ubia unatakiwa kueleza haki na wajibu wa pande zote ikiwemo kipengele cha kuuvunja. Kutegemea na aina ya ukiukwaji, aina mbalimbali za kuvunja, kurekebisha, kuponya n.k. zitaelezwa. Hivyo Waziri anabanwa na mkataba wa ubia na hana haki ya kutoa vitisho hivyo isipokuwa kama sheria inayoanzisha wakala huo au sheria nyingine yoyote inampa mamlaka mapana namna hiyo. Tunatilia mashaka kama Waziri ana mamlaka hiyo. Waziri anaweza kuwa ametoa maneno yake, na wewe unatakiwa kumkumbusha matakwa ya mkataba wa ubia.

Kama bei ya bidhaa unayosema imeshuka na kupelekea hasara, na kushuka huko hakujachangiwa na uzembe wenu, hatuoni kwa nini kuwe na uvunjifu. Miradi inapoanzishwa, inaanzishwa kwa misingi ya dhahania fulani, ambayo inabadilika kadiri muda unavyokwenda. Kama mkataba wa ubia una kipengele cha usuluhishi na Waziri anatishia kuvunja, tunawashauri mara moja muuwasilishe mgogoro huu kwenye usuluhishi. Kama mtahitaji amri ya Mahakama wakati usuluhishi unaendelea, mnaweza kupeleka maombi husika Mahakamani kwa ajili ya kupata nafuu ya zuio, wakati mkisubiri matokeo ya usuluhishi.

Inaweza kuwa muhimu kumueleza Waziri na mshauri wake wa masuala ya sheria Wizarani kwamba utaratibu wa kisheria ni lazima ufuatwe na kwamba kuvunja mkataba kutakuwa ni kinyume cha sheria. Serikali imewawajibisha maafisa wengi tu wa ngazi za juu kwa kushindwa kutekeleza masharti ya mikataba ambayo maafisa hawa waliivunja kinyume na sheria kwa kisingizio cha jina la Serikali ambapo ilipelekea Serikali kupata hasara ya mabilioni na matrilioni ya Shilingi kwenye usuluhishi. Mkataba ambao pande zinaingia ni lazima uheshimiwe kwa mapana yake; na lazima usomwe na sheria nyingine za nchi.

## Duka la dawa lisilo la mfamasia

**Nilikuja Tanzania kama mtalii wa tamaduni na nilishuhudia kwamba usambazaji wa madawa maeneo ya vijijini haukuwa wa kuridhisha. Ninataka kuja na kufungua biashara ya maduka ya dawa maeneo**

**ya vijijini na nimekwishaanza kufanya uchunguzi wa awali juu ya jambo hili, ikiwamo kupata maoni juu ya muundo wa biashara. Ninataka kuhakikisha madawa haya yanapatikana kirahisi na kwa bei nafuu. Hata hivyo, nimearifiwa kwamba kama sijasomea fani ya ufamasia siwezi kufanya biashara hiyo. Je, hii ni kweli? Nitawashukuru sana kwa mwongozo wenu kwenye jambo hili.**

*28 Oktoba 2013*

Sheria ya ndani inayosimamia na kudhibiti fani ya famasia na taratibu zake ni Sheria ya Famasia Na. 1 ya 2011. Ni sheria hii pia ambayo imeanzisha Baraza la Wafamasia ambalo ndilo lenye mamlaka pekee ya kusajili, kuandikisha na kuorodhesha wafamasia, wafamasia-mchundo (technicians) pamoja na wasaidizi wa wafamasia. Chini ya Sheria hii, ni kosa kwa mtu yeyote kufanya biashara ya famasi/duka la dawa isipokuwa kama mtu huyo ni mfamasia au amejiunga na chama cha wafamasia. Sheria hii pia kwenye kifungu cha 43 inatamka kwamba siyo ruhusa kwa mtu yeyote ambaye siyo mfamasia kutengeneza kwa kuuza, kusambaza au kutoa dawa isipokuwa kwa usimamizi wa karibu wa mfamasia. Adhabu ya kukiuka masharti ya kifungu hiki ni kulipa faini isiyopungua milioni moja au kifungo kisichozidi miezi sita au vyote kwa pamoja. Na kama mkosaji ni taasisi au kampuni, adhabu yake ni faini isiyopungua Shilingi milioni tano.

Turudi kwenye swali lako, uwekezaji unaotarajia kuufanya unawezekana isipokuwa unatakiwa ufanye biashara hiyo na mfamasia ili kuendana na matakwa ya sheria, na mfamasia huyo ni lazima awe amesajiliwa nchini Tanzania. Kitu ambacho pengine kitakupa changamoto zaidi ni kwamba kuna uhaba wa wafamasia nchini Tanzania na hivyo kumpata mfamasia, achilia mbali maeneo ya vijijini, inaweza kuwa ni changamoto. Sheria haijatatua jambo hili na tunakushauri uwasiliane na Wizara ya sekta husika ili kujadiliana kuhusu jambo hili.

## Mamlaka ya mji kukamata ng'ombe wangu

**Nina ng'ombe na mbuzi wengi. Ili kupunguza gharama ya kuwatunza huwa ninawatelekeza mtaani karibu na nyumbani ili waweze kula majani na kitu kingine chochote wanachokikuta/kilichojiotea. Nimekuwa nikifanya hivyo kwa miaka mingi, lakini pasipo mimi kujua hili wala lile, mamlaka ya manispaa imekamata mbuzi na ng'ombe wangu na kutaka nilipe faini. Zaidi, wameniamuru nisiwaachilie tena kama nilivyokuwa ninafanya. Je, hii ni halali? Je, mtu asiwalishe ng'ombe na mbuzi wake kwa amani kwenye majani yaliyojiotea kwenye ardhi ya nchi yangu ambayo mimi ni raia wake? Ninataka kuiwajibisha manispaa. Nifanye nini?**

*13 Januari 2014*

Tunaelewa manung'uniko yako na ni kweli ni mazoea ya muda mrefu ya watu kuacha mifugo yao ikizurura mitaani au barabarani. Hata hivyo, mazoea hayo yamezuiliwa na sheria za manispaa pamoja na kanuni zake ili kuhakikisha kwamba jiji linakuwa safi, kuzuia matatazo ya kiafya yasiyotarajiwa pamoja na kuzuia ajali. Tunaamini manispaa imekuzuia kufanya jambo hilo kwa mujibu wa sheria.

Kuwa tu raia hakumaanishi kwamba unaweza kufanya chochote kwenye nchi yako. Kuna kanuni na sheria za kufuata ili watu wote waishi kwa amani na utulivu. Hebu fikiria nini kitatokea jijini Dar es Salaam iwapo kila mkazi akaachia mbuzi na ng'ombe wake mitaani. Tunakushauri uwasiliane na mwanasheria wako.

## Kuwajibika maafisa wa umma

**Nimekuwa nikifanya kazi na baadhi ya wahasibu kwenye ofisi za serikali ambao najua wanaisababishia serikali hasara kubwa kwa sababu ya uzembe wao. Si wezi, bali wanakosa umakini na muda wote huwa na haraka ya kwenda nyumbani. Ni tatizo kubwa ambalo linahitaji utatuzi. Je, hakuna sheria ambayo inayoadhibu tabia kama hizi ambazo zinaisababishia serikali hasara kubwa?**

*24 Februari 2014*

Kifungu cha 10 cha Sheria ya Fedha za Umma kinatamka wazi kwamba:

Iwapo itatokea hasara au upungufu wa fedha za umma au fedha nyingine zilizotolewa au zilizokuwa chini ya usimamizi wa afisa wa serikali au iwapo hasara au uharibifu wa mali ya serikali au mali nyingine unatokea wakati mali hiyo ikiwa chini ya uangalizi wa afisa wa umma na ikiwa Waziri ameridhika baada ya kufanya uchunguzi wa kina kwamba uzembe au mwenendo mbovu wa afisa ndio uliosababisha au kuchangia kupatikana kwa hasara au upungufu huo; (a) Kiasi hicho kilichopotea au kupungua; au (b) thamani ya mali iliyopotea au kuharibika; au (c) gharama za kurudishia au kutengeneza mali iliyoharibika, kama itakavyokuwa, litakuwa ni deni la serikali na linaweza kurudishwa na afisa huyo kwa mujibu wa Sheria ya Watumishi wa Umma (Malipo ya Madeni) ya mwaka 1970.

Iwapo uzembe au utendaji mbovu wa afisa wa umma haukuwa ni sababu pekee iliyochangia hasara, upungufu au uharibifu unaotokana na kitendo kilichotajwa chini ya Kifungu kidogo cha (3), kiasi kitakacholipwa na afisa huyo kitakuwa ni kile tu ambacho gharama za kukirudisha au kukitengeneza, kupotea au kuharibika kama Waziri atakavyoona, baada ya kufanya uchunguzi wa kina, kitakuwa ni cha haki na sawa kwa kuzingatia kiwango ambacho afisa huyo amehusika katika upotevu, upungufu au uharibifu husika. Katika Kifungu hiki, rejeo/maana ya neno afisa wa umma itahusisha pia mtu ambaye aliwahi kuwa afisa wa umma.

Unaweza kuona, kutokana na maelezo hapo juu, kwamba kuna sheria maalum ambayo inairuhusu serikali kudai fidia kutokana na hasara iliyosababishwa na maafisa wa umma. Wahasibu wengi hawakijui kifungu hiki cha sheria.

## Wanadiplomasia hawagusiki

**Kwa nini wanadiplomasia hawagusiki nchini Tanzania? Sisi ni legelege sana kwenye suala hili. Tunawezaje kubadili hali hii? Nimeshtushwa.**

*17 Machi 2014*

Hatujui unamaanisha nini unaposema tunawezaje kubadili. Sisi ni wanachama wa Mkataba wa Kimataifa wa Vienna, na wanadiplomasia wetu wanapewa upendeleo huo huo kwenye nchi nyingine.

Unapaswa kutambua kwamba tunafaidika pia na mahusiano mazuri ya kidiplomasia tuliyonayo nchini Tanzania, ni wazi umepotoka na maoni yako hayakubaliki. Kwa kukuongezea mshtuko zaidi, Mkataba wa Vienna unaeleza yafuatayo: katika Ibara ya 9, nchi mwenyeji (wa ubalozi) inaweza wakati wowote na kwa sababu yoyote kutangaza kuwa haimhitaji/haimtaki mwanadiplomasia yoyote. Nchi husika iliyomtuma ni lazima imrudishe/imuondoe afisa huyo ndani ya muda muafaka, vinginevyo afisa huyo atapoteza kinga yake ya kidiplomasia.

Ibara ya 22: Nchi mwenyeji haiwezi kufanya upekuzi, wala kuchukua nyaraka au mali za ubalozi. Ibara ya 30 inapanua wigo wa kifungu hiki hadi kwenye makazi binafsi ya wanadiplomasia, na ndiyo maana unaona kwamba katika jiji la Dar, makazi binafsi ya wanadiplomasia yanajipambanua

wazi. Ibara ya 27: Nchi mwenyeji ni lazima iruhusu na kulinda mawasiliano baina ya wanadiplomasia/ubalozi na nchi zao. Ibara ya 29: Hairuhusiwi kuwakamata wala kuwafunga wanadiplomasia. Wana kinga dhidi ya mashtaka ya madai na jinai, ingawa nchi iliyomtuma inaweza kuondoa kinga hii chini ya Ibara ya 32. Chini ya Ibara ya 34, wanadiplomasia wana msamaha wa kodi mbalimbali, mathalani chini ya Ibara ya 36 wamesamehewa kulipia ushuru wa forodha. Ibara ya 31(1)(c) inahusu mambo ambayo hayakingwi na kinga ya kidiplomasia; shughuli ya kitaalam nje ya shughuli rasmi za kidiplomasia, na ndiyo maana wanadiplomasia wengi hawafanyi kazi yoyote nje ya kazi za kidiplomasia.

## Mgongano wa maslahi kwenye bodi ya TRA

**Miongoni mwa mambo mengine, nimegundua kwamba kuna wanabodi wa TRA ambao wana mgongano wa kimaslahi kwenye masuala ya manunuzi/ugavi. Je, hakuna Sheria inayowazuia kuwa sehemu ya wafanya maamuzi kwenye manunuzi husika?**

*23 Juni 2014*

Jedwali la 2 aya ya 4 ya Sheria ya Mamlaka ya Mapato inajibu swali lako. Sheria hii inaeleza kama ifuatavyo: 4(1) Mwanabodi ambaye anamaslahi ya moja kwa moja ama yasiyo ya moja kwa moja katika jambo linalojadiliwa au linalotaka kujadiliwa, baada ya kufahamu jambo husika, atapaswa kuweka wazi maslahi hayo haraka iwezekanavyo. (2) Maslahi yaliyoelezwa chini ya kifungu kidogo (1) yatarekodiwa kwenye muhtasari wa kikao cha Bodi, na mwanabodi aliyefichua maslahi yake, isipokuwa kama Bodi itaamua vinginevyo kuhusu suala hilo (a) hatahudhuria kwenye majadiliano yoyote ya Bodi kuhusu jambo hilo; (b) hatakuwa sehemu ya maamuzi ya bodi. (3) Kwa madhumuni ya kufanya maamuzi ya Bodi chini ya kifungu kidogo (2) kuhusu mwanabodi aliyeeleza maslahi yake chini ya kifungu kidogo (1), (a) hatakuwepo wakati wa majadiliano na katika kutoa maamuzi ya Bodi; au (b) hatamshawishi mwanabodi yeyote wala kushiriki katika kuifanya Bodi kutoa maamuzi. (4) Iwapo akidi ya kikao haitatimia kwa sababu ya mwanabodi kuondolewa kwenye majadiliano juu ya jambo ambalo ameeleza kuwa na maslahi nalo, wanabodi waliobaki wanaweza (a) kuahirisha majadiliano juu ya jambo hilo mpaka akidi itimie bila mwanabodi husika; au (b) kuendelea kujadili na kutoa maamuzi juu ya jambo hilo kana kwamba akidi imetimia.

Kwa hiyo, mwanabodi wa TRA ambaye anamaslahi binafsi ni lazima afichue maslahi husika, na ikiwa hatofanya hivyo, atakuwa amekiuka Sheria. Adhabu ya juu kabisa ya kukiuka Sheria hii ni kufungwa jela kwa miaka miwili.

## Kuishtaki serikali

**Kwa nini nisubiri siku 90 kuishtaki serikali? Au mwanasheria wangu ananichukulia mbumbumbu? Nini kitatokea kama idara ninayoishtaki haitoi utetezi wake? Kitu gani zaidi unaweza kunishauri?**

*18 Agosti 2014*

Sheria ya Mwenendo wa Mashtaka ya Serikali inaeleza wazi katika Kifungu cha 6 kwamba (1) bila kujali masharti ya vifungu vingine kwenye Sheria hii, kesi za madai zinaweza kufuguliwa dhidi ya serikali kwa masharti ya kifungu hiki. (2) Hakuna kesi dhidi ya serikali itakayo funguliwa na kusikilizwa isipokuwa pale tu mlalamikaji atakuwa amewasilisha kabla kwenye wizara ya serikali, idara au afisa anayehusika notisi siyo chini ya siku tisini juu ya nia yake ya kuishtaki serikali, ikieleza msingi wa dai lake dhidi ya serikali na atatuma nakala ya dai lake kwa Mwanasheria

Mkuu wa Serikali. (3) Kesi zote dhidi ya serikali, baada ya kuwasilishwa kwa taarifa zifunguliwe dhidi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, na nakala ya hati ya mashtaka ipelekwe kwenye wizara husika, idara au afisa ambaye anatuhumiwa kutenda kosa hilo ambalo ni msingi wa shtaka la madai. (4) Kesi zote dhidi ya serikali zitafunguliwa Mahakama Kuu kwenye Kitengo cha Mahakama Kuu katika eneo ambalo dai limetokea. (5) Bila kujali masharti ya kifungu kidogo cha (3), Mwanasheria Mkuu anaweza, isipokuwa kama mtu mwingine anastahili kushtakiwa, kushtakiwa au kuunganishwa kama mshtakiwa mwenza/pacha, kwenye kesi yoyote dhidi ya serikali. (6) Vifungu vya Sheria ya Watumishi wa Umma (Malipo ya Madeni) vitatumika kwa afisa yeyote aliyeisababishia serikali hasara, gharama na fidia kutokana na kushindwa kwake kupata uwakilishi wa kisheria katika kesi husika.

Ingawa haihusiani, iwapo idara ya serikali ikishtakiwa na haijajitetea kwa kupeleka utetezi, basi kesi itaendelea upande mmoja na inawezekana ukafanikiwa katika madai yako. Hata hivyo, mkuu wa idara ambaye ameshindwa kupeleka utetezi dhidi ya kesi anaweza kuwajibishwa yeye mwenyewe kwa kiasi cha fedha hizo chini ya Sheria ya Watumishi wa Umma (Malipo ya Madeni).

## Mamlaka ya TAKUKURU kufanya upekuzi

**Maafisa wa TAKUKURU walikuja kufanya upekuzi kwenye eneo letu. Tuliwasihi wajitambulishe, lakini walikataa na kulazimisha kuingia. Je, hii inaruhusiwa?**

*15 Septemba 2014*

Hujatuambia nini kilitokea baada ya wao kulazimisha kuingia. Tunaona jambo hili ni kinyume cha sheria kwa sababu Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa inaeleza yafuatayo kwenye Kifungu cha 11(1)-(1) Mkurugenzi Mkuu atampa ofisa wa Taasisi kitambulisho ambacho kitakuwa ni ushahidi wa utumishi wake kwenye Taasisi (2) Kila ofisa wa Taasisi atapaswa kumuonesha mtu atakayehitaji kitambulisho chake cha kazi (3) Ofisa wa Taasisi anayefanya upelelezi wa kosa linaloshukiwa kufanywa kwa mujibu wa Sheria hii au Sheria nyingine zinazohusiana na rushwa anaweza kumuomba msaada ofisa yeyote wa umma kwa kuzingatia matumizi yanayofaa ya mamlaka yake au utekelezaji wa majukumu yake kwa mujibu wa sheria hii.

Kifungu cha 12 kinahusu upekuzi ambapo kinaeleza: (1) Mkurugenzi Mkuu anaweza, kwa maandishi, kumuidhinisha ofisa yeyote kumpekua mtu yeyote iwapo, kwa sababu za msingi, itashukiwa kuwa mtu anayehusika anamiliki mali iliyopatikana kwa njia ya rushwa au kwa njia nyingine yoyote haramu au kupekua mahali popote, chombo cha usafiri, boti/meli, ndege au gari lingine lolote iwapo kuna sababu za msingi za kuamini kuwa mali yeyote iliyopatikana kwa njia ya rushwa au kwa njia haramu imewekwa, imetunzwa au kufichwa humo.

Hivyo, ingawa upekuzi wa majengo unaruhusiwa chini ya sheria, kama maafisa waliopo hawataki kuonesha utambulisho wao, watakuwa hawatoki TAKUKURU na inawezekana ulikuwa unashughulika na waharifu hasa ukizingatia kwamba walilazimisha kuingia ndani.

## Zabuni kufunguliwa kabla ya muda mwafaka

**Kampuni yetu iliomba zabuni kubwa ya ujenzi wa barabara. Wakati zabuni zinafunguliwa tuligundua kwamba lakiri ya zabuni ilikuwa imechezewa na bahasha imefunguliwa. Je, hili siyo tatizo kubwa?**

*22 Septemba 2014*

Ikiwa lakiri ya zabuni ilifunguliwa, zabuni inaweza kufutwa. Hata hivyo hii itategemea

na mazingira na ushahidi ambao utatolewa.

Ikiwa upo sahihi, mtu aliyefungua lakiri ana hatia kama ilivyoelezwa chini ya Kifungu cha 104 cha Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2011 ambayo inasema kwamba mtu anayefungua zabuni yoyote ambayo bado ina lakiri, ikiwa ni pamoja na zabuni zinazoweza kukusanywa kupitia mfumo wa kielektroniki na nyaraka yoyote inayotakiwa kufungwa, au kufungua na kuona yaliyomo kabla ya muda rasmi uliowekwa kwa ajili ya ufunguzi kwa umma wa nyaraka za zabuni, atakuwa ametenda kosa na akikutwa na hatia atawajibika kulipa faini isiyopungua Shilingi milioni kumi au kifungo kwa muda usiopungua miaka saba au vyote kwa pamoja, na kwa kuongezea, adhabu iliyotolewa chini ya kifungu hiki, mahakama itaagiza kiasi cha hasara aliyopata mlalamikaji afidiwe, ikishindikana mahakama itatoa amri ya kupokonywa mali binafsi ya mtu aliyehukumiwa ili kufidia hasara husika.

# Watoto, Mahusiano, Sheria za Ndoa na Talaka

Ndoa, talaka, na masuala yanayohusu ustawi wa watoto yanaweza kupelekea migogoro mizito ya kisheria. Je, unaweza kudai zawadi ulizoahidiwa kabla ya harusi, kumpa jina mwanao, au kutoa talaka kwa mwenzi wako kwa sababu ya unene uliopitiliza au kufuga ndevu? Haya ni baadhi tu ya maswali yaliyoulizwa na wasomaji wa safu yetu.

## Stahiki baada ya talaka

**Niliolewa miaka kumi iliyopita, nimemchoka mume wangu na ninataka talaka. Nimekuwa mama wa nyumbani na sikuwa na mchango wa moja kwa moja wa kifedha kwenye kununua mali ambazo mume wangu alizichuma wakati wa ndoa yetu. Mara zote amekuwa akiniambia nimekuwa baraka kwake, kwa kuwa tangu amenioa ameingiza pesa nyingi sana. Anajua ninataka takala lakini ameniambia wazi kuwa kama nikifungua kesi kudai talaka nitaishia mtaani na hatonipatia pesa ya matunzo wala kunilipa (kifuta jasho) chochote. Na anasisitiza kuwa mali zote ni za kwake na wanafamilia yake. Ni kweli sijaleta pesa taslimu nyumbani lakini nimemsaidia kusimamia biashara zake zote. Hivi, ni kweli sistahili chochote? Nifanyeje? Kusema kweli, sitaweza kuishi hata kidogo kwenye dunia hii kama mume wangu dhalimu atanifukuza bila kunipa chochote.**

*6 Februari 2012*

Hujatuambia kwa nini unataka talaka. Nchini Tanzania, hamuwezi tu kukubaliana kupeana talaka. Sheria ya ndoa inatoa sababu maalum kama vile uzinzi, ukatili, au kutelekezwa ambazo ni lazima uzieleze ili uweze kupata talaka. Mahakama pia, kabla ya kutoa amri ya talaka, ni lazima ijiridhishe kwamba ndoa yenu imevunjika kabisa na kwamba haiwezi kurekebishika kabla ya kutoa amri ya talaka.

Iwapo utaamua kuomba talaka Mahakamani, kuna maamuzi mengi ya Mahakama, ikiwemo kesi maarufu ya Mahakama ya Rufani ya Tanzania ambayo iliamua kwamba kazi za nyumbani zina mchango katika kuchuma mali za ndoa.

Kwa kuwa umemsaidia mmeo kuangalia nyumba yenu, pale anapokuwa mbali, pamoja na kusimamia mali za familia, unastahili mgawo sawa kwa mali mlizozichuma pamoja. Kwa kawaida, mgawo haujali kama mali zipo kwa jina la mmeo au la kwako.

Mmeo anadhani anaweza tu kukufukuza. Hiyo siyo kweli na sheria inakulinda. Mmeo anapaswa kusoma baadhi ya kesi maarufu za talaka ambapo wanaume wamekuwa masikini zaidi kwa sababu ya talaka kama ilivyo kwa kesi ya mwandishi maarufu Rupert Murdoch, aliyekuwa mcheza kikapu maarufu na nyota Michael Jordan, aliyekuwa mcheza gofu maarufu, Tiger Woods, muongoza filamu Steven Spielberg, muigizaji Harrison Ford na muimbaji Lionel Richie ambapo wote hao talaka ziliwagharimu mabilioni.

Tunakuonya pia kuwa kama wakati wowote uliwahi kutumia mali za familia vibaya kwa mfano kununua vito vya thamani visivyo vya lazima au ulitumia pesa kwa anasa, pesa hizo zitakatwa kwenye kiasi unachostahili kupewa. Ushauri wetu hapa ni kwa ajili ya kukuongoza tu na siyo kuharibu au kuvunja uhusiano wenu. Unaweza kumtafuta mshauri wa masuala ya ndoa kwa ushauri zaidi.

## Mke anataka talaka

**Mimi na mke wangu tulioana na kuishi kwa furaha hadi siku za hivi karibuni alipoanza kuibua barua-pepe za kabla ya ndoa yetu ambapo alikuta zenye ujumbe wa mapenzi kutoka kwa mpenzi wangu wa zamani. Anasema ningemwambia kuhusu uhusiano huo kabla ya ndoa. Nilimjibu kuwa hakuniuliza na sijawahi kuwasiliana na mpenzi huyo baada ya ndoa. Hata yeye alikuwa na wapenzi wake ambao taarifa zao sikuwahi kuzifuatilia kwa kuamini kwamba ya kale yamepita. Mke wangu anataka talaka. Nifanyeje?**

*20 Februari 2012*

Sheria ya Ndoa ya Tanzania ina vifungu mahususi ambavyo vinaeleza sababu zinazoweza kutolewa wakati wa kuomba talaka. Kwa mfano, mtu hawezi tu kupewa

talaka Tanzania kwa makubaliano yake na mume wake. Baadhi ya sababu za msingi ni ukatili, uzinzi na utelekezaji. Ni wazi kuwa haupo kwenye kundi la uzinzi, kama tutachukulia kuwa ulichotuambia kina ukweli ndani yake kwamba hujawahi kuonana na mpenzi wako baada ya ndoa. Inatuwia vigumu kuamini kwamba kutoka tu hewani mkeo ameamua kuangalia barua-pepe zako za miaka mingi iliyopita. Kama kuna kitu unatuficha tafadhali puuza jibu letu. Hata hivyo, tunajaribu kujibu swali lako tukiamini hujatuficha chochote.

Sababu nyingine ya kawaida ya talaka ni kutelekeza ambayo pia tunaamini haihusiki kwenye kesi yako. Ukatili ni sababu mojawapo lakini ni ya mbali sana. Kwa mfano, hivi mkeo anaweza kudai umekuwa mkatili kwa kutokumtambulisha kwake mpenzi wako wa zamani? Tuna mashaka kuna mazingira yasiyo ya kawaida ambayo hatuyajui.

Yote kwa yote, hatuoni namna kesi ya mkeo itafanikiwa kwa sababu ulizotueleza kwenye swali lako. Tunapendekeza mumtafute mshauri maana inaonesha kuna jambo unatuficha.

## Kuvunja haki ya faragha

**Nimempeleka kijana wangu wa kiume wa miaka 14 nchini Afrika Kusini kwenye shule ya michezo kwa ajili ya majaribio. Kabla hawajampokea, walimsindikiza bafuni na kumpima mkojo. Nilipinga, lakini waliniambia ni lazima apimwe. Je, kitendo hicho si kuvunja haki yake ya faragha kikatiba?**

*27 Februari 2012*

Suala hili limekuwa na mjadala kwa nchi nyingi na utafiti wetu unaonesha kwamba mara nyingi chuo kinachofanya vipimo huwa kinashinda. Wakati mwanao alipoenda kupima mkojo, inawezekana alisindikizwa lakini hakuna uwezekano kwamba alikuwa akichunguliwa wakati akichukua sampuli ya mkojo.

Ni lazima tukueleze kwamba, jibu letu kuhusu suala lako linaweza lisikidhi matakwa yako kwa sababu katiba yetu haitumiki nchini Afrika Kusini. Unaweza kuwasiliana na mwanasheria wa huko (Afrika Kusini) kwa mwongozo zaidi.

## Kutelekeza mtoto na kukataa kumpa chakula

**Nimekutana na mwanamke mmoja jijini Dar es Salaam ambaye hatoi mahitaji kwa watoto wake wadogo. Anasema ni yeye ndiye anayeamua juu ya ustawi wa watoto wake na siyo mtu mwingine. Hawajali japo ana uwezo wa kufanya hivyo. Je, hilo siyo kosa?**

*19 Machi 2012*

Mtu yeyote ambaye ni mzazi, mlezi au mtu mwingine ambaye ni mwangalizi halali au aliyepewa jukumu la kumlea mtoto ana wajibu wa kutoa mahitaji ya msingi ya maisha kama vile chakula, mavazi, malazi na kadhalika kwa ustawi bora wa mtoto. Kumwacha mtoto bila msaada ni kosa la kutelekeza ambalo linaadhibiwa kisheria. Kwa kuongezea, kukataa kutoa mahitaji ya msingi kiasi cha kudhohofisha afya ya mtoto pia ni kosa. Makosa haya adhabu yake ni kifungo cha miaka miwili jela, faini au vyote viwili kwa pamoja.

## Kumlazimisha mwenza kupima VVU

**Mimi na mpenzi wangu/rafiki wa kiume tupo kwenye mahusiano kwa miezi sita na tunakusudia kuoana. Nakubaliana na sharti lake lakini nina sharti kwamba wote wawili ni lazima tukapime VVU/UKIMWI kwanza kabla ya kuendelea. Jambo la kushangaza, amekataa anasema yeye ana afya na haoni haja ya kwenda kupima. Nioane nae? Nifanyeje?**

*30 Aprili 2012*

Sheria za Tanzania hazilazimishi upimaji wa VVU, isipokuwa kwa hiari ya mtu anayepimwa. Hata hivyo yapo mazingira ambayo upimaji wa VVU hauhitaji hiari kama vile: kwa amri ya Mahakama, uchangiaji wa viungo vya binadamu na makosa ya kingono. Mpenzi wako haangukii kwenye lolote kati ya hayo na hivyo huwezi kumlazimisha kwenda kupima.

Katika hali nyingine, ni vizuri kumfahamisha mpenzi wako kwamba ni kosa la jinai nchini kwetu kusambaza VVU kwa makusudi kwa mtu mwingine. Kosa hilo adhabu yake ni jela kati ya miaka 5 hadi 10. Kuwa na afya hakumaanishi kwamba hauna VVU/UKIMWI, tunawashauri mpate ushauri kutoka kwa mshauri wa masuala ya VVU/UKIMWI. Iwapo uolewe au usiolewe, kwa bahati mbaya kama wanasheria hatuna sifa za kujibu swali hilo.

## Mume wangu kumuoa mwanangu wa kuasili

**Nilikuwa kwenya ndoa kwa zaidi ya miaka 20 na ndoa yetu haikubarikiwa mtoto yeyote. Tuliasili mtoto ambaye tumemlea kwa miaka mingi. Mume wangu alifariki kwa ugonjwa wa kupoteza kumbukumbu na fahamu, kwa kiingereza 'Alzheimer', miaka mitano iliyopita. Hivi karibuni nilikutana na kijana mzuri na tukaoana na baadaye nikagundua kuwa ana mahusiano ya kimapenzi na mwanagu wa kuasili. Sikuwa na jinsi zaidi ya kudai talaka na mwishowe nikagundua kwamba mume wangu anataka kufunga ndoa na binti yangu wa kuasili. Wanasheria wangu wananiambia ni ngumu kuzuia wasioane kwa sababu ndoa ni mkataba wa watu wawili na kwa hiyo siwezi kuingilia. Nifanye nini?**

*30 Aprili 2012*

Wanasheria wako, wako sahihi kwamba ndoa ni mkataba. Lakini iwapo unaweza kuzuia ndoa hiyo, tunaamini unaweza. Kwa mujibu wa Sheria ya Ndoa ya Tanzania, baba amezuiliwa kumuoa mtoto wake mwenyewe au mtoto wa mwenzi wake wa awali. Mmeo anaweza kujenga hoja kwamba binti anayetembea naye kwa sasa siyo mwanao kwa sababu ulimuasili. Lakini sheria inamtambua kama mwanao na hivyo kwenye sheria zetu hawezi kumuoa.

Chini ya Kanuni ya Adhabu mwanamume yeyote ambaye amekatazwa kufanya ngono na mwanamke yeyote ambaye anamjua kuwa ni mjukuu wake, binti yake, dada yake au mama yake, mwanamume huyo atakuwa amekosa na akipatikana na hatia atastahili adhabu. Iwapo mwanamke ana umri wa chini ya miaka kumi na nane, mwanamume huyo atahukumiwa kifungo kisichopungua miaka thelathini, na iwapo mwanamke ana umri wa miaka kumi na nane au zaidi, mwanamume huyo atahukumiwa kifungo kisichopungua miaka ishirini. Haitakuwa na utetezi kwamba kitendo cha ngono kilifanywa kwa idhini ya mwanamke huyo.

Mwanao anafanya uhalifu. Sheria inatamka kwamba mwanamke yeyote mwenye umri wa zaidi ya miaka kumi na nane ambaye anaridhia na anamruhusu babu yake, baba yake, kaka yake au mtoto wake wa kiume kujamiiana naye (akijua kwamba huyo ni babu, baba, kaka au mtoto wake vyovyote itakavyokuwa) atakuwa ametenda kosa na atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha maisha au kifungo kisichopungua miaka thelathini na pia anaweza kuamriwa kulipa fidia ya kiasi kitakachoamriwa na Mahakama kwa yule aliyetendewa kosa hilo.

Kunaweza kutokea mjadala wa iwapo mume uliyeachana naye ni baba wa mtoto wa binti yako lakini yote kwa yote mume uliyeachana naye atakuwa ametenda kosa la uharimu.

Unaweza kuweka pingamizi kanisani ambako ndoa itafanyikia au unaweza kuomba Mahakamani. Unaweza pia kutoa taarifa kituo cha polisi kwa kitendo hicho, kwani kitendo cha uharimu ni kosa la jinai.

## Mke ananinyima penzi/unyumba

**Tangu nilipomuoa, mke wangu hajawahi kuniruhusu hata kumgusa. Anasema hayuko tayari kwa hilo. Nimechanganyikiwa na sijui nifanye nini. Naweza kupata amri ya Mahakama ya kumlazimisha ashiriki nami? Bado nampenda.**

*7 Mei 2012*

Unaposema hakuruhusu kumgusa, tunachukulia kwamba anakunyima unyumba, yaani anakunyima haki ya ndoa. Ndoa ni mkataba na moja ya masharti ya mkataba ni kwamba mtaishi kama mke na mume na kwamba hautanyimwa tendo la ndoa. Umenyimwa haki zako hizi kwa sababu mkeo hayuko tayari. Labda ungetamani akuambie hili mapema kabla hamjaoana lakini sasa umechelewa sana. Kwa hiyo swali lako ni iwapo unaweza kupata amri ya Mahakama ya kumlazimisha ashiriki tendo la ndoa.

Kutaka amri ya Mahakama kushinikiza tendo la ndoa ni kitendo cha kizamani, na siyo chaguo sahihi nyakati hizi. Kwa hiyo, hauna chaguo hilo, labda muendelee kuishi hivyo mpaka yeye atakapokuwa tayari au umpe talaka. Kunyimwa tendo la ndoa ni sababu mojawapo ambayo unaweza kuitumia kuomba talaka. Tafadhali elewa kwamba usimlazimishe kufanya mapenzi. Ingawa ni wanandoa na bado mpo kwenye mahusiano, mkeo anayo haki ya kusema hapana, na ikiwa utaendelea kumlazimisha unaweza kushtakiwa kwa kosa kubwa la ubakaji. Katika hali nyingine, unaweza kutafuta kujua sababu ya kukukatalia. Unaweza pia kufikiria kupata ushauri kutoka kwa mshauri wa ndoa.

## Idadi ya juu ya watoto

**Baba mkwe wangu amekuwa akiingilia ndoa yangu kwa miaka kadhaa sasa. Anasema kwamba nampa sana mwanae msongo wa mawazo kwa kumbebesha mimba za mara kwa mara. Siamini katika matumizi ya kondom na iko nje ya uwezo wangu kwani Mungu ametutunukia watoto wengi. Mwanasheria ameniandikia barua kwamba kuna Kanuni fulani ambazo zinataka familia lazima itumie uzazi wa mpango vinginevyo kuwe na ukomo wa idadi ya watoto ambayo mtu anatakiwa kuwa nao. Je, hii ni kweli?**

*4 Juni 2012*

Kwa uzoefu wetu wa miaka mingi, hatujawahi kuona sheria inayomlazimisha mtu kutumia uzazi wa mpango. Pia, hakuna sheria ambayo inaelezea idadi ya juu ya watoto ambayo mtu anatakiwa kuwa nao. Ingawa mwanasheria pamoja na baba mkwe wako wanakupotosha, siyo wazo baya kuanza kufikiria kutumia njia za asili za kuzuia ujauzito kwa sababu kudhibiti uzazi, baada ya kuwa na idadi fulani ya watoto, kunaweza kuwa na faida. Hilo nalo linategemea, na ni wazo letu tu. Kama wanasheria, hatuna ujuzi kuhusu njia za asili za uzazi wa mpango. Tunakushauri kuwasiliana na mshauri wa masuala ya jinsia na uzazi.

## Nataka kuoa msichana mwenye umri wa miaka 16

**Mimi ni mhitimu wa Chuo Kikuu. Ninaishi Dodoma na nipo kwenye mapenzi na msichana wa miaka 16. Sote tunapendana sana na tunataka kuoana. Wazazi wa msichana wamekataa kutupatia baraka za kuoana. Nimefanya kila linalowezekana kuwashawishi watupe baraka zao lakini haijazaa matunda. Ni mwanya gani mwingine ninao?**

*18 Juni 2012*

Sheria ilivyo kwa sasa inamtaka mwanamke ambaye hajafikisha umri wa miaka kumi na nane kupata idhini ya wazazi na kama hakuna wazazi basi mlezi kabla hajaolewa. Hata hivyo, kifungu cha 17 cha

Sheria ya Ndoa ya 1971 kinasema kwamba kama idhini imekataliwa unaweza kuomba Mahakamani ambayo baada ya kuridhika kwamba idhini imekataliwa bila sababu za msingi, inaweza kutoa idhini hiyo ambayo itakuwa sawa na idhini inayotolewa na wazazi au mlezi kutegemea na aliyepo.

Hata hivyo, inashauriwa kuoa/kuolewa katika umri mkubwa zaidi baada ya msichana kupata elimu ya juu zaidi. Ulimbwende wa msichana unaweza ukaishia miaka 20, lakini elimu yake itabakia; na inawezekana hicho ndicho wazazi wake wanafikiria, na sisi tunadhani siyo vibaya kuwa na fikra hizo.

Lazima pia tulilete suala hili moja kubwa kwenye akili yako. Tunachukulia kwamba unashiriki ngono na huyo msichana. Tafadhali elewa kwamba kifungu cha 130(2) (e) cha Kanuni ya Adhabu kinatamka kwamba mtu wa jinsia ya kiume atakuwa ametenda kosa la kubaka kama atakuwa amefanya tendo la ndoa na msichana au mwanamke kwa idhini au bila ya idhini akiwa chini ya umri wa miaka kumi na nane, isipokuwa kama mwanamke ni mke wake ambaye ana umri wa miaka kumi na tano au zaidi na hajatengana na mumewe.

Kutokana na maelezo hapo juu unaweza kuona kwamba hata kama mpenzi wako anaridhia kufanya ngono na wewe, kwa umri wake, siku akitoa taarifa hii polisi, unaweza kushtakiwa kwa ubakaji ambalo ni kosa kubwa sana.

## Kuhudumia ujauzito

**Mimi ni mtu mzima na nimepata ujauzito na najua siyo kosa kisheria. Mpenzi wangu ambaye alinipa ujauzito, hana tena mapenzi na mimi kwa sababu ananiona ati ni mkubwa na sivutii tena. Anashindwa kunisaidia na kusahau kuwa na yeye ana mama ambaye pia aliubeba ujauzito wake. Nifanye nini?**

*25 Juni 2012*

Kushika ujauzito kwa kawaida ni baraka na siyo laana na kama ulivyosema siyo kosa kisheria. Sheria ya Mtoto inamruhusu mama anaetarajia kujifungua kupeleka maombi ya matunzo Mahakamani na kama itaona sababu za msingi za kuamini kwamba mwanamume anaedhaniwa kuwa ni baba wa mtoto kweli ndiye na kwamba maombi ya matunzo yameletwa kwa nia njema na siyo kwa malengo ya kutishia au kwa shari, maombi yako yanaweza kufanikiwa. Hivyo una hiari ya kufungua maombi Mahakamani ukiomba amri ya matunzo kwa kipindi cha ujauzito. Kwa msaada zaidi tafadhali wasiliana na mwanasheria wako.

## Uhalali wa ndoa

**Mimi ni Mkatoliki ambaye niliolewa miaka minne iliyopita na kubarikiwa kupata watoto wawili. Hivi karibuni nimegundua kwamba mume wangu ana mke mwingine Dar es Salaam ambaye alimuoa kwa ndoa ya kikristo. Baada ya kufuatilia kwa karibu, nimegundua kwamba alimtelekeza mke na familia yake kwa ajili yangu na hakuna talaka iliyotolewa. Je, inawezekana mume wangu kuoa wake wawili?**

*2 Julai 2012*

Sheria ya ndoa ya Tanzania inatambua ndoa kama ni muungano wa mume na mke ambayo inakusudia kudumu mpaka mwisho wa maisha yao. Pia sheria inatambua ndoa ya kikristo kuwa ni doa ya mke mmoja. Ndoa ya mke mmoja ni ndoa kati ya mke mmoja na mume mmoja tu. Pia sheria inatambua njia zifuatazo ambazo zinaweza kufanya ndoa kufika mwisho; (a) kifo cha mmoja wa wanandoa (b) amri/tuzo ya Mahakama inayotangaza kuwa mmoja wa wanandoa anadhaniwa kuwa amefariki; (c) amri/tuzo ya Mahakama ya kubatilisha ndoa; (d) amri/tuzo ya talaka; au (e) kwa talaka iliyotolewa na Mahakama nje ya Tanzania.

Kwa kuwa mume wako hakupata talaka kabla ya kukuoa, ndoa yake ya kwanza ni halali na bado ipo. Sheria pia inazuia mtu mwenye ndoa ya mke mmoja kuingia kwenye ndoa nyingine. Kifungu cha 15 cha Sheria ya Ndoa kinasema kwamba hakuna mwanamume, akiwa kwenye ndoa ya mke mmoja, kufunga ndoa nyingine. Wakati mume wako alipokuoa, alikuwa hana sifa za kufanya hivyo, na ndoa yako inaweza kuwa batili. Tunakushauri uwasiliane na mwanasheria wako kwa muongozo zaidi.

## Kusajili uzazi/mtoto aliyezaliwa

**Mimi na mke wangu tuna mtoto mzuri wa kiume ambaye mke wangu alizalishwa nyumbani na mkunga wa jadi kijijini kwetu. Ninaamini mwanangu ana uwezo wa kipekee na sitaki kumsajili kama mtoto aliyezaliwa. Nifanye nini? Je, ni lazima nimsajili?**

*9 Julai 2012*

Sheria ya Uandikishaji Vizazi na Vifo inakulazimisha kumsajili mtoto wako aliyezaliwa. Sheria inatamka wazi kwamba kila mtoto aliyezaliwa hai baada ya kuanza kutumika Sheria hii na ambaye usajili wake ni wa lazima, itakuwa ni jukumu la baba au mama, na kama baba au mama wakishindwa, mkazi wa nyumba ambaye kwa uelewa wake, mtoto huyo amezaliwa, na kila mmoja aliyekuwepo wakati mtoto anazaliwa, kumsajili mtoto huyo ndani ya miezi mitatu tangu kuzaliwa.

Chini ya Sheria hii, kama mtu mwenye wajibu wa kusajili kizazi au kifo cha mtoto anashindwa kufanya hivyo atawajibika kulipa faini isiyozidi Shilingi laki tano au kifungo kisichozidi mwezi mmoja au vyote kwa pamoja.

Hivyo, kumsajili mtoto wako ni lazima na kuna kifungo ikiwa utakiuka. Sababu kwamba hutaki kumsajili mwanao kwa sababu ana uwezo wa kipekee haitambuliki kwenye sheria zetu. Hakuna uwezekano kwamba uwezo huo utapotea kwa kumsajili mwanao.

## Kuolewa tena

**Nilikuwa kwenye ndoa kwa miaka 10 kabla ya mume wangu kufariki miaka miwili iliyopita. Wakati wa ndoa yetu tulichuma mali kwa pamoja kwa sababu sote tulikuwa na kazi nzuri. Nimekutana na mtu ambaye ananipenda na tunataka kuoana. Ndugu wa mume wa zamani wanajaribu kunizuia kuolewa tena wakisema kwamba hairuhusiwi na kama nikifanya hivyo moja kwa moja wao watachukua mali zangu. Tafadhali naomba muongozo.**

*6 Agosti 2012*

Kifungu cha 68 cha Sheria ya Ndoa hakimkatazi mwanamke kuolewa tena na kinaeleza kwamba bila kujali mila zozote zinazoenda kinyume, mwanamke aliyefiwa na mume atakuwa huru (a) kwenda kuishi mahala popote apendapo; na (b) kukaa bila mume au kuolewa na mume yeyote atakayeridhika naye kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 17; Isipokuwa, kama aliolewa katika ndoa ya kiislamu, mjane huyo hatakuwa na haki ya kuolewa tena mpaka pale kipindi cha eda kitakapokwisha.

Kuhusiana na ndugu wa upande wa mume wako, kama mlimiliki mali hizo kama wamiliki-wenza (joint occupiers), basi umiliki wa mali hizo moja kwa moja unahamia kwako kama mmiliki mwenza uliyesalia baada ya kifo cha mume wako. Lakini kama umiliki wa mali hizo ulikuwa ni umiliki-shirika (occupiers in common), basi sehemu yako katika umiliki itabaki kwako na sehemu ya mume wako itahamishiwa kwa yeyote (mshirika mwingine) aliyetajwa kwenye wosia. Utofauti kati ya umiliki-wenza na umiliki-shirika ni

muhimu na watu wengi hawajui kutofautisha haya.

## Zawadi kwa msichana mzuri

**Nilikutana na msichana mzuri na tulianza mahusiano. Baada ya kumshawishi na yeye kukubali kuhusu kuoana, na ili kumfanya aridhike, nilimpatia zawadi nyingi sana, mojawapo ikiwa ni gari langu. Hivi karibuni nimeshtuka kuona kwamba ana mwanamume mwingine ambaye alikuwa anajifanya kama ni dereva wake na yupo kwenye mahusiano naye na tayari amekwisha toa mahari. Anakataa kunirudishia zawadi nilizomnunulia, likiwemo gari langu. Nifanye nini?**

*13 Agosti 2012*

Zawadi zilizotolewa wakati wa uchumba zinaweza kurudishwa kisheria kama uchumba huo usipozaa ndoa. Kifungu cha 71 cha Sheria ya Ndoa kinamruhusu mtu kufungua shauri Mahakamani ili kurudisha zawadi zilizotolewa wakati wa kusubiria ndoa ambayo hata hivyo haikufanikiwa, na inaweza kurudishwa kama Mahakama itajiridhisha kwamba zawadi hizo zilitolewa kwa sharti kwamba ndoa ifanyike na siyo vinginevyo. Wanasheria wako wanaweza kukuongoza zaidi.

## Rafiki yangu anatembea na mpenzi wangu

**Mimi ni msichana mrembo na niliyeelimika. Nina mpenzi ambaye tupo kwenye mahusiano kwa miaka mitatu. Hivi karibuni kuna mtu amenidokeza kwamba rafiki yangu wa karibu anatoka kimapenzi na mpenzi wangu. Ninakumbuka kipindi cha nyuma rafiki yangu alikuwa akimsifia mpenzi wangu na kumtamani. Kuna ujumbe wa kufurahisha ambao alikuwa anamtumia mpenzi wangu ukionyesha kwamba kuna kitu kinaendelea. Nataka nimfundishe rafiki yangu kwa kumshtaki kwa kuingilia maisha yangu. Anauvunja moyo wangu kitu ambacho ni sawa na kosa la jinai. Je, siwezi kupata zuio, kumzuia kutoka na mpenzi wangu? Ninawezaje kumrudisha mpenzi wangu kisheria? Tafadhali niongoze.**

*27 Agosti 2012*

Ingawa tunasononeka sana moyo wako kuvunjika, tafadhali elewa kwamba mwanamume unayetembea naye ni mpenzi tu na siyo mume wako. Ingawa kimaadili inaweza isiwe sahihi kwake kutembea na nyie wote wawili, hakuna sheria inayomzuia kutembea na mwanamke mwingine. Sheria ni tofauti na maadili, kwa bahati mbaya sana, hatujawahi kuona sheria inayozuia jambo hili.

Tabia za rafiki yako zinaweza kuwa za kikatili, zisizo na maadili na pengine zisikubalike; lakini siyo kinyume cha sheria na hivyo haiwezekani kushtaki. Sisi kama wanasheria hatuna utaalamu na masuala ya mahusiano na hivyo unaweza kufikiria kupata ushauri kuhusu mpenzi wako kama unaona anaweza kubadili tabia zake. Kinyume na hapo, huna jinsi, zaidi ya kuachana naye na kutafuta rafiki na mpenzi mwingine.

Zuio haliwezi kutolewa kwa sababu ulizoziainisha hapo juu. Rafiki yako havunji sheria kwa kutembea na mpenzi wako. Tuchukulie mpenzi wako na rafiki yako wanashiriki mapenzi, hakuna sheria inayomzuia yeye wala mtu mwingine yeyote kujihusisha kwenye mahusiano ya kimapenzi, ilimradi tu kama kuna idhini, wapenzi wana umri sahihi, na hakuna kitu kingine kisicho cha kawaida kwenye mahusiano hayo ya kimapenzi.

## Mama hawatunzi/kawatelekeza watoto

**Kuna mwanamke mmoja ambaye ana watoto wanne lakini hawatunzi Wanaonekana kuzurura na kulala maeneo ya Gymkhana. Je hakuna sheria inayowalinda watoto hao bila kujali kwamba ni mama yao**

**ambaye anawatesa?**

*15 Oktoba 2012*

Sheria ya Mtoto ina Vifungu ambavyo vinamtetea mtoto. Sheria hii ina muelezea mtoto kama ni mtu yeyote mwenye umri chini ya miaka kumi na nane na inaeleza kwamba maslahi ya mtoto yatakuwa ni zingatio la msingi katika masuala yote yanayohusiana na mtoto yanayosimamiwa na taasisi za umma au taasisi binafsi za ustawi wa jamii, Mahakama au mamlaka za kiutawala.

Sheria inatamka wazi kwamba mtoto atakuwa na haki ya kuishi na wazazi wake au walezi na kwamba mtu hatazuia haki ya mtoto kuishi na wazazi wake, walezi au familia na kukua katika mazingira salama isipokuwa kama itaamliwa na Mahakama kwamba kwa kuishi na wazazi au familia (a) kutasababisha madhara kwa mtoto; (b) kutamfanya mtoto apate manyanyaso makubwa; au (c) kutakiuka maslahi mapana ya mtoto. Kwa kuzingatia masharti ya kifungu hapo juu pale ambapo mamlaka husika yenye uhalali au Mahakama imeamua kwa mujibu wa sheria na taratibu husika kwamba ni kwa masilahi ya mtoto kumtenganisha kutoka kwa wazazi wake, mtoto atapewa matunzo/hifadhi/malezi bora mbadala yaliyopo.

Sheria pia inaeleza kwamba itakuwa ni wajibu wa mzazi, mlezi au mtu mwingine yeyote anayemlea mtoto kumtunza mtoto huyo na jukumu hilo linampa mtoto haki ya chakula, malazi, mavazi, huduma ya afya pamoja na kinga, elimu na muongozo, uhuru, na haki ya kucheza na kupumzika. Kutokana na maelezo hayo, tuna shauri utoe taarifa kwa afisa ustawi wa jamii wa eneo husika ili afanye uchunguzi husika na kupeleka maombi Mahakamani kwa maamuzi stahiki.

## Nyumba-ndogo/Kimada anataka pesa yangu

**Nilikuwa kwenye mahusiano kwa muda mrefu na mwanamke ambaye tuliachana hivi karibuni. Ili asimwambie yeyote kuhusu mahusiano yetu ikiwemo mke wangu, tuliingia mkataba kupitia mwanasheria kwamba nimlipe milioni 2.2 kila mwezi na kumlipia gharama za bima za matibabu. Makubaliano yalikuwa mwanamke huyo afunge mdomo wake na kwenda kuishi kwenye mji mwingine. Nimemlipa pesa hizo kwa miaka minne na sasa nipo kwenye hali mbaya ya kifedha, anasema nimevunja mkataba kwa kutokumlipa na anakusudia kunishtaki. Ninawezaje kukabiliana na hili. Je sijamzidishia malipo?**

*29 Oktoba 2012*

Jibu letu litajikita kwenye utekelezaji wa mkataba ambao mliingia na siyo iwapo ukishtakiwa mke wako atajua na hasa ndiyo sababu kubwa iliyokufanya uingie makubaliano hayo. Inaonesha ulitishwa na ulikuwa kwenye hali ya uoga wakati unaingia kwenye makubaliano hayo. Haijalishi kama wanasheria wako walihusika. Haijalishi pia kama umemlipa miaka kadhaa nyuma.

Maoni yetu ni kwamba mkataba huo ni batili kwa sababu unaenda kinyume na sera ya umma na uliingiwa kwa uoga baada ya kutishwa. Tukichukulia kwamba hujatuficha kitu, uwezekano wa mwanamke kushinda ni mdogo sana. Kama akikushtaki na wewe ufungue shtaka kinzani dhidi yake ukidai pesa zote ulizomlipa kwa miaka yote ya mkataba. Ili usije kuaibika, unaweza kufikiria kumJulaisha mkeo. Ila hilo ni hiari yako na pengine unaweza kufikiria kuonana na mshauri wa ndoa kabla hujamuambia mkeo.

Hakuna suala la kutosheleza kwa thamani, kwani tunaamini kwamba makubaliano hayo yalikuwa ni batili tangu mwanzo. Hivyo, Mahakama haitakwenda kwenye utoshelevu wa malipo.

## Ghiliba ya ndoa

**Nilikuwa na mpenzi kwa miaka minne lakini baadaye tuligombana na kila mmoja alikwenda njia yake kutokana na tofauti kubwa tuliyokuwa nayo. Baadaye alipata ugonjwa wa akili na hivyo niliamua kumtibia kwa sababu familia yake si wakazi wa Dar. Baada ya kupona, nilijikuta nimempenda tena, na kwa sababu hakuwa na kumbukumbu za iwapo nilichosema kilikuwa ni kweli ama la, akaendelea kuishi na mimi baada kumwambia kwamba tumeoana. Tumezaa watoto lakini sasa tumeanza tena matatizo. Siku moja baada ya mabishano nikamwambia ukweli na nikamfukuza nyumbani. Aliniripoti polisi na sasa nina kesi ya jinai. Inawezekanaje suala la mgogoro wa ndoa kama huu kuwa ni kesi ya jinai? Hivi polisi hawana kitu kingine cha kufanya?**

*19 Novemba 2012*

Suala lako ni la kipekee sana, amini usiamini, limeelezwa kwenye Kanuni ya Adhabu ambayo inatamka wazi kwamba mtu yeyote ambaye kwa makusudi na kwa kulaghai anamfanya mwanamke yeyote ambaye hakuolewa kihalali na yeye aamini kwamba ameolewa naye kihalali na akakaa naye kinyumba au akamwingilia mwanamke huyo huku akiamini kuwa ni mume wake amekosa na atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka kumi. Tunakushauri upate msaada wa kisheria kwa sababu suala lako siyo jepesi kama unavyolifikria.

## Haki ya mwanamke kwenye ndoa-dhahania

**Sikuwahi kuwa na ndoa rasmi lakini niliishi kwa furaha na mwanamume fulani kama mume wangu kwa miaka mitano hadi siku za hivi karibuni tulipoachana. Kipindi cha uhusiano wetu tulizaa watoto watatu na tulichuma mali kadhaa. Kwa masikitiko, hivi sasa tumetengana na mimi ninaishi kwenye moja wapo ya nyumba tulizojenga. Nimeshauriwa na rafiki yangu wa karibu kushtaki ili kupata talaka, mgawanyo wa mali pamoja na matunzo ya watoto. Hata hivyo watu wengine wanasema sitapata hata Shilingi kwa sababu hatukuwa na doa rasmi. Tafadhali nishauri.**

*26 Novemba 2012*

Sheria ya Ndoa inatamka kwamba ikiwa mwanamke na mwanamume wameishi pamoja kwa kipindi cha zaidi ya miaka miwili na kwa kipindi hicho wameishi kama mke na mume, kutakuwa na dhana inayoweza kukanushwa kwamba wameoana na hivyo kama mume wako wa zamani hana ndoa nyingine halali na jamii inayowazunguka inawachukulia kama mke na mume, kanuni ya ndoa-dhahania itatumika kwenye kesi yako. Unachotakiwa ni kuiridhisha Mahakama yenye mamlaka kwamba mmekuwa kwenye mahusiano kwa zaidi ya miaka miwili, watu walikuwa wanawachukulia kama mke na mume na kwamba mlichuma mali hizo kwa pamoja.

Kwenye dhana ya ndoa-dhahania, mwanamke atachukuliwa kama mke halali isipokuwa tu hataweza kupeleka maombi ya talaka au kutengana. Hivyo huwezi kupeleka maombi ya talaka au kutengana Mahakamani kwa sababu muunganiko wenu ulikuwa ni wa kidhahania tu. Hata hivyo sheria inakupa haki ya kuomba matunzo kwa ajili yako na mtoto. Una haki pia ya kuomba malezi/matunzo ya watoto mliowapata katika mahusiano yenu na nafuu nyinginezo, ikiwemo kugawana mali mlizochuma pamoja. Tunakushauri uwasiliane na mwanasheria wako kwa mwongozo zaidi.

## Gari aina ya Mercedes-Benz S-Class kwa ajili ya mke

**Mimi ni mwanamke mlimbwende sana, wengi wananitamani. Wanawake wengi**

**wanapinga ukweli huu, lakini nitakueleza wazi kwamba niliamua kuolewa na mtu tajiri. Kabla ya ndoa, aliahidi kuninunulia gari jipya aina ya Mercedes-Benz S-Class la mwaka 2011, gari ambalo hajaninunulia mpaka sasa. Anasema "amefulia", ingawa najua sio kweli, pengine anatumia faida ya kuwa tayari ameshanioa kutokutimiza ahadi yake. Je, ninaweza kufungua madai ya talaka kwa kuwa sitaki kuishi na mwanamume asiye mwaminifu? Naamini sheria inataka wanawake warembo kama mimi kuhudumiwa vizuri.**

*7 Januari 2013*

Sheria ya Ndoa ya Tanzania inatoa vigezo ambavyo vinapaswa kuzingatiwa katika kudai talaka pale ambapo ndoa inapokuwa imevunjika bila uwezekano wa kurekebishika. Sababu zifuatazo zimetolewa: (a) uzinzi uliofanywa na mmoja wa wanandoa, hasa kama tendo la uzinzi limefanyika zaidi ya mara moja au kutokoma kwa tabia hii licha ya kuonywa; (b) tabia ya uzinzi kwa upande wa mlalamikiwa; (c) ukatili, uwe wa kiakili au wa kimwili, unaosababishwa na mlalamikiwa kwa mlalamikaji au kwa watoto; (d) kupuuzwa kwa makusudi kwa mlalamikiwa; (e) mlalamikiwa kumtelekeza mlalamikaji kwa kipindi cha angalau miaka mitatu, na Mahakama imethibitisha kwamba ni kwa makusudi; (f) kutengana kwa hiari au kwa amri ya Mahakama, ambapo utengano huo umeendelea kwa angalau miaka mitatu; (g) kifungo cha maisha kwa mlalamikiwa au kipindi kisichopungua miaka mitano, kwa kuzingatia urefu wa muda wa kifungo na hali ya kosa ambalo alihukumiwa nalo; (h) ugonjwa wa akili kwa mlalamikiwa, ambapo angalau madaktari wawili, mmoja wao awe aliyehitimu au awe na uzoefu wa ugonjwa wa akili, kuwe na uhakikaa kuwa hakuna tumaini la kutibika au kupona kwa mlalamikiwa; (i) kubadilisha dini kwa mlalamikiwa, ambapo pande zote wakati wa ndoa walikua na imani moja na ambapo kwa mujibu wa sheria za imani hiyo, kubadilisha dini kunafuta ndoa au ni moja ya misingi ya kutengua ndoa.

Kutokana na maelezo hapo juu, ni dhahiri kwamba kukosa kwako Mercedes hakujitoshelezi kuingia kwenye vigezo vilivyoainishwa hapo juu. Hakika kutokununuliwa Mercedes Benz hakuwezi kuchukuliwa kuwa ni ukatili. Ikiwa unaomba tu talaka kwa sababu ya kutokununuliwa Benz, tunadhani huenda usifanikiwe kupata talaka hiyo. Tukudokezee tu kwamba katika nchi nyingine, tofauti na Tanzania, madai ya talaka yanaweza kufunguliwa kwa idhini ya pande zote. Kwa Tanzania, hali ni tofauti kwa kuwa hamuwezi kukubaliana kwenda Mahakamani kuomba talaka. Ni kweli Sheria ya Ndoa ipo nyuma ya wakati, lakini bado inabaki kuwa ni sheria nzuri hata leo. Mwisho, sheria haitofautishi wanawake wazuri na wanawake wabaya - kwanza uzuri wa mtu upo machoni pa mtazamaji. Mwanasheria wako anaweza kukuongoza zaidi.

## Harusi/Ndoa ya siri na kutokutoa taarifa

**Ninataka kuoa lakini nataka harusi/ndoa ya faragha sana. Sitaki kuujuza umma kuhusu nia yangu ya kutaka kuoa na sitaki mtu yeyote kuhudhuria ibada ya ndoa. Mimi ni mtu msiri sana na hivyo ningependa kujua kama sheria za Tanzania zinaruhusu sherehe hizo.**

*7 Januari 2013*

Sheria ya Ndoa inatamka bayana kwamba pale mwanamume na mwanamke wanapotaka kuoana, watatoa taarifa angalau siku ishirini na moja kabla ya siku wanayopendekeza kufunga ndoa. Hata hivyo, Msajili Mkuu anaweza, kwa leseni na kwa fomu maalum, kuondoa sharti la utoaji taarifa, kama inavyotakiwa chini ya sheria ikiwa, tu, ameridhika kwamba watu hao

hawako kwenye mahusiano yaliyozuiliwa, hakuna kipingamizi cha ndoa nyingine, watu hao hawako chini ya umri wa ndoa na ikiwa ni chini ya umri, basi idhini inayohitajika imepatikana na Msajili Mkuu lazima ajiridhishe kwamba, kuna sababu nzuri, na za kutosha kufanya hivyo.

Kwa hiyo inawezekana kuondokana na suala la kutoa taarifa kama inavyotakiwa chini ya sheria iwapo tu umetimiza masharti yanayotakiwa na pia Msajili Mkuu ameondoa sharti hilo la kutoa taarifa. Hata hivyo, sheria iko wazi kwamba mtu yeyote anaweza kuhudhuria sherehe ya ndoa ya kiserikali, hivyo hatuamini kama unaweza kuwa na sherehe ya ndoa binafsi; hata hivyo unaweza kufanya harusi ya faragha na idadi ndogo ya watu au unaweza kuamua kutokukaribisha mtu yeyote kwenye harusi yako na kufurahia wewe mwenyewe.

## Mume anataja majina ya vimada wake ndotoni

**Nimekuwa kwenye ndoa kwa miaka 12 hivi sasa na kwa kipindi cha miaka 3 iliyopita nimekuwa na shaka kwamba mume wangu amekuwa kwenye mahusiano na mwanamke fulani aliyekuwa akifanya nae kazi huko nyuma. Imekuwa vigumu kuthibitisha hili na daima amekuwa akikanusha. Wiki chache zilizopita, wakati amechoka sana kutokana na safari ya ughaibuni, mume wangu alitamka jina la mwanamke karibu mara tatu hivi akiwa usingizini. Nataka kudai talaka. Nifanye nini?**

*4 Machi 2013*

Sababu za kuomba talaka ni pamoja na ukatili na uzinzi ambazo husababisha ndoa kuvunjika pasipo kurekebishika. Kumtuhumu tu mmeo kwa kutaja jina la mwanamke mwingine usingizini siyo uzinzi. Ndoto ni ndoto - wakati mwingine upata njozi za kifo, wakati mwingine ajali, na wakati mwingine mizimu. Njozi nyingi si za kweli, hivyo ndivyo tunavyoamini. Unaweza kumpa faida ya shaka na kujadili hili na mshauri wa ndoa. Kwa vyovyote vile, katika maandalizi yako ya kudai talaka, ambayo unaonekana kusisitiza, unapaswa kushauriana na wanasheria wako.

## Ndoa ya jino la dhahabu

**Nilimuoa msichana ambaye nilimpa jino la dhahabu. Ili kuonesha upendo wetu, jino lake moja liliondolewa na kubadilishwa ili kuweka jino la dhahabu. Wakwe zetu wameharibu ndoa yetu na tumekuwa na ugomvi kila siku. Anataka talaka na nipo tayari kumpa lakini kwa sharti kwamba anipe jino langu la dhahabu au alinunue kutoka kwangu. Unawezaje kunisaidia?**

*1 Aprili 2013*

Jino ulilompatia ilikuwa ni kama zawadi ya ndoa na harusi kwa mke wako na likawa ni kama sehemu ya mali zake binafsi, na hivyo hakuna uwezekano wa kurudishiwa. Hata kama unaweza, itamaanisha kuling’oa kutoka kinywani mwa mkeo, kwa sababu kwa sasa limeshakuwa sehemu ya mwili wake. Kuna mamia ya kesi za kigeni ambazo zimewahi kuhoji iwapo jino la bandia ni sehemu ya mwili au la, na nyingi zake zimeamua kwamba jino bandia ni sehemu ya mwili wako baada ya kuwekwa.

Kwa kuzingatia hili, kuondolewa kwa jino ni kinyume na sera ya umma na tunaamini hakuna uwezekano kwamba unaweza kurudishiwa jino lako. Iwapo kama linaweza kuondolewa kwa urahisi, ulimpa kwa masharti gani, ikiwa ni pamoja na jino lake lililotolewa (ikiwa utashinda kesi dhidi yake) na kadhalika. Yote kwa yote, inaonekana una kesi ngumu dhidi ya mkeo. Labda kama unaweza kumpa punguzo na anaweza kununua, vinginevyo itakuwa vita kubwa ya kisheria Mahakamani.

## Ugomvi juu ya malezi ya watoto

**Mimi ni mwanamke ninayeishi Dar es Salaam. Miaka miwili iliyopita nilizaa mtoto wa kike ambaye baba yake mzazi ni mwalimu anayeishi Mwanza. Miezi nane baada ya kumzaa mtoto huyu nilisafiri nje ya nchi kibiashara. Nilimwacha mwanangu na bibi yake (mama wa baba wa mtoto) anayeishi Morogoro. Baada ya kurudi Tanzania nilikwenda kumchukua mtoto wangu lakini bibi amekataa kabisa kuniruhusu kumchukua mtoto wangu. Jibu analonipa ni kwamba, kulingana na mila zao siwezi kuishi na mtoto mpaka niolewe. Binafsi sina nia ya kuolewa kwa sababu huko nyuma niliwahi kuwa katika ndoa mbaya. Nifanye nini?**

*8 Aprili 2013*

Kisheria mtoto ana haki ya kuishi na wazazi wake. Haki hii imetolewa wazi chini ya Sheria ya Mtoto, Na. 21 ya 2009. Vivyo hivyo, kama mzazi pia una haki ya kumlea mwanao. Ikiwa bibi hataki kukuruhusu kumchukua mtoto wako tunakushauri kupeleka maombi Mahakamani ili kupata malezi ya mtoto. Chini ya Sheria ya Mtoto kuna dhana inayoweza kubatilishwa kwamba inafaa mtoto aliye chini ya umri wa miaka saba kulelewa na mama yake, ili kuamua iwapo dhana hiyo itumike kwenye mazingira fulani, itategemea na maelezo ya kesi husika lakini Mahakama itazingatia haja ya kutokumsumbua mtoto kwa kubadilisha mlezi.

Kwa kuwa hakuna mazingira ya usumbufu huo kwa malezi bora ya mwanao, tunadhani Mahakama itatumia dhana hiyo na kuamuru mtoto alelewe na mama yake. Mila ambazo bibi yake anazizungumzia hazipaswi kukuzuia kumlea mtoto wako. Unabaki kuwa mama mzazi wa mtoto labda kama kuna sababu nyingine ambazo hujatushirikisha, unastahili kupata matunzo ya mtoto (kutoka kwa baba). Zaidi ya hayo, ndoa kama taasisi ni uhusiano ambao watu wanapaswa kuingia kwa hiari yao wenyewe. Kwa hiyo sababu kwamba haujaolewa na baba wa mtoto wako haitoshelezi kukunyima haki yako ya kumlea mwanao. Mwanasheria wako anaweza kukuongoza zaidi.

## Uthibitisho wa baba wa mtoto

**Ninakabiliwa na hali isiyo ya kawaida ambayo inaniondolea furaha yangu. Nimekuwa na uhusiano wa kimapenzi na mwanamke mmoja kwa muda mrefu, na baadaye alipata ujauzito. Kwa bahati mbaya, alifariki wakati wa kujifungua. Bahati nzuri mtoto alipona. Baada ya mazishi, mwanamume mwingine alijitokeza na kudai kuwa yeye ndiye baba halisi wa mtoto na ule ujauzito wa marehemu ulikuwa ni wake. Ninaamini mimi ndiye nilikuwa mwanamume pekee kwake, na ndiye pekee niliyekuwepo wakati akijifungua. Kila mmoja wetu anadai kuwa ndiye baba, na ninaamini huyu mwanamume aliyejitokeza amepandikizwa tu. Je, sheria inasemaje kwenye hali kama hiyo? Vipi kuhusu gharama nilizotoa wakati wa ujauzito, ninawezaje kurudishiwa gharama zangu iwapo itabainika kuwa mtoto siyo wangu? Ninaweza kuruhusiwa kumtunza mtoto?**

*13 Mei 2013*

Masuala yanayohusu baba mzazi na matunzo ya watoto yanashughulikiwa na Sheria ya Mtoto, Na. 21 ya 2009. Sheria hii inatoa fursa kwa mtoto, mzazi, mlezi, afisa ustawi wa jamii au mtu yeyote mwenye maslahi na mtoto, kwa ruhusa maalum ya Mahakama, kupeleka maombi mahakamani ili kuthibitisha baba wa mtoto.

Sheria hii pia inaeleza namna ambavyo maombi haya yanatakiwa kufanywa. Inaruhusu maombi hayo kufanyika kabla mtoto hajazaliwa, baada ya kifo cha baba au mama wa mtoto, kabla mtoto hajafikia

umri wa miaka 18, au kwa ruksa maalum ya Mahakama, baada ya mtoto kufikisha umri wa miaka 18.

Kuhusu kurudishiwa gharama za wakati wa ujauzito, na mama wa mtoto akiwa amekwishafariki, hatuna uhakika utamshtaki nani ili akurudishie gharama hizo. Hakuna uwezekano wa shtaka lako kufanikiwa dhidi ya baba halisi wa mtoto, lakini wanasheria wako wanaweza kukuongoza zaidi.

Swali kuhusu malezi ya mtoto linahitaji umakini zaidi. Lengo kuu la sheria ni kuhakikisha kwamba maslahi bora ya mtoto yanazingatiwa. Kama mtoto ni wa kwako kweli, uwezekano ni mkubwa wa kuruhusiwa kumlea mtoto, baada ya kuzingatia uwezo wako wa kumtunza na kumlea, uwezo wa kifedha, n.k.

Inafahamika kwamba mtoto anaweza kulelewa vizuri zaidi na mwanamke kuliko mwanamume. Hivyo, uwepo wa mama yako au mwanamke mwingine kwenye familia yako mwenye uwezo wa kutoa mwongozo wa malezi au msaada stahiki, itasaidia sana iwapo kutakuwa na mgogoro juu ya malezi ya mtoto.

## Kuchanwa kwa hati za ndoa

**Bila mimi kujua, mwanangu wa kiume wa miaka 20 alikuwa anatembea na mwanamke ambaye anamzidi kama miaka 15 hivi. Mwanamke huyo alifanikiwa kumshawishi mwanangu amuoe na walikwenda kufunga ndoa ya Serikali jijini Dar es Salaam. Kwa bahati nzuri, dreva wangu ambaye nimekuwa nae kwa miaka 30, ndiye aliyemwendesha mwanangu mpaka sehemu ambayo walitakiwa kusaini hati za ndoa. Alihisi kuna kitu hakiendi sawa na hivyo akanipigia simu. Kwa haraka nilikwenda na kuingia kwenye ofisi ambayo zoezi la kutia saini lilikuwa likifanyika na sikuamini kumbe walikuwa wameshasaini. Nilichukua hati zile na kuzichanachana huku nikimwambia Msajili tatizo lililopo. Nina maswali mawili; moja inawezekana mwanamke mzee kama yule akamrubuni mtoto huyu wa miaka 20? Mbili, kwa kuwa hati zilichanwa na hivyo hakuna ushahidi wa ndoa, je ndoa hii bado ni halali?**

*24 Juni 2013*

Kwa kuanzia, mwanao yupo juu ya umri wa kisheria wa kuoa, hivyo wewe ujue au usijue, bado yeye anaweza kuoa. Hata hivyo, tunaelewa hisia zako kwamba kwa umri wake anaweza kuwa bado ni mdogo na hasa kuwa katika ndoa na mwanamke ambaye amemzidi sana umri. Ndoa ilifanyika pale walipokwenda kwa Msajili na kusaini hati zilizowekwa mbele yao na tunachukulia hati hizo zilishuhudiwa vyema. Inaonekana hilo lilifanyika hivyo wakati unaingia chumbani, mwanao alikuwa tayari ameshaoa. Kuchana tu hati za ndoa hakumaanishi kwamba ndoa imebatilishwa au haikufungwa. Ndoa bado ipo na namna pekee mwanao anaweza kutoka kwenye ndoa hiyo ni kufungua talaka. Hivyo kama mwanao atatoa au anahitaji talaka ni uamuzi wake na siyo wako. Wanasheria wako wanaweza kukuongoza zaidi.

## Hadhi ya ndoa ya kimila

**Mimi na mchumba wangu ni wakristo lakini mchumba wangu anataka kwanza tufunge ndoa ya kitamaduni kabla ya ndoa ya kanisani. Je, hilo linawezekana? Madhara yake ni yapi? Je, ndoa ya kimila inatambulika Tanzania?**

*1 Julai 2013*

Sheria ya Ndoa inatambua ndoa za kimila, kidini na kiserikali. Ndoa za kimila ndiyo hizo unazoziita ndoa za kitamaduni; ndoa za kidini ni zile zinazofungwa kidini, yaani, kiislamu, kikristo, kihindi n.k. Ndoa za kiserikali ni zile zinazofungwa na maafisa wa Serikali walioruhusiwa. Tanzana inatambua

ndoa za kimila na zina hadhi sawa na ndoa nyingine zozote yaani, za kiserikali na kidini. Unatakiwa kufahamu kwamba ndoa za kimila zinachukuliwa kama ni ndoa za wake wengi na hivyo anaweza kuoa mke zaidi ya mmoja na hivyo hivyo wewe unaweza usiwe mke pekee. Sheria ya Ndoa inatamka kwamba ndoa iliyofungwa Tanganyika (Tanzania Bara) inaweza kubadilishwa, kama mwanamume alikuwa na mke mmoja, kutoka ndoa ya mke mmoja kwenda wake wengi, kwa tamko maalum lililotolewa na mume na mke, kwamba wote kwa hiari yao wenyewe wamekubali mabadiliko hayo. Tamko hilo litatolewa mbele ya Jaji, Hakimu Mkazi au Hakimu wa Wilaya na litakuwa la maandishi, litasainiwa na mke na mume na mbele ya mtu anayeshuhudia wakati wa kulitoa.

Unatakiwa uelewe kwamba, hakuna ndoa inayoweza kubadilishwa, kutoka mke mmoja kwenda wake wengi na kutoka wake wengi kwenda mke mmoja kwa namna nyingine zaidi ya njia ya tamko kama ilivyoelezwa hapo juu. Hivyo kama mtaoana kwa ndoa ya kimila, ni lazima muibadilishe kuwa ndoa ya mke mmoja kwanza ndipo muendelee kuoana kanisani isipokuwa kwamba mmeo hatakiwi kuwa na mke mwingine kwa sababu kubadili kwenda ndoa ya mke mmoja hakutakuwa halali kama mmeo atakuwa na mke zaidi ya mmoja. Kama mtaoana kwa ndoa ya kikristo wakati ana mke mwingine, ndoa ya kikristo haitakuwa halali kwa sababu ndoa ya kimila itakuwa juu ya ndoa ya kikristo. Tunapendekeza umuulize kwa nini anataka kwanza ndoa ya kimila. Pia tunashauri nyote mumtafute mtaalam wa masuala ya ndoa.

## Kupata taarifa za simu

**Nadhani mke wangu anafanya udanganyifu kwa sababu wakati wote ametingwa sana na simu yake. Nilijaribu kupata meseji na historia ya miito kutoka kampuni ya simu anayotumia lakini walikataa kwa sababu kwamba taarifa hizo ni za siri na hawawezi kuzidukua/kuzivujisha kwangu. Ninawezaje kupata taarifa hizo kutoka kampuni ya simu? Tafadhali elewa, ninahitaji kuzipata bila yeye kujua. Napenda kuuliza pia, je kupiga busu ni uzinzi? Je, inawezekana mtu anayezini na mke wangu kuunganishwa kwenye kesi ya talaka?**

*16 Septemba 2013*

Kanuni za Mawasiliano (Ulinzi kwa Mtumiaji) zinatamka mwenye leseni kutofuatilia wala kutoa maudhui ya taarifa zozote za mteja zinazopitia kwenye mfumo uliopewa leseni, isipokuwa kama inavyotakiwa na kuruhusiwa na sheria inayotumika. Hivyo kampuni ya simu ipo sahihi kukuzuia kupata kumbukumbu za simu za mke wako.

Unatakiwa pia kuelewa kwamba haki ya faragha inalindwa na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kisheria, kampuni za mawasiliano zitawajibika kutoa taarifa hizo kama mwenye namba ataziomba au kwa amri ya Mahakama yenye mamlaka husika au kama polisi wanazihitaji kwa malengo ya kiuchunguzi.

Kama unaona ni lazima kwako kuthibitisha iwapo mke wako ni mwaminifu au siyo, tunakushauri uwasiliane na mkeo ili aiombe kampuni ya mawasiliano impatie taarifa zake za mawasiliano ambazo unaweza kuziangalia, vinginevyo, hakuna uwezekano kwamba Mahakama itatoa amri hiyo kwa sababu za udanganyifu pekee. Maelezo yako yanayofuata ni kwamba mke wako ambaye siyo mwaminifu (au mume kwa maana hiyo) hatoi ushirikiano kwa mwenzi wake. Hilo ni kweli na kwa bahati mbaya mke na mume wanachukuliwa tofauti pale linapokuja suala la faragha.

Kuhusu swali lako la pili, iwapo kubusu ni uzinzi. Kwa bahati nzuri au mbaya, uzinzi haujafafanuliwa kwenye Sheria ya

Ndoa ya Tanzania. Kupiga busu nako pia hakujafafanuliwa kwa sababu unaweza kuwa na busu la mdomo, shavuni na aina nyingine za busu, na baadhi yake zinategemea na aina ya mila na desturi za mahala ambapo mtu anaishi. Wakati mwingine zinaweza kuwa kitu cha kawaida bila kuchukuliwa kama ni uzinzi. Kwa mfano pale busu la mdomo linapochukua muda mrefu kidogo inaweza kuchukuliwa ni dalili za wazi kwamba mahusiano ya kiuzinzi yapo, wakati busu la shavu ni la kawaida siku hizi. Ni ngumu kukujibu swali lako bila kujua aina ya busu, muda, mara ngapi, watu wanaohusika n.k. Mara nyingi, ngono ya aina yoyote huchuliwa kama uzinzi.

Mwisho, ni iwapo mtu anayehisiwa kutembea na mkeo anaweza kuunganishwa kwenye maombi ya talaka, jibu ni ndiyo lakini kwa maelekezo ya Mahakama husika unaweza kumuunganisha mtu huyo kama mdaiwa mwenza. Unaweza pia kudai fidia kutoka kwa mtu huyo. Tunakushauri uwasiliane na mwanasheria wako kwa mwongozo zaidi.

## Mume anafuga ndevu na kuvaa hereni mbili

**Nimeolewa na mwanamume ambaye nimekuwa kwenye mahusiano naye kwa zaidi ya miaka kumi. Tulioana mwaka jana na ghafla ameamua kufuga ndefu na kuvaa hereni mbili, kitendo ambacho kinamwondolea mvuto na hivyo kunikera. Mwanzoni nilidhani ni utani, sasa chaguo liko wazi kati ya ndevu zake na talaka. Jambo hili ni la kushangaza lakini ndiyo ukweli wenyewe. Nimekubali matokeo na sitaki kuendelea tena. Hata hivyo mwanasheria wangu anasema kupata talaka kwa sasa na kwa sababu hizo haiwezekani. Hata hivyo, huyu ni mwanasheria yule yule ambaye mume wangu anamtumia na anaweza kuwa na maslahi binafsi. Je, ushauri wa mwanasheria huyu ni wa kweli? Tafadhali niongoze.**

*9 Desemba 2013*

Ni kweli Sheria ya Ndoa ya Tanzania imepitwa na wakati na hairuhusu talaka ya maridhiano. Sheria inataka kwamba ni lazima kuwe na sababu, miongoni mwazo ni , uzinzi, tabia za kingono zisizokubalika n.k. ili uwe na sababu halali za kuomba talaka. Muonekano au mabadiliko ya muonekano, kama ilivyo kwa kesi yako hapa, siyo sababu ya msingi ya kuomba talaka na haiwezi kutolewa chini ya sheria zetu.

Kwa kuwa ndoa yako ipo chini ya miaka miwili, isipokuwa kama unaweza kuthibitisha ugumu wa kipekee, sheria inazuia talaka ndani ya muda huo. Kuna kama kipindi cha kupoa/mpito ambacho, kwa miaka ya sasa, kimsingi kimepitwa na wakati.

Ziko juhudi za kubadilisha sheria yetu ya ndoa lakini kwa sasa huo ndiyo ukweli. Tunakushauri uwasiliane na mshauri wa ndoa ili aweze kuzungumza na nyote wawili juu ya jambo hili. Tunakutakia kila la heri.

## Picha za harusi magazetini

**Mimi ni mtu maarufu sana na nilifunga ndoa na kufanya harusi ya kifahari. Wakati wa harusi, baadhi ya mapaparazi/wapiga picha walijipenyeza na kunipiga picha. Nilitokea kwenye magazeti yote makubwa/maarufu na sasa mpenzi wangu/kimada amekasirika kuhusu ndoa yangu na mwanamke huyu mpya. Je, mnaweza kunisaidia? Ninaweza kuwashtaki wenye magazeti?**

*10 Machi 2014*

Hatujui ni msaada gani unahitaji kutoka kwetu. Kinachotuchanganya zaidi ni kwamba umeoa na bado unaendeleza mahusiano na mpenzi wako/kimada, ikiwa na maana kuwa una mahusiano ya kizinzi nje ya ndoa. Bila kujali kama wewe ni maarufu na kama hujui, uzinzi ni sababu mojawapo ya talaka na anayepaswa kukasirika ni mke wako na siyo mpenzi wako. Unatakiwa kukumbuka kiapo chako kwenye ndoa na unahitaji kuonana

na mshauri wa masuala ya ndoa na siyo wanasheria.

Kuhusu wapiga picha/mapaparazi, kwa taarifa chache tulizonazo kukuhusu, hatujui iwapo umekashfiwa au haki yako ya faragha imeingiliwa. Inavyoonesha, lalamiko lako kubwa ni kwamba mpenzi wako hana furaha na ndoa yako hiyo, jambo ambalo halikupi haki ya kuwashtaki wenye magazeti. Vile vile unadai kwamba wewe ni maarufu na kama ni kweli wewe ni maarufu kama unavyofikiria pia itakuwa ni ngumu kwako kuwashtaki wenye magazeti kwa shtaka la kukashfu. Watu maarufu wapo kwenye macho ya umma na ni lazima utegemee mambo kama haya kutokea. Tunakushauri uwasiliane na mshauri wa ndoa na pengine Mchungaji. Unahitaji kuelewa maana hasa ya kuwa kwenye ndoa. Wanasheria wanaweza wasiwe na msaada mkubwa katika hili lakini unaweza kuwajaribu pia.

## Kumwakilisha mtu kwenye ndoa

**Mimi ni mtu mwenye shughuli nyingi na ninafanya kazi kwenye kampuni kubwa sana nje ya Tanzania. Mchumba wangu anasisitiza tuoane chini ya sheria za Tanzania, kwangu ni vigumu sana kupata muda huo. Ninaweza kujaza fomu zangu za ndoa na kuzituma kwa Msajili Jijini Dar es Salaam na hivyo kutufungisha ndoa? Ninajua nchi nyingine zinaruhusu aina hizo za ndoa ambapo huhitaji kuwepo moja kwa moja. Katika namna nyingine, je kaka yangu anaweza kuhudhuria na kusaini cheti cha ndoa kwa niaba yangu kwa kutumia hati ya uwakilishi. Ninawezaje kuoa bila kufika Tanzania?**

*24 Machi 2014*

Ingawa tunafurahi kwamba una shughuli nyingi na unafanya kazi kwenye kampuni kubwa, ni lazima uwepo kwenye chumba cha kusaini vyeti vya ndoa. Huwezi kuwa kwenye ukumbi wa mkutano, Skype au kutuma karatasi zako. Ndoa ni tendo takatifu na Sheria ya Ndoa inaeleza kwa uwazi kwamba ni lazima uwepo na inatamka kwamba ndoa itakuwa batili iwapo pande zote mbili hazitakuwepo zenyewe wakati wa ndoa. Hatujawahi kusikia nchi inayoruhusu ndoa ya uwakilishi au masafa marefu.

Kuhusu kaka yako kuhudhuria ndoa, tafadhali elewa kwamba huwezi kumpa kaka yako hati ya uwakilishi kusaini vyeti vya ndoa. Kwa jinsi tunavyojua, iwapo atasaini, ataishia kuwa mume wa mchumba/mpenzi wako. Hata hivyo, wanasheria wako wanaweza kukuongoza zaidi.

## Uhanithi na ndoa

**Niliolewa na mwanamume kwa ndoa ya kutafutiwa mume, lakini nimekuja kung’amua kwamba ni hanithi. Ingawa ninatamani sana kumsaidia, lakini jambo hili haliwezekani kwa sababu hali yake haitibiki. Je, ndoa hii inaweza kusimama/ kuendelea?**

*24 Machi 2014*

Kwa ujumla uhanithi ni hali ya kimwili au kisaikolojia ambayo inamfanya mwenza kushindwa kushiriki tendo la ndoa. Hata hivyo, kukataa kufanya mapenzi na mwenzi wako siyo uhanithi, wala kushindwa kuzaa pia siyo uhanithi.

Kwa ujumla, iwapo utapeleka maombi ya talaka dhidi ya mpenzi wako kwa sababu za uhanithi, utahitaji kuthibitisha. Jambo hilo litakutaka uiombe Mahakama kumlazimisha mwenzi wako kufanyiwa uchunguzi wa kimwili na kisaikolojia na wataalamu wa afya waje kuthibitisha. Kifungu cha 39 cha Sheria ya Ndoa nchini Tanzania kinatamka kwamba kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 97 na 98, ndoa itakuwa batili iwapo: (a) wakati wa/ baada ya ndoa (i) upande wowote kushindwa

kushiriki tendo la ndoa; au (ii) upande wowote unaugua ugonjwa wa akili au kifafa; au (iii) mmoja wa wanandoa kudhihirika kuwa alikuwa na ugonjwa wa zinaa; au (iv) mwanamke kudhihirika kuwa alikuwa na mimba ya mwanamume mwingine; au (b) mwanandoa mmoja kukataa kwa makusudi kushiriki tendo la ndoa tangu ndoa ilipofungwa; au (c) mwanamke hajatimiza umri wa miaka 18 na ridhaa iliyotakiwa kutolewa chini ya kifungu cha 17 haijatolewa na Mahakama inaona kuna sababu nzuri za kutengua ndoa. Kifungu cha 40, ndoa batilifu itaendelea kuwa ndoa halali hadi hapo Mahakama itakapoitengua.

Kutokana na maelezo hapo juu, unaweza kuona kwamba kwa kuwa mume ameshindwa kushiriki tendo la ndoa, ndoa itakuwa batilifu, yaani, inaweza kutenguliwa na hivyo unaweza kuomba talaka. Sheria haisemi kwamba ndoa hiyo ni batili, yaani haipo tokea mwanzo, ikiwa na maana kwamba huwezi kuomba talaka. Wanasheria wako wanaweza kukuongoza zaidi.

## Kukataa kuongeza mke mwingine katika ndoa ya mitala

**Mimi ni mmoja wa wake wawili wa mwanamume fulani. Mume anatutegemea sana ili kuweza kuishi. Mimi mwenyewe nafanya kazi kwa bidii kwa ajili ya familia yetu. Cha kushangaza, mume wetu anataka kuongeza mke mwingine. Tumemkatalia lakini anasisitiza kwamba sisi sote tumeolewa kwenye ndoa ya mitala na hivyo hatuwezi kumzuia. Nina hofu juu ya ndoa yake mpya kwa sababu mwanamke anayetaka kumuoa afya yake inatiliwa mashaka. Tumetonywa kwamba tangazo la kusudio la kufunga ndoa limeshatolewa kwenye ofisi ya Msajili. Je, kuna namna ya kuepuka au kuzuia ndoa hii?**

*31 Machi 2014*

Kifungu cha 20 cha Sheria ya Ndoa kinazungumzia hali kama yako. Kifungu hicho kinatamka kwamba iwapo mwanamume aliyefunga ndoa ya wake wengi/mitala anatoa tangazo la kusudio la kufunga ndoa, mke wake, au kama ana mke zaidi ya mmoja, yeyote kati ya wake zake anaweza kuweka pingamizi kwa Msajili au afisa msajili ambaye tangazo la kufunga ndoa limetolewa kwa misingi kwamba kwa kuzingatia hali ya kipato cha mume, kuoa mke mwingine kunaweza kupelekea ugumu wa maisha usiomithilika kwa mke au wake zake wa sasa na watoto kama wapo; au mwanamke anayekusudia kumuoa ni mwenye tabia mbaya au anaugua magonjwa ya kuambukiza au ya zinaa au anaweza kuleta ugomvi/kutoweka utulivu. Mara pingamizi linapotolewa kwa Msajili au afisa msajili, ndoa hiyo haitafungwa mpaka pingamizi hilo litakapoamuliwa na Baraza la Usuluhishi wa Ndoa.

Tunashauri wewe na mke mwenzio kufuata njia iliyoelezwa hapo juu. Hili pia linaweza kutatuliwa na wazee kwenye ukoo wako. Vinginevyo unaweza kuwasiliana na mshauri wa masuala ya sheria za familia kwa hatua stahiki.

## Ndoa za jinsia moja nchini Tanzania

**Tumefunga ndoa ya jinsia moja na tunataka kutembelea Tanzania wakati wa siku za mapumziko. Ninataka kujua, je ndoa za jinsia moja zinaruhusiwa nchini Tazania?**

*31 Machi 2014*

Ndoa za jinsia moja haziruhusiwi kabisa nchini Tanzania. Sheria ya Ndoa inatambua ndoa kama ni muunganiko wa mwanamke na mwanamume na siyo mwanamume na mwanamume mwingine. Jambo hilo pia ni geni kwenye tamaduni za kitanzania na linachukuliwa kuwa ni utovu/ukosefu wa maadili. Mahusiano kama hayo ya mwanamume na mwanamume

yanaadhibiwa vikali chini ya Sheria ya Kanuni ya Adhabu.

Ingawa hauzuiliwi kuja nchini Tanzania, lakini tunakushauri kuwa makini na tabia na vitendo vyako. Unaweza kuwasiliana na mwanasheria wako kuhusu nini cha kufanya na cha kutokufanya.

## Akaunti ya pamoja ya mke na mume

**Mimi na mume wangu tumefungua akaunti ya pamoja benki Jijini Dar. Mimi pekee ndiye ninayefanya kazi kwenye familia na mume wangu hafanyi kazi yoyote na anatumia muda wake mwingi kuangalia televisheni. Kwa bahati mbaya nimekuwa nikiweka fedha kwenye akaunti ya pamoja kwa muda wa miaka 7 na sasa ninahitaji kuchukua fedha zangu. Mume wangu anakataa kusaini fomu ya kuchukua fedha iwapo sitampatia nusu ya fedha hizo. Benki haitaki kutoa fedha kwangu peke yangu. Ninaweza kuishtaki benki?**

*21 Aprili 2014*

Upo kwenye hali tatanishi sana. Umeweka fedha zako ulizozipata kwa shida kwenye akaunti ya pamoja. Kisheria, akaunti ya pamoja ni deni la wamiliki wote wa akaunti ya pamoja. Kuna kesi moja iliwahi kuamuliwa kwamba sababu tu kwamba mmoja wa wamiliki wa akaunti hachangii hakumzuii mtu huyo kunufaika. Benki ipo sahihi kwamba fedha zinamilikiwa kwa pamoja na haziwezi kutolewa kwako peke yako. Hatuoni namna ya kufanikiwa iwapo utaishtaki benki. Hata hivyo unaweza kuwasiliana na wanasheria wako kwa mwongozo zaidi.

## Idhini ya mwenza wakati wa kutengana

**Nilikwenda benki kuomba mkopo na niliulizwa iwapo nimeoa. Niliwaarifu nimeona lakini tumetengana kwa miaka minne sasa. Benki ilikubali kunipa mkopo kwa sharti kwamba niweke dhamana nyumba yangu. Hata hivyo, benki inataka ridhaa ya mke wangu na haitaki kuelewa kwamba mimi na mke wangu tumetengana. Nahitaji sana mkopo huu. Nifanye nini?**

*12 Mei 2014*

Sheria ya Ndoa inatambua kwamba ingawa mali inaweza kuwa kwa jina la mwenza mmoja, mwenza mwingine anaweza kuwa na mchango katika kupatikana, kusimamia na/au kulinda mali hiyo ingawa maslahi yake kwenye mali hiyo yanaweza yasiwe yamesajiliwa. Kuna kesi moja maarufu ambapo Mahakama ilikuwa na maoni kwamba hata kazi za ndani/nyumbani zinazofanywa na mke zinachukuliwa/zinahesabika kama mchango wake katika kupatikana na kusimamia mali ya familia.

Sheria ya Ardhi inazitaka taasisi za fedha kupata ridhaa ya mwenza kabla ya kukubali mali ya ndoa kuwa dhamana ili kulinda maslahi ya mwenza mwingine. Sheria ya Ndoa inatambua kwamba wanandoa wanaweza kuwa wametengana, ama kwa amri ya Mahakama au kwa hiari yao wenyewe. Hata hivyo, kutengana siyo kuachana na wakati wanandoa wanapokuwa wametengana, hakuna mgawanyo wa mali unaofanyika, ikiwa na maana kwamba, haki za mke wako, kama zipo, kwenye nyumba yenu bado zipo.

Isipokuwa kama umepata talaka, hakuna namna yoyote halali ya kutatua jambo hili isipokuwa kwa kumtafuta mke wako na kupata ridhaa yake kwa ajili ya kuweka dhamana nyumba yako. Kama hana maslahi yoyote kwenye mali, hatuoni kwa nini akatae kutoa ridhaa. Namna nyingine ni kutafuta dhamana nyingine kama vile mali binafsi au dhamana ya mtu mwingine. Mwanasheria wako anaweza kukuongoza zaidi.

## Daktari anaruhusu uzinzi

**Daktari wangu anasema kwamba nina moyo dhaifu na kwamba ili afya yangu**

**iimarike (hasa moyo wangu), ninahitaji kushiriki mapenzi na mwanamke mwingine, ingawa nipo kwenye ndoa ya mke mmoja. Daktari anasema hii itaniongeza maisha marefu. Si haki yangu ya kufanya mapenzi na mwanamke mwingine ambayo itapelekea kuimarisha kwa afya yangu inalindwa na Katiba? Nimesikia Sheria ya Ndoa inakataza uzinzi lakini inawezekanaje Sheria ya Ndoa ikiuke Katiba ya nchi? Je, hakuna upekee kwenye uzinzi?**

*2 Juni 2014*

Unaonekana kuchukulia kwamba daktari wako amekuruhusu kufanya mapenzi na mwanamke mwingine ili kuendelea kuwa na afya nzuri. Tuna mashaka sana na daktari uliyemuona na unaweza kupata ushauri zaidi kwingine. Ingawa sisi siyo madaktari, hii ni mara yetu ya kwanza kusikia kwamba mapenzi nje ya ndoa yanaweza kuimarisha moyo wako. Kimsingi, kwa elimu ndogo tuliyonayo kuhusu moyo, tuna uhakika kwamba kama utazidisha mapenzi ya nje ya ndoa, unaweza kupata ugonjwa wa shambulio la moyo.

Sheria haizungumzi mapenzi kwa namna uliyosema. Kwa kuwa umekubali mwenyewe kwamba wewe upo kwenye mahusiano ya mke mmoja, hauwezi kurudi na dawa mpya ya kufanya mapenzi nje ya ndoa yako. Haki zako za kikatiba zinalindwa, ziko juu ya sheria nyingine zote za nchi, lakini tafsiri yako kinadharia na kisheria haipo sahihi.

Tuna uhakika mke wako pia hawezi kukubali matibabu kama hayo, kama ambavyo wewe hutakubali ushauri wa aina hiyo kutoka kwa daktari wake. Tunakusihi sana upate ushauri mwingine na umuone mshauri wa ndoa. Kuna mahali kitu hakijaenda sawa. Na mwisho ni kweli, kama utafuata njia ya daktari wako, mke wako atakuwa na haki zote za kukupa talaka.

## Mume kupewa uraia wa kurithisha/ kuhamisha

**Mimi ni mwanamke Mtanzania ambaye nimeolewa na mwanamume wa nje na tumekubaliana kuishi na kuanzisha familia yetu nchini Tanzania. Hata hivyo, inanikera kwa sababu mume wangu anatakiwa kuomba na kupata kibali cha ukaazi kutoka Idara ya Uhamiaji nchini Tanzania. Amejaribu kuomba uraia kupitia uraia wangu lakini imekuwa ni ngumu kutokana na sababu nisizozijua. Kuomba na kupata kibali cha ukaazi imekuwa ni kama jinamizi kwa kuwa hatuwezi kuishi siku zote tukiomba kibali. Tafadhali tushauri hatua za kufuata ili aweze kupata uraia wa Tanzania kupitia ndoa yetu.**

*28 Julai 2014*

Sheria inayozungumzia uraia nchini Tanzania ni Sheria ya Uraia ya mwaka 1995 ambayo inatamka kwamba mwanamke aliyeolewa na mwanamume raia wa Jamhuri ya Muungano, wakati wowote wa uhai wa mume wake atakuwa na haki, baada ya kufanya maombi kwenye fomu maalum, ya kurithishwa uraia wa Jamhuri ya Muungano. Kutokana na kifungu hiki, ni mwanamume ndiye anayeweza 'kuhamisha' uraia wa mwanamke mgeni.

Kwa bahati mbaya Sheria ya Uraia haina kifungu kama hicho kwa mwanamke Mtanzania aliyeolewa na mwanamume wa kigeni. Hii ni bahati mbaya sana na mtu mwingine anaweza kusema ni ubaguzi dhidi ya wanawake.

Mume wako anaweza kuomba uraia (wa kujiandikisha/tajnisi) lakini ni lazima afanye hivyo kama mhamiaji mwingine anayetaka kupata uraia wa Tanzania kwa kuwa na sifa zilizoelezwa kwenye sheria kama ifuatavyo: (a) awe ameishi ndani ya Jamhuri ya Muungano miezi kumi na mbili mfululizo kabla ya tarehe ya maombi; na (b) kwa kipindi cha miaka kumi

kabla ya miezi 12 ya maombi awe ameishi ndani Jamhuri ya Muungano kwa muda ambao ni wastani wa miaka isiyopungua saba; na (c) anajua vizuri lugha ya Kiswahili au Kiingereza; na (d) ni mtu mwenye tabia nzuri; (c) kwa kuzingatia historia yake, anaonesha kuwa na nafasi ya kuwa na mchango mkubwa kwa maendeleo ya taifa katika nyanja ya uchumi na sayansi.

## Kupoteza mvuto wa mapenzi

**Niliolewa na mwanamume mwenye mvuto kwa kadri mwanamume anatakiwa kuwa. Kwa bahati mbaya benki anayofanyia kazi inamfanyisha kazi mpaka usiku sana, eti vitabu vya benki vinatakiwa kufungwa ndo aondoke. Hivi sasa mume wangu ana kilo zaidi ya 150, mara mbili ya uzito wa awali, na hanivutii tena. Nimepoteza mvuto wa mapenzi naye. Ninawezaje kumpa talaka haraka mume wangu kwa sababu simuoni akipungua uzito? Amejaribu mara nyingi lakini ameshindwa. Benki inapata faida kubwa, mume wangu hapati kitu, wakati wafanyakazi wengine wa benki wanapata ujira mnono. Je, ninaweza kuishtaki benki pia?**

*11 Agosti 2014*

Tunaanza na benki na tunaamini kwamba haki yako ya kuishtaki benki ipo mbali sana na hivyo huwezi kuishtaki. Hata hivyo, mume wako anaweza kuishtaki ila anatakiwa kuwa na sababu za msingi sana za kuegemea. Kwa mfano, je analipwa malipo ya muda wa ziada kwa kazi anazozifanya mpaka saa za usiku? Anafanya kazi kwenye mazingira salama? Je, benki inamjali kwa mujibu wa mkataba wa ajira? Je, kuna mazingira ya ndani ya benki ambayo yanachangia kuongezeka uzito kwa mfano kuwapatia wafanyakazi vyakula visivyo bora? Unahitaji kuwa na uelewa wa haya yote ili kuweza kuelewa haki ya mume wako kushtaki.

Kuhusu talaka, Sheria ya Ndoa hairuhusu talaka bila sababu za msingi. Kwa bahati mbaya kupoteza kwako mvuto wa mapenzi kwa mume wako siyo moja ya sababu iliyoelezwa na sheria. Kunenepa na kuzeeka siyo sababu za kuzitumia pia. Kama ingekuwa ni uzinzi, kushindwa kufanya mapenzi/ngono au ukatili, hapo sheria ingekuruhusu kuomba talaka. Tunakushauri kuwasiliana na mshauri wa ndoa ili kuokoa ndoa yako.

Unatakiwa kufikiri zaidi hatua zako kwa sababu inawezekana wakati huu ndiyo mume wako anakuhitaji zaidi kuliko wakati mwingine wowote. Isije kuonekana kama tunahubiri, usisahahu viapo vyenu vya ndoa, na usisahahu pia kwamba hata wanawake nao mara nyingi wanaongezeka uzito.

## Mume analazimisha kumpa mtoto jina

**Mimi nimeolewa na ninaishi Dar. Mimi na mume wangu ni wasomi na tunafanya kazi Serikalini. Mungu ametubariki kupata watoto watatu na hivi karibuni tunatarajia mtoto wetu wa nne, kwa kuwa ni mjamzito. Kwa bahati mbaya mume wangu ndiye pekee aliyewapa watoto wetu majina na amekuwa akiwapatia majina ya ukoo wake. Ameshamchagulia jina hata mtoto tunayemtarajia, na kupelekea kubishana kwa kuwa na nami nataka kumpatia jina mtoto huyu. Je, kuna sheria inayosimamia watoto kupewa majina? Tafadhali niongoze.**

*29 Septemba 2014*

Sheria ya Mtoto, Na. 21 ya 2009 chini ya kifungu cha 6 inaeleza kwamba mtoto atakuwa na haki ya kupewa jina, utaifa na kuwafahamu wazazi wake wa kumzaa na ndugu/jamaa wengine wa ukoo/familia tandaa. Inaeleza zaidi kwamba, mtu hatamnyima mtoto haki yake ya jina, utaifa na kufahamu wazazi wake wa kumzaa na ndugu zake wengine kwa kuzingatia masharti ya sheria nyingine. Pia, kila mzazi au mlezi

atakuwa na wajibu wa kusajili kuzaliwa kwa mtoto wake kwa Msajili Mkuu.

Kwa bahati mbaya hakuna sheria inayolazimisha iwapo baba au mama atoe jina la mtoto. Pia hatuna kesi yoyote ya kutuwezesha kukuongoza juu ya hili. Unaweza kuutatua mgogoro huu Mahakamani, lakini mfumo wa Mahakama umezidiwa na mrundikano wa kesi na huenda mpaka mgogoro unatatuliwa utakuwa tayari umejifungua.

## Mkataba wa ndoa

**Nilipokuwa Chuo Kikuu miaka tisa iliyopita, niliingia mkataba na rafiki yangu wa kike kuwa ikiwa wote wawili tutatimiza miaka 30 na hatupo kwenye ndoa au kuwa na mahusiano imara na mtu mwingine, basi tutaoana. Mwezi uliopita wote wawili tulitimiza miaka 30 na alinihakikishia kwamba hajaolewa na wala hayupo katika uhusiano wowote imara, anadai havutiwi tena na mimi, ingawa mimi ni tajiri na mwenye mamlaka. Huku ni kukiuka makubaliano, nataka kumpeleka Mahakamani ili alazimishwe kuolewa na mimi. Bado ninamhitaji.**

*29 Septemba 2014*

Mkataba wa ndoa si kama mkataba mwingine wowote. Hatima yake inaongozwa na upendo wa pande zote mbili. Unaweza kuwa bado unamuhitaji, lakini yeye hakuhitaji. Hata kama Mahakama itamshinikiza kuolewa na wewe, kitu ambacho haiwezi, basi kusudio kuu la ndoa litakuwa limekiukwa.

Sheria ya Ndoa inaeleza kwamba, "kesi inaweza kufunguliwa kudai fidia ya kukiuka ahadi ya ndoa iliyotolewa Tanganyika bila kujali ukiukwaji huo ulifanyika Tanganyika au kwingineko, na mdai, iwapo mdai/upande huo haujafikisha miaka kumi na nane, na mzazi wake au mlezi. Hakuna kesi itakayoletwa kwa ajili ya utekelezaji maalum wa ahadi ya ndoa/kulazimisha ndoa."

Kwa hiyo Sheria ya Ndoa inaruhusu madai juu ya hasara ambayo mtu anaipata kwa kuvunja ahadi ya ndoa. Katika kesi yako, inategemea na maelezo zaidi ambayo unaweza kuwapatia wanasheria wako, fidia inaweza kudaiwa lakini hatuamini kama una kesi nzuri. Kitu ambacho tuna uhakika nacho ni kwamba kama mwanamke huyu amebadili mawazo juu yako, basi itabidi uanze kutafuta tena. Haijalishi kama wewe ni tajiri na mwenye mamlaka – ni mwanamke ndiye atakayeamua iwapo aolewa na wewe au la.

## Kushikiliwa kwa mali za ndoa/familia

**Mume wangu amekuwa akifanya kazi kwenye shirika la umma na wakati wa ndoa yetu tumeweza kuanzisha vitega uchumi vya familia ikiwa ni pamoja na baa, supamaketi na saluni mbili zisizojali jinsia. Tumeweza pia kujenga nyumba nzuri ambayo hivi sasa tunaishi. Ninakiri kwamba mume wangu amechangia sehemu kubwa ya mtaji ingawa na mimi nimechangia sehemu kwa mkopo niliopata kutoka taasisi ya mikopo midogo iliyopo Dar es Salaam. Mimi pia sijui ikiwa mapato/mchango wa mume wangu umetoka kwenye vyanzo vingine au mshahara wake mnono na marupurupu tu. Kwa bahati mbaya, hivi sasa mume wangu na wenzake wameshtakiwa kwa makosa ya rushwa/ufisadi kutokana na madai ya ubadhirifu wa fedha ofisini kwao. Sasa nimeambiwa na rafiki yangu kwamba ikiwa mume wangu atakutwa na hatia, mali/uwekezaji wetu wote, ikiwa ni pamoja na nyumba tunayoishi, vitataifishwa na Serikali. Nataka kujua kama hii inawezekana. Je, ninaweza kufanya chochote kupinga jambo hili? Kwani ninahisi kuwa litanipotezea haki zangu kwa kuwa na mimi nimechangia kwenye uwekezaji huu.**

*24 Novemba 2014*

Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Namba 11 ya 2007 inazungumzia hali inayokukabili na inasema kwamba TAKUKURU inaweza, kwa kushirikiana na ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, kurejesha mapato yatokanayo na rushwa kwa kutaifisha na kuwa mali ya Serikali.

Sheria hii inaeleza zaidi kwamba pale ambapo mtu anapatikana na hatia ya kosa la rushwa chini ya Sheria hii, Mkurugenzi wa Mashtaka anaweza kuiomba Mahakama iliyomtia hatiani, au Mahakama nyingine yoyote inayofaa katika kipindi kisichozidi miezi sita baada ya mtu huyo kutiwa hatiani, kutoa amri ya kutaifisha mali yote iliyopatikana kwa njia ya rushwa. Kuhusu mapato ya rushwa, sheria imetoa maana kuwa ni mali yoyote ambayo inatokana na/au inapatikana na hatia ya makosa ya rushwa.

Hivyo, madhara ya sheria yaliyoelezwa hapo juu yanaweza kutumika kwa mume wako baada ya kutiwa hatiani ingawa hatujui ni kosa gani hasa ambalo mume wako ameshtakiwa nalo. Na nilazima tueleze kwamba utaifishaji siyo haki ya moja kwa moja ya TAKUKURU au Mkurugenzi wa Mashtaka, na hivyo uwe tayari kuthibitisha kwamba uwekezaji haukutokana na mapato ya uhalifu.

## Ndoa ya siri na fungate

**Ninataka kufanya harusi/ndoa ya siri na sitaki mtu yeyote ahudhurie ndoa/harusi yetu. Je, hii imeruhusiwa kwenye sheria za Tanzania? Je, ni lazima kwenda fungate baada ya ndoa? Mke wangu anasisitiza kwamba fungate ni sharti la ndoa.**

*1 Desemba 2014*

Sheria ya Ndoa, 1971 inaeleza kwamba, mtu yeyote anaweza kuhudhuria wakati wa kufungisha ndoa ya kiserikali kwa kadiri nafasi katika ofisi ya Msajili wa Ndoa wa Wilaya inavyoruhusu. Zaidi ya hilo, muumini yeyote wa dini ambayo ndoa hiyo inafungwa anaweza kuhudhuria ndoa hiyo. Vile vile, mwananchi yeyote anayehusiana na pande zote au upande mmoja wapo wa ndoa inayofungwa kwa imani ya kiislamu au kimila anaweza kuhudhuria.

Kutokana na maelezo hapo juu, hakuna ndoa inayoweza kufungwa kwa siri kwa sheria za Tanzania. Kitu pekee unachoweza kuomba ni kwamba mtu yeyote asijitokeze/asihudhurie wakati wa ndoa ama kwenye ofisi ya msajili wa ndoa au kwenye nyumba ya ibada, au popote unapotaka kufungia ndoa.

Kuhusu suala la fungate, tumeangalia sheria zetu na hatujaliona popote neno hili. Na kwa hakika siyo sharti la baada ya ndoa. Utafiti wetu umegundua kwamba fungate ni likizo ya kitamaduni wanayopewa wanandoa baada ya kuoana ili kusherehekea ndoa yao kwa ukaribu na usiri. Kwa sasa, fungate zinasherehekewa kwenye maeneo mujarabu na mahususi kwa wanafungate.

Hiki ni kipindi ambacho wanandoa wapya wanapata mapumziko kwa kushirikiana mambo ya faragha, na nyakati za ukaribu ambazo zinasaidia kuimarisha mapenzi kwenye mahusiano yao. Kipindi hiki kinawapa fursa ya kujuana kwenye mazingira mwanana. Ufaragha huu unaaminiwa kuleta mapumziko ya kiakili kuelekea mahusiano ya kimwili, ikiwa ni moja ya njia za awali za kuimarisha ukaribu wao siku za mwanzo wa ndoa.

Hivyo, ni uamuzi wako kama unataka kwenda fungate ama la. Sheria haikulazimishi ila inawezekana mke wako ana matumaini hayo. Hapo ni wewe tu utakavyomudu matarajio ya mkeo. Tunakutakia kila la heri.

## Kunyima haki ya matibabu kwa sababu ya dini

**Mimi nina imani kubwa kwamba Mungu ndiye mponyaji, na imani/dini yetu inakataza wazazi kuwapeleka watoto wao**

**hospitalini kupata matibabu. Tunaelekezwa kumwombea mtoto mgonjwa mpaka atakapopona. Kutokana na hilo, sijawapatia wanangu chanjo kadhaa. Je, kuna sheria inayopingana na imani hii?**

*8 Desemba 2014*

Sheria inatoa uhuru wa kuabudi kwa kila mtu nchini Tanzania. Hata hivyo, Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009 inaeleza wazi kwamba, mtu yeyote hatamnyima mtoto matibabu kwa sababu za kidini au imani nyinginezo. Hivyo, kwa kumnyima mtoto wako haki ya matibabu, unavunja sheria na unaweza kukumbana na mkono wa sheria. Utafiti wetu umekutana na aya ifuatayo kutoka kwenye Gazeti la Times la Uingereza ambayo ni muhimu kwako.

Mapingamizi ya kidini kuhusu matibabu ya kidunia yana mizizi ya kihistoria ambayo ilianza mwishoni mwa miaka ya 1800 nchini Uingereza ambapo dhehebu lililoitwa Peculiar People (Watu wa Kipekee) liliishia kushtakiwa kwa kuruhusu vizazi vya watoto wao kufariki kutokana na maamuzi yao ya kuwakataa madaktari na dawa. Hivi leo, mara kwa mara makundi mengi ya kidini yanakataa baadhi au huduma zote za afya kwa sababu za kidini, yakiwemo makundi ya Wakristo Wanasayansi, Mashahidi wa Yehova, Waamishi na Wasayantoloji. "Wenye imani kali hawa wanatuambia kwamba maisha yao yapo mikononi mwa Mungu na sisi kama madaktari, siyo Mungu," anasema Dakt. Lorry Frankel, Profesa wa Shule ya Tiba na mwandishi wa Mtanziko wa Kimaadili kwenye Tiba ya Watoto. Tunaheshimu imani za dini za watu na tunajaribu kuendana nazo, lakini hatuwezi kukataa matibabu ambayo yataokoa maisha. Frankel anasema aliwahi kuwapeleka Mahakamani waumini wa dini ya Mashahidi wa Yehova ambao walikataa kutoa damu kwa ajili ya watoto wao ambao walikuwa na hali mbaya. " Mungu anatupenda na sijawahi kumnyima mtoto matibabu" anasema Frankel.

Uponyaji wa miujiza/matibabu ya imani hayajathibitika. Kwa kushindwa kumpatia chanjo mtoto wako, unahatarisha maisha yake kizembe. Tunakushauri umpeleke mwanao akapate chanjo.

# Sheria za Biashara, Migogoro ya Kibiashara na Haki Miliki

"

Katika ulimwengu kamilifu, biashara hufanyika kwa uaminifu na kwa kuheshimu makubaliano. Kwa bahati mbaya, ulimwengu si kamilifu na hivyo siyo mara zote mambo huenda sawia. Wakati mwingine wafanyabiashara huwadanganya wateja, hughushi nembo/alama za biashara za kampuni shindani, hugombana na waleta bidhaa na hata hupinga tafsiri ya mikataba. Mambo kama haya yanapotokea, wakati mwingine, huwa ni lazima kutatua changamoto hizi kupitia mchakato rasmi wa kisheria, ikiwa ni pamoja na upatanishi, usuluhishi au kufikishana mahakamani. Na wakati mwingine, inawezekana hata kuwakamata wanaovunja mikataba na kuwaweka gerezani kwa miezi sita.

## Kuvunja mkataba

**Niliingia mkataba na mtu ambaye alinilipa malipo ya awali na malipo mengine kulipwa baadaye, lakini ameshindwa kunilipa deni lote, na muda tuliopatana umeshaisha. Baada ya kufuatilia kwa miezi mingi bila majibu yoyote kutoka kwake, yeye ameamua kulipeleka suala hili kwenye usuluhishi. Inanishangaza sana kuona upande uliokiuka masharti ndio unaopeleka suala hili kwenye usuluhishi. Nifanye nini? Ninachotaka ni pesa zangu tu.**

*2 Januari 2012*

Kuna uwezekano mkubwa kwamba mkataba wenu una kipengele cha usuluhishi ambacho kinaelekeza mgogoro upelekwe kwanza kwenye usuluhishi kabla ya kwenda Mahakamani. Usuluhishi ni uamuzi wa mgogoro kwa njia ya upatanishi unaofanywa na mtu mmoja au zaidi, ambapo msuluhishi/wasuluhishi ni mtu/watu huru wasio na maslahi katika mkataba au mgogoro husika, badala ya kwenda Mahakamani. Wasuluhishi uteuliwa na wahusika wenye mgogoro kulingana na masharti ya mkataba. Msuluhishi ana wajibu wa kusikiliza pande zote mbili na kutoa tafsiri sahihi ya sheria na kwa misingi ya haki na usawa. Kulingana na na tafsiri ya kipengele cha usuluhishi katika mkataba na usahihi wa maamuzi ya msuluhishi/wasuluhishi, tuzo iliyotolewa na msuluhishi/wasuluhishi inaweza kupingwa Mahakamani. Hujatueleza kama mkataba ulioingia una kipengele cha usuluhishi. Kama mkataba una kipengele hicho, unatakiwa kwenda kwenye usuluhishi (ingawa umeanzishwa na mdeni wako). Kama hakuna kipengele cha usuluhishi, huhitaji kwenda kwenye usuluhishi badala yake unaweza kufungua kesi ya kudai fidia Mahakamani.

Inaonekana umeshangazwa na kitendo cha mtu aliyekiuka mkataba ndiye amepekeka mgogoro kwenye usuluhishi. Kwa kawaida vipengele vya usuluhishi vimeundwa kwa namna ambayo kama mgogoro utatokea, upande wowote ulioathirika unaweza kupeleka mgogoro kwenye usuluhishi. Hujasema iwapo mgogoro umetokea kwa sababu malipo hayajafanyika. Je, huo ni mgogoro ambao unaweza kutafsiriwa kwa kuangalia kipengele cha usuluhishi? Hatuwezi kujibu hilo kwa sababu hatuna taarifa kamili. Ambacho tunaweza kusema kwa uhakika, ni kwamba upande uliokiuka unaonekana kuamini kwamba kuna mgogoro mahala na kwa hiyo umezuia malipo.

Kwa kujali muda na kuzingatia kiwango cha pesa, tunakushauri uendelee na usuluhishi kwa sababu usuluhishi ni njia ya haraka na mgogoro unaweza kutatuliwa ndani ya wiki chache tu.

## Mgahawa wa chakula bila mafuta unapotosha wateja

**Nimekuwa nikifanya biashara ya mgahawa kwa takribani miaka 30. Miezi sita iliyopita, umefunguliwa mgahawa mwingine karibu yangu wenye jina 'Kula Chakula Kisicho na Mafuta'. Ingawa jina la mgahawa huo linamaanisha kuuza chakula kisicho na mafuta, umekuwa ukiuza kuku waliokaangwa kwa mafuta, vibanzi (chipsi), chipsi-mayai na vyakula vinginevyo vilivyopikwa kwa mafuta. Sijali ushindani uliopo, lakini jina wanalotumia linapotosha watu ambao wanaishia kwenda hapo wakiamini watapata chakula kisicho na mafuta. Je, jina hili haliwapotoshi watu, ninaweza kufanya nini juu ya jambo hili? Swali langu la pili, ni je kampuni inaweza kubadilisha jina baada ya kusajiliwa?**

*2 Januari 2012*

Sheria ya Makampuni itakuwa upande wako iwapo kwa maoni ya Waziri wa Viwanda na Biashara jina ambalo kampuni

imesajiliwa nalo linapotosha uhalisia wa biashara/shughuli zake na kuna uwezekano wa kusababisha madhara kwa umma, anaweza kuelekeza kubadilisha jina lake. Kama maelekezo ya Waziri hayakupingwa Mahakamani ni lazima yatekelezwe ndani ya kipindi cha wiki sita tangu tarehe ya maelekezo kutolewa au ndani ya muda zaidi ya huo kama Msajili atakavyoona inafaa kuruhusu.

Sheria inaeleza zaidi kwamba kampuni inaweza, katika kipindi cha wiki tatu kuanzia tarehe ambayo maelekezo yalitolewa, kuiomba Mahakama kuyatengua; na Mahakama inaweza kutengua maelekezo hayo au kuyathibitisha na, kama ikiyathibitisha maelekezo, itabainisha kipindi ambacho yanapaswa kutekelezwa. Kama kampuni inakiuka kutekeleza maelekezo husika chini ya kifungu hiki, itatozwa faini ya kuendelea kukiuka.

Ushauri wetu ni wewe kumwandikia Waziri wa Viwanda na Biashara, umweleze hali ilivyo, huku ukiainisha, kwa maoni yako, madhara ambayo umma utayapata kutokana na jina hilo linalopotosha.

Tunajibu swali lako la pili kwa kukubali kwamba kampuni inaweza kwa azimio maalumu na kwa idhini ya maandishi ya Msajili kubadilisha jina lake. Kama Msajili atakataa kutoa idhini, atatoa sababu. Msajili ataingiza jina jipya kwenye orodha ya usajili, na hivyo jina jipya kuchukua nafasi ya jina la zamani, na atatoa taarifa ya mabadiliko hayo kwenye Gazeti la Serikali.

Ni lazima ieleweke kwamba, kampuni kubadili jina, katika mazingira yaliyoelezwa hapo juu, hakuathiri haki yoyote au wajibu wowote wa kampuni na wala hakuharamishi mashtaka yoyote yaliyokwishafunguliwa na kampuni au yaliyokwishafunguliwa dhidi ya kampuni hiyo kwa jina la zamani. Aidha, mashtaka yoyote ambayo kampuni ingeyafungua au yangefunguliwa dhidi yake kwa jina la zamani, inaweza kuyafungua au kufunguliwa dhidi yake kwa jina lake jipya bila athari yoyote.

## Mkataba kwa njia ya nukushi (faksi)

**Niliingia mkataba na muuza mbao kwa ajili ya kuniuzia mbao kwa bei fulani. Tulikubaliana masharti lakini kwa sababu ya mazingira yaliyokuwepo tuliingia mkataba kwa njia ya nukushi (nukulishi/faksi). Muuzaji amegeuka na anataka kuongeza bei ya mbao. Ninaweza kufanya nini?**

*9 Januari 2012*

Kwanza kabisa ni lazima tuseme kuwa hatuna taarifa kamili za kutuwezesha kukujibu kwa ufasaha. Hata hivyo sheria zetu zinatambua mkataba wa mdomo na wa maandishi. Kwa kesi yako, mbali na mkataba wa nukushi, kama unaweza kuthibitisha kwa matendo au namna nyingineyo kuwa hicho ndicho mlichokubaliana, tunaamini una kesi nzuri. Ushahidi wa ziada kuhusu mkataba wa nukushi unaweza kuhitajika kuthibitisha dhamira yenu. Mwanasheria wako anaweza kukuongoza zaidi.

## Kukamatwa kwa mdaiwa

**Nimeshinda kesi dhidi ya mtu na anakataa kunilipa. Nimejitahidi sana lakini inaonekana kama upole wangu kwenye kudai unatafsiriwa vibaya. Je, kuna vifungu vya ukamataji kama sijalipwa? Nini faida na hasara za njia hiyo?**

*13 Februari 2012*

Ndiyo, kuna vifungu ambavyo vinamruhusu mdaiwa kukamatwa ili kutekeleza Tuzo ya Mahakama. Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Madai ya Tanzania inatamka kwamba mdaiwa anaweza kukamatwa ili kutekeleza tuzo siku yoyote nyakati za mchana na kupelekwa Mahakamani haraka iwezekanavyo, na

Mahakama inaweza kuamuru afungwe. Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Madai pia inatamka kwamba kama tuzo iliyopelekea mdaiwa kukamatwa ni tuzo ya malipo ya fedha, mdaiwa akilipa fedha za kwenye tuzo pamoja na gharama za afisa aliyemkamata, afisa anaweza kumwachia huru mdaiwa mara moja.

Kifungo ni miezi sita na anaweza kuachiliwa kabla ya miezi sita kama tu atalipa au kwa maombi ya aliyeomba afungwe au kama mtu aliyeomba afungwe ameshindwa kumlipia mfungwa wake gharama za kujikimu akiwa gerezani.

Tafadhali, unataarifiwa kwamba sheria inakutaka mshinda tuzo, kumlipia mdaiwa wako gharama za kujikimu (kwa kadri ya nafasi yake kimaisha) anapokuwa gerezani, na kushindwa kulipa gharama hizo kwa kiwango kinachotakiwa kunaweza kufanya mdaiwa wako kuachiliwa huru.

Faida za kifungo ni kwamba mdaiwa anaweza kukulipa kwa kuhofia kifungo. Hasara kubwa ya njia hii ni kwamba, kama mfungwa hahofii kwenda jela miezi sita, utawajibika kuingia gharama za ziada za kumhudumia akiwa gerezani na bado usiweze kulipwa. Pesa zote unazozitumia kumhudumia mdaiwa akiwa gerezani zinaweza kuongezwa kwenye deni lako.

## Kesi imerudiwa

**Nilishinda kesi miezi 18 iliyopita, baadaye nikagundua kwamba niliowashinda kesi wamefungua tena kesi nyingine kwa jambo lilelile lakini safari hii wamefungua kwenye Mahakama nyingine. Na wala hawajasema chochote kuhusu ushindi wangu wa ile kesi ya awali. Kwa upande wangu, naona sina haja ya kujitetea kwenye kesi ambayo imekwishaamuliwa tayari. Tafadhali naomba muongozo.**

*12 Machi 2012*

Wakati haki ni lazima itendeke na ionekane inatendeka, pia kuna sera ya umma maarufu ambayo inasema ni lazima kuwe na ukomo wa mashtaka. Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Madai pia inarahisisha hili kwa kutamka kwamba hakuna Mahakama itakayosikiliza shauri au sehemu ya shauri ambalo lina uhusiano wa moja kwa moja au linafanana na shauri la awali kati ya watu walewale au mmojawapo akidai kuhusu suala lile linalofanana na shauri ambalo lilishafunguliwa na kutolewa maamuzi na Mahakama yenye mamlaka. Kwa hiyo ni lazima ujitetee kwenye shauri hili jipya na uibue hoja kuwa shauri hili limeshasikilizwa na kutolewa uamuzi na Mahakama.

## Sifuri ya ziada kwenye bei ya mkataba

**Niliingia kwenye mkataba ambapo thamani halisi ya bei ya kwenye mkataba ilitakiwa kuwa milioni 11 lakini tuliingia kwenye mkataba huku kukiwa na ongezeko la sifuri kimakosa kwenye oda ya manunuzi yaani Mil. 110. Tumemlipa muuzaji milioni 11 lakini anadai Mahakamani kwamba tumemlipa pungufu na anataka alipwe tofauti. Nimearifiwa kwamba Mahakama za Tanzania mara zote zinampendelea mtu wa aina hiyo. Tufanye nini?**

*2 Aprili 2012*

Kwanza kabisa kama kwa makusudi mliacha sifuri moja kwenye mkataba na thamani halisi ya bidhaa ni Shilingi milioni 110, muuzaji anaweza kushinda na mtaamuliwa kumlipa. Lakini, kama mlinunua bidhaa ambazo ni wazi kuwa thamani yake halisi ni Shilingi milioni 11 na mkaweza kuthibitisha kwamba bidhaa hizo thamani yake halisi ni kiasi hicho na yalikuwa makosa ya dhati, hatuamini kama mtashindwa Mahakamani.

Pia, jaribu tena kuangalia iwapo kiasi

hicho kiliandikwa kwa maneno. Kwa kawaida kwenye tafsiri, maandishi ya maneno yanasimama, ikiwa na maana kama kiasi kiliandikwa milioni 110 lakini maneno yakasomeka milioni kumi na moja, basi uwezekano ni kwamba Mahakama itatafsiri kiasi cha Shilingi milioni kumi na moja na si milioni 110 (za tarakimu).

Kilichoelezwa hapo juu kinaweza kuleta shida kama usambazaji wa huduma ulikuwa si wa kiwango maalum. Unaweza kupitia majadiliano yenu yote mliyoyafanya na kuyafanya sehemu ya ushahidi ili kuonesha kwamba huduma mliyokubaliana ilikuwa ni milioni 11 na siyo milioni 110.

Kwa kawaida Mahakama haiingilii kile pande zimekubaliana, isipokuwa kama kuna uharamu/ubatili kwenye mkataba. Kama nyaraka zako ziko sawa, hatuoni kwa nini Mahakama isiamue upande wako. Wanasheria wako wanaweza kukuongoza zaidi.

## Sehemu za mazishi/makaburini

**Kadiri muda unavyokwenda, gharama za kupata sehemu za mazishi ya binadamu kwenye makaburi ya Jiji zinazidi kuongezeka. Ni nani anamiliki makaburi haya? Je, mtu binafsi anaruhususiwa kuwa na makaburi yake binafsi kwa malengo ya kibiashara? Ninataka kuanzisha makaburi yangu binafsi ambapo familia ya marehemu italipa kodi ya pango kila mwaka, ambayo itajumuisha utunzaji wa makaburi yote kwa ujumla.**

*16 Aprili 2012*

Chini ya Kanuni za Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji) (Udhibiti Maendeleo) za 2008 ambazo zimetokana na Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji), mamlaka pekee iliyopewa jukumu la kuteua au kutenga maeneo kwa ajili ya mazishi ni miji, manispaa na majiji yanayohusika kutegemea na maeneo. Mamlaka ndiyo mmiliki wa makaburi na ndiyo yenyewe inayoamua tozo za huduma ambazo zipo kwenye makaburi haya. Chini ya Kanuni hizo, hakuna maiti ya mtu yeyote itakayoruhusiwa kuzikwa sehemu nyingine yoyote nje ya maeneo hayo, isipokuwa tu kwa kibali maalum kutoka kwa mamlaka husika. Hii ina maana kwamba mabaki yote ya marehemu yanatakiwa kuzikwa kwenye makaburi yaliyotengwa.

Sheria ipo kimya iwapo mtu binafsi anaweza kumiliki makaburi yake binafsi kwa malengo ya kibiashara. Hata hivyo, kwa kuwa inawezekana kwa jamii fulani ya dini kuwa na makaburi yake, hatuoni kwa nini mtu binafsi asiruhusiwe kuwa na makaburi yake iwapo makaburi hayo yapo kwenye maeneo ambayo yanaendana na mipango ya maendeleo ya miji kwenye mji husika. Tunakushauri uwasiliane na mamlaka za manispaa kwa ufafanuzi na muongozo zaidi.

Tozo yako ya pango ya kila mwaka inafurahisha sana. Unachojaribu kushawishi ni kwamba utaingia mkataba na familia ya marehemu ambapo utakuwa unapata kiasi fulani cha pesa kila mwaka, ni kama kumpangisha marehemu ili abaki kaburini. Tunajaribu kufikiria utafanya nini kama ikitokea hujalipwa, tuna hakika huwezi kufukua kaburi ili utoe mwili wa marehemu kwa sababu, kwa kufanya hivyo, utakuwa unavunja sheria. Angalia kwanza mpango wako wa biashara kwenye suala hili kabla ya kuanza.

## Mkataba wa kimataifa wa mauzo ya bidhaa

**Niliagiza bidhaa kutoka kwa muuzaji mchina nchini China ambazo ziliharibika sana zikiwa njiani kuja Tanzania. Mkataba ulikuwa ni muuzaji anawajibika hadi bidhaa zitakapopakiwa kwenye meli kwa ajili ya kusafirishwa (FOB). Tatizo pekee ni kwamba hatuna hakika ni wapi tufungue shauri -**

**Tanzania au China. Swala hili limetolewa taarifa kwenye ubalozi wa China ambao wanatupa ushirikiano lakini wanasema hili ni suala la kibiashara ambalo linahitaji utatuzi wa pande husika. Makubaliano yetu yanaongozwa na Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mauzo ya Bidhaa (CISG). Je, tunaweza kufungua kesi Umoja wa Mataifa. Tafadhali tushauri tunaendeleaje. Mwanasheria wetu anasema tunatakiwa kufungua shauri hapa.**

*23 Aprili 2012*

Mkataba wa Kimataifa wa Mauzo ya Bidhaa, ambao wakati mwingine unaitwa Mkataba wa Vienna, ni Mkataba unaosimamia biashara za mauzo ya bidhaa kimataifa. Mpaka kufikia Agosti 2010 ulikuwa umeridhiwa na nchi wanachama 77 na hivyo kuwa na idadi kubwa ya nchi wafanyabiashara, na kuufanya kuwa ni miongoni mwa sheria zenye mafanikio makubwa sana. Tanzania haijaridhia mkataba huu na hivyo hauwezi kutumika moja kwa moja hapa.

Mkataba huu unaepusha matatizo ya kuchagua sheria za kutumika kwa sababu wenyewe unatoa kanuni zinazokubalika, ambapo nchi wanachama, Mahakama na wasuluhishi wanaweza kuzitumia. Mkataba huu uliendelezwa na Tume ya Umoja wa Mataifa inayoshughulika na Maendeleo ya Sheria za Biashara za Kimataifa (UNCITRAL) na ulianza kutumika mwaka 1988.

Kupitishwa kwa mkataba huu kunatoa sheria sawa na za kisasa kwa mauzo ya bidhaa kimataifa ambazo zitatumika popote ambapo mikataba ya mauzo ya bidhaa itafanyika kwenye nchi wanachama. Katika mazingira hayo Mkataba huu utatumika moja kwa moja ili kuepuka kutumia kanuni za sheria ya kimataifa binafsi ili kuchunguza sheria zinazotumika kwenye mikataba, na hivyo kusaidia kuongeza uhakika na usanifu wa mauzo ya bidhaa kimataifa.

Turudi kwenye swali lako. Kwanza uliuliza kama unaweza kulitolea taarifa Umoja wa Mataifa. Jibu ni kwamba unaweza usifanikiwe kwa sababu UNICITRAL ilisaidia kuandaa sheria, lakini haisimamii sheria hii moja kwa moja.

Swali lako la pili ni unawezaje kuendelea. Kama kuna njia zozote za kutatua mgogoro huu kwa amani bila kwenda Mahakamani au usuluhishi, unatakiwa kuzingatia sana chaguo hilo. Katika utatuzi wa mgogoro kwa njia mbadala, kwa kawaida kutakuwa na kutoa na kuchukua (kuuma na kupuliza) na unatakiwa kuwa mwepesi kubadilika wakati wa majadiliano.

Tuchukulie mkataba hauna kipengele cha usuluhishi na njia mbadala ya utatuzi imeshindikana, hapo huna uchaguzi mwingine zaidi ya kuendelea Mahakamani. Swali linalofuata ni utamshtaki wapi muuzaji. Hatujaona mkataba wa mauzo lakini kwa maoni yetu unatakiwa kufungua shauri nchini China kwa sababu ni rahisi tu kwamba iwapo utashinda kesi utakuwa kwenye nafasi nzuri ya kutekeleza hukumu hiyo dhidi ya msambazaji wa kichina. Kama utashtaki Tanzania, hukumu iliyotolewa Tanzania haina nguvu ya kisheria nchini China kwa kuwa hakuna makubaliano ya utekelezaji hukumu kati ya China na Tanzania. Ni dhahiri upo kwenye wakati mgumu hivyo unatakiwa kuonana na wanasheria wa Tanzania na China.

## Hasara imesababishwa na zima moto, bima inakataa dai langu

**Nilikuwa namiliki mgahawa mzuri na wa hali ya juu Dar es Salaam ambao uliungua kwa moto. Nashukuru zimamoto walikuja lakini moto ulikuwa mkubwa sana na ulisababisha hasara kubwa. Kampuni yangu ya bima inataka kunilipa sehemu ndogo ya dai halisi, inataka kupunguza kiasi hicho kutokana na uharibifu uliosababishwa na maji ya zima moto. Wakala wangu anasema**

**nichukue tu kiasi hicho kwa sababu makampuni ya bima ni wajanja sana na wanalindwa na sheria. Kampuni yangu ya bima inasema sera yangu inahusu majanga ya moto tu. Je, hiyo ni kweli? Tafadhali nishauri.**

*25 Juni 2012*

Hatujaona sera yako ya bima ya moto iliyotolewa na mbima wako kwa sababu wakati mwingine kuna vitu vinaondolewa kwenye mkataba wa bima ili kupunguza wajibu wa mbima. Hata hivyo, kwenye kesi yako maelezo ambayo yanaweza kukupa matumaini kidogo ni yale ya kwenye sheria maalum ambayo inajihusisha na matukio hayo.

Sheria ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Na. 14 ya 2002 kifungu cha 26 (2) kiko wazi kwamba hasara yoyote iliyosababishwa na jeshi katika utekelezaji wa majukumu yake au matukio ya moto au majanga mengine au likijibu mlio wa tahadhari ya moto, yatachukuliwa kuwa yamesababishwa na moto katika maana ya sera yoyote ya bima ya moto.

Kutoka na maelezo hapo juu, hata kama sera yako imezuia fidia hiyo, ambayo tunashangaa kuisikia, sheria itakulinda na hivyo kipengele hicho hakitatiliwa maanani dhidi yako. Kumbuka kuwa wakati wote sheria inatawala dhidi ya mikataba binafsi.

Labda kama kuna taarifa unaficha, tunaamini una kesi nzuri dhidi ya kampuni yako ya bima. Usikimbilie tu kumuamini wakala wako inawezekana anataka tu kufunga faili ili aendelee na mambo mengine. Mawakala wanafurahia kukusanya malipo na mara nyingi wengi wao hawafurahii kufuatilia madai yako. Unahitaji kufanya maamuzi ya busara ya namna ya kuendelea na tunakushauri uwasiliane na wanasheria wako.

## Kutokuafikiana kuhusu msuluhishi

**Wakati wote niliamini kuwa usuluhishi ni njia bora ya kutatua migogoro, lakini mwishowe nikagundua kuwa wakati mwingine unaweza kuchukua muda mrefu zaidi kuliko Mfumo wa Mahakama. Kampuni yetu ina mgogoro na kampuni nyingine iliyoko Dar. Wanasheria wetu wameshindwa kukubaliana juu ya nani atakayekuwa msuluhishi. Ni mwezi wa tisa sasa na mgogoro wa nani awe msuluhishi haujatatuliwa. Tufanye nini? Je, tunaweza kwenda moja kwa moja Mahakamani?**

*2 Julai 2012*

Sheria ya Usuluhishi inaeleza cha kufanya katika mazingira hayo. Inatamka kwamba Mahakama inaweza kumteua msuluhishi kama kipengele cha usuluhishi kinasema mgogoro utatatuliwa na msuluhishi mmoja, na kama pande hazikubaliani baada ya mgogoro kutokea, watakubaliana kumteua msuluhishi. Hivyo, unaweza ukapeleka maombi Mahakamani na Mahakama inaweza kumteua msuluhishi ili kuwawezesha kuendelea na usuluhishi.

Kuhusu uwezekano wa kwenda moja kwa moja Mahakamani kuutatua mgogoro, hilo haliwezekani kwani pande zote zilikubaliana kufanya usuluhishi kwanza. Hata hivyo kama nyote mkikubaliana kuacha usuluhishi, Mahakama itakuwa na mamlaka ya kusikiliza mgogoro huo. Vinginevyo mnatakiwa kujikita kwenye usuluhishi.

## Alama (Nembo) ya biashara imesajiliwa na mtu mwingine

**Nimekuwa nikitumia jina la kampuni fulani kwa miaka 30 iliyopita. Hivi karibuni nimegundua kwamba kuna mtu amesajili jina langu kama nembo ya biashara. Wanasheria wangu wanasema muda wa kupinga usajili huu umekwisha. Nifanyeje?**

*16 Julai 2012*

Kwa madhumuni ya swali hili, tunachukulia kwamba kampuni yako imesajiliwa kwa jina hilo hilo chini ya Sheria ya Makampuni kama ilivyo kwenye Sheria ya Alama za Biashara na Huduma. Wafanyabiashara wengi wanaamini kwamba mara wanaposajili jina chini ya sheria ya Makampuni basi haina haja ya kusajili jina hilo kama nembo ya biashara. Wanakosea. Ni rahisi zaidi kusajili sehemu zote mbili kuliko kupigana vita kama unayotaka kuianza.

Ili kuondoa nembo ya biashara katika orodha ya usajili, unahitaji kufanya maombi maalum kwa Msajili wa Nembo za Biashara. Utahitaji kutoa maelezo ambayo yanajikita kwenye kesi yako. Mmiliki wa nembo iliyosajiliwa naye anayo haki ya kujibu madai yako kabla hamjasikilizwa.

Sababu unazoweza kuzitoa kwenye maombi yako ni pamoja na wewe kuwa wa kwanza kuanza kuitumia, ushindani usio wa haki, na kuchanganya wateja. Ni vyema kumtumia mtaalam wa nembo za biashara ili aweze kukuongoza kwenye mchakato huu.

## Kutapeliwa na muuzaji wa kifaa cha kupima mionzi

**Muuzaji wa vifaa vya kitabibu aliiuzia hospitali yetu mashine ya matibabu kwa njia ya mionzi (CT-scan) ambayo ni ghali sana. Tuliifunga na muuzaji alituhakikishia kwamba inafanya kazi vizuri sana. Ilichukua wiki mbili kuifunga na tulitekeleza masharti yote ya ufungaji. Wakati wahandisi wa kigeni walipotukabidhi, ndani ya masaa mawili tu tuliwaarifu wahandisi hao na muuzaji kwamba mashine haifanyi kazi vizuri kama walivyotuhakikishia. Sisi siyo hospitali kubwa na ilituchukua miaka mingi kuweka akiba ili kununua mashine na mwishowe tumetapeliwa. Baada ya kuchunguza tuligundua kwamba mashine ile kwa sasa haitumiki kwani imeshapitwa na wakati siku nyingi kutokana na teknolojia mpya. Tufanye nini ili kurudishiwa pesa zetu kwa sababu tuliwalipa pesa zao zote? Muuzaji anasema tusome mkataba na siyo barua-pepe tulizotumiana kabla ya mkataba. Barua-pepe zinasema wazi kwamba mashine ni ya kisasa na imetumika kwa miezi michache tu. Tafadhali tuongoze.**

*16 Julai 2012*

Hii siyo mara yetu ya kwanza kusikia hospitali za ndani kutapeliwa na kununua mashine za kitabibu zilizopitwa na wakati. Ingawa tunakuonea huruma, maswali yako hayako moja kwa moja. Hivyo tunahitaji kuona mkataba mlioingia ili tuweze kuwaongoza. Hata hivyo, tutajaribu kujibu maswali yako kwa ujumla.

Kwanza, kwenye mkataba huwa kuna ahadi na masharti/hakikisho. Mnahitaji kuona ahadi na masharti ambayo msambazaji aliwapatia. Moja ya hakikisho huwa ni kwamba mashine lazima iwe kwenye hali nzuri. Kama hakuna kipengele hicho na mkanunua mashine kama ilivyo, basi itawawia vigumu kurudishiwa pesa zenu.

Pili, mnaweza kuangalia kama mkataba unasema kwamba mkataba huu ni mkataba kamili kati ya pande zote kuhusiana na masuala yaliyomo ndani yake na unachukua nafasi ya makubaliano mengine ya aina yoyote nje ya mkataba, kama yapo.

## Wanahisa tajiri, kampuni masikini

**Kuna kampuni kubwa sana na yenye mafanikio makubwa hapa Tanzania kiasi kwamba imefungua makampuni mengine madogo kwa kila biashara inayofanya. Ninaiuzia bidhaa moja ya hizi kampuni ndogo, na mara zote inasumbua kulipa. Maswali yangu mawili: inawezekanaje kampuni ndogo ishindwe kulipa madeni yake wakati wanahisa wake ni makampuni makubwa na inamilikiwa na watu wenye pesa? Pili, je, ninaweza kudai pesa zangu moja kwa moja kwa wanahisa?**

*29 Oktoba 2012*

Swali lako la kwanza la inawezekanaje kampuni ndogo ishindwe kulipa madeni yake hatuwezi kulijibu. Ni suala la kiuhasibu na uiulize ofisi ya uhasibu. Swali lako la pili ni la kufurahisa sana na tunalijibu hapa chini.

Wamiliki wa kampuni ni tofauti na kampuni yenyewe ikiwa na maana kwamba kampuni ni mtu kisheria au taasisi inayojitegemea na haitangamani na wanahisa. Wanahisa wanamiliki hisa za kampuni na siyo mali zake. Mali za kampuni zinamilikiwa na kampuni. Wanahisa vilevile kwa kawaida hawana wajibu wa kulipa madeni ya kampuni kwa kuwa kampuni ndiyo iliyokopa na siyo mwanahisa kwa majina yake. Kama umewahi kukopa utagundua kwamba benki inataka wanahisa kusaini dhamana binafsi ambayo itawafanya wanahisa walipe madeni ya kampuni kwa sababu kwa kawaida hawawajibiki kulipa madeni hayo moja kwa moja.

Ili uweze kuwafikia wanahisa na kuwafanya wawajibike, unahitaji kuondoa mwavuli/ kinga/dhana ya kisheria kwamba kampuni hubeba majukumu yake yenyewe nje ya wamiliki wake. Ili uweze kufanikiwa kuondoa dhana hiyo unahitaji kuonesha mambo haya mawili; kwamba kuna umoja wa umiliki kwenye kampuni na kwamba hakuna tofauti iliyopo baina ya wanahisa na kampuni; na pili kwamba kama Mahakama itakataa kuondoa dhana hiyo kutasababisha dhuruma, kikwazo ama udanganyifu.

Maombi ya kuthibitisha vigezo hivyo si kitu rahisi na kuna vizuizi/vikwazo kadhaa ambavyo ni muhimu kuviweka wazi. Hakuna idadi kamili au masharti ambayo kanuni hii inaweza kutumika. Wakati mwingine Mahakama imetumia tu moja ya mambo haya mawili. Mambo ya kuzingatia katika kuondoa kinga/dhana hiyo ya kisheria kwamba kampuni hubeba majukumu yake yenyewe nje ya wamiliki wake yanahusisha kuchanganya pesa na mali za taasisi mbili (yaani za mwanahisa na kampuni), kampuni moja kushikilia mali za kampuni nyingine ambayo ina madeni, kuwa na umiliki sawa wa kampuni mbili, kutumia ofisi hizo hizo na wafanyakazi wale wale, kutumika kwa kampuni moja kama kificho cha kampuni nyingine, kutokuzingatia taratibu za uendeshaji kampuni, kutokutenganisha taarifa za kampuni, mtu kuzichukulia mali za kampuni kama zake au kutumia wakurugenzi na maafisa wa kampuni.

Kuhusu sharti la pili, kitu cha msingi ni kuthibitisha nia mbaya kwenye vitendo vya kampuni. Kesi nyingi zimetoa fafanuzi zifuatazo juu ya mambo gani ambayo siyo sehemu ya nia mbaya ya kampuni; ugumu tu wa kutekeleza hukumu au kushindwa kukusanya madeni, mwanahisa kuipa pesa kampuni ndogo ili kuisaidia kutatua matatizo ya kifedha, ilimradi isiwe kwa lengo la kuendeleza udanganyifu. Matokeo mengine ni pale inapoonekana aina fulani ya kampuni inatumika kukwepa sheria au kanuni. Katika mazingira hayo pia, Mahakama imeonekana kuzikubali kesi za mikataba ambazo malalamiko yanahusu aina fulani ya udanganyifu.

Hivyo ili uweze kuondoa kinga/dhana ya kisheria ya kampuni kubeba majukumu yake yenyewe nje ya wamiliki wake, ni lazima ujiridhishe juu ya baadhi ya mambo yaliyoelezwa hapo juu. Kama ilivyoelezwa hapo awali kwamba kutengua dhana hii siyo kazi rahisi. Mwanasheria wako anaweza kukuongoza zaidi.

## Kufunga mitambo ya umeme kwenye ardhi binafsi

**Ninamiliki ploti Dar ambapo kuna kampuni fulani ambayo inazalisha na kusafirisha umeme ilinipa notisi kwamba inataka kutumia ardhi yangu kupitisha nyaya za umeme na watanilipa. Siwataki kwenye ardhi yangu bila kujali kama watanilipa ama la. Ninaweza kulipinga hili?**

*5 Novemba 2012*

Sheria ya Umeme inatamka kwamba kampuni yoyote yenye leseni ya kuzalisha au kusafirisha umeme itakuwa na haki ya kuingia kwenye ardhi yoyote ili kuisaidia kutekeleza majukumu yake ya kutoa umeme na mmiliki wa mali hataruhusiwa kuingilia haki au mali ya kampuni hiyo. Pia kampuni imeruhusiwa na sheria baada ya kutoa notisi kwa mmiliki wa eneo kuingia kwenye ardhi hiyo kwa malengo ya kufanya matengenezo ya mtambo huo. Hata hivyo makampuni hayo yanatakiwa kumlipa fidia mmiliki wa ardhi hiyo na kama kuna mgogoro wowote, mgogoro huo utatatuliwa na Mahakama yenye mamlaka.

Hivyo huwezi kumzuia mmiliki wa kampuni kuingia kwenye ardhi yako, kama utakuwa na tatizo unaweza kuwasiliana na mwanasheria wako ambaye atakusaidia kupinga Mahamani.

## Kupinga usajili wa alama/nembo ya biashara

**Ninamiliki alama ya biashara nchini Tanzania na hivi karibuni nimekutana na jarida la alama za biashara la Wakala wa Usajili, Biashara na Leseni (BRELA) likitangaza alama ya biashara ambayo kwa maoni yangu ni sawa, au inakaribiana sana na alama yangu ya biashara. Ninataka kuipinga. Tafadhali niongozeni juu ya nini cha kufanya.**

*11 Februari 2013*

Sheria ya Alama/Nembo za Biashara na Huduma inamtaka Msajili wa Alama za Biashara kutangaza alama ya biashara kwa siku 60 kabla ya kuisajili. Madhumuni ya kutangaza alama ni kutoa fursa kwa umma kupinga usajili wa alama hizo ikiwa ni sawa au zinafanana na alama zao zilizosajiliwa au zisizosajiliwa. Kwa hiyo ni wazo zuri kwa umma na mashirika mengine kufuatilia jarida la alama za biashara. Kuhusu pingamizi, unaweza kupeleka pingamizi lako kwa Msajili wa Alama kwa kujaza taarifa ya kupinga ambayo inatakiwa kuwasilishwa ndani ya siku 60 tangu siku ya tangazo na inatakiwa kuwa kwenye fomu maalum kama ilivyotolewa kwenye Kanuni.

Taarifa ya pingamizi inapaswa kueleza kwa ufasaha sababu za pingamizi na inashauriwa sana pia uambatanishe na picha za alama yako na uzilinganishe na zile zilizotangazwa ili kuonesha ufanano au muendano ambao unaweza kusababisha mkanganyiko kwa umma. Taarifa ya pingamizi ikishawasilishwa kwa Msajili wa Alama, Msajili atampatia nakala mwombaji ambaye naye atatakiwa kuwasilisha maelezo kinzani juu ya taarifa yako ndani ya siku sitini za kuipokea. Msajili atawasilisha maelezo kinzani kwako na atapanga siku ya kuwasikiliza. Mara atakapowasikiliza na kupitia ushahidi uliotolewa kwake atatoa maamuzi iwapo alama hiyo isajiliwe ama la. Kama hujaridhika na maamuzi ya Msajili, unaweza kukata rufaa Mahakama Kuu. Kwa msaada zaidi tafadhali wasiliana na mwanasheria wako.

## Kipengele cha usuluhishi kwenye mkataba

**Ninaingia mkataba wa usambazaji na kampuni ya kitanzania. Swali langu ni kwa nini kuwe na kipengele cha usuluhishi kwenye mkataba wakati Tanzania ina mfumo wa Mahakama? Kipengele kinasomeka hivi: "Kutakuwa na msuluhishi mmoja atakayeteuliwa na pande zote mbili kwa pamoja kwa gharama za pande zote". Nini kitatokea kama hatutakubaliana juu ya uteuzi wa msuluhishi?**

*11 Machi 2013*

Usuluhishi ni njia mbadala ya utatuzi wa mgogoro na ni mbinu mojawapo ya usuluhishi nje ya Mahakama ambayo pande zenye mgogoro zinawasilisha mgogoro huo kwa mtu mmoja au zaidi anayeitwa

msuluhishi ambapo pande hizo zinakubali kufungwa na maamuzi ya msuluhishi ambayo yanaitwa tuzo. Ni mbinu ya usuluhishi ambapo msuluhishi anasikiliza kesi na kutoa maamuzi ambayo kisheria yatazibana pande zote.

Usuluhishi una faida zake. Kutegemea na ukubwa wa makubaliano, kwa kawaida utatuzi wa migogoro kwa usuluhishi ni njia rahisi, ya kuaminika, ya haraka, haina usumbufu na ni bora zaidi tofauti na Mahakama ambazo zinafungwa sana na kanuni ambazo wakati mwingine ni mzigo na ni ghali. Kupeleka mgogoro kwenye usuluhishi hakuishushii hadhi Mahakama kwa sababu bado unatakiwa uende Mahakamani ili kusajili tuzo ili iweze kuwa amri ya Mahakama kwa ajili ya utekelezaji. Kwa sasa, njia ya usuluhishi imeisaidia Mahakama kupunguza mrundikano wa kesi zinazosajiliwa Mahakamani. Kwa mikataba mikubwa, tunapendekeza kipengele cha mkataba kiwe na wasuluhishi wawili wanaoteuliwa na kila upande, na wao wamteue msuluhishi wa tatu ambaye anaJulaikana kama mwamuzi, na kuifanya idadi ya wasuluhishi kuwa watatu. Wakati mwingine hii inaonekana kuwa ghali na hivyo pande zenye mgogoro huamua kumteua msuluhishi mmoja tu.

Nchini Tanzania usuluhishi unaongozwa na Sheria ya Usuluhishi ambayo inatoa mamlaka kwa Mahakama kumteua msuluhishi pale ambapo hajateuliwa. Sheria hii inaipa Mahakama mamlaka ya kumteua msuluhishi, mwamuzi au msuluhishi wa tatu katika mazingira yafuatayo: (a) pale ambapo makubaliano yanasema mgogoro utawasilishwa kwa msuluhishi mmoja na baada ya mgogoro kuibuka pande zote mbili hawakubaliani na uteuzi wa msuluhishi; (ii) kama msuluhishi aliyeteuliwa amepuuza au amekataa au hawezi kusuluhisha na nafasi yake haijajazwa na pande zote hazijaziba nafasi; (c) pale ambapo pande zote mbili zimeteua wasuluhishi ambao wamepewa uhuru wa kumteua mwamuzi au mtu wa tatu na hawajamteua; (d) pale mwamuzi au mtu wa tatu amekataa, hawezi au amefariki na nafasi yake ipo wazi na wasuluhishi hawajaziba nafasi yake, yeyote kati yao anaweza kutoa notisi kwa pande zenye mgogoro au wasuluhishi, kulingana na mazingira, ya kukubaliana kumteua msuluhishi, mwamuzi au mtu wa tatu.

Sheria pia inaeleza kwamba iwapo uteuzi haujafanyika ndani ya siku saba tangu siku ya kupata notisi, Mahakama inaweza, kwa maombi ya upande uliotoa notisi na baada ya kuusikiliza upande mwingine, kumteua msuluhishi, mwamuzi au msuluhishi wa tatu ambaye atakuwa na mamlaka sawa ya kusikiliza mgogoro na kutoa tuzo/uamuzi kana kwamba ameteuliwa kwa idhini ya pande zote. Pia tunakushauri uweke kipengele cha mahali pa kufanyia usuluhishi na lugha itakayotumika wakati wa usuluhishi. Kupeleka mgogoro kwenye usuluhishi hakuchukui haki yako ya kupeleka maombi yenye udharula Mahakamani, na Mahakama katika maamuzi yake yoyote itakayotoa itazingatia kwamba pande zote zimekubaliana kusuluhishwa.

## Deni dhidi ya Wizara

**Niliiuzia Wizara nchini Tanzania vifaa vya matibabu na sijawahi kulipwa licha ya ahadi lukuki. Mwanasheria wangu anasema kwamba kuishtaki Wizara moja kwa moja haiwezekani. Sielewi kwa nini. Je, Serikali inalinda kesi kama hizo? Tafadhali niongoze.**

*25 Machi 2013*

Inawezekana kabisa kuishtaki Serikali kwa mujibu wa Sheria ya Mashtaka ya Serikali. Kifungu cha 6 cha Sheria kinaeleza bila utata kwamba, bila kujali masharti ya vifungu vingine kwenye Sheria hii, kesi za madai zinaweza kufuguliwa dhidi ya Serikali kwa masharti ya kifungu hiki. (2) Hakuna kesi

dhidi ya Serikali itafunguliwa na kusikilizwa isipokuwa mlalamikaji amewasilisha mapema kwenye idara au afisa anayehusika notisi siyo chini ya siku tisini juu ya nia yake ya kuishtaki Serikali, ikieleza msingi wa dai lake dhidi ya Serikali na atatuma nakala ya dai lake kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. (3) Kesi zote dhidi ya Serikali, baada ya kuwasilishwa kwa taarifa zifunguliwe dhidi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, na nakala ya hati ya mashtaka ipelekwe kwenye wizara ya Serikali, idara au afisa ambaye anatuhumiwa kutenda kosa hilo ambalo ni msingi wa shtaka la madai. (4) Kesi zote dhidi ya Serikali zitafunguliwa Mahakama Kuu kwenye Kitengo cha Mahakama Kuu eneo ambapo dai limetokea. (5) Bila kujali masharti ya kifungu kidogo cha (3), Mwanasheria Mkuu anaweza, isipokuwa mtu mwingine anastahili kushtakiwa, kushtakiwa au kuunganishwa kama mashtakiwa mwenza, kwenye kesi yoyote dhidi ya Serikali. (6) Vifungu vya Sheria ya Watumishi wa Umma (Malipo ya Madeni) vitatumika kwa afisa aliyeisababishia Serikali kupata hasara, gharama na fidia kutokana na kushindwa kwake kupata uwakilishi wa kisheria kwenye kesi. Hivyo, kutokana na maelezo hapo juu unaweza kuona kwamba unahitaji kutoa notisi ya siku 90 kabla ya kufungua shtaka.

## Kipengele cha usuluhishi kinazuia kukata rufaa

**Niliingia mkataba na kampuni ambayo imeingiza kipengele cha usuluhishi kinachosema kwamba tuzo hiyo ni ya mwisho, ina nguvu za kisheria na haiwezi kukatiwa rufaa. Usuluhishi ulifanyika nchini Kenya, ni wazi tuzo hiyo ukiisoma inakwenda kinyume na sera za umma na inakiuka sheria za Tanzania. Mkataba uliitaka kampuni yetu kutekeleza mkataba nchini Tanzania na kutumia sheria za Tanzania. Je, tuzo hiyo inaweza kutekelezwa nchini Tanzania ikiwa ni kinyume na sheria za hapa? Mwanasheria wangu anasema kuwa kutokukata rufaa dhidi ya tuzo hiyo kunaiweka kampuni yetu katika nafasi mbaya. Tafadhali niongoze.**

*1 Aprili 2013*

Usuluhishi unakusudia kuharakisha upatikanaji wa haki. Kwa kawaida tuzo haiwezi kupingwa isipokuwa kwa kanuni za haki ya asili na pale ambapo wasuluhisi wamekuwa na utendaji mbovu. Tuzo pia haiwezi kutekelezwa kama ipo kinyume na sera ya umma na inakiuka sheria za nchi ambako utekelezaji utafanyika. Hayo yakiwa kichwani mwako, kwa kuwa unadai tuzo inakiuka sera ya umma na sheria za nchi, tuzo inaweza kufutwa. Hilo pia limetamkwa chini ya Sheria ya Usuluhishi ya Tanzania ambapo kifungu cha 16 kinatamka wazi kwamba pale msuluhishi au mwamuzi ametenda vibaya au usuluhishi au tuzo imepatikana isivyo halali, Mahakama inaweza kutengua tuzo hiyo.

Kifungu cha 30 cha Sheria ya Usuluhishi pia kinatamka kama ifuatavyo: Masharti ya utekelezaji wa tuzo za kigeni; (1) Ili tuzo ya kigeni iweze kutekelezwa chini ya sehemu hii, ni lazima: (a) iwe imetokana na mkataba wa usuluhishi ambao ni halali chini ya sheria iliyo uongoza; (b) imetokana na baraza lililoundwa chini ya makubaliano na liliundwa kwa namna pande zilivyokubaliana; (c) imetolewa kwa kuzingatia sheria zinazoongoza usuluhishi kiasi cha kuuwezesha upande wowote kuchukua hatua muhimu kubatilisha tuzo kwenye chombo chenye mamlaka; (d) imekamilika kwenye nchi ilikotolewa; na (e) inahusu masuala ambayo ni halali kufanyiwa usuluhishi chini ya Sheria za Tanzania na utekelezaji wake ni lazima uwe haukinzani na sera ya umma au sheria za Tanzania. (2) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo hiki, tuzo ya kigeni haitatekelezwa chini ya sehemu hii kama Mahakama imeridhika

kwamba (a) tuzo imebatilishwa kwenye nchi ilikotolewa; au (b) mtu ambaye tuzo inatakiwa kutekelezwa dhidi yake hakupewa taarifa za usuluhishi kwa muda wa kutosha kumwezesha kupeleka utetezi wake au alishindwa kutokana na sababu za kisheria na hakuwakilishwa vyema; au, (c) tuzo haijajibu maswali yote yaliyowasilishwa au inamaamuzi juu ya mambo ambayo yapo nje ya makubaliano ya usuluhishi: Isipokuwa kama tuzo haijajibu maswali yote yaliyowasilishwa Mahakama inaweza, ikiona vyema, ama kuahirisha utekelezaji wa tuzo au kuamuru utekelezaji wake kwa masharti ya kutoa dhamana kwa mtu anayeomba kutekeza tuzo hiyo kama Mahakama itaona inafaa. (3) Kama mtu anayepinga utekelezaji wa tuzo ya kigeni anathibitisha kwamba kuna sababu zaidi ya kutokuwepo kwa masharti yaliyoainishwa kwenye aya (a), (b) na (c) ya kifungu kidogo (1) cha kifungu hiki, au uwepo wa masharti yaliyoainishwa kwenye aya ya (b) na (c) ya kifungu kidogo (2) cha kifungu hiki kinachompa haki ya kupinga uhalali wa tuzo, Mahakama inaweza, kama itaona inafaa, ama kukataa kutekeleza hukumu ama kuahirisha usikilizaji hadi kupita kwa muda ambao Mahakama itaona unafaa. Kabla hujajiamini kupita kiasi kuhusu maoni yako, unatakiwa umtafute mwanasheria wako akuongoze.

## Benki haifuati maagizo

**Ninauza vocha za simu na kuweka fedha zangu kwenye benki moja kubwa huko Mtwara. Ninapokwenda benki, nategemea msarifu kutenganisha noti za Shilingi 500, 1000, 2000 na 5000. Tatizo ambalo linanikabili kwa sasa ni kwamba meneja mpya ameniambia nizitenganishe mwenyewe kwa sababu inampotezea muda msarifu. Nashindwa kuelewa kwa nini benki haitaki kufanya kazi yake. Je, ninaweza kuishtaki benki?**

*3 Juni 2013*

Ikiwa uliingia kwenye aina hiyo ya "makubaliano ya kutenganisha" na benki yako, hapo benki inavunja wajibu wake. Hata hivyo, kwa tujuavyo mazoea ya soko nchini Tanzania na kwingineko, hatujawahi kukutana na benki inayopokea fedha rundo na kuanza kuzitenganisha kabla ya kuziweka. Uhusiano wa kawaida wa benki ya mteja ni kwa benki kulinda fedha zako. Unapaswa kushauriana na wanasheria wako lakini hakuna uwezekano wa kuiwajibisha benki.

## Kuvunja mkataba

**Ninataka kuvunja mkataba ambao niliingia. Ni sababu gani za kisheria ambazo ninaweza kuzitumia ili kuvunja?**

*8 Julai 2013*

Mikataba inatakiwa kuheshimiwa na sheria inakusudia kuhakikisha kwamba pande zinazoingia mkataba zinaheshimu kusudio la mkataba ili kuhakikisha kwamba biashara hazianguki. Sheria ya Mikataba, hata hivyo, inawapa wahusika katika mkataba sababu nyingi za kuvunja mkataba ikiwa tu sababu hizo ni halali. Unaweza kuvunja mkataba kama uliuingia kwa shurutisho, kudanganywa, yaani upande mwingine ulikuficha mambo ya msingi kuhusu mkataba, ubatili wa mkataba au kiini cha mkataba, kukosea jambo, yaani akili za pande za mkataba hazikuendana, kama ni mdogo/mtoto, yaani yupo chini ya miaka 18, kuvunja masharti ya mkataba, masharti ya awali hayakutekelezwa, n.k. Tunashauri mwanasheria wako akuongoze kwenye mkataba wako kabla hujafanya chochote.

## Kukodisha alama ya biashara

**Ninamiliki alama fulani ya biashara ambayo inakua sokoni. Nimefuatwa na wageni kutoka nje ya nchi ambao wanataka kutumia alama yangu ya biashara na wameniomba niwauzie. Sitaki kuuza alama**

**yangu ya biashara. Ninaweza kuzikodishia kampuni hizi alama yangu ya biashara ili niendelee kuimiliki na kuifurahia baada ya mkataba wa kuikodisha kuisha? Tafadhali niongoze.**

*1 Julai 2013*

Una wazo jema. Kwa bahati nzuri, Sheria ya Alama za Biashara na Huduma inamruhusu mmiliki wa alama ya biashara kuikodisha kwa mtu mwingine. Ila, inabidi uelewa kwamba ukodishwaji huo ni lazima usajiliwe kwa Msajili wa Alama za Biashara. Mchakato wa ukodishaji siyo mgumu. Wanasheria wako wanaweza kukuongoza zaidi.

## Upatanishi mahakama ya biashara

**Nimefungua kesi Mahakama ya Biashara Masjala ya Dar es Salaam dhidi ya mtu ambaye sitaki kumuona tena kwenye maisha yangu. Nimeshangaa kwamba Mahakama imeamuru kwamba tujaribu kutatua jambo hilo kwa njia ya upatanishi. Je, hiyo ni lazima, ukizingatia sitaki kupatana na huyu mhuni?**

*22 Julai 2013*

Kanuni za Mahakama ya Biashara zinatamka kwamba mtu ambaye anaingia kwenye upatanishi atakuwa na mamlaka ya mwisho ya kupatana juu ya suala lolote wakati wa upatanishi. Kanuni zinaendelea kusema kwamba, mtu anayehitaji idhini ya mtu mwingine kabla ya kupatana, kabla ya muda wa kuanza upatanishi, atapanga namna ya kuwasiliana na mtu huyo wakati wote wa upatanishi, bila kujali kama utafanyika wakati wa saa za kazi au baada ya saa za kazi.

Kama kesi haikutatuliwa au ilifutwa chini ya kanuni hizi, Mahakama itazielekeza pande zote kwenda kwenye upatanishi baada ya kutoa amri hiyo, Mahakama itamteua mpatanishi ambaye, ndani ya siku 7 baada ya kuteuliwa, atapanga tarehe ya kwanza ya upatanishi. Kanuni pia zinatamka kwamba pande au wakili wake au wote, kama wanawakilishwa, wataarifiwa kwa kutumia Fomu Na. 3 iliyopo kwenye Jedwali, na watahudhuria kipindi cha upatanishi, isipokuwa kama Mahakama itaamuru vinginevyo.

Kutokana na maelezo hapo juu, unaweza kuona kwamba upatanishi ni lazima. Hata hivyo, Mahakama inakuruhusu kumtuma mwakilishi ambaye atawasiliana na wewe ili uweze kukubali au kukataa upatanishi. Pia elewa kwamba, upatanishi hauharibu kesi yako hivyo usijali kwa sababu upatanishi unafanyika kwa usiri.

## Kudanganywa na benki ya kigeni

**Benki ya kigeni ilikuja Tanzania na kuniahidi faida kubwa kwa uwekezaji mpya wa huduma/bidhaa ambazo ilikuwa inazianzisha Mashariki ya Mbali. Niliona huduma/bidhaa hiyo ina faida kubwa lakini mwishowe nilijikuta tayari nimepoteza asilimia 30 ya uwekezaji wangu. Kulikuwa na mambo ya msingi sana ambayo benki haikuniweka wazi. Je, ninaweza kushtaki?**

*28 Oktoba 2013*

Kwanza kabisa, ni batili kwa benki kushawishi biashara nchini Tanzania. Kama wewe ni Mtanzania, pia ni batili kwako kufanya shughuli za kibenki nje ya nchi bila idhini ya Benki Kuu ya Tanzania. Kwa kuzingatia maelezo hapo juu, kama unaamini kwamba benki ilikudanganya, una kesi dhidi yake na unaweza kuishtaki. Hata hivyo kesi yako itazingatia kipengele cha uchaguzi wa sheria kilichopo kwenye mkataba ulioingia, ambapo uwezekano mkubwa itakuwa ni kufuata sheria za nchi ambako benki imesajiliwa. Kabla ya kushtaki tunapendekeza umuone mwanasheria mbobevu kwenye masuala ya benki za kimataifa. Ni lazima uelewe kuwa hakuna uwekezaji usio na vikwazo. Msemo wa zamani (wa kihasibu) ni

sahihi, kwamba: "Kadiri vikwazo vya biashara vinavyokuwa vingi, ndivyo biashara hiyo inavyotegemewa kutoa faida kubwa".

## Upande mwingine kushindwa kumteua msuluhishi

**Tupo kwenye mgogoro na upande mwingine ambapo mkataba unatoa usuluhisi wenye wasuluhishi watatu. Mimi nimeshamteua msuluhishi wangu lakini upande mwingine unapiga chenga/unachelewa kumteua msuluhishi wake kwa miezi 2 sasa. Je, nifanye nini?**

*3 Februari 2014*

Kifungu cha cha Sheria ya Usuluhishi kinaeleza wazi kwamba pale mkataba unaposema mgogoro utasuluhishwa na wasuluhishi watatu, kila upande kuteua msuluhishi mmoja na msuluhishi wa watatu kuteuliwa na wasuluhishi wawili walioteuliwa na pande mbili, isipokuwa kama kutakuwa na nia tofauti – kama upande mmoja umeshindwa kumteua msuluhishi ndani ya siku saba baada ya upande mwingine kumteua msuluhishi wake, na ameupatia upande unaokaidi notisi ya kufanya uteuzi, upande ulioteua msuluhishi unaweza kumteua msuluhishi huyo kuwa msuluhishi pekee kwenye mgogoro na tuzo ya msuluhishi huyo itazibana pande zote mbili kama kana kwamba aliteuliwa kwa idhini ya pande zote. Hivyo, kwa kuwa upande mwingine hauteui msuluhishi wake, unaweza kuendelea na msuluhishi mmoja na tuzo itaubana upande wa pili bila kujali kwamba kipengele cha usuluhishi kilikuwa kinatamka wasuluhishi watatu. Mwanasheria wako anaweza kukuongoza zaidi.

## Kutishiwa uhujumu uchumi

**Mimi ni muuzaji wa bidhaa za madawa muhimu pamoja na mashine kwenye baadhi ya hospitali za Serikali na kwa mwaka mmoja sasa hawajanilipa. Kiasi ninachowadai hivi sasa kinakaribia mamilioni ya Dola na nimekuwa napewa ahadi hewa. Nilitoa onyo la mwisho kwa mamlaka husika lakini niliambiwa niende kuonana na mtu mkubwa ambaye mara ya kwanza aliniambia nitalipwa, lakini baada ya kujibu kwamba siamini jambo hili na kwamba nitasitisha usambazaji na kuwashtaki, alinitishia kwamba kama nitafanya hivyo, nitashtakiwa chini ya Sheria ya Makosa ya Uhujumu Uchumi. Kwa ufupi alisema kwamba chini ya sheria za Tanzania, hasa sheria hii, bidhaa hizi ni muhimu kwenye mahospitali na sina hiari zaidi ya kuendelea kuzisambaza. Pia ameniambia kwamba kosa hili halina dhamana. Nifanye nini?**

*3 Februari 2014*

Hii ni mara yetu ya kwanza kusikia staili hiyo juu ya wajibu wa kulipa kimkataba. Kama alichokisema afisa huyo ni kweli, basi muuzaji yeyote wa vitu muhimu kwa uchumi, iwe nishati, maji, au ulinzi hawezi kushtaki wala kudai. Na hakuna mtu atakayekuwa tayari kufanya biashara na Serikali ya Tanzania na itakuwa inakiuka misingi muhimu ya sheria za mikataba.

Kwa kujibu swali lako, tukichukulia umetupatia maelezo sahihi, hakuna kinachokuzuia kusitisha huduma, kudai malipo na kushtaki kwa mujibu wa mkataba wa uuzaji. Uhujumu uchumi umeelezewa chini ya sheria na unahusu vitendo vilivyofanyika bila sababu za msingi na kwa malengo ya kuzorotesha uchumi au maslahi ya Tanzania au vinavyoweza kuharibu, kuzuia au kuingilia utoaji wa hudumu muhimu au uendeshaji wake.

Kutokana na tafsiri hiyo, huwezi kushtakiwa chini ya sheria hii kwa kuwa unadai kihalali fedha zako chini ya mkataba wa uuzaji/usambazaji. Kama ungekuwa unafanya hivyo kinyume na sheria kwa lengo la kuzorotesha

uchumi au maslahi ya Tanzania, sheria hiyo ingetumika.

Kuhusu dhamana, tafadhali elewa kwamba hili ni kosa lenye dhamana. Hata hivyo, dhamana haitatolewa kwenye mazingira yafuatayo: (a) kama inaonekana kwamba mtuhumiwa hapo awali aliwahi kuhukumiwa kwa kifungo cha miaka inayozidi mitatu; (b) kama mtuhumiwa hapo awali aliwahi kupewa dhamana na Mahakama na alishindwa kutii masharti ya dhamana au alitoroka; (c) kama mtuhumiwa ameshtakiwa kwa kosa la uhujumu uchumi linalodaiwa kufanyika wakati mtuhumiwa ameachiwa kwa dhamana na Mahakama; (d) kama itaonekana mbele ya Mahakama kwamba ni muhimu mshtakiwa awekwe mahabusu kwa ulinzi au usalama wake; (e) kama kosa ambalo mtu anashtakiwa nalo linahusu mali yenye thamani inayozidi Shilingi milioni kumi isipokuwa kama mtu huyo ataweka dhamana ya mali inayolingana na nusu ya thamani ya mali iliyohusika na inayobaki imewekewa dhamana; na (f) Kama ameshtakiwa kwa kosa lililo chini ya Sheria ya Madawa Hatarishi.

## Utekelezaji wa tuzo ya usuluhishi nchini Tanzania

**Tupo kwenye majadiliano na Serikali kuhusu mradi wenye thamani ya mabilioni ya Dola ambao tunataka uwe na kipengele cha usuluhishi kinachoruhusu kutumia ama sheria za Kituo cha Kimataifa cha Utatuzi wa Migogoro ya Uwekezaji (ICSID) au Mahakama ya Kimataifa ya Biashara (ICC). Je, Serikali ya Tanzania inakubali kufanya usuluhishi na kama jibu ni ndiyo, je tuzo husika inaweza kutekelezwa nchini Tanzania? Ni sababu zipi zinazoweza kutumika kukataa tuzo ya usuluhishi ya kigeni? Kama tukiishinda Serikali, je inaweza kudai kwamba tuzo inakwenda kinyume na sera ya umma hasa ikiwa haina fedha za kulipa? Je, Serikali inazingatia kwa kiasi gani usuluhishi?**

*17 Februari 2014*

Serikali inaingia mikataba mingi tu ambayo usuluhishi ni njia mojawapo inayotumika kutatua migogoro. Tanzania pia imeridhia mikataba ya kimataifa inayotambua utekelezaji wa tuzo zinazotokana na usuluhishi.

Kifungu cha 30 cha Sheria ya Usuluhishi kinatoa masharti ya utekelezaji wa tuzo za kigeni kama ifuatavyo; (1) Ili tuzo ya kigeni iweze kutekelezwa chini ya sehemu hii, ni lazima: (a) iwe imetokana na mkataba wa usuluhishi ambao ni halali chini ya sheria iliyouongoza; (b) imetokana na baraza lililoundwa chini ya makubaliano na liliundwa kwa namna pande zilivyokubaliana; (c) imetolewa kwa kuzingatia sheria zinazoongoza usuluhishi kiasi cha kuuwezesha upande wowote kuchukua hatua muhimu kubatilisha tuzo kwenye chombo chenye mamlaka; (d) imekamilika kwenye nchi ilikotolewa; na (e) inahusu masuala ambayo ni halali kufanyiwa usuluhishi chini ya Sheria za Tanzania na utekelezaji wake ni lazima uwe haukinzani na sera ya umma au sheria za Tanzania. (2) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo hiki, tuzo ya kigeni haitatekelezwa chini ya sehemu hii kama Mahakama imeridhika kwamba (a) tuzo imebatilishwa kwenye nchi ilikotolewa; au (b) mtu ambaye tuzo inatakiwa kutekelezwa dhidi yake hakupewa taarifa za usuluhishi kwa muda wa kutosha kumwezesha kupeleka utetezi wake au alishindwa kutokana na sababu za kisheria na hakuwakilishwa vyema; au (c) tuzo haijajibu maswali yote yaliyowasilishwa au inamaamuzi juu ya mambo ambayo yapo nje ya makubaliano ya usuluhishi:

Isipokuwa kama tuzo haijajibu maswali yote yaliyowasilishwa Mahakama inaweza, ikiona vyema, ama kuahirisha utekelezaji wa tuzo au kuamuru utekelezaji wake kwa masharti ya kutoa dhamana kwa mtu anayeomba kutekeza tuzo hiyo kama Mahakama itaona inafaa. (3) Kama mtu anayepinga utekelezaji wa tuzo ya kigeni anathibitisha kwamba kuna sababu zaidi ya kutokuwepo kwa masharti yaliyoainishwa kwenye aya (a), (b) na (c) ya kifungu kidogo (1) cha kifungu hiki, au uwepo wa masharti yaliyoainishwa kwenye aya ya (b) na (c) ya kifungu kidogo (2) cha kifungu hiki kinachompa haki ya kupinga uhalali wa tuzo, Mahakama inaweza, kama itaona inafaa, ama kukataa kutekeleza hukumu ama kuahirisha usikilizaji hadi kupita kwa muda ambao Mahakama itaona unatosha ili kuuwezesha upande huo kuchukua hatua muhimu kuliwezesha baraza lenye mamlaka kubatilisha tuzo.

Jambo jingine ambalo umelionesha, na ambalo mara nyingi linatumika ni sera ya umma ya kwamba iwapo tuzo itaruhusiwa kutekelezwa kwenye nchi ambayo inakwenda kutekelezwa ni kinyume na sera ya umma. Kwa ujumla, kutokuwepo kwa fedha siyo suala la sera ya umma na hivyo kuzuia utekelezaji wa tuzo ya usuluhishi. Kama itathubutu kufanya hivyo, Tanzania itakuwa inavunja mikataba ya kimataifa ya usuluhishi.

Kuhusu Serikali inaupa uzito gani usuluhishi, tafadhali elewa kwamba Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali inajishughulisha na mashauri mengi tu ya usuluhishi nje ya nchi, na inauchukulia usuluhishi kwa uzito mkubwa. Pamoja na kuupa usuluhishi uzito mkubwa, kama Serikali haitakwenda kwenye usuluhishi au ikishindwa kusimamia mchakato wa usuluhishi vizuri, itaharibu sifa ya nchi kwenye nyanja za kimataifa za biashara. Na hili siyo jambo ambalo Tanzania inaweza kulimudu katika hatua ya sasa ya ushindani wa kimataifa. Tunashauri upate ushauri wa kitaalam/maalum kutoka kwa mwanasheria wako.

## Mgogoro wa mpaka kwenye eneo la utafutaji gesi

**Tuna mgogoro na jirani ambaye ni mmiliki wa kitalu/eneo la utafutaji gesi na ametishia kupeleka mgogoro wetu kwa Kamishna wa Nishati na Petroli. Je, Kamishna huyu ana mamlaka ya kuamua mgogoro huu, na kama ndiyo, je maamuzi yake yanaweza kukatiwa rufaa?**

*24 Februari 2014*

Majibu ya maswali yako yote mawili ni ndiyo. Kamishna wa Masuala ya Nishati na Petroli anaruhusiwa kuamua migogoro kama hiyo. Pia, ni kweli, maamuzi yake yanaweza kukatiwa rufaa. Hili limeelezwa chini ya Sheria ya Utafutaji na Uzalishaji Petroli, 1980, ambapo inaeleza ifuatavyo:

Kamishna anaweza kufanya uchunguzi juu ya na kuamua kuhusu migogoro baina ya watu wanaojihusisha na utafutaji au uendeshaji, ama miongoni mwao wenyewe au miongoni mwao na pande nyingine (isipokuwa Serikali) zisizohusika, kuhusinana na (a) Mipaka ya eneo lolote la utafutaji au uendeshaji; (b) kitendo chochote kilichofanyika au kuacha kufanyika, au kinachodaiwa kufanyika au kutokufanyika, katika, au kuhusiana na utafutaji uendelezaji; (c) makadirio na malipo ya fidia kwa mujibu wa Sheria hii; au (d) masuala mengine yoyote ambayo yapo kwenye sheria.

Mtu yeyote ambaye hajaridhika na maamuzi, tuzo au amri ya Kamishna iliyotolewa kwa mujibu wa sehemu hii anaweza kukata rufaa kwenda Mahakama

Kuu ndani ya siku 60 baada ya kutolewa kwa maamuzi, tuzo au amri.

## Wanasayansi wa Magharibi wanadanganya uduni wa Afrika

**Mimi ni mwanasayansi na nimegundua mbinu/siri ambayo mataifa ya Magharibi yanaitumia kuhakikisha kwamba Afrika tunaendelea kubaki nyuma. Ninakaribia kutoa chapisho kwenye moja ya jarida maarufu kwamba fomula ya Kani = Tungamo X Mchapuko (F=MA) inapotosha na haina uhalisia kwa Afrika. Kutumia kwetu fomula hii kunatufanya tusiendelee. Nifanye nini kuiokoa Afrika? Ninaweza kumshtaki mvumbuzi?**

*4 Agosti 2014*

Kwanza tunapenda kukushukuru kwa kutuandikia kutoka Gaborone. Kama ilivyo kawaida yetu, tutakueleza ukweli, au kile tunachokiamini kuwa ni ukweli. Tunatumaini majibu yetu ya kawaida na kweli hayatakukasirisha na utaendelea kuwa msomaji wa safu yetu.

Fomula ya F=MA imekuwepo kwa mamia ya miaka iliyopita, na ilivumbuliwa na Bwana Isaac Newton. Sheria ya Newton imethibitishwa kwa kufanyiwa utafiti na uchunguzi kwa zaidi ya miaka 200, na ni kipimo bora kabisa cha mienendo yetu ya kila siku ya maisha. Fomula hii imefanya kazi katika miradi yote mikubwa ya kiuhandisi ambayo tumewahi kuisoma. Kimsingi fomula hii ni kati ya fomula zinazotumika sana na imefanya kazi ulimwenguni kote. Haina mipaka ya kijografia wala kisiasa, na inafanya kazi kwenye mazingira yote na bara lolote duniani.

Tunashindwa kuona mantiki ya swali lako kivipi unadai kwamba fomula imeisababisha Afrika kuwa nyuma. Hujatoa uthibitisho wowote kuhusu dai lako na tunaliona halina mashiko kusema kweli.

Kumshtaki Bwana Isaac Newton leo hii haiwezekani kwa kuwa huna haki ya kumshtaki. Pia, hakupandikiza fomula hii kwetu na hivyo hauna haki ya kumshtaki kwa namna yoyote ile. Uwezekano wa kuwashtaki warithi wake pia uko mbali sana. Pamoja na utafiti wako kuhusu F=MA, unaweza pia kuangalia mambo mengine yaliyopelekea matatizo ya Afrika.

Pia tunakushauri uzungumze na wataalamu wengine kwenye tasnia/fani yako ambao wanaweza kuoanisha F=MA na matatizo ya Afrika. Tunashindwa kuona uhusiano wowote na tumepata mtanziko.

## Hakuna kampuni Tanzania yenye uwezo wa kutukatia bima

**Sisi ni kampuni kubwa nchini Tanzania na jumla ya hatari na hasara zote tunazotaka kuzikatia bima ni kubwa kuliko uwezo wa kifedha/mtaji wa kampuni zote za bima za ndani ukiziunganisha pamoja. Hatuna amani kukata bima ya ndani. Je, ni lazima kukata bima ya ndani? Tunaweza kujikatia bima wenyewe? Tunawezaje kulishughulikia jambo hili?**

*25 Agosti 2014*

Sheria ya Bima iko wazi na inataka hatari na hasara zote kukatiwa bima na makampuni ya nchini Tanzania. Kifungu cha 133 cha sheria hii kinatamka kwamba (1) Waziri, kwa kanuni, ataelekeza kwamba sehemu ya bima au bima zote zinazogusa Watanzania au makampuni yaliyopo Tanzania ya aina yoyote kukata bima kwa makampuni ya Kitanzania. (2) Iwapo aina ya bima inayotakiwa kukatwa kwenye kampuni ya ndani haipatikani kwa mtu anayetaka bima hiyo, mtu huyo atakata bima ya kampuni isiyo ya Kitanzania isipokuwa kwamba (a) mtu huyo atapata kwanza idhini ya maandishi ya Kamishna; na (b) anatekeleza masharti ya kifungu cha 140. (3) Hakuna chochote kwenye kifungu hiki kitakachoathiri

matakwa ya vifungu vya sheria kuhusu fedha za kigeni zitakazo kuwa zikitumika wakati huo nchini Tanzania au chini ya udhibiti wa Benki Kuu ya Tanzania.

Zaidi, kifungu cha 140 kinaeleza kwamba sera yoyote ya bima inayomgusa Mtanzania au inayoigusa kampuni iliyosajiliwa Tanzania, ukiachilia mbali kampuni ya bima iliyosajiliwa chini ya Sheria hii, inayotolewa na kampuni ya bima ya kigeni itatolewa kupitia ofisi za wakala wa bima aliyesajiliwa Tanzania.

Kutokana na maneno ya vifungu tajwa hapo juu, ingawa ni lazima kukata bima kwa makampuni ya bima ya ndani, una hiari ya kupata msamaha wa kufanya hivyo kwa kumwandikia Kamishna wa Bima ili kupata idhini yake huku ukieleza kwa nini hatari husika haiwezi kukatiwa bima nchini. Kukosa uwezo kwa kampuni za ndani inaweza kuwa ni sababu nzuri lakini kampuni za ndani za bima zinaweza kuikabili hatari kupitia wakala wa ndani.

Hivyo, huwezi kujikatia bima wewe mwenyewe. Tunakusihi sana uwasiliane na wakala wako wa bima na/au Kamishna wa Bima ili kuona kwamba hatari husika inalindwa na sheria za ndani, vinginevyo unaweza kupata changamoto wakati wa kuwasilisha madai ya fidia.

Pia, unaarifiwa kwamba bila idhini ya Kamishna, fedha utakayolipwa na kampuni ya bima ya kigeni kama fidia ya madai yako, itatozwa kodi nchini kwa sababu ulikata bima kwa kukiuka Sheria ya Bima.

Mwisho, njia mojawapo ya kuepuka kukata bima kwenye kampuni za ndani ni kutumia kampuni mama kukatia bima mali zake zilizopo nje ya nchi. Hili haliwezi kuJulaikana kwenye sheria yetu kwa sababu ni maslahi yako yaliyopo nje ya nchi. Hata hivyo, hili linatakiwa kushughulikiwa kwa kufanya uchambuzi wa kina wa jambo husika, mtaalam wako wa bima anaweza kukuongoza juu ya hili.

## Kamishna anaelekeza madai yalipwe

**Je, Kamishna wa Bima anaweza kuilazimisha kampuni ya bima kulipa madai hata kama hayalipiki? Je, ni kitu gani ambacho kampuni ya bima inaweza kufanya dhidi ya uamuzi huo? Je, Kamishna anaweza kupindua uamuzi wa Mtendaji Mkuu wa Kampuni au bodi?**

*22 Septemba 2014*

Kamishna wa Bima ana jukumu la kusimamia sekta ya bima nchini, pamoja na kazi nyingine kama ilivyoelezwa chini ya Sheria ya Bima, Namba 10 ya 2009. Yeye si meneja wa kampuni ya bima wala si mkurugenzi na hawezi kupindua maamuzi yoyote yanayohusu madai yasiyolipika ya kampuni ya bima, Mtendaji Mkuu wake au bodi.

Hii ni mara yetu ya kwanza tunasikia malalamiko kama hayo dhidi ya Kamishna lakini ikiwa unashurutishwa/unalazimishwa kulipa, unaweza kukata rufaa ya uamuzi huo kwa Baraza la Bima chini ya kifungu cha 126(4) ambacho kinasema kwamba "mtu ambaye hajaridhika na uamuzi wa Kamishna chini ya Sheria hii anaweza, kwa muda wa mwezi mmoja kuanzia tarehe ambayo amepewa uamuzi huo kwa maandishi, kukata rufaa kwa njia ya maombi ya maandishi kwa Baraza ambalo linaweza, kuidhinisha, kubadilisha, kupindua au kutofautiana na uamuzi huo. Hatua hii lazima ifanyike ndani ya miezi miwili tangu siku ya kuwasilisha ombi hilo."

Ikiwa bado hujaridhishwa na maamuzi ya Baraza kwenye hoja za kisheria, unaweza kukata rufaa Mahakama Kuu ndani ya mwezi mmoja tangu uamuzi huo ulipowasilishwa kwako.

Ikiwa unachosema ni kweli, ambacho tunadhani kinashangaza, tunaamini una nafasi nzuri ya kufanikiwa. Tafadhali kumbuka kuwa uamuzi wa Kamishna unaokusudia kuukatia rufaa ni lazima uwe kwenye

maandishi. Haitawezekana kwenda kwenye Baraza kwa misingi tu ya shinikizo lolote, mfano, la maongezi ya simu na Kamishna.

# Haki za Walaji

"

Kuna namna nyingi ambazo haki za walaji zinaweza kukiukwa na wafanyabiashara ambao kimsingi wanapaswa kuzijua vyema. Vivyo hivyo, wakati mwingine walaji nao, kwa kubahatisha, hushtaki pasipokuwa na madai yoyote ya msingi. Katika sura hii, tumeweka mifano mingi ya tabia zote hizi mbili. Watu hudai haki katika hali zote mbili, lakini siyo wakati wote haki na madai huwa ni kitu kimoja.

## Kushtaki ng'ambo

**Baada ya kufika nje ya nchi tulichukua basi kutoka uwanja wa ndege kuelekea stendi. Tukiwa kwenye gari nilishikilia mmoja wa mshikio kwenye gari ambao ulikatika baada ya dereva kukanyaga breki ghafla. Nilidondokea upande wa nyuma na kupiga kichwa changu chini na kunisababishia maumivu makali mgongoni pamoja na kupata majeraha kichwani. Niliwasiliana na wakala wangu wa safari ambaye alinitaarifu kuwa siwezi kumshtaki yeyote kwa sababu nilikuwa ugenini na sikuwa na mkataba wakati tukio linatokea. Nifanye nini?**

*20 Februari 2012*

Wakala wako wa safari siyo mshauri wa masuala ya kisheria na anatakiwa kutoa ushauri kuhusu masuala ya safari pekee. Tunasema hivyo kwa sababu alikupotosha sana. Kuwa nchi ya kigeni hakuna maana kwamba huwezi kumshtaki mtu. Kutokuwa na mkataba siyo sababu ya kutokushtaki. Ulisafiri kwa ndege. Na kama ni hivyo unatakiwa kurejea masharti ya usafiri. Je, yanahusu stendi hadi stendi nyingine au kutoka unapoingia ndani ya ndege hadi unaposhuka. Kama ni stendi hadi stendi, una mkataba na kampuni ya ndege ambayo unaweza kuishtaki kwa majeraha kwa sababu wamevunja mkataba wa kukusafirisha kwa usalama.

Kama mkataba wako ni tangu unapoingia kwenye ndege na unaishia unaposhuka ndani ya ndege, bado unaweza kushtaki kwenye sheria ya madhara (tort). Chini ya sheria ya madhara huhitaji kuwa na mkataba na swali rahisi ni kama mtu aliyekusababishia majeraha alikuwa na wajibu wa kuwa mwangalifu kwako na iwapo kuna uvunjifu wa wajibu huo na hivyo kusababisha wewe kupata majeraha au madhara.

Kwa kesi yako, tunajibu yote haya kuwa ni ndiyo na tunaamini una kesi nzuri. Wakili wako atakuongoza juu ya nani wa kumshtaki, inaweza kuwa ni mmiliki wa basi, uwanja wa ndege/mamlaka ya uwanja wa ndege, shirika la ndege au hata dreva wa gari.

## Nywele kukatwa fupi mno

**Nilikwenda kwa kinyozi na kumuomba anipunguze kidogo nywele pamoja na masharubu yangu. Alikata nywele zangu zikabaki fupi mno na aliishia kukata nusu ya masharubu yangu. Sikuwa na namna nyingine zaidi ya kumwambia akate na nusu iliyobakia. Nilipotishia kumchukulia hatua za kisheria alinijibu kuwa sina mkataba naye. Nilitoa taarifa polisi lakini cha kushangaza nao walikataa hata kuchukua maelezo yangu. Ninaoa hivi karibuni na sina hakika kama niendelee na sherehe au la. Nifanyeje?**

*26 Machi 2012*

Ingawa tunakuonea huruma, hatuelewi ni kwa nini huna uhakika wa kuoa baada ya haya yaliyokusibu kwa kinyozi; kwa sababu nywele pamoja na sharubu zako zitaota tena. Pia hatuelewi uhusiano kati ya ndoa yako na mkato wa nywele na hatuwezi kutoa maoni iwapo uendelee au usiendelee kufunga ndoa yako.

Kuhusu kutoa malalamiko polisi, maoni yetu ni kwamba hii siyo kesi ya jinai. Kama polisi wakianza kusikiliza kesi kama hizi watakuwa na utitiri wa malalamiko. Vitendo vya polisi vilikuwa ni halali.

Sasa tuje kwenye suala la msingi la kukatwa masharubu na nywele. Tunaamini kwamba ulipokaa kwenye kiti cha kinyozi, ulikuwa unaingia mkataba na kinyozi ya kwamba yeye akukate nywele na wewe utalipia. Hilo linaanzisha mahusiano ya kimkataba na tunaamini unaweza kushtaki chini ya sheria za mikataba. Ingawa inaweza isiwe rahisi kwa sababu utatakiwa kuthibitisha kwamba kulikuwa na mkataba na ulipata hasara.

Hatuna kesi yoyote ya ndani kuhusu suala kama hili na hatuna hakika kwa kiasi gani Mahakama za Tanzania zinaweza kusikiliza suala kama hili. Mwanasheria wako anaweza kukuongoza zaidi.

## Kung'atwa na buibui ndani ya ndege

**Nilisafiri kwenda nje ya Tanzania kwa kutumia ndege maarufu sana. Wakati nikitumia choo katikati ya anga nilihisi maumivu makali sana miguuni ambapo mwanzoni nilihisi ni mishipa inavuta. Mguu wangu ulikuwa mzito na baada ya kutua uwanja wa ndege nilikwenda moja kwa moja kwenye kituo cha afya cha uwanjani hapo, ambapo niliarifiwa kwamba nilig'atwa na buibui asiye wa kawaida. Nimegundua kwamba kwa sasa moja ya changamoto kubwa ya vyoo vya kwenye ndege ni buibui na wengine ni hatari sana. Ingawa nilitibiwa kwenye kituo cha afya cha uwanjani hapo, nilipata maumivu makali na nililazwa hospitali kwa siku tatu. Shirika la ndege lililipia matibabu yangu lakini limekataa kunifidia zaidi. Je, ninaweza kushtaki?**

*26 Machi 2012*

Ulinunua tiketi na hivyo uliingia mkataba na shirika la ndege kuhakikisha kwamba unasafiri salama. Uwepo wa buibui ndani ya ndege ni uvunjifu mkubwa wa usalama wako pamoja na abiria wengine na kama ukiweza kuthibitisha kwamba ni kweli kulikuwa na buibui ndani ya ndege na hukuwaleta wewe kupitia viatu vyako au hukupata popote isipokuwa kwenye ndege, una kesi nzuri. Kanuni ya msingi katika sheria ni kwamba mlalamikaji ndiye mwenye wajibu wa kuthibitisha. Unahitaji kwanza kufanyia kazi ushahidi kabla kushtaki. Wanasheria wako wanaweza kukushauri zaidi.

## Wizi kwenye simu yangu

**Nilipata ujumbe kutoka kwenye simu ukinitaarifu kwamba nimeshinda bahati nasibu ya Shilingi milioni 50 na hivyo nitume ujumbe kwenye namba fulani. Nilifurahi sana na kufanya kama nilivyoelekezwa. Nikapata tena ujumbe mwingine ambao uliniambia niweke pesa kwenye simu yangu kiasi cha Shilingi 100,000 ikiwa ni mchango wangu wa tuzo na nikatuma tena ujumbe mwingine kwa namba hiyo hiyo. Ikaja kugundulika kwamba zile jumbe mbili nilizotuma zilikuwa ni kwa ajili ya kuhamisha pesa na nimepoteza pesa nyingi. Namba niliyoitumia pesa kwa sasa imefungwa kabisa. Nifanye nini? Je, kampuni ya simu inaweza kunirudishia pesa kwa sababu mtandao wao ndiyo uliosababisha tukio hili?**

*9 Aprili 2012*

Kuna msemo unaosema hakuna mlo wa bure. Ni lazima ukamatwe mahali na wewe inaonekana umekamatwa kwenye hili. Huu ni utapeli ambao umeenea sana hapa kwetu. Kwa ufupi, pesa zako zimeibwa na mtaalam ambaye ametumia mtandao wa kampuni yako ya simu kukuibia.

Wizi ni kosa la jinai na tunashauri utoe taarifa polisi. Polisi hawawezi kukurudishia pesa zako lakini angalau unakuwa na jalada polisi ambalo unaweza kulirejea wakati wowote.

Kuhusu kurudishiwa pesa zako, hakuna kampuni ya simu inayoweza kufanya hivyo, kwa sababu kufanya hivyo, kutaibua mlolongo wa matatizo. Pia kampuni inaweza kujenga hoja kwamba ulikuwa mzembe kwenye kuweka hela na kuzituma kwa mara ya pili ukitegemea kupata milioni 50. Unawezaje kushinda bahati nasibu bila kununua tiketi? Inahitaji akili ya kawaida tu kwamba kushinda bahati nasibu unahitaji kuchangia. Haya ni maswali ambayo utaulizwa kama utaamua kuichukulia hatua kampuni yako ya simu. Tunapendekeza ujielekeze kwanza kwenye

mambo hayo na mwanasheria wako kabla hamjaifungulia kesi kampuni ya simu.

## Udanganyifu shuleni

**Mimi ni mtendaji mkuu kwenye moja ya kampuni zenye mafanikio makubwa jijini Dar es Salaam. Ninasoma masomo ya jioni chuoni ambapo huwa ninakwenda na msaidizi wangu ili kunisaidia kuandika notsi wakati wa vipindi. Wanafunzi wenzangu waliniripoti kwa walimu na msaidizi wangu sasa amezuiliwa kuingia darasani nami. Je, hii ni haki? Nifanye nini?**

*23 Aprili 2012*

Swali lako ni "ufanye nini" Jibu ni "amka na uhalisia". Tunachukulia kwamba wewe ndio mwanafunzi na siyo msaidizi wako. Kwa nini uende na msaidizi wako darasani kukuandikia notsi wakati unaweza kuandika mwenyewe? Kitu kitakachofuata ni wewe kuomba ruhusa msaidizi wako akufanyie majaribio au mtihani.

Pia, msaidizi wako anakoma kuwa msaidizi baada ya saa za kazi. Tunadhani, kuhudhuria darasani siyo moja ya majukumu yake ya kazi na haipo kwenye maombi yake ya kazi. Anaweza hata kukushtaki kwenye Mahakama za Kazi kwa kwenda naye darasani. Ushauri wetu, nenda darasani mwenyewe na utumie ubongo wako. Kwa mwangaza tu, kama msaidizi wako ana akili kama wewe, unaweza kujikuta siku moja umekuwa msaidizi wake.

## Adhabu ya riba ni kubwa

**Nimecheleweshа kulipa mkopo na benki inanilipisha riba ya kijinga kwa sababu ya kucheleweshа. Nimejitahidi sana kutoa ushirikiano lakini biashara yangu haiendi vizuri sana. Je, kuna kiwango cha juu cha riba ambacho ninaweza kutozwa? Nifanye nini?**

*21 Mei 2012*

Nchini Tanzania, viwango vya riba vinaendeshwa na soko. Nchi nyingine, wana sheria za kuzuia mazoea ya kuwatoza watu riba kubwa kwa kuweka ukomo wa kiwango cha juu cha riba ambacho kinaweza kutozwa. Sheria hizi zimetungwa kuwalinda walaji. Kwa bahati mbaya, hakuna sheria za namna hiyo nchini Tanzania. Njia bora ya kukabiliana na hili ni kujadiliana na benki yako ili kurekebisha masharti ya mkopo. Utatakiwa kulipa malipo ya awali ya asilimia 10, njia hii angalau itakupa unafuu wa adhabu ya riba.

## Pesa kutolewa kwenye akaunti, benki imekataa kunirudishia

**Nilitoa benki kiasi cha Shilingi milioni 20 mnamo tarehe 31 Oktoba mwaka uliopita. Siku iliyofuata tu, yaani tarehe 1 Novemba, kiasi kingine cha Shilingi milioni 20 kilichukuliwa kwenye akaunti yangu kwa njia ya udanganyifu. Mwanzoni nilipojaribu kuchunguza sikushitukia, lakini sasa ukaguzi wa mwaka umefanyika na udanganyifu ule umegundulika. Benki inasema nimechukua muda mrefu sana kuwataarifu na hivyo siwezi kurudishiwa. Nifanye nini?**

*28 Mei 2012*

Huu ni udanganyifu wa kufurahisha ambapo kiasi cha kwanza kinachukuliwa mwisho wa mwezi na kiasi kingine kinachukuliwa mwanzo wa mwezi unaofuata. Benki ina jukumu la kimkataba la kulinda pesa zako na ingawa ni kweli umechelewa sana kuwataarifu, kuchelewa peke yake hakuwaondolei benki wajibu. Benki inaweza kusema kwamba udanganyifu ungeweza kudhibitiwa kama ungewataarifu mapema, lakini hili halina mashiko sana, labda tu ingeweza kupunguza kiasi ambacho wangetakiwa kukulipa. Kama unachotuambia ni kweli, una kesi nzuri dhidi ya benki na wakili wako anaweza kukuongoza zaidi.

## Kumshtaki dereva wa daladala

**Je, ninaweza kumshtaki dereva wa daladala ambaye alisababisha ajali kwenye daraja la Salenda, kwani kwa uzembe huo maelfu ya watu walikwama kwenye foleni na kuchelewa kufika kazini, na hivyo kuigharimu nchi mabilioni ya fedha kwa muda watu waliopoteza? Kama ningekuwa Rais wa Tanzania ningeruhusu madai hayo dhidi ya dereva wa daladala na mmliki wake. Je, sheria yetu inaruhusu hilo?**

*11 Juni 2012*

Chini ya kanuni ya uzembe na sheria ya madhara, kuna maswali machache unaweza kujiuliza. Je, dereva wa daladala ana wajibu wa kukujali? Kama anao, swali linalofuata ni je, alivunja wajibu huo? Kama dereva alivunja wajibu huo, na imekusababishia hasara, unaweza kufanikiwa ukimshtaki.

Wakati dereva wa daladala anaposababisha ajali, hafanyi hivyo kwa makusudi. Ni ajali kama ajali nyingine. Ana wajibu kwa mtu aliyemgonga, lakini je, wajibu huo unakuja hadi kwako ambaye hukupata madhara ya kimwili? Jibu ni hapana.

Kwa ujumla kwenye sheria ya madhara, anaweza tu kuwa na wajibu kwako kama na wewe ulijeruhiwa. Unaweza kusema kwamba amekuumiza kiuchumi lakini hasara hiyo ya kiuchumi ni ya mbali sana na inaweza ikaleta mshangao na kufungulia mafuriko ya madai. Kama majaji watakubali kesi za namna hiyo, madereva masikini wa daladala watatakiwa kuwafidia mabilioni ya Shilingi wale wote walioathirika; sera ya umma pamoja na kanuni za haki zitakiukwa kama mambo yangekuwa hivyo.

Kwa ufupi na kwa bahati mbaya sana, huwezi kumdai dereva wa daladala. Pia hatujui nchi ambayo inaweza kukubali wazo hilo. Utakapokuwa Rais, unaweza kufikiria kutunga sheria maalum juu ya hili; hata hivyo sheria ya sasa haiungi mkono mawazo yako.

## Utapeli kuhusu tiba ya VVU/UKIMWI

**Mimi ni mwanamke mwenye miaka 36 na ninaishi na VVU/UKIMWI tangu miaka minne iliyopita. Mwaka jana nilikutana na rafiki yangu anayeishi Shinyanga na akaniambia kuhusu mtu anayeponya ugonjwa huu. Akaniambia mtu huyo ni maarufu sana na anafahamika kuhusu tiba zake za asili na kwamba anahitaji kuniona ili kuandaa mpango wa matibabu. Nilifurahi sana kusikia hivyo na niliandaa safari ya kuelekea Shinyanga. Mganga akasema ugonjwa wangu utapona ndani ya miezi miwili, na niache dawa zote za hospitali nilizokuwa nazitumia. Hivyo nikaacha kutumia dawa zote ikiwemo zile za kufubaza makali ya VVU (ARV). Sasa ni mwaka mmoja umepita na ugonjwa haujaondoka na hali yangu imezorota zaidi kuliko ilivyokuwa mwanzo. Hivi sasa nimesikia mganga yule wa kienyeji ni tapeli na alikuwa tu anataka pesa zetu. Hakuna taarifa juu ya mtu aliyewahi kuponywa naye na wagonjwa wengi aliowahi kuwatibu wamefariki. Nimeanza tena kuhudhuria kliniki na daktari wangu ananiambia kwamba kiwango cha kinga zangu za mwili (CD4) kimeshuka sana kutokana na kuacha kutumia dawa za kufubaza makali ya virusi vya ukimwi (ARV). Ni hatua gani za kisheria ninaweza kuchukua dhidi ya mtu huyu?**

*25 Juni 2012*

Chini ya sheria zetu, kitendo kilichofanywa na mganga wa kienyeji ni kosa la jinai. Kifungu cha 27 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na VVU/UKIMWI (2008) kinaeleza kwamba kama mtu yeyote anataka kutoa maelezo au taarifa kuhusu tiba ya VVU/UKIMWI ni lazima kwanza ifanyiwe uthibitisho wa kisayansi kabla ya tangazo kutolewa. Sheria inatamka kwamba kuchapisha taarifa kuhusu tiba ya VVU/UKIMWI ni lazima iambatane na ushahidi

wa kabla na baada ya tiba ya VVU na matokeo ya vipimo.

Sheria inatamka kwamba mtu yeyote anayetoa au anayesababisha kutolewa kwa maelezo au taarifa kuhusu tiba, kinga au kudhibitiwa kwa VVU/UKIMWI kinyume na kifungu hiki anatenda kosa na akitiwa hatiani atalipa faini isiyopungua milioni moja au kifungo kisichozidi miezi sita au vyote kwa pamoja.

Tunakushauri umripoti mganga huyo polisi. Zaidi, kwenye sheria za mikataba na sheria ya madhara, unaweza kumshtaki na kudai fidia. Wanasheria wako wanaweza kukuongoza zaidi.

## Nimetumia dawa lakini bado ni mnene

**Duka la dawa lilitangaza kwamba kama nitakunywa kikombe cha dawa ya poda iliyochanganywa na maji moto kila siku nitapungua uzito. Uzito wangu kabla sijanunua dawa hiyo ghali ulikuwa ni kilo 128. Nimetumia Shilingi milioni moja kwenye hiyo bidhaa lakini uzito wangu bado haujapungua. Kila ninapokutana na muuza dawa ananiambia kwamba kuna mabadiliko fulani anayaona lakini vipimo vya uzito/mzani vinakataa. Kuna kanuni zozote zinazozuia tabia hii ya wauza dawa?**

*23 Julai 2012*

Tunasikitika kusikia unapata shida ya kupungua uzito. Changamoto hii inawakumba watu wengi kipindi hiki na hata kipindi cha nyuma. Pamoja na dawa ambayo haifanyi kazi ni muhimu kuongeza kiwango cha mazoezi na upunguze ulaji wa chakula. Kutegemea poda ya miujiza pekee kunaweza kusikusaidie. Vyovyote vile daktari wako anaweza kukuongoza.

Turudi kwenye swali lako. Chini ya Sheria ya Famasia ya 2009, mtu haruhusiwi kutangaza biashara ya dawa, vifaa-tiba au dawa za tiba asilia kwa namna ambayo ni ya uongo, kupotosha, au katika namna ambayo itajenga picha isiyo halisi kuhusu tabia, thamani, uwingi, muundo, faida, usalama au ubora, kadri iwavyo. Mtu anayekwenda kinyume na sheria hii atatozwa faini isiyopungua Shilingi milioni mbili na isiyozidi Shilingi milioni kumi au kifungo cha miezi sita lakini kisichozidi miaka mitatu au vyote kwa pamoja. Kama ni kampuni itawajibika kulipa faini isiyopungua Shilingi milioni tano lakini isiyozidi Shilingi milioni kumi na tano.

Kama unaamini kwamba umepotoshwa, chini ya Sheria hii unaweza kwenda kuliripoti duka la dawa husika kwenye Baraza la Wafamasia.

## Majeraha nikiwa ukumbi wa mazoezi/ jimu

**Baada ya kujiunga na jimu moja jijini Dar, nilidhani ingenisaidia kupunguza uzito na kurudisha muonekano wangu. Wiki mbili tu baada ya mafunzo nilitoa taarifa kwa mkuu wa mafunzo kwamba moja ya mashine ninazotumia ilikuwa na hitilafu. Nilimuonesha mkufunzi wangu tatizo na aliniambia kwamba atalirekebisha. Niliendelea na mazoezi na wiki ya tatu waya uliokuwa unashikilia mashine ulikatika na kuniumiza kwenye uti wa mgongo. Maumivu yalikuwa ni makali sana kiasi kwamba nilipelekwa hospitali na gari ya wagonjwa. Hospitali ya Dar ilinirejea hospitali ya Nairobi ambako nilifanyiwa upasuaji. Bado natembelea magongo na nina msongo mkubwa wa mawazo. Niliporudi Dar, kwa ukarimu nilikwenda jimu kuangalia walichokifanya baada ya tukio. Kwa masikitiko makubwa, hata kabla sijafungua kinywa na kusalimia, mmiliki wa jimu ile aliniambia kama nimekwenda pale kuwatisha, basi watakwenda Mahakamani kujitetea na kwamba mimi nilikuwa mzembe kwenye kutumia mashine na kwamba nilitia saini kanusho/kifungu kinachoiondolea jimu wajibu kwa majeraha**

**yoyote ya watumiaji. Je, hii ina maana kwamba hawagusiki? Nifanye nini? Nataka niwape funzo.**

*17 Septemba 2012*

Kama wamiliki wa jimu ni jeuri hivyo na kama uliumia kiasi hicho, hatua pekee unayoweza kuchukua ni kuwashtaki. Huhitaji kufikiria kuhusu hili kwa muda mrefu. Ni wakati mwafaka wa suala hilo kupelekwa Mahakamani na wanaohusika wawajibishwe. Kutia saini kanusho hakuna maana kwamba huwezi kuishtaki jimu. Kanusho ni njia ambayo wamiliki wanajaribu kujipunguzia wajibu. Wala isikutishe. Jimu ina wajibu wa kimkataba wa kutoa mafunzo kwa kutumia vifaa salama, kitu ambacho wameshindwa kukifanya.

Ripoti ya madaktari wako wa Dar na Nairobi zitakuwa na msaada mkubwa sana, ikiwepo uwezekano wa kumleta daktari kama shahidi-mtaalam (expert witness) wakati wa kusikilizwa kesi ili kuthibitisha kiwango cha majeraha na kilichoyasababisha. Unaweza pia kuwa mbunifu kwa kile unachokidai. Unaweza kudai kila kitu ilimradi tu uweze kuthibitisha. Unaweza kudai gharama za matibabu, kipato kilichopotea, kipato kijacho kitakachopotea, gharama za safari, mvurugo wa hisia, n.k., kama unaweza kuthibitisha uhalali wake. Tunakushauri umtafute mwanasheria wa kukusaidia.

## Benki kutaifisha hati

**Nilikopa pesa benki ili kununua gari. Nimeshindwa kurejesha mikupuo 7 ya mwisho na benki wanataka kushikilia gari langu. Nilipojua hilo nilimuomba rafiki yangu anayetumia benki hiyo hiyo kuazima pesa kwa kutumia mojawapo ya hati zangu. Wakati rafiki yangu alipoomba mkopo, benki waliona jina langu kwenye hati, hivyo walikataa kumkopesha na walikataa pia kurejesha hati wakisema sasa watauza nyumba na mali yenye hati. Je, benki wana haki ya kufanya hivyo?**

*24 Septemba 2012*

Hatuwezi kujibu swali lako bila kuona nyaraka za mkopo wa gari. Hata hivyo, kwa uzoefu wetu kwenye masuala kama hayo, hatuoni uwezekano kwamba ulitoa hati kama dhamana ya mkataba wa mkopo wa gari. Na kama hivyo ndivyo, benki haiwezi kushikilia hati, achilia mbali kuuza mali hiyo. Mwanasheria wako awaandikie barua na kama hawatoi ushirikiano, unaweza kuendelea kuishtaki benki. Kushikilia hati yako kunaweza kutafsiriwa kama ni kunyimwa haki yako ya kumiliki mali na unaweza kushtaki kudai fidia mbali mbali.

## Mafuta machafu, injini imepasuka

**Nilinunua mafuta kwenye pampu ya petroli Mikocheni ambayo yalipelekea injini ya gari langu kupasuka. Fundi wangu alithibitisha kwamba tatizo hilo limetokana na petroli kuchanganywa na mafuta ya taa. Sasa nimegundua kwamba kituo hicho cha mafuta kinafahamika kwa shughuli hiyo. Nifanye nini?**

*24 Septemba 2012*

Tunakushauri utoe taarifa juu ya suala hili kwenye Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji (EWURA) ambayo imeanzishwa na Sheria ya Udhibiti wa Nishati na Maji na inaJulaikana kwa ufanisi wake. Kama malalamiko yakiwasilishwa kwa Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji, na Mamlaka ikajiridhisha kwamba una maslahi na suala linalolalamikiwa na kwamba lalamiko lako lina mashiko, EWURA itafanya uchunguzi juu ya lalamiko hilo.

Baada ya kufuata taratibu zilizowekwa kwenye sheria, Mamlaka ya Udhibiti wa

Nishati na Maji inaweza ikatoa amri zifuatazo (a) kumtaka mtu alipe pesa; (b) kumtaka mtu kusambaza bidhaa au huduma ndani ya kipindi fulani; (c) kumtaka mtu asambaze bidhaa au huduma kwa vigezo na masharti yaliyowekwa; kumtaka mtu alipe gharama kwa mtu mwingine au kwa mtu aliyehudhuria wakati wa kusikiliza shauri au kutoa nyaraka; (e) kufuta shauri. Wanasheria wako wanaweza kukuongoza zaidi.

## Kinanda ni kibovu, pesa haijarejeshwa

**Mimi ni mtaalam wa kupiga kinanda na ni mwalimu. Nilinunua kinanda kwenye moja ya maduka ya kielektroniki, bila kujua kwamba vitufe vyote vimechanganywa. Vitufe viwili tu vinafanya kazi vizuri na vingine viko tofauti kabisa. Niliporudi dukani muuzaji alinionesha ilani kwamba bidhaa ikiuzwa hairudishwi. Nimejaribu kumueleza mmiliki wa duka lakini hatoi ushirikiano. Ninawezaje kushughulikia hili?**

*8 Oktoba 2012*

Ilani tu kwamba bidhaa hairudishwi siyo kizuizi cha wewe kurudisha bidhaa ambayo haina ubora unaostahili. Ilani inakusudiwa tu kupunguza dai kwa mwenye duka lakini ilani hizo haziwezi kumuondolea wajibu au kufidia uvunjifu wa mkataba. Uliponunua kinanda, uliingia mkataba wa mdomo ambapo ulilipia kinanda na akakupatia. Moja ya sababu za kununua kinanda ni kukitumia na siyo kukiweka tu kama pambo/maonesho. Vitufe vinapoharibika huwezi kukitumia. Kinanda chenye tatizo hilo la vitufe hakina kazi kwako na mwenye duka wako amevunja mkataba.

Kama mwenye duka haelewi mantiki hiyo unaweza kumpelekea barua kupitia mwanasheria wako, na kama hilo halifanyi kazi, una haki zote za kumshtaki muuza duka Mahakamani. Ushauri wetu unajikita kwenye ukweli kwamba siyo wewe uliyeharibu vitufe hivyo. Hicho ndicho mwenye duka anaweza kukisema na ujiandae kupeleka ushahidi wa kupinga madai kama hayo. Suala la vifaa vya kielektroniki kutokufanya kazi vizuri ni la kawaida kwenye soko la Tanzania na kwingineko.

## Kampuni ya simu kushindwa kutoa huduma

**Ninatumia huduma za mtandao wa simu ambapo huduma zake hazina maana. Mara nyingi unampigia mtu simu unaambiwa haipatikani wakati simu iko hewani. Pia ninapata jumbe ambazo sijaziomba zinazonikaribisha kununua miito ya simu, miongoni mwa mambo mengine. Ninawezaje kulizuia hili?**

*22 Oktoba 2012*

Mamlaka inayowajibika na masuala ya makampuni ya simu Tanzania ni Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA). Hivyo, kama una malalamiko, unaweza kuwasilisha kwenye Mamlaka ya Mawasiliano na pia unaweza kukata rufaa kwenda Tume ya Ushindani kama bado hujaridhika na huduma. Mfumo huu wa malalamiko umetolewa na sheria. Njia rahisi zaidi kwako ni kufikiria kubadilisha mtoa huduma.

## Zebaki kwenye vipodozi

**Kuna bidhaa fulani za urembo ambazo zina zebaki ndani yake na zinaingizwa Tanzania. Wakati nchi nyingine zimeshapiga marufuku bidhaa za aina hiyo, ambazo zinatumiwa na wanawake kupambana na uzee na kung'arisha ngozi, baadhi ya maduka makubwa Tanzania yanaziuza. Hili linawezaje kuzuiliwa? Nani anawajibika kwa tabia hizi mbaya? Hakuna sheria inayosimamia?**

*12 Novemba 2012*

Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA) ni chombo cha usimamizi, ndani ya Wizara ya

Afya na Ustawi wa Jamii, chenye dhamana ya kusimamia ubora na usalama wa chakula, dawa, vipodozi na huduma za kitabibu. Unaweza kulitolea taarifa jambo hilo TFDA ili ichukue hatua za haraka. Ukitembelea tovuti yao pia utaona idadi ya bidhaa zote za urembo ambazo imezisajili.

Kuingiza bidhaa za zebaki pia ni haramu chini ya Sheria ya Usimamizi wa Umoja wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EACCMA). Nyongeza ya Pili ya Sheria hii imetamka wazi kwamba, sabuni zote pamoja na bidhaa za vipodozi zenye zebaki zimezuiliwa kuingizwa kwenye nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Umoja wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki mtu yeyote anayeingiza bidhaa za aina hiyo akitiwa hatiani atawajibika kwa kifungo kisichozidi miaka mitano au faini ambayo ni sawa na asilimia 50 ya ushuru wa bidhaa husika au vyote kwa pamoja. Hivyo waingizaji wa bidhaa hizi wanaweza kufungwa jela.

Na kwa maslahi ya jumla, Sheria ya Usimamizi wa Umoja wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ni sheria inayotumika kwenye nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na kwamba inatumika kwenye muundo wa jumla wa forodha kwa bidhaa zinazoingizwa. Hivyo kama nchi moja mwanachama akiagiza bidhaa fulani, kodi inayolipwa ni hiyo hiyo ktika nchi zote tano za Afrika Mashariki.

## Majeraha makubwa kwenye bwawa la kuogelea

**Sherehe ya mahafali iliandaliwa na baadhi ya wanafunzi kwenye makazi fulani binafsi. Kila mtu alifurahia kuogelea bila kujua kwamba moja ya bomba linalosambaza maji bwawani mfuniko wake umepotea na kusababisha majeraha makubwa kwa mwanafunzi mmojawapo. Je, ninaweza kumshtaki mmiliki wa bwawa, wakati tulitumia bwawa bure?**

*10 Desemba 2012*

Kutokana na swali lako inaonesha wazi kwamba wewe siyo mwanafunzi uliyeumia na hivyo hakuna uwezekano kwamba utafanikiwa iwapo utamshtaki mmiliki wa bwawa. Hata hivyo, rafiki yako aliyejeruhiwa ana kesi nzuri dhidi ya mmiliki wa bwawa, bila kujali kama bwawa hilo mliogelea bure au la.

Ingawa mmiliki wa bwawa hakuwa na mkataba wowote na nyinyi wa kuwapa bwawa, bado ana wajibu wa kisheria kuhakikisha kamba bwawa hilo ni salama kwa matumizi. Ni wazi kuwa kupotea kwa mfuniko wa kufungia maji, kunaweza kumsababishia mwogeleaji kupoteza maisha kwa kubanwa kwenye bwawa.

Swali la kwanza kujiuliza ni iwapo mmiliki wa bwawa alikuwa na wajibu wa kuwajali hata kama aliwapa bure. Tunaamini alikuwa nao. Swali la pili ni iwapo mmiliki wa bwawa amevunja wajibu huo. Jibu ni ndiyo. Na swali la mwisho la kujiuliza ni kama kutokana na mmiliki wa bwawa kuvunja wajibu wake, kuliwasababishia nyinyi hasara au maumivu. Kutegemea na ushahidi mtakaotoa, uwezekano wa kufanikiwa ni mkubwa sana.

## Dawa bandia ya malaria

**Mwanangu wa miaka 2 alitibiwa ugonjwa wa malaria na alipewa dawa zilizotengenezwa na mzalishaji wa ndani. Dawa hazikuwa na nguvu na baadaye zilimletea matatizo zaidi, ambayo yalipelekea akatibiwe nje ya nchi. Bahati nzuri mwanangu alipona. Je, ninaweza kumshtaki mzalishaji?**

*24 Desemba 2012*

Ni kweli, unaweza kumshtaki mzalishaji. Kitu muhimu kwenye kesi yako ni kuthibitisha ulichokidai hapo juu. Unatakiwa pia kufikiria kutoa taarifa juu ya jambo hili kwa Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania (TFDA) ambayo nayo inaweza kuchukua hatua sambamba na hatua yako ya kumshtaki mzalishaji. Mwanasheria wako anaweza kukuongoza zaidi.

## Kushindwa kwa vizuia mimba

**Kifaa cha shaba kiliingizwa ndani yangu ili kuepuka kupata mimba kwani tayari nina watoto watano. Kwa bahati mbaya ni mjamzito tena na nina uhakika kuwa ni kwa sababu kifaa hakikuingizwa vizuri. Je, ninaweza kumshtaki mtengeneza kifaa? Je, ninaweza kutoa mimba kwa sababu siwezi kutunza watoto wote?**

*21 Januari 2013*

Kwa ujumla, mtengenezaji anaweza tu kuwajibika kama unaweza kuthibitisha kwamba kifaa chenyewe kilikuwa na kasoro fulani. Kutokana na ukweli hapo juu, inaonekana kwamba shida ilikuwa kwenye uingizaji ambao umesababisha mimba hii isiyotarajiwa. Kesi nzuri ipo chini ya sheria ya madhara na unaweza kumshtaki daktari na pengine hospitali, ambayo inaweza kuwajibika chini ya dhima ya mwajiri. Hata hivyo, ni lazima ukumbuke kwamba aina hii ya uzazi wa mpango haina ufanisi kwa 100% na kumekuwa na matukio mengi ulimwenguni kote ambapo wanawake wamepata mimba wakiwa na kifaa hiki cha shaba. Daktari wako alitakiwa akuelezee waziwazi na kama hakufanya hivyo, hiyo ni sababu nzuri ya kumshtaki. Kwa kawaida kiwango cha fidia kwenye kesi kama hizi siyo kikubwa sana. Pia huwezi kumshtaki daktari na kutoa maombi ya kutoa mimba kwa kuwa utoaji mimba ni kinyume cha sheria. Utoaji Mimba nchini Tanzania unaruhusiwa tu ikiwa inathibitishwa na daktari kuwa ni muhimu ili kulinda afya ya mama. Sababu yako ya kutoa mimba kwamba tayari una watoto wa 5 haina nguvu yoyote Mahakamani. Kabla ya kuchukua hatua yoyote, tafadhali wasiliana na mwanasheria wako.

## Maji ya kuoga ya moto sana

**Nilikuja Dar na kukaa kwenye hoteli ya nyota ya juu (kifahari). Wakati wa kuoga maji ya moto yaliniunguza vibaya sana kwani bomba lilitoa maji yaliyokuwa ya moto sana. Nilizungumza na bosi wa hoteli kuwa kama sehemu ya fidia aniruhusu kukaa bure kwa wiki moja lakini alikataa. Nimemripoti kwenye Bodi ya Utalii ya Tanzania lakini hawajachukua hatua yoyote. Nifanye nini?**

*28 Januari 2013*

Kwenye mabomba ya maji ya kuoga ambayo tunayajua kuna koki mbili - moja ya maji baridi na nyingine ya maji ya moto. Tuna uhakika kwamba hoteli “ya kifahari” uliyokaa ingekuwa na kitu sawa na hicho. Kwa hiyo, hatuna hakika namna ulivyojiunguza wakati unaoga. Labda mmiliki nae anajiuliza swali kama hili. Ingawa tunasikitika kwa hilo, hakuna namna ambayo unaweza kupata fidia yoyote kama yalikuwa ni makosa yako. Kama bomba la maji ya kuoga lilijibadilisha ghafla kutoka kwenye joto hadi moto sana, basi huenda isiwe ni kosa lako na unaweza kuwa na kesi dhidi ya hoteli. Ni kweli unaweza kushtaki lakini tunashauri uwasiliane na mwanasheria wako kabla ya kuchukua hatua yoyote.

## Umeme kukatika chumba cha upasuaji

**Mmoja wa ndugu zangu alikuwa akifanyiwa upasuaji na mara umeme ulikatika. Jenereta za hospitali zilikua hazifanyi kazi na kwa bahati tu ndugu yetu alinusurika. Ilibidi apelekwe nje ya nchi kwa ajili ya matibabu**

**zaidi na alikuwa hospitali kwa wiki 6. Je, tunaweza kuiwajibisha hospitali hiyo?**

*28 Januari 2013*

Inafahamika wazi kwamba kuna tatizo la kukatika umeme mara kwa mara hapa Dar na kwa hospitali ambayo ina chumba cha upasuaji ambacho hakina jenereta ya dharura au kuwa na jenereta ambayo haifanyi kazi ni hatari sana na pia ni uzembe mkubwa sana wa hospitali. Kutokana na ukweli ambao umetupatia, tunaamini una kesi nzuri sana ambayo unaweza kudai fidia ya kila aina. Hata hivyo Mahakama za Tanzania hazitoi fidia kubwa. Tunakushauri uwasiliane na mwanasheria wako ili aweze kukuongoza zaidi.

## Huduma mbaya kwa wateja wa kampuni ya simu

**Mimi ni mteja wa kampuni ya simu nchini Tanzania ambapo mfumo wake wa huduma kwa wateja ni mbaya sana. Ninapiga huduma kwa wateja mara kwa mara lakini nasubirishwa kwa muda mrefu. Wakati mwingine inachukua miito kumi na unapata tu ujumbe wa kawaida kwamba "watoa huduma wetu wanahudumia wateja wengine, usikate simu utahudumiwa na mhudumu anayefuata." Wakati mwingine inachukua hadi dakika 30 kabla ya kuhudumiwa. Katikati ya mazungumza mtoa huduma anakata simu na inabidi nianze upya tena. Je, nina haki yoyote na nawezaje kujilinda dhidi ya kampuni hii ya simu? Wananikera.**

*4 Februari 2013*

Kero yako inaweza kutatuliwa na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania ambayo ni taasisi inayosimamia makampuni yote ya simu nchini Tanzania. Kanuni za Ubora wa Huduma za Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta za mwaka 2011 zinatamka kwamba muda wa mteja kusubiri kuongea na mtoa huduma za miito ni chini ya dakika tano. Hivyo unaweza kupeleka malalamiko kwa kampuni ya simu ukieleza wazi malalamiko yako, na kampuni ya simu inahitajika kujibu malalamiko hayo ndani ya siku 21 kutoka siku ya kupokea malalamiko. Ikiwa hujaridhika na jibu lao, unaweza kuendelea kupeleka malalamiko kwa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA).

Mamlaka ya Mawasiliano itafanya uchunguzi juu ya malalamiko na inaweza kuitaka kampuni ya simu kupeleka nyaraka yoyote kama itahitajika. Mara baada ya Mamlaka ya Mawasiliano kukamilisha uchunguzi, itaziandikia pande zote mbili kuhusu kusikilizwa kwa malalamiko na kutoa tarehe ya kusikilizwa au ikiwa hakuna haja ya kusikilizwa, basi Mamlaka itawashauri jinsi itakavyoendelea na ufumbuzi wa jambo hilo. Baada ya kusikiliza, Mamlaka ya Mawasiliano itafanya maamuzi na itatoa mwongozo ikiwa ni pamoja na, kama itaona inafaa, kutoza faini. Watu wengi hawajui kuhusu haki zao dhidi ya makampuni ya simu - baadhi ya waendeshaji wa simu pia hawajui jambo hili. Pia inaonekana unawasiliana mara kwa mara na watoa huduma za mawasiliano - tunatumaini kwamba tatizo sasa limetatuliwa.

## Asilimia 5 ya malipo ya huduma kwenye mgahawa

**Nilikwenda na baadhi ya marafiki kupata chakula cha jioni na nilitozwa asilimia 18 ya kodi ya ongezeko la thamani pamoja na malipo ya huduma ya asilimia 5. Kwa nilivyoambiwa, chakula hakilipiwi kodi ya ongezeko la thamani. Je, malipo hayo hapo juu siyo kinyume cha sheria?**

*11 Februari 2013*

Kuna baadhi ya bidhaa hazilipiwi kodi ya ongezeko la thamani kama vile mikate na aina fulani ya vyakula. Hata hivyo, unapokuwa kwenye mgahawa chakula kinapopikwa na

unapopewa inamaanisha kwamba unapewa huduma za upishi na hivyo asilimia 18 ya kodi ya ongezeko la thamani inahusika. Swali la kufurahisha zaidi ni asilimia 5. Tumepitia sheria za kodi na hatujaona kodi ya aina hiyo mahali popote. Ni maoni yetu kwamba mgahawa unatoza asilimia 5 kama bakshishi ya lazima kwa wahudumu . Hoja ya bakshishi inajikita kwenye dhana kwamba kila mmoja anafuata mfumo wa Marekani wa kuacha "tip" kwa mhudumu. Marekani mfumo huu unatokea kwa sababu mhudumu halipwi na hivyo wanajilipa kupitia malipo haya ya bakshishi. Inawezekana ndiyo maana wahudumu wa kimarekani wanawajali sana wateja wao.

Maoni yetu ni kwamba, haikuwa lazima kutozwa asilimia 5. Unaweza kukataa, labda kama mwanzoni kabla ya kula uliambiwa kuhusu asilimia 5 na uliridhia, ikiwa na maana kwamba, uliingia mkataba na mmiliki wa mgahawa kwamba utalipa asilimia 5 kama ada ya huduma bila kujali kiwango cha huduma utakayopata. Tunashangaa kama ulitoa "tip" ya asilimia 5 ambayo ni kutozwa malipo mara mbili.

## Kutoga mdomo kumesababisha maambukizi

**Nilikwenda kliniki ambayo inatoboa mahali popote unapotaka. Mtaalam wa kutoga, ambaye anadai amesomea Ulaya, aliniambia kila kitu kuhusu mashine na kipaji ikiwemo namna wanavyochora mwilini. Kwa kiasi fulani alinishawishi kutoga mdomo wangu kitu ambacho nilifanya. Aliniambia kwamba wakati mwingine inaweza kuleta maambukizi na akaongeza pia kwamba hata hewa wakati mwingine inaweza kusababisha maambukizi kwa hiyo hakuna cha kuhofia. Niliendelea kutoga ambako sasa kumepelekea mdomo wangu kuvimba kufikia ukubwa wa mpira wa gofu. Siwezi kula wala kuongea na wakati wote nipo kwenye maumivu. Ninatumia dozi tatu na dawa za kupaka lakini haijasaidia. Nilielekezwa kwa mtaalam na nataka kujua kama naweza kuishtaki kliniki na mtaalam juu ya jambo hili. Mshauri wangu wa masuala ya sheria ananiambia napoteza muda wangu kwa sababu hiyo ni sehemu ya kutogwa kwenye maeneo kama hayo. Nifanye nini?**

*18 Februari 2013*

Mshauri wako wa kisheria hayuko sahihi. Kwa kukutaarifu tu kwamba taratibu hizo zinaweza kukuletea madhara ya maambukizi, miongoni mwa mambo mengine, hakukuondolei haki ya kuiwajibisha kliniki au mtaalam aliyekutoga. Inaweza kupunguza fidia ambazo unaweza kuzipata Mahakamani kwa sababu uliarifiwa juu ya hilo ila haliwezi kuiondolea kabisa kliniki na mtaalam wajibu. Inaonesha kulikuwa na uzembe mkubwa mahala fulani wakati wa matibabu. Inawezekana kifaa hakikusafishwa vizuri au hakikutumika vizuri. Kwa hakika kulikuwa na wajibu wa kujali, ambao ulivunjwa na kukusababishia madhara haya. Tunashauri kwamba upeleke barua ya madai kwa kliniki na mtaalam wake angalau uwaambie walipie gharama za matibabu. Wakishindwa kufanya hivyo wasiliana na mwanasheria wako ambaye anaweza kukuongoza juu ya hatua za kuchukua ili kufungua shauri.

## Kusafirishwa mji tofauti

**Niliingia uwanja wa ndege wa Nyerere kwenda Kilimanjaro. Siku hiyo kulikuwa na ndege nyingine za shirika hilo hilo zilizokuwa zinakwenda maeneo mengine, lakini kwa kutokuelekezwa vizuri, mimi na abiria mwenzangu tuliishia kusafiri na ndege isiyo sahihi na kupelekwa Mtwara. Ndege ya kurudi ilikuwa imejaa na nililazimika kutumia siku nzima Mtwara ambako pia nililazimika kukata tiketi**

**nyingine ya kurudi Dar. Je, ninaweza kulishtaki shirika la ndege?**

*25 Machi 2013*

Ni kweli unaweza kushtaki shirika la ndege. Mafanikio ya kesi yako yatategemea ushahidi utakaotoa na kuthibitisha hasara uliyoipata. Kabla ya kushtaki tunashauri ulipatie taarifa shirika la ndege juu ya nia yako ya kushtaki na ujaribu kulimaliza suala hili nje ya Mahakama.

Tunaamini una kesi nzuri lakini hatuna hakika na fidia unayoweza kuipata. Mwanasheria wako atakuongoza zaidi.

## Deni baya limejifuta, kwa nini nilipe

**Niliruhusiwa kutoa pesa zaidi ya kiasi kilichomo kwenye akaunti yangu hadi kufikia deni la Shilingi milioni 100 kwa muda wa miezi kumi na miwili. Nilitoa dhamana binafsi na kwa kuongezea niliweka dhamana ya ploti ya ardhi eneo la Mbezi, Dar es Salaam. Kutokana na matatizo ya kibiashara ambayo yalikuwa nje ya uwezo wangu na ambayo benki inajua, nilishindwa kurejesha mkopo wangu na hatimaye benki ilifuta akaunti yangu ya mkopo ambayo kwa sasa inasomeka sifuri. Cha kushangaza, mwanasheria wa benki hivi karibuni aliniletea barua ya kudai deni halisi pamoja na riba iliyoongezeka. Je, hii ni sawa? Nilidhani mkopo umefutwa na benki ilielewa msimamo wangu kwamba ingawa sikulipa mkopo huo, haikuwa makusudi. Hii siyo haki kabisa. Tafadhali shauri.**

*22 Aprili 2013*

Mkopo wako ulifutwa na benki ili kuendana na miongozo ya Benki Kuu, pamoja na kanuni bora za uendeshaji wa benki. Hii haina maana kwamba mkopo haupaswi kulipwa. Kufuta mkopo ni maingizo ya kiuhasibu kwenye vitabu vya benki ili hali halisi ya kifedha ya benki iweze kuJulaikana. Kama kwa kufuta tu mkopo mkopaji angekuwa amesamehewa wajibu wake wa kulipa, hadi hivi sasa benki zingefunga biashara, na kila mtu angeacha kulipa. Siyo tu kwamba fikra zako haziko sahihi, lakini pia ardhi yako uliyoweka dhamana ipo hatarini kuuzwa. Pia kumbuka kwamba unapozembea, na kadiri unavyochelewa kulipa deni lako ndivyo utakavyozidi kulipa riba, kwa sababu adhabu ya riba ndiyo huzidisha deni kwa wazembeaji. Wanasheria wako wanaweza kukuongoza zaidi.

## Mtaalam wa nusu kaputi alinitania

**Nilikuwa na maumivu makali ya tumbo na baada ya kuwasili hospitali, daktari aliniambia ninahitaji kufanyiwa upasuaji wa tumbo mara moja na kwamba nitalala usingizi wakati wa upasuaji. Niliandaliwa kwa ajili ya upasuaji na kupelekwa chumba cha upasuaji. Daktari aliuliza jina langu, kisha akaniuliza jina langu la pili, kisha akaniuliza jina langu la kati - alionekana kupendezwa zaidi nami wakati wa upasuaji. Baada ya muda, alirudia tena kuniuliza majina yangu. Nina asili ya Asia na majina yangu si rahisi kuyatamka. Kisha akasema kwamba nisiwe na wasiwasi, kwamba sitakufa. Hii ilisababisha kuwa na wasiwasi sana wakati wa upasuaji na bado nina wasiwasi hata sasa. Je, maneno ya mtaalam wa nusu kaputi siyo kashfa? Ninaweza kumshtaki kwa kunichezea?**

*29 Aprili 2013*

Ikiwa tumeelewa swali lako vizuri unataka kumshtaki mtaalam wa nusu kaputi wako kwa kukutania. Pia unataka kumshtaki kwa kukuuliza jina lako mara kadhaa na kwako wewe hayo yote yalikusababishia wasiwasi wakati wa na baada ya upasuaji. Hatujui kivipi ungeweza kuwa na wasiwasi wakati wa upasuaji wakati ulilala. Pia inaonekana wazi kwetu kwamba mtaalam wa nusu kaputi alikuwa akifanya kazi yake tu. Itifaki ya kawaida inaeleza kwamba maswali

huulizwa kwa mgonjwa ili kuhakikisha kwamba mgonjwa anayefanyiwa upasuaji ni mgonjwa sahihi. Kwa kuulizwa jina lako mara kadhaa haimaanishi kwamba mtaalam wa nusu kaputi "alivutiwa na wewe" bila kujali unachomaanisha unaposema "alivutiwa na wewe." Kwa nia ya kitabibu, ni kweli mtaalam wa nusu kaputi, atavutiwa na mgonjwa aliyepo kwenye meza ya upasuaji. Je, hilo linatoa haki ya kumshtaki? Hatufikirii hivyo. Maneno kwamba hutakufa, au utapona, kwa hakika hayawezi kuwa kashfa. Tunaamini yalikuwa na maana ya kukupunguzia msongo.

Isipokuwa kama kuna kitu hujatuambia, hatuoni namna unavyoweza kumshtaki mtaalam wa nusu kaputi. Hata hivyo, wanasheria wako wanaweza kukuongoza zaidi.

## Bima ya maisha kwa mwanajeshi

**Mimi ni askari kwenye majeshi ya Tanzania na hivi karibuni nilitembelea nchi ya Ulaya ambapo askari wote wana mikataba ya bima ya maisha binafsi ili kulinda familia zao. Nilipofika Tanzania, nilimfuata wakala wa bima kwa ajili ya kupata bima ya maisha na akasema kwa kuwa nilikuwa jeshini sihusiki. Aliongezea pia kwamba sera ya bima ya maisha pia haifidii vifo vya kujitakia. Je, hii ni kweli? Je, ninapataje bima?**

*27 Mei 2013*

Sheria ya Bima ya mwaka 2009 inasema wazi katika kifungu cha 111 kwamba (1) sera ya bima ya maisha ambayo inatamka kuwa sera itakuwa batili iwapo mtu aliyekatiwa bima akiwa timamu ama ana ugonjwa wa akili anakufa kwa matendo yake mwenyewe au amehukumiwa kwa makosa makubwa kwa muda fulani itakuwa batili; (a) kwa muda unaozidi miaka miwili tangu siku ya kutolewa kwa sera hiyo bila kujali masharti ya sera yanayokwenda kinyume; au (b) pale mpewa bima anapofariki kutokana na matendo yake mwenyewe au amehukumiwa kwa makosa makubwa baada ya kuisha kwa muda ulioelezwa au baada ya miaka miwili tangu kutolewa kwa sera ya bima, chochote kinachoanza. (2) Bima ya maisha ambayo haina kifungu kama ilivyoelezwa kwenye kifungu kidogo (1) haitakuwa batili kwa sababu ya mtu aliyepewa bima, akiwa na akili timamu au kichaa, anajiua au anahukumiwa kwa makosa makubwa wakati wowote baada ya sera kutolewa.

Unaweza kuona kutokana na maelezo hapo juu, kama mtu anajiua kwa matendo yake ndani ya miaka miwili ya sera, sera ya bima haitamlinda. Hata hivyo sheria inamlinda mtu aliyepewa bima kwa kusema kwamba baada ya miaka miwili ya sera, neno lolote la kwenye sera ambalo halitoi ulinzi kwa kifo cha kujitakia ni batili, ikiwa na maana kwamba unalindwa. Ni kweli makampuni mengi ya bima hayalijui hili na sera zao zinaweka kipengele kama hiki kinyume na sheria.

Kifungu cha 112(1) cha Sheria ya Bima kinatamka kwamba sera ya bima ya maisha ambayo inatamka sera itakuwa batili pale aliyepewa bima anafariki kutokana na huduma za kijeshi ambazo anazifanya chini ya Serikali ya Tanzania kwenye operesheni zozote za kijeshi dhidi ya adui itakuwa batili. Katika kifungu kidogo cha (2) cha Sheria inatamka kuwa hakuna mtoa bima atakayekataa kumpa mtu sera ya bima ya maisha kwa sababu kwamba anatoa au anaelekea kutoa huduma za kijeshi nchini Tanzania. Hivyo kitendo cha wakala wako/au mtoa bima ni batili. Hivyo mtoa bima hawezi kukataa kukupa bima kwa sababu tu eti wewe ni mwanajeshi.

## Begi kumdondokea abiria

**Nilisafiri kwa ndege katika daraja la kawaida, ambapo mtu mmoja aliweka begi**

**lake kubwa kwenye keria ya mizigo ndani ya ndege. Nusu ya begi hilo haikujifunga vizuri kutokana na kujazwa manukato ambayo aliyanunua kwenye maduka ambayo hayalipi ushuru. Nilimweleza kuhusu jambo hilo, kwamba awaeleze wahudumu wa ndege waliweke sehemu nyingine lakini alikaidi. Badala yake alilisukumia tu kwa ndani likakaa. Nililalamikia jambo hili kwa mhudumu wa ndege, lakini hakujali. Tukiwa katikati ya safari, wakati nikiwa nimelala, mtu mwingine alifungua sehemu ya mizigo. Chupa mbili za manukato zilinidondokea kichwani, na kupelekea kutokwa na damu. Mara moja nilihudumiwa na mtoa huduma ya kwanza na daktari aliyekuwepo kwenye ndege. Nataka kuchukua hatua. Nimshtaki nani na kivipi?**

*13 Mei 2013*

Kuna kiwango cha mwisho cha mzigo ambacho abiria anaruhusiwa kukibeba, kwa kawaida ni kilo 12. Na hii ni kwa sababu za kiusalama, ikiwa ni pamoja na kuelewa kwamba keria ya ndani ya ndege haiwezi kuchukua zaidi ya uzito fulani.

Inawezekana kabisa kwamba begi la abiria huyo lilikuwa na uzito mkubwa kuliko unaoruhusiwa. Hivyo, shirika la ndege limevunja mkataba wenu wa usafiri, na unaweza kuwashtaki. Eneo jingine mwanasheria wako anaweza kukushauri ni kumshtaki mhudumu wa ndege kwa kuzembea wito wako. Ni wazi pia unaweza kumshtaki mwenye mzigo na abiria aliyefungua sehemu ya mizigo wakati wa safari.

Swali jingine ni wapi hasa utashtaki? Hatuna taarifa za kutosha zinazotuwezesha kujibu swali hili, lakini inawezekana ukashtaki nchini Tanzania, au nchi uliyoanzia safari. Kabla hujashtaki ni vizuri ukazingatia gharama za kisheria utakazotumia na fidia unayoweza kufidiwa.

## Msusi amebadili nywele kuwa nyekundu

**Ninaolewa wiki mbili zijazo na nilikwenda saluni kutengeneza nywele zangu. Nilimweka wazi kabisa msusi kwamba ninahitaji apake nywele zangu utando/ufito wa rangi nyekundu isiyokolea. Msusi amekoleza rangi na nywele zinakaribia kuwa damu ya mzee na kichwa changu kinaonekana chekundu. Imeniharibia hisia zangu na nina mawazo. Ninaonekana mbaya kuliko unavyodhani. Ninaweza kumwajibisha msusi?**

*3 Juni 2013*

Kutokana na wingi wa maswali inawezekana tunakujibu swali lako wakati tayari harusi yako imekwishafanyika, kwa hilo tunaomba radhi. Tuje kwenye swali lako, tunaamini kwamba kama ulikuwa wazi kwa ulichokuwa unakitaka na msusi alielewa maelekezo yako, unaweza kumshtaki chini ya makubaliano yako ya mdomo na msusi. Changamoto itakuwa kwenye ushahidi kwa sababu unaweza kudai kama ulivyosema kwenye swali lako na msusi akaja na kitu tofauti kabisa. Unaweza kujaribu kutafuta mashahidi ambao walikuwa saluni siku hiyo, na zaidi unaweza kufuatilia rekodi ya msusi. Anaweza kuwa amewabadilisha wengine kuwa na vichwa vyekundu pia. Ni muhimu ushahidi ukusanywe kabla ya kufungua kesi. Wanasheria wako wanaweza kukuongoza zaidi.

## Mtoto alijeruhiwa katika mchezo wa kuruka ngome

**Nilimpeleka mtoto wangu kwenye sherehe na kutokana na usimamizi mbaya alidondoka wakati wa mchezo wa kuruka ngome na alitakiwa kusafirishwa kwa matibabu maalumu nje ya nchi. Mwanangu sasa anatembelea magongo na anahitaji upasuaji mwingine kwa sababu aliumia**

**vibaya sana. Ninatambua kwamba hii ilikuwa ni sherehe iliyojawa na furaha, lakini kwa hakika kuna sheria ambayo inawataka waandaaji kuwalinda watu, hasa watoto wadogo. Nimshtaki nani?**

*3 Juni 2013*

Wanasheria wako wanaweza kufikiria kuwashtaki waandaaji binafsi, kampuni ambayo iliandaa sherehe, au kampuni ya ulinzi inayowajibika kutoa ulinzi, muuguzi wa zamu (kama hawakulisimamia hili vizuri), mtu anayewajibika kusimamia mchezo wa kuruka ngome, kampuni iliyokodi vifaa vya mchezo wa kuruka ngome, na mtu mwingine yeyote ambaye ama moja kwa moja au kwa namna isiyo dhahiri alichangia kuumia kwa mtoto wako. Hii pia inahusisha mzazi yeyote ambaye alikuwa pale wakati au angekuwa na wajibu wa kuangalia ngome ya kuruka.

Ni kweli kwamba ilikuwa ni sherehe tu, lakini haiwezi kuwaondolea wajibu wa kuwaangalia watu wanaowakaribisha. Kimsingi, hata kama mtoto wako hakualikwa na alienda tu, waandaaji bado walikuwa na wajibu wa kumwangalia. Mtu anayekaribisha ana wajibu wa kujali, na kwa swali lako inaonesha wazi kwamba wamevunja wajibu ambao ulipelekea majeraha. Ukiwa na ushahidi sahihi Mahakamani, ikiwemo ushahidi wa kitaalam wa daktari, una kesi nzuri, isipokuwa labda kama kuna kitu umezidisha.

## Dawa ya kuchoma/kufukiza kuua mbu ni bandia

**Tanzania ina bidhaa nyingi bandia ambazo ni aibu kuhusisha hata dawa za malaria. Sasa nimegundua kwamba dawa za mbu ambazo tunazichoma majumbani mwetu ili kufukuza mbu pia ni bandia. Nimekuwa nikitumia dawa fulani kwa miaka mingi na miezi michache iliyopita nilibadilisha na kuanza kutumia dawa mpya ya malaria ambayo imepelekea wanangu kuugua malaria mara 3. Niliamua kuipeleka dawa hiyo kwa mwanafunzi wa kemia Chuo Kikuu ch Dar es Salaam ambaye alifanya uchunguzi na kuhitimisha kwamba viambata viwili ambavyo ndiyo visababishi vikubwa vya mbu kukimbia vimekosekana kwenye dawa hizi za mbu. Hii ina maana nimekuwa nikitumia dawa za mbu bandia na siyo ajabu ndiyo maana tumeugua malaria mara nyingi sana. Nifanye nini kwa kuwa nilizinunua kwenye duka dogo la jirani?**

*1 Julai 2013*

Sababu tu kwamba umezinunua kwenye duka haina maana kwamba huwezi kumshtaki mtengenezaji na/au muagizaji. Unaweza kushtaki kama tunavyokuelekeza hapa chini.

Wajibu wa mtengenezaji ni kanuni au dhana ya kisheria ambayo inawawajibisha watengenezaji au wauzaji husika kwa madhara yanayosababishwa na bidhaa zisizofaa zinazouzwa kwa walaji. Wajibu wa mtengenezaji kwa kawaida unaangaliwa kwenye misingi mitatu. Wa kwanza ni uzembe, ambao ni kushindwa kuchukua tahadhari ya kutosha ili kuzuia bidhaa sizizofaa zitokanazo na mchakato wa utengenezaji, au kushindwa kuwapa tahadhari ya kutosha juu ya hatari inayoambatana na utumiaji wa bidhaa hiyo. Pili, ni kuvunja wajibu, ambayo ina maana ya kushindwa kutimiza masharti ya madai au ahadi kuhusu ubora au utendaji wa bidhaa fulani, na mwisho ni wajibu wa moja kwa moja, ambapo muuzaji au mzalishaji anawajibika kwa bidhaa zisizofaa hata kama masharti ya uzembe au wajibu hayajavunjwa. Hivyo mwanasheria wako anaweza kukuongoza namna ya kuendelea kufungua kesi.

Aidha, ubora wa bidhaa nchini unaohusu dawa za mbu unasimamiwa na Mamlaka

ya Chakula na Dawa (TFDA) ambayo ndiyo inayoruhusu uingizaji wa bidhaa hizi. Mamlaka hii ina huduma za maabara na unaweza kutoa taarifa juu ya dawa hizi bandia kwa Mamlaka. Dawa hizo zinaweza kukamatwa na Mamlaka na tunakusihi kutoa taarifa ili watu wengine wasiathirike na dawa hizi bandia za mbu.

## Msusi kuunguza nywele za bi harusi

**Siku chache kabla ya harusi yangu nilikwenda kwa rafiki yangu kutengeneza nywele. Wakati wa kukausha nywele zangu, chuma kilishikilia nywele zangu na kuniunguza sehemu kubwa ya mbele. Lilikuwa ni tukio baya sana kwangu na lilinipelekea kukosa kabisa furaha wakati wa harusi. Sionekani kama bi harusi na picha zangu zinatisha. Ninawezaje kumwajibisha mwanamke huyu? Nataka nimfundishe kwa kumdai mabilioni.**

*15 Julai 2013*

Kuna masuala kadhaa ya kuvutia hapa. Kwa kuanzia, kama rafiki yako hajasomea ususi na alikuwa akikusaidia bure, itakuwa ni ngumu sana kwako kuweza kufanikiwa kama utaamua kufungua kesi dhidi yake. Kama rafiki yako amesomea ususi na bado alikusaidia kutengeneza nywele bure, unaweza kumshtaki kwa sababu atahukumiwa kwa kuzingatia utaalamu anaotakiwa kuwa nao msusi.

Mwisho, kama rafiki yako ni msusi na alilipwa kwa kazi ya kukutengeza nywele, unaweza kumshtaki chini ya sheria za mikataba na kudai fidia pia. Tunaomba kukutaarifu kwamba Mahakama za Tanzania hazitoi fidia kubwa hivyo usitegemee mabilioni unayoyazungumzia. Wanasheria wako wanaweza kukuongoza zaidi.

## Ndege zinaruka kwenye anga langu

**Ninamiliki eneo kubwa la ardhi karibu na uwanja wa ndege na kuna ndege fulani ambayo kila wakati hupita juu ya ardhi yangu wakati wa kuingia Dar es Salaam. Naamini huu ni sawa na uvamizi wa ardhi yangu na nahitaji kufidiwa kwenye hili. Nifanyeje ili kuitoza ndege inayopita juu ya ardhi yangu mara kwa mara?**

*2 Septemba 2013*

Ikiwa ndege zote zingelazimishwa kulipa hicho unachokidai, wangetumia muda mwingi kushughulikia madai/ankara za watu kama wewe kuliko kufanya biashara ya ndege. Pia, ungefanya usafiri wa ndege kuwa mgumu. Tukirudi kwenye swali lako, jibu lake ni rahisi tu, -hapana. Huwezi kudai chochote kwenye ndege kwa sababu anga lipo juu ya ardhi yako, ambalo kwa sasa halitumiki, na hautatumia na wala siyo la kwako. Ndege haijafanya uvamizi wowote. Wanasheria wako watakuongoza zaidi.

## Mtu mnene, kiti kidogo

**Nilisafiri kwa ndege kutoka Dar kwenda ng'ambo na nilipangiwa kukaa karibu na mtu mnene sana. Alikuwa na zaidi ya kilo 160, sina hakika namna alivyoweza kukaa kwenye daraja la kawaida (Economy). Wakati alipolala alikuwa akikoroma na alikuwa akinigusa kwa mikono yake. Je, hakuna ukomo wa uzito kwenye daraja la kawaida? Lazima nikiri kwamba ulikuwa ni mtihani mkubwa sana kwangu. Ingawa namuonea huruma abiria huyo, nafikiri ndege ingekuwa na sehemu ya watu wanene. Baada ya ndege kuondoka, kila ninapomuona mhudumu mwembamba, anaonekana mnene kwangu. Nifanye nini?**

*16 Septemba 2013*

Hukuweka wazi ni shirika gani la ndege hilo, lakini nikujibu kwa ujumla, hakuna sheria zinazotaka mtu mnene kununua tiketi mbili au kutumia daraja la biashara. Hata hivyo, kuna ndege chache sana ambazo kwa

sasa zinataka abiria wa namna hiyo kwa ajili ya usalama na starehe za abiria wengine, kununua tiketi mbili, na kama ndege haijajaa, pesa ya tiketi ya pili inarudishwa. Kimsingi, baadhi ya ndege zina sera zinazobana zaidi kwamba huwezi kuingia kwenye ndege kama una tiketi ya daraja la kawaida na kama siti ya ndege haikutoshi.

Kutokana na maelezo hapo juu, na kwa kuwa ulikuwa na mkataba wa usafirishaji na ndege, tunashauri uombe ndege ikufidie kutokana na kero uliyoipata. Inawezekana ndege kukupa tiketi ya bure. Mwanasheria wako anaweza kukuongoza zaidi.

## Kumwajibisha muuguzi

**Muuguzi aliyekuwa anamhudumia mgonjwa wangu alimwacha na kuondoka hospitali wakati alikuwa bado yupo kwenye zamu. Muuguzi hakutoa dawa muhimu ambazo daktari alielekeza na ikapelekea kukaa muda mrefu hospitali. Muuguzi huyo pia anafahamika kwa kukosa heshima hapa hospitalini na kuwadhalilisha wagonjwa anaowauguza/hudumia. Je, kuna rejista kuu ambapo ninaweza kulalamika na kufanya nesi huyu aondolewe?**

*7 Oktoba 2013*

Watu wengi hawajui hili lakini kuna sheria maalum ambayo inasimamia mwenendo wa wauguzi. Sheria ya Uuguzi na Ukunga inayo rejista ambayo inasimamiwa na Baraza lililoanzishwa chini ya Sheria hii. Ulichokieleza hapo juu ni tuhuma kubwa za mwenendo mbaya wa kitaaluma, na kama ni kweli, inaweza kupelekea nesi kuondolewa kwenye rejista.

Taratibu ni wewe kupelekea malalamiko yako kwa njia ya maandishi kwa Baraza ambalo linaweza kuita ushahidi zaidi kama utahitajika, na kufanyia uchunguzi suala hilo. Muuguzi atakuwa ha haki ya kujibu tuhuma zako na Baraza litatoa maamuzi yake ambayo ni pamoja na kuondoa jina la muuguzi kwenye rejista. Sheria pia inatamka kwamba mtu yeyote atakayehisi kuwa ameonewa kutokana na maamuzi ya Baraza, ndani ya miezi mitatu tangu alipoarifiwa maamuzi hayo anaweza kukata rufaa dhidi ya maamuzi hayo kwa Waziri mwenye dhamana ya afya.

Waziri anaweza kufuta au kuruhusu rufaa yoyote au kurekebisha au kubadilisha maamuzi ya Baraza au kutoa amri yoyote anayoona inafaa. Zaidi Waziri anaweza ndani ya mwezi mmoja baada ya kutathimini rufaa kumpa notisi ya tathmini hiyo mtu husika na mtu huyo kama hajaridhika na maamuzi ya Waziri, ndani ya miezi mitatu anaweza kupeleka suala hilo Mahakama Kuu. Wanasheria wako wanaweza kukuongoza zaidi.

## Alama za vidole benki

**Mimi ni mkurugenzi wa kampuni nchini Tanzania lakini ninaishi nje ya nchi. Kama raia wa kigeni, na kuhitaji kufungua biashara zaidi nchini Tanzania, niliamua kufungua akaunti ya benki Dar. Nilishtushwa sana pale benki iliponiomba alama za vidole ikisema kwamba ni hitaji la kisheria. Hii ndiyo mara yangu ya kwanza kusikia kuhusu jambo hili. Nilishangazwa sana kwa namna benki ilivyonifanyia wakati vidole vyangu vilipowekwa kwenye kikopo cha wino. Kimsingi wino uliingia kwenye moja ya shati zangu. Benki nyingine iliniambia hawachukui alama za vidole. Nifanye nini? Katika hali nyingine, wakati nikiongea na benki yangu kuhusu kuhamisha fedha kiasi cha Dola milioni moja kuingia kwenye akaunti yangu iliniambia kwamba kuna sheria za kutoa taarifa kwa aina hiyo ya uhamishaji fedha kwenye akaunti yangu. Ninaona haya yote ni maajabu, ninahofia kuwekeza hapa.**

*21 Oktoba 2013*

Kanuni za Kuzuia Utakatishaji wa Fedha Haramu ya mwaka 2012 kwenye kifungu cha 5 (1) inaeleza wazi kwamba mtoa taarifa (Benki ni mtoa taarifa) atachukua taarifa kutoka kwa, au kuhusiana na, mtu ambaye ni raia wa nchi nyingine na siyo mkazi wa Jamhuri ya Muungano; kutoka kwa mtu huyo: (a) majina kamili na anuani ya makazi; (b) tarehe na mahali pa kuzaliwa; (c) utaifa; (d) pasipoti; (e) viza; (f) Namba ya Utambulisho wa Mlipa Kodi, kama namba hiyo imetolewa kwa mtu huyo; (g) yoyote au zote kati ya, namba za simu, namba ya faksi, anuani ya posta na barua-pepe; (h) saini na alama za dole gumba. (2) Iwapo mtoa taarifa anafahamu au anatakiwa kufahamu kwamba mtu anayezungumziwa katika kanuni ndogo (1) hana uwezo wa kisheria wa kuanzisha uhusiano wa biashara au kumaliza shughuli mojawapo bila msaada wa mtu mwingine, mtoa taarifa atatakiwa, pamoja na kupata maelezo yaliyo tajwa katika kanuni ndogo (1), kupata kutoka kwa mtoa msaada (a) majina kamili na anuani ya makazi; (b) tarehe na mahali pa kuzaliwa; (c) utaifa; (d) pasipoti; (e) viza; (f) Namba ya Utambulisho wa Mlipa Kodi, kama namba hiyo imetolewa kwa mtu huyo; (g) saini na alama za dole gumba; (h) yoyote au zote, namba za simu, namba ya faksi, anuani ya posta na anuani ya barua-pepe.

Kutokana na maelezo hapo juu, unaweza kuona kwamba chini ya Kanuni hizi ni lazima kupata alama zako za vidole. Hivyo kama malalamiko yako ni kuhusu kuchukuliwa alama za vidole, hakuna unachowezakufanya. Mshangao wako pia hauko wazi sana kwetu kwa kuwa nchi nyingi zenye matatizo lukuki yanayohusu utakatishaji fedha, ugaidi, madawa, usafirishaji haramu na mambo kama hayo, zinataka alama za vidole za watu zichukuliwe.

Kama malalamiko yako ni kuchafuliwa shati lako, unaweza kuishtaki benki, lakini ujue kama fidia ipo, itakuwa ni kidogo sana. Ada za Mahakama na gharama za kuendesha kesi hiyo zinaweza kuwa ni kubwa zaidi kuliko unachoweza kukipata.

Kwa kujibu kuhusu taarifa za "benki nyingine", tafadhali chukua tahadhari kwamba mtu huyo anakupotosha. Sheria ya Kuzuia Utakatishaji wa Fedha Haramu na Kanuni zake ni kali sana na kama kuna ukiukwaji, inatoa adhabu ya kifungo kwa wote, benki pamoja na wewe mwenyewe.

Kuhusu shughuli zisizo za kawaida kwenye akaunti, ni kweli Sheria ya Kuzuia Utakatishaji wa Fedha Haramu na Kanuni zake zinataka miamala hiyo kutolewa taarifa kwenye Kitengo cha Kudhibiti Biashara ya Fedha Haramu.

Hivyo, kufungua kwako akaunti, kusita kwako kuchukuliwa alama za vidole na ukweli kwamba mara baada ya kufunguliwa akaunti unataka kufanya muamala wa mamilioni ya Dola kutachukuliwa kwa mashaka makubwa na muamala huo ni lazima benki yako iutolee taarifa. Kushindwa kuripoti juu ya miamala hiyo kunaweza kuisababishia benki yako adhabu kali. Kwa maelezo zaidi, tunakushauri uwasiliane na wanasheria wako.

## Kupotosha jina la bia

**Nimekuwa nikinywa bia fulani kwa sababu matangazo yao yanaonesha watu wote wanaokunywa wamezungukwa na wanawake wazuri. Mwaka ulioisha, ambao nilikuwa nakunywa bia hiyo, sikuwahi kufanikiwa kuzungukwa na wanawake wazuri hata mara moja. Ninaweza kuishtaki kampuni ya bia kwa kunidanganya na kunipoteza fedha?**

*18 Novemba 2013*

Ni kweli kwamba kushtaki siyo jambo gumu sana lakini tunaamini suala hili unalipeleka mbali. Hatujawahi kuona tangazo lolote Tanzania la kampuni ya bia ambalo linatamka wazi kwamba kama utakunywa

zaidi bia zake, utazungukwa na wanawake wazuri. Matangazo unayoyaona ni chombo cha kutangazia umma na yanatumia watu wenye sura nzuri ili kuwavutia watu kununua bidhaa husika. Tunaamini una kesi dhaifu sana kutokana na maelezo uliyoyatoa. Pia, hatujui ni hasara gani ya kifedha umeipata hasa ukizingatia umekunywa bia zote. Mwanasheria wako anaweza kukuongoza zaidi.

## Kukosa 'dili' kubwa baada ya shirika la ndege kusitisha safari

**Nilikuwa nasafiri kwenda kuhudhuria mkutano muhimu sana huko Amerika ya Kusini. Shirika la ndege lilifuta safari zake dakika ya mwisho, hivyo nikalazimika kuchukua ndege nyingine, lakini sikufanikiwa kufika kikaoni kwa wakati. Matokeo yake nilipoteza 'dili' la maisha yangu. Nataka kushtaki shirika la ndege na kudai angalau Dola milioni 10. Tafadhali niongoze.**

*25 Novemba 2013*

Ingawa tunakusikitikia kwa kukosa 'dili' la maisha, kuna Mikataba maalum ya kimataifa ambayo inaweka kiwango cha juu cha fedha ambacho shirika la ndege linaweza kutoa kama fidia kwenye mazingira kama yako.

Kipekee kabisa, Mkataba wa Montreal unaweka kiwango/ukomo wa madai kama hayo. Kwa hiyo ni vigumu kudai kiasi cha fedha ulichotaja. Tanzania pia iliridhia Mkataba huo miaka 10 iliyopita na hivyo ni Mkataba wenye nguvu zote za kisheria nchini.

Sababu ya msingi ya Mkataba huu ni kulinda mashirika ya ndege yasidaiwe fidia bila kikomo. Vinginevyo itafanya uendeshaji wa mashirika ya ndege uzidi kuwa ghali. Tunakushauri uwasiliane na mwanasheria wako.

## Mende kwenye chakula

**Nilikwenda kwenye mgahawa wa kifahari ambao kila mmoja anategemea kwamba una jiko safi kuliko yote Tanzania. Amini usiamini, nilikula mende bila kujua. Niligundua baada ya kwenda haja kubwa kesho yake. Ninataka kumshtaki mmiliki wa mgahawa. Ninawezaje kufanya hivyo?**

*2 Januari 2014*

Inatuwia vigumu kuamini kwamba mende uliyemla alitoka siku ya pili baada ya kwenda chooni. Kutokana na baiolojia tunayoijua, ni wazi kwamba mende uliyemla angekuwa amesagwasagwa na mfumo wako wa mmeng'enyo wa chakula. Utafiti wetu unaonesha hakuna uwezekano wa mende huyo kutoka pamoja na kinyesi siku iliyofuata, labda kama alitengenezwa kwa shaba. Vilevile inatuwia vigumu kuamini ulijuaje kama ulijisaidia mende labda kama ulikuwa unafuatilia kinyesi chako, jambo ambalo watu wachache sana kwa kawaida hufanya.

Tukiacha hayo, iwapo suala lako la kula mende ni la kweli, basi una madai ya kimkataba na kimadhara dhidi ya mgahawa. Kama mgahawa ni kampuni yenye dhima ya ukomo, basi unatakiwa uishtaki kampuni na siyo mmiliki. Kama mgahawa unamilikiwa na mtu mmoja, unaweza kumshtaki mmiliki.

Mwisho, changamoto kubwa uliyonayo ni kuthibitisha kwamba ulikula mende. Unawezaje kuthibitisha kuwa mende uliyejisaidia ametoka kwenye mgahawa uliokwenda? Wanasheria wako wanaweza kukupa mwongozo zaidi.

## Kushinda bahati nasibu nje ya nchi

**Nilishinda gari ya kifahari kwenye mashindano ya bahati nasibu yaliyofanyika nje ya Tanzania. Ninakusudia kuileta nchini Tanzania lakini nimeambiwa ninatakiwa kulipa gharama kubwa za kodi/tozo ya uingizaji. Je, hakuna kifungu kinachotoa**

**msamaha kwa masikini kama mimi? Ninaweza kufanya nini zadi? Si ninaweza kuishusha gari nchini Kenya na kuiendesha hadi Dar? Je, hiyo itakuwa njia rahisi?**

*13 Januari 2014*

Ni kweli gari yako ya kifahari itatozwa kiasi kikubwa cha kodi ya uingizaji. Kodi nyingine uliyosahau kuitaja ni asilimia 18 ya kodi ya ongezeko la thamani ambayo utapaswa kuilipa. Uingizaji unasimamiwa na Sheria ya Usimamizi wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ambayo inatumika Afrika Mashariki yote, ikiwa na maana kwamba, haijalishi utashusha gari yako nchini Tanzania au Kenya, kodi hiyo hiyo itatozwa.

Hiari nyingine uliyonayo ni kuiuza gari kokote iliko hivi sasa. Hata hivyo, tafadhali elewa kwamba chini ya Sheria ya Kodi ya Mapato unaweza kutakiwa kulipa kodi ya mapato kwenye kipato ulichokipata ikiwa na maana kwamba kama Mamlaka ya Mapato (TRA) italigundua hilo, utatozwa kodi ya mauzo hata kama mauzo yamefanyika nje ya nchi.

Chini ya Sheria ya Kodi ya Mapato, kuna kifungu ambacho kinamruhusu Waziri wa Fedha kukusamehe kutozwa kodi kwenye kipato hicho kinachostahili kutozwa. Hata hivyo, ni mamlaka ya hiari na si lazima, na sina uhakika kama kuna uwezekano wa kupata msamaha kwenye mali iliyopatikana kwa kushinda mchezo wa bahati nasibu. Mshauri wako wa kodi anaweza kukuongoza zaidi.

## Dawa ya meno yenye nzi

**Nilinunua dawa ya meno kwenye duka kubwa Jijini Dar na nilipokuwa nasafisha meno yangu niligundua kwamba kulikuwa na nzi kwenye dawa ya meno. Nilishtuka sana na niliamua kumwaga dawa yote kutoka kwenye kifungio chake na niliambulia kuona nzi wengi na chembechembe/mabaki mengi kwenye dawa ya meno. Tangu hapo nimekuwa ni mwoga sana wa kununua bidhaa zilizofungwa hata kama zimerembwa vizuri kiasi gani. Ninaweza kufanya nini?**

*3 Februari 2014*

Kama unaamini kwamba “bidhaa zilizofungashwa vizuri” haziwezi kuingiliwa na nzi au uchafu mwingine, basi utakuwa unakosea sana. Kuna kesi nyingi ambazo baadhi ya kampuni zenye majina makubwa zimewahi kufanya makosa makubwa kama vile chupa za vinywaji kukutwa na mende, vipodozi vya kupaka mdomoni kuwa na nywele za nguruwe, gari kuwa na vikanyaga mwendo visivyo sahihi, ndege yenye injini mbovu, kochi zenye panya waliokufa ndani yake, madawa yaliyopakiwa vibaya, kanda za video ambazo mkanda wake unatoka, kompyuta kuunguza mapaja ya watumiaji, n.k. Ni lazima uelewe kwamba ni binadamu kama wewe ndiyo wanaopakia na kutengeneza na ingawa hatupendi vitokee, lakini wakati mwingine vinatokea.

Ukweli kwamba ulinunua dawa ya meno kwenye supamaketi (duka kubwa) haimaanishi kwamba huwezi kumshtaki mtengenezaji huko aliko. Kimsingi, unaweza kushtaki supamaketi, muuzaji wa jumla ambaye aliuzia supamaketi, na muingizaji kama ni tofauti na muuzaji wa jumla. Wanasheria wako wanaweza kukuongoza zaidi kwa sababu unahitaji ushahidi thabiti kuthibitisha jambo hili. Tuhuma tu peke yake hazitakufikisha mbali.

## Malipo ya ankara za maji baada ya kuhama

**Nilikuwa ninamiliki na kuishi kwenye nyumba fulani Jijini Dar es Salaam na miezi michache iliyopita niliiuza na hivyo kuhamia sehemu nyingine. Cha kushangaza nimepokea ankara za maji yaliyotumika baada ya mimi kuiuza. Nimeitaarifu**

**mamlaka ya maji juu ya jambo hili na nikajaribu kuelezea kwamba nimehama na kuiuza nyumba hiyo mwezi mmoja nyuma, kwa hiyo wamdai mmiliki wa sasa, lakini mamlaka ya maji imekataa na inasisitiza nilipe. Je, hii ni halali? Ninawezaje kupinga jambo hili?**

*10 Machi 2014*

Kanuni za Usambaziji Maji Na. 90 za mwaka 2013 zinatamka kwamba iwapo na kila mtumiaji wa maji anapokoma kutumia jengo lolote linalosambaziwa maji au anakoma kutumia maji yanayosambazwa na mamlaka, mtumiaji huyo atatoa taarifa/notisi ya awali isiyopungua siku tatu kwa maandishi kwa mamlaka ya maji na baada ya kupokea taarifa hiyo mamlaka ya maji itakata maji kwa gharama za mtumiaji.

Kanuni zinatamka zaidi kwamba mmiliki, mkazi au mtumiaji wa jengo linalowajibika kulipia huduma za maji na ambaye atatoa taarifa ya kusudi lake la kuondoka kwenye jengo au anakoma kutumia maji yanayosambazwa na mamlaka ya maji atawajibika kulipia mpaka mwisho wa mwezi ambao huduma hiyo imeondolewa au imesitishwa. Kutokana na vifungu vya kanuni hii, ni wazi kwamba ulitakiwa kutoa taarifa kwamba unaondoka na mamlaka ya maji ingesitisha maji ili kuhakikisha kwamba mtumiaji mpya anajitambulisha kwenye mamlaka ya maji na anaingia mkataba mpya wa kupewa maji.

Kwa kuwa hukutoa taarifa, ankara hizo zinajikusanya kwa jina lako na mamlaka ya maji haijui kama umeuza nyumba. Tunapendekeza ulipe gharama hizo na uzidai kwa mtumiaji wa sasa. Mwanasheria wako anaweza kukushauri njia mbadala.

## Muuguzi mtovu wa nidhamu

**Mara kwa mara nimekuwa nikimpeleka mzee wangu kwenye hospitali fulani ya Serikali kwa ajili ya matibabu. Cha kushangaza, kuna muuguzi mmoja ambaye anatoa lugha chafu sana kwa wagonjwa. Kuna malalamiko mengi kutoka kwa wagonjwa lakini ni kama ameziba masikio. Je, kuna mfumo wa kudhibiti wauguzi wasio na maadili/mienendo ya kitaaluma?**

*31 Machi 2014*

Ipo Sheria ya Uuguzi na Ukunga, Na. 1 ya 2010 ambayo inaweka vifungu vinavyotoa ulinzi, ukuzaji na uhifadhi, usalama na ustawi wa afya za jamii kupitia elimu na mienendo ya usimamizi na udhibiti wa wauguzi na wakunga. Hii ni sheria mahsusi ambayo inasimamia mienendo/tabia za wauguzi kama ambayo umeilalamikia kwenye swali lako.

Moja ya sababu zinazoweza kumzuia mtu kufanya kazi ya uuguzi ni pamoja na kuwadhalilisha wagonjwa kwa maneno, kimwili, kingono au kihisia pamoja na mambo mengine kama yalivyoainishwa kwenye sheria. Namna ya kulitatua jambo hili ni kupeleka malalamiko kwa Baraza la Wauguzi na Wakunga, ambapo Msajili wa Baraza ambaye pia ni Mtendaji Mkuu atayashughulikia malalamiko kwa usahihi. Sheria inatoa adhabu kali dhidi ya wauguzi ikiwemo kuondoa majina yao kwenye rejista ya wauguzi. Tumearifiwa kwamba ni malalamiko machache sana yamepelekwa kwa sababu watu wengi hawajui njia hii. Mwanasheria wako anaweza kukufafanulia zaidi.

## Kalamu ni chanzo cha kushindwa mtihani

**Mimi ni mwanafunzi wa chuo na ninataka kuishtaki kampuni ambayo kalamu zake nimekuwa nikizitumia kwa muda mrefu. Niliitumia kalamu yao kwenye chumba cha mtihani lakini ilishindwa kuandika, nilijawa na hofu, na sikufaulu mtihani. Hivi sasa sina budi kurudia mtihani. Je, ninaweza**

**kuishtaki kampuni iliyotengeneza kalamu?**

*31 Machi 2014*

Tumeshangaa ulishindwaje kuandika mtihani. Bila shaka kulikuwa na wanafunzi wengine wenye kalamu za ziada. Kwa vyovyote vile usingeshindwa kabisa kuandika mtihani kwa kukosa kalamu. Una kesi ya kufurahisha lakini kuna vizingiti vingi unatakiwa uvivuke, ni wazi una kesi dhaifu sana. Kwa mfano, kalamu inaweza kushindwa kuandika kwa sababu ya namna ulivyoitunza, ulivyoibeba n.k. Siyo rahisi kuelekeza lawama zote kwa mtengenezaji.

Hata hivyo, kama kalamu za mtengenezaji zina historia ya kutokuandika, una kesi dhidi yake lakini fidia utakayoipata ni ndogo sana. Tuna uhakika kwamba mtengenezaji hawezi kubeba lawama za wewe kushindwa kufanya na hivyo kutofaulu mtihani. Pia inatuwia vigumu kuamini juu ya jambo hilo na tunakushauri uwasiliane na mwanasheria wako.

## Picha za watoto kwenye chapisho la shule

**Mwanangu anasoma shule bora Jijini Dar ambapo shule inawapa hiari wazazi kuchagua iwapo wanapenda au hawapendi picha za watoto wao kuwekwa kwenye makala za matangazo ya shule. Kutokana na sababu zangu binafsi sikutaka picha ya mwanangu ichapishwe lakini nilishtuka kuona shule imeendelea kuichapisha. Nilimfuata mkuu wa shule ambaye alinibwatukia na kuanza kunihoji kwa nini nilipinga. Nifanye nini? Je, wanaweza kumfukuza mtoto wangu kwa sababu ya kukataa kwangu?**

*28 Aprili 2014*

Una kesi nzuri dhidi ya shule na mkuu wa shule. Kama ulikataa picha isichapishwe, miongoni mwa mambo mengine, haki ya faragha ya mtoto wako ni lazima iheshimiwe kwa ukamilifu. Mkuu wa shule kujaribu kupindisha suala hili hakubadili ukweli kwamba picha ya mwanao imechapishwa wakati hukupenda ichapishwe.

Inategemea unataka kuwa mkali kiasi gani, lakini hatuoni sababu ya kumwinamia mkuu wa shule. Iarifu shule haraka iwezekanavyo kwamba wasisambaze chapisho hilo na warudishe machapisho yote ambayo tayari wameshayasambaza (japo ni ngumu sana kufanyika). Kama hawatekelezi, unaweza kuendelea kuishtaki shule, na miongoni mwa maombi yako yawe kwamba shule ielekezwe kuzuia usambazaji wa chapisho na ulipwe fidia ya kifedha kwa madhara waliyokusababishia.

Kuhusu iwapo wanaweza kumfukuza mwanao kwa sababu ya jambo hili, jibu ni kwamba hawawezi. Kama watafanya hivyo, shule haitaonewa huruma na hakimu au jaji yeyote juu ya jambo kama hili. Wasiliana na mwanasheria wako kwa maelezo zaidi.

## Vipodozi vinaunguza ngozi

**Nilitembelea duka moja Jijini Dar ambapo kulikuwa na kundi la watu wanagawa vipodozi vya kujichubua ngozi bure. Nilitumia bidhaa hiyo ambayo iliharibu kabisa sehemu ya chini ya uso wangu. Simjui msambazaji lakini maelezo ya mawasiliano ya mtengenezaji yapo kwenye kopo/mkebe. Mwanasheria wangu anasema ninatakiwa kumjua aliyenipatia bidhaa ili kuwa na haki ya kushtaki, lakini simkumbuki. Mwanasheria wangu pia ana maoni kwamba sina mkataba na muuzaji kwa sababu nilipewa bure, akimaanisha ni ngumu kupata fidia. Tafadhali niongoze kwa kuwa nimedhamiria kumwajibisha yeyote.**

*28 Aprili 2014*

Ni kweli kwamba hauna mkataba na

muuzaji lakini hilo halikuzuii kumshtaki muuzaji na/au mtengenezaji kwa bidhaa mbovu ya ngozi. Kimsingi, kiasi cha fidia kinaweza kuwa kikubwa kuliko hata kwenye mkataba, hivyo hiki siyo kizuizi kabisa. Haki zako kama mlaji zinalindwa kwa ukamilifu chini ya sheria ya madhara. Mtengenezaji ana wajibu wa kukulinda, amevunja wajibu huo na kukusababishia madhara hayo. Tunashauri umshtaki mtengenezaji moja kwa moja ambaye umeweza kumtambua. Mwanasheria wako anaweza kukuongoza zaidi.

## Maunzi laini (Software) mbovu

**Nilinunua maunzi laini ya mahesabu mtandaoni ambayo ina matatizo. Inazidisha faida, na haichukui gharama zote. Maunzi laini hii inaonekana nzuri sana unapoinunua, lakini unagundua dosari unapoanza kuitumia. Faida ilionekana kuongezeka, na nilianza kuwekeza pesa kwenye maeneo mengine, mwishowe nimejikuta kwenye mkwamo kifedha. Nifanye nini?**

*28 Aprili 2014*

Kitu cha kwanza unachotakiwa kukifanya ni kubadilisha maunzi laini hiyo. Tatizo la kununua bidhaa mtandaoni ni kwamba ni ngumu kupima ubora, ni vyema kabla ya kununua kitu ukapata maoni/uzoefu wa watumiaji wengine. Una kesi dhidi ya mtengenezaji na muuzaji wa maunzi laini lakini hatuna uhakika iwapo unaweza kufidiwa kwa kiasi gani. Inategemea na mahala ilikosajiliwa kampuni ya mauzo na iwapo ipo. Tunashauri uwasiliane na wanasheria wako wakusaidie kukufanyia utafiti.

## Bidhaa ya kielektroniki mbovu

**Nilinunua deki ya kuchezea sahani ya muziki (DVD player) kwenye duka moja Kariakoo lakini ilikuwa haifanyi kazi. Niliirudisha lakini waliikataa, ikabidi nilazimishe wanibadilishie kwa kuwa walikuwa wanakataa. Baada ya saa kadhaa ya mabishano, muuzaji alikubali kunibadilishia, lakini nayo siku ya pili tu ilikuwa haifanyi kazi tena. Niirudisha tena lakini safari hii walikataa katakata kuipokea wala kunirudishia fedha yangu. Walinionesha ilani iliyosema kwamba mtu yeyote anayenunua bidhaa anafanya hivyo kwa hatari yake mwenyewe, na kwamba bidhaa ikishanunuliwa hairudishwi wala fedha hazirejeshwi. Rafiki yangu anayejua sheria ananiambia kwamba sharti hilo linaifanya kesi yangu kuwa dhaifu. Nifanye nini? Siyo haki kwa mwenye duka kuchukua fedha yangu wakati mimi sijafaidi deki.**

*5 Mei 2014*

Sheria pekee inayokutetea ni Sheria ya Ushindani ya mwaka 2003 (FCA) ambayo ni sheria inayokuza na kulinda ushindani halali wa biashara, kuwalinda watumiaji dhidi ya masoko ongofu na kuweka masharti mengine yanayohusiana na hayo.

FCA inataka uwepo wa bidhaa bora kama inavyoeleza kwenye kifungu cha 31(1) ambacho kinatamka kwamba iwapo mtu anasambaza, kwa njia ya mauzo au mnada kwa mtumiaji katika mzunguko wa biashara, kutakuwa na sharti lisilo la moja kwa moja kwamba bidhaa inayouzwa kwa mkataba wa mauzo ya bidhaa ni ya ubora unaotakiwa, isipokuwa kwamba hakutakuwa na sharti hilo kwa mujibu wa masharti ya kufungu hiki: (a) kama mteja amepewa angalizo/ameelezwa wazi kuhusu ubovu wa bidhaa kabla ya kuingia mkataba/kununua; au (b) kama mteja mwenyewe amekagua bidhaa kabla ya kuingia mkataba, kwa bidhaa ambazo ubovu wake unaweza kubainika kwa kufanya ukaguzi.

Hivyo, kama ulielezwa juu ya ubovu, au kama ubovu ungegundulika wakati wa ukaguzi wa bidhaa, basi haustahili kulipwa.

Hata hivyo, kwenye suala lako, inaonekana kwamba hukuelezwa jambo hili na usingeweza kujua kama kulikuwa na ubovu.

Zaidi, kifungu cha 35 kinatamka kwamba (1) Iwapo; (a) mtu anauza bidhaa kwa mteja katika mazingira ya kibiashara; na (b) masharti ya sehemu hii yamevunjwa, mteja, kwa masharti ya kifungu hiki, atakuwa na haki ya kusitisha mkataba kwa; (i) kumpatia muuzaji taarifa ya maandishi ikielezea uvunjifu huo; au (b) kurudisha bidhaa kwa muuzaji na kumpatia taarifa ya mdomo au maandishi ikielezea masharti yaliyovunjwa. (2) Iwapo mtumiaji anasitisha mkataba kwa mujibu wa masharti ya kifungu hiki wa mauzo ya bidhaa dhidi ya mtu yeyote, kusitisha huko hakutakuwa halali kama; (a) taarifa haijatolewa au bidhaa hazijarudishwa ndani ya muda mwafaka iwapo mnunuzi alikuwa na nafasi nzuri ya kuzikagua bidhaa; (b) iwapo usitishaji unatokana na taarifa baada ya mteja kupatiwa bidhaa lakini kabla taarifa haijatolewa; (i) bidhaa imeharibiwa na mlaji, imepotezwa au imeharibiwa kwa sababu isiyohusiana na ubovu; (ii) mlaji amesababisha bidhaa kutokufaa kutokana na matumizi au anashindwa kuchukua hatua muhimu kuzuia bidhaa isifae kwa matumizi; au (iii) bidhaa zimeharibiwa kwa matumizi yasiyokuwa ya kawaida. (3) Iwapo mkataba wa mauzo ya bidhaa kwa mlaji umesitishwa na mtu yeyote kwa mujibu wa masharti ya kifungu hiki; (a) iwapo bidhaa imemfikia mlaji kabla ya taarifa ya kusitisha haijamfikia, au amerudishiwa bidhaa, bidhaa itarudi kuwa mali ya muuzaji baada ya kupewa taarifa au kurudisha bidhaa; na (b) mlaji anaweza kurudishiwa pesa na muuzaji la kiasi au thamani ya fedha iliyolipwa au ya bidhaa aliyoitoa. (4) Haki ya kusitisha mkataba iliyotolewa chini ya kifungu hiki ni nyongeza kwa, na haikinzani na haki ya fidia nyingine zinazotolewa chini ya Sheria hii au Sheria nyingine yoyote.

Kutokana na maelezo hapo juu unaweza kuona kwamba, bila kujali masharti ya duka yaliyotumika kukuarifu kwamba hawatakurudishia fedha yako, sheria inaruhusu kurudishiwa na unaweza kulishtaki duka juu ya hili. FCA imeanzisha taasisi imara inayoitwa Tume ya Ushindani (FCC), na ni muhimu kutoa taarifa kwao juu ya bidhaa hizi zisizo na ubora.

Pia unatakiwa uelewe kwamba, masharti yoyote ya jumla ni lazima yasajiliwe FCC. Kifungu cha 36 cha FCA kinatamka kwamba kila vigezo na masharti ambayo yatatumika kuongoza mauzo kwa mlaji yanapotaka kutumika ama kwa jumla au kwa sehemu, katika mkataba wa jumla, vigezo na masharti hivyo ni lazima visajiliwe na Tume kwa mujibu wa kanuni zilizotungwa chini ya Sheria hii.

Hatujaona kanuni mahsusi lakini unaweza kuwasiliana na FCC ili kuona kama ni kweli duka limesajili vigezo na masharti hayo. Yote kwa yote, hatukubaliani na maoni ya rafiki yako, na kwa kusoma kwetu swali lako tunaona kuwa una kesi dhidi ya muuza duka. Mwanasheria wako anaweza kukuongoza zaidi.

## Sijaridhika na mafao ya NSSF

**Nimekuwa mwanachama wa NSSF kwa miaka mingi sasa na sijaridhika na mafao ambayo nitapewa hivi karibuni. Ningepata fedha zaidi kama ningeweka akiba fedha hiyo kwenye akaunti maalum ya benki au kununua dhamana za serikali na hati fungani kutoka Benki Kuu. Hakuna anayehoji kuhusu mafao haya ya NSSF. Wengi wanaangalia fedha waliofanikwa kujitunzia, bila kujua kwamba si NSSF iliyoweka bali ni wao wenyewe na waajiri wao. Nifanye nini kupinga jambo hili?**

*23 Juni 2014*

NSSF inafahamika kama ni mmoja wa mifuko inayofanya vizuri sana kati ya mifuko ya hifadhi ya jamii nchini Tanzania

na tumeshangazwa na malalamiko haya. Hata hivyo, hujatupatia tathmini ya kina ili kutuwezesha kutoa maoni zaidi juu ya iwapo mafao hayo yanatosha ama la.

Kifungu cha 81 cha Sheria ya NSSF kinaeleza yafuatayo: (1) Malalamiko yote kuhusu mafao yataamuliwa kwanza na Mkurugenzi Mkuu. (2) Kama mafao yanatokana na masuala ya kimatibabu, yatapelekwa kwenye bodi ya matibabu kwa ajili ya maamuzi. (3) Kama Mkurugenzi Mkuu au mpewa bima hajaridhika na maamuzi ya bodi ya matibabu, anaweza kupeleka maamuzi hayo kwenye Baraza lililoanzishwa na kifungu cha 84. (4) Maamuzi yote kuhusu madai yatatolewa kwa mlalamikaji kwa njia ya maandishi.

Kifungu cha 83 kinaeleza zaidi kwamba chini ya Sheria ya NSSF inaanzishwa Bodi ya Rufaa ya NSSF ambayo itakuwa na mamlaka ya kusikilia rufaa zinazotoka kwa Mkurugenzi Mkuu kuhusu madai ya mafao yanayotokana na kifungu cha 81.

Kutokana na vifungu hivyo, tunakushauri umwandikie Mkurugenzi Mkuu kuhusu malalamiko yako, na kama hautaridhika na maamuzi yake, unaweza kukata rufaa kwenda kwenye Baraza. Unaweza kabisa kupinga mafao utakayopewa.

## Ufadhili wa masomo Marekani

**Mimi ni mwanafunzi wa kawaida na nilimfuata mtu mmoja nchini ili anisaidie kupata ufadhili wa masomo ya chuo kikuu. Alisema anaweza kunisaidia kupata ufadhili kamili lakini alinitaka nitoe Dola za Marekani 8,000 kama malipo ya awali ili kukidhihirishia chuo kwamba angalau nina fedha kiasi na hivyo kuwashawishi wanifadhili kiasi kilichobaki. Nilitekeleza sharti hilo lakini hadi hivi leo sijasajiliwa wala sijapata ufadhili. Mtu aliyeniahidi anadai bado yupo chuoni anashughulikia suala hilo. Nifanye nini?**

*7 Julai 2014*

Kutokana na maelezo ya hapo juu, inaonesha umetapeliwa. Kupata ufadhili wa chuo kunaamuliwa na ufaulu/alama zako, shughuli nyingine nje ya masomo, wadhamini na kadhalika. Hatuoni uhusiano wa Dola za Marekani 8,000 na kupata ufadhili. Mwakilishi wako anafanya ufadhili uonekane kama kitu kinachonunuliwa dukani. Kimsingi, mtu huyo hahitaji kuwa chuo ili upate ufadhili, na hizi ni dalili kwamba unachezewa. Ili kurudishiwa fedha zako, unaweza kufikiria kumshtaki. Lakini kabla hujafanya hivyo unaweza kufikiria kuchukua hatua za kijinai ambapo anaweza kukurudishia fedha zako.

## Ndege haina choo

**Nilisafiri kutoka Dar es Salaam kwenda Mwanza kwa kutumia ndege ndogo na nilipata matatizo makubwa angani kwa kuwa hakukuwa na choo kwenye ndege. Kwa aibu kubwa, ilinibidi kutumia kopo ili kujisaidia. Je, hakuna sheria inayotaka ndege kuwa na vyoo?**

*14 Julai 2014*

Kifungu cha 3 cha Kanuni za Usafiri wa Anga za mwaka 2006 kinaeleza sharti hilo na kinatamka kwamba (1) Taasisi ambayo kitovu chake cha biashara kipo nchini Tanzania itaruhusiwa kutoa huduma za usafiri wa anga ndani ya Jamhuri ya Muungano au kati ya Jamhuri ya Muungano na nchi nyingine yoyote kama itakidhi vigezo vifuatavyo (a) ina ofisi na vifaa kwa ajili ya mauzo ya tiketi kwenye maeneo inakofanya safari zake; (b) ina ndege za kutosha ili kuendana na ratiba za safari na angalau iwe na ndege mbili; (c) kwa ndege inayofanya safari zake kwa dakika tisini au zaidi, itakuwa na huduma za choo; (d) itakuwa na ratiba iliyoidhinishwa na Mamlaka na itajikita kwenye ratiba hiyo; (e) mara kwa mara itawasilisha taarifa za safari na takwimu nyingine ikiwemo ushuru kuhusiana na safari zake, kama itakavyoelezwa na Mamlaka ya

Anga; (f) iwe na uwezo wa kutoa huduma kwa wateja wanaosafiri au uwezo wa kuajiri kampuni kwa ajili ya kutoa huduma kwa wasafiri katika kila uwanja wa ndege inakofanya shughuli zake.

Umiliki wa ndege hautakuwa kigezo cha kuanzisha ratiba za safari za ndege lakini ndege yoyote itakayotumiwa na mtoa huduma za ndege itatakiwa kusajiliwa nchini Tanzania, isipokuwa kama Mamlaka itaelekeza vinginevyo.

Unaweza kuona kutokana na maelezo hapo juu kwamba kama ilikuwa ni ndege iliyopangiwa kutoa huduma za usafiri, na kama muda wa kuruka ni zaidi ya dakika 90, basi itakuwa ni lazima kwa ndege hiyo kuwa na huduma za vyoo. Unayo haki ya kushtaki na unaweza kutoa taarifa juu ya jambo hili kwenye Mamlaka ya Usafiri wa Anga ambayo inaweza kuchukua hatua stahiki.

## Huduma mbovu ya intaneti

**Ninatumia mtoa huduma za intaneti ambaye hana ufanisi wala haaminiki kabisa. Mara nyingi intaneti haifanyi kazi na inapofanya kazi inakuwa na kasi ndogo sana. Mtoa huduma hutoa sababu nyingi na maneno matamu ili kunihadaa nisimchukulie hatua. Je, ni nani anasimamia watoa huduma za intaneti na kwa nini hachukui hatua?**

*21 Julai 2014*

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) ni chombo cha kisheria chenye dhamana ya kusimamia watoa huduma za intaneti nchini Tanzania.

Pamoja na hiari ya kusitisha makubaliano na mtoa huduma na kumshtaki kwa kukusababishia hasara unayoipata, kuna kanuni zinazoitwa Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Ubora wa Huduma), 2011 ambazo zinadhibiti ubora wa huduma za intaneti, na zinakutaka utoe taarifa juu ya jambo hili kwa TCRA. Huwezi kuilaumu TCRA kama haujatoa taarifa juu ya jambo hili.

Kanuni ya 11 inatamka kwamba mpewa leseni ambaye anatoa huduma za intaneti atatakiwa kufikia malengo ya ubora wa huduma kama ilivyowekwa kwenye Jedwali la Nne la Kanuni hizi. Jedwali la nne linaeleza kwamba kiwango cha mtu kufanikiwa kuingia kwenye intaneti iwapo mtandao wa mtumiaji na mtandao wa intaneti unafanya kazi vizuri, kwa watumiaji wanaotumia intaneti kupitia mitandao ya simu waweze kuunganishwa angalau kwa muda wa asilimia 90; na wale wanaotumia huduma binafsi/kukodi ni lazima waweze kuunganishwa angalau kwa muda wa hadi asilimia 99.

Zaidi, Jedwali la Nne linaeleza kwamba kiasi/kiwango cha uhamishaji taarifa ambacho kinapatikana kwa ajili ya kupakua na kupakia mafaili fulani kati ya tovuti na kompyuta ya mtumiaji kinatakiwa kuwa angalau asilimia 80 ya kile kinachotangazwa na mtoa huduma.

Kipengele kinachowatishia zaidi watoa huduma za intaneti kipo katika kanuni ya 15 ambayo inaeleza kwamba mtu yeyote anayekiuka kifungu chochote cha Kanuni hizi anatenda kosa na kama atakutwa na hatia atawajibika kulipa faini isiyopungua Shilingi milioni 5 au kwenda jela kwa muda wa miezi 3 au vyote kwa pamoja. Tunakushauri upeleke suala hili TCRA ili wasaidie kutatua tatizo la huduma ya intaneti. Utakuwa umegundua kwamba kanuni hizi ni kali sana na zinatoa hadi adhabu ya kifungo kwa mtoa huduma za intaneti ambaye anakiuka kanuni hizi.

## Jumbe nyingi za maandishi kutoka makampuni ya simu

**Kampuni yangu ya simu inanitumia jumbe nyingi za maandishi ambazo hazina maana kwangu. Jumbe hizi zinanipotezea muda wangu na kumaliza chaji ya betri/simu. Ninawezaje kuzuia hili?**

*21 Julai 2014*

Jumbe hizi au hata miito ya simu ambayo hujaomba wakutumie ni batili kwenye sheria zetu. Kanuni ya 7 (1) ya Kanuni za Kielektroniki na Mawasiliano ya Posta (Ulinzi kwa Mtumiaji) zinaeleza kwamba katika kutoa matangazo yoyote kwa lengo la kuitangaza biashara, mpewa leseni atatoa taarifa kwa kuzingatia mipaka ya kijiografia au kiufundi kuhusu uwepo wa huduma kwa watumiaji. (2) mpewa leseni atahakikisha kwamba matangazo (a) hayakiuki ubora wa huduma; (b) hayakinzani na kanuni za ushindani; (c) hayazidi kipindi cha miezi mitatu; (d) yanaweza kuongezwa kwa kipindi cha miezi miwili zaidi kwa idhini ya Mamlaka na baada ya kutekeleza matakwa ya ubora wa huduma. (3) Wakati wa kutangaza bidhaa au huduma, mtoa huduma ataeleza kwa uwazi gharama za jumla za kifurushi pamoja na vigezo na masharti husika. (4) Mtoa huduma hatajihusisha na matangazo kwa njia ya simu, jumbe fupi au njia nyingine za kielektroniki isipokuwa pale: (a) mteja ameridhia huduma; (b) mwanzoni mwa mawasiliano, anaonesha utambulisho wa mtoa huduma au mtu mwingine ambaye yanafanyika kwa niaba na lengo hasa la mawasiliano; (c) mawasiliano hayo yanatoa mchanganuo wa gharama za jumla za bidhaa au huduma husika za mawasiliano.

Kutokana na maelezo hapo juu, unaweza kuona kwamba kutumiwa jumbe nyingi fupi za maandishi bila idhini yako ni kinyume cha sheria na unatakiwa utoe taarifa TCRA ambayo itaweza kuchukua hatua stahiki ambazo ni pamoja na kifungo.

## Ilani kwenye maegesho ya magari

**Ninaendesha gari aina ya Vogue ambayo ninaipenda kama vile ninavyopenda familia yangu. Ninaijali kama ni sehemu ya familia yangu, na ili kuilinda, ninalipa ada kubwa ya maegesho kila mwezi kwenye jengo moja mjini lenye maegesho maalum. Cha kushangaza, mmiliki wa jengo hilo ameweka ilani kila mahali kwenye jengo kwamba "Hawajibiki kwa madhara yoyote" (parking at your own risk) . Inashangaza sana, kwa sababu ninalipa ada kubwa kwa ajili ya maegesho. Je, natakiwa pia kuajiri kampuni ya ulinzi kulinda gari yangu? Sheria inasemaje? Mmiliki anawezaje kujiondoa kwenye wajibu/madhara wakati huo huo anadai fedha nyingi ya maegesho?**

*3 Novemba 2014*

Sheria ya madhara inawataka wamiliki wa majengo kuhakikisha kwamba majengo yao ni salama kwa watu walioalikwa humo. Mmiliki wa jengo ambalo unaegesha gari lako yupo katika biashara ya kukodisha eneo kwa ajili ya maegesho na pia anadai ada kwa kila mtu anayeegesha katika jengo hilo. Hivyo, anawajibika kuchukua hatua zote za kuhakikisha kwamba magari yaliyoegeshwa kwenye eneo lake la biashara ni salama dhidi ya wizi au uharibifu.

Ikiwa magari yataharibiwa au kuibiwa kwa sababu ya uzembe wa mmiliki au mfanyakazi wake, anaweza kuwajibika chini ya sheria ya madhara. Alama/ilani hizo kwamba hawajibiki kwa lolote, hakumuondolei wajibu yakitokea madhara, isipokuwa kama anaweza kuthibitisha kwamba alichukua hatua za kutosha ili kuhakikisha kwamba magari yanakuwa salama na kwamba uharibifu wowote au wizi wa gari au vipuri haukusababishwa na uzembe wake au wa mfanyakazi wake.

Ilani/alama kwamba egesha kwa hasara yako ni za kawaida sana, na zinakuwa ni juhudi za wamiliki wa majengo/maegesho kujaribu kuzuia au kupunguza uwezekano wa wajibu/kutoa fidia huko baadaye. Hata hiyvo alama/ilani hiyo isikuzuie kudai fidia kutoka kwa mmiliki kama ikitokea kitu chochote kimeibwa au kimeharibiwa.

Vivyo hivyo, unaweza kuona alama/ilani kama hizo katika nyumba/kumbi za kufanyia

mazoezi ya viungo, ambapo wamiliki wa kumbi hizo pia wanasema kwamba wale wanaofanya mazoezi katika kumbi zao wanafanya hivyo kwa hasara/hatari yao wenyewe. Kama ilivyoelezewa juu, alama/ ilani hizi ni juhudi tu za kuzuia au kupunguza wajibu.

## Sonara kudanganya uzito wa kito

**Nimekuwa nikinunua vito vya dhahabu kwa miaka mingi kutoka kwa sonara mmoja Dar ambaye mara nyingi hunipa punguzo kubwa. Miezi mitatu iliyopita nilikwenda na nikanunua seti mbili za hereni. Baada ya kuondoka kwa sonara sikuwa na uhakika na uzito wa gramu wa hereni na nikarudi ili kubandikiwa lebo zinazoonesha uzito halisi wa kila hereni. Kwa bahati nzuri au mbaya nilipotea njia na kujikuta kwa sonara mwingine wa jirani yake nikiamini kuwa ndiye ambaye nimetoka kwake. Kwa bahati tu mhudumu/mtu aliyekuwa pale alinipa ushirikiano sana na alikubali kunipimia hereni. Bila kutegemea, uzito ulikuwa mdogo sana kuliko ambavyo mzani wa muuzaji ulinionesha, ikiwa na maana kwamba mzani wake umerekebishwa kuonesha uzito mkubwa makusudi ili kuwadanganya wateja. Nafikiri nimedanganywa na huyu sonara kwa muda wa miaka 10. Kuna sheria yoyote inayosimamia mizani ambayo masonara wanatumia?**

*10 Novemba 2014*

Kuna Sheria maalum - Sheria ya Mizani na Vipimo ambayo inakulinda. Kimsingi, mizani hiyo inapaswa kukaguliwa mara kwa mara na una haki zote za kulitolea taarifa jambo hili kwa Wakala wa Vipimo Tanzania (WMA) ambao watachukua hatua stahiki. WMA wanaweza kumlipisha faini na/au kumfunga sonara huyo. Pia una haki ya kulitolea taarifa polisi kwa ajili ya uchunguzi kwa sababu hili ni suala ambalo wanunuzi wengi wa vito vya dhahabu wanalilalamikia kutoka kwa masonara kama hao. Tabia kama hizi ni za kijinai na zinaadhibiwa kwa kifungo.

## Noti zilizochanika

**Nilipewa noti zilizochanika ambazo benki yangu imekataa kunibadilishia. Nifanyeje, na haki zangu ni zipi?**

*1 Desemba 2014*

Kubadilishiwa noti zilizochanika ni sehemu ya majukumu ya Benki Kuu ya Tanzania. Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania inazungumzia hilo na inaeleza kwenye kifungu cha 29(1) hakuna mtu atakayestahili kubadilishiwa na benki sarafu au noti yoyote iliyopotea, iliyoharibika au isiyokamilika/ yenye dosari au noti iliyokatwa au sarafu iliyochezewa. (2) Bila kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1), Benki inaweza kumpa fedha yenye thamani yoyote mtu ambaye ameleta noti inayozungumziwa kwenye kifungu kidogo cha (1). (3) Mazingira, masharti na mipaka ambayo fedha iliyopotea, kuibiwa au noti isiyokamilika au sarafu iliyoharibika inayoweza kubadilishwa na Benki, itabadilishwa kwa hiari ya Benki husika. (4) Kwa madhumuni ya kifungu hiki, sarafu itachukuliwa kuwa imechezewa iwapo itakuwa imeharibiwa, imedunishwa, au imepunguzwa kwa namna isiyokuwa ya kawaida, au imeharibiwa muonekano wake kwa kupondwa, kuchongwa au kukatwa bila kujali kama ina thamani au la.

Kutokana na maelezo hapo juu, unaweza kuona kwamba ni Benki Kuu ya Tanzania pekee ndiyo yenye mamlaka ya kuamua aina gani ya noti iliyochanika iipokee. Kwa mfano, kama una vipande vyote viwili vya noti, basi Benki Kuu ya Tanzania kwa kawaida inakubali kubadilisha na kwa kawaida hufanya hivyo kwa wakati.

# Sheria za Makampuni na Kibenki, Migogoro ya Wanahisa/Wabia

"

Kumiliki au kuendesha kampuni kunaweza kuibua migongano mingi ya kisheria. Wadai wanaweza kuwa watata, wanahisa kushindwa kuelewana, na uuzaji wa mali za kampuni unaweza kupelekea madeni yasiyotarajiwa. Kwa bahati nzuri, mengi ya matatizo haya yanaweza kuepukika ikiwa viongozi wa makampuni hayo wataelewa haki na wajibu wao na kuweka makubaliano yanayopunguza uwezekano wa kutokea migogoro ya kisheria.

## Kampuni ya mwanahisa mmoja

**Nataka kufungua kampuni kwa jina langu na ninataka kuwa mwanahisa pekee. Je, hilo linaruhusiwa?**

*30 Januari 2012*

Msajili wa Makampuni hawezi kukuruhusu kusajili kampuni chini ya wanahisa wawili. Moja ya vifungu vya Sheria ya Makampuni inasomeka kama ifuatvyo: Ikiwa wakati wowote idadi ya wanachama wa kampuni ikiwa chini ya watu wawili, na ikaendelea kufanya shughuli zake ikiwa hivyo kwa zaidi ya miezi sita, kila mwanachama aliyepo wakati kampuni inafanya kazi baada ya miezi sita huku akijua kampuni inafanya kazi na wanachama chini ya wawili, atawajibika (pamoja na kampuni) kulipa madeni yote ambayo kampuni iliyaingia kipindi hicho.

Mswada wa Marekebisho Mbalimbali ya Sheria za Biashara ya 2011 ni Mswada mpya ambao kwa sasa unajadiliwa na bunge na ukishapitishwa, utaruhusu kampuni kuwa na mwanahisa au mwanachama mmoja. Mabadiliko haya mapya yanasema;

Kampuni ya mwanahisa mmoja itaundwa na mwanachama mmoja. Orodha ya wanachama wa kampuni itajumuisha; (a) jina na anuani ya mwanachama pekee; na (b) utambulisho na maelezo kwamba kampuni ina mwanachama mmoja.

Sheria pia inatamka kwamba kama kampuni itaongeza mwanachama kutoka mmoja kuwa wawili au zaidi, mabadiliko hayo yataingizwa kwenye daftari la kampuni la usajili yakieleza (a) jina na anuani ya mtu ambaye mwanzoni alikuwa mwanachama pekee; (b) maelezo kwamba kampuni imekoma kuwa ya mwanachama mmoja; (c) tarehe ya mabadiliko yalipofanyika.

Marekebisho yanaongeza pia kwamba kampuni au afisa wa kampuni ambaye anakiuka vipengele vya kifungu hiki anatenda kosa na akitiwa hatiani atawajibika kwa faini ya Shilingi milioni tano au kifungo cha miaka miwili au vyote kwa pamoja.

Kama Mswada utapitishwa na bunge, utaweza kusajili kampuni yenye mwanahisa mmoja.

Kwa sasa una hiari ya kusajili jina la biashara kwa kutumia jina lako kama mfanyabiashara binafsi. Hii itakupa fursa kamili ya kusimamia biashara yako.

Kikwazo pekee kwa mfanyabiasha binafsi ni kwamba hana kinga kwa mali zake binafsi, hivyo madai yoyote dhidi ya biashara yake, yanaweza kulipwa kutokana na mali zake binafsi (kama mali za biashara hazitoshi).

## Kununua mali au hisa

**Ninafanya majadiliano na upande unaotaka kuniuzia kampuni fulani ambayo inazalisha bidhaa maarufu. Nikiwa kwenye majadiliano sina hakika kama kipi kina faida kwangu kati ya kununua hisa zote za kampuni au ninunue tu mali za kampuni. Je, hiki ni kitu kimoja?**

*13 Februari 2012*

Uamuzi wako wa kununua hisa za kampuni peke yake au la kwa kiasi kikubwa utategemea na kigezo/zingatio la kodi. Kwa mfano, unaponunua hisa muuzaji ni lazima alipe kodi ya faida ya mtaji na pia kodi ya ushuru wa stempu kwa ajili ya kuhamisha hisa. Lakini pia, unaponunua hisa za kampuni unakuwa mwanachama wa kampuni, kwa hiyo unabeba vyote, mali na madeni ya kampuni.

Hofu kubwa kwa wafanyabiashara wengi ni madhara yatokanayo na kodi. Sheria inairuhusu Mamlaka ya Mapato kukagua mahesabu hadi kwa muda wa miaka mitano ya nyuma. Hii ina maana kwamba baada ya kuichukua kampuni, Mamlaka ya Mapato inaweza kulazimisha kampuni kulipa kodi (ya miaka mitano nyuma), na ukiwa kama mwanachama wa kampuni unaweza kuumia. Kama unataka kununua hisa

za kampuni, inashauriwa kuvipitia vizuri vitabu vya mahesabu vya kampuni na kuvikagua upya ili kuhakikisha kuwa mahesabu yako sawa. Kwenye mkataba wa mauzo ya hisa, unatakiwa pia kuwa na kipengele ambacho muuzaji atawajibika kwako na kwa kampuni katika kufidia malimbikizo ya kodi za miaka ya nyuma lakini yaliyokadiriwa baada ya kuuziana hisa.

Tuje kwenye mauzo ya mali. Hii itakuruhusu kufanya biashara kwa mwavuli wa kampuni yako huku kukiwa hakuna mzigo mkubwa wa kodi. Aina hii ya biashara haihamishi madeni ya kampuni na ni njia inayopendelewa hapa nchini kwa kuchukua mali za kampuni. Hata hivyo kodi ya ongezeko la thamani inaweza kutumika kutegemea na aina ya mali na aina ya biashara unayofanya.

Umesema kampuni inazalisha bidhaa maarufu, basi usisahau kuzijisajilia nembo ya biashara kwa sababu mara nyingi thamani ya bidhaa ipo kwenye nembo kuliko mali zenyewe. Unatakiwa kumuona mkaguzi au mshauri wako wa kodi kwa maelezo zaidi.

## Katiba na waraka/kanuni za kampuni

**Ninafanya kazi na benki yangu na kwa kuwa kiwango cha ukopaji kimeongezeka nimeshauriwa kujisajili na kuwa kampuni, kitu ambacho sipingi. Mhasibu wangu ameniandikia nyaraka kubwa anaiita katiba na kanuni za kampuni. Hiyo katiba na kanuni za kampuni ni nini na inawezaje kusaidia? Kitu gani kingine unachoweza kuniambia kuhusu katiba na kanuni za kampuni?**

*27 Februari 2012*

Tumegundua kuwa ni makampuni machache sana yana katiba na kanuni zao. Makampuni mengi yananakili tu katiba na kanuni zao kutoka kwa waandishi waliowatangulia na kusababisha makosa. Watu wengi hawajui madhara ya uandishi mbovu wa katiba na kanuni za kampuni.

Kwa kuanzia, katiba na kanuni za kampuni ni nyaraka mbili tofauti ingawa zinaonekana kama ni kitu kimoja. Katiba ya kampuni inakuwa na masharti muhimu ambayo kwayo kampuni inaruhusiwa kusajiliwa ambayo imejikita kuelezea maeneo ya utendaji kazi wa kampuni husika. Kampuni haiwezi kufanya chochote kilichopo nje ya katiba yake na hakuna kampuni inayoweza kusajiliwa kabla ya kuwa na katiba. Pia, malengo ya katiba ya kampuni ni kuwawezesha wanahisa pamoja na wakopeshaji wa kampuni kujua mipaka ya shughuli za kampuni. Ni lazima ielezwe kwamba katiba ya kampuni haiwezi kuchukuliwa kwamba inazuia mamlaka ya kampuni iliyopewa chini ya Sheria ya Makampuni au sheria nyinginezo.

Kwa upande mwingine, Kanuni za Kampuni ni nyaraka ambayo kila mwanahisa hawezi kuikanusha na anawajibika kwayo na kwa malengo yake. Kanuni hizi zinabeba kanuni ambazo zinaongoza masuala na shughuli za ndani za kampuni. Kanuni hizi zipo chini ya na zinasimamiwa na katiba ya kampuni ambayo ndiyo nyaraka kuu inayobeba muundo wa jumla wa kampuni. Kama kuna mgongano kati ya katiba na miongozo, katiba inasimama. Hata hivyo kama kuna utata kwenye katiba, kanuni hizi zinaweza kutumika kuondoa utata huo. Kanuni za kampuni kwa kawaida zinaJulaikana kama nyaraka ya biashara na ni lazima itafsiriwe katika namna ambayo inaipa hadhi ya kibiashara. Kanuni hizi huweka masharti au sheria ndogo kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za kampuni.

## Kampuni inakataa kuhamisha hisa za mume wangu

**Mume wangu alikuwa mmiliki wa hisa nyingi zaidi katika kampuni iliyopo Arusha na alifariki mapema mwaka uliopita. Kwenye wosia wake, mimi ni msimamizi wa mirathi na pia ni mnufaika na miezi michache iliyopita nimethibitishwa na Mahakama Kuu Kanda ya Arusha kuwa**

**msimamizi. Nimetumia mirathi hiyo kuhamisha hisa kwa majina yangu, kama wosia unavyosema, lakini kampuni inakataa ikidai kwamba hawakutaarifiwa juu ya hili. Je, nifanyeje?**

*27 Februari 2012*

Tumejitahidi sana kufupisha urefu wa swali lako kwa sababu suala lenyewe liko wazi, na mawazo yako yametufurahisha japo siyo ya msingi kwa sasa.

Sheria ya Makampuni ipo wazi kwamba kuionesha kampuni nyaraka yoyote ambayo kisheria ni ushahidi tosha wa usimamizi wa mirathi ya marehemu ambayo ilitolewa kwa mtu au kwa Wasii ambaye anasimamia mirathi chini ya Sheria ya Kabidhi Wasii Mkuu (Mamlaka na Wajibu) (Sura ya 27) itapokelewa na kampuni kama ushahidi unaojitosheleza juu ya mirathi hiyo isipokuwa kampuni haitawajibika kutoa notisi juu ya hilo bila kujali chochote kutoka kwenye kanuni zake. Kwenye hili, Sheria ya Makampuni inakulinda.

Hujatuambia sababu za wanahisa au wakurugenzi kukataa kuhamisha hisa. Hatuoni kama wana haki hiyo hasa kwa sababu hisa hizo umezirithi kutoka kwa mume wako kupitia wosia.

Kama tabia hiyo itaendelea, mwanasheria wako anaweza kufikiria kulipeleka suala hilo Mahakamani kuwalazimisha wanahisa wengine kutambua uanahisa wako. Kwa sasa inaonesha unaibiwa ndani ya kampuni na tunashauri usichelewe kuchukua hatua zaidi.

## Mwanahisa hajatoa mtaji wa kampuni

**Tulisajili kampuni ambapo kila mwanahisa kati ya watu wanne alitakiwa kuweka Shilingi milioni 10 kwenye mtaji wa kampuni. Wakati sisi watatu tayari tumekwishalipia sehemu ya mtaji wa kampuni na hisa, mwanahisa wa nne anakataa kulipa anasema eti hana pesa. Alitudokeza kwamba kisheria kama kampuni imesajiliwa yeye tayari anakuwa ni mwanahisa. Inaonekana anataka kuwa mwanahisa bila kulipia hisa. Tufanyeje?**

*5 Machi 2012*

Kwa kanuni nyingi za kampuni hasa kama mmechukua zile za kwenye Jedwali la Kwanza la Sheria ya Makampuni ya Tanzania, kifungu kifuatacho kinasomeka; kampuni itakuwa na umiliki wa mwanzo/chini na wa juu kwenye kila hisa (ikiwa si hisa isiyolipwa kamili/taslimu) kwa pesa zote (kama zimelipwa sasa hivi au la) zilizotakiwa au zilizolipwa kwa muda maalum uliowekwa kuhusiana na hisa; lakini wakurugenzi wanaweza wakati wowote kutangaza kwamba hisa yoyote ama yote au sehemu yake imesamehewa kwa masharti ya kanuni hii. Umiliki wa kampuni, kama upo, juu ya hisa utahusu kwenye kiasi chochote kilicholipwa kuhusiana nayo.

Sheria pia inaeleza kampuni inaweza kuuza, kwa namna ambayo wakurugenzi wameamua, hisa zozote zinazomilikiwa na kampuni ikiwa kiasi kuhusiana na umiliki kinalipwa sasa hivi na hakilipwi ndani ya siku kumi na nne zilizo wazi baada ya taarifa kwa maandishi kupewa mwenyehisa, au mtu anayestahiki kupewa kutokana na sababu ya kifo cha au kufilisika kwa mmiliki, kudai malipo na kueleza kwamba iwapo taarifa haikutekelezwa hisa zinaweza kuuzwa.

Ili kutekeleza uuzaji huo wakurugenzi wanaweza kumuidhinisha mtu kuhaulisha hisa alizouziwa, au kwa mujibu wa maelekezo ya mnunuzi wa hisa hizo. Mnunuzi atasajiliwa kama mmiliki wa hisa zilizomo katika uhaulishaji huo, na hatazuiwa kuona maombi ya pesa za kununulia, wala jina lake katika hisa halitaathiriwa na upungufu au kutofaa katika mwenendo kuhusiana na mauzo.

Mapato halisi ya mauzo yatapokewa na kampuni na kutumika katika malipo ya sehemu ya kiasi hicho kuhusiana na umiliki uliopo kama ambavyo yanalipwa, na

bakaa/bakaya, kama ipo, italipwa (baada ya kuwasilisha hati ya hisa zilizouzwa kwenye kampuni kwa ajili ya kufutwa kwa kuzingatia umiliki kama huo kwa kiasi ambacho hakilipwi sasa hivi kama ilivyokuwa kwenye hisa kabla ya mauzo) kwa mtu anayestahiki kumiliki hisa, katika tarehe ya mauzo.

Kutokana na yaliyoelezwa hapo juu, ni wazi kuwa kampuni ina umiliki kwenye hisa ambazo hazijanunuliwa. Kwa hiyo mnaweza kuitisha mkutano wa bodi na kuhamisha au kuuza hisa hizo. Mwanahisa wa nne hawezi kumiliki kitu ambacho hajakilipia. Hii ndiyo kanuni muhimu inayotumika hapa.

## Mgogoro na wanahisa wenzangu

**Tulianzisha kampuni ambayo kwa sasa ndiyo kinara hapa Tanzania. Mwanzoni tulikuwa wanahisa wawili, lakini baadaye kila mmoja wetu alimuongeza mwanae na hivyo tuko wanne. Tuna mgogoro kwenye kampuni ambapo mmoja wa wanahisa wa mwanzo ni mzee sana na anakataa kuingia mkataba wa mauzo wenye faida kubwa. Hata mwanae hakubaliani naye. Tunawezaje kutatua jambo hili? Tufanye nini ili kuhakikisha kwamba hatuingii kwenye matizo haya siku za usoni?**

*28 Mei 2012*

28 Mei 2012

Ni bahati mbaya sana mnaingia kwenye hali hii baada ya kutengeneza kampuni yenye mafanikio makubwa. Nyinyi siyo peke yenu ambao mnakumbana na matatizo kama haya. Makampuni mengi Afrika Mashariki yana matatizo kama hayo. Makampuni yanasahau utofauti uliopo kati ya usimamizi na utawala. Makapuni mengi pia hayaelewi umuhimu wa kutenganisha akaunti zao binafsi na zile za makampuni. Kuchukua fedha kwenye mali au kuchukua pesa taslimu ni hatari sana na imezoeleka sana mitaani. Makampuni kadiri yanavyokua ndivyo yanavyojikuta kwenye matatizo mbali mbali siku za usoni.

Umetuuliza maswali mawili. Tunaanza kwanza kujibu swali la pili kwa sababu hatuna taarifa za kutosha kukuongoza kuhusu swali la kwanza. Swali la pili, ni nini mngefanya ambacho kingewasaidia kuwaepusha na hali kama hiyo?

Pamoja na kuhakikisha kwamba mnakuwa na usimamizi na uongozi mzuri, ni muhimu sana kwa wanahisa wa kampuni kuingia mkataba. Mkataba wa wanahisa ni makubaliano kati ya wanahisa wa kampuni ambao unaongezea na wakati mwingine kupunguza matumizi fulani ya vifungu vya Katiba na Kanuni za Kampuni (MEMARTS). Zipo sababu nyingi za kwa nini mnatakiwa kuingia kwenye mkataba huo. Moja, mkataba wa wanahisa ni nyaraka binafsi na hivyo haiwezi kukaguliwa na umma kama Katiba na Kanuni za Kampuni. Ni rahisi sana kuurekebisha mkataba wakati wowote kuliko kurekebisha Katiba na Kanuni za Kampuni. Mkataba wa wanahisa pia unaweza kuongeza au kutoa hatua za kuwalinda wanahisa wenye hisa kidogo kwenye kampuni.

Mkataba wa wanahisa pamoja na vipengele vingine unakuwa na mambo yafuatayo; lini na nani mwanahisa anaweza kumuuzia hisa zake, ni idadi gani ya wanahisa wanatakiwa kukubaliana ili wazo liweze kupitishwa (kwa yale mambo ambayo yanatakiwa kufanywa na wanahisa), haki za pamoja, yaani, kama wanahisa wakubwa wanataka kuuza hisa zao, mwanahisa aliyesalia naye ni lazima auze hisa zake bila kujali anapenda ama la. Kunaweza pia kuwa na kipengele cha namna ya kuteua menejimenti, uteuzi wa wakaguzi pamoja na kipengele cha usuluhishi, ambapo mwanahisa anajua wazi nini cha kufanya na wapi pa kwenda kama mgogoro ukiibuka.

Wakati wote inashauriwa kwamba mkataba wa wanahisa uwepo wakati wa usajili wa kampuni ili kuepusha migogoro

kutokea. Kwa bahati mbaya makampuni mengi ya wazawa hayana mikataba ya aina hiyo, na hivyo kupelekea kuwa katika hatari ya mogogoro baina ya wanahisa.

Kuhusu haki zenu, tunahitaji kujua asilimia za umiliki wenu, iwapo mkataba wa wanahisa upo, nani anasimamia kampuni na kivipi "dili" hilo linavyoweza kuinufaisha kampuni na wanahisa wake. Tunawashauri mpate ushauri wa wanasheria wenu ambao wanaweza kuwaongoza baada ya kuona hali halisi na kupitia nyaraka.

## Kulinda siri za kampuni

**Kuna kampuni fulani najadiliana nayo ili inunue kampuni yangu. Bado hatujaafikiana juu ya masharti ya mkataba lakini wanahitaji kuangalia vitabu vyangu ili kujua najiendeshaje. Nini kitatokea kama wakikataa kuinunua baada ya kujua siri zangu zote? Ninawezaje kujilinda na hili?**

*4 Juni 2012*

Hili ni swali la kuvutia sana na linawaacha njia panda wakurugenzi wengi wa makampuni. Unawezaje kuweka usawa kati ya kutoa taarifa zako nyingi na usiweze kuingia mkataba kwa kushindwa kubadilika na kupelekea wateja kukasirika.

Njia ya kawaida kabisa ya kujilinda ni kupitia kuingia mkataba wa usiri, wakati mwingine unaJulaikana kama mkataba wa kutokutoa siri. Katika utaratibu kama huo, utawapatia taarifa ambazo hawawezi kuzitumia kwa namna yoyote ile ikiwemo kushindana na wewe.

Mkataba wa usiri kwa kawaida hutiwa saini katika hatua za awali za majadiliano kwa mfano, kabla ya mnunuzi mtarajiwa kuruhusiwa kuangalia taarifa za muuzaji au vinginevyo kupewa taarifa za siri. Mkataba huu ni kipaumbele chako kama muuzaji kwa kuwa kinahusu usiri juu ya biashara yenyewe lakini pia kinahusu kutoa taarifa nyeti kuhusu biashara yako.

Kwenye kuandika mkataba huu hakikisha neno "siri/taarifa za siri" linatafsiriwa kwa upana na kwamba mkataba unaeleza mazingira machache tu ambayo taarifa hizo za siri zinaweza kutumika. Mpokeaji wa taarifa anaweza kuomba kuondolewa ulinzi baadhi ya taarifa, kwa mfano taarifa ambazo tayari anazo, taarifa ambazo zipo kwa umma tofauti na zile ambazo zimesambaa kutokana na kuvuja kwa mkataba wa mpokeaji; pamoja na taarifa ambazo zimetafutwa/kuandaliwa na mpokeaji kivyake. Tatizo linalokuja ni kwamba kama utadai zimevuja, utajuaje kwamba taarifa fulani mnunuzi alikuwa nazo kabla ya kuanza majadiliano.

Wakati wote kuna ukomo wa katazo la kutotoa taarifa za siri pale zinapohitajika kisheria au kwa amri ya Mahakama, isipokuwa kwamba mwombaji wa taarifa hizo lazima ampatie mtu anayetakiwa kutoa taarifa hizo notisi mapema.

Kama upande unaotoa taarifa, unaweza kutaka kuwepo na makubaliano na mpokeaji ambapo atakuwa tayari kuwajibika kwa uvunjifu wa makubaliano hayo au kwa mwakilishi wake (wakiwemo maafisa, wakurugenzi, waajiliwa, wafanyakazi, wakopeshaji, wanasheria na washauri wa kifedha). Unaweza pia kuweka ukomo wa kupata taarifa za siri kwa kundi la watu wachache wa mnunuzi au wawakilishi wake ambao wanahitaji kujua taarifa hizo, na taarifa wanazopewa hawatakiwi kuzisambaza kwa wawakilishi wao wengine isipokuwa kama wawakilishi hao watakuwa tayari kubanwa na masharti ya mkataba wa siri.

Kipengele kingine ambacho kwa kawaida kinakuwepo kwenye makubaliano ya namna hiyo ni cha wewe kudai kurudishiwa au kuharibiwa kwa taarifa hizo za siri baada ya kumalizika kwa majadiliano. Wakati mnunuzi anapofanya upembuzi wa kina, mnunuzi anakutana na wafanyakazi wako muhimu na

hivyo kunatakiwa kuwa na kipengele kwenye mkataba ambacho kitamzuia mnunuzi kuwashawishi au kuwaajiri wafanyakazi wako kwa kipindi fulani. Ujanja ni wewe kuomba kiasi fulani cha pesa ambacho hakitarudishwa kama makubaliano yakishindikana. Mwanasheria wako anaweza kukuongoza zaidi.

## Malengo ya ahadi na hakikisho

**Nimeingia mkataba wa mauzo ya mali na inaonekana kama kuna utofauti tangu wakati natia saini na kukamilisha mkataba. Kwa nini kuonekane kuna tofauti? Pia kuna ahadi na mahakikisho mengi ambayo mnunuzi wa kampuni yangu ameingiza kwenye mkataba. Nifanye nini?**

*4 Juni 2012*

Kusaini mkataba ni pale unapoweka kalamu yako kwenye karatasi. Kukamilisha ni pale shughuli yenyewe inapokuwa imeanza na inaweza kuwa na masharti kadhaa. Hii ni kawaida kwenye mikataba hasa ile ambayo inahusu mali nyingi. Huna haja ya kuhofu juu ya hilo.

Kuhusu ahadi na hakikisho, vipengele hivi vinampa mnunuzi kuona kupitia ratiba ya muuzaji, maelezo yanayotakiwa na yasiyotakiwa kwenye ahadi na hakikisho ambapo mnunuzi anapima matokeo ya uchunguzi wake alioufanya. Pia huunda masharti ya kukamilisha kwa sababu usahihi wa ahadi na hakikisho la muuzaji ndiyo yatakuwa masharti ya mnunuzi kuendelea na biashara na kinyume chake. Zaidi, ahadi na hakikisho vinaunda msingi wa fidia ya madai kama mnunuzi anaweza kuthibitisha kwamba ahadi na masharti haya kuwa ya kweli. Ni vizuri ukasoma kila leno hasa kwa sababu yameandaliwa na mnunuzi.

Kukosekana kwa usahihi wowote kwenye ahadi na hakikisho wakati wa kutia saini na kukamilisha vinaweza kuupa upande mwingine haki ya kutokuendelea na biashara, kuacha dili, kushtaki na kudai fidia. Kama shughuli inahusisha mwanya kati ya kusaini na kufunga, mnunuzi atahitaji kwamba ahadi na hakikisho la muuzaji vilivyotolewa wakati wa kutia saini viletwe wakati wa kukamilisha. Inashauriwa sana kwamba mwanasheria wako ahusishwe ili kukuongoza kwenye hili.

## Kampuni kumiliki hisa kwenye kampuni nyingine

**Iwapo naunda kampuni mpya, je ninahitaji kuwa na watu wa kawaida kuwa wanahisa au kampuni nyingine inaweza kuwa mwanahisa pia? Nani watakuwa wakurugenzi?**

*2 Julai 2012*

Kampuni inaweza kuwa mwanahisa wa kampuni nyingine bila kizuizi chochote. Kampuni yenye hisa itakuwa na sifa za kuteua idadi ya wakurugenzi kwenye kampuni mpya ambayo utaiunda. Sheria kama ilivyo sasa, inakutaka angalau uwe na wanahisa wawili kwenye kampuni mpya.

## Kubadili biashara kutoka binafsi kwenda kampuni yenye dhima ya ukomo

**Nimekuwa wakala wa bidhaa za kimataifa za Ulaya kwa miaka 25 hadi hivi karibuni nilipoambiwa nibadilishe biashara hii na kuwa kampuni yenye dhima ya ukomo. Hii ni kwa lengo la kuendeleza biashara. Nilitekeleza na sasa kampuni ina bodi ya wakurugenzi na wanahisa. Miaka michache tangu nifanye mabadiliko hayo, kampuni yangu imeshtakiwa, na wanahisa wake pia wameshtakiwa. Kuna haja gani ya kuwa na kampuni yenye dhima ya ukomo kama wanahisa wake nao pia wanaweza kushtakiwa? Nifanye nini?**

*10 Desemba 2012*

Huwezi kumzuia mtu kumshtaki mtu

mwingine. Ni suala la Mahakama kuamua kama shtaka hilo lina mashiko au la. Hata hivyo, kwenye kesi ya zamani ya Kiingereza ya Solomon dhidi ya Solomon ambayo bado ni sheria nzuri hata sasa, kampuni yenye dhima ya ukomo ni taasisi inayojitegemea dhidi ya wanahisa wake. Hii ina maana kwamba, kampuni inaweza kushtaki na wala siyo wanahisa wanaoweza kushtaki ama kushtakiwa. Wanahisa hawawajibiki kwa madeni ya kampuni hata kama wanamiliki kampuni. Hii ndiyo sababu mtu anaunda kampuni yenye dhima ya ukomo. Matokeo ya maamuzi ya Mahakama kwenye kesi ya Solomon dhidi ya Solomon ilikuwa ni kuimarisha dhana ya kampuni kuwa ni taasisi inayojitegemea kama ilivyoelezwa kwenye Sheria ya Makampuni. Hivyo, wadai wa kampuni iliyofilisika hawawezi kuwashtaki wanahisa wa kampuni kwa madeni ambayo kampuni inadaiwa.

Ingawa hujatuambia ni aina gani ya kesi iliyofunguliwa dhidi ya kampuni yako, kanuni hizo hapo juu zina uwezekano mkubwa wa kukupendelea. Mwanasheria wako anaweza kukuongoza zaidi.

## Kuhamisha hisa

**Nilihamisha hisa zangu za kampuni kwenda kwa mtu mwingine kwa kusaini mkataba na kumkabidhi cheti cha hisa. Mnunuzi ananiambia kwamba nilitakiwa kusaini karatasi nyingine. Je, hii ni kweli? Saini yangu ni ghali na nataka kumtoza fedha zaidi kwa kusaini karatasi hizi, mnaweza kunisaidia?**

*11 Februari 2013*

Uhamisho wa hisa unatambulika kisheria pale tu kodi husika zinapolipwa. Hivyo, kusaini tu mkataba na kukabidhi cheti cha hisa hakuna maana yoyote. Tutaelezea mchakato wa uhamisho wa hisa hapa chini. Unapaswa kuwasilisha kwa Mamlaka ya Mapato taarifa za fedha za miaka mitatu iliyopita za kampuni ambayo hisa zake unataka kuzihamisha kwa ajili ya makadirio ya thamani ya hisa. Ukipata thamani ya hisa utawasilisha mkataba wa mauziano ya hisa na fomu ya kuhamisha hisa ikiambatana na cheti cha usajili wa kampuni ambayo hisa zake zinahamishwa, Katiba ya Kampuni, Kanuni za Kampuni pamoja na cheti cha namba ya utambulisho wa mlipa kodi. Mamlaka ya Mapato itakadiria kodi ya faida ya mtaji inayolipwa kwa kuzingatia tofauti kati ya bei uliyonunulia hisa na bei unayouzia (au thamani ya soko, yoyote kubwa). Muuzaji anawajibika kulipa kodi ya faida ya mtaji wakati mnunuzi analipa kodi ya ushuru wa stempu. Katika hatua hii ndipo hisa zinahamishwa.

Kwa upande wako, inaonekana kama umelipwa fedha ya manunuzi na umesaini mkataba wa kuuziana hisa. Hivyo kuna uwezekano mkubwa kwamba hujalipa kodi ya faida ya mtaji, ikiwa na maana kwamba, hisa bado zipo mkononi mwako. Kabla hujapata mawazo ya kufurahisha, tafadhali chukua taarifa kwamba kwa kuwa tayari umekwishapokea fedha ya manunuzi hakuna uwezekano wa kulipwa zaidi. Kimsingi kama hujasaini fomu za kuhamisha hisa, mnunuzi ana kesi dhidi yako na anaweza kupeleka maombi Mahakamani kukutaka utekeleze, yaani usaini fomu ya uhamisho wa hisa. Saini yako ya thamani inaweza kubadilika na kuwa na thamani zaidi kama muuzaji akiamua kupeleka maombi Mahakamani. Kama malipo ya fedha yapo sawa, unashauriwa ama kusaini fomu ya hamisho la hisa au kutafuta msaada wa mwanasheria au kufanya vyote.

## Benki inanisumbua sana

**Nimekopa fedha benki na nimeweka moja ya majengo yangu dhamana. Kila wakati ninapotaka kufanya chochote kwenye jengo benki inasema kuwa ni lazima nipate idhini yao. Ninapotafuta idhini, hawanijibu kwa wakati. Kimsingi, Mkurugenzi Mtendaji**

**kila wakati anasafiri na naambiwa ni yeye pekee anayepaswa kutoa idhini. Hii inaumiza biashara yangu. Kwa rekodi hiyo, safari hii nilipotaka kupanua sehemu ya nyuma ya jengo, niliiandikia benki na baada ya kusubiri siku 21 bila jibu, niliendelea kujenga. Benki hiyo sasa imeniandikia kuwa nimevunja masharti ya mkopo na wanakusudia kuitisha deni lote kwa mkupuo mmoja. Nifanye nini? Kuna wakati benki iliniambia nisipake jengo langu rangi fulani kwa kuwa itapunguza thamani ya dhamana na hivyo dhamana itaathirika! Ninawezaje kuepukana na kero hii?**

*18 Februari 2013*

Inawezekana hati ya mkopo inakutaka kupata idhini ya benki kwa upanuzi au marekebisho au kitu kingine kinachoathiri dhamana. Hata hivyo, ni sharti la kawaida kibiashara kwamba idhini hiyo isicheleweshwe au kuzuiwa kwa muombaji bila sababu za msingi, na hivyo, kuchelewesha huko kunakupa haki ya kushtaki. Kuhusu suala la kuitisha mkopo, tunaamini benki haiwezi kuitisha mkopo wote. Kimsingi, ujenzi na upanuzi wa jengo unaongeza thamani ya dhamana na ni kwa maslahi bora ya benki. Unaweza kuwasiliana na mwanasheria wako ambaye atakuongoza zaidi.

Kuhusu rangi ya jengo lako, hii ni hiari yako na hakuna namna benki yako inaweza kukuamrisha kufanya hilo kwenye hati ya mkopo. Kwa uzoefu wetu kwenye masuala ya benki nchini Tanzania, hii ni mara yetu ya kwanza kusikia benki inafanya vitendo vya namna hiyo. Kuhusu ni vipi utaepukana na kero hii, ushauri rahisi, ni kubadilisha benki kwa sababu hakuna uhaba wa benki nchini Tanzania. Kama una mzunguko mzuri wa fedha na dhamana nzuri, benki za Tanzania zinatafuta wateja kama wewe.

## Benki za nje nchini Tanzania

**Miaka kadhaa iliyopita maafisa wa mabenki kutoka nje waliniita ili kuonana nao jijini Dar es Salaam. Niliona hilo ni jambo la kushangaza kwa sababu maafisa hao wanatoka benki kubwa duniani ambazo ati hazina ofisi nchini Tanzania. Hata hivyo, nilionana na mmojawao ambaye alinionesha huduma mbalimbali wanazotoa Ulaya, kuanzia akaunti za muda maalum mpaka huduma za fedha za kigeni. Je, hii ni halali?**

*24 Juni 2013*

Kuna masuala na maswali kadhaa ya kufurahisha umeyaibua. Tunaanza na lililo jepesi. Benki hizi za kigeni, chini ya sheria ilizozisajili, zinaruhusiwa kufungua akaunti na kutoa huduma kwa raia wa kigeni. Hii ina maana kwamba kwenye nchi zao ofa waliyokuwa wanakupa ni halali. Hata hivyo, kwako wewe, tuchukulie wewe ni raia wa Tanzania, kuna vikwazo chini ya sheria zetu za kubadilisha fedha.

Kwa mfano, kuna ukomo wa kiasi cha fedha za kigeni unachoweza kubeba unapoondoka nchini. Hizi ni sheria zinazolinda ili kuhakikisha kwamba fedha yetu, kutokana na uchumi mdogo ukilinganisha na nchi zenye nguvu za viwanda, haziathiriki. Kuhusu iwapo unaweza kufungua akaunti nje ya nchi, jibu ni ndiyo lakini ni mpaka Benki Kuu ikuruhusu. Hili liko wazi kwenye Waraka wa Fedha za Kigeni wa mwaka 1998 ambapo ufunguaji wa akaunti nje ya nchi au uhamishaji wa fedha nje ya nchi ni moja ya shughuli zilizozuiliwa na zinahitaji idhini ya Benki Kuu ya Tanzania. Hivyo ili uweze kufungua akaunti nje ya nchi, itakulazimu kupata idhini ya Benki Kuu, na idhini hiyo haitolewi kirahisi isipokuwa kama utatoa sababu za msingi.

Pia tunataka kukuJulaisha kwamba chini ya sheria yetu ya utakatishaji fedha haramu, utakatishaji fedha umetafsiriwa kwa upana sana kuwa ni kitendo cha mtu au watu kujihusisha moja kwa moja au kwa njia nyingine katika kubadili, kuhamisha, kuficha,

kupoteza chanzo, kutumia au kujipatia fedha au mali inayoaminika kupatikana kwa njia haramu na vitendo hivyo vina lengo la kukwepa madhara ya kisheria yatokanayo na vitendo hivyo ikiwemo makosa yaliyoainishwa katika kifungu cha 12.

Afisa wa benki pamoja na wewe nyote mnaweza kushtakiwa chini ya sheria hii kama fedha zenu zitaJulaikana kwamba hazijatozwa kodi au kwa ujumla tuseme "fedha chafu." Kama mtatiwa hatiani mnaweza kufungwa, kwa hiyo chukua tahadhari. Wanasheria wako wanaweza kukuongoza zaidi.

## Kubadili jina la kampuni

**Mimi ni mmoja wa wamiliki wa kampuni ambayo haifanyi vizuri sana. Niliwasiliana na kiongozi wa kiroho ambaye aliniambia kwamba tunahitaji kubadilisha jina la kampuni. Mbia mwingine mwenye 50% hakubaliani na hili. Taratibu za kubadili jina zikoje? Je, ninaweza kubadili jina peke yangu kwa sababu mimi ndiyo mwendeshaji? Jina jipya ninalotaka kujiandikisha ni sawa na jina la kampuni nyingine. Nifanye nini?**

*22 Julai 2013*

Hilo limezungumziwa kwenye-kifungu cha 31 cha Sheria ya Makampuni ambacho kinasema (1) Kampuni inaweza kwa azimio maalumu na kwa idhini ya maandishi ya Msajili kubadilisha jina lake. Kama Msajili atakataa kutoa idhini, atatoa sababu. (2) Kama kwa bahati mbaya ama la, Kampuni kwenye usajili wake wa kwanza au wakati wa kusajili jina jipya, kama Msajili ataona kwamba jina ambalo kampuni imesajiliwa nalo linafanana sana na jina jingine ambalo limesajiliwa, kampuni hiyo ya kwanza inaweza kubadilisha jina lake kwa idhini ya Msajili, na kama akielekeza hivyo, ndani ya miezi sita tangu kusajiliwa kwa jina hilo, itabadilisha ndani ya muda wa wiki sita tangu siku ya maelekezo au kwa kipindi kirefu zaidi kama Msajili ataona inafaa kuruhusu. (3) Kama kampuni itabadilisha jina lake chini ya kifungu hiki, itampatia notisi Msajili ndani ya siku 14 na Msajili kwa kuzingatia masharti ya kifungu 30 (2) ataingiza jina jipya kwenye orodha ya usajili katika nafasi ya jina la zamani, na atatoa taarifa ya mabadiliko hayo kwenye Gazeti la Serikali; hati ya usajili ya mabadiliko kulingana na hali, na mabadiliko ya jina yataanza kutumika kutoka tarehe ambayo hati ya mabadiliko imetolewa. (4) Mabadiliko ya jina la kampuni chini ya kifungu hiki hayaathiri haki yoyote au wajibu wowote wa kampuni, au kuathiri taratibu zozote za kisheria kwake au dhidi yake; na taratibu zozote za kisheria ambazo zinaweza kuendelea au kuanza dhidi yake kwa jina lake la zamani zinaweza kuendelea au kuanzwa dhidi yake kwa jina lake jipya.

Kutokana na maelezo hapo juu, unahitaji azimio maalum kubadilisha jina ikiwa na maana kwamba hili ni suala la wanahisa, wewe peke yako huwezi kubadilisha jina. Wanasheria wako wanaweza kukuongoza zaidi.

## Waraka/Kanuni za jumla za kampuni

**Kama nina mahusiano ya kibiashara na kampuni ya uzalishaji lakini waraka/kanuni zake zinabainisha kuwa kampuni ina uwezo wa kujishughulisha na kila kitu, je waraka huo ni halali?**

*19 Agosti 2013*

Sheria ya Makampuni inatamka kwamba iwapo kanuni/waraka wa kampuni unaeleza kwamba madhumuni ya kampuni ni kuendesha biashara kama kampuni ya kibiashara kiujumla (a) lengo la kampuni ni kuendesha biashara yoyote au kufanya shughuli yoyote; na (b) kampuni ina uwezo wa kufanya mambo yote ambayo ni muafaka au mazuri kwa ajili ya kuendesha biashara au

shughuli yoyote. Kutokana na maelezo hapo juu, ni halali kwa waraka kuwa na malengo ya jumla. Hata hivyo, unaweza kuwasiliana na wanasheria wako kwa mwongozo zaidi.

## Sheria ya kipekee ya bima

**Ninamiliki 15% ya kampuni ya bima Tanzania. Maswali yangu ni matatu. Je, kuna hitaji maalum kwamba wanahisa peke yao hawawezi kuwateua wakurugenzi kwenye kampuni ya bima? Kama nitaamua kuuza hisa zangu ninahitaji kupata idhini ya Kamishna wa Bima? Ninayaona haya yote kuwa ni ya kipekee na ni kinyume na kanuni za soko huria. Kama idhini inatakiwa, je inachukua muda gani kupata?**

*7 Oktoba 2013*

Majibu ya maswali yako mawili ya kwanza ni ndiyo. Sheria ya Bima inatamka wazi kwamba kampuni ya bima itamridhisha Kamishna kwamba theluthi ya wakurugenzi wake ni wakurugenzi wasio washiriki. Sheria pia ina mtafsiri "mkurugenzi asiye mshiriki" kuwa ni mtu ambaye (a) anamiliki hisa asilimia 25 au zaidi kwenye kampuni ya bima; (b) ameajiriwa na kampuni au kampuni shiriki; au (c) ni mkurugenzi au anamiliki asilimia 25 ya hisa kwenye kampuni shiriki. Hivyo kwenye kesi ya kampuni yako, theluthi ya wakurugenzi walioteuliwa hawatakiwi kuwa washiriki. Sababu za kuwa na wakurugenzi wanaojitegemea ni kuhakikisha kwamba uendeshaji wa shughuli hauathiriwi na mgongano wa maslahi.

Sheri ya Bima pia inatamka kwamba uhamishaji wa umiliki wa hisa za bima unaohusisha asilimia kumi ya hisa za kura, muunganisho, kugawa au mpangilio mwingine wa aina hiyo utakuwa ni kwa idhini ya maandishi ya Kamishna. Kamishna anaweza, kama sharti la kutoa idhini, kutaka marekebisho yafanyike kuhusiana na mchakato wa uhamishaji, uuzaji, uunganishaji, ugawaji au mpangilio mwingine wa aina hiyo. Kamishna anaweza, kwa maandishi, kuhitaji taarifa kama zitakuwa ni muhimu kwa muombaji kuzipeleka wakati anafanya maombi ya idhini.

Hatuna uhakika ni kitu gani unakiona kuwa ni cha kipekee kwenye Sheria ya Bima. Unaelewa kwamba bima ni biashara inayosimamiwa karibu sehemu zote za ulimwengu, na vifungu vya namna hiyo kwenye sheria ya bima ni vya kawaida. Kujificha nyuma ya kanuni za soko huria hakumaanishi kwamba sekta hii isisimamiwe. Mamlaka ya Usimamizi wa Bima, ni taasisi ya kisheria inayosimamia biashara ya bima, inasifika kwa kuwa na ufanisi, imejipanga na hutoa maamuzi yake kwa haraka. Wanasheria wako wanaweza kukuongoza zaidi.

## Kupunguza mtaji wa hisa

**Kampuni yetu iliingia mikataba fulani ya uchimbaji madini ambayo sasa imefikia kikomo. Tunakusudia kupunguza mtaji wa hisa kwa sababu tumepunguza uzalishaji/shughuli. Je, sheria za Tanzania zinaruhusu hilo na tunawezaje kulifanikisha?**

*6 Januari 2014*

Sheria ya Makampuni ina kifungu maalum juu ya jambo hili. Kifungu cha 69 kinatamka kwamba (1) kampuni yenye ukomo wa hisa au kampuni yenye ukomo wa dhamana na yenye mtaji wa hisa inaweza, ikiwa imeidhinishwa na waraka/kanuni zake na kwa masharti yaliyomo humu, kwa azimio maalumu kupunguza mtaji wake wa hisa kwa namna yoyote, na hasa, inaweza: (a) kufuta au kupunguza dhima kwenye hisa zake zozote kuhusiana na mtaji wa hisa ambao haukulipiwa; au (b) ama kwa kufuta au bila ya kufuta au kupunguza dhima ya hisa zake zozote, kufuta mtaji wa hisa wowote ambao umepotezwa au usiowakilishwa na mali zilizopo; au (c) ama kwa kufuta au

bila ya kufuta au kupunguza dhima ya hisa zake zozote, kuilipa hisa yoyote iliyolipwa ambayo ni zaidi ya mahitaji ya kampuni; na inaweza, ikiwa kama ni lazima, kubadilisha katiba yake kwa kupunguza kiasi cha mtaji wake wa hisa na hisa zake ipasavyo. (2) Taarifa inayotolewa ya nia ya kupendekeza azimio maalumu la kupunguza mtaji wa hisa wa kampuni itakuwa imeambatanishwa na hati ya mkurugenzi inayoonesha kampuni kujimudu kiuchumi/kuweza kulipa madeni, iliyotolewa kwa mujibu wa kifungu cha 70 na, ikiwa inafaa, ripoti ya wakaguzi wa hesabu iliyoandaliwa kwa ujibu wa kifungu cha 70. (3) Bila ya kuathiri kifungu cha 71, azimio maalumu lilipopitishwa kupunguza mtaji wa hisa wa kampuni halitatumika mpaka baada ya azimio kusajiliwa na Msajili, na azimio katika hali yoyote, halitasajiliwa na Msajili mpaka siku thelathini na tano kuanzia tarehe liliyopitishwa. (4) Azimio maalumu linalopunguza mtaji wa hisa wa kampuni litatangazwa katika Gazeti la Serikali, na kwa kampuni ya umma, gazeti la kitaifa, katika kila hali ndani ya siku tano za kazi baada ya azimio kupitishwa. Kama kampuni inashindwa kutekeleza kifungu kidogo hiki, wakurugenzi watatozwa faini. Tafadhali elewa kwamba tangazo la kupunguza mtaji wa hisa ni la lazima. Wanasheria wako wanaweza kukuongoza zaidi.

## Wajibu wa wanahisa na wakurugenzi

**Mimi ni mkurugenzi wa kampuni lakini siyo mwanahisa. Hata hivyo, maamuzi ninayoyafanya wakati wa mkutano wa bodi wa robo mwaka yanaashiria kama mimi ndo mmiliki. Ninashindwa kuelewa wajibu wangu ni upi kama mimi siyo mwanahisa. Je, hakuna sheria inayosema mkurugenzi ni lazima awe mwanahisa? Tafadhali niongoze.**

*10 Februari 2014*

Kuwa mkurugenzi, si kumiliki kampuni. Wewe ni sehemu tu ya muundo wa kiutawala wa kampuni ambao menejimenti inaripoti. Wewe siyo meneja wa kampuni wala mmiliki bali upo katikati. Hivyo, unahudhuria mikutano ya bodi na siyo ya wanahisa.

Bodi ya wakurugenzi, ikiwemo na wewe, mnateuliwa na wanahisa na mnawakilisha maslahi ya wanahisa kwenye mikutano ya bodi. Ukiwa kama mkurugenzi, labda kama kuna vifungu maalum vinavyoruhusu, haustahili kulipwa gawio wala faida nyingine zinazolipwa kwa wanahisa ingawa unaweza kupata posho za ukurugenzi.

Ni muhimu kama mkurugenzi kuelewa majukumu yako ni yapi, na uweze kuweka mpaka kati ya majukumu yako na majukumu ya utawala pamoja na wanahisa. Kama mkurugenzi huendeshi kampuni bali unateua utawala ili uendeshe shughuli za utendaji. Hivyo, mkurugenzi hajihusishi moja kwa moja na shughuli za uendeshaji wa kampuni.

Kitu kimoja ambacho unapaswa kufanya ni kusisitiza kampuni ikukatie bima ya wajibu wa mkurugenzi ili ikulinde pale maamuzi ya bodi ya wakurugenzi yanaposababisha hasara au madhara kwa mtu yeyote. Kwa mfano, sheria zetu nyingi zinasema kwamba mkurugenzi anaweza kushtakiwa Mahakamani kwa matendo au kutokutenda kwa kampuni. Katika mazingira kama hayo, ada za mawakili, fedha kwa ajili ya dhamani na mambo kama hayo ni lazima yakingwe na bima, vinginevyo, mkurugenzi anaweza kushindwa kutekeleza masharti ya dhamana na kujikuta anafungwa gerezani. Mara nyingi wakurugenzi hawaelewi wajibu mzito unaoambatana na majukumu yao .

Hivyo, sisitiza bima sahihi juu ya majukumu yako kama mkurugenzi. Uzoefu wetu nchini Tanzania unaonesha kwamba makampuni mengi pamoja na wakurugenzi hawana, au hawajawahi kusikia kuhusu, bima ya wajibu wa mkurugenzi.

Kwa ujumla, isipokuwa kama katiba ya

kampuni inatamka vinginevyo, hakuna sheria inayoeleza kwamba mkurugenzi ni lazima awe mwanahisa. Sababu tu kwamba unafanya maamuzi makubwa haimaanishi kwamba moja kwa moja umekuwa mwanahisa. Wanasheria wako watakuongoza zaidi.

## Haki ya mwanahisa kukagua mahesabu ya kampuni

**Ninamiliki robo ya hisa za kampuni na sina uhakika kama kampuni inafanyiwa ukaguzi sahihi wa mahesabu yake. Je, kama mwanahisa ninaweza kudai kampuni ifanyiwe ukaguzi wa mahesabu?**

*17 Februari 2014*

Kampuni ni lazima imteue mkaguzi katika mkutano wake wa mwaka. Kama huridhishwi na mkaguzi wenu unaweza kutumia kifungu cha 171 cha Sheria ya Makampuni kutaka ukaguzi ufanyike. Kifungu cha 173 kinatamka kwamba (1) Mwanachama yeyote au wanachama wanaomiliki hisa zisizopungua asilimia kumi ya thamani ya mtaji wa hisa wa kampuni au kundi lolote linalohusika la kampuni binafsi linalostahili kusamehewa chini ya kifungu cha 171 au, kama kampuni hiyo si yenye mtaji wa hisa isiwe chini ya asilimia kumi ya wanachama wa kampuni, wanaweza, kwa taarifa ya maandishi (notisi) iliyowekwa kwenye ofisi ya kampuni iliyosajiliwa kwa kipindi cha mahesabu ya kampuni lakini kwa kipindi kisichozidi mwezi mmoja kabla ya ukomo wa muda wa mahesabu, kuitaka kampuni ifanyiwe ukaguzi wa akaunti zake kwa kipindi hicho cha ukaguzi. (2) Iwapo taarifa imetolewa chini ya kifungu kidogo cha (1), kampuni itatakiwa kumteua mkaguzi kwa kipindi cha ukaguzi kinachohusiana na taarifa iliyotolewa.

Hivyo, unaweza kufanya ukaguzi. Njia mbadala ni kuhakikisha mnabadilisha mkaguzi wa mahesabu kwenye mkutano mkuu ujao. Katika mazingira ya kawaida ya kibiashara, unatakiwa kubadilisha mkaguzi wa mahesabu kila baada ya miaka michache. Wanasheria wako wanaweza kukuongoza zaidi.

## Kununua/kuhamisha mkopo

**Sisi ni benki mpya nchini na tunataka kununua/kuhamisha deni kutoka benki nyingine linalohusu mmoja wa wakopaji wake ambaye anataka kuhamia kwetu. Tatizo tulilonalo ni namna gani tutailipa benki hiyo, kuachiliwa hati na kusajiliwa upya kwa jina letu. Itafika mahali tutakuwa hatuna dhamana ya mkopo na bodi yetu haitaki hilo litokee. Tafadhali tuongoze.**

*28 Julai 2014*

Kama bodi yenu ina mambo ya kizamani, mnaweza kujikuta mnashindwa kupata fedha sokoni/kufanya biashara. Mchakato siyo mgumu kama unavyofikiri. Tutakuongoza wewe au mwanasheria wako kufuata hatua zifuatazo: (1) pata uthibitisho kutoka kwenye benki hiyo kuhusu kiasi halisi kinachotakiwa kulipwa ili kumaliza kabisa mkopo; (2) wakati huo huo hakikisha nyaraka zenu zote za mkopo ziko tayari na zimesainiwa; (3) iandikie benki hiyo ukiiarifu kwamba unakusudia kuhamisha/kununua mkopo, na kwamba baada ya kumaliza kulipa deni lote wawe tayari kutoa nyaraka halisi (ikiwemo hati kama ipo) kwenu moja kwa moja ikiwa ni pamoja na fomu zote zilizosainiwa kuachilia/kuweka huru dhamana. (4) Mara benki itakapothibitisha kwamba itatekeleza mambo yote matatu hapo juu, unaweza kuendelea kutoa mkopo kwa mkopaji kwa kuilipa benki hiyo nyingine; (5) baada ya hapo iweke huru dhamana iliyowekwa kwa benki nyingine na wakati huo huo fanya usajili wa dhamana hiyo kwa jina la benki yenu.

Utaratibu wa namna hiyo hapo juu ni wa kawaida sana katika taasisi za benki na kwa uzoefu wetu, benki zimekuwa zikitekeleza ahadi zake linapokuja suala la kuachia na

kuweka huru dhamana za mikopo. Jambo moja la kuchukua tahadhari ni kuhakikisha kwamba benki hiyo ina hati halali za mkopo na dhamana, ambazo zinaweza kuthibitishwa na Msajili wa Hati Wizara ya Ardhi. Tunakushauri kufanya hivyo kwa sababu inaweza kutokea benki nyingine inashikilia hati bandia ambazo pia ni nyingi mtaani. Wanasheria wako watakupatia taarifa zaidi.

## Kampuni, mkurugenzi na karatasi maalum za barua (letter head)

**Nimeanzisha kampuni ya teknolojia ya habari ambayo imeanza kazi. Je, ni sharti la sheria kwamba kila kampuni inapaswa kuwa na karatasi maalum za barua (letterheads)? Ni nini kinachopaswa kuwekwa upande wa juu wa karatasi hiyo? Ninaona ni ghali sana kuchapisha karatasi hizi na hivyo kutafuta namna ya kukwepa. Nifanye nini?**

*29 Septemba 2014*

Ni kweli utahitaji kuwa na karatasi maalum za barua pale unapoandika barua rasmi, hivyo hatuna uhakika unamaanisha nini hasa. Kuchapa karatasi maalum za barua si ghali na wakati wote una hiari ya kuzichapa moja kwa moja kwa kutumia mashine ya kupiga chapa (printa). Kuhusu utaratibu wa kuandaa kichwa cha barua/karatasi hizo, kifungu cha 213 cha Sheria ya Makampuni kinaeleza kwamba kila kampuni, katika nyaraka zote za shughuli ambazo jina la kampuni linaonekana juu au ndani yake ambazo zimetolewa au kupelekwa na kampuni kwa mtu yeyote katika sehemu yoyote ya nchi, itaeleza katika herufi zinazosomeka kuhusiana na kila mkurugenzi kama ni shirika, jina la shirika, na kuhusiana na kila mkurugenzi kama mtu binafsi, maelezo yafuatayo (a) jina lake la sasa, au ufupisho wake, na majina ya ukoo ya sasa; (b) majina yoyote ya zamani na majina ya ukoo; isipokuwa, kama katika hali/mazingira maalumu yamejitokeza ambayo yanafanya, kwa maoni ya Msajili, kuwa kuna haja ya kutotumika matakwa haya, Msajili anaweza, kutoa kwa amri, kwa mujibu wa masharti kama yatakavyoelezwa katika amri husika, kutotumika sehemu ya/au yote ya masharti yaliyowekwa.

Vile vile, kama kampuni inakiuka kutekeleza kifungu hiki, kila ofisa wa kampuni ambaye anahusika katika ukiukaji akitiwa hatiani na kwa kila kosa atatozwa faini isiyozidi laki tano, na kwa madhumuni ya kifungu kidogo hiki, ikiwa shirika ni ofisa wa kampuni, kila ofisa wa shirika atachukuliwa kuwa ofisa wa kampuni. Neno "mkurugenzi" linajumuisha mtu yeyote ambaye maelekezo au miongozo yake wakurugenzi wa kampuni wamezoea kutekeleza na neno "ofisa" litatafsiriwa ipasavyo. Neno "vifupisho" ni pamoja na vifupisho vya jina vinavyofahamika.

Inabidi tuweke wazi kwamba, makampuni mengi nchini Tanzania hayazingatii Sheria ya Makampuni ambayo inataka vichwa vya barua viwe na majina ya wakurugenzi, miongoni mwa mambo mengine.

## Kukopa kwenye benki za kigeni

**Ninataka kukopa Dola za Marekani 300,000 kutoka taasisi ya kigeni. Nimearifiwa kwamba kuna vikwazo kuchukua mikopo kwenye benki za kigeni na kwamba ni lazima nikope ndani ya nchi. Je, hiyo ni kweli? Je, ninahitaji kusajili mkopo huu mahala popote? Ni bora nifanye siri.**

*24 Novemba 2014*

Sheria haikatazi watu kukopa fedha kwenye benki za kigeni ilimradi tu benki hizo ziwe zimesajiliwa kisheria kwenye nchi zinapofanya shughuli zake. Waraka wa Fedha za Kigeni Na. 6000/DEM/EX.REG/58 wa tarehe 24 Septemba 1998 unalazimisha mikopo yote ya nje ya nchi kusajiliwa na Benki Kuu

ya Tanzania na kupewa namba ya usajili wa deni. Utatakiwa kuipa Benki Kuu taarifa kamili kuhusu mkopo na taasisi iliyokupatia mkopo huo.

Kwa bahati mbaya kama hauna namba ya usajili wa deni, hautaweza kutuma fedha/ rejesho kwa mkopeshaji na ndiyo maana kuna umuhimu wa kusajili mkopo huo. Utagundua kwamba utaratibu huu ulianzishwa na Benki Kuu ya Tanzania ili kufuatilia mikopo inayoingizwa nchini, na kuhakikisha kwamba mkopeshaji analipwa kwa urahisi.

Mikopo ya kigeni nchini inakatwa kodi kwenye marejesho ya riba, kupitia kodi ya zuio kwenye riba, na hivyo tunakushauri kuwasiliana na mtaalam wa kodi ili aweze kukuongoza kwenye hili.

## Kuwajibika kwa deni la muuzaji

**Biashara ya rafiki yangu ilikuwa matatizoni na ili kunusuru/kutatua hali hiyo niliamua kununua mali zote za kampuni yake na siyo hisa. Huu ulikuwa ni mwongozo wa mshauri wa kodi ambapo tuliambiwa kwamba mali zinahamishika. Ni miezi michache tangu tukamilishe suala hili, baadhi ya wadeni wa kampuni ikiwemo Mamlaka ya Mapato Tanzania wamenifuata kwa madeni ya kampuni ya rafiki yangu. Je, ninawajibika kwa namna yoyote? Tafadhali niongoze.**

*24 Novemba 2014*

Sheria ya Uhamisho wa Biashara (Ulinzi wa Wadai) inaeleza kwamba, mtu yeyote anayenunua jina, sehemu ya mali au mali ya biashara yoyote iwe ya mauzo au utengenezaji au biashara yoyote inayofanana na hiyo, bila kujali makubaliano yoyote yanayokwenda kinyume, atawajibika kwa madeni yote ambayo biashara ilikuwa inadaiwa tangu siku ya manunuzi, isipokuwa kama taarifa ya kukusudia kununua ilichapishwa kwa mujibu wa kifungu cha nne kwa muda wa miezi miwili lakini usiozidi miezi sita kabla ya siku ya iliyopangwa kufanyika mauzo. Kifungu cha 4 cha Sheria kinataka taarifa za kina kuhusu jambo hilo kuchapishwa kwenye Gazeti la Serikali na kwenye magazeti mengineyo na isainiwe na muuzaji na mnunuzi.

Hivyo, kama ulitangaza mauzo, basi usitegemee tatizo lolote la kisheria. Lakini, kama hukutangaza, basi wadeni na TRA wana haki ya kukufuata. Hata hivyo, sheria inasema kwamba utafidiwa na muuzaji kuhusiana na madeni yote unayowajibika kuyalipa chini ya Sheria hii.

## Ufungaji wa kampuni kwa hiari

**Ninataka kufunga kampuni yangu kwa hiari kwa sababu ina madeni mengi kuliko mali. Je, kuna sheria inayonizuia kufanya hivyo?**

*1 Desemba 2014*

Sheria ya Makampuni, Na. 12 ya mwaka 2002 inaeleza kwamba, inapotokea pendekezo la kufunga kampuni kwa hiari, wakurugenzi au, inapotokea kampuni ina zaidi ya wakurugenzi wawili, wengi wao, kwenye mkutano wa wakurugenzi wanaweza kuazimia kisheria kwamba wamefanya ukaguzi kuhusu masuala yote ya kampuni na baada ya kufanya hivyo wametoa pendekezo kwamba kampuni itaweza kulipa madeni yake yote, pamoja na kiwango halisi cha riba, ndani ya kipindi kisichozidi miezi 12 kuanzia siku ya ufungaji, kama ilivyoelezwa katika azimio.

Hivyo, kama mtu yeyote ambavyo angetegemea, kampuni ambayo ina madeni mengi kuliko mali haiwezi kufungwa kwa hiari na wachama wa kampuni. Kampuni hiyo inaweza tu kufungwa kwa amri ya Mahakama. Kama ukijaribu kufanya hivyo, unaweza kuwajibika kijinai. Kwa msaada zaidi wa kisheria, tafadhali wasiliana na mwanasheria wako.

## Malipo kwa kutumia Shilingi ya Tanzania nje ya Tanzania

**Ninaishi Marekani na niliingia mkataba wa mauzo ya mali/vifaa vyangu fulani nchini Marekani kwa Shilingi ya Tanzania. Mkataba ulikuwa nitalipiwa Marekani kwa Shilingi za Tanzania. Kuna mtu ameniambia hiyo hairuhusiwi. Je, mtu anaweza kuondoka nchini na Shilingi ya Tanzania?**

*8 Desemba 2014*

Inatuwia vigumu kuelewa kwa nini utumie Shilingi ya Tanzania kununua vifaa vilivyopo nchini Marekani wakati upo Marekani. Labda kama tumelielewa vibaya swali lako, kutumia Shilingi ya Tanzania nje ya Tanzania kwa shughuli inayohusisha matumizi ya Shilingi za Tanzania ni batili labda kama umepata idhini ya Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania.

Utakubali kwamba kutumia fedha nchini Tanzania siyo rahisi na kunaongozwa na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Kigeni. Tunakushauri uwasiliane na Benki Kuu ya Tanzania ili kupata idhini hiyo. Pia, ni batili kuondoka nchini Tanzania na Shilingi za Tanzania ambazo inazidi kiasi ambacho ni sawa na Dola hamsini za Marekani bila idhini ya moja kwa moja kutoka Benki Kuu. Hivyo, kwa viwango vya sasa vya ubadilishaji fedha, huwezi kwenda nje ya nchi na zaidi ya Shilingi za Tanzania 85,000.

# Sheria za Madini, Biashara na Uwekezaji wa Kimataifa

Nchi ya Tanzania hukaribisha uwekezaji mkubwa katika miundombinu. Hata hivyo, kuna mapungufu kadhaa kwenye maeneo fulani ya kiuchumi ambayo yanaweza kukuathiri pasipo kutarajia. Hapa tunaangazia sheria kadhaa muhimu ambazo wawekezaji wa ndani na nje wanapaswa kuzifahamu.

## Kununua hisa nje ya nchi

**Kuna kampuni moja ya Uingereza ambayo imetangaza kuuza hisa zake. Ni kampuni yenye heshima kubwa na ninataka kuwekeza kwenye kampuni hiyo. Je, ninahitaji kupata ruhusa ya mamlaka za Tanzania kabla ya kuwekeza? Natumia pesa zangu na sielewi kwa nini natakiwa kupata ruhusa.**

*23 Januari 2012*

Kwa sheria za Tanzania, kama mtu anataka kuwekeza kwenye kampuni ya kigeni nje ya nchi ni lazima aitaarifu na apate kibali kutoka Benki Kuu. Ni kweli pesa ni zako, lakini vifungu hivyo vipo kwa ajili ya kuhakikisha kwamba mtaji hautoroshwi nje ya nchi. Tanzania ikiwa ni nchi inayoendelea, inajitahidi kufanya watu wake wawekeze kwenye nchi yao ili kukuza uchumi wa ndani. Ni sahihi kuwa, Benki Kuu inayo mamlaka ya kukukatalia kuwekeza nje ya nchi.

## Mgeni kununua leseni ya utafutaji madini

**Ninakusudia kununua leseni ya utafutaji madini ya dhahabu hapa Tanzania. Kuna mtu yuko tayari kuniuzia. Hofu yangu kubwa ni iwapo sheria inaruhusu mtu kuhamisha haki hii kwa kampuni ambayo inamilikiwa na wageni kwa 100%. Njia gani nyingine nizifuate ili kuhakikisha kwamba leseni yangu ya uchimbaji ni halali na sitakuwa matatani siku zijazo?**

*13 Februari 2012*

Kwa mujibu wa Sheria ya Madini ya 2010 leseni ya utafutaji madini ni haki ya madini. Kifungu cha 9 cha sheria hii kinaongeza kwamba mmiliki wa leseni au kama kuna mmiliki zaidi ya mmoja, kila mmoja ni mmiliki wa leseni hiyo na kwa kuzingatia kifungu kidogo cha (2) anayo haki ya kutoa leseni hiyo kwa mtu mwingine. Kifungu kidogo cha (2) kinaeleza kwamba leseni maalum au leseni ya kawaida ya uchimbaji madini au sehemu yake hazitahamishwa kwenda kwa mtu mwingine bila idhini ya maandishi ya mamlaka iliyotoa leseni hizo.

Kwa upande wako, leseni ya utafutaji madini ya dhahabu inaweza kuhamishiwa kwako bila kizuizi chochote. Kuhusu suala lako la uhalali, tunakushauri sana ufanye uchunguzi wa kina ili kumtambua mmiliki halali wa leseni ya madini na iwapo hajavunja masharti ya leseni hiyo ya uchimbaji. Kwa kuanzia, unaweza kufanya ukaguzi Wizara ya Nishati na Madini, ili kuhakikisha kwamba masharti ya leseni yamezingatiwa. Unaweza pia kufikiria kutembelea eneo lenyewe ili kuona shughuli zinazoendelea.

Changamoto kubwa ni kumtambua mmiliki wa leseni. Kwa bahati mbaya Tanzania haina mfumo wa kitaifa wa utambuzi na hivyo kuna changamoto ya kuthibitisha utambulisho wa mtu. Ingawa unaweza kumuomba muuzaji pasipoti yake au kadi yake ya mpiga kura, bado njia hizo haziwezi kukuthibitishia kwa 100%. Mwanasheria wako anaweza kukuongoza zaidi.

## Tafsiri ya mkataba wa kugawana uzalishaji

**Nimekuwa nikiangalia mkataba wa kugawana uzalishaji na sielewi kwa nini Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania lipewe sehemu ya mafuta kama gawio la faida? Pia inatuwia vigumu kuelewa kwa nini kuwe na ukomo wa kiwango cha matumizi ambacho mwekezaji anaweza kurudishiwa?**

*27 Februari 2012*

Hatujui kwa nini hutaki Shirika la Maendeleo ya Petroli lipewe gawio la mafuta kama faida wakati linazalisha na lina leseni. Mafuta yanachimbwa kwenye ardhi ya Tanzania na Shirika la Maendeleo ya Petroli

na Watanzania wote wana haki ya kushiriki kupitia makubaliano haya. Na hiki ndicho kinachopigiwa chepuo kwa sasa labda kama unamaanisha kwamba Shirika lipatiwe gawio la faida kwa pesa taslimu na siyo mafuta kitu ambacho hatukubaliani nacho kwa kuwa mafuta pia yanahitajika nchini.

Kuhusu gharama za mkataba kama zinaweza kurudishwa kwenye mafuta ghafi yanayozalishwa, Mkataba hauzuii kurudishwa labda kama mafuta ghafi yaliyochimbwa kwa mwaka huo ni kidogo ukilinganisha na asilimia kubwa unayotaka kurejeshewa kwa kipindi hicho, ambapo gharama zote zilizosalia zinapelekwa mwaka unaofuata, kitu ambacho ni sawa.

## Kununua leseni ya madini

**Kampuni yetu ni kampuni kubwa ya uchimbaji madini na ipo kwenye majadiliano na mmiliki wa leseni ya awali ya uchimbaji madini. Itachukua muda gani kuhamisha leseni hiyo?**

*21 Mei 2012*

Kwa bahati mbaya Sheria ya Madini, 2010 haiwaruhusu ninyi, kama kampuni ya kigeni, kununua leseni ya awali ya uchimbaji madini. Sheria iko wazi kwamba leseni ya awali ya uchimbaji haitatolewa kwa mtu binafsi, ushirika au kampuni isipokuwa (a) Kama ni raia wa Tanzania (b) Kama ni ushirika unaoundwa na watanzania tu (c) Kama ni kampuni (i) iwe ni kampuni inayoundwa na wanahisa wa Tanzania tu (ii) wakurugenzi wake wote ni watanzania na (iii) umiliki wake wa moja kwa moja au la, ufanywe toka Tanzania na watu wote ambao ni raia wa Tanzania.

Hii inaweza kuonekana kama inawabana baadhi lakini inakusudia watu wa ndani kunufaika na shughuli za madini na hili si ajabu kwani nchi yingine pia zina sera kama hizi ili kukuza uchimbaji wa ndani. Njia rahisi ya kununua leseni ya awali ni kuibadilisha kuwa leseni ya madini ya kawaida ambayo baadaye inaweza kubadilishwa kuja kwenye kampuni yenu. Ubadilishaji kutoka leseni ya awali ya uchimbaji kuja kuwa leseni ya kawaida kunahitaji ujuzi na uwezo wa kifedha, uchunguzi pamoja na tathmini ya athari za mazingira kufanyika.

## Mgeni nchini Tanzania

**Mimi ni raia wa kigeni, kwa sasa nipo Dar es Salaam kwa ajili ya shughuli za kibiashara. Ninatamani kuanzisha biashara nchini Tanzania kwa sababu naona fursa nyingi na nataka niingize bidhaa kutoka nchini kwangu na kuja kuziuza hapa. Nia yangu ni kufungua kampuni lakini rafiki yangu ananiambia lazima niwe na ubia/ushirika na raia wa Tanzania kwa sababu ni takwa la kisheria kabla ya kuunda kampuni. Je, ninaweza kusajili kampuni ambayo ni yangu peke yangu?**

*18 Juni 2012*

Usajili wa makampuni nchini Tanzania unaongozwa na Sheria ya Makampuni ambayo haina kizuizi ambacho rafiki yako anakizungumzia. Ndiyo, kuna baadhi ya nyanja za kiuchumi ambazo umiliki wa ndani unahitajika lakini siyo uagizaji na uuzaji bidhaa kama ulivyoonesha. Inawezekana rafiki yako anataka ubia na wewe ndiyo maana amesema hivyo.

Kama tumekuelewa vyema kuhusu swali lako la pili, ni kwamba unataka kuunda kampuni ndogo lakini unataka kuwa mwanahisa peke yako. Kwa sasa hilo haliwezekani lakini Sheria ya Makampuni inarekebishwa na inasubiri ruhusa ya Rais ambapo utaruhusiwa kufanya hivyo, yaani, wewe uwe mwanahisa pekee. Kwa sasa mnatakiwa kuwa wanahisa angalau wawili (bila kujali ni raia wa nchi gani).

## Kuhuishwa leseni ya utafutaji madini

**Mimi ni raia wa Tanzania mwenye leseni nyingi za utafutaji madini kwenye mikoa ya magharibi mwa Tanzania. Je, haki ya kuhuisha leseni ni ya moja kwa moja? Ninatakiwa kufanya nini?**

*3 Septemba 2012*

Chini ya Sheria ya Madini 2010, leseni ya utafutaji madini itakuwa halali kwa kipindi cha miaka 4 ya mwanzo. Pale ambapo maombi ya kuhuisha leseni yamefanyika kwenye fomu maalum, kwa kipindi cha kwanza cha kuhuisha kwa muda usiopungua miaka mitatu. Pale ambapo maombi ya kuhuisha yamefanyika kwa kipindi cha pili cha uhuishaji wa leseni, kwa kipindi kisichopungua miaka miwili. Hivyo leseni yako ya utafutaji madini inaweza kuhuishwa kama ilivyoelezwa hapo juu lakini ni lazima uwe hujawahi kuvunja masharti ya umiliki wa leseni hiyo ya utafutaji.

Leseni ya utafutaji madini inamtaka mmiliki, miongoni mwa masharti mengine, kutumia, kwa kipindi fulani, walau kiasi fulani cha fedha kwenye eneo ambalo ana haki nalo. Hili ni moja ya masharti ambayo wamiliki wengi wa leseni za utafutaji wanakiuka na unatakiwa kuwa makini kwenye hili kwa sababu Wizara inaweza kuliibua hili (usipotumia kiasi hicho) kama kigezo cha kukuzuia kuhuisha leseni.

Uhuishaji wako wa leseni ya utafutaji ni lazima ufanyike mwezi mmoja kabla ya tarehe ya mwisho ya leseni, na moja ya jukumu la Mamlaka ya utoaji wa leseni ni kuhuisha leseni ambazo mmiliki wake hajakiuka masharti, na kwamba mmiliki ametumia asilimia hamsini ya eneo ambalo aliliombea leseni kwa mara ya kwanza. Hivyo wakati wa kuhuisha leseni yako kitalu chako kitagawanywa mara mbili.

## Ukanda maalum wa uwekezaji

**Ninawezaje kufungua kampuni kwenye Ukanda Maalum wa Uwekezaji? Nitapata faida gani kwa kufanya hivyo? Sheria ipi inasimamia uwekezaji kwenye Ukanda huo?**

*17 Septemba 2012*

Unaweza kufungua kampuni kwenye Ukanda Maalum wa Uwekezaji (EPZ) kama walao asilimia 80 ya bidhaa zako ni kwa ajili kusafirisha kwenda nje ya nchi na jumla ya mapato yako ya usafirishaji nje yasiwe chini ya Dola za Marekani 500,000 kwa mwekezaji wa nje na Dola za Marekani 100,000 kwa mwekezaji wa ndani. Mamlaka ya Ukanda Maalum wa Uwekezaji pia itakutaka uwekeze kwenye teknolojia za kisasa na uajiri watu wa ndani.

Pia utapata motisha kama ilivyotolewa chini ya Sheria ya Ukanda Maalum wa Uwekezaji ya mwaka 2002 ambayo ndiyo inaongoza Kanda hizi; motisha ni kama vile kusamehewa ushuru wa forodha, Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) na kodi nyingine zinazotozwa kwenye malighafi na bidhaa za mitambo na mashine, utasamehewa kulipa kodi za makampuni kwa kipindi cha mwanzo cha miaka kumi, utasamehewa kodi ya zuio kwenye pango, faida na riba kwa kipindi cha miaka 10 ya kwanza. Pia utasamehewa kodi zote na ushuru ambao unatozwa na mamlaka za serikali za mitaa kwa bidhaa na huduma zinazozalishwa kwenye Ukanda Maalum wa Uwekezaji kwa kipindi cha miaka 10, kupata bima ya usafirishaji ng'ambo, kusamehewa ukaguzi wa awali au wa baada ya usafirishaji, ukaguzi wa forodha kwenye Kanda, viza za muda mfupi kwa mafundi, watawala, wataalamu pamoja na wakufunzi kwa kipindi hadi cha siku 60, kusamehewa ushuru wa forodha, kodi ya ongezeko la thamani na bidhaa zingine zinazolipiwa kodi kuhusiana na uingizwaji wa gari moja ya utawala, gari za

wagonjwa, vifaa vya zimamoto, na hadi basi mbili, kuzichukulia bidhaa za Ukanda Maalum wa Uwekezaji kama bidhaa zilizoko safarini, kusamehewa kulipa VAT kwenye vifaa na tozo za utunzaji wa bidhaa. Mamlaka ya Ukanda Maalum wa Uwekezaji ina tovuti yenye kuhabarisha sana (www.epza.co.tz).

## Ubadilishaji leseni ya Ukanda Maalum wa Uwekezaji (EPZ)

**Nimewekeza kwenye moja ya Kanda Maalum za Uwekezaji jijini Dar es Salaam. Kutokana na kuporomoka kwa soko la kimataifa la uwekezaji hivi karibuni, ninahitaji zaidi kuuza bidhaa kwenye soko la ndani. Kwa kufanya hivyo, nimeambiwa na Mamlaka ya Ukanda Maalum wa Uwekezaji kwamba nitapoteza hadhi yangu ya Ukanda Maalum wa Uwekezaji. Tafadhali niongoze.**

*24 Septemba 2012*

Leseni uliyonayo ulipewa chini ya Sheria ya Ukanda Maalum wa Uwekezaji [Sura ya 373 iliyorejewa mwaka 2002] kama ilivyofanyiwa marekebisho na Marekebisho na Sheria ya Ukanda Maalum wa Uwekezaji (2006) ambayo inalenga kukuza uuzaji wa bidhaa nje ya nchi. Mtizamo wa Sheria hii pia ni kutengeneza ushindani wa soko la kimataifa kwa bidhaa zinazozalishwa nchini kwetu.

Kubadilisha aina ya biashara na kujikita kwenye soko la ndani kutaua dhana nzima ya leseni uliyopewa. Kama unapenda kujikita kwenye soko la ndani, hautastahili tena kunufaika na haki za wawekezaji wa Ukanda Maalum wa Uwekezaji. Zaidi, Mamlaka chini ya Sheria ya Ukanda Maalum wa Uwekezaji kifungu cha 7(2)(c) imepewa mamlaka ya kufuta leseni ya mwekezaji pale ambapo mwekezaji aliyepewa leseni ya uwekezaji kwenye Ukanda Maalum anampatia mtu mwingine leseni kabla ya kupata idhini ya Mamlaka.

Kwa ufupi, huwezi kujibadilisha na kuwa muuzaji wa soko la ndani kwa zaidi asilimia 20 iliyoruhisiwa bila kupoteza hadhi yako ya Ukanda Maalum wa Uwekezaji.

## Mapitio ya mkataba wa kugawana uzalishaji (PSA)

**Sisi ni kampuni kubwa ambayo imeingia Mkataba wa Kugawana Uzalishaji na Shirika la Maendeleo ya Petroli kwa ajili ya kutafuta mafuta nchini Tanzania. Hivi karibuni tumekuta ripoti inayosema kwamba serikali inakusudia kupitia mikataba yote ya kugawana uzalishaji. Uwezekano ukoje kwa jambo hili kutokea na sisi haki yetu itakuwa ipi? Swali letu jingine ni kwamba Mamlaka ya Mapato Tanzania inawaletea shida wakandarasi wetu wadogo kwenye suala la kodi ingawa sisi tumesamehewa kodi. Je, tunaweza kuwashtaki Mamlaka ya Mapato ili waache unyanyasaji?**

*1 Oktoba 2012*

Kulikuwa na taarifa kwenye vyombo vya habari kwamba Wizara ya Nishati na Madini imeielekeza bodi mpya ya Wakurugenzi ya Shirika la Maendeleo la Petroli kupitia mikataba yote ya kugawana uzalishaji ambayo haina tija kwa Tanzania. Hata hivyo, hilo halikutokea na Wizara ilishalitolea ufafanuzi.

Mkataba wa Kugawana Pato la Uzalishaji ni kama tu ilivyo mikataba mingine kwamba ukishaingia hauwezi kubadilika isipokuwa tu kama kuna uvunjifu au kuna makubaliano ya pamoja ya kuufanyia marekebisho. Wizara ilitamka kwamba inaheshimu utawala wa sheria. Hivyo, angalau hivi sasa Wizara imewahakikishia wawekezaji kwamba mikataba hii ya kugawana uzalishaji haitapitiwa upya.

Ulituuliza kwamba uwezekano ukoje kwa jambo hili kutokea. Jibu letu ni kwamba

uwezekano ni mdogo sana kwa mikataba mliyoingia kupitiwa tena. Uwekezaji nchini Tanzania unalindwa dhidi ya utaifishaji. Tanzania pia ni mwanachama wa mikataba mbali mbali ya kimataifa inayohusu ulinzi na ukuzaji wa uwekezaji wa kigeni. Miongoni mwa mikataba ya uanachama huo wa kimataifa ni Mkataba wa Kimataifa wa Kulinda Wawekezaji (MIGA) na Kituo cha Kimataifa cha Kutatua Migogoro ya Uwekezaji (ICSID). Kwa kufungua tena mikataba hii ya kugawana uzalishaji, Tanzania inaweza kutangazwa vibaya kimataifa, kitu ambacho haiwezi kuhimili katika hatua yake hii ya maendeleo. Itatuma ishara mbaya kwa jamii ya kimataifa ya wawekezaji.

Kuhusu suala lako la kodi, hatuwezi kujibu kama uko sahihi ama la kwenye suala lako la tafsiri ya kipengele cha msamaha wa kodi kwenye makubaliano yenu. Hata hivyo, kuzungumza tu kwa ujumla ni kwamba msamaha mmepewa nyinyi na siyo wakandarasi wenu wadogo na labda kama wametajwa moja kwa moja kwenye mkataba wenu wa kugawana mapato/uzalishaji, wanawajibika kulipa kodi.

Kuwashtaki Mamlaka ya Mapato kwa udhalilishaji hakutawasaidia nyinyi wenyewe wala Mamlaka yenyewe. Ndiyo maana kwa dhumuni hilo, Mamlaka ya Mapato imetenga idara ambayo inashughulika na elimu ya mlipa kodi ambayo inafafanua masuala ya kodi hata kabla ya uingizaji kutoka nje. Mtazamo wetu ni kwamba wawekezaji wengi wanaingiza bidhaa bila hata kuwasiliana na Mamlaka ya Mapato ili kuangalia kama wanastahili kusamehewa. Ni muhimu kwa washauri wenu wa kodi kushauriana na Mamlaka ya Mapato kwenye maeneo ambayo yana utata kabla ya kuanza. Sheria inaruhusu matumizi ya mashauriano ya awali.

## Kukataa kusajili kampuni ya kigeni

**Nilikwenda kwenye ofisi za Wakala wa Usajili, Biashara na Leseni (BRELA) na niliambiwa kuwa siwezi kusajili kampuni ambayo wanahisa wake wengi ni wageni. Nimeshtuka sana kuona kwamba Tanzania bado ina kasumba mbaya ya kudhibiti biashara. Nifanye nini?**

*28 Januari 2013*

Huwezi kwenda BRELA na kupata taarifa kama hizi. Kusajili kampuni yenye wanahisa wengi wa kigeni inaruhusiwa Tanzania. Kimsingi Tanzania inakaribisha makampuni kuja kusajiliwa hapa na kuanza biashara. Tanzania haina tabia yoyote ya kuzuia biashara. Labda, ama umeenda kwenye ofisi isiyo sahihi au ulikutana na mtu asiyehusika. Tunashauri ukutane na Msajili au Naibu wake. Mwanasheria anaweza pia kukuongoza kwenye hatua za kuchukua ili kusajili kampuni yako. Mchakato ni rahisi sana.

## Umiliki wa leseni ya awali ya uchimbaji madini

**Sisi ni kampuni ya kigeni ambayo imeingia kwenye ubia wa asilimia 25, ambapo asilimia 75 zinamilikiwa na kampuni ya ndani. Ubia wetu umeanza kununua leseni ya awali ya uchimbaji madini ili tuweze kufanya uchimbaji mkubwa. Tutaajiri maelfu ya watu. Tunaweza kubadilisha leseni ya awali ya uchimbaji madini kuwa leseni ya madini?**

*3 Juni 2013*

Sheria ya Madini inatamka kwa uwazi kabisa kwamba leseni ya awali ya uchimbaji haitatolewa kwa mtu binafsi, ushirika au kampuni isipokuwa (a) Kama ni raia wa Tanzania (b) Kama ni ushirika, uwe ni ushirika unaoundwa na watanzania tu (c) Kama ni kampuni (i) iwe ni kampuni inayoundwa na wanachama wa Tanzania tu (ii) wakurugenzi

wake wote ni watanzania na (iii) na umiliki wake wa moja kwa moja au la, ufanywe toka Tanzaniana na watu wote ambao ni raia wa Tanzania.

Kutokana na maelezo hapo njuu, ingawa mna asilimia 25 kwenye ubia, ni lazima muelewe kwamba leseni ya awali ya uchimbaji madini ipo kwa ajili ya watanzania pekee wenye makampuni au binafsi na hivyo ubia wenu kwa kupata leseni ya awali ya uchimbaji unakiuka Sheria ya Madini, na kampuni yenu inaweza kutozwa faini na/ au wakurugenzi/ mameneja wanaweza kufungwa kwa kipindi kisichozidi miezi kumi na mbili. Pia elewa kwamba kama mlianza uchimbaji mkubwa wa madini mkiwa na leseni ya awali ya uchimbaji, yaani kusema, bila kubadilisha leseni ya awali ya uchimbaji kuwa leseni ya uchimbaji, Sheria ya Madini inatamka kwamba madini yoyote yaliyopatikana wakati wa uchimbaji usioruhusiwa au shughuli za madini ikiwemo vifaa vinavyohusika kwenye uchimbaji huo vitataifishwa.

## Hakuna idhini kwenye mkataba wa kugawana mazao ya uzalishaji

**Tuna Mkataba wa Kugawana Mazao ya Uzalishaji (PSA) na TPDC na Wizara lakini mkataba hauna kipengele maalum kinachoweka wazi ikiwa tunataka udhibiti wa baadhi ya mambo nje ya mkataba huu kama tunahitaji kupata idhini ya Wizara. Je, hatuongozwi na masharti ya kwenye Mkataba tuliousaini?**

*24 Juni 2013*

Mikataba ya kugawana mazao ya uzalishaji (PSA) inasimamiwa na Sheria ya Utafutaji na Uzalishaji Petroli, 1980 (PEPA). Kifungu cha 54 cha PEPA kinaweka masharti mapana ya kupata idhini ya Waziri kuhusiana na hati ambayo maslahi ya kisheria au usawa kwenye, au yanayoathiri leseni iliyotengenezwa, iliyotolewa, thwa au iliyoshughulikiwa na inatamka kwamba "isipokuwa kama Waziri ataidhinisha (a) uhamishaji wa leseni; au (b) hati ambayo maslahi ya kisheria au usawa kwenye, au yanayoathiri leseni iliyotengenezwa, iliyotolewa, iliyoathiriwa au iliyoshughulikiwa moja kwa moja au vinginevyo, inahamisha au kitu kingine kama kinavyofanya kazi kama ilivyotolewa kwenye aya (b), hakitakuwa halali. Kifungu cha 54(2) kinaeleza zaidi kwamba maombi ya kupata idhini ya Waziri chini ya kufungu kidogo (1) yatapelekwa kwa Kamishna kwa mujibu wa Kanuni.

Kutokana na maelezo hapo juu, inategemea na ni udhibiti kiasi gani, na iwapo utaathiri mkataba, utahitaji kuomba idhini. Mikataba mingi ya kugawana mazao ya uzalishaji wa madini ina vifungu vinavyohusu mabadiliko ya udhibiti; ingawa kama mkataba hausemi, sheria inatamka kwamba idhini lazima ipatikane kama ilivyoelezwa hapo juu. Mkataba hauwezi kuwa juu ya sheria na hivyo vifungu vinavyozungumzia idhini ni lazima vitafsiriwe kwenye mkataba. Hii pia inahusu vifungu vyote vya Sheria ya Utafutaji na Uzalishaji Petroli, bila kujali kama vimetajwa moja kwa moja kwenye mkataba wa kugawana uzalishaji au la. Wanasheria wako wanaweza kukuongoza zaidi.

## Utoaji haki madini

**Mimi ni mkurugenzi wa kampuni ambayo inamiliki leseni nyingi za utafutaji madini chini ya sheria mpya ya madini. Kuna leseni fulani ambazo zimekiuka masharti kwa kutolipa kodi za mwaka ambazo zimeongezeka kwa zaidi ya 100% katika miaka kadhaa iliyopita. Nimesajili kampuni nyingine na nipo kwenye mchakato wa kupata hati/haki madini mpya kwenye eneo ambalo mmiliki wa leseni ya awali ameliacha. Ninaweza kuendelea na maombi?**

*22 Julai 2013*

Sheria ya Madini ipo wazi kwamba haki madini haitatolewa kwa mtu, ushirika au kampuni au kwa mmoja wa washirika, wanahisa au wakurugenzi wa ushirika au kampuni ambayo imekiuka haki madini nyingine au muda wake umekwisha au haki madini imefutwa: isipokuwa kwamba: (a) mtu, ushirika au kampuni ambayo imekiuka; (b) au mshirika, mwanahisa au mkurugenzi wa ushirika au kampuni ambayo imekiuka, anaweza kupewa haki madini baada ya kutimiza wajibu uliokiukwa . Kutokana na maelezo hayo unaweza kuona kwamba kwa kuwa umekiuka, huwezi tena kuomba haki madini mpaka urekebishe ulichokiuka.

Pia tunataka kukukumbusha kwamba Sheria ya Madini inatamka kwamba leseni ya utafutaji madini haitatolewa kwa mtu, ushirika/ubia, kampuni, au kwa mshirika, mwanahisa au mkurugenzi wa ushirika au kampuni ambayo inamiliki zaidi ya leseni halali 20 za utafutaji madini, isipokuwa kama eneo lote la utafutaji madini halizidi mita za mraba 2000.

Ulieleza kwamba unamiliki leseni nyingine nyingi za utafutaji madini. Hivyo, kama unamiliki zaidi ya leseni 20 na jumla ya eneo ya leseni hizo ni zaidi ya mita za mraba 2,000, moja kwa moja unazuiliwa kupewa leseni zaidi za utafutaji. Wanasheria wako wanaweza kukuongoza zaidi.

## Umiliki ardhi wa kampuni ya mafuta na gesi

**Sisi ni kampuni kubwa ya mafuta na gesi nchini Tanzania na tunataka kuwekeza kwenye mtambo ambao utatugharimu makumi ya mabilioni ya Dola za Marekani. Tuna maswali mengi. Kwanza, je Kampuni ya mafuta na gesi inaweza kumiliki ardhi nchini Tanzania? Je, mwekezaji mwingine yeyote anaweza kumiliki ardhi Tanzania? Hatutaki kuingia kwenye mkataba mrefu wa upangaji na mmiliki wa ardhi kwa sababu mkataba unaweza kuvunjwa. Tafadhali tuongoze.**

*29 Julai 2013*

Sheria ya Ardhi ya Tanzania inakataza kwa uwazi makampuni ya kigeni kumiliki ardhi (umiliki wa kupanga) labda kama yana Hati ya Motisha ya Uwekezaji chini ya Sheria ya Uwekezaji (Hati ya Motisha). Hivyo, kampuni ya kigeni yenye Hati ya Motisha inaweza kumiliki ardhi. Cha kuzingatia hapa ni kwamba Sheria hii inahusu tu makampuni ya mafuta na gesi kiasi cha kuyahakikishia kuhamisha mtaji, faida na gawio na kuyalinda dhidi ya utaifishaji.

Nje ya hayo, Sheria hii haiyahusu makampuni ya mafuta na gesi pamoja na makampuni ya madini, ikiwa na maana kwamba makampuni hayo hayana sifa za kuomba hati ya motisha kwa maana ya Sheria hii, hivyo hayawezi kumiliki ardhi. Suala lako kuhusu kuwekeza mabilioni kwenya ardhi na siyo kumiliki linahitaji kupelekwa kwenye Wizara husika pamoja na Shirika la Maendeleo ya Petroli. Isipokuwa kama sheria imebadilika ili kuruhusu wawekezaji wakubwa, hivyo uwekezaji wa kumiliki ardhi, sheria kama ilivyo sasa inakuzuia kumiliki ardhi.

Kama utaamua kutumia njia ya kupanga kwa muda mrefu, ni lazima uhakikishe kwamba muda wa upangaji unakuwa ni mrefu sana na kipengele cha kuvunja mkataba kiwe kinabana sana na kimeandikwa kwa kukupendelea. Unaweza pia kuhahikisha kwamba mmiliki havunji masharti ya umiliki wa ardhi vinginevyo kama hati-miliki itanyang'anywa, upangaji wako utakoma moja kwa moja kwa sababu utakuwa hauna pa kusimamia. Wanasheria wako wanaweza kukuongoza zaidi.

## Kujadiliana upya mikataba ya mafuta na gesi

**Mimi ni mtumishi mkongwe wa umma na nimeshiriki kwenye sekta ya mafuta na gesi kwa miaka mingi sasa, ninataka kujua kwa nini Serikali imeingia kwenye mikataba ya hovyo na makampuni haya ya mafuta, na iwapo Serikali inaweza kujadiliana upya masharti ya mikataba hiyo. Nimeambiwa Qatar ilichukua baadhi ya mali za makampuni binafsi wakati gesi ilipogunduliwa. Hii ni gesi yetu kwa nini tunyimwe haki ya kushiriki katika kuichuma? Kwa nini wananchi wasinufaike na ugunduzi wa gesi iliyopo Tanzania? Kwa upande mwingine, ninaamini kwamba mafuta yameshagunduliwa lakini makampuni haya yanaificha Serikali. Tafadhali niongoze kwenye mambo yote mawili hapo juu.**

*16 Desemba 2013*

Mikataba hii ambayo Serikali na Shirika la Maendeleo ya Petroli imeingia na makumpuni ya mafuta na gesi inaitwa Mikataba ya Kugawana Uzalishaji/Mazao (PSA) ambayo inasimamiwa na Sheria ya Petroli (Utafiti na Uzalishaji) ya 1980. Mikataba ya kugawana uzalishaji/mazao ni aina maalum ya makubaliano ambapo tangu mwanzo na hata kabla makampuni hayajaanza uzalishaji, inakuwa na masharti yaliyofikiwa kuhusu kugawana rasilimali, misamaha ya kodi, ajira, mafunzo, kiwango cha uwekezaji, kugawana faida n.k. Mikataba hii ina nguvu kubwa ya kisheria kwa sababu inatungwa chini ya vifungu maalum vya Sheria ya Petroli (Utafiti na Uzalishaji).

Mikataba hii imejikita kwenye misingi kwamba, makampuni ya mafuta na gesi, kama wakandarasi chini ya mikataba ya kugawana uzalishaji, yanawekeza mamia ya milioni ya Dola. Unachoshauri ni uwezekano tu, na uwezekano huo ni kama tu makampuni haya yatakuwa tayari kujadiliana upya. Kama makampuni haya yakikataa kujadiliana upya, ambacho pia kinaweza kutokea, Serikali haiwezi kuyatoa kwenye mkataba wa kugawana uzalishaji.

Sababu tu kwamba kuna ugunduzi mkubwa ambao haukutegemewa awali, hakumaanishi kutelekeza/kukiuka makubaliano ya awali  na makampuni haya. Kimsingi, Sheria ya Uwekezaji imeeleza kwenye kifungu cha 22 dhidi ya aina hizo za utaifishaji inasema: (1) Kwa kuzingatia kifungu kidogo (2) na (3) cha kifungu hiki (a) hakuna biashara itakayotaifishwa ama kuchukuliwa na Serikali, na (b) hakuna mtu anayemiliki, yote au sehemu ya mtaji wa biashara yoyote, atalazimishwa na sheria kukabidhi maslahi yake kwenye mtaji kwa mtu mwingine yeyote. (2) Hakutakuwa na utaifishaji, bila kujali yote au sehemu ya biashara ambayo sheria hii inatumika na Serikali isipokuwa kama utaifishaji huo utafuata taratibu za kisheria ambayo itakuwa na vifungu vya (a) malipo ya fidia kwa haki, utoshelevu na ya haraka, na (b) haki ya kuzifikia Mahakama au haki ya usuluhishi kwa ajili ya maamuzi ya maslahi au haki za mwekezaji na kiasi cha fidia anachostahili. (3) Fidia yoyote inayo stahili kulipwa chini ya kifungu hiki italipwa kwa haraka na ruhusa ya kubadilisha kwenye fedha inayobadilishika, kama inahusika, itatolewa.

Kutokana na maelezo hapo juu, mwekezaji anapewa ulinzi kamili kwenye ardhi ya Tanzania. Juhudi zozote za utaifishaji kama hizo unazopendekeza ni wazi zinataigharimu nchi kwa hadhi  pamoja na kifedha. Vile vile kuhusu ugunduzi wa madini, wakati wa kuandika jibu hili, hatujasikia kuhusu ugunduzi huo. Hata hivyo, kama kutakuwa na ugunduzi wowote, Sheria ya Petroli (Utafiti na Uzalishaji) pamoja na Mikataba ya Kugawana Uzalishaji zinataka taarifa hizo kutolewa ndani ya siku 30 kwa Waziri wa Nishati na Madini.

Utakuwa umegundua kwamba Wizara ya Nishati na Madini inasimamia masuala hayo kwa umma, na tunaamini kama kungekuwa na ugunduzi huo, umma ungekwishaarifiwa mpaka sasa.

Kama unadokeza kwamba makampuni ya mafuta na gesi yanaificha taarifa hizo Serikali, hii itakuwa ni uvunjifu wa Sheria ya Petroli (Utafiti na Uzalishaji) pamoja na Mikataba ya Kugawana Uzalishaji, ambayo inaweza kuyasababishia matatizo makubwa makampuni haya.

Mwisho, hatujui kuhusu Qatar kuchukua mali za makampuni hayo binafsi ya mafuta na gesi. Tunachokijua, sehemu zote ambazo Serikali imefanya utaifishaji huo, kwa mfano, Amerika ya Kusini, kuliziingiza serikali husika kwenye matatizo makubwa.

Kama mtumishi wa umma mkongwe, tumeshtushwa na msimamo mkali kuhusu Mikataba ya Kugawana Uzalishaji/Mazao. Unahitaji kufikiria tena kuhusu msimamo wako vinginevyo mapendekezo yako yanaweza kuigharimu sana Tanzania.

## Mkataba wa kugawana uzalishaji/ mavuno (PSA) unakiukwa

**Tumeingia mkataba wa kugawana uzalishaji/mavuno na Serikali ya Jamhuri ya Muungano ambao unatoa misamaha mbali mbali ya kodi, ambayo baadhi yake, inakataliwa na Mamlaka ya Mapato (TRA). Hii inatuweka kwenye wakati mgumu kifedha. Tunashangaa kwa nini Serikali iliingia kwenye makubaliano kama hayo ambayo hayaheshimiwi. Unaweza kutuongoza juu ya nini cha kufanya?**

*14 Aprili 2014*

PSA ina nguvu kubwa ya kisheria chini ya Sheria ya Utafutaji na Uzalishaji Petroli, 1980, na imeelezwa kwa uwazi chini ya sheria hii. Hivyo, PSA haiwezi kupingwa iwapo ilisainiwa kwa usahihi, na una haki ya kuishtaki Serikali ili kushinikiza utekelezaji au kudai fidia kutegemea na hasara uliyoipata. Iwapo PSA ina kipengele cha usuluhishi wa migogoro, ambacho kwa kawaida huwepo, basi unaweza kuuwasilisha mgogoro kwenye usuluhishi baada ya kufuata taratibu zilizowekwa kwenye kipengele hicho . Lakini kabla hujakimbilia kufanya hivyo, tafadhali soma hapa chini.

TRA haina mamlaka ya kutoa msamaha wa kodi na ndiyo maana wakati mwingine inaonekana kali. TRA ni taasisi ya kukusanya kodi na inawajibika kufuata sheria za kodi. Kwa mfano, kama hauna msamaha maalum chini ya Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) utawajibika kulipa VAT na kudai kurudishiwa. Kama hujasamehewa rasmi chini ya Sheria ya Usimamizi wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, utawajibika kulipa ushuru wa forodha kwa uingizaji. Kwa kuwa una msamaha chini ya PSA, unatakiwa kuomba msamaha huo wa kodi huku ukiambatanisha PSA kwenye maombi ya msamaha wa kodi. Wizara pekee yenye mamlaka ya kutoa msamaha wa kodi ni Wizara ya Fedha. Hivyo, kabla hujatafuta nafuu zilizopo kwenye kipengele cha usuluhishi tunashauri ujaribu kurasimisha misamaha iliyotolewa kwenye PSA, na iwapo itakataliwa wakati PSA ina misamaha hiyo, basi kukataa huko kutakuwa ni mgogoro unaopaswa kusuluhishwa. Shirika la Maendeleo ya Petroli (TPDC) linaelewa fika jambo hili na uzoefu wetu unaonesha kwamba huwa wanatoa ushirikiano.

Serikali ipo makini sana kuepusha mgogoro wowote na wawekezaji kwenye maeneo iliyoingia mkataba na tunakushauri uwasiliane na Mawaziri kamili wa sekta husika ambao wanaweza kuingilia na kutatua jambo hili. Wanasheria wako wanaweza kukuongoza zaidi.

## Kiasi kilichotumika kwenye leseni ya utafutaji madini

**Nilikwenda kuhuisha leseni yangu ya utafutaji madini lakini niliambiwa niambatanishe kwenye maombi yangu kiasi cha fedha nilichokitumia kwenye eneo la utafutaji. Hii ndiyo mara ya kwanza nimeambiwa kufanya hivyo. Pia, kwa sasa sina akaunti kwa sababu nawasubiri wawekezaji wa kigeni kuja kuungana nami. Je, kuna kanuni zinazoweka kiwango cha chini cha matumizi?**

*9 Juni 2014*

Kifungu cha 30 cha Sheria ya Madini kinaeleza kwamba kiasi cha fedha kitakachotumika kwa kilomita ya mraba kwa leseni ya utafutaji kwa mwaka kitaelekezwa katika Kanuni, na kwa sababu hiyo, Kanuni zitatoa kiwango elekezi juu ya malighafi za ujenzi, kundi la madini ya vito, madini ya chuma, nishati, almasi ya Mwadui (kimberlite) na madini ya viwandani, kiwango kinaweza kutofautiana.

Zaidi, Kanuni za Haki Madini zinaeleza kwamba kiasi cha fedha kitakachotumika iwapo leseni ya utafutaji ni kwa ajili ya utafutaji wa madini yote isipokuwa madini ya vito na malighafi za ujenzi, kitakuwa (a) kwa utafutaji wa awali kiasi cha fedha kitakachotumika kwa kilomita moja ya mraba kitakuwa ni Dola 500; (b) kwa uhuishaji wa leseni wa kwanza kiasi cha fedha kitakachotumika kwa kilomita moja ya mraba kitakuwa ni Dola 2,000; (3) kwa uhuishaji wa leseni wa mara ya pili kiasi cha fedha kitakachotumika kwa kilomita moja ya mraba kitakuwa ni Dola 6,000. (3) kiasi cha fedha kilichoelezwa kwa madhumuni ya kanuni ndogo (1) kama kitatumika kwenye utafutaji wa malighafi za ujenzi kiasi cha fedha kitakachotumika kwa kilomita moja ya mraba kitakuwa ni Dola 100. (4) Kiasi cha fedha kilichoelezwa kwa madhumuni ya kanuni ndogo (1) kama kitatumika kwenye utafutaji wa madini ya vito kiasi cha fedha kitakachotumika kwa kilomita moja ya mraba kitakuwa ni Dola 250.

Ni wazi kwamba viwango vya fedha vilivyoelezwa hapo juu ni vya lazima, na kushindwa kutumia kiasi cha fedha kama ilivyoelezwa kunaweza kupelekea kukataliwa kuhuisha leseni yako kwa kuwa utakuwa umevunja masharti ya matumizi. Washauri wako wanaweza kukushauri zaidi.

## Nimetulia baada ya kuhodhi leseni ya madini

**Tuna leseni ya utafutaji madini fulani, lakini tunashindwa kuendelea na uchimbaji kwa sababu ya hali ya soko ilivyo. Mtaji pia ni changamoto kwa sababu ya hali ya uchimbaji kushuka kwa ujumla. Mshauri wetu anasema kwamba tunaweza kuomba leseni ya kuhodhi halafu tukatulia. Je, hiyo inawezekana na kuna hatari gani tunaweza kukumbana nazo hata baada ya kuwa na leseni ya kuhodhi?**

*20 Oktoba 2014*

Mshauri wako yupo sahihi kwamba unaweza kuomba leseni ya kuhodhi ili uendelee kuhodhi eneo hilo mpaka hali ya mradi na kiuchumi itakapoimarika. Hata hivyo, leseni ya kuhodhi inatolewa kwa kipindi cha miaka mitano na inaweza kuhuishwa kwa kipindi kingine cha miaka mitano, kwa masharti ya kuhifadhi/kulinda madini pamoja na mazingira kama itakavyoelezwa kwenye leseni ya kuhodhi. Hivyo, huwezi kutulia moja kwa moja mara unapopata leseni hiyo.

Zaidi ya hayo, Waziri anaweza, kwa taarifa ya maandishi, kumtaka mmiliki wa leseni ya kuhodhi kueleza kwa nini kampuni (nyingine) isiombe/isipewe leseni maalum ya uchimbaji kwenye eneo lililo chini ya leseni ya kuhodhi. Sheria ya Madini pia inasema kwamba iwapo mmiliki wa leseni ya kuhodhi anashindwa

kuonyesha sababu kwa muda unaofaa, uliotolewa katika taarifa au akatoa sababu ambazo Waziri anaona kuwa hazijitoshelezi, Waziri anaweza kwa taarifa nyingine kumtaka mmiliki wa leseni ya kuhodhi kuomba leseni maalum ndani ya siku sitini tangu siku ya kupatiwa taarifa na kuisalimisha leseni ya kuhodhi.

Unaweza kuona hapo juu kwamba, kwa mfano, iwapo kampuni nyingine zina nia ya kuchimba kwenye eneo ambalo umepewa leseni ya kuhodhi, zinaweza kumwomba Waziri akupe taarifa ya kuonesha sababu, na ikiwa utashindwa kuomba leseni maalumu ya uchimbaji, leseni yako ya kuhodhi utanyang'anywa na kupoteza kabisa eneo hilo.

Ingawa kuna mchakato ambao Wizara inapaswa kuufuata kabla ya kukunyang'anya leseni ya kuhodhi, hata hivyo, huwezi kwenda kwenye fungate baada ya kupata leseni hiyo na lazima uzingatie masharti ya leseni husika.

## Mgogoro na mmiliki jirani wa kitalu cha mafuta

**Tunajishughulisha na uchunguzi/utafutaji mafuta kwenye vitalu vilivyopo kina kirefu cha maji baharini, na tuna mgogoro wa mpaka na jirani yetu. Je, kuna utaratibu rasmi ambao ninaweza kuufuata kutatua hii?**

*17 Novemba 2014*

Unaongozwa na Sheria ya Utafutaji na Uzalishaji Petroli, 1980, ambayo inaeleza chini ya kifungu cha 76(1) kwamba Kamishna anaweza kufanya uchunguzi juu ya na kuamua kuhusu migogoro baina ya watu wanaojihusisha na utafutaji au uendeshaji, ama miongoni mwao wenyewe au miongoni mwao na pande nyingine (isipokuwa Serikali) zisizohusika, kuhusiana na 76(1)(a) Mipaka ya eneo lolote la utafutaji au uendeshaji; 76(1)(b) kitendo chochote kilichofanyika au kuacha kufanyika, au kinachodaiwa kufanyika au kutokufanyika, katika, au kuhusiana na utafutaji uendelezaji; 76(1)(c) makadirio na malipo ya fidia kwa mujibu wa Sheria hii; au 76(1)(d) masuala mengine yoyote kama yalivyoelezwa kwenye sheria. 76(2) Kamishna anaweza, kwa hiari yake, kukataa kuamua mgogoro wowote uliopelekwa kwake chini ya sehemu hii na kama akikataa, atazitaarifu kwa maandishi pande zenye mgogoro sababu za kukataa huko. 76(3) Kamishna anaweza kutoa tuzo yoyote au amri ambayo ni muhimu katika kutekeleza maamuzi yake kuhusiana na mwenendo wa sehemu hii, na anaweza kuuamuru upande wowote wa mgogoro kuulipa upande mwingine wa mgogoro fidia stahiki.

Zaidi, kifungu cha 78(1) kinaeleza kwamba mtu yeyote ambaye hajaridhika na maamuzi, tuzo au amri ya Kamishna iliyotolewa kwa mujibu wa sehemu hii anaweza kukata rufaa kwenda Mahakama Kuu ndani ya siku 60 baada ya kutolewa kwa maamuzi, tuzo au amri.

Cha kushangaza, kifungu cha 78(2) kinaeleza kwamba hakuna rufaa itakayokatwa kwenda Mahakamani dhidi ya maamuzi ya Kamishna yaliyotolewa chini ya kifungu cha 76(2).

Hivyo, kuhusu mgogoro wenu wa mpaka, unaweza kuuwasilisha kwa Kamishna wa Nishati ambaye anaweza kufanya uchunguzi na ndiye mwenye mamlaka ya kufanya maamuzi, ambayo hata hivyo yanaweza kukatiwa rufaa kwenda Mahakama Kuu. Mbadala, unaweza kwenda moja kwa moja Mahakama Kuu au Mahakama nyingine zenye mamlaka ili kutatua mgogoro huu.

# Migogoro baina ya Watu Binafsi

Marafiki, wanafamilia na majirani wanaweza kugombana kwa mambo mengi, hata hivyo, siyo kila mgogoro unaweza kutatuliwa mahakamani. Hapa, tunaangazia mambo ambayo mfumo wetu wa kisheria unaweza ama kumsaidia au kutomsaidia mlalamikaji.

## Nimelipa bila mkataba wa mkopo

**Nilimkopesha rafiki yangu anayeishi mkoani Mwanza kiasi cha Shilingi milioni 2. Kwa kuwa mimi ni mstaarabu, nilimuingizia fedha kwenye akaunti yake na nikapata stakabadhi ya ingizo la muamala husika. Alinipigia na kuthibitisha kuwa amepata pesa. Ni miezi sita sasa na sioni dalili zozote za kunilipa. Sasa hivi amenigeuka kuwa hatukuwa na makubaliano yoyote ya mkopo. Je, ninaweza kutumia stakabadhi ya ingizo la muamala benki Mahakamani?**

*20 Februari 2012*

Mikataba inaweza kuwa ya maandishi au mdomo ingawa inashauriwa kuwa na mikataba ya maandishi kwa madhumuni ya uwazi na ushahidi. Ingawa swali lako ni iwapo unaweza kutumia stakabadhi ya ingizo la muamala benki Mahakamani, tunaamini swali lako la msingi ni namna gani unaweza kupeleka suala lako Mahakamani na kuthibitisha kwamba ni kweli pesa hizo zilikuwa ni mkopo.

Kukosekana kwa ushahidi wa uwepo wa mkataba wa mkopo inakuwia vigumu lakini unaweza kuwa na mashahidi wakiwemo marafiki na familia ambao walijua kuhusu mkopo huo. Labda kama atakiri Mahakamani, stakabadhi yako ya malipo pekee haiwezi kuwa ushahidi unaojitosheleza. Wanasheria wako wanaweza kukuongoza zaidi.

## Kulipwa deni na marehemu

**Nilimuazima pesa nyingi sana rafiki yangu ambaye sasa amefariki. Sikujua kuhusu kifo chake na wakati nilipogundua tayari Mahakama ilishateua msimazi mirathi na mali zote za marehemu zilikuwa zimekwisha gawiwa. Ninawezaje kurudishiwa pesa zangu hasa ukizingatia kwamba mali zote zipo mikononi mwa wanufaika?**

*23 Julai 2012*

Sheria ya Uthibitisho wa Wosia na Usimamizi wa Mirathi inamruhusu mdai kuzifuata mali za wanufaika na kurudisha deni lake. Hata hivyo, kisheria, msimamizi wa mirathi anatakiwa kutangaza iwapo kuna mtu yeyote anamdai marehemu kabla hajaanza kugawa mali za marehemu. Kama msimamizi wa mirathi ametangaza kama sheria inavyotamka utatakiwa kuieleza Mahakama kwa nini hukupeleka madai yako kwa msimamizi wa mirathi wakati alipotangaza. Mwanasheria wako anaweza kukuongoza zaidi.

## Mkopeshaji anakataa kupokea pesa

**Miaka michache iliyopita niliazima pesa kwa rafiki yangu ambayo nilitakiwa kulipa kwa riba kwa miezi sita. Siku ya malipo nilimuendea alikataa kupokea pesa kwa sababu ambazo hazieleweki. Mwanzoni ilionekana kama utani lakini baadaye haikuwa hivyo. Niliendelea kumshawishi achukue pesa kwa sababu ipo kwa makubaliano lakini alikataa kupokea. Baadaye alisafiri na hivi karibuni amerejea na amenifungulia kesi Mahakamani akidai pesa zake, riba pamoja na faida aliyopoteza kutokana na kumcheleweshea/ kutokumlipa pesa zake, wakati madai hayo siyo kweli. Riba anayodai ni mara tatu ya kiasi alichonikopesha. Baada ya kufanya uchunguzi nimegundua kwamba ilikuwa ni mbinu ya kukataa kulipwa ili adai riba zaidi. Ninawezaje kuendelea na suala hili? Pesa ya kumlipa ilikuwepo lakini alikataa kupokea. Je, kuna haja ya mimi kulipa kipindi hiki?**

*5 Machi 2012*

Hii ndiyo mara yetu ya kwanza kusikia mkopeshaji anakataa kupokea pesa na riba kwa mujibu wa makubaliano hasa pale kiasi cha mkopo kinalipwa ikiwemo na riba. Tunajibu swali lako kwa misingi kwamba hakuna unachotuficha.

Kwa ujumla, kukataa kwa mkopeshaji

kupokea pesa hakumuondolei mdaiwa wajibu wa kulilipa deni hilo, kwa sababu deni halifi kwa kukataa kwa mkopeshaji. Ni jukumu la mkopaji kumtafuta mkopeshaji na kulipa deni kitu ambacho wewe ulifanya. Hata kama mkopeshaji amekataa kupokea pesa, mkopaji ni lazima aendelee kuwa tayari kulipa.

Utetezi wako unatakiwa uhusishe yote uliyotamka hapo juu kwamba wakati wote ulikuwa tayari kulipa ila ni kwa sababu tu mkopeshaji alikataa kupokea pesa zake. Wakati wa usikilizaji unatakiwa utoe ushahidi wa namna hiyo.

Kuhusiana na ulazima wa kulipa sasa, hakuna uwezekano kwamba anaweza kupokea pesa hizo kwa sasa. Kama unatudokeza kwamba kukiwa na kesi deni linafutika, tafadhali elewa kuwa hilo haliwezekani. Ni lazima uendelee kujiandaa kulipa kiasi ulichokopeshwa pamoja na riba ambayo ilikuwa stahiki yake pale mwanzoni. Kama utafanikiwa utatakiwa kulipa kwa mpango wa awali na unaweza kupewa gharama za kuendesha kesi. Tunakushauri pia ujaribu kupembua maelezo yako kwa sababu inatuwia vigumu sana kuamini.

## Kifungo katika madai

**Rafiki yangu aliniazima pesa na hajanilipa licha ya juhudi nyingi za kufuatilia. Nilimshtaki Mahakamani ambapo alikiri kweli kwamba anadaiwa na hukumu ilitolewa dhidi yake. Ni mwaka sasa tangu hukumu na hajanilipa hata Shilingi. Hii inanitatiza sana kwani siyo kwamba hana hela ya kulipa bali ni bahili na mbinafsi. Je, anaweza kufungwa jela kama mfungwa wa madai?**

*16 Aprili 2012*

Kama hujafanya hivyo basi, ni lazima kwanza upate Tuzo ya Mahakama kutekeleza maamuzi hayo. Tuzo inatengenezwa kutokana na hukumu uliyonayo. Baada ya hapo unaweza kupeleka maombi Mahakamani kwa ajili ya kutekeleza tuzo ya malipo ya pesa kwa kumkamata na kumfunga kama mfungwa wa madai. Ukumbuke kwamba Mahakama haina wajibu wa kutoa hati ya kukamata; isipokuwa inaweza kuamua kumuita mdaiwa mbele yake na kumtaka atoe sababu za kwa nini asifungwe kama mfungwa wa madai. Kama Mahakama itajiridhisha kwamba mdaiwa hana nia ya kulipa hasa kama anao uwezo wa kufanya hivyo itatoa hati ya kukamatwa na mdaiwa atafungwa kama mfungwa wa madai.

Wakati akiwa gerezani utatakiwa kulipa fedha za matunzo yake kila mwezi. Pesa hizo za matunzo zitatolewa kila mwanzo wa mwezi hadi pale mdaiwa atakapotoka gerezani au pale atakapolipa deni. Gharama unazoingia kumtunza zinaweza kurudishwa na mdaiwa.

## Mpenzi wangu wa zamani anatumia jina langu kwenye wimbo

**Mpenzi wangu wa zamani ni mwimbaji maarufu nchini Tanzania na katika wimbo wa hivi karibuni, ambao unavuma sana, ametumia jina langu. Ninaweza kumdai fidia? Siyo haki kabisa yeye kujiingizia fedha kwa kutumia jina langu. Tafadhali nisaidie jinsi gani ninaweza kulisimamia jambo hili?**

*18 Februari 2013*

Tulisoma swali lako lote ulilotutumia kwa barua-pepe na jina ulilotaja humo (ambalo hatukuchapisha kwa sababu jina lake na la kwako yangeJulaikana). Maoni yetu ni kwamba jina lako, ambalo ni jina la kwanza tu, linatumiwa na mamilioni ya wanawake duniani kote. Wimbo, ambao tulilazimika kuusikiliza ili kujibu swali hili, pia haukutaja jina la pili wala kudokeza kuhusu wewe. Kwa kweli, jina la kwanza limetumiwa kwa ubunifu mno na ni vigumu kwako kuthibitisha kwamba umechafuliwa. Pia tunashangaa sana kwamba unafikiri ni jina lako na sio sauti

ya uimbaji na msaanii ndivyo vilivyofanya wimbo kuvuma. Unaweza kupata maoni ya pili kutoka kwa mwanasheria mwingine lakini fikra zako, kwa maoni yetu, ni za mbali sana labda kama kuna taarifa zaidi ambazo hujatuweka wazi.

## Kuvunja mkataba wa kusambaza nywele

**Kuna mweka wigi ambaye amekuja mjini kuwawekea mawigi vijana na wazee. Nilipokuwa na mafundi ususi wangu, alinifuata na kuahidi kunilipa kiasi fulani ikiwa nitampa nywele zangu. Baada ya kumpatia nywele mara tatu, amekataa kulipa chochote akisema kwamba nywele hizo zingepotea tu hata hivyo. Nifanye nini? Nimeambiwa ni mchawi na ni lazima nikae naye mbali.**

*4 Machi 2013*

Mweka wigi amevunja masharti ya kukulipa chini ya mkataba. Ukweli kwamba ungekwenda tu kutupa nywele hizo hata hivyo, madai ambayo labda ni ya kweli, hakubadili ukweli kwamba hajakulipa chini ya mkataba. Inawezekana kuwa hamkuandikishana lakini chini ya sheria zetu mkataba wa mdomo pia unaruhusiwa. Unaweza kuamua kumshtaki, na yeyote aliyewasikia mkiingia kwenye mkataba huu, anaweza kuletwa kama shahidi Mahakamani ili kuthibitisha. Wanasheria wako wanaweza labda kuanza kwa kumtumia barua/notisi ya madai kabla ya kumpeleka Mahakamani. Utahitaji kufanya uchambuzi wa faida na gharama ambazo utazitumia na kiasi unachoweza kupata kama fidia kabla ya kukimbilia Mahakamani. Kuhusu suala la mweka wigi kuwa mchawi, hatuwezi kutoa maoni. Uchawi nchini Tanzania ni kosa na unaweza kutoa taarifa polisi.

## Uhalali wa hati ya kubadili umiliki wa ardhi

**Mwaka 2009 niliuza nyumba yangu iliyopo Wilaya ya Kinondoni na niliomba kwa mafanikio hati ya kubadili umiliki wa ardhi kutoka kwa Kamishna wa Ardhi. Hata hivyo, kabla sijalipa ada za kisheria, nilihamishiwa mkoani Kigoma kwenye kituo changu kipya cha kazi ambako nilikaa miaka miwili bila kuja Dar es Salam. Mwaka huu nimepata likizo na kuja Dar es Salaam kumalizia mchakato wa kuhamisha umiliki lakini cha ajabu maafisa ardhi wameniambia nianze upya mchakato. Je, hii ni sawa? Tafadhali nishaurini.**

*12 Machi 2013*

Kutokana na maelezo hapo juu, ni wazi kuwa umechelewa kulipa ada za kisheria za hati ya idhini iliyotolewa kwako. Hati ya idhini ya kubadili umiliki ina ukomo wake kisheria ambao ni mwaka mmoja tangu siku ilipotolewa. Msajili hawezi kuingiza kwenye rejesta mabadiliko ya umiliki wa ardhi hadi pale tozo, kodi na ada mbalimbali zinapokuwa zimelipwa. Kwa kuwa muda wa hati ya idhini ya kubadili umiliki umekwisha, huna chaguo jingine isipokuwa kuanza upya mchakato.

## Kunasa sauti za chumbani

**Nina sababu ya kuamini kwamba jirani yangu anafuatilia na kunasa sauti na mienendo ya chumba changu. Je, ninaweza kumshtaki jirani yangu? Hali hii imepelekea mahusiano mabaya na mpenzi wangu ambaye anajua kuhusu hili na sasa amepunguza upendo. Nifanye nini?**

*18 Machi 2013*

Una haki ya faragha na yeye kunasa masuala yako ya chumbani ni uvunjifu wa faragha wa moja kwa moja. Kesi ina mashiko na unaweza kumshtaki jirani yako. Hata hivyo utahitaji kuthibitisha kuwa kweli alikurekodi na hiyo inaweza kuwa

ni changamoto. Zaidi, kama utahitajika kutoa ushahidi, itabidi utoe kifaa hicho cha kurekodi ili kisikike Mahakamani na unaweza usipende fedheha zaidi, hivyo unatakiwa kuwa mwangalifu. Kuhusu nini unachoweza kufanya, ni ama kushtaki, kuhama, kupunguza sauti au kuongeza upana wa ukuta. Kelele za chumbani ni za kawaida na hatuwezi kukushauri uache kuzipiga. Mpango wa kisheria unaweza kukamilishwa na wanasheria wako, ambao unatakiwa kuwasiliana nao.

## Kuvunja mkataba

**Ninataka kuvunja mkataba ambao niliingia. Ni sababu gani za kisheria ambazo ninaweza kuzitumia ili kuvunja?**

*8 Julai 2013*

Mikataba inatakiwa kuheshimiwa na sheria inakusudia kuhakikisha kwamba pande zinazoingia mkataba zinaheshimu kusudio la mkataba ili kuhakikisha kwamba biashara hazianguki. Sheria ya Mikataba, hata hivyo, inawapa wahusika katika mkataba sababu nyingi za kuvunja mkataba ikiwa tu sababu hizo ni halali. Unaweza kuvunja mkataba kama ulishurutishwa, ulidanganywa, yaani upande mwingine uliwakilisha isivyo mambo ya msingi kuhusu mkataba, ubatili wa mkataba au kiini cha mkataba, kukosea jambo, yaani akili za pande za mkataba hazikuendana, kama ni mdogo/mtoto, yaani yupo chini ya miaka 18, kuvunja masharti ya mkataba, masharti ya awali hayakutekelezwa, n.k. Tunashauri mwanasheria wako akuongoze kwenye mkataba wako kabla hujafanya chochote.

## Nimeng'atwa na mbwa koko

**Nilikuwa matembezini mtaani kwa furaha, kabla ya kung'atwa na mbwa koko. Nilipata majeraha makubwa na ninataka kushtaki? Tafadhali niongoze.**

*15 Julai 2013*

Hatujui ni mwongozo gani unautaka. Kimsingi, huwezi kumstaki mbwa na kama ni mbwa koko maana yake huwezi kumpata mmiliki wa mbwa huyo. Lakini kama utampata mmiliki, anaweza kushtakiwa na kufunguliwa mashataka ya jinai chini ya sheria zetu kwa kushindwa kulinda usalama wa watu wengine. Tunashauri uwasiliane na wanasheria wako.

## Anakaidi kulipa licha ya amri ya Mahakama

**Rafiki yangu alimuuzia nafaka mtu fulani lakini hajawahi kumlipa. Walipambana katika Mahakama ya Mwanzo na rafiki yangu alishinda na Mahakama ilimuamuru mtu huyo kulipa kiasi fulani cha pesa ndani ya mwezi mmoja. Kiasi kilichoamuriwa siyo kikubwa na nina uhakika wa asilimia 100 kwamba mdaiwa anakimudu. Rafiki yangu alimuandikia mtu huyo na kumuomba amlipe lakini cha kushangaza mtu huyu alimjibu kwa maandishi kwamba ni bora afe kuliko kumlipa. Sijui ni kwa nini anafanya hivi wakati ana uwezo wa kulipa. Kwa uelewa wangu hakuna rufaa iliyokatwa dhidi ya maamuzi yaliyotolewa dhidi yake na muda wa kukata rufaa umekwisha. Je, hiyo siyo kinyume cha sheria?**

*17 Machi 2014*

Chini ya Kanuni ya Adhabu, kifungu cha 114(1)(j) kinatamka kwamba, mtu yeyote ambaye ana namna ya kulipa fidia au gharama au kiasi kingine chochote kwenye kesi za madai au kesi za jinai iliyotolewa dhidi yake na Mahakama ya Mwanzo, iwapo kwa makusudi atakataa au kudharau baada ya kupewa taarifa ya kumtaka alipe kuhusiana na amri ya malipo mengine yoyote ama kwa awamu au la anatenda kosa na atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miezi sita na faini ambayo haitazidi Shilingi mia tano.

Inawezekana mtu aliyeuziwa nafaka hakijui kifungu hiki na kutokujua pekee si kinga/msamaha. Lakini tabia aliyoionesha mtu huyu haikubaliki na inatweza heshima ya Mahakama na hivyo kuadhibika. Kwa kuwa hili ni kosa la jinai, tunakushauri ufungue shauri la jinai ili utawala wa sheria uheshimiwe. Wanasheria wako wanaweza kukuongoza zaidi.

## Kudhalilishwa na ndugu kwenye hafla

**Mimi ni mtu maarufu na tajiri hapa Jijini Dar es Salaam na niliandaa karamu kwenye ukumbi wa kifahari ili kusherehekea kumbukumbu ya ndoa yangu. Kwenye sherehe hiyo nilialika watu wengi maarufu wa Jiji la Dar es Salaam wakiwemo wanamuziki, wanasiasa na wakuu wa makampuni. Kwenye kadi ya mwaliko nilibainisha aina na rangi ya vazi la sherehe. Miongoni mwa waalikwa alikuwa ni mjomba wangu kutoka mkoani ambaye nilimualika tu ilimradi lakini sikutegemea kama angefika. Kwa bahati mbaya alihudhuria na alivaa kandambili na nguo za bei rahisi zisizoendana na sherehe kiasi kwamba walinzi walimchukulia kama mvamizi hadi nilipoingilia kati na kutaka aruhusiwe kuingia. Mbaya zaidi, alianza kuzunguka ukumbini na kujitambulisha kwa wageni kwamba yeye ni mjomba wangu na anajivunia mafanikio yangu. Nimekatishwa tamaa sana na haya yote kwa kuwa wageni watafikiri kwamba ninatoka kwenye familia masikini. Ninataka kumwajibisha mjomba wangu. Je, kuna namna ambayo ninaweza kufanya hivyo kisheria?**

*19 Mei 2014*

Kikanuni unatakiwa kuelewa kwamba ili uweze kuwa na haki ya kushtaki, ni lazima uoneshe kwamba una madai halali dhidi ya mtu unayetaka kumshtaki; pili, umenyimwa madai hayo; tatu, mtu unayemshtaki ndiye aliyekunyima haki yako; na nne, umepata hasara.

Tukirudi kwenye malalamiko yako, umekubali kwamba ulimruhusu mjomba wako aingie, hivyo hakuwa mvamizi kwenye sherehe yako, hii pia ikiwa na maana kwamba ulimkubali pamoja na mavazi yake. Wakati huo ulikuwa na fursa ya kumzuia asiingie kwa kuzingatia mavazi ya sherehe.

Kuhusu kuwaambia wageni kwamba yeye ni mjomba wako, hapo hatuoni tatizo kwa sababu kulingana na maelezo yako, ni wazi kwamba huo ni ukweli. Kwa bahati mbaya hadhi au utajiri wako hauwezi kubadilisha ukweli kwamba yeye ni mjomba wako na ataendelea kuwa hivyo maisha yote.

Tunakushauri utafute mpatanishi ili aweze kuondoa tofauti zenu. Mtakapokufa, wewe na mjomba wako mtazikwa futi sita ardhini, na kwa kile tunachokisoma kwenye maandiko, hakutakuwa na tofauti kati ya tajiri na masikini. Unahitaji msaada wa mwanasheria na mshauri wa masuala ya kijamii.

## Mzinga wa nyuki mtaani kwetu

**Jirani yangu ameweka mizinga mingi kwenye mti ambao kivuli chake kinafika nyumbani kwangu. Ninajali sana urembo wangu na hivyo ninatumia manukato na mafuta yenye harufu kali. Ninaogopa nyuki wanaweza kuning'ata kwa sababu ya hii harufu. Ni kitu gani halali ninaweza kukifanya?**

*30 Juni 2014*

Sheria inayoelezea kutundika/uwekaji mizinga ni Sheria ya Nyuki, 2002, na inawalinda watu wote pasipokujali uzuri/urembo wao. Sheria hii inaeleza kwamba kama Mkurugenzi au afisa aliyeruhusiwa ameridhika kwamba ufugaji nyuki kwenye eneo fulani ni kero au ni hatari kwa afya au usalama wa umma; au kwa sababu nyingine

yoyote anaona kwamba eneo hilo halifai kwa ufugaji nyuki, anaweza, kutoa amri kwa mtu huyo ya kumzuia kufuga kwenye eneo hilo; au kumuamuru mtu huyo kuweka idadi maalum ya mizinga kwenye eneo hilo.

Kama mtu huyo akishindwa kutekeleza amri ya Mkurugenzi au ya afisa aliyeruhusiwa, Sheria inaeleza kwamba, iwapo Mkurugenzi au afisa aliyeruhusiwa ameridhika kwamba mtu huyo ameshindwa kutekeleza maelekezo yaliyotolewa kwenye amri iliyotolewa na Mkurugenzi au afisa aliyeruhusiwa, atampekeka Mahakamani.

Hivyo kwa kuzingatia hayo, unaweza kutoa taarifa juu ya malalamiko yako kwa Mkurugenzi anayesimamia ufugaji wa nyuki. Mkurugenzi atamtuma afisa aliyemruhusu kuchunguza jambo hilo na wataamua jambo la kufanya. Kama maamuzi haya hayataamuliwa kwa upande wako, unaweza kufungua kesi ya madhara iliyojikita kwenye usumbufu na uiombe Mahakama ikupe zuio la kudumu dhidi ya jirani yako. Tafadhali wasiliana na mwanasheria wako kwa mwongozo zaidi.

# Sheria za Ajira na Uhamiaji

"

Wengi wetu hutumia maisha yetu yote tukiwa kazini. Mara nyingi, mahali pa kazi panaweza kuwa chanzo cha migogoro. Je, makubaliano ya malipo ya ziada/motisha yaliyoandikwa kwenye menyu ya chakula yanaweza kutumiwa na mfanyakazi kudai malipo husika? Je, waajiri wanaweza kulazimisha kuwatembelea wafanyakazi majumbani mwao? Na je, tabia ya bosi kusomea gazeti chooni inaweza kuwa kigezo tosha kumshitaki? Katika sura hii tunajibu maswali yote haya na mengine mengi yakiwemo yale yanayohusu sheria za uhamiaji na matokeo ya safari za anga za mbali.

## Kupima VVU kwa lazima

**Niliomba kazi ya uhudumu wa mapokezi kwenye kampuni fulani hapa Dar na nilikubaliwa baada ya kufanyia usaili wa kina. Baadaye nikaambiwa niende kwenye hospitali iliyopangwa kwa ajili ya kupima damu. Nilipofika hospitali mhudumu wa maabara alichukua damu yangu na akaambatanisha kwenye fomu ambayo ilionesha kwamba vipimo vinatakiwa kufanyika. Nilijua ninatakiwa kupima VVU na mara moja nilikataa kufanya/kuendelea na vipimo. Nilichukua sampuli ya damu yangu nakuondoka hospitali. Je, Kampuni inaweza kunifanyia vipimo bila idhini yangu? Je, hiyo siyo kinyume cha sheria?**

*30 Januari 2012*

Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Virusi vya UKIMWI inaeleza kwamba vipimo vya VVU vitafanyika kwa idhini ya mhusika. Hakuna mtu atalazimika kupima VVU bila idhini yake isipokuwa kwa amri ya Mahakama au mtu huyo anachangia damu au viungo au amedhalilishwa kingono. Kwa uelewa wetu wewe siyo mmojawapo.

Kilichofanywa na kampuni ni uvunjifu wa sheria kwa sababu hata Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini inakataza aina hiyo ya ubaguzi kwa waajiriwa; hivyo basi mwajiriwa kuwa na VVU au kutokuwa navyo, hakutaathiri ajira yake.

Hospitali nayo inawajibika kwa sababu walikupima au walikaribia kukupima VVU bila kwanza kupata idhini yako. Una kesi dhidi ya mwajiri wako mtarajiwa na hospitali pia. Mwanasheria wako anaweza kukuongoza zaidi.

## Kipengele cha dhamiri kwenye mkataba

**Mimi ni daktari kutoka ng'ambo na niko kwenye majadiliano na hospitali fulani hapa Dar kuhusu mkataba. Hospitali inataka nifanye kazi zote na haiko tayari kukubaliana na takwa langu la kuwepo na kipengele cha dhamiri kwenye mkataba wangu. Nifanyeje?**

*7 Mei 2012*

Kipengele cha dhamiri kinakuruhusu kutokufanya baadhi ya shughuli za kitabibu ambazo kimaadili haukubaliani nazo. Kipengele hiki kimekuwa kikitumika sana kwenye mikataba ya madaktari hasa wanaopinga utoaji mimba. Nchini Tanzania, utoaji mimba ni haramu na ni kosa la jinai kwa hiyo hauna haja ya kuwa na hofu juu ya hilo kwa sababu lipo moja kwa moja kwenye sheria, huwezi kumtoa mtu mimba isipokuwa kwa sababu za kitabibu. Hata hivyo, kama utakuwa na masuala mengine ya kimaadili, bila shaka unaweza kuzungumza na mwajiri wako. Wazo mbadala, unaweza kutafuta mwajiri mwingine kwa kuwa pande za mkataba ziko huru kujadiliana masharti ambayo wataona yanawafaa kwenye mkataba wao.

## Mkataba wa ajira unatamka siwezi kufanya kazi kwingine

**Mimi ni mhasibu ninafanya kazi Dar es Salaam kwenye kampuni ya uzalishaji na usambazaji bidhaa. Ni mwaka wangu wa 17 nipo kwenye kampuni na sioni tija yoyote. Mshahara wangu umebaki uleule kwa miaka sita sasa. Siku za hivi karibuni faida ya kupewa matibabu imeondolewa na kwa ujumla sina tena furaha ya kazi. Nilimwambia bosi aniongeze mshahara lakini kama kawaida aliahidi ataniongezea, na kwamba biashara bado haiendi vizuri kwa hiyo aliniomba niwe mvumilivu. Ninakaribia miaka 55 na sielewi niwe mvumilivu mpaka lini. Kampuni shindani imenifuata ili nikafanye nao kazi na wameshanipa barua ya ofa. Nilipomtaarifu**

**mwajiri wangu alinionesha mkataba wangu wa ajira ambao nilitia saini miaka mingi iliyopita ambao unanizuia kufanya kazi kwa mtu mwingine yeyote. Mwanasheria wa kampuni ananitisha kwamba watanishtaki kwa kuvunja mkataba. Ninawezaje kuishi kama nikizuiliwa kufanya kazi kwa mtu mwingine isipokuwa mwajiri wangu? Huu ni utumwa mamboleo na najiona mpumbavu sana nilipokubali kusaini mkataba wa aina hiyo. Nifanye nini?**

*16 Julai 2012*

Jibu letu siyo refu sana. Kulingana na maelezo yenye utata uliyotupatia, hatuoni kwa nini usiweze kufanya kazi kwa mtu mwingine. Nani atailisha familia yako kama ukiacha kufanya kazi? Je, kuna kipengele kwenye mkataba wako kinachosema utalipwa hata kama utakuwa haufanyi kazi kwa kuwa huruhusiwi kufanyakazi kwa mtu mwingine? Mkataba wako unaweza kufanikiwa kama ungekuwa ni mkataba wa biashara lakini huu hauwezi kutekelezwa dhidi yako. Pia ni kipengele kisicho na maana kuwepo kwenye mkataba na kinaweza kuondolewa Mahakamani.

## Kufanya kazi siku ya sikukuu

**Ninafanya kazi kwenye Wizara fulani Dar es Salaam na wakati wa sikukuu ya Pasaka bosi wangu aliniita ofisini kwa kazi ya dharura. Sikuwa na hiari bali kuitikia wito. Je, ninaweza kuitwa kazini katika siku kuu kama hii?**

*3 Septemba 2012*

Sheria ya Siku za Mapumziko inatamka wazi kwamba itakuwa ni halali kwa Mkuu wa Idara ya Serikali kufungua ofisi siku ya sikukuu na kumuita mfanyakazi yeyote anayefanya kazi kwenye idara hiyo kufanya kazi kama ataona inafaa. Hivyo, kama aliyekuita alikuwa ni Mkuu wako wa Idara, anastahili kufungua ofisi na kumuita yeyote kwenye idara hiyo kufanya kazi. Ulisema kwamba kazi hiyo ilikuwa ya dharura, ambapo inampa mkuu wako wa idara sababu zaidi za kukuita ofisini.

## Kuachishwa kazi bila fidia

**Mwaka 2007, bosi wangu alinishuku kwamba nimeiba mali fulani za ofisi. Suala hilo liliripotiwa polisi na nilishtakiwa kwa kumwibia mwajiri. Kesi iliendelea kwa miaka mitatu na niliachiwa huru. Nilimfuata bosi wangu anilipe fidia kwa tuhuma alizonizushia lakini alikataa kabisa. Nifanye nini kurudisha kipato changu kwa kipindi cha miaka mitatu?**

*1 Oktoba 2012*

Kwanza kabisa kumuibia mwajiri ni kosa lenye dhamana. Hivyo madai yako ya kwamba ulikuwa unasubiri kuachiliwa na kuja na madai ya kipato cha miaka mitatu inaweza isiwe sawa. Una hiari ya kumfungulia shtaka la madai bosi wako au kampuni na kudai fidia ya shtaka la kukusudia/hila. Shtaka la kukusudia/hila ni kumfungulia mtu kesi ya jinai bila kuwa na sababu za msingi. Sheria hii ya madhara inaweka uwiano kati ya kanuni zinazoshindana, yaani uhuru wa kwamba kila mmoja ana wajibu wa kumfikisha mhalifu kwenye haki na hitaji la kuzuia tuhuma za uongo/husuda dhidi ya watu wasio kuwa na hatia.

Sheria inatoa haki kwa wale wote wanaoshtakiwa bila sababu na kwa makusudi. Ili uweze kufanikiwa, unatakiwa uthibitishe kwamba kulikuwa na mashtaka dhidi yako bila kuwa na sababu yoyote ya msingi, shtaka lilitungwa kwa makusudi na ulishinda kesi, na hakuna rufaa yoyote iliyokatwa. Ni muhimu kuthibitisha kwamba madhara uliyoyapata yamesababishwa na kushtakiwa. Kutokana na maelezo yako ni ngumu kusema kama mwajiri wako alikuwa na makusudi wakati alipokuripoti na iwapo alikuwa na sababu

za msingi kufanya hivyo. Wakati unafungua shauri lako unakumbushwa kuwa iwapo kesi yako ya shtaka la kukusudia likishindwa, utaamriwa kulipa gharama za kesi. Hivyo ni muhimu upate ushauri wa kitaalam kutoka kwa mwanasheria kabla ya kuchukua uamuzi wa kushtaki.

## Madhara mara mbili kwenye ajira

**Mimi ni Afisa Rasilimali-watu Mkuu kwenye moja ya makampuni ya madini yanayoongoza hapa Tanzania. Hivi karibuni wizi ulitokea kwenye kampuni yetu ambao uliripotiwa polisi. Watuhumiwa wengi wamekamatwa miongoni mwao ni wafanyakazi wetu (walinzi) na kufikishwa Mahakamani. Bado wameshtakiwa kwa kosa la kumuibia mwajiri wao. Bosi wangu anataka wafukuzwe kazi kwa sababu wao wenyewe kwa mdomo walimuomba awasamehe na kukiri kwamba wameshiriki kufanya uhalifu ule. Kiuhalisia wamekana shtaka la wizi Mahakamani. Je, ninaweza kuendelea na taratibu za kinidhamu dhidi yao? Tafadhali nishauri.**

*8 Oktoba 2012*

Sheria inayoongoza masuala ya ajira hasa Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini Na. 26 ya 2004 imetamka bila utata kwenye Kifungu cha 37 (5) kwamba hatua ya kinidhamu ya aina ya adhabu, kuachishwa au kufukuzwa haitachukuliwa kwa mfanyakazi ambaye anashtakiwa kwa kosa la jinai mpaka maamuzi ya mwisho ya Mahakama yatakapotolewa na rufaa inayohusiana na kesi hiyo.

Hivyo maamuzi yako unayokusudia dhidi ya wafanyakazi kama kweli yanahusiana na suala la wizi, yatakuwa ni kinyume cha kifungu cha sheria tulichokinukuu. Kifungu hicho kilikusudia kuwalinda wafanyakazi dhidi ya mashtaka/madhara mara mbili, lakini kuna baadhi ya maeneo ya sheria bado hayajajitosheleza. Mtaalam wako wa masuala ya ajira anaweza kukuongoza zaidi kwa sababu hakuna uwezekano wa kupenda kuendelea kuwa na wafanyakazi ambao wamekiri kwa bosi wako kuwa wamehusika kwenye tukio/wizi.

## Mkono wa kwaheri wakati wa kuachishwa kazi

**Niliajiriwa kwenye kampuni fulani ya ujenzi hadi nilipoachishwa kazi hivi karibuni. Nililipwa stahiki zangu zote isipokuwa mkono wa kwaheri (kiinua mgongo) ambao ninaamini nilipunjwa. Mwajiri wangu aliniambia alipiga hesabu kwa kuzingatia sheria za kazi na siyo kipengele cha kwenye mkataba wangu ambacho kinatamka kwamba malipo ya kiinua mgongo yatakuwa ni sawa na malipo ya miezi sita ya mshahara wangu wa wakati huo. Changamoto ni kwamba kama nitalipwa kiasi hicho kwa kuzingatia sheria za kazi, kiwango hicho kitakuwa ni kidogo zaidi tofauti na ambavyo ningelipwa kwa kufuata kilichopo kwenye mkataba wa ajira. Je, mwajiri ana haki ya kufanya hivyo? Nifanye nini?**

*22 Oktoba 2012*

Mkono wa kwaheri (malipo ya kiinua mgongo) ni miongoni mwa malipo ambayo mwajiri anastahili kulipa baada ya kuvunja mkataba wa ajira. Malipo hayo hata hivyo ni kwa mfanyakazi aliemaliza miezi 12 mfululizo ya utumishi na mwajiri huyo, na kwamba mkataba wake haujasitishwa kwa sababu za utendaji mbovu, uwezo, kutoendana au mahitaji ya uendeshaji ya mwajiri.

Ukokotoaji wa malipo ya kiinua mgongo kwa mujibu wa Sheria ya Kazi na Mahusiano Kazini Na. 6 ya 2004 ni kiasi cha mshahara wa angalau siku 7 kwa kila mwaka wa utumishi uliokamilika akiwa na mwajiri huyo mpaka kwa kiwango cha juu cha miaka kumi. Hivyo

kwa mtu aliyefanya kazi kwa miaka mitano, kiinua mgongo chake kitakuwa ni mshahara wake wa siku 35. Kama atafanya kazi kwa miaka 20, kiinua mgongo chake kitakuwa ni mshahara wake wa siku 70.

Kwa upande wako, tunadhani mwajiri wako hakuwa sahihi kutumia kikokotoo cha kisheria kama kikokotoo cha malipo ya kiinua mgongo kilikuwa wazi kwenye mkataba wa ajira na siyo chini ya siku 7. Kwa kifupi, sheria inatoa tu kikokotoo cha chini na haimzuii mwajiri kutumia kikokotoo cha juu zaidi ambacho kinampendelea mfanyakazi. Kwa kuzingatia hayo na kwa kuzingatia ukomo wa muda wa kushtaki, unaweza kupeleka suala lako kwenye Tume ya Usuluhishi na Uamuzi ili kupata amri ya kumlazimisha mwajiri wako kuheshimu mkataba wa ajira na kukulipa malipo ya kiinua mgongo chako kama inavyostahili.

Kitu kimoja zaidi cha kuzingatia. Kuna kanuni kwamba sheria inatawala dhidi ya mikataba ya pande ambazo zimeingia. Kauli hii ni lazima itafsiriwe kwa kuzingatia masharti ya sheria na mkataba. Kama sheria ingekuwa inasema mshahara wa siku saba ndo ukomo wa kiinua mgongo kwa mwaka, kipengele cha malipo ya kiinua mgongo kwenye mkataba wenu kingekuwa ni haramu. Sheria imeweka kima cha chini na hivyo kipengele cha malipo ya kiinua mgongo kwenye mkataba wako ni halali.

## Mkataba kwenye kadi ya orodha ya chakula (menu) mgahawani

**Mimi ni msaidizi wa mfanyabiashara mkubwa mjini. Siku moja tulitoka kwa ajili ya chakula cha mchana, aliniambia kwamba ninastahili motisha. Alichukua kadi ya orodha ya chakula ya mgahawa na nyuma yake aliandika jinsi motisha hiyo itakavyokuwa na masharti ninayotakiwa kuyatimiza. Nimetimiza masharti yote na sasa amekengeuka na kusema kwamba mkataba hauwezi kumfunga kwani haupo kwenye karatasi ya kisheria. Je, ni kweli? Kwa nini watu tajiri huvunja mikataba?**

*21 Januari 2013*

Inafurahisha sana kuona kwamba una mkataba nyuma ya kadi ya orodha ya chakula ya mgahawa. Mikataba mingine muhimu imewahi kuandikwa kwenye maeneo ya ajabu ulimwenguni kote - tumesikia mikataba iliyoandikwa kwenye magome ya miti, kwenye mchanga wa bahari, kwenye tishu iliyosainiwa bafuni na mikataba iliyoingiwa wakati watu wanapiga mbizi angani (hatujui waliwezaje kusaini). Maudhui muhimu ya mkataba ni kwamba lazima kuwepo na ofa, kukubaliwa, nia ya kuunda mahusiano ya kisheria, malipo na maudhui ya mkataba lazima yawe ya kisheria. Tunaona kwamba yote haya yapo kwenye mkataba wako na hivyo mkataba wako unamfunga bosi wako. Hakuna hitaji kwamba mkataba ni lazima uwe kwenye karatasi ya kisheria. Swali lako la mwisho la kwa nini matajiri wanavunja mikataba yao mara nyingi sio la kisheria na hatuwezi kulijibu. Hata hivyo nukuu ya mvumbuzi wa Ujerumani aliyeJulaikana kama Robert Bosch inakuja akilini mwetu na inasema kwamba "silipi mshahara mzuri kwa sababu nina fedha nyingi; nina fedha nyingi kwa sababu ninalipa mshahara mzuri".

## Kibali cha ukaazi na mabadiliko ya ajira

**Mimi ni mtaalam wa kigeni niliyeajiriwa kwenye kampuni fulani ambayo imenisaidia kupata kibali cha ukaazi daraja B ambacho kinaniwezesha kufanya kazi nchini Tanzania. Wakati ninafanya kazi nchini nimepata ofa nzuri kwenye kampuni nyingine na natamani kuhamia huko. Ninawezaje kuendelea na hili?**

*4 Februari 2013*

Sheria ya Uhamiaji inatamka wazi kwamba iwapo mtu mwenye kibali cha ukaazi daraja B ataacha kufanya kazi iliyoelezwa kwenye kibali au anafanya kazi kwa masharti yoyote nje ya kazi iliyopo kwenye kibali, uhalali wa kibali utakoma mara moja na uwepo wa mtu huyo nchini Tanzania utakuwa ni kinyume cha sheria. Hivyo, mara ajira yako inapokoma na kampuni yako ya sasa, kibali cha ukaazi pia kitakoma mara moja na utakuwa na siku 30 tu za kuondoka nchini. Ni lazima ukubali kwamba, kama mtaalam wa kigeni, sheria zetu hazikuruhusu kubadilibadili kazi. Siyo kwa maslahi ya taasisi iliyosajiliwa Tanzania unayofanyia kazi wala sera ya umma. Hata hivyo, ni lazima ieleweke kwamba, Mkurugenzi wa Uhamiaji ana hiari ya kurekebisha masharti ya kibali kama ataona inafaa. Unaweza kufanya maombi hayo kwa Mkurugenzi ili kupata idhini ya kufanya kazi kwenye kampuni nyingine. Ruhusa hii pia iambatane na barua ya kutokuwa na pingamizi kutoka kwa mwajiri wa sasa.

## Wafanyakazi kuunda chama cha wafanyakazi

**Nina kampuni kubwa yenye wafanyakazi wapatao hamsini. Kuna tetesi kwamba wafanyakazi wangu wanataka kuanzisha chama cha wafanyakazi wakivutwa na mfanyakazi mmoja, ambaye ndiye kinara wa hili wazo. Siungi mkono wazo hili kwa sababu ni vigumu kudhibiti. Ninawezaje kuwazuia kuunda chama cha wafanyakazi? Pia nataka kumuachisha kazi mfanyakazi huyu kwa utovu mkubwa wa nidhamu. Ninawezaje kuendelea na nia yangu?**

*4 Februari 2013*

Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini ya inaeleza kwamba kila mfanyakazi ana haki ya kujiunga na chama cha wafanyakazi na kushiriki katika shughuli halali za chama hicho. Aidha, sheria inakataza ubaguzi wa aina yoyote kwa mfanyakazi aliyejiunga na chama cha wafanyakazi au kushiriki katika shughuli halali za chama hicho.

Kutokana na matakwa ya sheria hapo juu, hauwezi ama kuwazuia wafanyakazi kuanzisha au kujiunga na chama cha wafanyakazi na wala hauwezi kumfukuza mfanyakazi kwa sababu tu ya kudai haki hizo. Ukifanya hivyo, utaishia kwenye Tume ya Usuluhishi na Maamuzi, na uwezekano mkubwa ni kuwa utashindwa katika shauri hilo. Inabidi ufanye maamuzi kwa tahadhari, kwa sababu hapa Tanzania, kama ilivyo katika nchi nyingine, ili umfukuze mfanyakazi inabidi ufuate utaratibu uliowekwa kisheria na uwe na sababu ya/za msingi za kumfukuza mfanyakazi. Mwanasheria wako anaweza kukupa mwongozo zaidi.

## Muda wa kuwasilisha shauri la kazi

**Niliachishwa kazi na ninahisi uamuzi huo haukuwa sahihi. Nimefikiri kwa muda nini cha kufanya na nimeambiwa kwamba naweza kuwasilisha mgogoro kwenye Mahakama ya Kazi ndani ya siku 30. Ninaogopa naweza kuwa nje ya muda kwa siku moja au mbili. Je, ninahitaji kuhesabu Jumamosi, Jumapili na siku za sikukuu? Tafadhali niongoze.**

*4 Februari 2013*

Unaonekana unataka kupinga kuachishwa kazi isivyo halali na hauna hakika jinsi siku 30 za kufungua malalamiko zinapaswa kuhesabiwa. Kanuni za Taasisi za Kazi (Usuluhishi na Uamuzi) zinaelezea namna ya kuhesabu siku. Kanuni hizi zinatamka kwamba kwenye kuhesabu siku, siku ya kwanza itaondolewa na siku ya mwisho itajumuishwa. Hata hivyo, siku ya mwisho itaondolewa kama inaagukia siku zaa Jumamosi, Jumapili au siku ya sikukuu. Kama muda umekwisha, sheria inakuruhusu kupeleka maombi ya kuongezwa muda isipokuwa unapaswa kutoa

sababu za msingi za kuchelewa. Unashauriwa kuwasiliana na mtaalam wa masuala ya kazi kwa mwongozo zaidi.

## Mfanyakazi kutokomea na taarifa tepevu (data) za kampuni

**Sisi ni kampuni ya programu ambayo imeajiri mafundi programu wengi jijini Dar es Salaam. Moja ya vipengele muhimu vya mkataba wetu ni kwamba mfanyakazi hawezi kuondoka ofisini na data za kampuni au funguo za programu. Hata hivyo, mfanyakazi mmoja mwandamizi ameondoka kwenye kampuni na kompyuta mpakato na amejiunga na mshindani wetu. Tunaweza kufanya nini?**

*18 Machi 2013*

Hali hii inatokea mara nyingi sana na sasa ni wakati muafaka kwa waajiri kuchukua hatua kali dhidi ya wafanyakazi hao ili liwe funzo kwa wafanyakazi wengine. Hatua tunazopendekeza hapa chini zinaweza kuonekana ni za gharama sana lakini ni muhimu kuzingatia ili usiweke mfano mbaya. Tunashauri umtaarifu mwajiri mpya juu ya uvunjifu huu na uwezekano wa uvunjifu ambao mwajiri huyo anajihusisha nao. Kama mwajiri mpya hatazingatia, tunashauri uwashtaki wote wawili, mfanyakazi wako wa zamani pamoja na mwajiri wake mpya chini ya sheria za mikataba au madhara, ukiwadai fidia, miongoni mwa nafuu nyingine. Unapaswa kuandaa ushahidi wako vizuri - kwa mfano, ukweli kwamba ameondoka na kompyuta mpakato ni moja ya ushahidi muhimu ambao unaweza kuongeza uzito. Wanasheria wako wanaweza kukuongoza zaidi. Unaweza pia kuangalia uwezekano wa kutoa taarifa polisi kwa sababu inaonekana kama kuna ujinai vile vile.

## Malipo ya muda wa ziada benki

**Nilikuwa meneja wa tawi la benki nchini Tanzania. Hivi karibuni nilifukuzwa na ninataka kudai malipo ya masaa yote niliyofanya kazi zaidi ya masaa rasmi. Je, nina madai halali?**

*22 Aprili 2013*

Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini inatamka kwamba mwajiri hatakiwi kumtaka au kumruhusu mfanyakazi kufanya kazi kwa masaa zaidi ya 12 kwa siku. Na kwamba, kiwango cha juu katika siku za kawaida au saa ambazo mfanyakazi anaweza kuruhusiwa au kutakiwa kufanya kazi ni - siku sita katika wiki yoyote; saa 45 katika wiki yoyote; na masaa tisa katika siku yoyote.

Hata hivyo Sheria hiyo hiyo inakwenda mbali zaidi na kuondoa kutumika vifungu vya hapo juu kwa wafanyakazi wanaowasimamia wafanyakazi wenzao kwa niaba ya mwajiri na ambao wanaripoti moja kwa moja kwa uongozi wa juu.

Hivyo kwa suala lako, hakuna uwezekano kwamba madai yako ya malipo ya saa za ziada yanaweza kukubaliwa - wanasheria wako wanaweza kukuongoza zaidi.

## Kumbukumbu ya kuzaliwa, siku yangu mbaya

**Nimekuwa nikifanya kazi kwenye kampuni fulani kwa miaka kumi, na wakati wote nimekuwa nikipewa mapumziko kila ifikapo kumbukumbu ya siku yangu ya kuzaliwa. Hivi karibuni bosi wangu amebadilika, na bosi huyu mpya amezuia mapumziko yangu ya kisheria. Jambo hili limenikasirisha sana kwa kuwa ni siku yangu maalum, kama ilivyo kwa mtu mwingine yeyote. Ninaweza kufanya nini juu ya kunyimwa haki yangu ya kupata likizo ya siku ya kuzaliwa?**

*13 Mei 2013*

Jibu tunalotaka kukupatia halitakufurahisha. Hakuna likizo ya siku ya kuzaliwa kwenye sheria zetu. Iwapo mkataba wako wa ajira unatamka kwa uwazi kwamba likizo

hiyo ipo, utakuwa na madai, lakini hata sisi hatujawahi kuona mkataba wa namna hiyo. Tuonavyo, likizo yako ya kumbukumbu ya kuzaliwa ilikuwa ya kimazoea zaidi kuliko kimkataba. Hatujawahi kusikia nchi yeyote yenye likizo ya aina hiyo. Hatuoni kama una madai yoyote dhidi ya mwajiri, wanasheria wako wanaweza kukuongoza zaidi.

## Kuazima/kukodi wafanyakazi

**Baada ya kuingia mkataba na kampuni ya kutusambaza/kuazimisha wafanyakazi, Mamlaka ya Mapato wamekuja na kudai kwamba fedha tulizolipa kwa mtoa huduma huyu kimsingi ni mishahara ya wafanyakazi tuliopewa na hivyo walitakiwa kutozwa kodi, kulipiwa pensheni ikiwemo tozo ya kuendeleza ufundi stadi. Sheria inamtafsiri vipi mfanyakazi, na je, Mamlaka ya Mapato wana madai halali juu yetu? Je, ni halali kwa kampuni yetu kuingia makubaliano ya namna hayo?**

*27 Mei 2013*

Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini inamtafsiri mfanyakazi kama ni mtu ambaye (a)ameingia kwenye mkataba wa ajira; au (b) ameingia kwenye mkataba mwingine wowote ambapo (i) mtu huyo anatakiwa kufanya kazi yeye binafsi kwa ajili ya mtu wa upande mwingine wa mkataba na (ii) upande mwingine huo si mteja wa taaluma yoyote, biashara, au kazi inayofanywa na mtu; au (c) anachukuliwa kuwa ni mfanyakazi na Waziri kwa mujibu wa kifungu cha 98(3).

Kifungu cha 98 (3) kinatamka kwamba Waziri, baada ya kushauriana na Baraza, anaweza, kwa notisi katika Gazeti la Serikali, kuwafanya watu fulani kuwa waajiriwa kwa madhumuni ya kifungu hiki, masharti yoyote ya Sheria hii au sheria nyingine yoyote ambayo Waziri anawajibika. Chini ya sheria za kazi za Tanzania mtu anayempa huduma mtu mwingine ikiwemo kazi maalum anachukuliwa kuwa mwajiriwa mpaka pale inapothibitishwa vinginevyo kama moja au zaidi ya dhahania zilizoainishwa chini ya kifungu cha 61 cha Sheria ya Taasisi za Kazi zipo.

Kifungu cha 61 cha Sheria ya Taasisi za Kazi Na. 7 ya mwaka 2004 kinatamka: Kwa mujibu wa sheria ya ajira, mtu ambaye anafanya kazi au anatoa huduma kwa mtu yeyote anayedhaniwa, mpaka itakapothibitishwa vinginevyo, kuwa ni mfanyakazi, bila kujali aina ya mkataba, ikiwa moja ya au zaidi ya vigezo vifuatavyo vitakuwepo; (a) namna ya mtu anavyofanya kazi chini ya uangalizi au maelekezo ya mtu mwingine; (b) masaa ya kazi ya mtu yako chini ya uangalizi au maelekezo ya mtu mwingine; (c) labda ikiwa kuna mtu anafanya kazi kwenye chama mtu huyo ni sehemu ya chama hicho; (d) mtu anayefanya kazi kwa mwingine kwa wastani wa masaa angalau 45 kwa mwezi kwa kipindi cha miezi mitatu iliyopita; (e) mtu ni tegemezi kiuchumi kwa mtu mwingine ambaye anafanya kazi au anatoa huduma; (f) mtu amepewa vifaa vya biashara au dhana za kazi na mtu mwingine; au (g) mtu anafanya kazi au anatoa huduma kwa mtu moja tu.

Kutokana na maelezo mafupi hapo juu, mtoa huduma amewaajiri wafanyakazi hawa ambao wapo kwenye ofisi yako. Hatuoni ubatili wowote kwenye mkataba mlioingia, kama mtoa huduma amesajiliwa kwa madhumuni ya kodi na analipa kodi. Hata hivyo, kama mtoa huduma hajasajiliwa kulipa kodi, Mamlaka ya Mapato itaishia kukufuata wewe. Wanasheria wako wanaweza kukuongoza zaidi.

## Kustaafu kwa lazima kwa wakurugenzi wenye miaka 70

**Nimekuwa mkurugenzi wa kampuni nchini Tanzania tangu nilipokuwa na miaka 30. Uteuzi ulifanywa na mmiliki mwenye hisa nyingi ambaye pia alikuwa ni rafiki yangu**

**na nimekuwa nikifurahia posho kwa miaka 40. Mmiliki mwenye hisa nyingi alifariki na mwanae amekuwa si mwema kwangu. Hapo mwanzoni, kutokana na uzoefu na cheo changu, hakunifukuza ukurugenzi, lakini baada ya kutimiza miaka 70 ameniomba niachie ngazi kwa sababu sheria hairuhusu mkurugenzi kutumikia akiwa na umri zaidi ya miaka 70. Ninawajua mamia ya watu wenye miaka zaidi ya 70 na bado ni wakurugenzi. Sheria hii, kama ni kweli, imepitwa na wakati. Je, sheria hiyo ipo? Nimeangalia Katiba na Kanuni za kampuni nazo pia zinatamka umri wa kustaafu ni miaka 70. Ninaweza kupata amri ya zuio ya Mahakama kwa sababu bado nahitaji sana posho/malipo yangu ya ukurugenzi.**

*10 Juni 2013*

Kifungu cha 194 cha Sheria ya Makampuni kinatamka ifuatavyo miongoni mwa mambo mengine, kwamba; (1) Kwa kuzingatia masharti mengine ya kifungu hiki, hakuna mtu atakayeweza kuteuliwa kama mkurugenzi wa kampuni chini ya kifungu hiki iwapo wakati wa uteuzi wake alikuwa hajatimiza umri wa miaka ishirini na moja au ametimiza umri wa miaka sabini. (2) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu hiki kama ilivyoelezwa kabla, mkurugenzi wa kampuni ambaye yuko chini ya kifungu hiki atalazimika kuacha kazi yake wakati wa kuhitimisha mkutano mkuu wa kuanzia mwaka wa pili baada ya kufikia umri wa miaka sabini: Isipokuwa kwamba matendo yaliyofanywa na mtu akiwa mkurugenzi yatakuwa halali bila ya kujali kwamba baadaye itagundulika na kwamba uteuzi wake ulikuwa umesitishwa kwa mujibu wa kifungu hiki. Kifungu hiki kama kitasomwa pamoja na Katiba na Kanuni za Kampuni, ambacho ulisema kwamba umri wa kustaafu ni miaka 70, vinakulazimisha kustaafu kwa lazima.

Kifungu cha 194 (5) ni kifungu kinachokuokoa ambacho kinatamka kwamba hakuna chochote katika masharti yaliyotangulia ya kifungu hiki kitakachozuia uteuzi wa mkurugenzi katika umri wowote, juu ya umri wa miaka kumi na nane au kumtaka mkurugenzi kustaafu wakati wowote, kama uteuzi wake ni au ulifanywa au kuthibitishwa na kampuni katika mkutano mkuu, lakini taarifa maalumu itahitajika kuhusu azimio la kumteua au kuidhinisha uteuzi wa mkurugenzi kuweza kutumika kwa madhumuni ya kifungu kidogo hiki na taarifa yake iliyotolewa na kampuni kwa wanachama lazima ieleze au lazima iwe imeeleza umri wa mtu ambaye inamuhusu. Hivyo kama Kampuni ikipitisha azimio la kubadili ukomo wa umri wa miaka 70, unaweza kuendelea. Unaweza kumshawishi mtoto wa rafiki yako ili uendelee kukaa.

Kuhusu suala la kupata amri ya Mahakama ili uendelee kubaki kama mkurugenzi, tafadhali elewa kwamba wakurugenzi wanateuliwa na wanahisa na mwanahisa ana mamlaka kamili ya kuteua au kuwaondoa wakurugenzi. Hakuna uwezekano kwenye kesi yako kwa Mahakama kuweza kuingilia kwa sababu tu kwamba kipato chako pekee ni mshahara wa ukurugenzi. Wanasheria wako wanaweza kukuongoza zaidi.

## Mfanyakazi anakataa kufanya kazi wakati wa notisi

**Ninamiliki kampuni ya ushauri yenye wateja wakubwa. Hivi karibuni mmoja wa wafanyakazi wangu alinipa notisi ya kusitisha ajira yake. Hata hivyo, baada ya kutoa notisi hafanyi tena kazi anazopangiwa kwa sababu kwamba anaacha kazi kwenye kampuni yangu. Mwishowe ameanza kuchelewa na wakati mwingine hafiki kabisa kazini. Mfanyakazi anaweza kukataa kufanya kazi kwa sababu tu ametoa notisi ya kuacha kazi? Sheria za kazi zinasemaje?**

*17 Juni 2013*

Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini inatamka wazi kwamba kama mfanyakazi atakataa kufanya kazi wakati wa kipindi cha notisi, mwajiri anaweza kukata kutoka kwenye fedha yoyote inayodaiwa na mfanyakazi huyo wakati wa kusitishwa ajira, sawa na kiasi ambacho kingedaiwa na mfanyakazi kama mfanyakazi huyo angefanya kazi wakati wa kipindi cha notisi.

Kama muda wa notisi usingekuwa mfupi hivyo, ungekuwa na haki ya kuvunja mkataba wa ajira kwa msingi wa utendaji mbovu kwa mujibu wa taratibu za kisheria. Sababu tu kwamba mfanyakazi anaacha kazi haina maana kwamba afanye anachotaka. Kesi na sheria za kazi zinamtaka mwajiri na mfanyakazi kuheshimu mkataba wa ajira uliopo wakati wa kipindi cha notisi.

## Uvujishaji wa siri za kampuni

**Ninamiliki kampuni na nimeajiri maafisa waandamizi kwa ajili ya kujadiliana mikataba. Kwa zaidi ya miaka miwili tumekuwa tukipata hasara kwa sababu ambazo hazikuwa wazi. Hivi karibuni nimegundua maafisa wangu wawili wamekuwa wakivujisha taarifa kwa washindani wetu ili kujinufaisha kifedha. Ninataka kuwafukuza kazi. Je, itakuwa ni halali? Zipi ni taratibu za kuwafukuza wafanyakazi hao?**

*8 Julai 2013*

Sheria zetu za kazi zinatamka kwamba kusitisha mkataba kunawezekana kama tu kuna sababu za msingi na za halali ambazo zinalazimisha usitishaji lakini taratibu halali kabla ya kuwafukuza ni lazima zizingatiwe. Kwa taarifa ulizotupatia, afisa mwandamizi amevunja mkataba wa ajira na hivyo anawajibika kwa utendaji mbovu ambao ni sababu ya msingi ya kuchukua hatua za kinidhamu dhidi yake. Taratibu halali kabla ya kufukuza zinamtaka mwajiri kufanya uchunguzi wa kina juu ya tuhuma na kumpa ripoti mfanyakazi husika. Kikao cha nidhamu ni lazima kifanyike na baada ya kumsikiliza, unaweza kuamua kumfukuza. Ni muhimu kuwa na ushahidi wa kutosha juu ya tuhuma ulizoeleza vinginevyo kama utashtakiwa na mfanyakazi kwa kumwachisha kazi isivyo halali, unaweza kumlipa mishahara ya miezi 12 kama fidia. Si vibaya, kupata ushauri wa mtaalam wa masuala ya kazi ili aweze kukusaidia kwenye mchakato huu.

## Kukosekana kwa usawa wa muda wa notisi kwenye ofa ya ajira

**Mimi ni mhasibu wa shirika la umma na nimepokea ofa ya ajira kutoka kampuni ya kigeni kwenye sekta ya madini. Wakati bado natafakari iwapo nikubali au la, nimegundua vitu vichache vya ajabu kwenye barua yao ya ofa. Mojawapo ni kwamba kama ninataka kusitisha mkataba wangu wa ajira ninatakiwa kutoa notisi ya miezi mitatu. Ila kama kampuni inataka kusitisha mkataba itanipatia notisi ya miezi miwili tu au mshahara wa miezi miwili badala ya notisi. Je, hii ni sawa kwenye sheria za kazi? Naona kama kampuni inanufaika kuliko mimi. Nimeambatanisha barua ya ofa ili uipitie na kunijibu. Tafadhali niongoze.**

*15 Julai 2013*

Kifungu cha 41 cha Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini Na. 6 ya 2004 kinajibu swali lako kwa uwazi. Kifungu hiki kinatamka kwamba kama mkataba wa ajira unaweza kusitishwa kwa notisi, muda wa notisi hautakuwa pungufu ya siku saba, kama notisi inatolewa katika mwezi wa kwanza wa ajira; na baada ya hapo- siku nne, kama mfanyakazi ameajiriwa kwa mkataba wa siku au wiki; au siku 28, kama mfanyakazi ameajiriwa kwa mkataba wa mwezi.

Sheria hii pia inaruhusu mkataba kutoa muda wa notisi ambao ni mrefu kuliko unaotakiwa hapo juu ikiwa, muda wa notisi uliokubaliwa ni sawa kwa wote; mwajiri na mfanyakazi. Unaweza kumfahamisha mwajiri wako mtarajiwa juu ya hili inaweza kuwa walipitiwa kwa upande wao. Hatupo kwenye nafasi ya kuupitia mkataba wote lakini tunapenda kukutahadharisha kwamba barua yako ya ajira inatamka wazi kwamba hautakiwi kuisambaza kwa wasiohusika, kitu ambacho wewe umekwishakifanya. Unatakiwa uwasiliane na wanasheria wako kwa maoni ya kina.

## Kusafiri kwa daraja la biashara dhidi ya daraja la kawaida

**Bosi wangu ananibagua ingawa mimi ni mkuu wa idara ya fedha. Yeye ni mtendaji mkuu wa kampuni ambayo nafanyia kazi na wakati tukiwa na safari ya kazi, yeye anasafiri daraja la biashara wakati mimi ananitupa kwenye daraja la kawaida lisilo na starehe. Je, tabia hiyo ya mwajiri wangu siyo ya kibaguzi? Nataka nimshtaki mwajiri wangu?**

*15 Julai 2013*

Kabla hujakimbilia kuhitimisha kuhusu ubaguzi, ambao tunakubali kwamba unatambulika kwenye sheria zetu za kazi, ni lazima uelewe kwamba ubaguzi unatakiwa uangaliwe kwa mazingira ya kila kesi vinginevyo maamuzi mabaya yanaweza kufungua mafuriko ya mashtaka kwa waajiri. Kwenye kesi yako unahitaji kuangalia sera ya kampuni kuhusu safari, ni daraja gani wakuu wengine wa vitengo wanasafiri nk. Ni kawaida kwa mabosi kusafiri daraja la biashara na wengine daraja la kawaida . Ni moja ya raha za kuwa bosi. Kwa mfano bosi anaweza kuwa na meza kubwa na ofisi, gari kubwa, msaidizi binafsi, mshahara mkubwa na vyote hivi vinaweza visiwe ubaguzi. Kabla hujawa na hisia za kuishtaki kampuni yako, tunakushauri uangalie hali halisi kwa ujumla na uwasiliane na mtaalam wako wa masuala ya kazi.

## Kazi hatarishi kwa mjamzito

**Mimi ni fundi kwenye kampuni ambayo nimekuwa nikifanya kwa muda wa miaka minne sasa. Ingawa msimamizi anajua kwamba kwa sasa ninatarajia kujifungua miezi miwili ijayo, amekuwa akinipa kazi ngumu na za kusimama kwa masaa mengi. Ninajua ananifanyia kusudi kwa sababu dada yangu alikataa kuolewa nae. Kuna lolote ninaweza kufanya kutatua suala hili?**

*5 Agosti 2013*

Tunataka kukueleza kwamba Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini inatamka wazi kwamba mwajiri haruhusiwi kumtaka au kumruhusu mfanyakazi mjamzito au mfanyakazi anayenyonyesha mtoto kufanya kazi katika mazingira hatarishi kwa afya yake au ya mtoto wake.

Kipimo hicho hapo juu ni tegemezi, inategemea na aina gani hasa ya kazi unayopewa. Yote kwa yote, kama kazi unazopewa ni hatari kwa ujauzito wako, hiyo ni kinyume na sheria na msimamizi wako anatakiwa kuacha tabia hiyo.

Ili kutengeneza mazingira mazuri ya kazi na kuzuia matumizi mabaya ya madaraka, unaweza kutoa taarifa juu ya hili kwa mkubwa wako, vinginevyo unaweza kushtaki kama ilivyoelezwa hapo juu.

Katika hali nyingine, kama unategemea kujifungua ndani ya mwezi mmoja tunashangaa kwa nini bado upo kazini. Sheria hiyo hiyo inakupa hiari ya kuanza likizo ya uzazi muda wowote ndani ya wiki nne kabla ya tarehe ya kujifungua. Hivyo, unaweza kumuomba mwajiri wako kuanza likizo ya uzazi. Wanasheria wako wanaweza kukuongoza zaidi.

## Mwajiri mkali muda wa kunyonyesha

**Mimi ni mama wa mapacha naishi nje kidogo ya jiji la Dar na nimeanza kazi hivi karibuni baada ya kumaliza likizo yangu ya uzazi. Hata hivyo, magumu ninayokumbana nayo kwa sasa hayavumiliki kwa sababu afisa rasilimali-watu ameniambia kwamba sera ya kampuni inaruhusu masaa mawili tu ya kunyonyesha ikiwemo muda wa chakula cha mchana. Hivyo muda wa kunyonyesha, muda wangu wa chakula cha mchana wa saa moja pia upo ndani yake. Je, hii ni kwa mujibu wa sheria za kazi? Tafadhali niongoze.**

*19 Agosti 2013*

Sheria ya Kazi na Mahusiano Kazini Na 6 ya mwaka 2004 ipo wazi kwenye kifungu cha 33(10), inaeleza kwamba kama mfanyakazi ananyonyesha mtoto, mwajiri atalazimika kumruhusu kumnyonyesha mtoto wakati wa saa za kazi kwa muda wa masaa mawili kwa siku. Sheria haijasema kwamba masaa mawili yanahusu muda wa chakula cha mchana, na kama ingekusudia ingesema kwa uwazi. Sera ya kampuni yenu haiendani na kifungu hiki. Muda wa kunyonyesha ulikusudiwa kwa mtoto na chakula kwa mfanyakazi. Unaweza kumfahamisha afisa rasilimali-watu ili sera ya kampuni irekebishwe kuendana na vifungu vya sheria. Vinginevyo unaweza kuomba msaada zaidi kutoka kwa mwanasheria au afisa kazi kama kampuni yako itaendelea kushikilia msimamo wake.

## Ninampenda bosi wangu

**Ninafanya kazi kwenye kampuni kubwa na nipo kwenye mahaba mazito na bosi wangu. Ni mtu bora sana kuwahi kuonana nae. Yeye pia ananipenda na tumetumia nyakati fulani kuwa pamoja. Tatizo pekee ni kwamba anasema kwa kuwa yeye ni bosi na mimi ni msaidizi wake, ni kinyume cha utaratibu yeye kujihusisha na mimi kimapenzi. Je, sheria inamzuia kufanya hivyo? Ninawezaje kumfanya awe wangu?**

*23 Septemba 2013*

Hatujui sheria yoyote ambayo inamzuia bosi kutembea na msaidizi wake. Kimsingi, kuna hadithi nyingi ambapo bosi hasa anamuoa msaidizi wake. Tatizo ni kwamba baadhi ya makampuni yana kanuni/sera ama taratibu zake za ndani ambapo mahusiano ya namna hiyo yanaonekana kutokuwa sahihi, na taratibu za makampuni husika zinazuia hilo. Kwa mfano, kama wewe na bosi wako mpo kwenye mahusiano inaweza kukufanya usijikite kwenye kazi yako, n.k. Katika kujibu hili tunachukulia wote hampo kwenye ndoa. Kwa bahati mbaya kama wanasheria hatuna sifa za kujibu swali lako la pili na namna gani tunaweza kukusaidia awe hawara yako.

## Posho ya usafiri kurejea mahali nilipoajiriwa

**Niliajiriwa na kampuni fulani ya madini na kituo changu cha kazi kilikuwa ni Dar es Salaam mpaka mkataba wangu ulipositishwa. Niliajiriwa kutoka Kigoma ambako ndiko nilikokuwa nafanyia kazi na kuishi. Kampuni hii kwa sasa inakataa kuilipia familia yangu posho ya safari kwenda kigoma wakati ilikuwa inaJulaikana wazi kwamba nilihamia Dar es Salaam na familia yangu wakati naajiriwa. Je, mwajiri yuko sawa juu ya maamuzi haya?**

*23 Septemba 2013*

Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini Na. 6 ya 2004 ipo wazi kwenye kifungu cha 43 (1) ikieleza kwamba kama mkataba wa mfanyakazi umesitishwa katika mahali ambapo sipo mfanyakazi alipoajiriwa, mwajiri atatakiwa aidha, kumsafirisha mfanyakazi na vitu vyake kwenda sehemu aliyoajiriwa; kulipa gharama za usafirishaji wa mfanyakazi kwenda mahali alipoajiriwa; au kumlipa mfanyakazi posho ya usafiri kwenda sehemu

aliyoajiriwa na posho ya gharama kwa kila siku wakati wa kipindi, kama kipo, kati ya tarehe ya kusitishwa kwa mkataba na tarehe ya kumsafirisha mfanyakazi. Usafirishaji wa familia umeelezwa kwa uwazi, kukataa huko kunakufanya ustahili kulipwa posho ya kujikimu kuanzia siku ya kusitishwa kazi mpaka siku ya kulipwa/kusafirishwa.

Sheria pia inatamka kwa uwazi kuwa nauli itakuwa sawa sawa na angalau nauli ya basi kwenda kituo cha basi kilicho karibu na sehemu uliyoajiriwa. Hata kesi za kisheria pia zinawataka waajiriwa wanaodai posho wanazolipwa za kurudi sehemu walikoajiriwa au fedha inayolipwa kwa ajili ya kujikimu haitoshi wanashauriwa kupunguza hasara inayotokana na kuedelea kukaa kwenye vituo vyao vya kazi. Mwanasheria wako anaweza kukuongoza zaidi.

## Jinsi ya kuthibitisha mimi ni Mtanzania

**Nimezaliwa katika Mkoa wa Mwanza miongo michache iliyopita na tangu wakati huo nimeishi na kukaa Tanzania. Baba yangu na mama yangu wote ni watanzania ingawa wa makabila tofauti. Mimi ni mfanyabiashara na biashara zangu zinanitaka kusafiri sehemu mbalimbali ndani ya nchi hasa kwenye mikoa ya mipakani. Baada ya kusikia kwamba wahamiaji haramu wanafukuzwa nchini, nina hofu kwamba naweza kuwa mmoja wa waathirika kwa sababu marafiki zangu wengi wananiambia kwamba nafanana na watu wa nchi jirani. Ninawezaje kuthibitisha kwamba mimi ni Mtanzania? Tafadhali niongoze.**

*30 Septemba 2013*

Sababu tu kwamba unafanana na watu wa nchi jirani haimaanishi kwamba wewe siyo Mtanzania. Hapa nchini masuala ya uraia yanaongozwa kisheria na kwa maana hiyo Sheria ya Uraia (Sura 357 iliyorekebishwa mwaka 2002) inahusika. Hakuna sheria inayosema Mtanzania lazima awe na mwonekano wa namna fulani.

Kwa ujumla, sheria zetu zinatambua aina tatu za uraia ambazo ni uraia wa kuzaliwa, uraia wa kurithi na uraia wa tajnisi. Mtu yeyote aliyezaliwa Tanzania anachukuliwa kuwa ni raia wa Jamhuri ya Muungano kama wakati wa kuzaliwa baba yake au mama yake alikuwa ni raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pia, mtu yeyote aliyezaliwa nje ya Jamhuri ya Muungano siku au baada ya siku ya Muungano atachukuliwa kuwa ni raia wa Jamhuri ya Muungano kwa kurithi kama mmoja wa wazazi wake ni raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuzaliwa au kwa kujiandikisha. Mwisho, mtu yeyote ambaye siyo raia wa Tanzania, ama kwa kuzaliwa au kwa kurithi anaweza kuomba uraia wa Tanzania wa kujiandisha kwa Waziri anayehusika na masuala ya uraia.

Aidha, Sheria ya Uraia ya Tanzania inatoa uwezekano wa kutoa hati ya uraia/ukaazi ili kuondoa shaka. Sheria hii chini ya kifungu cha 21 inatamka kwamba, Waziri anaweza, kwa mazingira yoyote anayoona yanafaa, kwa maombi ya mtu yeyote ambaye uraia wake wa Jamhuri ya Muungano una mashaka, iwe kwenye suala la maelezo ama kisheria, atathibitisha kwamba mtu huyo ni raia wa Jamhuri ya Muungano; na hati iliyotolewa chini ya kifungu hiki, isipokuwa kama ilitolewa kwa njia ya udanganyifu au kuficha maelezo ya msingi, lakini bila kuathiri ushahidi wowote kwamba alikuwa ni raia kwa siku ya awali.

Kutokana na hayo, tunaamini isikuwie vigumu kuthibitisha uraia kwa sababu maelezo yako yanajieleza yenyewe. Hivyo, tunakushauri ufuatilie mchakato wa kuwa na cheti cha kuzaliwa na kitambulisho kutoka mamlaka husika kama bado hujafanya hivyo. Wanasheria wako wanaweza kukuongoza zaidi.

## Kumfukuza mhudumu wa mapokezi kwa sababu ya ubonge

**Mimi ni mfanyabiashara maarufu nchini Tanzania mwenye biashara za rejareja kwenye mikoa mbalimbali ndani ya nchi. Kwenye ofisi yangu ya mauzo nimeajiri warembo kama wahudumu wa mapokezi nikijua kwamba yeyote anayekuja ofisini kwangu atavutiwa na kunipa dili. Mmoja wa wafanyakazi wangu ambaye ni mhudumu wa mapokezi ameongezeka sana uzito kiasi kwamba amepoteza mvuto. Kwa bahati mbaya ameajiriwa kwa mkataba wa kudumu. Ninawezaje kumuondoa kwa sababu najua ataendelea kuwa mnene kila siku?**

*14 Oktoba 2013*

Ingawa umeajiri warembo kukufanyia kazi kama moja ya mkakati wako wa soko, linapokuja suala la kusitisha ajira ya mfanyakazi, sheria za kazi zinaendelea kutumika na zinatakiwa zifuatwe. Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini inataka kila usitishaji wa mkataba wa ajira ufanyike kwa haki, kinyume na hapo itakuwa ni ubatili. Kwa kusitisha ajira kwa haki , sheria inataka kwanza kuzingatia na kufuata taratibu halali kama ilivyo elezwa kwenye sheria na pili kuwa na sababu za msingi za kusitisha. Tukija kwenye swali ulilouliza, hatuoni kama utaweza kumuachisha kazi kwa mjibu wa sheria mfanyakazi huyu. Hujatuambia iwapo uzito wa mfanyakazi wako umemfanya ashindwe kutekeleza majukumu yake au umepelekea utendaji mbovu wa kazi. Tunafikiri pamoja kuwa kitendo cha kumfukuza msichana huyo kwa sababu ya unene ni cha kibaguzi, vile vile hakikubaliki kutokana na kukosekana kwa sababu za msingi kusitisha ajira yake. Kama hutaki aendelee kuwa mapokezi unaweza kuzungumza naye na kumpatia majukumu mengine kama inakubalika. Vinginevyo unatakiwa kuwa muwazi kwa mfanyakazi wako kuhusu uzito wake, mpeleke kwenye madarasa ya kupunguza uzito ikiwemo kumuunganisha jimu, vyakula n.k.

Yote kwa yote, kama kwa mfano ukiwa wakala wake wa urembo, na kuongezeka uzito hakumwezeshi kutekeleza majukumu yake, na kwa bahati mbaya watu wanene kwa kawaida hawana mvuto kama walivyo wembamba. Hivyo, kwa kuzingatia utendaji kazi halisi wa mfanyakazi, unaweza, kabla ya kumpa nafasi ya kupunguza uzito, kusitisha ajira yake lakini ni lazima ufuate taratibu sahihi chini ya sheria. Wanasheria wako wanaweza kukuongoza zaidi.

## Mwajiri anafuatilia/anadukua meseji za simu kwa siri

**Niliajiriwa kwenye kampuni fulani kama Afisa Masoko na Mauzo. Kampuni ilinipatia simu za kisasa kwa ajili ya matumizi na namba yangu binafsi ilikuwa ikitumika. Sikujua kama kampuni inadukua meseji zangu kwenye simu hadi siku nilipogombana na mmoja wa mabosi zangu. Hii ni baada ya bosi kugundua na kuanza kunituhumu kutembea na mfanyakazi mwenzangu, ambaye ni mpenzi wake kitu ambacho nilikuwa sijui. Sasa nimepewa notisi ya kueleza ni kwa nini natumia simu ya ofisi kusababisha vurugu kazini kwa kuingilia uhusiano wa mapenzi ya bosi wangu. Ninaogopa kwamba ninaweza kufukuzwa juu ya jambo hili. Je, kampuni inaweza kupata taarifa kama hizo kutoka kwenye kampuni ya simu hata kwenye masuala kama haya ya maisha ya kimapenzi ambayo hayahusiani na kazi? Tafadhali niongoze vyema kwa sababu bosi amedhamiria kukabiliana na mimi.**

*14 Oktoba 2013*

Tunaamini kampuni ilikupa simu ili kazi zako zifanyike kwa ufanisi. Hatuna uhakika wa namna kampuni ilivyopata meseji hizo, lakini uwezekano ni mkubwa kwamba mtoa

huduma za simu, ambaye ndiye mtunzaji pekee wa taarifa hizo tunayemjua, alitoa nakala kwa bosi wako.

Yote kwa yote, huko hasa ni kuingilia faragha na kuna wajibu chini ya Sheria ya Mawasiliano Kielektroniki na Posta na Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Ulinzi kwa Watumiaji), 2011, ambazo zimetungwa chini ya Sheria hii. Uingiliaji huu wa faragha ni jambo kubwa na unaweza kufikiria na kufungua malalamiko kwa Mamlaka ya Mawasiliano (TCRA) dhidi ya kampuni ya mawasiliano na mwajiri wako.

Kuhusu notisi ya kueleza sababu iliyotolewa kwako, kwanza tunapenda kueleza kwamba labda kama kuna taarifa zimekosekana kwenye swali lako, notisi hiyo imejikita kwenye masuala ambayo hayahusiani na masuala ya kazi, labda kama mlikuwa mnashiriki mapenzi katika saa za kazi. Inaonekana ni bosi wako ndiye anayekufuatilia na siyo kampuni unayoifanyia kazi.

Mwisho, hujatuambia kama tuhuma za kutembea na mpenzi wa bosi wako ni za kweli au la. Kama ni kweli, unapaswa kuwa makini na matokeo ya utendaji kazi wako. Mara nyingi, mahusiano ya ofisini yanaweza kupunguza ufanisi, kitu kinachoweza kuwa sababu halali ya kufukuzwa kazi. Tunaamini hujatoa taarifa zote za kutuwezesha kujibu swali lako kwa ufanisi na tunashauri ueleze kila kitu kwa mwanasheria wako kwa mwongozo sahihi.

## Viza ya kutembelea mwezini

**Nimeambiwa kwamba kwa kuwa Marekani ndilo taifa la kwanza kwenda mwezini, na kusimika bendera yake huko, ili kuzuru mwezini basi unahitaji viza ya Marekani. Je, hilo ni kweli?**

*21 Oktoba 2013*

Swali lako ni la kufikirika sana. Kwa uelewa wetu, hakuna mtu aliyewahi kuwa na umiliki wa mwezi. Kimsingi, mataifa ya kwanza kutembelea mwezini, Urusi na Marekani, pia ni wanachama wa Mkataba wa Anga za Nje ambao unaeleza kwamba mwezi pamoja na vitu vingine vyote vya anga za nje ni mali ya binadamu wote. Pia kuna Mkataba wa Mwezi wa mwaka 1979 ambao uliweka zuio kwa matumizi ya rasilimali za mwezi kwa taifa moja.

Ingawa ni kweli kwamba mwaka 1969 Marekani ilichomeka bendera yake mwezini, kitendo hicho hakiipi Marekani umiliki wa mwezi na wala Marekani yenyewe haijawahi kudai kuwa ndiyo mmiliki. Kwanza kwenda mwezini ni changamoto; na hivyo kutekeleza masharti ya viza kwenda mwezini kwa ulimwengu wa sasa, haiwezekani. Hivyo kama unapanga kwenda huko, unaweza kwenda. Ni eneo lisilohitaji viza. Tunakutakia kila la heri.

## Vyama viwili vya wafanyakazi ndani ya kampuni moja

**Mimi ni mwekezaji wa kigeni ninayemiliki kiwanda nje ya jiji la Dar es Salaam na nimeajiri idadi kubwa ya watu. Hivi karibuni watu watatu waliojitambulisha kama maafisa kutoka kwenye chama fulani cha wafanyakazi walifika ofisini kwangu wakitaka waruhusiwe kuongea na wafanyakazi wangu na kuwaunganisha kwenye chama chao cha wafanyakazi. Nilikataa ombi hilo kwa sababu tayari nina chama cha wafanyakazi kiwandani kwangu. Sasa wameniandikia kunitaka niwaeleze tarehe na mahali ambapo watakuwa na muda wa kuongea na wafanyakazi. Sijawajibu kama tahadhari hadi nishauriwe kisheria. Je, ombi hili ni la kawaida? Tafadhali nishauri.**

*28 Oktoba 2013*

Ombi hili ni la kawaida kwa kuwa chama cha wafanyakazi kinachoomba kinatekeleza

haki yake chini ya Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini. Sheria hii inatamka wazi kwamba kila mwakilishi aliyeruhusiwa na chama cha wafanyakazi kilichosajiliwa atakuwa na haki ya kuingia kwenye majengo ya mwajiri kwa lengo la kutafuta wanachama, kuwasiliana na wanachama, kukutana na wanachama waliochini ya mwajiri na kuendesha mikutano ya wafanyakazi katika maeneo ya kazi. Pamoja na hayo, Chama cha Wafanyakazi kilichosajiliwa kinaweza kuanzisha tawi lake mahala pa kazi ambapo wanachama wake kumi au zaidi wameajiriwa.

Kwenye suala lako, kitu pekee unachohitaji kujiridhisha ni iwapo hao wanaojiita maafisa ni kweli wanatoka kwenye hicho chama, isijekuwa ni "vishoka", ambao ni wengi. Kama ukijiridhisha kuwa ni maofisa halali, basi jiridhishe pia kama chama hicho kimesajiliwa. Wewe kama mwajiri huwezi kuwazuia maofisa kusajili wanachama, hata kama kuna chama kingine. Mwisho wa yote, uanachama kwenye chama cha wafanyakazi ni hiari ya mfanyakazi na siyo mwajiri. Pia, ni wafanyakazi ndiyo wanaoamua iwapo wajiunge na vyama vya wafanyakazi ama la. Unaweza kuwasiliana na wanasheria wako kwa msaada zaidi.

## Kunyimwa kazi ya uhudumu wa ndege

**Mimi ni mwanamke mrefu na mwenye muonekano mzuri. Niliomba kazi ya uhudumu wa ndege katika shirika la ndege la ndani na ninajua kwamba matokeo ya mtihani wa nadharia niliongoza kati ya washindani wengine 20 walioomba. Aidha, kwenye mtihani wa vitendo nilikuwa wa pili kwa ubora, lakini, nasikitika, nilinyimwa kazi ati kwa sababu nina mapaja manene kuliko safu za njia za kutolea huduma katika ndege (aisle), wakimaanisha kwamba sehemu ya kupita abiria ndani ya ndege ni nyembamba kwangu kupita. Je, huu siyo ubaguzi? Kama tatizo ni hilo kwenye daraja la kawaida, basi ningeweza kufanya kazi kwenye daraja la biashara ambalo nafasi kati ya safu za viti ni pana. Ninataka kushtaki. Tafadhali niongoze.**

*25 Novemba 2013*

Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini Na. 6 ya 2004 inamtaka kila mwajiri kuhakikisha kwamba anaendeleza fursa sawa katika ajira na kujitahidi kuondoa ubaguzi mahala pa kazi. Pia ni kosa kwa mwajiri kufanya ubaguzi wa dhahiri au usiokuwa wa dhahiri kwa misingi ya rangi, utaifa, kabila au sehemu anayotoka, asili, uasili wa Taifa, asili ya kijamii, maoni ya kisiasa au kidini, Mwanamke au Mwanamume, jinsia, ujauzito, kuolewa au kutoolewa au majukumu ya familia, ulemavu, VVU/UKIMWI, umri au maisha anayoishi. Hata hivyo, utofauti kwenye kanuni hiyo ya msingi ni kwamba, siyo ubaguzi kutofautisha, kuzuia au kupendelea mtu yeyote kwa msingi wa mahitaji ya asili ya kazi.

Tukirudi kwenye swali lako tunaona kwamba hali yako inaingia kwenye tofauti iliyotolewa na sheria kwamba haitakuwa ubaguzi kutofautisha, kuzuia au kupendelea mtu yeyote kwa msingi wa mahitaji ya asili ya kazi.

Hivyo, kama sehemu ya kupita abiria ndani ya ndege ni nyembamba kwa mfanyakazi mtarajiwa kuna chaguzi mbili tu kwa mwajiri. Ya kwanza, ambayo utakubali kwamba ni ya ghali, ni kuomba mtengeneza ndege aongeza ukubwa wa njia. Ya pili ni kukataa kukuajiri, kama shirika la ndege lililivyofanya. Unatakiwa kuwasiliana na wanasheria wako ambao wanaweza kukuongoza zaidi.

## Kutukana na kutumia lugha ya matusi

**Bosi wangu ni mgeni, anatumia sana lugha ya matusi dhidi yangu. Ni mazoea/tabia yake na kila mmoja ofisini ni shahidi juu ya jambo hili. Je, lugha hiyo siyo kosa chini ya sheria za Tanzania?**

*30 Desemba 2013*

Kifungu cha 89 (1) cha Kanuni ya Adhabu kinatamka kwamba, Mtu yeyote ambaye (a) anatumia lugha chafu, ya matusi au ya usafihi kwa mtu mwingine yeyote kwa namna ambayo huenda ikaleta uvunjifu wa amani; au (b) anazozana au, kwa namna nyingine yoyote, ataleta fujo kwa namna ambayo huenda ikaleta uvunjifu wa amani, atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miezi sita. Kutokana na maelezo hapo juu, utagundua kwamba lugha hiyo ya matusi ambayo inaweza kusababisha uvunjifu wa amani ni kosa la jinai. Sheria haitoi hiari ya kulipa faini ukishatiwa hatiani, bila kujali nafasi aliyonayo, anaweza kuishia jela kwa miezi sita.

## Idara ya uhamiaji Dar

**Nilitua kwenye Uwanja Ndege wa Mwalimu Nyerere miezi michache iliyopita na niliulizwa iwapo nimekuja kwa ajili ya utalii au biashara. Nilijibu kwamba nilikuwa nimekuja kwa ajili ya biashara, ambapo walinitaka nilipe Dola za Marekani 200. Hata hivyo, nilishauriwa kuchukua viza ya utalii ambayo niliambiwa ni rahisi na ni haraka kuishughulikia lakini ninatakiwa kulipa ada ya kuiandaa viza, kiasi cha Dola za Marekani 50. Nililipia kiasi hicho lakini baadaye niligundua kwamba ingawa ni kidogo kuliko kiasi cha kupata viza ya biashara, sikupewa risiti kwa ajili ya ada ya kuandalia. Nilijaribu kuomba risiti lakini kwa kuwa kulikuwa na msururu mrefu kwa ajili ya viza, niliacha vinginevyo ningepoteza muda mwingi kubishana. Je, ninaweza kupata risiti hiyo?**

*13 Januari 2014*

Hatuijui kama kuna ada ya kuandalia viza za utalii. Kimsingi, umewapa rushwa maafisa wa uhamiaji bila kujua kwamba ilikuwa ni rushwa, japo tunaona kwamba ilikuwa wazi. Huwezi kupata risiti hizo kwa sababu hakuna risiti kwa ajili ya ada ya kuandalia viza. Zaidi, ukiwa na viza ya utalii wakati ulikuja kwa shughuli za kibiashara, ina maana kwamba biashara yoyote uliyokuwa unaifanya nchini Tanzania ilikuwa ni haramu pia ni kosa chini ya sheria zetu za uhamiaji. Wanasheria wako wanaweza kukuongoza zaidi.

## Kanuni za mavazi kwenye ofisi ya serikali

**Ninafanya kazi kwenye ofisi fulani ya Serikali na bosi wangu ameniambia kwamba niache kuvaa mavazi mafupi. Inawezekana ananitaka/ananitamani na hiyo ndiyo sababu hasa. Cha kushangaza hamwambii mke wake ambaye anavaa mavazi mafupi na wakati mwingine jinzi/suruali za kubana anapokuja ofisini kumtembelea. Je, ana haki ya kuniamulia nini cha kuvaa na kuacha kumwambia mkewe? Tafadhali nishauri iwapo maoni yake juu ya urefu wa sketi na kukodolea macho sketi yangu ni halali au ni kosa la unyanyasaji kingono?**

*24 Februari 2014*

Hatujawahi kuona sheria ambayo inasema kwamba ni kosa la unyanyasaji kingono ikiwa mwanamume, katika mazingira ya kawaida, atamwangalia mwanamke hasa mahala pa hadhara. Kimsingi, kama unavaa sketi fupi, ni wazi macho ya mwanamume yataangalia tu. Iwapo anaendelea kuangalia sketi na siyo wewe, hilo linaweza kuwa ni kosa lakini hilo siyo swali lako na hivyo hatutalijadili hapa. Kama kumuangalia mwanamke aliyevaa sketi fupi ni kosa, basi wanaume wengi wangekuwa wameshtakiwa wakiwemo waendesha mashtaka wa umma na polisi.

Mawazo ya bosi wako kwenye urefu wa sketi yako yanatokana na waraka wa Serikali. Waraka wa Utumishi wa Umma Na. 3 wa mwaka 2007 unaeleza namna mtumishi wa umma anavyotakiwa kuvaa akiwa kazini.

Baadhi ya mavazi yaliyokatazwa ni pamoja na nguo fupi na za kubana, jinzi, fulana, kandambili na nguo zinazoonesha maungo ya mwili. Hivyo, kwa kuwa unafanya kazi Serikalini, moja kwa moja unazuliwa kuvaa sketi fupi kazini kwako. Hata hivyo, hauzuiliwi kuvaa sketi fupi nje ya ofisi.

Mke wa bosi wako siyo mtumishi wa umma na hafungwi na waraka huo. Kama unafikiri kubadilisha kutoka kuvaa sketi fupi hadi kuvaa jinzi ya kubana, kama mke wa bosi wako, tafadhali elewa kwamba hilo pia Waraka unalikataza. Kama unataka kuendelea kufanya kazi Serikalini tafadhali fikiria kubadili mavazi yako. Wanasheria wako wanaweza kukuongoza zaidi.

## Wafanyakazi wenye ulemavu wanadai posho kubwa kwa kazi za nje ya ofisi

**Kwenye kampuni yangu wafanyakazi wanasafiri sana kwenda kuwahudumia wateja wetu wa mikoani. Tumekuwa tukiwalipa posho za nje ya ofisi/kituo cha kazi ikiwa ni posho za safari pamoja na posho nyinginezo. Hivi karibuni tumeingia kwenye matatizo na wafanyakazi wetu wawili ambao ni walemavu. Wanadai kwamba wanatakiwa kupendelewa/watendewe tofauti na wafanyakazi wengine kwenye suala la posho ya nje ya ofisi kwa sababu wao ni walemavu. Wanasema hilo ni takwa la kisheria. Tumekwama na hatujui iwapo hilo ni jambo la kisheria, na je tufanye nini?**

*14 Aprili 2014*

Labda kwa ufafanuzi tu, kisheria, mtu mwenye ulemavu ni mtu mwenye udhaifu au upungufu wa viungo, fahamu au akili na ambaye uwezo wake wa utendaji kazi umepungua kutokana na vikwazo vya kimtazamo, kimazingira na kitaasisi. Hakuna kifungu chochote cha sheria, ikiwemo Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini wala Sheria ya Taasisi za Kazi wala kanuni zake, ambacho kinawalazimisha waajiri kuwalipa watu wenye ulemavu kwa viwango tofauti na wafanyakazi wengine hasa inapokuja suala la posho za nje ya kituo cha kazi.

Jambo jingine linalofanana na mtazamo wa hapo juu, Sheria ya Watu wenye Ulemavu Na. 9 ya 2010 chini ya kifungu cha 33 inamtaka mwajiri kutokuwachukulia watu wenye ulemavu tofauti na wasiokuwa na ulemavu, kuhusiana na pamoja na mambo mengine, katika utoaji wa faida zozote au masuala mengine yanayohusiana na ajira. Hili ni kwa pande zote mbili.

Kutokana na jambo hilo, hakuna kifungu cha sheria ambacho kinakulazimisha kutekeleza matakwa ya ziada ya wafanyakazi hawa. Hata hivyo, kutegemea na uwezo wa kampuni, unaweza kuwasaidia kuhusu malalamiko/magumu ambayo wanayapata wanaposafiri na kujaribu kuwasaidia kama jambo tu la kiungwana/kistaarabu. Wanasheria wako wanaweza kukuongoza zaidi.

## Uhamiaji wakali sana

**Sisi ni kampuni ya kigeni iliyosajiliwa na kufanya kazi nchini Tanzania. Hivi karibuni maafisa wa Idara ya Uhamiaji walivamia ofisi yetu na kuanza kufanya upekuzi na kuulizia kuhusu pasipoti za wafanyakazi wetu wa kigeni. Uhamiaji walikuwa wakatili na wakali sana kiasi kwamba walitutisha hasa pale mmoja wa wafanyakazi alipoomba kwenda kwake, mlango unaofuata, ili kuchukua kibali chake. Je, upekuzi wa aina hiyo unaruhusiwa kisheria? Idara ya Uhamiaji inahitaji kufanyiwa mafunzo ya huduma kwa wateja - je, mafunzo haya hayatolewi kwa watumishi wa umma nchini Tanzania? Vitendo vyote nilivyoeleza hapo juu vilinaswa na kamera zetu za CCTV.**

*21 Aprili 2014*

Chini ya sheria zetu, maafisa uhamiaji wana mamlaka ya kuingia jengo lolote wakati sahihi na kufanya uchunguzi wa suala lolote linalohusu uhamiaji. Pia, afisa uhamiaji bila kuwa na hati ya ukamataji anaweza kumkamata mtu yeyote ambaye ana sababu za kuamini kwamba ni mhamiaji haramu au anakiuka sheria za nchi za uhamiaji. Pia, katika kutekeleza majukumu yao, sheria imewapa mamlaka maafisa uhamiaji ya kusimamisha, kuingia na kukagua ndani ya ndege, treni, gari, chombo cha moto, meli, jengo, ardhi, ghala, kontena au boti yoyote iliyopo nchini Tanzania. Sheria pia inatamka kwamba mtu yeyote aliyekamatwa, aliyepekuliwa au aliyewekwa kizuizini na maafisa uhamiaji anatakiwa kuarifiwa kwa haraka iwekekanavyo na kwa lugha anayoielewa sababu za kukamatwa, kupekuliwa au kuwekwa kizuizini.

Turudi kwenye swali lako, upekuzi uliofanywa na Idara ya Uhamiaji ni halali. Lakini kinachoonekana kukutatiza ni namna maafisa uhamiaji walivyoingia kwenye ofisi za kampuni yako na walivyofanya mambo yao kwa ukali.

Una haki ya kutendewa vyema. Kama unaamini kama unavyoamini kwamba hukutendewa vyema, una haki zote za kufungua malalamiko kwa Mkurugenzi wa Huduma za Uhamiaji. Tunatumaini umechukua majina ya maafisa uhamiaji. Hatuwezi kujibu oni lako/swali lako la mwisho kuhusu ujuzi/elimu ya huduma kwa wateja lakini linaweza kuwa sehemu ya hoja zako kwa Mkurugenzi wa Uhamiaji.

## Mafao kukatwa marejesho ya mkopo binafsi

**Niliacha kazi wiki chache zilizopita. Wakati nimeajiriwa nilikopa kwa sharti kwamba nitalipa mkopo huo ndani ya miaka mitatu lakini niliacha kazi kabla ya miaka mitatu. Mwajiri wangu amezuia baadhi ya mafao yangu ya kuacha kazi kwa ajili ya kulipa deni. Anasisitiza na kunionesha kipengele cha mkataba wa mkopo ambacho kinasema kwamba "mkopo utalipwa mara moja baada ya kukoma kwa mkataba wa ajira na mwajiri atakata mafao ya kuacha kazi ili kufidia mkopo." Je, hilo linaruhusiwa kisheria? Naona kama hii siyo sawa kwa sababu bado nina uwezo wa kulipa deni kwa muda uliobaki.**

*12 Mei 2014*

Labda kwa ufafanuzi tu, unatakiwa uelewe kabisa kwamba chini ya kifungu cha 28 cha Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini, Na. 6 ya 2004 (ELRA), mwajiri anaruhusiwa kumkata mfanyakazi mshahara wake. Ingawa kuna masharti mengi ya kutimiza ili kufanya hivyo, kwa suala lako masharti hayo yatatimizwa kama kutakuwa na idhini ya maandishi (angalia kifungu cha 28 (1) (b) cha ELRA). Tunaamini idhini hiyo ipo wazi kwenye suala lako. Hasa, kitendo cha kusaini mkataba wenye sharti la wazi kwamba mkopo utalipwa wakati wa kusitisha ajira, kilimpatia mwajiri haki ya kukata mafao kwa ajili ya kulipa mkopo, na hivyo kudhihirisha mtizamo wetu. Waajiri wengi wanatoa mikopo bila sharti hili ambalo kwa bahati mbaya linawapa ugumu pale mfanyakazi anapojiuzuru au anapoacha kazi kabla mkopo haujalipwa. Kimsingi, tunafanya kazi na waajiri wengi na wakati wote tunawashauri kipengele hiki kiwe wazi kwenye mkataba wa mkopo.

Ili kupata uhalisia, jaribu kujiweka katika nafasi ya mwajiri. Utategemeaje kurudishiwa mkopo wako wakati huna dhamana yoyote na hauna uhakika ni wapi mdaiwa anaishi? Hakuna shaka kwamba ulipewa mkopo kwa kutegemea ajira ya mwajiri wako na kwa kuwa haupo tena, mwajiri anaruhusiwa kudai malipo husika. Wanasheria wako wanaweza kukuongoza zaidi.

## Haki ya kufanya kazi

**Katiba yetu inatoa haki ya kufanya kazi na kupewa ujira kwa kazi iliyofanyika. Mimi ni mhitimu wa hivi karibuni na nimekuwa nikiomba kazi karibu miaka miwili bila mafanikio. Nimeomba hadi kazi za Serikali; lakini kwa kasumba ya kujuana, hawajawahi kuniita. Nafikiri kifungu hiki cha katiba kinavunjwa hasa kwa wahitimu wa sasa. Je, ninaweza kufungua kesi dhidi ya Serikali na kuilazimisha kututafutia kazi? Taratibu zake ni zipi?**

*19 Mei 2014*

Tunaelewa kwamba ajira ni changamoto kwa sababu kuna wahitimu wengi kuliko ajira zilizopo. Haki ya kufanya kazi na haki ya ujira/malipo ya kazi zimewekwa kwenye katiba ili kuhakikisha kwamba haki hizo zinalindwa. Ajira inaweza kuwa ya kujiajiri, kuajiriwa Serikalini au kuajiriwa kwenye sekta binafsi. Hivyo kama hujapata ajira Serikalini, angalia fursa nyingine za ajira.

Uwepo wa kifungu cha Katiba kuhusu haki ya kufanya kazi hakumaanishi kwamba Serikali itamhakikishia kila mtu kuwa na kazi. Tunakushauri utumie ubunifu kujipatia kipato halali, kesi dhidi ya Serikali haiwezi kufanikiwa. Unaweza kuwasiliana na mwanasheria wako kwa mwongozo zaidi.

## Kuajiri polisi wanene

**Je, hakuna viwango/vigezo vya kuanzia pale jeshi la polisi linapoajiri maafisa wake? Mmoja wa rafiki zangu ambaye mwili wake haufai na ana uzito wa kilogramu 180 ameajiriwa. Swali langu jingine ni kwa nini maafisa polisi wanakuwa ni wakatili sana? Na je, ni lazima polisi kubeba bunduki anapomsindikiza mfungwa?**

*9 Juni 2014*

Kanuni za Kudumu za Polisi (PGO) zinaeleza miendo ya polisi kwa ujumla. Taratibu za kuajiri maafisa polisi zimeelezwa kwenye PGO ambapo umri, elimu, afya ya mwili na rekodi za uhalifu vinazingatiwa. Ni kweli kwamba polisi dhaifu hawawezi kufanya kazi nzuri mitaani, lakini ni lazima uelewe kwamba siyo polisi wote wanakwenda kwenye maeneo ya matukio. Baadhi ya wakuu wa polisi ni wanene zaidi na wanabaki vituoni kwa sababu wanafanya kazi nyingi za kiofisi na kupanga mikakati. Rafiki yako anaweza kuwa ameajiriwa kwa sababu ni mtaalam wa eneo fulani, na kabla hujapeleka malalamiko popote, unatakiwa kujiridhisha.

PGO pia inaeleza kwamba afisa wa polisi bila kujali yupo kazini au la anatakiwa kuwa mwenye heshima kwa umma, na kama hana heshima au anafanya ukatili kwa mwananchi yeyote atachukuliwa hatua za kinidhamu. Vilevile, chini ya PGO, afisa wa polisi anayesindikiza wafungwa anatakiwa kubeba bunduki na pia wanawajibika kutoa usafiri kwa wafungwa kwa kutumia gari ya polisi.

## Likizo wakati wa kombe la dunia

**Timu yangu inacheza Kombe la Dunia. Ingawa likizo yangu kwa mwaka huu imekwisha, nilimuomba mwajiri wangu anipe wiki nne nyingine za ziada mwaka huu. Kwanza ni tukio la kipekee, na la mara moja maishani. Mwajiri wangu amenikatalia kwenda, na tiketi zangu siwezi kuzitumia. Je, ninaweza kumshtaki mwajiri kwa unyanyasaji alionifanyia? Ninaweza kulalamika kwa Waziri juu ya jambo hili? Ninawezaje kuwaharibia maisha hawa mabosi wangu?**

*23 Juni 2014*

Tumesoma swali lako mara nyingi ili kuhakikisha kwamba hatujaacha jambo lolote la msingi. Lakini hata baada ya kusoma tena na tena, bado majibu yetu hayatakupendeza.

Kwanza hatuelewi kwa nini hili ni kombe lako la mwisho kuangalia. Haujatueleza

na unajua fika kwamba kombe la dunia linachezwa kila baada ya miaka minne. Pili, kama umemaliza likizo yako kwa mwaka, huwezi kulazimisha kupata likizo ya bila malipo bila idhini ya mwajiri wako, ambaye anaweza kukataa. Kwa ufupi, likizo hizo ni za hiari. Tatu, kombe la dunia siyo sababu ya msingi ya kumfanya mwajiri wako akuruhusu kwenda. Nne, labda kama bosi wako alikuambia ununue tiketi, huwezi kufanikiwa kumshtaki mwajiri wako kwa sababu ya tiketi zako kupotea.

Unaweza kumwandikia Waziri lakini hawezi kufanya chochote. Waziri haendeshi ofisi bali mabosi zako. Kama ukijaribu kuharibu maisha ya mabosi zako, wanaweza kukuwajibisha hivyo usijaribu kufanya mambo kwa pupa kwa sababu kombe la dunia litakwisha hivi karibuni lakini wewe utaendelea kuishi na mabosi wako. Hatutaki kuonekana kama washauri wa mambo ya kijamii, lakini tunakushauri kwamba busara inapaswa kutawala mihemko au hisia zisizokuwa na msingi.

## Kutembelea kituo cha kimataifa cha anga za juu

**Nimegundua njia mpya na rahisi ya kuruka kwenda kituo cha kimataifa cha anga za juu na ninataka kujua iwapo nitazuiliwa. Kwa jinsi nilivyosoma, hii ni sehemu/ eneo lisilomilikiwa na mtu, na hivyo kila binadamu ana haki ya kwenda angani na kwenye kituo cha kimataifa cha anga za juu. Je, iwapo nikikutana na maafisa wa uhamiaji jijini Dar niwaambie nini?**

*30 Juni 2014*

Tumepokea maswali yako mengi kuhusu anga na tunaamini tulikujibu moja ya swali hilo mwaka jana. Kwa bahati mbaya una maswali mengine 20 magumu na mengi yake siyo ya kisheria na hivyo hatutayajibu. Hata hivyo, tumechagua hili ambalo lina chembe ya sheria.

Kwa kuanzia na kituo cha anga za juu cha kimataifa, hiki kilifadhiliwa na nchi za Marekani, Urusi, Canada na nchi nyinginezo. Hakuna nchi ya Kiafrika ikiwemo Tanzania ambayo ilifadhili, na inaeleweka hivyo. Hivyo, huna haki ya moja kwa moja ya kwenda huko. Pia hatuna uhakika wa namna unavyoweza kufika huko, na kama umebuni njia nyepesi ya kwenda angani, basi tunakushauri uwasiliane na mashirika ya anga ya Marekani na Urusi, miongoni mwa mashirika mengine, kwa kuwa watatamani kuujua uvumbuzi wako mpya. Ufikirie pia kuusajili ili mtu mwingine asiibe uvumbuzi wako.

Mkataba kuhusu Kanuni Zinazoongoza Shughuli za Mataifa katika Uchunguzi na Matumizi ya Anga za Juu, ikiwemo Mwezi na Magimba Mengine ya Anga unaeleza kwamba chunguzi zote za anga za juu zitafanywa kwa nia njema na zitakuwa wazi kwa mataifa yote yanayotii sheria za kimataifa. Hakuna taifa litakalodai umiliki wa anga za juu au gimba lolote. Shughuli zitakazofanywa anga za juu zitakuwa ni lazima ziendane na sheria za kimataifa na mataifa yatakayofanya shughuli hizo ni lazima yakubali wajibu wa taasisi za kiserikali na zisizo za Serikali zinazohusika. Vifaa vinavyopelekwa katika anga za juu vitakuwa ni mali ya taifa husika na watu wake.

Vitu, sehemu au chembe zitakazopatikana nje ya mamlaka ya nchi zitarudishwa baada ya kutambuliwa. Nchi itakayopeleka kifaa katika anga za juu itawajibika kimataifa kwa hasara yoyote itakayojitokeza.

Kutokana na utafiti wetu, ambapo pia tunakusihi ufatilie zaidi na kuthibitisha, tunaamini Tanzania haijasaini mkataba huu. Hata hivyo, tunaamini kwamba mkataba utatumika nchini Tanzania kama utaamua kwenda huko. Hivyo, ingawa unaweza usikaribishwe kwenda kwenye kituo cha anga za kimataifa, uko huru kwenda anga za kimataifa kama unaweza, jambo ambalo unadai unaweza.

Kuhusu uhamiaji, wanaweza wasikuamini. Hata hivyo, hawawezi kukuzuia kwenda angani na watagonga mhuri wa kutoka Jamhuri ya Muungano. Utakaporudi kutoka angani hautakuwa na mhuri wa taifa lolote na tunakushauri uwaeleze maafisa wa uhamiaji hali ilivyokuwa. Kimsingi, siku utakayorudi huku ukitumia njia mpya uliyonayo, utakuwa mtu wa kwanza kutoka Afrika kwenda anga za juu kama mtalii wa safari ya haraka. Kwa hatua hiyo, uhamiaji hawatakusababishia usumbufu mwingi.

John F. Kennedy alieleza yafuatayo wakati anawahamasisha wafanyakazi wa NASA kwenda mwezini: "Tumechagua kwenda mwezini. Tumechagua kwenda mwezini katika muongo huu na kufanya mambo mengine siyo kwa sababu ni rahisi, bali kwa sababu ni ngumu, kwa sababu lengo hili litasaidia kuunganisha na kupima ukubwa wa nguvu na ujuzi wetu, kwa sababu tupo tayari kukubali changamoto hiyo, hatuko tayari kuahirisha kile ambacho tunataka kufanikisha, na wengine vivyo hivyo."

Siyo vibaya kuota, kwa sababu ndoto hutimia. Yasiyowezekana yanawezekana na tunakutakia kila la heri kwenye mpango wako.

## Kiinua mgongo kwa utendaji mbovu

**Kampuni yangu imeshtakiwa kwenye Tume ya Usuluhishi na Uamuzi na mmoja wa waliokuwa wafanyakazi wake ambaye alifukuzwa kazi kwa wizi wa vitendea kazi fulani. Baada ya kumfukuza tulimlipa mafao yake ya kuachishwa kazi isipokuwa kiinua mgongo/mkono wa kwaheri. Ingawa anakiri kufukuzwa kihalali, mfanyakazi huyu anadai kulipwa kiinua mgongo kwa sababu amefanya kazi kwa miaka kumi. Je, mfanyakazi huyu anastahili kulipwa malipo haya? Tafadhali nishauri.**

*7 Julai 2014*

Kifungu cha 42 cha Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini, Na. 6 ya 2004 pamoja na Kanuni ya 26 ya Kanuni za Kazi na Mahusiano Kazini (Mwenendo Bora), 2007 Tangazo la Serikali Na. 42 la 2007 vinatambua kiinua mgongo/mkono wa kwaheri kama mojawapo ya mafao ya kuachishwa kazi. Kiinua mgongo kimetafsiriwa kumaanisha kiasi cha mshahara wa angalau siku 7 kwa kila mwaka wa utumishi, kwa miaka yote mfululizo, lakini miaka hiyo isizidi kumi.

Hata hivyo, sheria hiyo hiyo haimpi wajibu mwajiri wa kulipa kiinua mgongo kwa mfanyakazi aliyeachishwa kazi kwa sababu za utendaji mbovu. Maamuzi yenu ya kukataa kumlipa mfanyakazi huyo malipo ya kiinua mgongo hayawezi kubatilishwa, na madai ya mfanyakazi huyo kwa namna yoyote hayatafanikiwa. Tunakushauri uwasilishe vyema kesi yako kwenye Tume ya Usuluhishi na Uamuzi kwa mujibu wa vifungu vya sheria vilivyotajwa hapo juu.

## Kuwarudisha wakimbizi

**Je, kuna sheria inayowalinda wakimbizi wanapoingia nchini? Je, Tanzania ina uwezo wa kuhimili wimbi la wakimbizi? Kwa nini wasirudishwe nchini kwao? Je, ni halali wakimbizi kuja Tanzania?**

*8 Septemba 2014*

Kuna Mkataba wa Kimataifa Unaosimamia Hadhi ya Wakimbizi. Mkataba huo uliidhinishwa na Mkutano Mkuu wa Umoja wa Mataifa mwaka 1951. Ulianza kutumika tarehe 22 Aprili 1951 na mwanzoni ulikuwa unalinda wakimbizi wa Ulaya pekee kuanzia 1 Januari 1951 (baada ya Vita ya Pili vya Dunia), ingawa nchi zilikuwa na hiari ya kutoa tangazo kwamba vifungu vya mkataba huo vitatumika kwenye maeneo mengine.

Itifaki ya mwaka 1967 iliondoa ukomo wa muda na kuanza kuwalinda wakimbizi "bila kujali mipaka ya kijiografia" lakini matangazo

yaliyotolewa na nchi wanachama wa Mkataba kuhusu mipaka ya kijiografia yaliingizwa pia. Tanzania imeridhia Mkataba huu na hivyo una nguvu ya kisheria nchini Tanzania.

Ibara ya 1 ya Mkataba kama ulivyofanyiwa marebisho na Itifaki ya mwaka 1967 inamtafsiri mkimbizi kama ni mtu ambaye kutokana na hofu ya kweli ya kuteswa kwa sababu ya rangi, dini, utaifa, uanachama wa kikundi fulani cha kijamii, au maoni ya kisiasa, yupo nje ya nchi yake, na ameshindwa au, kutokana na hofu hiyo, hana nia ya kutegemea ulinzi wa nchi hiyo; au ambaye, hana utaifa na yupo nje ya nchi yake ya ukaazi kutokana na matukio kama hayo, hawezi au, kutokana na hofu hiyo, hana nia ya kurudi kwenye nchi hiyo."

Nchi za Afrika zilipitisha Mkataba wa Afrika Kuhusu Matatizo Maalum ya Wakimbizi Afrika na kuongeza tafsiri ya mkimbizi kuwa ni mtu yeyote aliyelazimika kuikimbia nchi yake kutokana na machafuko ya nje, kazi, ukoloni au matukio yanayovuruga usalama kwenye taifa lake.

Katika kanuni za jumla za sheria za kimataifa, mikataba mbalimbali inayotumika inazifunga nchi wanachama wa mikataba hiyo na ni lazima itekelezwe kwa nia njema. Nchi kama Tanzania ambayo imeridhia Mkataba wa Wakimbizi zinatakiwa kuwalinda wakimbizi waliopo kwenye nchi zao kwa mujibu wa masharti ya mikataba hiyo.

Vipo vifungu vingi ambavyo nchi wanachama wa Mkataba wa Wakimbizi na Itifaki yake ya mwaka 1967 ni lazima wavitekeleze na kifungu kimojawapo, ambacho ni muhimu, ni nchi husika kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi (UNHCR) katika kutekeleza majukumu yake na kuisaidia UNHCR kusimamia utekelezaji wa vifungu vya Mkataba.

Mkimbizi anatakiwa kuwa huru dhidi ya adhabu za kuingia au kuwepo nchi nyingine kinyume cha sheria, kama ikithibitika kwamba aliingia kwa nia njema; yaani, kama mkimbizi anaamini kwamba kuna sababu za msingi za kuingia au kuwepo kinyume cha sheria, mfano kutokana na hofu ya kupoteza uhuru, na kama amejitambulisha kwa haraka kwenye mamlaka zinazohusika. Haki hii inalindwa na Ibara ya 31 ambayo inatamka kwamba Nchi Wanachama hazitatoa adhabu, kwa sababu ya kuingia au kuwepo kinyume cha sheria, kwa wakimbizi wanaotoka moja kwa moja kwenye nchi ambayo imewatishia usalama au uhuru wao kwa mujibu wa ibara ya 1, wanapoingia au wanapokuwa kwenye ardhi yao bila idhini, kama watajitokeza wao wenyewe bila kuchelewa kwenye mamlaka husika na kueleza sababu za uingiaji au uwepo wao kinyume cha sheria.

Haki za wakimbizi dhidi ya kulazimishwa kurudi kwao kwa nguvu/kutofukuzwa imeelezwa kwenye Mkataba wa mwaka 1951 kuhusu hadhi ya wakimbizi ambao unaeleza kwamba Nchi Wanachama hazitamfukuza au kumrudisha mkimbizi kwa namna yoyote kwenye mipaka ya nchi ambayo maisha yake au uhuru wake umetishwa kutokana na sababu za rangi, dini, utaifa uanachama wa kikundi fulani cha kijamii, au maoni ya kisiasa. Hivyo wakimbizi walioko Tanzania hawawezi kurudishwa. Tanzania pia inapata msaada mzuri wa kifedha na kiufundi kutoka UNHCR ili kuwasaidia wakimbizi hao.

Tanzania pia ina sera ya wakimbizi ambayo inaendana na yaliyosemwa hapo juu. Kwa mujibu wa UNHCR, kuanzia mwaka 1997 mpaka 2002, Tanzania ilikaribisha wakibizi wengi na ilitambuliwa/ilisifika kimataifa juu ya jambo hili.

## Bosi kusomea gazeti chooni

**Bosi wangu anasomea magazeti chooni. Je, si kinyume cha sheria, na vipi naweza kumshtaki? Hii siyo haki kwa wafanyakazi wenzake na inaonesha ni jinsi gani kampuni yetu ilivyo ya kibaguzi.**

*13 Oktoba 2014*

Hatuna hakika ni vipi kwenda na magazeti chooni siyo haki kwako. Unataka kumshtaki bosi wako kwa nini? Je, ni kunyimwa kusoma gazeti ndiko ambako umeguswa nako? Njia bora zaidi ni kuiangalia tabia hii katika mtazamo wa sheria za afya ingawa hatuoni sheria yoyote inayohusika na hili.

Njia rahisi labda ni kufikiria kununua magazeti yako mwenyewe au kuiomba ofisi ya utumishi/raslimali-watu izungumze na bosi ili aache kwenda na magazeti chooni. Kutoa taarifa juu ya jambo hili kwa Taasisi ya Usalama na Afya Mahala pa Kazi pia inawezekana.

Aidha, hatujui kivipi usomaji wa magazeti unaonyesha ubaguzi mahali pa kazi. Isipokuwa kama kuna mambo mengine ambayo haujatueleza, maoni yako juu ya ubaguzi hayana msingi na ni ya kufikirika tu.

## Mwajiri/Bosi analazimisha kutembelea familia zetu

**Ninafanya kazi katika kampuni fulani inayofanya shughuli zake ndani na nje ya nchi. Miezi michache iliyopita mtaalam wa kigeni amehamishiwa Tanzania kama Mkurugenzi Mtendaji wetu. Bosi mpya amekuja na mabadiliko mengi ikiwa ni pamoja na sharti kwamba ni lazima atembelee makazi na nyumba za mameneja waandamizi wake wote. Mimi ni mmoja wa mameneja hao na ninaona kwamba hili ni suala lisilo la kiajira kabisa na halimhusu mwajiri wangu. Je, mwajiri ana haki kutembelea nyumba za wafanyakazi? Je, hakuna sheria inayosimamia hili? Ninahisi hii ni kuingilia mambo/uhuru binafsi.**

*3 Novemba 2014*

Bila shaka anachodhamiria kukifanya bosi wako kinaweza kuonekana ni cha ajabu katika mazingira ya kitanzania na tofauti na kile ulichokizoea. Vilevile sheria za ajira hazina takwa/sharti kwamba ni lazima mwajiri atembelee nyumba au makazi ya mfanyakazi. Mwajiri wako anaweza kufanya hivyo kuonesha heshima na mbinu ya kuwa karibu na wafanyakazi wake waandamizi. Hata hivyo, kwa mtazamo wa kiutumishi, kujua wafanyakazi wako wanapoishi ni muhimu. Ni kawaida kwa maafisa utumishi/raslimali-watu kuthibitisha, kati ya mambo mengine, taarifa za wafanyakazi ikiwa ni pamoja na makazi na anwani ya makazi.

Hata hivyo, huwezi kuadhibiwa kwa kushindwa kumkaribisha mwajiri wako nyumbani kwako. Kwa kuwa sheria za kazi zipo kwa ajili ya kuhakikisha maelewano mahali pako pa kazi, unaweza kulipeleka suali hili kwenye ofisi ya utumishi, chama cha wafanyakazi kilichopo ofisini kwako, na/au katika ngazi za juu kimataifa ili liweze kutatuliwa.

## Uchaguzi wa mfuko wa hifadhi ya jamii

**Nimeajiriwa kwenye kampuni binafsi nchini Tanzania. Mwajiri wangu ana mkataba na moja ya mifuko ya hifadhi ya jamii uliosajiliwa nchini Tanzania ili wafanyakazi wake wote wajiunge na mfuko huo. Sitaki kuwa mwanachama wa mfuko huo kwani nina mfuko niliouchagua mwenyewe. Je, ninalazimika kujiunga na mfuko wa hifadhi ya jamii ambao mwajiri wangu ameingia nao mkataba?**

*10 Novemba 2014*

Sheria ya Mamlaka ya Mifuko ya Jamii, 2008, inaeleza kwamba kila mwajiri katika sekta rasmi atawajibika kuwasajili wafanyakazi wake kwenye mfuko wowote wa lazima, isipokuwa kwamba itakuwa ni haki ya mfanyakazi kuchagua mfuko wa lazima ambao atasajiliwa. Kulingana na kifungu hicho, haufungwi na mkataba ambao mwajiri wako ameingia na mfuko wa hifadhi za jamii. Unaweza kuchagua mfuko wako mwenyewe.

# Sheria za Mazingira na Urithi wa Mali za Kale

"

Kuweka mlinganyo baina ya kulinda mazingira na mfumo wezeshi wa kiuchumi/kimaendeleo ni kitu kigumu kwa nchi yoyote, ikiwemo Tanzania. Mara nyingi, shughuli za kimaendeleo zinaweza kufanyika baada ya kupata vibali na kufuata taratibu husika. Ni pale tu ambapo sheria husika hazifahamiki au zinapuuzwa, ndipo wafanyabiashara wanaweza kujikuta katika migogoro ya kisheria.

## Mamlaka chini ya sheria ya hifadhi mali za kale

**Ninaishi Musoma kwenye eneo la kihistoria ambalo limezungukwa na majengo yaliyojengwa au yaliyokuwepo tangu miongo mingi iliyopita. Na mimi pia nimerithi eneo hilo ambalo vizazi vingi vimepitia na historia ya familia yetu pia inaJulaikana sana hapa. Miezi minne iliyopita maafisa kutoka Idara ya Hifadhi za Mali za Kale ya Wizara ya Maliasili na Utalii walikuja kukagua kitu walichokiita mnara wa makumbusho kwenye eneo langu. Natamani kujua haki zangu ni zipi kama kweli makumbusho hayo yapo kwenye eneo langu.**

*16 Januari 2012*

Sheria ya Hifadhi za Mali za Kale inatoa uhifadhi na ulinzi wa maeneo ya kihistoria ambayo yana akiolojia, historia au masalia ya asili. Waziri chini ya sheria ya Hifadhi za Mali za Kale ana mamlaka ya kutangaza, kwa amri iliyochapishwa kwenye Gazeti la Serikali, mahala popote, eneo lolote au jengo kuwa alama/sehemu ya makumbusho. Kwa hiyo, Idara ya Mambo ya Kale haiwezi tu, kuamka siku moja, kuja kwenye eneo lako na kudai kuwa eneo lako ni sehemu ya makumbusho. Ili patambuliwe hivyo, utangazwaji wa eneo au jengo husika ni lazima ufanyike kwanza.

Chini ya Sheria ya Hifadhi za Kale, Mkurugenzi wa Hifadhi za Mali za Kale na mtu yeyote aliyepewa mamlaka na Mkurugenzi anaweza kwa muda wowote unaofaa (a) kuingia na kukagua mnara/sehemu wa/ya makumbusho (b) kuzungusha uzio, kukarabati, kulinda na kuhifadhi makumbusho yoyote (c) kukagua na kufukua masalio kwenye makumbusho yoyote na kuondoa masalio ambayo hayajavumbuliwa, isipokuwa (i) kama mnara wa makumbusho upo kwenye eneo la makazi ya watu, Mkurugenzi au mtu mwingine aliyepewa mamlaka atatoa taarifa ya angalau masaa arobaini na nane kabla kwa wakazi wa eneo hilo akielezea dhamira yake ya kutekeleza mamlaka aliyopewa chini ya kifungu hiki kidogo. Sheria pia inaeleza kuwa mtu yeyote ambaye kwa makusudi atamzuia Mkurugenzi au mtu yeyote aliyepewa mamlaka na Mkurugenzi kutekeleza mamlaka yake atakuwa ametenda kosa chini ya sheria hii.

Kama kweli eneo lako lina mnara/alama wa/ya makumbusho, chini ya sheria hii, Mkurugenzi ana mamlaka ya kuingia na kuona mnara/alama wa/ya makumbusho baada ya kukupatia taarifa ya masaa 48 kabla ya kuja kwenye eneo lako. Kwa upande wako, inaonesha hujapewa taarifa hiyo.

Tunapenda kukuJulaisha kwamba mnara wa makumbusho na maeneo yaliyopo chini ya Sheria ya Hifadhi za Mali za Kale ni maarufu, na yametangazwa katika Gazeti la Serikali na hakuna uwezekano kwa maafisa wa idara kuja tu ghafla na kuvamia eneo lako bila taarifa ya awali. Tunapendekeza sana ujiridhishe juu ya uhalali wa hao waliojiita maafisa kutoka Wizarani.

## Kibali cha kuchimba shimo

**Ninamiliki nyumba kubwa ya ghorofa tatu eneo la Upanga na ninataka kuchimba kisima kwenye eneo langu. Swali langu ni kwa nini nipate kibali kwa kitu ninachotaka kufanya kwenye ardhi yangu? Huko siyo kuvunja haki yangu ya uhuru kikatiba? Nifanyeje?**

*16 Januari 2012*

Unakwenda mbali na hicho unachokiita haki ya kikatiba. Kumiliki tu ardhi hakukupi haki ya kuwa mfalme kwenye ardhi hiyo. Haki uliyonayo kisheria ni juu ya uso wa ardhi. Chochote unachokifanya nje ya uso wa ardhi unahitaji ruhusa kukifanya. Kwa mfano, kama unaamini ardhi yako ina dhahabu na unataka kufanya shughuli za uchimbaji, kuna taratibu

ambazo unahitaji kuzifuata na ambazo zinaweza kupelekea hati yako ya umiliki wa ardhi (kwa matumizi ya kawaida) kusitishwa ili kupisha uchimbaji wa madini; kwa kuwa, dhahabu siyo mali yako hata kama ipo kwenye ardhi yako.

Ili uchimbe kisima, mamlaka za maji lazima zikuruhusu kufanya hivyo kwa kuwa kisima chako kinaweza kuwa na madhara kwa visima vya jirani na hata vilivyo mbali. Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji inatamka wazi kwamba mtu yeyote, kinyume na matakwa ya vifungu vya sheria hii, atakayejenga, zamisha au panua kisima au shimo la maji bila kuwa na kibali cha uchimbaji kutoka Bodi ya Maji ya Ardhini (Basin Water Board) atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atawajibika kwa faini isiyopungua Shilingi laki tano au kifungo kisichozidi miezi sita au vyote kwa pamoja.

Pia, elewa kwamba, sheria ya Matumizi ya Maji (Udhibiti na Usimamizi) ya mwaka 1974, ambayo imefutwa na sheria hii mpya, ilikwenda mbali zaidi kwa kueleza umbali wa kisima na kisima kuwa angalau mita 230 na kiwango cha juu cha kuvuna maji kwa siku (kwa kisima) kisizidi lita 22,700. Hii ni kwa ajili ya kuleta usawa na matumizi bora ya maji. Sheria inafanya kazi kwa wote bila kujali kama unamiliki nyumba ya ghorofa Upanga au kwingineko.

## Kuwinda nje ya msimu wa uwindaji

**Je, Tanzania ina miezi ambayo uwindaji hauruhusiwi? Unawezaje kupata kibali msimu huo?**

*16 Januari 2012*

Nchini Tanzania, uwindaji hufanyika kwa miezi sita tu kwa mwaka na miezi iliyobaki inaitwa msimu uliofungwa.

Kwa mujibu wa Sheria ya Uhifadhi Wanyamapori, 2009, Mkurugenzi wa Wanyamapori anaweza kutoa kibali cha kuwinda wakati wa msimu uliofungwa, lakini kibali hicho kinaweza kutolewa kwa idhini ya Waziri. Sheria inatamka kwamba mtu yeyote anayewinda wakati wa msimu uliofungwa bila kibali anaweza kutozwa faini au kufungwa au vyote kwa pamoja.

## Mota kwenye baiskeli

**Nimefunga mota kwenye baiskeli yangu ili itumie mafuta ya taa. Je ninatakiwa kuisajili kama gari?**

*23 Julai 2012*

Kisheria, baiskeli itachukuliwa kama chombo ambacho kina matairi mawili yanayoendeshwa kwa njia ya pedo au mkono kwa kutumia nguvu ya mtu anayeendesha pekee. Baiskeli yako ukiiwekea mota ili itumie mafuta ya taa inakuwa inajiendesha yenyewe na hivyo itabadilika na kuwa pikipiki, kama ilivyoelezwa kwenye Sheria ya Usalama Barabarani. Hivyo itatakiwa kusajiliwa. Utatakiwa pia kuikatia bima baiskeli yako uliyoibadilisha.

## Kufuga viumbe-maji nchini Tanzania

**Nimerudi nchini Tanzania baada ya kuhitimu masomo yangu kwenye moja ya nchi za Scandinavia. Wakati wa masomo yetu, mimi na rafiki yangu tulikubaliana kufungua mashamba makubwa ya ufugaji samaki (kilimo cha samaki). Je, sekta hii inasimamiwa? Ninahitaji kufanya nini? Tafadhali nishauri kwa kuwa ninasubiria kwa hamu kubwa kuanzisha biashara hii na mbia wangu mtarajiwa.**

*27 Agosti 2012*

Sekta ya uvuvi inasimamiwa na Sheria ya Uvuvi, miongoni mwa sheria nyingine. Chini ya Sheria ya Uvuvi, ni lazima kwanza kupata kibali kabla ya kuanza shughuli hiyo. Kama unataka kukopa fedha kutoka benki za ndani, ni lazima uhakikishe kwamba unasajili

kampuni na ni lazima kuwe na makubaliano ya wanahisa. Ikiwa ni sehemu ya shughuli zenu na kutegemea na ukubwa wa mradi wenyewe, mnaweza kutakiwa kufanya tathmini ya athari za mazingira na kupata kibali cha matumizi ya maji. Siyo vibaya kuonana na wanasheria wenu ili waweze kuwasaidia kufanikisha hilo.

## Urithi wa kihistoria wa waanzilishi wa taifa

**Mimi ni mwanaharakati wa kitanzania ninayepigania usawa na haki. Nimegundua kwamba baadhi ya makazi ya viongozi wa zamani yanapewa kipaumbele maalum na kuangaliwa sana kwa kutumia pesa za umma. Je, kuna sheria yoyote inayoitaka serikali kuzitunza sehemu hizo? Je, sheria inaruhusu pesa za umma kutumika kwenye masuala kama hayo?**

*10 Septemba 2012*

Ni kazi na wajibu wa serikali kudhibiti na kusimamia utunzaji, uendelezwaji na kuheshimu urithi wa kihistoria, malighafi za maandishi na vitu vingine vikiwemo vinavyoonekana na visivyoonekana vya waanzilishi wa taifa. Sheria inayosimamia jambo hili ni Sheria ya Waanzilishi wa Taifa (Taratibu za Kuenziwa). Hata hivyo, kwa madhumuni ya usahihi waanzilishi wa taifa ni Rais wa kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Rais wa kwanza wa Zazibar. Hatuna uhakika kama sehemu unayoirejea ni sehemu ya waanzilishi kwa mujibu na maana iliyotolewa na Sheria hii. Hata hivyo hatuoni tatizo kwenye sheria kwani sheria inatunza historia ya taifa letu. Taifa lisilo na historia yake halina maana. Unahitaji kusoma Sheria hii ili kuelewa zaidi taratibu za kuheshimu na kutunza urithi wa kihistoria wa waanzilishi wa taifa letu na masuala yanayohusiana na hayo. Uhifadhi wa namna hiyo siyo mgeni kwa mataifa mengine pia, kuenzi na kuheshimu waanzilishi wa taifa letu ni muhimu.

## Uchimbaji kwenye hifadhi ya misitu

**Mimi ni mchimbaji mdogo na ninataka kununua leseni ya awali ya uchimbaji. Hata hivyo leseni hiyo ni sehemu ya hifadhi ya misitu. Je, hifadhi ya misitu inaathiri haki za uchimbaji. Ninaweza kuinunua? Je leseni hizo zimetafsiriwaje?**

*5 Novemba 2012*

Sheria ya Misitu inaruhusu shughuli za uchimbaji kwenye hifadhi ya misitu lakini ni lazima upate idhini ya Wizara ya Maliasili na Utalii kabla ya kuanza hizo shughuli. Pia kuna ada ya kulipa kwa heka ili kuruhusiwa kuchimba kwenye hifadhi ya misitu.

Sheria ya Madini inatamka kwamba leseni ya awali ya uchimbaji haitatolewa kwa mtu binafsi, ushirika au kampuni isipokuwa (a) Kama ni raia wa Tanzania (b) Kama ni ushirika ni ushirika unaoundwa na watanzania tu (c) Kama ni kampuni (i) iwe ni kampuni inayoundwa na wanachama/wanahisa watanzania pekee (ii) wakurugenzi wake wote ni watanzania na (iii) na umiliki wake wa moja kwa moja au la, ufanywe toka Tanzania na watu wote ambao ni raia wa Tanzania. Kuhusu maana ya leseni ya awali ya uchimbaji, Sheria ya Madini 2010 inatoa maana maalum kwamba ni leseni ya uchimbaji mdogo ambao mtaji wake ni chini ya Dola za Marekani 100,000 au pesa linganifu yake kwa Shilingi za kitanzania.

## Hoteli kufungwa

**Nina hoteli jijini Mwanza katika mwambao wa Ziwa Viktoria. Miezi michache iliyopita baadhi ya maafisa mazingira walikuja kuangalia majengo yetu na sasa wametupa taarifa tufunge hoteli yetu. Wametupatia orodha ya mambo ya kuyafanya kabla ya kuruhusu urejeshwaji wa huduma zetu.**

**Wanawezaje kufunga hoteli namna hii wakati kuna wageni ndani? Baadhi ya matakwa ya amri ya urejeshwaji hayana mantiki, kwani ili tuyatimize, ama itatubidi tuihamishe hoteli yetu kutoka ziwani au basi tuhamishe ziwa kutoka Mwanza. Hii siyo haki. Tafadhali niongoze.**

*25 Machi 2013*

Chini ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira 2004, Baraza lilioanzishwa chini ya Sheria hii lina mamlaka makubwa ya kufungia maeneo ambayo ni tishio kwa mazingira. Viwanda na hoteli pia ni taasisi lengwa na sheria hii. Kifungu cha 151 cha Sheria kinasomeka (1) Kwa kuzingatia masharti yaliyo ndani ya Sheria hii, Baraza linaweza kutoa amri kwa mtu yeyote itakayohusiana na jambo lolote juu ya usimamizi wa mazingira itakayoJulaikana kama amri ya urejeshwaji wa mazingira. (2) Amri kuhusu urejeshwaji wa mazingira itatolewa kwa madhumuni ya (a) kumtaka mhusika kurejesha mazingira yaliyoharibika; (b) kumzuia mhusika asifanye shughuli yoyote inayoweza kuharibu mazingira; (c) kulipisha fidia kutoka kwa mtu anayeharibu mazingira ili kuwalipa waathirika ambao mazingira yao yameharibiwa au maisha yao yameathiriwa na uharibifu huo wa mazingira na kitendo ambacho ndicho kimesababisha kutolewa kwa amri hiyo. (d) kumtoza mhusika fidia ambayo itakadiriwa na Baraza kuwa ni gharama sahihi iliyotumiwa na mtu yeyote mwenye mamlaka ya au asasi iliyoidhinishwa kurejesha mazingira yaliyoharibiwa katika hali yake ya awali kabla ya uharibifu huo.

Amri ya urejeshwaji wa mazingira inaweza kuwa na masharti maalum ambayo ni lazima uyatekeleze kabla ya amri hiyo kuondolewa. Sheria inatamka zaidi kwamba katika kutekeleza mamlaka kwa mujibu wa Sehemu hii, Baraza (a) litaongozwa na misingi ya usimamizi wa ubora wa mazingira kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii; na (b) litawaeleza watu waliopewa amri hiyo haki waliyonayo ya kukata rufaa kwenye vyombo vilivyotajwa vyenye mamlaka ya kusilikiza rufaa. Sheria pia ina vifungu ambavyo vinaanzisha Baraza la Rufaa la Mazingira ambapo unaweza kukata rufaa dhidi ya maamuzi ya Baraza. Kama amri ya urejeshwaji iliyotolewa kwako haitekelezeki, unaweza kukata rufaa. Hata hivyo, kabla ya kufanya hivyo, unatakiwa kusoma tena amri ya urejeshwaji kwa sababu inatuwia vigumu kuamini kwamba Baraza linaweza kuwaamrisha kuondoka kutoka ziwani. Wanasheria wako wanaweza kukuongoza zaidi.

## Leseni kwa ajili ya kulisha wanyama

**Mimi ni raia mwema ninayeishi jijini Dar es Salaam. Ninataka kuiunga mkono Serikali katika sera yake mpya ya Kilimo Kwanza ambayo inalenga kuhamasisha ukuaji wa sekta ya kilimo. Nimepanga kujikita kwenye biashara ya kutengeneza chakula cha mifugo kutoka kwenye rasilimali mbalimbali ambazo zinapatikana kwa wingi na urahisi katika eneo langu. Aidha, nina rafiki yangu kutoka Ulaya ambaye amenipa ofa ya kunitumia mashine ndogo kwa lengo hilo. Hata hivyo, Afisa wa Serikali ya Mtaa wangu ameniambia kwamba ninaweza kuhitajika kuwa na leseni. Je, hii ni kweli? Inakatisha tamaa sana kuona kuna urasimu mwingi katika mpango wa Rais.**

*15 Aprili 2013*

Ukweli ni kwamba unataka kuunga mkono juhudi za Serikali kupitia Sera ya Kilimo Kwanza. Hilo ni wazo zuri lakini halimaanishi kwamba sheria zisifuatwe. Unaonekana kushtushwa sana na sheria zetu nchini Tanzania. Katika sekta yako, kama zilivyo nchi nyingine inasimamiwa, vivyo hivyo Tanzania pia. Kuanzisha biashara yako unahitaji kutekeleza sheria inayosimamia utengenezaji wa vyakula vya wanyama.

Sheria inayosimamia ni Sheria za Nyanda za Malisho na Vyakula vya Mifugo Na. 13 ya 2010. Sheria hii inatoa utaratibu wa usimamizi na udhibiti wa ardhi ya malisho, vyakula vya mifugo na biashara na masuala yanayohusiana na hayo. Kwenye Sheria hii, vyakula vya mifugo vimeelezewa kuhusisha vyakula vya mifugo, virutubisho vya kwenye chakula cha mifugo pamoja na vyakula vya kuongeza virutubisho kwenye vyakula vya mifugo.

Sheria hii pia inaweka kosa kwa mtu kutengeneza vyakula vya wanyama bila kibali. Hivyo ili uweze kufanikisha biashara yako unahitaji kwanza kulisajili eneo ambalo utalitumia kutengeneza vyakula hivyo. Maombi yako ya kibali hiki yanatakiwa kupelekwa kwa Mkurugenzi kwenye moja ya idara za Wizara ya Mifugo na Maendeleo ya Uvuvi.

## Rufaa dhidi ya maamuzi ya waziri

**Nimeomba kibali cha mazingira na nimeambiwa kuwa kuna uwezekano wa Waziri kukataa. Je, akikataa naweza kwenda Mahakamani?**

*14 Oktoba 2013*

Chini ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, limeanzishwa Baraza la Rufaa la Mazingira. Kifungu cha 204 cha Sheria hii kinatamka kwamba Baraza la Rufaa litatekeleza wajibu wa kusikiliza rufaa kwa mujibu wa Sheria hii kuhusu masuala yaliyoletwa mbele yake. Pia, kifungu hicho kinaeleza kwamba mtu yeyote ambaye hataridhika na (a) uamuzi wowote wa Waziri kuhusu; (b) kuwekwa au kushindwa kuwekwa kwa masharti yoyote, ukomo au kizuizi kinachotolewa chini ya Sheria hii au kanuni zilizotungwa chini ya Sheria hii; na (c) uamuzi wa Waziri wa kuidhinisha au kutoidhinisha Tathmini ya Athari kwa Mazingira, anaweza, katika muda wa siku thelathini toka siku ya tukio ambalo haridhiki nalo, kukata rufaa kwenye Baraza la Rufaa kwa utaratibu uliowekwa na Baraza husika.

Kutokana na maelezo hapo juu, njia sahihi kwanza ni kukata rufaa kwenda kwenye Baraza na baadaye, kama hutoridhika na maamuzi ya Baraza, Mahakama Kuu. Kwa upande wako, kwa kuwa maamuzi bado hayajatolewa, unapaswa kwanza kusubiri maamuzi kabla hujaenda kwenye Baraza.

## Amri ya zuio la ujenzi wa jengo

**Ninafanya mradi mdogo wa ujenzi yapata nusu kilomita kutoka ukingo wa mto. Kuna miradi mingine ya ujenzi inaendelea katika eneo hilo, hivyo mradi wangu wa ujenzi siyo wa kwanza kwenye eneo hilo. Wiki chache zilizopita baadhi ya maafisa mazingira wametoa amri ya zuio dhidi ya ujenzi ingawa nina kibali cha ujenzi. Je, hii ni halali na kwa nini ujenzi uhitaji kibali cha mazingira?**

*4 Novemba 2013*

Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004 inatamka kwenye kifungu cha 81 kwamba (1) Mtu yeyote, awe mpendekezaji au mwenye mradi au shughuli ya aina yoyote iliyobainishwa katika Jedwali la Tatu la Sheria hii, ambapo Tathmini ya Athari kwa Mazingira inatakiwa kufanywa kwa sheria inayosimamia mradi au shughuli hiyo au kama haipo sheria hiyo, kwa kanuni zilizotengenezwa na Waziri, atafanya au kuhakikisha tathmini ya athari kwa mazingira ya shughuli au mradi huo inafanyika kwa gharama yake mwenyewe. (2) tathmini ya athari kwa mazingira itafanyika kabla ya kugharamiwa au kuanza kwa mradi au shughuli husika. (3) Kibali au leseni ya kufanya mradi au shughuli yoyote kwa mujibu wa sheria yoyote iliyoandikwa haitampa mpendekezaji au mwenye mradi haki ya kufanya au kusababisha kufanyika mradi au shughuli bila hati ya tathmini ya athari kwa

mazingira iliyotolewa chini ya Sheria hii.

Jedwali la tatu linatoa aina pana zifuatazo; (a) shughuli yoyote isiyoendana na mazingira halisi ya mahali husika; (b) jengo lolote lenye ukubwa usioshabihiana na mazingira ya mahali husika; (c) 1. mabadiliko makubwa katika matumizi ya ardhi. 2. Maendeleo mijini. 3.Usafirishaji. 4.Mabwawa, mito na vyanzo vya maji. 5.Unyunyiziaji toka angani. 6.Uchimbaji madini, au kokoto au mchanga. 7.Shughuli za misitu. 8.Kilimo pamoja na ufugaji. 9.Viwanda vya usindikaji na vya kutengeneza bidhaa. 10. Miundombinu ya umeme. 11. Usimamizi wa haidrokaboni, pamoja na uwekaji au uhifadhi wa gesi asilia na mafuta ya kuendeshea mashine na yale yenye asili ya kulipuka. 12. Utupaji taka. 13. Maeneo ya hifadhi za asili. 14. Mitambo ya kuzuia nguvu za nyuklia. 15. Maendeleo makubwa katika bioteknolojia pamoja na uingizaji na majaribio ya viumbe vilivyofanyiwa mabadiliko ya vinasaba vya kijeni. 16. Shughuli yoyote nyingine kama itakavyoainishwa kwenye kanuni.

Kama unavyoweza kuona maendeleo ya miji yanahitaji tathmini ya athari ya mazingira na hivyo unatakiwa kuomba na kufanyiwa tathmini hiyo na mamlaka husika.

## Aina tofauti za taka

**Nimehamia Tanzania na inaniwia vigumu kuamini kwamba bado hakuna sera/sheria za kuhakikisha kuwa kaya zinalazimishwa kutenganisha taka na kuzipeleka kwenye malori ya takataka kulingana na aina zake. Kukusanya/kulundika taka za kila aina kwa kuzichanganya ni hatari sana kwa mazingira na ni vigumu kuziregesha taka hizo (recycling). Je, hili linaweza kutatuliwa?**

*17 Novemba 2014*

Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004 ina kifungu maalumu kinachohusiana na hili. Kifungu cha 114 (1) kinasema ili kuhakikisha kwamba taka ngumu zinapunguzwa kufikia kiwango cha chini katika maeneo yaliyo chini ya mamlaka yake, Serikali za Mitaa zitaagiza (a) kuwa aina tofauti za taka, takataka, mabaki au uchafu, zichambuliwe na kutenganishwa kwenye chanzo chake; (b) kuweka viwango vya kuongoza aina, saizi, umbo, rangi na vipimo vingine kwa ajili ya jaa za taka zinavyotumika; na (c) kuweka utaratibu kwa kushirikisha viwanda na sekta binafsi na Asasi Zisizo za Kiserikali katika kupanga, kukuza weledi miongoni mwa wazalishaji, wachuuzi, wasafirishaji, watengenezaji viwandani na watu wengine kwa nia ya kupata vibebeo vya taka vinavyofaa na utenganishaji wa taka kutoka kwenye chanzo.

Kwa bahati mbaya, na kwa kadiri ya utafiti wetu, mamlaka za mitaa jijini Dar es Salaam hazijatoa mwongozo wa jinsi gani taka zinaweza kutenganishwa kutokea kwenye vyanzo vyake. Sheria inaeleza kuwa mamlaka za Serikali za Mitaa ni lazima zitoe mwongozo kuhusu hili, lakini kwa kadri tunavyojua hazijafanya hivyo.

Unaweza kwenda moja kwa moja kwenye Serikali yako ya mtaa na kuhoji. Wakishindwa kukujibu au wasipokupa majibu mazuri, basi unaweza kufungua kesi Mahakamani ili Mahakama iamuru Serikali ya mtaa kutenda kwa mujibu wa sheria.

## Kuvua kwa chombo kidogo

**Mimi ni mtaalam wa kigeni ninayefanya kazi nchini Tanzania na ninapendelea kutumia siku za mwisho wa wiki kuvua samaki nikiwa na mwanangu. Hivi karibuni nimeambiwa na mwenzangu kwamba kuvua kwa aina yoyote bila kuwa na kibali hakuruhusiwi, hasa kwa mgeni kama mimi, na kwamba ninaweza kujiingiza kwenye matatizo makubwa ya kisheria. Je, hii ni kweli?**

*22 Desemba 2014*

Sheria ya Uvuvi ya mwaka 2003 inaeleza kwamba mtu yeyote hatajishughulisha na shughuli ya uvuvi bila kuomba na kupata kibali husika cha uvuvi kutoka kwa Mkurugenzi au afisa mwingine yeyote aliyeruhusiwa. Sheria ya Uvuvi inatoa msamaha kwa uvuvi unaotumia njia zifuatazo: (a) uvuvi mdogo wa kutanda uduvi, kuvua kwa kutumia ndoano bila kutumia chombo cha uvuvi bila kujali ni uvuvi wa kujistarehesha, kwa matumizi ya nyumbani au mauzo, isipokuwa kwenye mikondo au mabwawa yaliyotangazwa; na (c) nyavu ndogo.

Kwa jinsi tulivyoelewa swali lako, inaonekana unavua baharini kwa kutumia boti, kitu ambacho hakiangukii kwenye mojawapo ya misamaha. Hivyo, leseni inahitajika na tunakushauri uiombe.

# Wanasheria, Tafsiri ya Sheria na Taratibu za Kimahakama

“

Ni jambo moja kuwa na hoja halali ya kisheria na ni jambo jingine kuelewa na kumudu kanuni na taratibu za uendeshaji kesi mahakamani. Masuala kama sheria ya ushahidi, kupotea nyaraka, ukomo wa muda wa kufungua kesi, tafsiri potofu, ada za mahakama na hata kifo cha mdaawa yanaweza kutokea pasipo kutarajia. Hapa, tunaelezea baadhi ya changamoto za kawaida zinazowakabili wadaawa na namna ya kutatua changamoto hizo.

## Kutoa ushahidi katika shtaka lenye upande mmoja tu

**Niliishtaki kampuni kwenye Mahakama ya Hakimu Mkazi na kesi iliendelea bila mdaiwa kuwepo. Jambo la ajabu wakati hukumu ikisomwa, Mahakama haikunipa ushindi kwa madai kwamba sikuthibitisha vyema kesi yangu. Je, hili ni sawa? Je, Mahakama haikupaswa kuniamini na kunipa hukumu kwa sababu mdaiwa hakusema chochote na hakuita shahidi yeyote kwa sababu hakuwepo?**

*26 Machi 2012*

Ni kanuni/dhana ya kisheria kwamba kila dai lazima lithibitishwe kwa kulinganisha mizania ya uwezekano kati ya pande mbili. Inawezekana hukuthibitisha shauri lako kwa viwango vinavyohitajika. Kwa wakati huu hatuwezi kuilaumu Mahakama kwa sababu hatujui ushahidi gani uliutoa Mahakamani na Mahakama iliupimaje ushahidi huo. Hilo linaweza tu kufanyika baada ya kupitia hukumu na mwenendo wa shauri. Kuwa tu na kesi ya upande mmoja hakumaaniishi kwamba ni lazima ushinde kesi. Ni sawa na kupiga penati kwenye goli la wazi, ambapo uwezekano wa kukosa pia upo.

## Kudanganya mahakama

**Mdai amepeleka Mahakamani kiapo ambacho kimejaa uongo mtupu ndani yake. Kimsingi, uongo mwingine upo wazi kabisa kiasi kwamba Jaji yeyote mjanja anaweza akagundua. Je, kudanganya huko siyo kosa kisheria?**

*6 Agosti 2012*

Kudanganya kwenye kiapo au kutoa ushahidi wa uongo ni kosa. Sheria inatamka kwamba mtu yeyote ambaye, katika kesi yeyote, au kwa ajili ya kuanzisha kesi yeyote, kwa kujua akitoa ushahidi wa uongo kuhusu jambo lolote ambalo ni muhimu kwa hoja yeyote inayotegemewa katika kesi hiyo au inayokusudiwa kutolewa katika kesi hiyo, atakuwa ametenda kosa la kusema uongo na itakuwa sio muhimu kama ikiwa ushahidi umetolewa kwa kiapo au la; kama ushahidi wa uongo umetolewa kwa mdomo au kwa maandishi. Pia, mtu yeyote ambaye atasaidia, atashiriki, atashauri, atatuma, au atashawishi mtu mwingine kutoa ushahidi wa uongo, atakuwa ametenda kosa la kushawishi kutoa ushahidi wa uongo. Ikiwa atatiwa hatiani kwa kosa la kutoa ushahidi wa uongo atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka saba.

## Kodi ya ongezeko la thamani kwenye ada ya mahakama ya biashara

**Mwanasheria wangu alifungua kesi yenye thamani ya mamilioni ya Dola na ada ilikadiriwa kutokana na ankara ya wakili ya asilimia 2. Hata hivyo, kwenye ankara kuna kiambata cha kodi ya ongezeko la thamani. Je, kodi ya ongezeko la thamani inalipwa kwenye ada zinazolipwa Mahakamani?**

*12 Agosti 2013*

Hapana, kodi ya ongezeko la thamani hailipwi. Pia, asilimia 2 kwa Mahakama ya Biashara ukomo wake ni Shilingi milioni 10 na hivyo kama madai ya kwenye kesi yako ni mamilioni ya Dola, ada ya juu kabisa inatakiwa kuwa ni Shilingi milioni 10 na siyo asilimia 2 ya kiasi kinachobishaniwa. Tunakushauri kukokotoa tena kwa sababu unazidisha malipo kwa mujibu wa ankara. Unaweza pia kudai risiti ya malipo halisi ya Mahakamani kutoka kwa wakili wako na risti hiyo itakupa makadirio sahihi.

## Ada za mahakama ya biashara ziko juu sana

**Kuna kesi tunataka kuifungua Mahakama ya Biashara, mwishowe tukakuta ada ni asilimia 3 ya thamani ya dai. Dai letu ni kiasi kinachozidi bilioni 20 na hivyo ada ya**

**Mahakama itakuwa milioni 600. Hakuna namna ya kupunguza ada za Mahakama? Inawezekanaje Mahakama itoze ada kubwa hivyo kwa kesi?**

*13 Agosti 2012*

Mahakama Kuu Kitengo cha Biashara ni moja ya Mahakama zinazopendwa sana Afrika Mashariki na zina Majaji mahiri sana. Sera ya Mahakama hiyo ni kumaliza kesi kwa haraka iwezekanavyo. Penye haraka pana gharama. Malalamiko yako kwenye ada za Mahakama yamefanyiwa kazi siku za hivi karibuni na Kanuni za Ada za Mahakama ya Biashara, 2012, ambazo zimeanza kutumika hivi karibuni. Muundo mpya wa ada ni asilimia 2 ya thamani ya dai isipokuwa ada ya jumla haitazidi Shilingi milioni 10. Kanuni hizi mpya zinafuta kanuni za zamani na hivyo ada ya juu kabisa kwenye Mahakama ya Biashara ni Shilingi za Tanzania milioni 10.

Kanuni hizi pia zinatamka kwamba kama kesi imetatuliwa nje ya Mahakama au kwa majadiliano ndani ya miezi sita tangu ilipofunguliwa, Msajili anaweza kutoa amri kwamba theluthi ya ada hiyo arudishiwe mdaawa aliyeomba.

Na kwa ufafanuzi tu, ada ya zamani haikuwa moja kwa moja asilimia 3 bali kwenye milioni 20 ya kwanza na baadaye asilimia 1. Hivyo kwenye shauri lako la Shilingi bilioni 20, ada ingekuwa Shilingi milioni 204 na siyo Shilingi milioni 600.

## Nyekundu ni damu, nyekundu ni Simba

**Kwa miaka mingi bendera yetu ya taifa ina rangi ya kijani, njano, nyeusi na bluu na kila rangi ikiwa na maana yake. Hata hivyo, kwenye historia ya nchi yetu kumekuwa na vita mbalimbali ikiwemo ile ya Maji Maji ambapo wazee wetu wengi walifariki. Tanzania pia imesaidia nchi nyingine nyingi kwenye mapambano ya kutafuta uhuru na hivyo ninaamini kwamba kungekuwa na rangi nyekundu kwa ajili ya damu kwenye bendera yetu. Pia watanzania wengi ni mashabiki wa timu ya Simba na hivyo rangi nyekundu pia ingekuwepo. Ninawezaje kuendelea ili kutoa pendekezo juu ya hili?**

*20 Agosti 2012*

Sababu zako za kuongeza rangi kwa sababu za kivita na mapambano zinaeleweka. Lakini sababu kwamba watanzania wengi ni mashabiki wa klabu ya Simba haina mashiko sana kwa kubadilisha rangi ya bendera yetu ya taifa kwani wapo washabiki wa Yanga pia ambao nao wana rangi tofauti.

Kifungu cha 5 cha Sheria ya Nembo za Taifa kinatamka kwamba Rais, kwa tamko maalum, anaweza kubadilisha bendera ya taifa au nembo. Ni muhimu kukumbuka kwamba ingawa Rais ana mamlaka hayo, sheria haitaji sababu za Rais kufanya mabadiliko hayo. Ni hiari ya Rais kuona kama sababu zako ni nzuri ama la na iwapo bendera ibadilike ama la. Kama unavyojua, bendera yetu haijawahi kubadilika tangu mwaka 1964. Kwa mabadiliko yoyote, utatakiwa upeleke wazo lako kwa Rais ili alizingatie.

## Sheria za Tanzania zinawataja wanaume pekee

**Nimesoma sheria nyingi za Tanzania (zilizoandikwa kwa Kiingereza), wakati wote zinataja jinsia ya kiume pekee. Atafanya hiki, atafanya kile, atawajibika kwa, n.k. Je, hii ina maana sheria hazitumiki kwa jinsia dhaifu - ya kike.**

*20 Agosti 2012*

Uko sawa kwamba sheria kwa lugha ya Kiingereza inawataja wanaume lakini haiwaondoi wanawake. Sheria ya Utafsiri wa Sheria (Interpretation of Laws Act) ambayo kwa ujumla inatumika kutafsiri sheria zote inatamka wazi kwenye kifungu

cha 8 kwamba, katika sheria yoyote maneno yanayoonyesha jinsia ya kiume (he, his) yatajumuisha vilevile jinsia ya kike (she, her); maneno yanayoonyesha jinsia ya kike yatajumuisha pia jinsia ya kiume; maneno ya umoja yatajumuisha vilevile wingi na maneno ya wingi yatajumuisha umoja. Hivyo popote inapoleta maana, sheria inatumika kwa jinsia zote ya kike na kiume.

## Usiri kati ya mwanasheria na mteja wake

**Usiri wa mahusiano ya mwanasheria na mteja wake ni nini na je, dhana hiyo inatumikaje hapa Tanzania? Ninawezaje kuwa na uhakika kwamba ninalindwa ninapoongea na mwanasheria wangu? Ninaweza kutoa taarifa zote kwa mwanasheria?**

*20 Agosti 2012*

Usiri baina ya mwanasheria na mteja wake ni moja kati ya mafaa ya zamani sana yanayotambulika kisheria. Msingi wake mkuu ni kwamba, upendeleo huu unamhakikishia mtu anayetafuta ushauri au huduma kutoka kwa mwanasheria kuwa huru na kutokuogopa kwamba siri zake zitafichuliwa. Msingi wake mkuu ni kutoa ushauri bora wa kitaalam. Kukiwa na uhakika wa usiri wa taarifa atoazo kwa wakili wake, mteja anazungumza kwa uwazi na ukweli na kumpatia taarifa zote wakili wake. Kwa maneno mengine, mteja akiwa amekingwa na upendeleo, anakuwa na utayari zaidi kuwasiliana na wakili wake vitu ambavyo asingeweza kuvizungumza. Kinadharia, uwazi na uaminifu huo utamsaidia mwanasheria katika kutoa ushauri sahihi na wa kitaalamu zaidi, na mteja atakuwa salama akielewa kwamba maelezo yake kwa mwanasheria hayatatumika dhidi yake.

Kisera na kihaki, upendeleo wa mwanasheria na mteja una athari za moja kwa moja: mwanasheria kwa lazima ama kwa hiari yake hawezi kuweka wazi masuala aliyoyapata kwa usiri kutoka kwa mteja wake wakati alipotafuta ushauri wa kisheria kwake. Ingawa hakuna mtazamo/uamuzi mmoja kuhusiana na upendeleo wa mwanasheria na mteja, lakini unafafanuliwa kama ifuatavyo; kama mwanasheria ameombwa ushauri wa aina yoyote akiwa kama mwanasheria, mawasiliano yanayohusu ushauri huo, yaliyotolewa na mteja kwa siri, moja kwa moja yatalindwa na hayatatangazwa na mteja wala mwanasheria wake, isipokuwa tu kama kutakuwa na idhini ya kuyaweka wazi.

Hivyo, bila kujali upendeleo wa mwanasheria na mteja unatekelezwa vipi, kuna mambo manne ya msingi ya kuzingatia ili kuonesha kwamba kuna upendeleo huo: (1) Mawasiliano (2) yaliyotolewa na watu wenye mafaa/upendeleo (3) kwa siri (4) kwa lengo la kutafuta, kupata au kutoa msaada wa kisheria kwa mteja.

Wakati wote inashauriwa uangalie mgongano wa maslahi ili kuhakikisha kwamba mwanasheria wako hamuwakilishi mteja wa upande wa pili. Kitu kibaya ni pale wewe na mtu mwenye mgogoro nae mnashirikiana mwanasheria mmoja. Kama zilivyo nchi nyingine zenye mfumo wa sheria ya Kiingereza (Umoja wa Madola), upendeleo wa mwanasheria na mteja upo pia nchini Tanzania.

## Mashahidi zaidi kwenye rufaa

**Mwaka 2001 mimi na wenzangu tulishtakiwa Mahakama ya Wilaya kwa makosa mawili; kuiba kwa mtumishi wa umma pamoja na kukutwa na silaha hatarishi. Baada ya kusikilizwa, sikuwa na kesi ya kujibu tofauti na watuhumiwa wenzangu. Jambo la kushangaza, Mkurugenzi wa Mashtaka alikata rufaa Mahakama Kuu na Jaji aliwaita tena mashahidi watatu na alimuita shahidi mwingine mmoja mpya na kusikiliza**

**ushahidi wao. Mwishowe, Mahakama Kuu ilibatilisha amri ya kuachiwa kwangu na kueleza kwamba nina kesi ya kujibu na hivyo nijiunge na watuhumiwa wenzangu kwa ajili ya utetezi kwenye Mahakama iliyokuwa inasikiliza shtaka hilo. Je, Jaji alikuwa sahihi kusikiliza ushahidi mpya?**

*10 Septemba 2012*

Chini ya Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, sheria inaruhusu Mahakama katika hatua yoyote ya shauri kumuita mtu yeyote kama shahidi au kumuita tena, kama ushahidi wake unaonekana kuwa ni muhimu kwa uamuzi wa haki wa kesi. Pia Mahakama ina mamlaka katika kushughulikia rufaa kutoka Mahakama ya chini, na iwapo itaona ushahidi wa ziada ni muhimu, inaweza ama kuchukua ushahidi huo au kuagiza uchukuliwe na Mahakama ya chini. Hata hivyo Mahakama Kuu ni lazima irekodi sababu za kuchukua ushahidi wa ziada na isitumie vibaya uhuru huo na kugeuza kesi kuanza upya, kuziba mapengo ya kesi ya Jamhuri au kubadilisha aina ya kesi dhidi ya mtuhumiwa. Hatuna rekodi za Mahakama na hivyo hatuwezi kutoa maoni ya iwapo Mahakama Kuu ilieleza sababu za kuita ushahidi huo. Wanasheria wako wanaweza kukuongoza zaidi.

## Majaji wanaharibu karatasi

**Mimi ni wakili mpya na nilikwenda kupitia faili la Mahakama ambalo ninahusika nalo. Kitu kikubwa ambacho sikuridhika nacho ni kwamba niliona Jaji anatumia ukurasa mmoja kuandika mistari michache kwa maandishi mkubwa ambayo hata mwenye chongo anaweza kusoma. Je, huu siyo upotevu wa rasilimali za umma? Kama majaji wote wanaandika kama hivyo, tunahitaji kukata miti mingi zaidi kuzalisha karatasi. Kwa nini majaji wasipunguze matumizi ya karatasi?**

*17 Septemba 2012*

Kutokana na maelezo yako hapo juu, haujaridhika na namna Majaji wanavyotumia nafasi za kwenye karatasi; yaani, pale wanapoandika mienendo ya kesi wanapoteza karatasi nyingi kwa kuandika kwa maandishi makubwa. Huu ni mtazamo unaobadilika lakini kama unaona maandishi ni makubwa sana, labda unaweza kumuandikia Jaji Mkuu ukimpa wazo lako na yeye anaweza kuwaandikia majaji na mahakimu kutumia karatasi vyema. Siyo vibaya kumuonesha Jaji Mkuu baadhi ya karatasi zenye maandishi hayo makubwa ili aweze kupata uhalisia wa suala lako.

## Kesi isiyomalizika

**Nilifungua kesi ya kudai fidia Mahakama ya Wilaya Kinondoni Dar es Salaaam. Hii ni mara ya sita kesi inaahirishwa eti kwa sababu hakimu anaumwa. Mtu anayeahirisha kesi yenyewe hana hata utashi wa kutoa haki achilia mbali utashi wa kuita kesi mapema. Tunakwenda Mahakamani na kukaa masaa mengi na mwishowe tunaambiwa hakimu hayupo. Hakuna anayeiona Mahakama hii kuwa inafaa na ni bora ikafungwa ili majengo yake yatumike kwa shughuli nyingine za kiserikali kuliko Mahakama zisizo na kazi. Kutokana na kuchelewa niliamua kwenda kuifungua Kisutu kwa sababu niliambiwa ni Mahakama ya haraka, lakini upande wa pili umeniwekea pingamizi kwamba siwezi kufungua kesi hapa. Nifanye nini?**

*24 Septemba 2012*

Tunasikitika kusikia kuhusu ucheleweshaji unaokutana nao. Kama unaona usimamizi wa Mahakama hiyo siyo mzuri, unaweza kumuandikia Jaji Mkuu barua ya malalamiko ambaye anaweza kuamuru kesi ihamishiwe kwa hakimu mwingine ili aendelea na shauri lako. Masuala kama haya, kwa kawaida, huwa hayaripotiwi kwa Jaji Mkuu, ila yakiwa

yanalipotiwa (tunadhani) Mahakama zitajirekebisha.

Sasa tujibu swali lako, sheria yetu inakataza kufungua kesi mpya kama kuna kesi nyingine inaendelea katika Mahakama nyingine juu ya dai/suala hilohilo na kati ya wadaawa wale wale. Hili limetamkwa kwenye kifungu cha 8 cha Sheria ya Mwenendo wa Kesi za Madai kwamba hakuna Mahakama itakayosikiliza shauri au sehemu ya shauri ambalo lina uhusiano wa moja kwa moja au linafanana na shauri la awali kati ya wadaawa wale wale au mmoja wapo akidai kuhusu suala lile lile au linalofanana na shauri ambalo lilishafunguliwa na kutolewa maamuzi na Mahakama yenye mamlaka ya kutoa nafuu inayoombwa. Uwezekano ni mkubwa kwamba pingamizi litafanikiwa na utajikuta umerudi tena Mahakama ya Wilaya ya Kinondoni. Mwanasheria wako anaweza kukuongoza zaidi.

## Kutafsiri sheria

**Kuna kesi inanihusu ambapo sheria haipo sawa kwa maana kwamba kuna baadhi ya maneno yenye utata lakini ni muhimu sana kwenye kufanikiwa au kushindwa kwa kesi yangu. Kila upande unajaribu kutafsiri sheria kwa upande wake. Je, sheria inatakiwa itafsiriweje? Kwa nini watunga sheria wasiandike sheria katika namna isiyoleta mkanganyiko kama huo?**

*8 Oktoba 2012*

Kanuni ya kwanza ya tafsiri ya sheria ni kwamba maneno au virai kwenye sheria za kitaalamu vinatafsiriwa katika maana za kitaalamu. Vinginevyo, maneno hayo yatatumika katika maana zake za kawaida. Maneno na virai pia ni lazima vitafsiriwe kwa kanuni za kisarufi. Hizi ni baadhi ya nyenzo za tafsiri za maana za kawaida za sheria. Kesi mbalimbali zimetamka kwamba kama hakuna cha kurekebisha, kuondoa au kuboresha kwenye sheria husika, maneno na sentensi kwenye sheria hiyo yanapaswa kutafsiriwa katika maana zake za kawaida na za asili.

Njia nyingine ya kutafsiri sheria ni kanuni ya dhamira ambayo majaji wanaitumia kugundua dhamira ya bunge. Katika kutumia kanuni hii, kimsingi Mahakama inajiuliza swali, je nini tatizo ambalo sheria iliyopita haikuweza kutatua na bunge lilitaka litatuliwe wakati wanatunga sheria hii ambayo Mahakama inaipitia?

Njia nyingine ya kawaida inayotumika ni kanuni-dhahabu (golden rule) ambayo inamruhusu jaji kuacha maana ya kawaida ya neno ili kuepuka matokeo yasiyotarajiwa. Kwa bahati mbaya hujatuambia ni sheria gani au ni maneno gani ambayo yanabishaniwa lakini ukitafsiri sheria husika kanuni hizo hapo juu zinaweza kutumika.

Kujibu swali lako la pili, kwamba ni kwa nini mwandishi wa sheria asikaze sheria ili kuepuka mianya, unaweza kuona kwamba wakati mwandishi anapoandika anaweza kushindwa kutabiri mazingira au matukio yote. Kikubwa ni kwamba sheria inabadilika ili kuendana na kesi zinazoibuka mara kwa mara na ili kuhakikisha kwamba sheria inabaki na uhalisia wakati wote. Kuandika sheria siyo kazi rahisi.

## Mkalimani anapotosha mahakama

**Nilikuwa na kesi ambapo upande mwingine ulikuwa unatoka nje ya nchi na ulikuwa na mkalimani. Baada ya kesi kuisha kuna mtu aliniambia kwamba mkalimani hakuwa mkweli wakati anatafsiri. Je, hilo siyo kosa?**

*3 Desemba 2012*

Hakika ni kosa. Kanuni ya Adhabu inaeleza wazi hali kama hiyo, isemapo kwamba mtu yeyote ambaye, ameapishwa kama mkalimani katika kesi, kwa makusudi akitoa maelezo muhimu katika kesi hiyo huku akijua kuwa

ni ya uongo, au ambayo haamini kuwa ni ya kweli, atakuwa ametenda kosa la ushahidi wa uongo. Kifungu cha 104 kinaeleza zaidi kwamba mtu yeyote anayetenda kosa la kutoa ushahidi wa uongo au kushawishi ushahidi wa uongo atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka saba. Hata hivyo, kifungu cha 105 kinatamka kwamba Mahakama haitamhukumu mtu aliyetoa ushahidi wa uongo au aliyeshawishi mtu mwingine kutoa ushahidi wa uongo kwa kutegemea ushahidi wa mtu mmoja tu katika kuthibitisha uongo wa habari yoyote inayodaiwa kuwa ni ya uongo.

## Amri ya mahakama ya kuondolewa kielelezo/kizibiti

**Miaka michache iliyopita niliibiwa redio yangu. Nilitoa taarifa polisi na baada ya uchunguzi, redio hiyo ilipatikana kwenye nyumba ya mtuhumiwa ambaye baadaye alishtakiwa Mahakamani kwa kosa la wizi. Polisi walibaki na redio yangu kama kielelezo. Baada ya mahudhurio ya muda mrefu Mahakamani pasipo kusikilizwa, mwendesha mashtaka aliiomba Mahakama kuondoa shtaka dhidi ya mtuhumiwa na hivyo mtuhumiwa aliachiwa huru. Nimeshauriwa kupeleka maombi kwenye Mahakama hiyo hiyo ili kupata amri ya kuwaruhusu polisi kuiachia redio yangu. Ni nyaraka gani nahitaji kuwa nazo? Na uwezekano wa kufanikiwa ukoje?**

*10 Desemba 2012*

Sheria inamruhusu mwendesha mashtaka kuondoa kesi Mahakamani lakini huo siyo mwisho wa kesi. Polisi wana hiari ya kumkamata tena mtuhumiwa na kumfungulia mashtaka upya. Hatuna hakika kama polisi bado wana nia ya kuendelea na kesi dhidi ya mtuhumiwa. Tukichukulia kama polisi wanakusudia kufungua tena kesi, wanao uhuru wa kuendelea kuishikilia redio yako kama sehemu yao ya ushahidi.

Kwa upande mwingine, kama polisi wameacha kuendelea na mashtaka dhidi ya mtuhumiwa, unastahili kuchukua redio yako kama kweli ni yako. Kwa maoni yetu, kwa kuwa hakuna shtaka lililobadilishwa dhidi ya mtuhumiwa, Mahakama haina mamlaka tena kuhusiana na shtaka hilo lililoondolewa. Njia ya haraka ya kupata redio yako ni kuifuatilia polisi. Kama hiyo ikishindikana, mwanasheria wako anaweza kukuongoza zaidi juu ya taratibu za kupeleka maombi maalum Mahakamani.

## Sifurahishwi na kanuni za mahakama ya biashara

**Nimesoma kwa masikitiko makubwa Kanuni za Mahakama ya Biashara ambazo zimetumwa kwenye mabenki na sijafurahishwa na urasimu uliowekwa kwenye Kanuni hizi. Nafikiri kuna ajenda ya kujaribu kuifanya Mahakama ya Biashara kuwa kama Mahakama nyingine – za taratibu na kuchosha.**

*3 Desemba 2012*

Hatuna uhakika ulitaka kuuliza nini hapo juu. Kimsingi, tulipoona swali lako hatukuwa na uhakika wa namna ya kulijibu. Hata hivyo baada ya kusoma na kutokukubaliana kabisa na maoni yako, tunatumia fursa hii kukuongoza kwenye vifungu vichache vya kanuni hizi mpya za Mahakama ya Biashara, ambazo hasa zinakusudia kumaliza kesi kwa haraka. Pia tuna mashaka kama Kanuni za Mahakama ya Biashara ulizosoma ni sahihi kwa sababu kwenye Kanuni hizi kila kitu kimekusudia kuepuka ucheleweshaji.

Kanuni ya 17 inatamka kwamba (1) bila kujali Kanuni ya 9 hadi 33 ya kifungu cha 33 cha Sheria ya Mwenendo wa Kesi za Madai, njia mbadala ya wito inaweza kufanyika kwa barua-pepe au faksi kwa kutumia anuani ambayo ilitolewa au iliyokuwa ikitumiwa

na pande zote kwenye mahusiano yao ya biashara. (2) nakala ya wito itatumwa moja kwa moja Mahakamani kwa njia ya mtandao. (3) Kwa kuondoa shaka, ripoti ya mtandao kwamba imetumwa itachukuliwa kama ushahidi kwamba wito umefika. Hivyo unaweza kuona kwamba kanuni mpya zimeanzisha mfumo huu mpya wa wito kwa njia ya kielektroniki.

Kanuni ya 32 inatamka (1) isipokuwa kwa mazingira ambayo hayajatolewa kwenye kanuni hizi, Vifungu vya VIIIA na VIIIB vya Sheria ya Mwenendo wa Kesi za Madai havitatumika kuamua kasi ya kesi za biashara. (2) Kesi zote za biashara zitaamuliwa ndani ya miezi kumi tangu siku zinapoanza, na siyo zaidi ya miezi kumi na miwili. (3) Ndani ya siku 30 kabla ya kuisha kwa muda uliowekwa na kanuni ndogo (2) upande wowote wa kesi unaweza, kwa mdomo kuomba kuongezwa muda wa kesi kuisha, na Mahakama baada ya kuridhika na sababu za msingi zilizotolewa, itakubali ombi hilo kwa gharama za upande uliiomba kuongezwa muda, isipokuwa kama itaamuru vinginevyo. Hivyo, unaweza kuona kwamba kwenye kanuni hizi kesi ni lazima iishe kwa kipindi cha miezi 12, kitu ambacho ni cha manufaa kwa benki.

Kanuni ya 58 inatamka kwamba Mahakama inaweza, kwa maombi ya upande wowote, kuruhusu shahidi kutoa ushahidi bila kuwa kwenye chumba cha Mahakama, kupitia video kwa gharama za muombaji. Hapa pia unaweza kuona kwamba siyo lazima shahidi atoke mbali na kuja Mahakamani kuhudhuria usikilizwaji wa kesi. Anaweza tu kutoa ushahidi kupitia mtandao kitu ambacho kinaweza kuokoa muda na kuokoa gharama pia.

Kanuni ya 67 inatamka kwamba (1) Mahakama, baada ya kumaliza kusikiliza kesi, itatoa maamuzi ndani ya siku sitini kama ni hukumu na ndani ya siku thelathini kama ni maamuzi madogo. (2) Ikiwa jaji atashindwa kutimiza masharti ya kanuni ndogo (1) ataeleza kwenye rekodi ya Mahakama sababu za kushindwa kufanya hivyo.

(3) Mwishoni mwa kila hukumu, Mahakama itaweka, kwa ufupi, nafuu zilizotolewa na Mahakama. Hii pia ina faida kwa benki kwa sababu itawahakikishia maamuzi ya haraka.

Mara nyingi mawakili wanakwenda Mahakamani bila kujiandaa  na hivyo kuanza kusoma mafaili kwenye korido za Mahakama. Hili limetatuliwa na Kanuni ya 44 inayotamka kwamba (1) Wakili anayekuja Mahakamani ni lazima (a) awe na uelewa wa kesi na ameruhusiwa kufanya makubaliano yote ya msingi na ya kikanuni, kwa niaba ya mteja; na (b) ajiandae kujadili maombi yoyote ambayo yamewasilishwa na ambayo bado hayajaisha. (2) Kushindwa kutekeleza masharti ya kwenye kanuni hii kutapelekea wakili kulipa gharama, isipokuwa kama kutakuwa na sababu za msingi.

Kanuni ya 64 inaanzisha utaratibu wa hoja fupi za maandishi ambapo inatamka kwamba hoja zitafanyika kwa mdomo zikitanguliwa na hoja fupi za maandishi ambazo zitatolewa kwa Jaji angalau siku tatu za kazi kabla ya siku ya kutolewa kwa hoja za mdomo, isipokuwa kwamba kushindwa kupeleka hoja fupi za maandishi haitakuwa sababu ya kuahirisha au kuongeza muda ili kupeleka hoja hizo na kwamba kesi itaendelea kusikilizwa bila kujali kwamba hoja hizo za maandishi hazijaletwa Mahakamani.

Ushahidi wa awali hivi sasa utatolewa kwa kiapo chini ya Kanuni ya 49 ambayo inatamka kwamba (1) kwa shauri lolote lililoanza kwa hati ya madai, ushahidi wa awali utatolewa kwa maelezo ya kiapo. (2) Maelezo yataletwa ndani ya siku saba za kukamilika kwa mapatano na kutolewa kwa upande mwingine kama ilivyoelekezwa na Mahakama. Isipokuwa kwamba jukumu la kuwapa mashahidi hoja halihusiani na jukumu la kuleta hoja hizo Mahakamani

na kuwapatia upande mwingine. Hili pia litapunguza muda wa kumaliza kesi.

## Tarehe ya kuanza kutumika kwa sheria

**Ni wakati gani sheria inaanza kutumika? Napata ugumu sana kufahamu ni lini sheria inapoanza kutumika na kinyume chake. Vipi kuhusu kanuni zilizotungwa chini ya sheria hiyo? Vipi kama Kanuni zinaleta vifungu vipya ambavyo havipo kwenye sheria mama?**

*24 Desemba 2012*

Sheria ya Utafsiri wa Sheria inaelezea ni wakati gani Sheria itaanza kutumika. Kifungu cha 14 kinatamka kwamba kila sheria itaanza kutumika katika tarehe ya kuchapishwa kwake katika Gazeti la Serikali, isipokuwa kama imeelekezwa vinginevyo au kama imeelekezwa katika sheria husika au katika sheria nyingine kwamba sheria hiyo itaanza kutumika katika tarehe nyingine, itaanza kutumika tarehe hiyo. Sheria hii pia inatamka kwamba ikielekezwa kwamba sheria itaanza kutumika siku fulani, basi sheria hiyo itaanza kutumika kuanzia alfajiri ya siku hiyo.

Pale ambapo inaonekana tarehe katika nakala ya Sheria iliyochapishwa, au inayodaiwa kuchapishwa na Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali, ikionesha kuwa ndiyo tarehe ambapo Rais aliridhia na kusaini Sheria hiyo au sehemu yake, tarehe hiyo inayoonekana ndiyo itakayochukuliwa kama ushahidi kuwa siku hiyo ndiyo ambamo Rais aliweka saini yake katika Sheria hiyo, na Mahakama zitaridhia hivyo. Hivyo ili uweze kuelewa ni lini Sheria itaanza kutumika, utahitaji kusoma Sheria yenyewe na kuona kama kuna tarehe nyingine imetajwa, vinginevyo ni tarehe ya kuchapishwa kwenye Gazeti la Serikali.

Kuhusu Kanuni, Sheria ya Utafsiri wa Sheria inatamka wazi kwamba Sheria Ndogo haitakuwa kinyume na masharti ya Sheria Mama ambayo imetoa mamlaka ya kutungwa kwa Sheria Ndogo hiyo, au sheria nyingine, na Sheria Ndogo itakuwa batili kwa kiasi inachokinzana na matakwa ya Sheria Mama. Pia, pale Sheria Ndogo inapoelekea kutungwa kwa kutekeleza mamlaka fulani au mamlaka nyingine, itachukuliwa kuwa imetungwa kwa kutekeleza mamlaka zote ambazo zimepelekea kutungwa kwa Sheria hiyo. Itachukuliwa kwamba panapokuwa hakuna ushahidi vinginevyo, masharti yote na hatua za mwanzo muhimu ya kutungwa kwa Sheria Ndogo zitakuwa zimefuatwa na kutekelezwa.

Sheria hii pia inaeleza kwamba pale Sheria inatoa uwezo wa kutunga Sheria Ndogo, itachukuliwa kwamba imejumuisha mamlaka ya kutekeleza kwa utaratibu kwa namna hiyo na kwa mujibu wa masharti (kama yatakuwepo) ya kurekebisha au kufuta Sheria Ndogo yoyote; na kama mtu aliyepewa mamlaka hayo atakuwa amebadilishwa kabisa au kupewa mtu mwingine, uwezo uliotolewa chini ya kifungu kidogo hiki, juu ya mtu wa mwanzo unaweza ukafanywa na mtu aliyebadilishwa juu ya mambo yote au vitu ambavyo viko chini ya mamlaka yake kama vile ni mtu wa mwanzo. Na pale ambapo Sheria inampa uwezo mtu wa kutunga Sheria Ndogo kwa madhumuni ya jumla na pia kwa madhumuni yoyote maalum yanayohusiana na maudhui hayo, kutajwa kwa madhumuni maalum hakutaathiri ujumla wa mamlaka au uwezo wa kutunga Sheria kwa madhumuni ya jumla yaliyoainishwa.

## Ushahidi wa kielektroniki mahakamani

**Mpenzi wangu wa zamani anaendelea kunitumia barua-pepe za vitisho, dharau na maneno machafu zenye nia ya kuniumiza. Nimevumilia kwa muda mrefu lakini anaendelea na sasa anatuma barua-pepe zinazonihusu kwa familia yangu. Nilitaka**

**kutoa taarifa polisi kwa sababu najua ni kosa la jinai lakini wengine wananiambia ni kupoteza muda kwa sababu sina ushahidi mwingine zaidi ya barua-pepe. Tafadhali nishauri iwapo barua-pepe zinakubalika Mahakamani kama ushahidi.**

*31 Desemba 2012*

Sheria ya Ushahidi iliyofanyiwa marekebisho inabainisha kwamba ushahidi wa kielektroniki unapokelewa Mahakamani kama ushahidi mwingine. Pia kuna maamuzi ya Mahakama Kuu ambapo Jaji aliruhusu ushahidi wa kielektroniki, hivyo ushahidi huo unaweza kupokelewa Mahakamani.

Hata hivyo, upande wa pili unaweza kupinga upokelewaji wa barua-pepe hizo kwa sababu za kisheria na Mahakama itafanya maamuzi kuhusu hilo. Tunakusisitiza utoe taarifa polisi juu ya jambo hili, na kuzitoa barua-pepe hizo kama ushahidi na sheria itachukua mkondo wake.

## Kusimamiwa na mwanasheria ambaye si Mtanzania

**Nilishindwa kesi Mahakama Kuu, Dar es Salaam na nimeamua kukata rufaa. Je, mwanasheria wangu wa Uingereza ambaye anafanya kazi huko London anaruhusiwa kuniwakilisha Mahakama ya Rufaa ingawa tumekwisha kufungua rufaa? Je, ni kipindi gani cha notisi ambacho Mahakama ya Rufaa inatoa kabla ya kupanga kusikiliza rufaa?**

*11 Machi 2013*

Kuna wanasheria wengi wenye uwezo nchini Tanzania; hata hivyo, kama bado unaamini kwamba mwanasheria wako wa Uingereza anaweza kuwa bora zaidi kwenye kesi hiyo, basi Kanuni za Mahakama ya Rufaa [Kanuni ya 33 (4)] inasema kwamba mtu yeyote anayeweza kuwakilisha kama wakili au mwanasheria kwenye Mahakama yoyote yenye mamlaka isiyo na ukomo katika nchi yoyote ya Jumuiya ya Madola, kama atapewa leseni na Jaji Mkuu na kwa sharti la kulipa ada maalum, atakuwa na haki ya kusikilizwa mbele ya Mahakama kuhusiana na rufaa yoyote au maombi, ikiwa ni pamoja na rufaa kinzani inayosikilizwa ndani yake, au rufaa mbili au zaidi au maombi yaliyounganishwa kwa ajili ya kusikilizwa. Hivyo mwanasheria wako wa Uingereza anaweza kukuwakilisha Mahakama ya Rufani kwa masharti ya kupata leseni kwanza kutoka kwa Jaji Mkuu. Tafadhali elewa kwamba Jaji Mkuu anaweza kukukatalia maombi yako, hivyo kuwasilisha maombi peke yake haimaanishi kwamba utakubaliwa.

Kuhusu taarifa ya awali ya kusikiliza, Kanuni zinatamka kwamba Msajili wa Mahakama ya Rufani atazipatia pande zote mbili za rufaa taarifa katika kipindi kisichoopungua siku kumi na nne kuhusu tarehe iliyopangwa kusikilizwa rufaa; lakini haitakuwa lazima kuupatia upande wowote taarifa hiyo ya siku ya kusikiliza kama uliridhia siku hiyo ya kusikilizwa kwa rufaa. Vile vile elewa kwamba Kanuni zinatoa taratibu pale unapobadilisha mwanasheria wako na zinatamka kwamba pale upande wenye maombi au rufaa unapobadilisha wakili, au ukiwa unawakilishwa na wakili, unaamua kujiwakilisha wenyewe au, baada ya kujiwakilisha wenyewe unaamua kumhusisha wakili, kwa haraka iwezekanavyo, utatoa taarifa kwa Msajili juu ya mabadiliko na utaupatia upande mwingine unaojiwakilisha au unaowakilishwa, kama itakavyokuwa.

## Hakuna msimamizi wa mirathi ya marehemu

**Miaka mitano iliyopita nilifungua shauri la ardhi Mahakamani ili kurudishiwa ardhi yangu ambayo majirani zangu walivamia na kujenga nyumba. Wakati kesi ikiendelea, mlalamikiwa/mshtakiwa alifariki na nimearifiwa kuwa kulingana**

**na suala lenyewe, haki yangu ya kushtaki inaendelea licha ya kifo chake. Tatizo ni kwamba hakuna mtu yeyote aliyeomba kuteuliwa kuwa msimamizi wa mirathi. Inavyoonekana hakuna. Ni miaka miwili tangu kesi isimame kwa sababu hii. Nifanye nini? Ninahitaji kesi hii iendelea kwa sababu nitashindwa kuiendeleza ardhi kutokana na kupanda gharama za ujenzi.**

*18 Machi 2013*

Ni kweli iwapo wakati kesi inaendelea na mshtakiwa akifariki haki ya mashtaka inaendelea, kesi haifi badala yake Mahakama inaweza, baada ya kuombwa, kumruhusu msimamizi wa mirathi ya marehemu ili kuendelea na shauri. Kwenye kesi yako kuna uwezekano mkubwa marehemu hana mwakilishi wa kisheria wa kuunganishwa kwenye kesi. Tukichukulia maelezo uliyotupatia ni sahihi, kama unaweza kuiridhisha Mahakama kwamba marehemu hana mwakilishi, inaweza kuendelea kusikiliza kesi yako bila kuwepo kwa muwakilishi wa marehemu.

Mbadala wake, tunakushauri uombe Mahakamani ili Wasii au Afisa wa Mahakama ateuliwe ili kuwakilisha mirathi ya marehemu kwa madhumuni ya shauri na hukumu yoyote au tuzo itakayotolewa itambana Wasii au Afisa wa Mahakama kama ambavyo ingembana msimamizi wa mirathi ya marehemu angekuwa sehemu ya kesi, lakini kabla Mahakama haijamteua Wasii au Afisa wa Mahakama kuwa msimamizi wa mirathi ya marehemu, kama itakavyokuwa, itatoa taarifa kwa watu wote wenye maslahi na mirathi ya marehemu. Unashauriwa hivyo.

## Huduma za kielektroniki kwenye kesi

**Siwezi kumpata mlalamikiwa kwenye kesi yangu ya biashara ambayo nimeifungua kwenye Mahakama ya Biashara jijini Dar es Salaam. Mwanasheria wangu anasema tunaweza kumpatia kwa njia ya barua-pepe. Je, sheria yetu inaruhusu hilo? Ni kwa kasi gani kesi inatakiwa kuendeshwa kwenye Mahakama ya Biashara?**

*18 Machi 2013*

Kanuni za Mwenendo wa Mashauri Mahakama ya Biashara, Kanuni ya 17 inatamka kwamba bila kujali Kanuni ya 9 hadi 33 ya kifungu cha 33 cha Sheria ya Mwenendo wa Kesi za Madai, njia mbadala ya wito inaweza kufanyika kwa barua-pepe au faksi/nukushi kwa kutumia anuani ambayo ilitolewa au iliyokuwa ikitumiwa na pande zote kwenye mahusiano yao ya biashara. (2) nakala ya wito itatumwa moja kwa moja Mahakamani kwa njia ya mtandao. (3) Kwa kuondoa shaka, ripoti ya mtandao kwamba imetumwa itachukuliwa kama ushahidi kwamba wito umefika.

Kuhusu suala la kasi, Mahakama ya Biashara ipo kwa ajili ya kumaliza kesi mapema. Zaidi, kanuni ya 32 (2) inatamka kwamba ndani ya siku 30 kabla ya kuisha kwa muda uliowekwa na kanuni ndogo (2) upande wowote wa kesi unaweza, kwa mdomo kuomba kuongezwa muda wa kesi kuisha, na Mahakama baada ya kuridhika na sababu za msingi zilizotolewa, itakubali ombi hilo kwa gharama za upande uliiomba kuongezwa muda, isipokuwa kama itaamuru vinginevyo. Hivyo muda wa juu kabisa wa kesi kusikilizwa Mahakama ya Biashara ni miezi 12 isipokuwa kama kuna maombi ya kuongezwa muda yamefanyika na kuridhiwa na Mahakama.

## Akidi bungeni

**Mimi ni mwanasheria wa kigeni na nilitembelea Tanzania miezi michache iliyopita. Nilikuwa nafuatilia vikao vya bunge lenu na nilishangaa kuona ukumbi wa bunge kuwa na wabunge wachache sana. Nashangaa ni kivipi bunge linaweza**

**kuendelea na majadiliano kama wabunge hawapo ukumbini. Katika nchi nyingine, na hata katika baadhi ya sheria, mfano vifungu vya Sheria ya Makampuni (Companies Act), zinaweka idadi ya chini inayotakiwa (akidi) kuwepo kabla ya kikao kuendelea. Nafasi ikoje kwa Tanzania? Pia, je Tanzania ina kinga sawa na nchi nyingine kuhusu kuwashtaki wabunge kwa maneno yaliyotamkwa wakati wa vikao vya bunge? Vipi kama mapigano yakiibuka ndani ya bunge?**

*5 Agosti 2013*

Suala la akidi kama ambavyo umelieleza hapo juu, limeelezwa vizuri kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo inatamka kwenye Ibara ya 94 kwamba (1) Kiwango cha kila kikao cha Bunge ni nusu ya Wabunge wote. (2) Isipokuwa kama imeelezwa vinginevyo katika Katiba hii, kila swali litakalotolewa kwa ajili ya kupata uamuzi wa Bunge litaamuliwa kwa kufuata wingi wa kura za Wabunge waliohudhuria kwa kupiga kura. (3) Spika, Naibu wa Spika, au mtu mwingine atakayeongoza kikao cha Bunge, hatakuwa na kura ya kawaida bali atakuwa na kura ya uamuzi kukitokea usawa wa kura. (4) Kanuni za Bunge zaweza kuweka masharti kwamba Mbunge yeyote atakayepiga kura juu ya jambo lolote ambalo yeye binafsi ana maslahi nalo atahesabiwa kuwa hakupiga kura.

Kutokana na maelezo hapo juu, unaweza kuona kwamba ili bunge liendelee na shughuli zake kihalali, ni lazima angalau nusu ya wabunge wawepo. Kwa kusoma kwetu Katiba, hii ni ibara ya lazima na kikao cha bunge hakiwezi kuendelea kama akidi iliyoelezwa kwenye katiba haijatimia.

Kuhusiana na kinga ya wabunge, ibara ya 100(1) ya Katiba inatamka kwamba kutakuwa na uhuru wa mawazo, majadiliano na utaratibu katika Bunge na uhuru huo hautavunjwa wala kuhojiwa na chombo chochote katika Jamhuri ya Muungano, au katika Mahakama au mahali penginepo nje ya Bunge. (2) Bila ya kuathiri Katiba hii au masharti ya sheria nyingine yoyote inayohusika, Mbunge yeyote hatashtakiwa au kufunguliwa shauri la madai Mahakamani kutokana na jambo lolote alilolisema au kulifanya ndani ya Bunge au alilolileta Bungeni kwa njia ya maombi, muswada, hoja au vinginevyo.

Ingawa kuna uhuru mkubwa na kinga kwa mienendo ya wabunge wanapokuwa bungeni kama ilivyoelezwa hapo juu, kama ukitokea ugomvi bungeni, ngumi kupigwa haswa, hilo ni kosa la jinai na kinga hailindi mapigano ya aina hayo.

## Utekelezaji wa tuzo ya mahakama

**Nilishindwa kesi Mahakama Kuu na nimetoa taarifa ya kukata rufaa Mahakama ya Rufaa. Mwanasheria wangu ananiambia nisiwe na wasiwasi kwa kuwa mdai hawezi kutekeleza tuzo dhidi yangu kwa kuwa faili liko Mahakama ya Rufaa na siyo Mahakama Kuu. Ni kweli? Kiasi ni kikubwa sana na hii inanifanya kuwa na wasiwasi sana. Nifanye nini?**

*29 Aprili 2013*

Kwa kutoa tu taarifa ya kukata rufaa haimaanishi kwamba umezuia utekelezaji wa tuzo. Kanuni ya 11 ya Kanuni za Mahakama ya Rufaa, 2009, inatamka wazi kwamba (1) Hakuna adhabu ya kifo au viboko itatekelezwa mpaka muda wa kutoa taarifa ya rufaa umekwisha au kama taarifa ya rufaa imetolewa mpaka rufaa imeamuliwa. (2) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo (1), kukata rufaa, hakuwezi kusimamisha adhabu yoyote, au kusimamisha utekelezaji, isipokuwa Mahakama inaweza - (a) kwenye kesi yoyote ya jinai, kama taarifa ya rufaa

imetolewa kwa mujibu wa kanuni ya 68, kuamuru kwamba mkata rufaa aachiliwe kwa dhamana au kwamba utekelezaji wa hati ya kuuza mali za mtuhumiwa usitishwe kusubiri maamuzi ya rufaa; na (b) katika kesi yoyote ya madai, kama taarifa ya rufaa imetolewa kwa mujibu wa kanuni ya 83, rufaa haiwezi kuzuia utekelezaji wa tuzo au amri inayokatiwa rufaa isipokuwa kama Mahakama Kuu au Baraza husika limeamua, wala tuzo haiwezi kuzuiwa kutekelezwa kwa sababu tu kwamba rufaa dhidi ya tuzo au amri hiyo imekatwa; lakini; Mahakama, inaweza kama kuna sababu nzuri zimetolewa, kuamuru kusimamishwa utekelezaji wa hukumu au amri hiyo. (c) kama maombi ya kuzuiwa utekelezaji yametolewa dhidi ya tuzo au amri inayokatiwa rufaa, kabla ya kuisha muda uliotolewa kwa ajili ya kukata rufaa, Mahakama, inaweza baada ya kuoneshwa sababu nzuri, kuamuru kusimamisha utekelezaji. (d) Hakuna amri ya kuzuia utekelezaji itatolewa chini ya kanuni hii isipokuwa kama Mahakama imeridhika; (i) mleta maombi atapata hasara kubwa kama amri hiyo haitatolewa; (ii) maombi yameletwa bila kucheleweshwa bila kuwa na sababu ya msingi; na (iii) mleta maombi ametoa dhamana ya kutosheleza kulipa tuzo endapo atashindwa katika rufaa yake. Kutokana na maelezo hapo juu, unaweza kuona kwamba shauri kuwa Mahakama ya Rufaa, au wewe kukata rufaa siyo kigezo cha kuzuia utekelezaji tuzo. Siyo vibaya kufikiria kuomba kusimamisha utekelezaji kwa kuzingatia masharti yaliyoelezwa hapo juu.

## Wakili hafanyi kazi yake inavyotakiwa

**Nimekuwa kwenye kesi kwa miaka 12 sasa. Hivi karibuni, nimegundua kwamba wakili wangu alifanya makosa makubwa sana ya kiufundi na ninaamini aliyafanya makosa hayo kwa makusudi ili kuniharibia kesi yangu. Nilitoa taarifa juu ya hili kwenye Kamati ya Mawakili lakini jambo hili halijashughulikiwa kama ilivyotakiwa. Njia zipi nyingine mbadala ninazo? Kwa hakika sheria ya Tanzania inatakiwa kulinda maslahi ya wateja na kuwawajibisha mawakili. Nikiuliza tofauti, je wakili yeyote aliyepo kwenye daftari la mawakili anaweza kufanya kazi za uwakili?. Tafadhali niongoze.**

*12 Agosti 2013*

Mbali na kuripoti jambo hilo kwa Kamati ya Maadili ya Mawakili iliyoanzishwa chini ya Sheria ya Mawakili, Majaji pamoja na Mahakama Kuu wana mamlaka ya kuwaadhibu mawakili. Sheria inatamka kwamba; (1) hakuna kilichopo ndani ya Sheria hii ambacho kitaondoa, au kuingilia mamlaka aliyopewa Jaji Mkuu au Jaji yoyote wa Mahakama Kuu kushughulika na utovu wa nidhamu au makosa ya mawakili. (2) Bila kuathiri masharti ya jumla ya kwenye kifungu kidogo kilichotangulia, na bila kujali kwamba hakuna mahojiano yaliyofanywa na Kamati (a) Jaji Mkuu au Mahakama Kuu watakuwa na mamlaka, kwa sababu zozote za msingi, kumuonya wakili yeyote au kumsimamisha kufanya kazi kwa kipindi chochote maalum, au kutoa amri ya kuondoa jina lake kwenye Daftari la Mawakili; (b) Jaji yeyote wa Mahakama Kuu atakuwa na mamlaka ya kumsimamisha wakili kwa namna hiyo hiyo kwa muda mfupi, huku akisubiria kupelekwa, au kuzuiwa kusimamishwa huko, na Mahakama Kuu; (c) Wakili yeyote ambaye hajaridhika na maamuzi au amri ya Jaji Mkuu au Jaji wa Mahakama Kuu yaliyotolewa kwa mujibu wa aya (a), anaweza, ndani ya siku 30 toka siku ya maamuzi hayo au amri hiyo, kukata rufaa (i) kwa maamuzi au amri ya Jaji wa Mahakama Kuu, kwa Kamati ya Nidhamu ya Mawakili; na (ii) kwa maamuzi au amri ya Jaji Mkuu, Mahakama ya Rufaa: Isipokuwa

kwamba kama maamuzi au amri inayokatiwa rufaa ilitolewa na Jaji wa Mahakama Kuu aliyeteuliwa na Jaji Mkuu kuwa mwanachama wa Kamati ya Nidhamu ya Mawakili chini ya kifungu cha 4(1) (a) cha Sheria hii, Jaji huyo hatakaa kusikiliza rufaa hiyo na Kamati, na kwa hali hiyo, Jaji Mkuu anaweza kumteua Jaji mwingine wa Mahakama Kuu kama ilivyoelezwa chini ya kifungu kidogo (3) cha Kifungu cha 4 cha Sheria hii; na isipokuwa pia kwamba kama ni rufaa kwenda Mahakama ya Rufaa dhidi ya maamuzi au amri ya Jaji Mkuu, Jaji Mkuu hatakaa kusikiliza rufaa hiyo.

Kutokana na maelezo hapo juu, kama unaamini kwamba suala lako halikutatuliwa vyema na Kamati ya Nidhamu ya Mawakili, njia ya mwisho ni kumuandikia Jaji Mkuu ambaye ndiye mwenye mamlaka ya kuwaadabisha mawakili.

Kujibu swali lako la pili, tunakupeleka kwenye kifungu cha 35 cha Sheria ya Mawakili ambacho kinaeleza wazi kwamba (1) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 3 mtu hatakuwa na sifa za kufanya kama wakili isipokuwa (a) jina lake lipo kwenye Daftari la Mawakili; (b) ana cheti halali cha kufanya kazi ya uwakili; (c) ana leseni ya biashara, na mtu ambaye hana sifa kwenye sehemu hii ataJulaikana kama “mtu asiye na sifa”

Hivyo, kuwa tu kwenye daftari la mawakili hakukupi haki ya kufanya kazi za uwakili. Kila wakili ni lazima awe na cheti cha uwakili na leseni halali ya biashara na bila hivyo, mtu hawezi kufanya kazi za uwakili.

## Kuondolewa kesi baada ya kupatana

**Nilimshtaki kaka yangu Mahakamani kutokana na mgogoro wa umiliki wa ardhi. Kutokana na kushirikisha wazee wetu, tumepatana na tumekubaliana kupangilia tena mipaka yetu. Nimeshauriwa kuondoa kesi Mahakamani ili kila kitu kifanyike kama tulivyokubaliana. Je, kuna taratibu za kufanya hivyo? Je, nitaweza tena kufungua kesi kama kaka yangu hataheshimu tulichokubaliana? Tafadhali niongoze.**

*19 Agosti 2013*

Kisheria, kama mtu alivyo na uhuru wa kufungua kesi, vivyo hivyo anao uhuru wa kuiondoa kesi hiyo Mahakamani kama hataki kuendelea nayo. Hili ni suala la upande mmoja zaidi, kwa sababu linamhusu mdai pekee hata kama pande zote mbili zimefikia makubaliano ya kutatua mgogoro.

Katika hali ya kawaida, kama mtu anaona kwamba hapo baadaye anaweza kuhitaji kuendeleza suala hilo hilo Mahakamani, hapo ombi la kuondoa kesi na uhuru wa kuirudisha linatakiwa lifanyike. Kwenye suala lako, wewe pia upo huru kuitoa kesi kama umeafikiana na kaka yako. Hata hivyo, sheria inawapa hiari ya kusajili maafikiano hayo Mahakamani ili yawe tuzo ya Mahakama. Usajili wa makubaliano yenu utasaidia kuondoa sintofahamu za kuheshimu makubaliano kati yako na kaka yako. Tunaona uchaguzi huu wa pili ni mzuri zaidi kwa mazingira yako, lakini wanasheria wako wanaweza kukuongoza zaidi.

## Ushahidi wa ziada Mahakama ya Rufaa

**Wakili wangu aliacha ushahidi muhimu na sasa anasema hatuwezi kuutoa ushahidi huo katika Mahakama ya Rufaa pamoja na umuhimu wake katika kushinda kesi yangu. Je, hii ni kweli? Sheria inasema nini?**

*19 Agosti 2013*

Kimsingi Mahakama ya Rufaa husikiliza suala la kisheria pekee na si maelezo/ushahidi mpya. Hata hivyo, Kanuni za Mahakama ya Rufaa za mwaka 2009 zinatamka wazi kwenye kanuni ya 36(1) kwamba kwenye rufaa yoyote inayotoka Mahakama Kuu au Baraza ambapo Mahakama Kuu au Baraza hilo lilisikiliza kesi hiyo kwa mara ya kwanza (original jurisdiction), Mahakama ya Rufaa inaweza (a) kutathmini ushahidi na maelezo; na (b)

kwa hiari yake, na kwa sababu za msingi, kuchukua ushahidi wa ziada au kuelekeza kwamba ushahidi wa ziada uchukuliwe na Mahakama iliyosikiliza shauri kwa mara ya kwanza au wakala (Kamishna). (2) Kama Mahakama inachukua ushahidi wa ziada, inaweza kuuchukua kwa kumhoji shahidi au kwa kiapo na Mahakama inaweza kuruhusu mtu aliyetoa ushahidi wa kiapo kudodoswa na upande kinzani. (3) Kama ushahidi wa ziada utachukuliwa na Mahakama iliyosikiliza shauri, itathibitisha ushahidi huo kwa Mahakama na kutoa maelezo kuhusu maoni yake juu ya uaminifu wa shahidi au mashahidi na kama ushahidi utachukuliwa na wakala (Kamishna), atathibitisha ushahidi huo kwa Mahakama bila kutoa maoni yake juu ya uaminifu wa shahidi au mashahidi.

Kutokana na maelezo hapo juu, unaweza kuona kwamba ushahidi wa ziada unaweza kuruhusiwa Mahakama ya Rufaa. Tunakushauri uwasiliane na mwanasheria wako tena kwa mwongozo zaidi.

## Mahakama inapoteza karatasi

**Nini tofauti kati ya kuondoa na kufuta rufaa? Kwenye rufaa mbele ya Mahakama ya Rufaa ya Tanzania, rufaa yetu iliondolewa kwa sababu nakala ya tuzo ya Mahakama Kuu haikuambatanishwa kwenye rekodi ya rufaa. Majaji wa Mahakama ya Rufaa si wangemuambia tu Msajili wa Mahakama Kuu ambaye yuko umbali chini ya mita 500 kutoka Mahakama ya Rufaa kuiwasilisha ili rufaa iendelee tofauti na kuiondoa na kufunguliwa upya? Je, huo siyo upotevu wa karatasi kwa kuiondoa rufaa, wakati Majaji wa Mahakama ya Rufaa wakijua kwamba rufaa hiyo itarudishwa tu siku ya pili? Je, upotevu huo wa karatasi siyo ukiukwaji wa sheria za mazingira za nchi? Ni wazi kuwa kwa mbinu hizi za medani, Mahakama ya Rufaa inaongeza idadi ya miti ambayo inakatwa nchini Tanzania na hivyo kuongeza upotevu wa misitu ya nchi yetu maridhawa. Tafadhali nishauri.**

*9 Septemba 2013*

Kwa ufafanuzi, kuondoa rufaa kunamaanisha kwamba hakuna rufaa sahihi ambayo inaweza kusikilizwa/kumalizwa na kwa sababu hiyo inaweza kufunguliwa tena. Kwa upande mwingine, amri ya kufuta rufaa inamaanisha kwamba, rufaa sahihi imekwisha na ambapo mara nyingi haiwezi kurudishwa tena. Haki ya kukata rufaa inatokana na sheria na upande unaotaka kuipata haki hiyo ni lazima utekeleze kwa ukamilifu masharti yaliyowekwa na sheria.

Mahakama ya Rufaa inaongozwa na Kanuni zake za mwaka 2009. Kanuni hizi, kwa lazima, zinataka miongoni mwa mambo mengine, kuambatanisha nakala ya Tuzo ya Mahakana Kuu kwenye rekodi ya rufaa. Imeamuliwa mara nyingi na Mahakama ya Rufaa kwamba, kushindwa kupata na kupeleka Mahakamani nakala ya tuzo ya Mahakama Kuu siyo tu kwamba ni mbinu za kisheria au za kitaratibu, bali inagusa mamlaka na umuhimu wa rufaa na hivyo kufanya rufaa hiyo kukosa sifa.

Nchi nyingi duniani zimepunguza idadi ya matatizo ya kikanuni ili masuala ya msingi kwenye rufaa yasikilizwe. Nchini Tanzania na mawakili wengi wanaamini kwamba, masuala ya kikanuni, wakati mwingine, yanaweza kuwa kikwazo katika utekelezaji wa haki na maamuzi mengi ya kikanuni yamekuwa yakitolewa na Mahakama ya Rufaa kuliko inavyofanyika kwenye kesi za msingi. Kubanwa sana na kanuni, kumepelekea idadi kubwa ya mapingamizi ya awali ambayo yanaibuliwa Mahakama ya Rufaa na hivyo kuongeza kuchelewesha utoaji haki ya msingi.

Kama ulivyosema kwa usahihi, kama rufaa ikiondolewa, una hiari ya kuirudisha lakini kwa kuzingatia sheria ya ukomo. Kutokana na maelezo ya hapo juu, umbali kutoka

Mahakama ya Rufaa na Mahakama Kuu au madai ya upotevu wa karatasi haviwezi kusaidia kwenye sheria za sasa na kwa namna yoyote hayawezi kubadilisha matakwa ya kisheria au kikanuni.

Hata hivyo, ni lazima tuongezee kwamba, kiuhalisia, hoja zako zinavutia sana na zinaweza kusaidia kuongeza kasi ya utoaji haki. Aidha, Mahakama, zikizingatia hoja za msingi/jadidi zaidi katika maamuzi badala ya kufuta kesi kwa makosa ya kiufundi, zinaweza kusaidia kupunguza gharama kwa pande zote na Mahakama ya Rufaa yenyewe wakati inasikiliza rufaa. Wanasheria wako wanaweza kukuongoza zaidi.

## Mdaiwa amefariki kabla ya hukumu kusomwa

**Miaka michache iliyopita mjomba wangu alifungua kesi ya madai Mahakama ya Wilaya dhidi ya mtu fulani. Pande zote mbili zilikwisha sikilizwa na mjomba wangu anasubiri hukumu. Hata hivyo, hivi karibuni tumesikia kwamba huyo mtu (Mdaiwa) amefariki na tuna hofu juu ya taarifa hii. Mjomba wangu anatamani kujua mwisho wa kesi yake kama atashinda. Tunaweza kumshtaki mke wake badala yake? Tafadhali shauri.**

*9 Septemba 2013*

Kwa kuwa kesi ilishasikilizwa, sheria ipo wazi kwamba, bila kujali kama haki ya kushtaki bado ipo ama la, hakutakuwa na kukoma kwa kesi kwa sababu ya kifo cha upande wowote katikati kabla ya kumaliza kusikilizwa na usomwaji hukumu. Hukumu itasomwa bila kujali kifo na itakuwa na nguvu na matokeo kama ambavyo ingesomwa kabla ya kifo kutokea. Hivyo, kama mjomba wako akishinda kesi, tunakushauri uwasiliane na wanasheria wako kwa hatua zaidi za kisheria ikiwemo pamoja na mambo mengine, utekelezaji wa tuzo inayotarajiwa. Kuhusu kumshtaki mke, kama hamkufanya hivyo kwenye hatua za mwanzo kwa sababu hamkuwa na kesi dhidi yake, hauna uwezekano wa kufanya hivyo hivi sasa.

## Kifo cha mdaiwa pekee kwenye kesi ya madai

**Nilifungua kesi dhidi ya mdaiwa pekee kwa kuvunja mkataba. Kabla ya kuanza kusikilizwa, mdaiwa alifariki. Hali ya kesi yangu ikoje? Nani atakuwa mbadala wa mshtakiwa na hatua gani nizifuate?**

*28 Oktoba 2013*

Iwapo mdaiwa amefariki, sheria inamruhusu mdai kuomba kumwingiza msimamizi wa mirathi ya marehemu kwenye kesi ndani ya siku 90 tangu siku ya kifo. Kama ndani ya muda uliowekwa kisheria hakuna maombi yaliyofanywa, kesi itakoma dhidi ya mshtakiwa aliyefariki isipokuwa kama mdai ataomba na kukubaliwa kuongezwa muda wa kufanya hivyo. Wanasheria wako watakuongoza juu ya nyaraka muhimu kwa lengo la kufanya maombi ya kumwingiza msimamizi wa mirathi au kuongezwa muda.

## Mdai anakataa kulipwa deni nje ya mahakama

**Mimi ni muuzaji wa bidhaa mbali mbali za kuagiza nje, biashara hii inanifanya nisafiri nje ya nchi kila wakati. Baada ya kuwasili nchini Tanzania miezi michache iliyopita nilikuta nyaraka kutoka Mahakamani zikinitaka kupeleka utetezi wangu ndani ya siku 21 kwenye kesi iliyofunguliwa na mmoja wa wateja wangu. Sina tatizo la kumlipa mteja madai yake yote tatizo ni kwamba sijui malalamiko yake kwa sababu alikuwa anawasiliana na mawakala wangu. Nilimuonea huruma lakini baada ya kumuita kwa ajili ya malipo anasisitiza kwamba tunatakiwa kuonana Mahakamani kwa sababu hawezi kupokea malipo labda**

**Mahakama ikiruhusu. Tafadhali nishauri namna ya kulitatua tatizo hili.**

*25 Novemba 2013*

Chini ya Sheria za Taratibu katika Kesi za Madai, wakati wowote kesi inapofunguliwa dhidi yako kama huna pingamizi dhidi ya madai, kama mshtakiwa, unaruhusiwa kukubali madai yote au sehemu ya madai. Kwa kuwa hupingi kesi iliyofunguliwa dhidi yako hivyo uko tayari kulipa, unaweza kutoa notisi ya kukiri madai kwa mteja wako na uipeleke Mahakamani na uiombe Mahakama itoe hukumu ya kukiri. Mahakama inaweza, baada ya maombi hayo, kutoa amri au kutoa hukumu kama itakavyoona inafaa.

Hata hivyo kama upo tayari kupatana, unaweza kumtaarifu mteja wako kuhusu jambo hili na anaweza kuiondoa kesi yake baada ya kumlipa. Inaonekana kama mteja wako anafikiri kwamba mara akishafungua kesi hawezi kuitoa. Hiyo siyo kweli. Kwa mrundikano wa kesi tulionao, Mahakama iko tayari kuharakisha utatuzi wa kesi kama hizo.

## Mahakama moja inasema kaskazini, nyingine kusini

**Kulikuwa na kesi mbili zenye pande tofauti tofauti zikiendelea kwenye Mahakama mbili tofauti. Mambo yalikuwa yanafanana sana. Mahakama moja ikaamua tofauti kabisa na nyingine. Inawezekanaje Mahakama zikafanya makosa makubwa kama hayo? Nimetoa taarifa kwa Jaji Mkuu. Tafadhali niongoze zaidi.**

*23 Desemba 2013*

Tunakupa pole kwa kuvunjika moyo lakini ni kawaida kwa mambo kama haya kutokea kwenye mifumo mingi ya Mahakama duniani, Tanzania ikiwa ni mojawapo. Na hii ndiyo sababu kunakuwa na Mahakama ya Rufaa moja kwenye nchi na pande zote zinaweza kukata rufaa kwenda Mahakama hiyo ambapo mwishoni hukumu moja itatolewa.

Kuna kanuni ya kusimama kwa maamuzi ya nyuma ambapo majaji wanatakiwa kujifunga/kuzingatia na maamuzi ya zamani. Kwa ujumla, Mahakama za juu hazina usimamizi wa moja kwa moja wa rekodi za Mahakama za chini, ikiwa na maana kwamba hazianzi tu zenyewe wakati wowote kubadili maamuzi ya Mahakama za chini. Kwa kawaida mzigo huo umeachwa kwa wenye kesi kukata rufaa dhidi ya maamuzi (yakiwemo yale yanayokiuka maamuzi ya awali) kwenda Mahakama za juu. Kama jaji akienda kinyume na maamuzi ya awali yanayombana na kesi haikukatiwa rufaa, maamuzi yanaweza kusimama.

Mahakama ya chini haiwezi kuamua tofauti na maamuzi ya awali yanayoifunga, hata kama itaona kwamba siyo ya haki; inaweza tu kuelezea tumaini lake kwamba pengine Mahakama ya juu au bunge litarekebisha sheria husika. Kama Mahakama itaamini kwamba maendeleo au mabadiliko ya wakati huo kwenye hoja za kisheria yanafanya maamuzi ya awali yanayoibana kutokuwa na msaada, na inatamani kuyaepuka na kusaidia sheria kubadilika, inaweza kuamua kwamba maamuzi yanayoifunga ama hayaendani na maamuzi ya sasa, ama itayatofautisha kwa kuonesha tofauti za msingi baina ya kesi hizo. Kama hukumu hiyo ikifika kwenye rufaa, Mahakama ya Rufaa itakuwa na fursa ya kupitia maamuzi ya awali na kesi iliyopo kwenye rufaa, kuipindua kesi ya awali na kutoa maamuzi mapya ya Mahakama ya juu.

Kutoa kwako taarifa kwa Jaji Mkuu juu ya jambo hilo kunaweza kusikusaidie kwa sababu hatua uliyoichukua ni ya kiutawala. Kesi hiyo inatakiwa ikatiwe rufaa. Wanasheria wako wanaweza kukuongoza zaidi.

## Kesi ya mwaka 1996 bado ipo Mahakamani

**Kesi yangu ni ya mwaka 1996 na bado ipo**

**Mahakamani. Ni miaka 18 tangu niifungue. Huu ni ucheleweshaji mkubwa. Nifanye nini?**

*30 Desemba 2013*

Ni kweli kwamba kuna mrundikano mkubwa wa kesi kwenye Mahakama za Tanzania. Kesi zinacheleweshwa kwa sababu za kukosekana kwa mashahidi, upande wa mlalamikaji na mlalamikiwa na kukosa umakini kwa wadaawa, ikiwemo kutokuhudhuria Mahakamani kwa mawakili wanaoziwakilisha pande zote mbili. Ni bahati mbaya sana umekuwa Mahakamani kwa kipindi kirefu hivyo.

Tunakushauri umuandikie Jaji Kiongozi na umueleze kuhusu jambo hili. Kama unavyojua, tumearifiwa kwamba Jaji Mkuu ameelekeza kwamba Majaji wabaki kazini wakati wa msimu wa likizo ili kumaliza kesi za muda mrefu zilizopo mbele yao. Utagundua mawakili wengi wakilalamikia kuhusu kulazimishwa kuendelea na kesi msimu wa likizo ya Mahakama ambayo kwa kawaida inaanza Disemba 15 na inaisha Februari 1 mwaka unaofuata.

## Kukubaliana kuhusu gharama za kesi

**Nimeshinda kesi ya madai dhidi ya kampuni kubwa na baada ya hukumu tulikubaliana kwamba kampuni itanilipa gharama za kesi kiasi cha Shilingi Milioni 70 na tuliandikishana hivyo. Nilipokwenda Mahakamani kwa ajili ya kusajili makubalino yetu, karani alikataa kupokea na aliniambia kwamba wahusika katika kesi hawawezi kukubaliana juu ya gharama bali ni Mahakama ndiyo inayotakiwa kuthibitisha na kutoa maamuzi ya gharama halisi ambazo upande ulioshinda kesi ulitumia. Je hiyo ni kweli kisheria? Tafadhali nishauri.**

*3 Februari 2014*

Tunapingana na ushauri wa karani. Kanuni za Malipo ya Mawakili na Uamuzi wa Gharama za Kesi zinaruhusu hilo. Badala ya kufungua maombi ya kuomba Mahakama ithibitishe gharama za kesi (bill of cost), Kanuni zinaruhusu wadaawa kufungua na kusajili makubaliano baina ya pande husika yakionesha gharama za kulipwa kwa upande ulioshinda. Baada ya hapo pande zote zitamuomba Afisa Mtoza Gharama/Kodi wa Mahakama, kwa barua, kusajili makubaliano hayo na yatakuwa na nguvu za kisheria sawa na hati ya utozaji kodi ya Afisa Mtoza Gharama wa Mahakama. Hata hivyo, iwapo Afisa Mtoza Gharama wa Mahakama ataona kwamba gharama hizo ni kubwa sana, anaweza kuelekeza kwamba gharama hizo zitozwe kwa kuzingatia Kanuni zilizotajwa hapo juu. Hivyo, tunakushauri uwasiliane na wanasheria wako au Msajili wa Mahakama Kuu au Hakimu Mfawidhi husika kwa mwongozo zaidi.

## Adhabu ya kifo

**Iwapo adhabu ya kifo imetolewa nchini Tanzania, je mtuhumiwa ana haki ya kukata rufaa? Kama rufaa bado inaendelea kusikilizwa, na hakuna zuio la utekelezaji, je mtu huyo anaweza kunyongwa? Zipi ni kanuni za kuzuia utekelezaji kwenye rufaa za madai na ni wakati gani taarifa ya rufaa inatakiwa kufunguliwa?**

*3 Machi 2014*

Ni kweli kuwa mtu anaweza kukata rufaa dhidi ya adhabu ya kifo/kunyongwa hadi kufa. Kanuni ya 11(1) ya Kanuni za Mahakama ya Rufaa inatamka kwa uwazi kwamba hakuna adhabu ya kifo au viboko itatekelezwa mpaka muda wa kutoa taarifa ya rufaa umekwisha au kama taarifa ya rufaa imetolewa mpaka rufaa imeamuliwa. Hivyo, kwenye rufaa za jinai, mara mtu anapotoa taarifa/notisi ya rufaa, adhabu ya kifo wala viboko haitatekelezwa mpaka rufaa hiyo iwe imeamuliwa.

Kwenye rufaa za madai, zuio la utekelezaji ni lazima liombwe na likubaliwe. Hakuna zuio la moja kwa moja. Kanuni ya 11(2)(d) inatoa misingi ifuatayo ili amri ya zuio la utekelezaji liweze kutolewa; Hakuna amri ya kuzuia utekelezaji itatolewa chini ya kanuni hii isipokuwa kama Mahakama imeridhika; (i) mleta maombi atapata hasara kubwa kama amri hiyo haitatolewa; (ii) maombi yameletwa bila kucheleweshwa kusiko kuwa na msingi; na (iii) dhamana imetolewa na mwombaji kwa ajili ya utekelezaji wa tuzo au amri hiyo iwapo atashindwa kesi katika rufaa.

Taarifa ya rufaa ni lazima itolewe ndani ya siku thelathini tangu siku ya maamuzi yanayokatiwa rufaa. Wanasheria wako wanaweza kukuongoza zaidi.

## Rufaa kwenye mahakama kuu kitengo cha biashara

**Mimi na marafiki zangu wawili tunamiliki kampuni ya huduma za teknolojia ya mawasiliano inayofanya shughuli zake jijini Arusha, Dar, Mwanza na Mbeya. Tunapata shida ya kulipwa fedha zetu kutoka kwa wateja wetu wengi licha ya juhudi kubwa za kuwakumbusha. Tuliomba ushauri kutoka kwa mwanasheria wetu wa kampuni ambaye alituambia kwamba kwa kiwango tunachokidai, tufungue shauri katika Mahakama ya Hakimu Mkazi. Ni jambo la kushangaza sana kuona kwamba tunapoteza kesi za wazi namna hii licha ya kutumia muda mwingi Mahakamani. Tunaamini hata mwanafunzi wa sheria angetupa ushindi kutokana na madai na ushahidi tuliotoa kuwa wazi. Hivi sasa tunataka kukata rufaa dhidi ya maamuzi haya yanayonukia rushwa. Je, tunaweza kukata rufaa Mahakama Kuu Kitengo cha Biashara ambapo tumeambiwa kwamba kesi zinaendeshwa kwa haraka. Je, kiasi kinachodaiwa bado kitakuwa ni kikwazo/tatizo? Tafadhali tushauri.**

*7 Aprili 2014*

Chini ya kanuni zinazotumika Mahakama Kuu Kitengo cha Biashara, kiwango cha madai ya awali kwenye kesi za biashara ni kuanzia Shilingi za Tanzania (TZS) milioni 100 kwa mali isiyohamishika na angalau TZS milioni 70 kwa mali inayoweza kukadiriwa katika fedha.

Vivyo hivyo, Mahakama Kuu Kitengo cha Biashara ina mamlaka ya kusikiliza rufaa dhidi ya maamuzi ya Mahakama za chini kuhusu mashauri ya kibiashara. Rufaa inaweza kuwa dhidi ya maamuzi yote au sehemu ya maamuzi na unatakiwa kutoa taarifa ya kusudio la kukata rufaa ndani ya siku 14 tangu siku maamuzi yalipotolewa.

Kama hujaridhika na maamuzi yaliyotolewa unaweza kutumia fursa hii kwenye Mahakama Kuu Kitengo cha Biashara. Kama ulivyoeleza, Mahakama ya Biashara inazingatia sana umalizikaji wa kesi kwa kasi. Hata hivyo, unahitaji kuelekezwa vizuri na mwanasheria mwenye uzoefu na Mahakama Kuu Kitengo cha Biashara kuhusu namna, muda na mbinu mahsusi kwenye kufugua rufaa yako.

## Ajali kusababishwa na uzembe

**Miaka mitano iliyopita nilipata ajali mbaya sana wakati napita kwenye jengo ambalo lilikuwa linajengwa. Ilinichukua miaka mitano kutibiwa na kurudi kwenye hali yangu ya kawaida. Nilijeruhiwa sana na ilikuwa kidogo nifariki lakini nashukuru Mola niliweza kupona. Sasa nimerudi na ninataka kuishtaki kampuni ambayo ilikuwa na tenda ya kujenga na mwingine yeyote anayestahili kushtakiwa. Licha ya fedha, ninataka kuhakikisha kwamba watu hawa wanawajibishwa. Kwa mfano, naona watu wanatumia ghorofa za chini wakati juu bado ujenzi unaendelea. Aidha, bado ninaona watu wakirandaranda kwenye eneo la ujenzi bila kuwa na kofia ngumu, na hata wale wenye nazo ni za ubora wa chini kiasi kwamba hata kindi au kirukanjia**

**anaweza kuivunja. Baada ya kuwasiliana na mwanasheria wangu, nilishtuka kusikia kwamba nilitakiwa kushtaki ndani ya miaka tatu na kwa kuwa miaka tatu imepita siwezi kumshtaki mtu yeyote. Inawezekanaje sheria kuwa na masharti magumu namna hiyo? Mnawezaje kunisaidia? Kwa nini Tanzania ina sheria ya namna hiyo?**

*7 Aprili 2014*

Ni kweli kwamba kuna Sheria ya Ukomo ambayo inaelezea muda ambao mashauri mbali mbali yanaweza kuwasilishwa Mahakamani. Suala kama lako linaangukia kwenye sheria ya madhara, na ukomo wa kushtaki ni miaka tatu.

Kifungu cha 44 kinamruhusu Waziri (wa Sheria) kukuongezea muda mwingine wa mwaka mmoja na nusu. Kinatamka kwamba, "iwapo Waziri ataona kwamba kwa kuangalia mazingira ya kesi yoyote, ni sawa na haki kufanya hivyo, anaweza, baada ya kushauriana na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwa amri iliyotolewa kwa mkono wake, kuongeza muda wa ukomo wa kesi yoyote usiozidi nusu ya muda uliowekwa kwenye sheria." Hata hivyo, kifungu hiki kinaweza kisikusaidie sana kwa sababu madai yako yana miaka mitano.

Kwa bahati nzuri kifungu cha 16 cha Sheria hii kinakuokoa ambapo kinatamka kwamba, iwapo muda wa kushtaki au muda wa kuomba utekelezaji umeanza na kabla ya muda wa ukomo uliowekwa kwa kesi au maombi hayo kwisha, mtu ambaye muda huo umeanza amepata ulemavu, katika kuhesabu ukomo wa muda unaotumika kwenye kesi au maombi hayo, wakati ambao mtu huyo alikuwa na ulemavu hautapigiwa mahesabu. Kwa bahati mbaya ulemavu haujatafsiriwa na wala wewe hujatupatia maelezo ya kutosha kuhusu majeraha uliyoyapata, tunaamini wanasheria wako wanaweza wakatumia upenyo huu ambao uko wazi kwako.

Vile vile, wanasheria wako wanatakiwa kuzingatia kifungu cha 20 cha Sheria ya Ukomo ambacho kinatamka kwamba, "katika kuhesabu ukomo wa muda uliowekwa kwa ajili ya kesi au maombi ya kutekeleza tuzo, wakati ambao mdaiwa alikuwa nje ya Jamhuri ya Muungano utaondolewa." Kwa kutumia kifungu cha 16 na 20 tunaamini suala lako linaweza kuendelea.

Sheria hizi za ukomo ni za kawaida kwenye nchi nyingine. Kwa mujibu wa Sheria za Halsbury za Uingereza, lengo na matokeo ya sheria za ukomo ni kuwalinda washtakiwa kwa sababu kuu tatu, ambazo zinaunga mkono uwepo wa sheria za ukomo, ambazo ni: (a) mdai mwenye madai halali ayaendeshe kwa umakini; (b) mdaiwa anaweza kuwa amepoteza ushahidi muhimu wa kujitetea/kukanusha tuhuma dhidi yake; na (c) madai ya muda mrefu yana ukatili zaidi ndani yake kuliko haki.

## Kushindwa kesi ya upande mmoja

**Nilifungua kesi dhidi ya mfanyabiashara ambaye niliingia naye mkataba wa kuniuzia bidhaa fulani ambazo alishindwa kuniletea. Kwa sababu hakuwepo siku ya kusikiliza kesi licha ya kuarifiwa, Jaji aliamua kusikiliza kesi hiyo bila ya yeye kuwepo. Nilikuwa shahidi pekee na wakati wa kusikiliza niliwasilisha mkataba ambao tulitiliana saini mbele ya wakili na Mahakama iliupokea kama kielelezo/kizibiti. Jaji alitunuku ushindi upande wa pili kwa maelezo kwamba sikutoa ushahidi unaothibitisha kama mkataba ulisainiwa na pande zote mbili katika mkataba. Nafikiri Jaji hakuwa sahihi. Tafadhali niongoze.**

*21 Aprili 2014*

Kabla Mahakama haijatoa hukumu na kutunuku ushindi upande wowote kwenye kesi za madai, ni suala la kisheria kwamba kesi hiyo ni lazima iwe imethibitishwa kwa mizani

ya uwezekano (balance of probabilities). Kanuni hii inatumika hata kama kesi inasikilizwa upande mmoja, kama ilivyokuwa kwako. Ni muhimu kuelewa kwamba kwenye Mahakama zetu, kinachoangaliwa ni kile kinachothibitishwa na siyo kilichopo kwenye akili yako au unachokiamini kuwa ni cha kweli.

Kwa kuwa hatujui ukweli wote kuhusu kesi yako, hatuwezi kukosoa uamuzi wa Jaji kwa kuzingatia maelezo uliyotupatia. Sheria ya Ushahidi inatamka kwa uwazi kwamba iwapo waraka umesainiwa na mtu yeyote, saini au mwandiko wa kwenye waraka huo ni lazima uthibitishwe kuwa ni wa mtu huyo. Kwenye kesi yako ni wazi kwamba uliamua kutoa ushahidi peke yako bila kumuita shahidi aliyeshuhudia mkataba akiwemo wakili uliyemtaja. Tunaamini hiki ndicho kilikuangusha.

Sababu tu kwamba kesi ilisikilizwa ukiwepo upande mmoja haiondoi wajibu wa kutimiza vigezo vilivyowekwa kisheria. Njia pekee iliyobaki ni kukata rufaa na tunashauri uwasiliane na wanasheria wako.

## Shahidi kupoteza kumbukumbu

**Nimepata wito wa kutoa ushahidi kwenye kesi ya madai. Ushahidi wangu utajikita kwenye mikataba mbalimbali, na ingawa nina uelewa nayo, siwezi kukumbuka kila mkataba. Nimeanza kukariri mikataba hiyo nikiwa najiandaa lakini naona inanichukua muda mrefu na kwa umri wangu, siwezi kukumbuka kila kitu. Hii inanisababishia msongo wa mawazo kwa kuwa mimi ni shahidi muhimu. Nifanye nini? Je, kuna njia nyepesi ya kukariri mikataba?**

*12 Mei 2014*

Wakati wote sheria inatambua uwepo wa jamii na watu wake. Sheria inapotungwa, inazingatia uhalisia, na katika mazingira ya suala lako, sheria inatambua kwamba mashahidi ni binadamu na wanaweza kusahau baadhi ya mambo.

Sheri ya Ushahidi inahusika katika mazingira haya kwa kuwa inaongoza namna ushahidi unavyotakiwa kutolewa na kitu gani kina sifa ya kuwa ushahidi Mahakamani. Katika kuweka kumbukumbu ya ushahidi na kutoa ushahidi, sheria inamruhusu shahidi anayehojiwa, kujikumbusha kwa kurejea andiko lililoandikwa na yeye mwenyewe wakati wa shughuli husika. Sheria pia inaruhusu kujikumbusha hata kwa kutumia nakala panapo ruhusa ya Mahakama.

Hivyo, huna haja ya kujifungia darasani na kuanza kukariri. Unaweza kuomba kurejea mkataba na utapewa nakala ili ujikumbushe. Hata hivyo, unahitaji kufahamu maelezo ya kesi kwa sababu kazi yako ni kuisaidia Mahakama kutoa maelezo ya kweli na muhimu ambayo yataisaidia Mahakama kutenda haki. Mwanasheria wako anaweza kukuongoza zaidi.

## Kulipa deni kwa awamu

**Nimeshtakiwa kwa kuvunja mkataba wa mkopo Mahakama Kuu Kitengo cha Biashara. Sitaki kujitetea kwa sababu sikatai deni. Hivi sasa ninasubiri tu malipo kutoka taasisi moja ya umma ambayo nategemea kuyapata baada ya kikao cha Bunge la Bajeti. Ninachoogopa ni namna Mahakama itakavyochukulia iwapo mdai atakataa ombi langu. Tafadhali niongoze.**

*19 Mei 2014*

Kanuni za Mahakama Kuu Kitengo cha Biashara za mwaka 2012 zinamruhusu mdaiwa kukiri dai na kuomba muda wa kulipa deni analodaiwa. Hili linatakiwa lifanyike na lipelekwe Mahakamani pamoja na ungamo la kukiri deni. Kanuni hizi pia zinaitaka Mahakama kutoa hukumu juu ya kiasi kinachodaiwa na kilichokubaliwa baada

ya kupelekewa ungamo la kukiri deni.

Hata hivyo, iwapo mdai atakataa ofa ya mdaiwa kuhusu muda wa malipo, ataeleza sababu za kukataa wazo la mdaiwa. Katika hali kama hiyo, Msajili wa Mahakama Kuu Kitengo cha Biashara atafanya maamuzi kwa kuzingatia maelezo ya pande zote mbili, na kutoa amri ya malipo ya awamu ambayo yatalipwa kama atakavyoona inafaa. Mtu yeyote asiyeridhika atapeleka maombi kwa jaji ambaye maamuzi yake hayatakatiwa rufaa.

Hoja nyingine ya kuzingatia ni kwamba, kama ombi la kulipa kwa awamu likiruhusiwa na ukashindwa kulipa kama mlivyokubaliana, haki ya kulipa kwa awamu itakoma na mdai atakuwa na haki ya kutekeleza tuzo kwa kiasi kilichobaki mpaka kiishe bila kutoa taarifa zaidi. Njia nyingine, unaweza kufikiria kufanya makubaliano na mdai na madai hayo yanaweza kurekodiwa na kuwa tuzo ya Mahakama.

## Mahakama imekataa gharama

**Nilitumia ofisi ya wanasheria wa Ulaya ambayo nayo iliwateua wenzao wa nchini Tanzania ili kusimamia kesi iliyofunguliwa hapa nchini. Tulitumia fedha nyingi kuendesha kesi na tulishinda kesi na tulipewa nafuu ya kulipwa gharama za kesi hiyo. Ninaamini tunastahili gharama zetu zote za kuendesha kesi, Mahakama imekataa karibu nusu ya gharama tulizoomba kufidiwa licha ya kupeleka risiti zote, hili limetushangaza sana. Je, hii ni kawaida?**

*9 Juni 2014*

Kanuni za Malipo ya Mawakili na Uamuzi wa Gharama za Kesi ndizo zinazotumika kwenye suala la utozaji gharama. Afisa Mtoza Kodi/Gharama kwenye maombi ya gharama chini ya Kanuni hizi ni Msajili wa Mahakama Kuu.

Kanuni zinatamka kwamba bila kujali kitu chochote kwenye Kanuni hizi, kwenye kila gharama, iwe kwenye masuala yasiyobishaniwa au yanayobishaniwa, Afisa Mtoza Kodi ataruhusu gharama zote ambazo ataona kuwa zilikuwa ni za lazima na sahihi katika uendeshaji kesi, lakini, isipokuwa dhidi ya mtu aliyeingia gharama hizo, hakuna gharama zitakazoruhusiwa ambazo Afisa Mtoza Kodi ataona zimetokana na kuzidisha mahesabu, uzembe au makosa, au malipo ya tozo au gharama maalum za mashahidi au watu wengine, au matumizi mengine yasiyokuwa ya kawaida.

Kanuni zinaeleza kwamba malipo yote ya gharama yatatozwa kwa viwango maalum, isipokuwa kama Jaji wa Mahakama Kuu atathibitisha kwa sababu maalum viwango vinavyotokana na aina na umuhimu, au ugumu, au uharaka wa kesi ambapo gharama zinaweza kutozwa kwa kiwango cha juu. Kwa mfano, kwenye kesi inayobishaniwa, wakili anaweza kutoza asilimia 3 ya kiasi kinachobishaniwa.

Elewa kwamba kanuni zinaeleza zaidi kwamba katika kesi yenye umuhimu mkubwa au yenye ugumu usiokuwa wa kawaida, wakili atakuwa na haki ya kulipwa na ataruhusiwa kulipwa na mteja wake, ada maalum ikiwa ni nyongeza ya malipo yaliyoelezwa kwenye Kanuni hizi. Isipokuwa, katika kukadiria ada maalum, Mahakama itazingatia; (a) aina na mazingira ambapo shughuli au sehemu yake ilifanyikia; (b) aina na kiasi cha fedha au maslahi husika; (c) aina na kiwango cha kazi na wajibu husika; (d) idadi, ugumu na umuhimu wa nyaraka za kuandaa na kuchunguzwa; au mazingira mengine yoyote husika ambayo yanaweza kujitokeza.

## Rufaa katika mahakama ya ukomo

**Nimekata rufaa Mahakama ya Rufaa dhidi ya Maamuzi ya Mahakama Kuu ya Tanzania**

**ambayo sikuridhika nayo. Mwanasheria wangu hakufika na rufaa ilifutwa. Je, sheria ni kali kiasi hicho? Pia nina hoja kuwa Mahakama haina mamlaka kisheria kuisikiliza kesi husika na ninataka kuibua suala hili je, ni wakati gani sahihi wa kuibua pingamizi langu?**

*7 Julai 2014*

Swali lako la kwanza limezungumzwa kwenye Kanuni za Mahakama ya Rufaa kanuni ya 112 ambayo inatamka kwamba: kama siku yoyote iliyopangwa kusikiliza rufaa, mleta rufaa hajafika, rufaa inaweza kufutwa na rufaa kinzani inaweza kuendelea, labda kama Mahakama itaona inafaa kuahirisha kusikiliza rufaa, ila endapo rufaa imefutwa au rufaa kinzani iliyoruhusiwa imekwishasikilizwa, mleta rufaa anaweza kuiomba Mahakama kusikiliza rufaa au kusikiliza upya rufaa kinzani. Isipokuwa kwamba, mleta rufaa ataonesha sababu za msingi zilizomzuia kuhudhuria wakati rufaa imeitwa kwa ajili ya kusikilizwa.

Kama unataka rufaa yako irudishwe, wakili wako atatakiwa kupeleka maombi ya kurudisha rufaa na aoneshe sababu za msingi za kutokuhudhuria. Vinginevyo, unaweza kumshtaki kwa uzembe wa kitaaluma.

Kuhusu pingamizi la awali ambalo unataka kuliibua, Kanuni za Mahakama ya Rufaa, Kanuni ya 107 inaeleza kwamba mdaiwa anayetaka kuweka pingamizi la awali dhidi ya rufaa kusikilizwa atampatia mleta rufaa taarifa ya siku tatu kabla ya siku ya kusikiliza, akielezea sababu za pingamizi lake kama vile sheria maalum, kanuni na maamuzi anayotaka kuyasimamia, na wakati huo huo atapeleka nakala tano za taarifa hiyo kwa Msajili wa Mahakama ya Rufaa na nakala za sheria au maamuzi, kama itakavyokuwa, ataziambatanisha kwenye taarifa. Iwapo mdaiwa akishindwa kutekeleza masharti ya Kanuni hii, Mahakama inaweza kukataa kusikiliza pingamizi au inaweza kuahirisha kusikiliza kwa masharti na amri ya malipo ya gharama kama itakavyoona inafaa.

## Makosa ya uchapishaji kwenye sheria

**Kuna sheria fulani ya Bunge ina makosa makubwa ya uchapishaji. Je, inahitaji kurudishwa bungeni ili ikatungwe upya au ikarekebishwe? Mchakato wake ni upi?**

*7 Julai 2014*

Kwanza hatujui una uhakika gani kwamba sheria ina makosa ya kiuchapishaji. Hata hivyo, tuchukulie upo sahihi, Sheria ya Utafsiri wa Sheria ina kifungu maalum kwa ajili ya jambo hilo na inaeleza kwenye kifungu cha 26 (3) kwamba ikiwa kutakuwa na kosa lolote la maandishi au uchapishaji wa Muswada wa Sheria au Sheria yenyewe kwenye Gazeti la Serikali, Mwandishi Mkuu wa Sheria au afisa yeyote wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali aliyepewa madaraka kwa maandishi kwa niaba hiyo na Mwandishi Mkuu wa Sheria anaweza kwa amri iliyochapishwa katika Gazeti la Serikali kutoa maelekezo ya kusahihisha makosa hayo na kila agizo litasomeka pamoja na Muswada au Sheria inayohusiana nayo na Muswada huo au Sheria, kuanzia tarehe ya kuchapishwa itaanza kutumika kama ilivyosahihishwa.

Tunashauri uwaandikie Mwandishi Mkuu wa Serikali au Mwanasheria Mkuu ili waweze kuliangalia. Kwa ufupi, kama ni makosa ya uchapaji, sheria haihitajiki kurudishwa bungeni.

## Kuzuia utekelezaji wa tuzo Mahakama Kuu

**Nimekata rufaa kwenda Mahakama ya Rufaa baada ya kushindwa Mahakama Kuu. Wakati huo huo nimefungua maombi ya kuzuia utekelezaji wa tuzo Mahakama Kuu wakati tukisubiri maamuzi ya rufaa. Mwanasheria wangu aliniambia kwamba**

**itakuwa ni rahisi kupata amri ya kuzuia utekelezaji wa tuzo Mahakama Kuu. Upande wa pili umeweka pingamizi la awali ukidai kwamba Mahakama Kuu haina mamlaka ya kusikiliza maombi ya kuzuia utekelezaji wa tuzo. Tafadhali niongoze.**

*4 Agosti 2014*

Kwa kuzingatia maamuzi ya hivi karibuni ya Mahakama ya Rufaa, tunaona kwamba pingamizi la awali litakubaliwa na maombi yako ya kuzuia utekelezaji Mahakama Kuu yatatupiliwa mbali.

Kanuni ya 11(2)(b) ya Kanuni za Mahakama ya Rufaa inatamka kwamba: (b) katika kesi yoyote ya madai, kama taarifa ya rufaa imetolewa kwa mujibu wa kanuni ya 83, rufaa haiwezi kuzuia utekelezaji wa tuzo au amri inayokatiwa rufaa isipokuwa kama Mahakama Kuu au Baraza limeamua, wala tuzo haiwezi kuzuiwa kutekelezwa kwa sababu tu kwamba rufaa dhidi ya tuzo au amri hiyo imekatwa; lakini; Mahakama, inaweza kama kuna sababu nzuri zimetolewa, kuamuru kusimamishwa utekelezaji wa hukumu au amri hiyo. (c) kama maombi ya kuzuiwa utekelezaji yametolewa dhidi ya tuzo au amri inayokatiwa rufaa, kabla ya kuisha muda uliotolewa kwa ajili ya kukata rufaa, Mahakama inaweza baada ya kuoneshwa sababu nzuri, kuamuru kusimamisha utekelezaji. (d) Hakuna amri ya kuzuia utekelezaji itatolewa chini ya kanuni hii isipokuwa kama Mahakama imeridhika; (i) mleta maombi atapata hasara kubwa kama amri hiyo haitatolewa; (ii) maombi yameletwa bila kucheleweshwa kusiko kuwa na msingi; na (iii) dhamana imetolewa na mwombaji kwa ajili ya utekelezaji wa tuzo au amri hiyo endapo atashindwa katika rufaa. (e) bila kujali chochote kilichopo kwenye kanuni ndogo ya (d), Mahakama, inaweza kutoa amri ya upande mmoja ya kuzuia utekelezaji mpaka kusikilizwa kwa rufaa au maombi.

Kwa maelezo hapo juu, pamoja na hukumu mbalimbali za Mahakama ya Rufaa, tunaona kwamba ni kweli Mahakama Kuu haina mamlaka ya kusikiliza zuio lako kwa kuwa tayari umeshafungua rufaa yako. Huwezi kujichagulia Mahakama na ungepaswa kuomba zuio la utekelezaji Mahakama ya Rufaa kwa mujibu wa Kanuni za Mahakama ya Rufaa. Vile vile umeshachelewa kupeleka maombi ya kuomba zuio la utekelezaji Mahakama ya Rufaa na utatakiwa kupeleka maombi ya kuongezwa muda wa kupeleka zuio, na maombi ya namna hiyo hukubaliwa kwa nadra sana, na yanatakiwa kuambatana na hoja za msingi ili yaweze kufanikiwa. Tunashauri wanasheria wako wajaribu kuangalia upya maombi yako yaliyopo Mahakama Kuu.

## Ada ya wakili ni kubwa

**Nilijadiliana na mwanasheria wangu kuhusu ada yake kwa ajili ya kusimamia suala fulani na hivi sasa limekwisha na ninaona ada ya wakili ni kubwa sana. Nimeamua nisimlipe na hivyo kuomba ushauri wako wa namna ninaweza kufanikisha jambo hili. Tafadhali niongoze.**

*4 Agosti 2014*

Ingawa tunakupongeza kwa kuwa wazi na kutuambia sababu hasa ya kukataa kumlipa wakili wako, tunaamini kwamba pamoja na nia yako kutokuwa ya haki, umefungwa katika kona nne za mkataba ambao uliingia na mwanasheria wako. Huwezi tu wewe mwenyewe kujiamulia kupunguza ada. Una hatari ya kushtakiwa na mwanasheria wako kwa kutokulipa ujira wake.

Tunakushauri ujadili jambo hili na mwanasheria wako na kuona kama anaweza kukubali kupitia upya ada. Kama ikishindikana, tunashauri umlipe mwanasheria wako kama mlivyokubaliana. Vinginevyo, mtafute mwanasheria mwingine ili akuongoze juu ya suala hili.

## Jaji kunena maneno ya kibaguzi

**Nikiwa kama mwanasheria wa kigeni nilishangaa kumsikia jaji aliyekuwa anasikiliza kesi niliyokuwa na maslahi nayo akitamka maneno ya kibaguzi na yenye upendeleo. Alilifanya hili mbele ya maafisa wengine kama 10 hivi mahakamani. Ninawezaje kumfungulia malalamiko Jaji huyu? Je, Majaji wote wana kasumba hii?**

*25 Agosti 2014*

Kifungu cha 25 cha Sheria ya Huduma za Mahakama kinaanzisha Kamati ya Maadili ya Majaji ambayo ina mamlaka ya kufanya uchunguzi/upelelezi na mahojiano dhidi ya Majaji wa Mahakama ya Rufaa, Jaji Kiongozi, Majaji, Maafisa wa Mahakama na Mahakimu.

Kazi ya Kamati ni kupokea malalamiko, kumpatia Jaji husika malalamiko husika, kupeleka malalamiko kwenye Kamati, kusikiliza malalamiko, kumuonya Jaji husika na kuchukua hatua nyingine yoyote ambayo inaweza kuona ni ya muhimu katika mazingira husika. Maneno ya kibaguzi ya Jaji yanaweza kulalamikiwa, na unashauriwa kupeleka jambo hili kwenye Kamati hii kwa hatua zaidi.

Malalamiko yoyote dhidi ya Jaji wa Mahakama ya Rufaa, Jaji Kiongozi na Jaji yanaweza kupelekwa kwenye Tume au Kamati na Jaji wa Mahakama ya Rufaa, Jaji Kiongozi, Afisa wa Mahakama, Hakimu, Afisa Sheria, Wakala wa Serikali, Wakili au mtu mwenye maslahi na jambo husika au katika mazingira mengine, mtu anayeweza kutoa ushahidi wa kutosha kuhusu malalamiko husika. Malalamiko yanatakiwa kuwa na taarifa za kutosha ili kuiwezesha Kamati kuyafanyia kazi na malalamiko hayo ni lazima yasainiwe na mlalamikaji.

Hatujui kama ni mtumiaji wa mara kwa mara wa mahakama za Tanzania, Majaji wetu wanafahamika kwa ukarimu wao na hili linaweza kuwa ni tukio la bahati mbaya tu, linaloweza kuwa limechochewa na kilichokuwa kinaendelea mahakamani. Hata hivyo, unashauriwa kufuata njia zilizoainishwa hapo juu.

## Kuidhinishwa kwa Katiba mpya ya Tanzania

**Je, Katiba mpya ya Tanzania imeshaidhinishwa? Inakuwaje hatujaisoma na bado itatuhusu?**

*6 Oktoba 2014*

Tumeruka maswali mengi yaliyotangulia kutufikia ili kujibu swali hili ambalo lilikuja siku chache tu zilizopita. Tumeamua kujibu swalii hili kwa sababu tumepokea maswali mengine ya namna hii siku chache zilizopita, na tumezingatia umuhimu wa swali hili katika kipindi hiki.

Jibu ni fupi sana. Rasimu ya Katiba imeidhinishwa na Bunge. Kisha itawasilishwa kwa Rais kabla ya kuchapishwa kwa ajili ya umma kuisoma. Baada ya hapo, itapigiwa kura, na kama idadi kubwa ya watu itaiunga mkono, itakuwa Katiba rasmi na si vinginevyo. Hivyo, kuna mchakato ambao ni lazima ufuatwe ili Katiba iweze kupitishwa na utapata nafasi ya kuisoma na kupiga kura ya kuikubali au kuikataa.

## Sheria ya ukomo inaumiza

**Tulienda Mahakamani kushtaki juu ya kuvunja mkataba fulani, na kesi imekuwa Mahakamani tangu mwaka 2004. Ilichukua Mahakama/jaji miaka 10 (hadi mwaka 2014) kuamua kwamba haikuwa na mamlaka ya kuendesha kesi hii kwa sababu kiasi kilichohusika kilikuwa juu zaidi ya kile Mahakama yake ina mamlaka ya kusikiliza. Tuliifungua kesi upya kwenye Mahakama yenye mamlaka, na upande wa pili sasa umeweka pingamizi la awali kwamba tupo nje ya muda. Nina wasiwasi sana kwa kuwa inaonekana kwamba ni kweli tupo nje ya muda kuendelea na madai yetu, kwa sababu mwanasheria wangu anasema**

**kwamba kushtaki kwenye kesi inayohusu sheria ya mkataba ni lazima ufanye hivo ndani ya miaka sita tangu siku ya tukio, ambayo kwa hakika imekwishapita muda mrefu.**

*20 Oktoba 2014*

Kifungu cha 21 (1) cha Sheria ya Ukomo kinasema kwamba katika kuhesabu kipindi cha ukomo wa muda kilichowekwa kwa kesi yoyote, muda ambao mdai anaendesha mashtaka, kwa bidii ya kutosha katika kesi nyingine ya madai, iwe katika Mahakama ya kwanza au katika Mahakama ya rufaa, dhidi ya mshtakiwa, hautahesabiwa, kama kesi hiyo inatokana na sababu zile zile na iliendeshwa kwa uaminifu kwenye Mahakama ambayo, kutokana na kukosa mamlaka au sababu nyingine ya hali kama hiyo, ilikuwa haina uwezo wa kusikiliza kesi hiyo.

Unaweza kutumia kifungu hicho hapo juu ili uondoke kwenye mtego huu. Tunaamini utakuwa na mafanikio ikiwa ulikuwa unaendesha kesi yako ya kwanza kwa juhudi na umakini wa kutosha. Tafsiri ya 'umakini' inategemea na mazingira ya kesi husika.

## Hakimu hajui mabadiliko ya sheria

**Hakimu aliyesikiliza kesi alikuwa hajui mabadiliko ya kifungu cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai. Je, hili ni jambo la kubishaniwa wakati ni wazi kwamba kifungu kinachozuia dhamana kimefutwa?**

*17 Novemba 2014*

Uko sahihi. Mahakimu wote na majaji wanatakiwa kutambua uwepo wa sheria na mabadiliko yake. Kifungu cha 22 cha Utafsiri wa Sheria kinaeleza kwamba kila sheria itahesabiwa kuwa iko wazi na inafahamika kwa umma wote, isipokuwa kama kutakuwa na maelezo ya kuonyesha vinginevyo, na Mahakama zote zitatilia maanani kuwa sheria zote zinafahamika kwa umma.

Hata hivyo, ni busara kumtahadharisha hakimu kuhusu mabadiliko ya sheria na nakala ya marekebisho na namna mabadiliko hayo yalivyoakisiwa. Vile vile mwanasheria wako ana wajibu wa kuiongoza Mahakama. Hatuoni sababu kwa nini upinge kufanya hivyo. Hatuoni kama itapelekea mabishano ya aina yoyote.

## Sheria za Kiswahili dhidi ya sheria za Kiingereza

**Kuna sheria ilitungwa kwa Kiswahili lakini imetafsiriwa kwenda Kiingereza. Hata hivyo, ninaposoma toleo la Kiingereza, ninahisi baadhi ya vifungu havijatafsiriwa vizuri. Nini kinatokea kwenye mazingira kama hayo?**

*8 Desemba 2014*

Sheria ya Utafsiri wa Sheria ina kifungu maalum ambacho kinaelezea jambo hili. Kifungu cha 84 kinaeleza ifuatavyo: (1) Lugha za Sheria za Tanzania zitakuwa ni Kiswahili au Kiingereza au lugha zote mbili. (2) Pale ambapo Sheria yoyote imetafsiriwa kutoka lugha moja kwenda lugha nyingine na kuchapishwa kwa lugha zote mbili, na iwapo itatokea mgongano au kutakuwa na mashaka ya maana ya maneno au maelezo, lugha ambayo imetumika wakati wa kupitisha Sheria hiyo na Bunge, ndiyo itakayopewa kipaumbele (3) Pale ambapo Sheria imeandikwa kwa lugha zote mbili na ukatokea mgongano au mashaka kuhusiana na maana ya neno lolote au maelezo, tafsiri ya Kiingereza ndiyo itakayotumika.

Hivyo, kama mwanzoni sheria iliandikwa kwa Kiswahili halafu baadaye ikatafsiriwa kwa Kiingereza, basi toleo la Kiswahili ndilo litatumika. Hata hivyo, kama sheria iliandikwa kwa lugha zote mbili, basi toleo la Kiingereza litapewa kipaumbele. Kwa bahati mbaya hujatutajia sheria unayoirejea hivyo

tunashindwa kukuongoza zaidi.

## Nyaraka za kuthibitishia kesi

**Niliuza bidhaa kwa wakala mmoja wa Serikali na sijalipwa. Mkataba unasema kwamba migogoro yote itaamuliwa nchini Tanzania. Je, kutokulipwa fedha kabisa chini ya mkataba ni mgogoro wa kisheria kweli? Zaidi, kuna baadhi ya nyaraka zipo kwa wakala huyo ambazo ninataka kuzitumia kwenye kesi yangu. Je, ninaweza kupata nyaraka hizo?**

*15 Desemba 2014*

Tunaanza kwa kujibu swali lako la pili. Kupata nyaraka kutoka kwa mshtakiwa ni kitu cha kawaida kwenye Nchi za Magharibi kwa njia inayoitwa “ugunduzi” au “discovery” kwa lugha ya Kiingereza.

Ugunduzi ni hatua ya awali kabla ya kusilizwa kwa kesi ambapo kila upande, kupitia Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Madai, unaweza kupata ushahidi kutoka upande pinzani kwa kutumia njia za ugunduzi zikiwemo kuomba kujibiwa maswali, kupewa nyaraka, kuomba kukiri na viapo. Inaonekana kama ni kitu cha kipekee sana, lakini inawezekana kupata nyaraka za upande mwingine ambazo kimsingi zinaunga mkono kesi yako.

Kifungu cha 18(1) cha Sheria ya Mwenendo wa Mashtaka dhidi ya Serikali kinaeleza kwa uwazi kwamba kwa kuzingatia na kwa masharti ya sheria iliyotungwa (a) katika kesi yoyote ya madai iliyopo Mahakama Kuu au Mahakama za chini ambapo Serikali ni upande mmoja wapo, Mahakama inaweza kuitaka Serikali kufanya ugunduzi wa nyaraka na kutoa nyaraka kwa ajili ya ukaguzi; na (b) katika kesi nyingine yoyote kama ilivyoelezwa kwenye aya (a) ya kifungu hiki kidogo, Mahakama inaweza kuitaka Serikali kujibu maswali: Isipokuwa kama kifungu hiki hakitaathiri sheria au kanuni yoyote ambayo inazuia kutolewa kwa nyaraka yoyote au kujibu swali ambalo litaathiri maslahi ya umma.

Ni muhimu kuelewa kwamba sheria hii pia inaruhusu nyaraka kutokutolewa iwapo, kwa maoni ya Waziri, maslahi ya umma yataathirika kutokana na kutolewa kwa nyaraka hizo. Kutokana na maelezo hapo juu, unaweza kutumia kifungu hicho cha sheria kupata nyaraka kutoka kwa wakala wa Serikali.

Vilevile iwapo kutokufanyika malipo ni mgogoro, jibu fupi ni kwamba ni mgogoro, na kama utashindwa kulipwa una haki zote za kwenda kwenye Mahakama za ndani. Kutegemea na kiasi husika, tunakushauri uende Mahakama Kuu, Divisheni ya Biashara.

## Jukumu la mwanasheria kwa mteja

**Kama nimetenda kosa, tusema nimeua na nikafichua kwa mwanasheria wangu, je mwanasheria wangu anaweza kunigeuka? Si ni jukumu la mwanasheria kunitetea, bila kujali niko sahihi au siko sahihi? Hata hivyo, namlipa mwanasheria wangu kwa ajili ya kitu gani?**

*8 Desemba 2014*

Kwenye sheria za jinai, kama unakiri kwa mwanasheria wako kwamba umetenda kosa, mwanasheria wako anatakiwa akuongoze Mahakamani kukiri kutenda kosa hilo. Kuwa tu mwanasheria wako hakumaanishi kwamba anatakiwa kuipotosha Mahakama, kitu ambacho kinaweza kupelekea haki kupotea/ kutotendeka.

Kwa mfano, kama unamwambia mwanasheria wako kwamba ulifanya mauaji, basi mwanasheria wako, akiwa kama afisa wa Mahakama, ni lazima akuambie ukiri Mahakamani. Kama ukikataa, chini ya kanuni za kimaadili na haki, anatakiwa akatae kesi yako. Pia, kutegemea na nchi ambayo mwanasheria wako anafanya kazi, hawezi

kuruhusiwa kutoa ushahidi dhidi yako Mahakamani kwa kuwa ungamo lako kwake linalindwa chini ya mafaa/upendeleo wa mteja na mwanasheria.

Kazi ya mwanasheria ni kuhakikisha kwamba kesi yako inakuwa ya haki kwa mujibu wa Katiba na Kanuni ya Adhabu. Mwanasheria hatakiwi kudanganya au kupika ushahidi. Mwasheria anaweza kuwa mbunifu lakini ndani ya mipaka ya sheria.

## Mwanasheria "kishoka"

**Kuna mtu namjua hapa mjini ambaye siyo mthibitishaji wala kamishna viapo wa umma, lakini anajifanya kuwa ndiye. Je, hili siyo kosa nchini Tanzania?**

*15 Desemba 2014*

Sheria ya Wathibitishaji Umma na Makamishna Viapo inaeleza kwenye kifungu cha 6 kwamba (1) kwa kuzingatia kifungu cha 10, mtu yeyote anayejifanya kuwa mthibitisha umma (Notary Public) au kamishna wa viapo (Commissioner for Oaths) au anapokea ada au zawadi kama mthibitisha umma au kamishna wa viapo, isipokuwa kama ana leseni halali iliyotolewa kwa mujibu wa Sheria hii, atakuwa anatenda kosa na atawajibika kulipa faini isiyozidi Shilingi elfu moja na kwa kosa la pili na kuendelea atahukumiwa kifungo kisichozidi miezi sita au faini isiyozidi Shilingi elfu mbili au vyote kwa pamoja.

Kwa hiyo, Mthibitishaji Umma na Kamishna wa Viapo bandia anatenda kosa ambalo lina kifungo. Zaidi, nyaraka zote zilizothibitishwa na mtu huyo zinaweza kubatilishwa.

# Utakatishaji Fedha na Jinai ya Kampuni

Kama ilivyo kwa watu binafsi, wakati mwingine makampuni pia hufanya uhalifu. Katika sura hii, tunatoa mifano kadhaa ya tabia hizi, na kuelezea jinsi kampuni zinavyoweza kuadhibiwa kama taasisi, au kupitia wafanyakazi na wamiliki wake. Pia, tunajadili sheria ya utakatishaji fedha nchini Tanzania, kwa kujikita zaidi kwenye madhara yake, hasa kwa taasisi za fedha.

## Mkurugenzi ameshiriki kwenye udanganyifu

**Mimi ni mkurugenzi na mwanahisa wa kampuni moja ya uzalishaji nchini Tanzania. Mkurugenzi Mtendaji ambaye pia ni mwanahisa amekuwa akifuja pesa za kampuni kwa kutoingiza miamala mingi ya mapato katika vitabu vya kampuni. Hili liligunduliwa hivi karibuni na mkaguzi wa kujitegemea ambaye pia aligundua kuwa Mkaguzi wa Ndani wa kampuni amekuwa akila njama na Mkurugenzi Mtendaji kuficha miamala hiyo na kutangaza faida ndogo. Je, hilo si kosa la jinai?**

*26 Machi 2012*

Sheria ya jinai Tanzania inayoitwa Kanuni ya Adhabu inaelezea mazingira hayo. Inatamka kwamba mtu yeyote ambaye ni mkurugenzi au afisa wa shirika au kampuni, ikiwa atapokea au anamiliki mali yoyote ambayo ni ya shirika au kampuni tofauti na malipo ya deni la haki au uhitaji, na kwa nia ya kudanganya, anaacha ama kufanya maingizo yote na ya kweli katika vitabu vya kihasibu na katika hesabu za shirika au kampuni, au anaacha kuagiza au kuelekeza maingizo kufanyika; au akiwa mkurugenzi, afisa au mwanachama wa shirika au kampuni, anatenda mojawapo kati ya vitendo vifuatavyo, kwa dhamira ya kudanganya, ndio kusema; anaharibu, anabadili, anachana, au anaghushi kitabu chochote, nyaraka, dhamana yenye thamani au hesabu yoyote, ambayo ni mali ya shirika au kampuni, au maingizo yoyote katika kitabu chochote, nyaraka au hesabu au anashiriki kwa siri katika kitendo hicho; anafanya au anashiriki kwa siri katika kufanya, maingizo yoyote ya uongo katika kitabu chochote, nyaraka au hesabu; au anaacha, au anashiriki kwa siri katika kuacha, kuandika habari ndani ya kitabu chochote, nyaraka au hesabu, atakuwa anatenda kosa, na atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka kumi na nne.

Kutokana na maelezo hayo utaona kwamba hili ni kosa la jinai na mkurugenzi mtendaji anaweza kukumbana na kifungo kikali kama madai haya yatathibitika kuwa ya kweli.

Nje ya ujinai, unaweza pia kufungua shauri Mahakamani ya kurudisha fedha ambazo zimetumika vibaya ikiwemo faida ambazo hazikutangazwa. Kesi ya jinai pekee inaweza isipelekee kurudisha na ndiyo maana tunashauri ufungue kesi ya madai. Ni busara kupata ushauri wa kisheria kukusaidia kwenye suala hili.

## Kutunza taarifa za dereva

**Ninamiliki teksi mbili Jijini Dar es Salaam na nimeajiri madereva wawili. Mwezi uliopita mmoja wa madereva wangu alihusika kwenye ajali, amekimbia na hajakamatwa mpaka leo. Jambo la kushangaza, maafisa polisi wamenijia na kuniomba taarifa za maandishi za jina pamoja na leseni ya dereva aliyekimbia. Sina taarifa hizo ingawa namjua tu jina lake. Polisi wameniambia ni kosa kutokutunza taarifa za dereva. Naona suala hili kama ni la kazi zaidi kuliko kuwa la barabarani. Ninawezaje kuzuia unyanyasaji huu?**

*11 Juni 2012*

Mwajiri anatakiwa kutunza taarifa za wafanyakazi wake siyo tu kwa malengo ya kutii sheria, lakini pia taarifa hizo zinaweza kusaidia kwenye mambo mengine mengi ya msingi. Kwa mfano, vipi kama mfanyakazi wako amekuibia na hauna taarifa zozote za kusaidia kumpata?

Kimsingi, ingawa kwa malengo tofauti, Sheria ya Usalama Barabarani pamoja na Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini zinamtaka mwajiri kutunza taarifa za wafanyakazi wake.

Kwenye kesi yako, tunachukua kifungu

cha 79 cha Sheria ya Usalama Barabarani ambacho kinamtaka kila mwajiri wa dereva wa gari au tela kutunza taarifa za maandishi kuhusu jina la dereva na namba ya leseni yake. Ni wazi wewe hujatimiza hilo.

Kifungu cha 113 kinatamka kwamba mtu yeyote anayekiuka au anashindwa kutii vifungu vya Sheria ya Usalama Barabarani atakuwa ametenda kosa linaloadhibiwa kwa kulipa faini au kifungo. Hii ina maana kwamba kama kifungu cha 79 kikisomwa pamoja na kifungu cha 113 cha Sheria ya Usalama Barabarani, utakuwa na hatia ya kutenda kosa na unaweza kutozwa faini au kufungwa.

Polisi wako sawa kwa kile walichokwambia na hatuoni huo kama ni unyanyasaji. Katika hali nyingine, tunakushauri uanze kutunza taarifa za madereva wako ili kutii sheria, na kwa faida yako katika kuendesha biashara yako. Kutunza taarifa za wafanyakazi siyo tu suala la sheria bali ni kielelezo cha weledi wa hali ya juu katika usimamizi wa biashara. Kutunza taarifa hakukuhusu wewe peke yako kama mmiliki wa taksi bali kwa kila mtu anayeajiri dereva. Kuhusu suala lako la sasa, tunapendekeza uwasiliane na wanasheria wako.

## Bill Gates wa Afrika

**Nimebuni biashara fulani. Soko lake ni kubwa sana, ninataka kujua iwapo kisheria ninaweza kuwazuia watu wengine kufanya biashara kama hiyo kwa angalau miaka ishirini. Ninataka umiliki/utawala kamili ili niwe na pesa nyingi kama Bill Gates.**

*26 Novemba 2012*

Tuna furaha kwamba umebuni biashara ambayo inahitajika na tuna imani biashara hiyo itakuwa ni msaada mkubwa kwa umma. Pia tunakutakia kila la heri katika juhudi zako za kuwa Bill Gates wa Afrika.

Hata hivyo, Sheria ya Ushindani inakataza kitendo au tabia ambayo inalenga kuharibu au kuzuia ushindani. Kwa ujumla, mtu haruhusiwi kisheria kutawala soko kwa sababu ushindani ndiyo unaotakiwa. Unapaswa pia kuelewa kwamba kuna adhabu kali sana kwa kutenda au kuacha kutenda vitendo vyenye lengo la kutawala soko kwa kuzuia au kuondoa ushindani. Tunakushauri upate huduma ya mwanasheria ili akuongoze zaidi.

## Utakatishaji fedha benki

**Sisi ni benki kubwa yenye kuaminika na ya kimataifa na tuna matawi nchini kote. Hivi karibuni chini ya Sheria ya Kuzuia Utakatishaji Fedha Haramu, tumetakiwa kutoa kila aina ya nyaraka juu ya utambulisho wa wateja wetu fulani. Je, ni lazima tutoe ushirikiano? Maafisa wanatufuata na wanataka alama za vidole za wateja wetu ambao wamekuwa wateja wetu kwa miaka zaidi ya 10. Je, tunapaswa kuwaficha? Je, sio kinyume cha sheria kuombwa taarifa kama hizo? Je, taarifa zinapaswa zitunzwe kwa muda gani? Je, mkataba wa bima utatulinda kama tukipewa adhabu ya faini?**

*14 Januari 2013*

Iwe ni benki kubwa, inayoaminika na ya kimataifa au ndogo yenye mtaji mdogo na isiyoendeshwa kwa ufanisi, haileti tofauti yoyote linapokuja suala la Sheria ya Kuzuia Utakatishaji Fedha Haramu ya mwaka 2006. Kimsingi, baadhi ya matukio mengi makubwa ya utakatishaji fedha kihistoria yamefanyika katika mabenki. Sheria imefafanua wazi mtoa taarifa ni nani na inahusisha, wafanya-biashara wa fedha, wahasibu, madalali, wafanyabiashara wa vito vya thamani, mdhibiti, afisa wa forodha, wanasheria na mabenki ikiwa ni pamoja na taasisi za fedha. Hivyo, chini ya Sheria hii, benki yako ni mtoa taarifa na lazima izingatie Sheria na Kanuni zilizotungwa chini yake. Kuna Kanuni mpya zilizotungwa chini ya Sheria hii.

Ukiacha kanuni nyingine, kanuni ya 3 ni muhimu kwa swali lako ingawa ni ndefu, tunainakili hapa kama ilivyo kwa sababu ni muhimu sana. Inasema hivi: 3(1) Endapo mtoa taarifa anamhudumia mtu binafsi ambaye ni raia, au ni mkazi wa Jamhuri ya Muungano, atachukua taarifa zifuatazo kutoka kwa mtu huyo (a) majina kamili na anuani ya makazi; (b) tarehe na mahali pa kuzaliwa; (c) ikiwa ni raia, kadi ya usajili ya mpiga kura au kadi ya utambulisho wa kitaifa, pasipoti, cheti cha kuzaliwa au leseni ya udreva; (d) ikiwa ni mkazi, pasipoti, hati ya kusafiria, vibali vya makazi au leseni ya udreva ya mtu huyo; (e) barua ya utambulisho kutoka kwa mamlaka husika kama vile mwajiri au afisa wa Serikali; (f) kitambulisho cha mfanyakazi na barua ya utambulisho kutoka kwa mwajiri; (g) Namba ya Utambulisho wa Mlipa Kodi, kama namba hiyo imetolewa kwa mtu huyo; (h) chochote au vyote kati ya, namba za simu, namba ya faksi, anuani ya posta na anuani ya barua-pepe; (i) anuani ya makazi ya mteja ikiwa ni pamoja na alama muhimu za karibu na makazi ya mteja mtarajiwa; (j) ikiwa mteja ni mwanafunzi (k) barua ya utambulisho kutoka kwenye taasisi ya mteja iliyosainiwa na mkuu wa taasisi au mwakilishi wa mkuu wa taasisi; (l) kitambulisho cha mwanafunzi; (m) aina ya shughuli anayofanya; (n) saini na alama za vidole; na (o) bili za huduma anazotumia, kama inafaa. (2) Ikiwa mtoa taarifa anafahamu au anatakiwa kufahamu kwamba mtu anayezungumziwa kwenye kanuni ndogo (1) hana uwezo wa kisheria wa kuanzisha uhusiano wa biashara au kufanya shughuli mojawapo bila msaada wa mtu mwingine, mtoa taarifa atawajibika, pamoja na kupata maelezo yaliyotajwa katika kanuni ndogo (1) kupata kutoka kwa mtoa msaada (a) majina kamili na anuani ya makazi; (b) tarehe na mahali pa kuzaliwa; (c) Namba ya Utambulisho wa Mlipa Kodi, kama namba hiyo imetolewa kwa mtu huyo; (d) yoyote au zote kati ya, namba ya simu, namba ya faksi, anuani ya posta na ya barua-pepe; (e) anuani ya makazi ikiwa ni pamoja na alama muhimu za karibu na makazi yake; (f) uhusiano wa biashara na mtu anayemsaidia; na (g) saini na alama za vidole. (3) Iwapo mtoa taarifa anachukua alama za vidole chini ya Kanuni hizi, atatumia wino wenye ubora ili kuwezesha kupatikana kwa alama za vidole. (4) alama za vidole zitachukuliwa katika mfululizo ufuatayo (a) iwapo mtu huyo ana mikono yote miwili, alama za dole gumba la mkono wa kulia zitachukuliwa; (b) iwapo mtu huyo hana mkono wa kulia, alama za dole gumba la mkono wa kushoto zitachukuliwa; (c) ikiwa mtu huyo hana vidole gumba vyote viwili, basi kidole kinachofuata kitatumika, kwa kuanza na kidole cha kulia; na (d) ikiwa mtu huyo hana vidole, mtoa taarifa anaweza kuchukua kiganja au vidole vya miguuni. (5) Ikiwa mtu huyo hana mikono wala miguu, basi idhini ya kipekee kutoka kwa usimamizi wa mtoa taarifa itatakiwa kupatikana baada ya kurekodi hali hiyo.

Kutokana na maelezo hapo juu, ni wazi kwamba lazima uchukue alama za vidole vya mteja. Kanuni ya 30 inatamka kwamba mtoa taarifa atatunza kumbukumbu kwa muda usiopungua miaka kumi, hivyo hoja yako kuwa mteja wako ni wa zamani haina mashiko. Maafisa wanaokuulizia kumbukumbu wana haki ya kufanya hivyo. Chini ya Sheria hii, ikiwa benki yako imetenda kosa itakuwa na hatia ya kulipa faini kati ya shiling milioni 500 na bilioni moja, au kuamriwa kulipa kiwango sawa na mara tatu ya thamani halisi ya mali katika soko, kwa kuzingatia kiwango chochote kitakachokuwa kikubwa. Kuhusu suala lako la bima, utahitaji kuangalia sera yako lakini kutokana na sera za kawaida ambazo tumeziona sokoni, tuna shaka kama kampuni ya bima itakulinda kwa hilo. Mshauri wako wa masuala ya sheria anaweza kukuongoza zaidi.

## Benki kutoa taarifa juu ya utakatishaji fedha

**Ninafanya kazi benki kama msarifu na ninaona watu na kampuni ndogo ndogo wanaleta fedha taslimu makumi ya mamilioni kila siku. Je, hakuna sheria inayozitaka benki kutoa taarifa kama hizo kwa mamlaka yoyote ili watu hawa watozwe kodi na miamala yao ifuatiliwe? Inawezekana kabisa kuwa fedha hizi zimetokana na biashara ya madawa ya kulevya au utakatishaji wa fedha kutoka kwenye shughuli za ugaidi.**

*25 Februari 2013*

Sheria ya Kuzuia Utakatishaji wa Fedha Haramu na Kanuni za Kuzuia Utakatishaji Fedha Haramu, 2012, zinaeleza kwa uwazi juu ya jambo hili. Kuhusu taarifa zinazotakiwa kutolewa kuhusiana na miamala kwa Kitengo cha Kudhibiti Biashara ya Fedha Haramu kilichoanzishwa chini ya kifungu cha 4(2) na 17 cha Sheria, Kanuni ya 23 inataka taarifa zifuatazo (a) tarehe na muda wa muamala, au, ikiwa kuna mfululizo wa miamala kipindi ambacho miamala hiyo ilifanyika; (b) aina ya fedha au mali husika; (c) kiasi au thamani ya mali husika; (d) fedha ambayo muamala huo ulifanyika; (e) njia ambayo muamala huo ulifanyika; (f) namna ambayo fedha au mali zilizohusika; (g) kiasi kilichohusika; (h) sarafu ambayo fedha hizo zilihusika; (i) kusudi la muamala; (j) majina ya taasisi nyingine au mtu aliyehusika katika miamala; (k) namba za akaunti ya benki katika taasisi nyingine inayohusika kwenye muamala; (l) jina na tawi au ofisi ambapo muamala ulifanyika; na (m) maoni au ufafanuzi wa mtu aliyefanya muamala ameyatoa kuhusiana na muamala.

Kanuni ya 24 inaeleza zaidi namna ya kutoa taarifa ambapo mtoa taarifa, zikiwemo benki, kutengeneza taarifa inayohusiana na mali inayohusiana na ufadhili wa shughuli za ugaidi na Kanuni ya 25 inatoa maelezo maalum ambayo yanatakiwa kujazwa yanayohitajika na Kitengo cha Kudhibiti Biashara ya Fedha Haramu pale akaunti ya benki inapotumika kufanya shughuli zinazotia mashaka. Kwa ufupi, benki yako ni mtoa taarifa chini ya Sheria na kama benki yako inashindwa kutoa taarifa kuhusu aina hiyo ya shughuli zenye mashaka kwa Kitengo cha Kudhibiti Biashara ya Fedha Haramu, mameneja wako au wakurugenzi wanaweza kufungwa au kutozwa faini. Unatakiwa kujadiliana na meneja wako wa benki ambaye anaweza kuamua ni miamala ipi itolewe taarifa.

## Kutaifisha kipato cha rushwa

**Je, kuna sheria nchini Tanzania ambayo mapato yatokanayo na rushwa yanaweza kutaifishwa na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (PCCB)? Taratibu zake ni zipi?**

*29 Aprili 2013*

Jibu la swali lako la kwanza ni ndiyo. Kuhusu utaratibu, Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa inatamka kwenye kifungu cha 40(1) kwamba Taasisi inaweza, kwa kushirikiana na ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, kuchukua Mapato ya rushwa kupitia utaifishaji wa Serikali. (2) Pale ambapo mtu anapatikana na hatia ya kosa la rushwa chini ya Sheria hii, Mkurugenzi wa Mashtaka anaweza kuiomba Mahakama iliyomtia hatiani, au Mahakama nyingine yoyote inayofaa katika kipindi kisichozidi miezi sita baada ya mtu huyo kuwa hatiani, amri ya kutaifisha mali yote iliyopatikana kwa njia ya Rushwa. (3) Kwa madhumuni ya sehemu hii, "kipato cha rushwa" humaanisha mali yoyote ambayo inatokana au inapatikana na hatia ya makosa ya rushwa. Ni lazima ieleweke kwamba kutaifisha siyo kwa moja kwa moja, ni lazima ruhusa ya Mahakama ipatikane. Sheria hii pia inatamka kwamba kama amri ya kutaifisha imetolewa, mali zote zilizotaifishwa zitakuwa ni za Jamhuri ya Muungano.

## Sheria ya kuzuia na kupambana na rushwa ni dhaifu

**Kwa nini Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa ni dhaifu sana? Sielewi kwa nini sheria hii haikutungwa kukamata wala rushwa wakubwa?**

*20 Mei 2013*

Hatuna uhakika unamaanisha nini unaposema ni dhaifu. Kama ukiisoma Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa utagundua kuwa ni kali na inahusisha, angalau kwa ujumla, aina zote za rushwa, kiasi kwamba kujipatia manufaa ni kinyume cha sheria na kunashtakika. Kwa mfano, kifungu cha 23 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa kinatamka kwa upana sana kwamba, mtu yeyote ambaye anashawishi, anapokea au anajipatia kwa ajili yake mwenyewe au kwa ajili ya mtu mwingine yeyote, manufaa yoyote pasipo malipo halali ambayo anajua au ana sababu ya kuamini kuwa ni pungufu, (a) kutoka kwa mtu yeyote anayemfahamu au ana sababu ya kuamini kuwa amekuwa, au kuwa, au anaweza kujihusisha katika jambo au shughuli yoyote naye au kuhusiana ka namna yoyote ile na shughuli zake za kiofisi au za ofisa yeyote ambaye yeye yupo chini yake; au (b) kutoka kwa mtu yeyote ambaye anajua au ana sababu ya kuamini kwamba ana maslahi au ambaye anahusiana na au anatenda kwa niaba ya mtu anayehusika au mwenye uhusiano huo, anakuwa anatenda kosa na ikiwa atapatikana na hatia atahukumiwa kulipa faini isiyopungua Shilingi millioni kumi au kufungwa jela kwa kipindi kisichopungua miaka saba au adhabu zota kwa pamoja. (2) Pamoja na adhabu zinazotajwa katika kifungu kidogo cha (1), Mahakama -itaamuru kwamba kiasi cha fedha cha -manufaa yoyote yaliyopokewa na ofisa huyo, au sehemu yoyote ya manufaa hayo, itaifishwe na Serikali. Tunapendekeza usome tena Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa ili kujiridhisha kwamba unasoma sheria hiyo hiyo ambayo sisi tumeisoma. Kama una maswali zaidi wanasheria wako wanaweza kukuongoza.

## Kutangaza biashara kwa kutumia Bendera ya Taifa

**Kuna kampuni naijua ambayo inatumia vibaya bendera yetu kwa kuuza bidhaa kana kwamba bidhaa hizo zimeidhinishwa na Jamhuri ya Muungano. Je, hakuna sheria inayosimamia hili?**

*5 Agosti 2013*

Sheria ya Nembo za Taifa inatamka wazi juu ya matumizi batili ya Bendera ya Taifa, Nembo ya Taifa au vitu vingine vinavyofanana na hivyo kwa kuzuia mtu yeyote kutumia Bendera ya Taifa, Nembo ya Taifa au vinavyofanana na Bendera ya Taifa au Nembo ya Taifa: (a) kama alama ya biashara kwa vitu vinavyouzwa au vinavyotangazwa kuuzwa; (b) katika kuendeleza au kutangaza biashara yoyote, kiwanda, kazi au fani; (c) kwenye kitu chochote kinachouzwa au kinachotangazwa kuuzwa au kinachokusudiwa kuuzwa au kutolewa kwa ajili ya kuuzwa; (d) juu ya kitu chochote kinachotumika na mtu yeyote isipokuwa kwa matumizi yaliyoidhinishwa na Waziri.

Hivyo, kama kampuni au mtu anatumia bendera kama unavyodai, hilo ni kosa na mtu huyo anaweza kuhukumiwa kifungo mpaka miaka miwili jela. Unahitaji kuendelea na kutoa taarifa polisi. Hata hivyo, tafadhali elewa kwamba siyo matumizi yote ya Bendera ya Taifa ni batili, unapaswa kuwasiliana na mwanasheria wako kwa mwongozo zaidi.

## Kifungo kwa makampuni

**Nimekuwa nikisoma sheria za Tanzania na mara nyingi nimeona kwamba makampuni yanaweza kuadhibiwa na kutiwa hatiani. Najua kwamba watu binafsi wanaweza**

**kufungwa, lakini unawezaje kuifunga kampuni?**

*10 Juni 2013*

Hatujui ni sheria gani unairejea haswa, lakini kuna sheria nyingine zinasema kwamba wakurugenzi watafungwa, ikiwa na maana kwamba kukutwa na hatia/jinai kwa makampuni ni sawa na kukutwa na hatia kwa wakurugenzi.

Sheria ya Utafsiri wa Sheria za Tanzania pia inatamka kwenye kifungu cha 71 kwamba (1) Sheria yoyote inayoainisha makosa ambayo adhabu zake baada ya kutiwa hatiani (baada ya utetezi), au kutiwa hatiani kusikohitaji utetezi (summary conviction), itahusisha pia kampuni, mashirika, taasisi na watu binafsi. (2) Pale ambapo chini ya sheria iliyoandikwa, kutaifisha au adhabu inalipwa kwa mwathirika, italipwa kwa kampuni pale ambapo mwathirika ni kampuni. (3) Isipokuwa kama imeelekezwa vinginevyo, pale ambapo adhabu imeainishwa katika sheria dhidi ya kosa ambalo adhabu yake haijumuishi kulipwa kwa faini, Mahakama ambayo inasikiliza kesi hiyo inaweza, kwa mkosaji ambaye ni shirika, kampuni au taasisi kutoza faini (a) pale ambapo adhabu ni kifungo kisichozidi miezi sita, faini itozwe ya Shilingi Milioni Mbili; (b) pale ambapo adhabu ni kifungo kisichozidi miezi sita lakini kisichozidi mwaka mmoja itatolewa, faini itozwe ya Shilingi Milioni Tatu; (c) pale ambapo adhabu ni kifungo kinachozidi mwaka mmoja lakini hakizidi miaka miwili itatolewa, itozwe faini ya Shilingi Milioni Tano; (d) pale ambapo adhabu ni kifungo kinachozidi miaka mitatu itatolewa, itozwe faini ya Shilingi Milioni Kumi.

Unaweza kuona hapo juu kwamba kampuni, kama wakurugenzi hawatafungwa, watatozwa faini kama mbadala wa "kifungo".

## Kesi ya kampuni kwa jina la meneja

**Mimi ni Meneja Mwendeshaji na pia Mkurugenzi Mkuu wa kampuni ya kimataifa inayofanya shughuli zake nchini Tanzania. Kampuni imeshtakiwa, lakini cha ajabu na bahati mbaya ni kwamba mshtakiwa kwenye nyaraka tulizoletewa anaonekana kuwa ni jina langu kama Meneja Mkuu. Ninahofia hili na baada ya kumuuliza rafiki niliarifiwa kwamba kwenye nchi hii popote inapofunguliwa kesi dhidi ya kampuni ya kimataifa, meneja mkuu ndiye anayetakiwa kushtakiwa ili kuhakikisha utekelezaji iwapo Mahakama itaamuru malipo. Je, hii ni kweli kwa sheria za Tanzania? Tafadhali niongoze.**

*17 Juni 2013*

Ni mtu au taasisi inayojitegemea pekee ndiyo inayoweza kushtaki au kushtakiwa. Sheria zetu zinataka kesi zifunguliwe dhidi ya upande au pande sahihi. Kwenye kesi yako siyo sahihi kwa mdai kumshtaki Meneja Mkuu badala ya kampuni kwa sababu ya kanuni ya muda mrefu kwenye sheria kwamba kesi zote za kampuni au dhidi yake ni lazima zifunguliwe kwa jina la kampuni.

Zaidi, siyo kweli kwamba sheria zetu zinataka kesi zote dhidi ya kampuni za kimataifa zifunguliwe kwa jina la meneja au mkurugenzi mkuu. Hivyo inaonekana mtu asiye sahihi ameshtakiwa. Uzoefu wetu unaonesha kesi nyingi zilizofunguliwa dhidi ya watu ambao siyo taasisi zinazojitegemea zikiondolewa na majaji au mahakimu. Unaweza kuweka pingamizi la namna hiyo. Wanasheria wako wanaweza kukuongoza zaidi.

## Kutokutoa taarifa kuhusu fedha za kigeni

**Ninawajua wasafirishaji wa bidhaa nje ambao wanatoa taarifa za uongo kuhusu kiasi cha fedha wanachopata na kuidanganya Serikali. Je, hakuna sheria inayowawajibisha? Ninataka niwataje watu hawa ambao wanapata fedha nyingi lakini**

**wanawasilisha kiduchu tu. Kwa kiasi gani wakurugenzi wanawajibika?**

*11 Agosti 2014*

Moja ya sheria za Tanzania ambayo ni kali sana kuhusu masuala kama hayo ni Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Kigeni ambayo inaeleza kwa uwazi yafuatayo: Mtu yeyote anayetoa taarifa za uongo kuhusu shughuli yoyote iliyoelezwa kwenye Sheria hii au Kanuni zinazotokana na Sheria hii akiwa na lengo la (a) kukwepa kueleza kiasi halisi cha fedha za kigeni alichokipata; au (b) anachelewa kulipa kiasi cha fedha za kigeni alichokipata ambacho anatakiwa kukilipa; au (c) anabaki na kiasi chochote cha fedha za kigeni kinacholipwa nje ya Jamhuri ya Muungano, atakuwa ametenda kosa na endapo akikutwa na hatia atawajibika kwa kifungo cha miaka isiyozidi kumi au faini sawa na hiyo, kwa kiasi kisichozidi mara tatu ya kiasi cha fedha kilichotakiwa kulipwa ambacho au mtu huyo anadaiwa, au vyote viwili, kifungo pamoja na faini.

Sheria pia inaeleza kwamba wakurugenzi watawajibika kwa kosa hilo hata kama litakuwa limetendwa na kampuni. Kifungu cha 14 kinaeleza ifuatavyo: (a) Iwapo kosa la kifungu hiki limetendwa na kampuni, basi pamoja na kampuni, mtu yeyote wakati kosa linatendeka alihusika kama mkurugenzi, au afisa ambaye alikuwa kwenye menejimenti ya usimamizi wa kampuni hiyo, atakuwa ametenda kosa na atawajibika na ataadhibiwa isipokuwa kama atathibitisha mbele ya Mahakama kwamba alikuwa hana uelewa na asingeweza hata kwa uchunguzi wa kina kujua utendwaji wa kosa hilo.

Unaweza kuona kwamba sheria hii inatoa adhabu ya kifungo pamoja na faini ya hadi mara tatu ya kiasi husika. Wakurugenzi pia wanaweza kuwajibika isipokuwa kama wanaweza kuthibitisha kwamba walikuwa hawajui kama kosa limefanyika. Kwa kuzingatia maelezo hapo juu, unaweza kufanya inavyotakiwa.

## Uchunguzi wa akaunti ya benki

**Je, sisi kama benki tufanyaje kama polisi wanatupigia simu mara kwa mara na kututaka tuwapatie taarifa zote za akaunti ya mteja? Je, tunalazimika kufanya hivyo? Wanadai kupiga simu kutoka makao makuu ya polisi.**

*1 Septemba 2014*

Kama benki msifanyie kazi taarifa za mdomo na kwa hiyo mnatakiwa kufuatilia iwapo mtu anayewapigia ni polisi kweli - inawezekana kabisa watu hawa ni matapeli kwa sababu polisi kwa kawaida wangewaandikia barua rasmi huku wakieleza kifungu cha sheria wanachokitumia kuomba taarifa fulani na sababu za kufanya hivyo, vinginevyo kila akaunti ya mtu inaweza kuchunguzwa. Tafadhali elewa kwamba kuchunguza/kusimamia akaunti ni zoezi endelevu tofauti na polisi na Mamlaka ya Mapato ambao huomba taarifa za kifedha za akaunti fulani tu.

Kuhusu usimamizi/uchunguzi wa akaunti, Sheria ya Mapato Yatokanayo na Uhalifu inaeleza wazi kwenye kifungu cha 65 kwamba (1) Mkurugenzi wa Mashtaka anaweza kutuma maombi kupatiwa amri ya usimamizi ikielekeza taasisi ya fedha kutoa taarifa za kibenki kwa Inspekta Jenerali wa Polisi kuhusu shughuli za fedha zilizofanyika kupitia kwenye akaunti ya mtu fulani katika taasisi hiyo ya kifedha. (2) Amri ya usimamizi itatumika kuhusiana na kumbukumbu za kifedha zilizofanywa katika kipindi kilichoelezwa katika amri. (3) Mahakama haitatoa amri ya usimamizi mpaka iridhike kwamba kuna sababu adili za kutilia shaka kwamba mtu yule mwenye akaunti ambayo taarifa zake zinatafutwa (a) ametenda au anatiliwa shaka kutenda kosa maalum; (b) alishiriki katika utendaji wa kosa au anatiliwa shaka ya kujihusisha na utendaji wa kosa maalum; au (c) amefaidika dhahiri au kwa

namna isiyo dhahiri kutokana na utendaji wa kosa maalum. (4) Amri ya usimamizi itaelezea jina au majina ambayo akaunti inaaminika kushikwa na aina ya taarifa ambayo taasisi ya fedha inatakiwa kutoa. (5) Taasisi yoyote ya fedha ambayo itavunja amri ya usimamizi au itatoa habari za uongo au zinazopotosha itakuwa inatenda kosa na itawajibika kulipa faini isiyozidi Shilingi milioni moja.

Kama unavyoweza kuona, Mkurugenzi wa Mashtaka ni lazima aombe Mahakamani amri ya usimamizi/uchunguzi na awapatie amri hiyo kabla hamjaanza kumpatia taarifa mara kwa mara/kwa uendelevu. Wanasheria wako wanaweza kukuongoza zaidi.

## Kampuni inashtakiwa kwa uhalifu

**Kampuni yetu ilikabiliwa na changamoto fulani na imeshtakiwa kwa kosa la jinai. Siku ya kwanza ya kusikilizwa kesi hatukufika Mahakamani kwa sababu wito wa Mahakama uliwasilishwa kwa katibu muhtasi (sekretari) wetu na siyo kwa afisa yeyote mwandamizi. Mwanasheria wetu alitufafanulia kwamba wito haukuwasilishwa vizuri na hivyo hakuna haja ya kuhudhuria. Tulikubaliana naye, na sasa tumearifiwa kwamba Mahakama iliendelea kusikiliza kesi bila uwepo wetu na imetukuta na hatia. Tunawezaje kuhukumiwa wakati hatukuhudhuria?. Tafadhali tuongoze.**

*27 Oktoba 2014*

Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai inatamka kwamba kuwasilishwa kwa wito kwenye kampuni iliyosajiliwa unaweza kufanywa kwa kupeleka kwa katibu muhtasi, meneja mwenyeji au afisa mwingine mwandamizi wa kampuni katika ofisi ya kampuni iliyosajiliwa au kwa barua iliyosajiliwa iliyoelekezwa kwa afisa mtendaji mkuu wa kampuni na katika suala la barua iliyosajiliwa, uwasilishwaji utachukuliwa kuwa umefanyika wakati barua imefika katika njia ya kawaida ya posta.

Unaweza kuona kwamba wito uliwasilishwa sawa sawa kupitia kwa katibu muhtasi wako na sio lazima uwasilishwe kwa mkurugenzi au afisa mkuu. Kinachoweza kukuokoa ni pale sheria inaposema, katika shauri la shirika/kampuni/taasisi, mwakilishi hakuhudhuria katika muda ulitotajwa na wito au taarifa au kama mwakilishi huyo amehudhuria lakini ameshindwa kujibu shtaka, Mahakama itaamuru jibu la 'kukana kosa' kuandikwa na shauri litaendelea kama vile shirika limetoa jibu la kukana kosa.

Hii inamaanisha kwamba ikiwa haukuhudhuria siku ya kwanza ya kusikilizwa, basi jibu la 'kukana kosa' lilitakiwa liandikwe na Mahakama. Kwa hiyo ikiwa hii ilikuwa mara ya kwanza kesi hiyo iliitwa basi kampuni yako isingetakiwa kutiwa hatiani. Tunapendekeza umdokezee mwanasheria wako juu ya kifungu tajwa hapo juu cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai.

## TAKUKURU kudai nyaraka za siri

**Sisi ni wawekezaji nchini Tanzania na tumeambiwa na Ofisi ya Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kuwapatia mikataba yetu iliyoingiwa Tanzania na pia kujipeleka mbele yao. Je, hii siyo kazi ya polisi, na je, ni lazima Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ahudhurie? Mikataba hii ni ya siri na hatuwezi kuifichua. Tafadhali tuongoze.**

*27 Oktoba 2014*

TAKUKURU imeanzishwa chini ya Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa ambayo ni sheria ya adhabu inayohusika, pamoja na mambo mengine, na mambo ya rushwa. Hivyo, TAKUKURU haina uhusiano na polisi, na imepewa mamlaka kuchunguza mambo ya rushwa.

Kifungu cha 10 (1) cha Sheria hii kinatamka kwamba Ofisa wa Taasisi anayepeleleza kosa kwa mujibu wa Sheria hii anaweza –

(a) kumwamuru/kumuita mtu yeyote kuja kwake kwa ajili ya kuhojiwa kwa mdomo au kwa maandishi kuhusiana na jambo lolote ambalo linaweza kusaidia katika upelelezi wa kosa; (b) kumwamuru mtu yeyote kutoa kitabu, waraka au nakala iliyothibitishwa, na kitu chochote kinachoweza kusaidia katika upelelezi wa kosa. (c) kwa taaarifa ya maandishi, kumtaka mtu yeyote kutoa maelezo ya kiapo au uthibitisho ikieleza taarifa hiyo ambayo ianaweza kusaidia katika upelelezi wa kosa. (2) kwa maelekezo ya Mkurugenzi wa Mashtaka, Mkurugenzi Mkuu anaweza kuendeleza upelelezi wa makosa yanayohusiana na rushwa yaliyoanzishwa na polisi au chombo kingine cha kusimamia sheria. (3) Mtu yeyote ambaye, wakati wa upelelezi au wakati wa mashtaka yanayohusiana na kosa linaloshukiwa kutendwa chini ya sheria hii, huku akijua (a) akitoa au kusababishwa kutolewa kwa taarifa za uongo kwa ofisa wa upelelezi juu ya kosa lililotendwa; au (b) akimpotosha ofisa yeyote wa upelelezi, atakuwa anatenda kosa na akipatikana na hatia atahukumiwa kulipa faini ya kiasi kisichopungua Shilingi laki moja na kisichozidi Shilingi millioni mbili au kwenda jela kwa muda wa mwaka mmoja au adhabu zote mbili kwa pamoja.

Tafsiri nyepesi ya kifungu cha 10 hapo juu ni kuwa sheria inaruhusu afisa yeyote wa TAKUKURU kuomba na kupewa waraka husika. Hivyo, sheria hii iko juu ya kifungu chochote cha usiri kwenye mikataba yenu na lazima upeleke nyaraka hizo TAKUKURU. Kama usipotoa ushirikiano au hautatoa nyaraka hizo utakuwa unafanya kosa na unaweza kukumbana na kifungo.

## Wajibu wa kijinai kwa wakurugenzi

**Kama kampuni inashtakiwa chini ya Sheria ya Usalama wa Taifa, je, wakurugenzi na mameneja wa kampuni wanaweza kuwajibika? Hivi si kwamba wao ni wafanyakazi tu wa kampuni?**

*10 Novemba 2014*

Sheria ya Usalama wa Taifa inasema wazi kwamba iwapo kosa la kifungu hiki limetendwa na kampuni, basi pamoja na kampuni, mtu yeyote wakati kosa linatendeka alihusika kama mkurugenzi, au afisa ambaye alikuwa kwenye menejimenti ya usimamizi wa kampuni hiyo, atakuwa ametenda kosa na atawajibika na ataadhibiwa isipokuwa kama ataithibitishia Mahakama kwamba alikuwa hana uelewa na asingeweza hata kwa uchunguzi wa kina kujua utendwaji wa kosa hilo. Sheria hii inatoa hukumu hadi kifungo cha maisha na hivyo unapaswa kushauriana na mshauri wako wa kisheria ikiwa unahusika na makosa chini ya sheria hii.

## Makubaliano ya kupanga bei

**Kuna kada ya uzalishaji wa bidhaa fulani ambapo ni wazi kwamba wazalishaji watatu wakubwa, ambao walikuwa washindani, wamekula njama na kupanga bei moja kwa wote ili kuondoa ushindani. Je, huu siyo ubatili?**

*10 Novemba 2014*

Sheria ya Ushindani ya mwaka 2003 inaeleza kwamba mtu hataruhusiwa kufanya au kutekeleza makubaliano kama lengo au matokeo ya makubaliano hayo ni kupanga bei baina ya washindani. Kupanga bei baina ya washindani maana yake ni kupanga, kuweka vikwazo, au kudhibiti bei, ushuru, malipo ya ziada au malipo mengine kwa ajili ya, au kwa makubaliano au masharti ambayo upande mmoja katika makubaliano husambaza au hupata; au huhiari kufanya usambazaji au kupata, bidhaa au huduma, katika kushindana na upande wowote kwenye makubaliano. Mtu yeyote ambaye kwa makusudi au kwa

uzembe anafanya jambo lolote kinyume na kifungu hiki anatenda kosa. Sheria inaweka faini kubwa kwa tabia kama hizo.

# Hati ya Uwakilishi, Kifo, Mirathi na Wosia

"

Inasikitisha kwamba, wakati mwingine, kifo cha mpendwa wetu huweza kusababisha vita kali ya kisheria baina ya aliowaacha hai. Wakati mwingine wosia huibiwa, au huambatana na masharti magumu ambayo wanufaika hawako tayari kuyatelekeza. Jambo la kushukuru ni kwamba hali hizi zote mbili zinasimamiwa na sheria, ambayo inatoa kinga/nafuu kwa wale wote wanaoathirika kwa namna moja au nyingine.

## Wosia haujasainiwa na mwanasheria

**Mwanasheria wangu hakusaini wosia wangu na sasa amefariki. Je, hilo linabatilisha wosia? Nina hofu sana kwa sababu sitaki kuacha wosia batili. Tafadhali niongoze?**

*2 Januari 2012*

Kwanza kabisa, hakuna sharti kwamba wosia wako ni lazima usainiwe na mwanasheria wako. Hivyo haijalishi kama wakili wako amefariki au yungali hai; hupaswi kuwa na hofu.

Pili, wosia wako unaweza kubadilishwa wakati wowote, ikiwa na maana kwamba hata kama wakili aliyeuandaa mwanzoni hayupo tena, unaweza kuendelea kubadili wosia wako. Ikumbukwe, wosia ni nyaraka inayoweza kubadilika, tena ni muhimu, inapolazimu, upitiwe kila mwaka au kila baada ya miaka miwili. Iwapo bado una mashaka, tunakushauri uandike wosia mpya na utafute mashahidi wawili wausaini mbele yako.

## Kutumia hati ya uwakilishi kudai talaka

**Mimi ni mwanamke niliyeolewa na nina watoto wawili. Kutokana na vitendo vya kukosa uaminifu vya mume wangu, ndoa yetu kwa sasa haivumiliki. Kama ambavyo yeye hawezi kukubali mimi kuwa na mtu mwingine, mimi pia siwezi kukubali yeye kuwa na mtu mwingine kwa sababu hilo siyo lengo la ndoa. Mbaya zaidi, mume wangu amezaa mtoto na mwanamke huyo. Je, mimi nina haki zozote kwa mtoto huyo? Nimepeleka maombi ya talaka Mahakamani na nimempa dada yangu hati ya uwakilishi ambayo inamruhusu dada yangu wa Dar es Salaam kufanya liwezekanalo ili kunisaidia kupata talaka. Mume wangu anapinga talaka na hakimu anayesikiliza amekataa kuendelea na kesi anataka niwepo mwenyewe Mahakamani. Je, mtu mwenye hati ya uwakilishi hawezi kunisaidia kupata talaka?**

*9 Aprili 2012*

Hatuna hakika unamaanisha nini kuhusu haki yako juu ya mtoto. Kibaiolojia wewe siyo mama yake. Uhusiano hapa unaletwa na mume wako, ya kwamba yeye ni mume wako na ni baba wa mtoto. Hauna uhusiano mwingine wowote na hivyo huwezi kuwa na haki juu ya mtoto. Mama wa mtoto ni mwanamke mwingine japo amezaa na mume wako.

Sasa tunajikita kwenye suala la talaka. Kutokana na maelezo hapo juu hatuna uhakika wa sababu hatujui sababu ambazo umeziainisha kwenye maombi yako ya talaka. Tunadhani kuwa maelezo ya kwenye maombi au dhidi ya maombi yanataka mtu awepo na atoe ushahidi. Ifahamike wazi kwamba mwakilishi wa mwomba talaka siyo shahidi mahususi na anaweza tu kuwepo Mahakamani kwa niaba ya upande uliomteua na kufanya vitu vilivyotajwa kwenye hati ya uwakilishi.

Mwenye hati ya uwakilishi anaweza tu kuwepo Mahakamani kama shahidi kuhusiana na mambo ambayo yapo ndani ya uelewa wake. Hawezi kutolea maelezo ambayo yapo nje ya uelewa wake ambao ameupata kutoka kwa aliyempa mamlaka hayo bila kutoa ushahidi kuhusu mambo hayo yeye mwenyewe. Inaonesha kwamba hakimu anaamini kwamba kuna maelezo ambayo yapo ndani ya uelewa wako ambayo hayawezi kutolewa na mwakilishi wako na ndiyo maana amekutaka wewe mwenyewe uende Mahakamani. Hatuoni kama hii si haki na kwa ajili ya kupata utatuzi wa haraka unaweza kukata rufaa.

## Wosia umeibiwa

**Wifi yangu ameiba Wosia wa mume wangu kwenye kabati letu. Nina uhakika kwa**

**sababu kuna mali fulani ya mume wangu anaitolea macho sana ambayo ninatakiwa kupewa. Nifanye nini?**

*13 Agosti 2012*

Kanuni ya Adhabu iko wazi kabisa kwamba iwapo kitu kilichoibwa ni waraka wa wosia, iwe mtoa wosia huo yupo hai au amefariki, mkosaji atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka kumi. Tunakushauri utoe taarifa polisi ambapo wao watafanya uchunguzi na kutegemea na matokeo ya uchunguzi, wanaweza kumfungulia mashataka wifi yako. Anaweza kufungwa jela miaka kumi.

## Kunyofolewa viungo vya marehemu

**Miaka miwili iliyopita nilimpoteza baba yangu hospitali kwa ajali ya gari. Tukiwa hospitalini, Mganga Mkuu wa hospitali aliomba idhini ya mama yangu ili atoe baadhi ya viungo vya marehemu kwa ajili ya matibabu ya watu wengine. Je, ni halali kunyofoa viungo vya maiti? Tafadhali niongoze.**

*20 Agosti 2012*

Sheria zetu zinamruhusu mganga mkuu wa hospitali kutoa au kuruhusu kutoa sehemu yoyote ya mwili wa marehemu kama atajiridhisha kwamba kiungo hicho kinahitajika kumtibu mtu mwingine. Hata hivyo, Mganga Mkuu huyo anatakiwa kwanza kupata idhini ya mwenza wake, mzazi au mlezi wa marehemu kama watakuwepo. Neno "kama watakuwepo" maana yake ni ndani ya muda ambao utawezesha utoaji wa kiungo hicho kikiwa katika hali ya kufaa kwa matumizi yaliyokusudiwa. Msingi wa sheria hii ni wazi kwamba viungo vya marehemu vinaweza kutumika ili kuokoa maisha ya watu wengine. Hivyo ombi la Mganga Mkuu kwa mama yako lilikuwa ni halali.

## Mnufaika wa wosia

**Mume wangu alifariki na kuacha vifaa muhimu vya muziki kwa ajili ya rafiki yake aliyemtaja kwenye wosia. Sikumjua mtu huyo, lakini kama wasii nilifuatwa na mtu mmoja ambaye alijitambulisha kama ndiye mtu aliyetajwa kwenye wosia. Baada ya kupata uthibitisho wa wosia nilimpatia mtu huyo vifaa vyote vya muziki vilivyotajwa kwenye wosia. Mwaka mmoja baadaye alikuja mtu mwingine ambaye alidai kwamba ndiye aliyetajwa kwenye wosia. Uchunguzi wangu umebaini kwamba mtu wa kwanza alikuwa ni tapeli wakati yule aliyekuja mwaka mmoja baadaye alikuwa ndiye mwana bendi mwenzake na mume wangu, na ndiye aliyestahili kupata vifaa hivyo. Je, nifanye nini?**

*30 Desemba 2013*

Kanuni ya Adhabu ina kifungu kinachozungumzia suala hilo na inatamka kwamba, mtu yeyote ambaye, kwa dhamira ya kumhadaa mtu yeyote, kwa uongo anajiwakilisha kuwa ni mtu mwingine, aliye hai au aliyekufa, atakuwa anatenda kosa. Iwapo uwakilishi huo ni kwamba mkosaji huyo ndiye mwenye haki ya wosia au kwa sheria kupata mali fulani yoyote, anatenda kosa kupata mali hiyo au kuimiliki, atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka saba. Ingawa haitakuwa rahisi kumpata tapeli, tunashauri utoe taarifa polisi ili hatua stahiki ziweze kuchukuliwa.

## Wosia wa Kiislamu dhidi ya aina nyingine za wosia

**Je, sheria za kuandika/kuandaa wosia ni zipi na vipi kama mimi ni Muislamu na sitaki sheria za Kiislamu zitumike kugawanya mali zangu pale ninapokuwa nimefariki? Je, hilo linawezekana? Nifanye nini?**

*10 Februari 2014*

Sheria za Kiislamu hazina muundo maalum wa namna wosia unavyopaswa kuandikwa. Hata hivyo, kwenye wosia vitu vifuatavyo ni lazima viwepo: jina la mtoa wosia, majina ya wanufaika, jina la wasii akiwemo wasii mbadala pamoja na aina za mali na namna unavyopenda zigawanywe. Kama mtoa wosia anaweza kusoma na kuandika, basi wosia huo ni lazima ushuhudiwe na mashahidi wawili au zaidi (inashauriwa kwamba mmoja awe na uhusiano na mtoa wosia na mwingine asiyekuwa na uhusiano). Hata hivyo, kama mtoa wosia hajui kusoma, basi watu wasiopungua wanne washuhudie wosia huo, wawili kati yao wawe na uhusiano na mtoa wosia na wawili wasiwe na uhusiano naye.

Zaidi, tafadhali elewa kwamba mtoa wosia pamoja na mashahidi ni lazima wote wawepo wakati wa kushuhudia wosia na kila mmoja amshuhudie mwenzake akisaini wosia kwa wakati huo huo. Baada ya kifo, sheria itakayotumika kugawanya mali itakuwa ama sheria ya kidini au ya kimila kutegemea na maisha aliyokuwa akiishi marehemu.

Kuhusu mali za Muislamu, iko wazi kwamba mtoa wosia anaweza kugawa theluthi tu ya mali zake, na zinazosalia zitagawanywa kama ilivyoelezwa kwenye Korani Tukufu. Sheria ya Uthibitisho wa Wosia na Usimamizi wa Mirathi pamoja na Kanuni zake hazizungumzi iwapo Muislamu anaweza kuamua kutokugawa mali za marehemu kwa mujibu wa sheria za Kiislamu. Hata hivyo, kuna maamuzi ya Mahakama yanayotamka kwamba mtoa wosia wa Kiislamu anaweza kueleza wazi kwenye wosia kwamba hataki mali zake zigawanywe kwa mujibu wa sheria za Kiislamu.

Ingawa unapuuzwa, wosia ni waraka muhimu sana ambao ni lazima uuandike kwenye maisha yako. Siku moja wosia wako utazungumza na siyo mdomo wako. Tafadhali wasiliana na mwanasheria wako kwamaelezo zaidi.

## Hati ya uwakilishi

**Iwapo nimepewa hati/ruhusa ya uwakilishi, je, ninaweza kumpa mtu mwingine hati hiyo ya uwakilishi? Kwa ufupi, ninataka kumteua mtu mwingine aniwakilishe, ingawa mimi ndiye mteule wa awali wa "mtoa ruhusa".**

*3 Machi 2014*

Hati ya uwakilishi (Power of Attorney) ni ruhusa ya maandishi ya kuwepo au kumuwakilisha mtu mwingine kwenye masuala binafsi, biashara au masuala mengine ya kisheria. Mtu anayemruhusu mtu mwingine kutenda kwa niaba yake anaitwa "mtoa ruhusa" na mtu anayepewa uwakilishi huo anaitwa "mpokea ruhusa", mwakilishi au wakala.

Mtu anayetoa nguvu ya uwakilishi, anaweza tu kufanya hivyo kama ana akili timamu. Kwenye baadhi ya hati za uwakilishi, mtoaji anatamka kwamba anataka waraka huo uendelee kutumika hata wakati ambao yeye hajiwezi. Aina hii ya hati ya uwakilishi inaitwa hati ya uwakilishi ya kudumu (kwa kuwa mtu hajiwezi), kwa uelewa wetu, hati ya aina hii haijawahi kujaribiwa nchini Tanzania kwa kuwa iwapo mtu hajiwezi, mtu huyo hawezi kutoa hati ya uwakilishi iliyo halali. Kama mtu hana uwezo wa kutoa hati ya uwakilishi (na hana hati ya uwakilishi ya kudumu), namna pekee mtu mwingine anaweza kutenda kwa niaba yake ni ama kuangalia wosia wa mtu huyo au kupeleka maombi Mahakamani ili kuteuliwa kuwa mlezi ambaye atatenda/atafanya kwa maslahi ya mtu huyo.

Turudi kwenye swali lako, hakuna uwezekano wa wewe kumkasimisha mtu mwingine mamlaka yaliyopo chini ya hati ya uwakilishi, isipokuwa kama hati hiyo ya uwakilishi inatamka wazi kukuruhusu kufanya hivyo. Ni kanuni ya kisheria kwamba, mamlaka yaliyokasimishwa hayawezi

kukasimishwa zaidi. Wanasheria wako wanaweza kukuongoza zaidi.

## Wosia wa mume unakataza kuolewa

**Mimi ni mjane mrembo na tajiri. Mume wangu aliacha wosia wakati alipofariki kwa ajali miaka minne iliyopita. Baada ya mume wangu kufariki, wosia unaodaiwa kuwa ni wake uliwasilishwa na bila kuwa na masharti mengine, mume wangu alisema sitakiwi kuolewa atakapofariki. Nimejitahidi kuendana na matakwa yake lakini hivi sasa nimezama kwenye dimbwi zito la mahaba/huba na mwanamume mwingine ambaye ninataka kuolewa nae. Wanangu wamekua na wanamalizia elimu yao ya upili/sekondari, hivyo siyo watoto tena. Wakwe zangu wameijua nia yangu na wamenionya nisijaribu kuolewa tena. Je, sharti hili ni la kisheria? Je, ninalazimika kufuata wosia? Je, wakwe wanaweza kuizuia ndoa yangu ya pili? Je, sharti hili linaathiri mali nilizorithi? Tafadhali niongoze.**

*17 Machi 2014*

Ni jambo la kushangaza kukuta sharti kama hilo kwenye wosia. Kisheria, masuala ya wajane yanasimamiwa kwa uwazi na Sheria ya Ndoa (Sura ya 29 iliyorekebishwa Mwaka 2002) ambayo chini ya kifungu cha 68 inatamka kwamba bila kujali mila zozote zinazokwenda kinyume, mwanamke aliyefiwa na mume atakuwa huru (a) kwenda kuishi mahala popote apendapo na kukaa bila mume au kuolewa na mume yeyote atakayeridhika naye. Isipokuwa, kama aliolewa katika ndoa ya kiislamu, mjane huyo hatakuwa na haki ya kuolewa tena mpaka pale kipindi cha eda kitakapokwisha, ambacho ni kipindi cha miezi 4 na siku 10 baada ya kifo, kipindi ambacho kwenye suala lako kimepita sana.

Licha ya kuwepo masharti magumu kwenye wosia, hakuna kitu chochote halali kinachoweza kukuzuia kuolewa na mwanamume mwingine. Wakwe hawawezi kuzuia kufanyika kwa ndoa yako ya pili. Kwa busara tu, unaweza kutumia wazee ili wakusaidie kutatua jambo hili. Uzoefu wetu unaonesha kwamba, kwa tamaduni zetu za kitanzania, wajane kuolewa tena siyo jambo geni.

Vile vile kuhusu ulichokirithi, kitaendelea kuwa ni cha kwako na kwa maoni yetu kitaendelea kuwa ni mali yako bila kujali kwamba kulikuwa na sharti kama hilo kwenye wosia wa mmeo. Hata hivyo, tunashauri wanasheria wako waliangalie jambo hili.

## Wosia unakataza kuolewa

**Nilikuwa karibu sana na baba yangu ambaye alifariki na kuniachia mali nyingi sana. Kwenye wosia aliandika kwamba nisiolewe kwa sababu wakati wa uhai wake tulikubaliana kwamba niwe mtawa (sista). Nilizungumza na baadhi ya marafiki zangu ambao walianiambia kwamba kwenye sheria zetu siwezi kuolewa na hata kama nikiolewa, cheti cha ndoa kitakuwa ni batili. Je, jambo hilo ni la kweli? Nina hofu kwamba kama nitaolewa roho ya marehemu haitapumzika kwa amani.**

*16 Juni 2014*

Hiyo siyo kweli kabisa. Kuolewa ni haki ya kiulimwengu hakuna wosia wala nyaraka nyingine yoyote inayoweza kukuzuia kuolewa. Haijalishi baba yako anataka nini, linapokuja suala la haki binafsi kama hiyo, wewe ndiye mwamuzi wa mwisho. Hivyo, kwa mujibu wa sheria unaweza kuendelea kama utakavyoona inafaa. Wanasheria wako wanaweza kukuongoza zaidi. Kwa bahati mbaya kama wanasheria hatuwezi kutoa maoni au kujibu kuhusu roho ya marehemu kwa sababu siyo suala la kisheria. Ni suala ambalo linaweza kujibiwa vema na viongozi wako wa kiroho/kidini.

## Mke kuiba wosia

**Je, inawezekana mke kumuibia mume wake? Kaka yangu amefariki na nina hakika alimuachia mke wake wosia, ambaye ametoweka nao na hauJulaikani ulipo.**

*22 Septemba 2014*

Kifungu cha 264 cha Kanuni ya Adhabu kinatamka kwamba ili kuondoa mashaka, inatangazwa hapa kuwa mume anaweza kuwa na hatia kwa kumuibia mke wake au mke kwa kumuibia mumewe. Kanuni ya Adhabu pia inasema kwamba iwapo kitu kilichoibiwa ni waraka wa wosia, iwe mtoa wosia huo yupo hai au amefariki, mkosaji huyo atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka kumi. Hivyo, kutoweka kwa mke kunaweza kutolewa taarifa polisi, na ikiwa ameiba wosia, anaweza kukamatwa na kushtakiwa.

## Wasii hajalipa ada za leseni

**Baba yetu alifariki miaka kadhaa iliyopita na alimteua rafiki yake kuwa wasii. Taratibu zote za utoaji wa uthibitisho wa wosia zilifuatwa baada ya kifo cha baba yetu na Mahakama ikamteua rafiki wa baba yetu huyo kuwa wasii/msimamizi wa mirathi. Hivi karibuni tumegundua kwamba wasii hakulipia kodi mojawapo ya leseni za awali za uchimbaji (madini) ambazo marehemu baba yetu alikuwa anazimiliki. Hivi sasa leseni tumenyang'anywa na tumeamriwa kuondoka kwenye mgodi kwa kuwa amepewa mtu mwingine. Je, kama warithi, kuna njia tunayoweza kumshtaki wasii kwa sababu tulimpa taarifa zote kabla, na hivi karibuni alitudanganya kwamba alikuwa ameshalipa ada? Kaka yangu ambaye ni mshauri wa masuala ya uchimbaji/madini tayari ameanza kufuatilia jambo hili kwa Kamishna wa Madini kuuliza juu ya kupokonywa huko, ninachotaka kujua kutoka kwenu ni kama tunaweza kumwajibisha wasii. Tafadhali tuongoze.**

*3 Novemba 2014*

Sheria ya Uthibitisho wa Wosia na Usimamizi wa Mirathi (Sura 352 iliyorekebishwa Mwaka 2002) inamwajibisha wasii au msimamizi wa mirathi kwa matumizi mabaya au kuacha kutenda/kuchukua hatua kunakosababisha uharibifu wa mirathi. Hivyo, pale wasii au msimamizi wa mirathi anapotumia vibaya mali za marehemu, au akaiweka katika hatari ya kupotea au kuharibika, atapaswa kulipa hasara hiyo au uharibifu huo uliojitokeza. Pia, pale wasii au msimamizi wa mirathi anaposababisha hasara katika mali kwa kukataa kuijumuisha kama sehemu ya mali ya marehemu, atapaswa kulipa fidia. Kwa hiyo, inaweza kusemwa kwa uhakika kwamba kulingana na ukweli hapo juu, inaonekana mna sababu/hoja nzuri za kuchukua hatua dhidi ya msimamizi wa mirathi. Watu wachache sana wanajua jambo hili, kwamba watu waliochaguliwa kuwa wasimamizi wa mirathi wanapaswa kuelewa ya kwamba wanaweza kuwajibika kwa matendo yao.

# Sheria za Majengo, Ardhi na Mipango Miji

"

Kumiliki jengo au ardhi kunaambatana na haki na wajibu ambao hauwezi kubadilishwa kwa vitendo au hata kwa makubaliano. Haki ya kumiliki jengo/ardhi uliyonayo kisheria na haki ya kumiliki unayodhani unayo, siyo lazima zifanane.

## Mkataba wa pango kwa muda mrefu unachanganya

**Mimi na mwenye nyumba tuliingia kwenye mkataba wa upangaji mwaka 2009 kwa kipindi cha miaka 15 na utafika kikomo 2024. Hivi sasa tumegudua kuwa hati ya umiliki ina miaka 12 kufika ukomo yaani 2021. Je, inawezekana muda wa mkataba kuwa mrefu kuliko muda wa kwenye hati. Katika hali nyingine, kama mwenye nyumba anapokea kodi wakati amekwisha kunipatia notisi ya kusitisha mkataba, je, ninaweza kumbana mwenye nyumba kwa sababu amepokea kodi?**

*6 Agosti 2012*

Kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi, mmiliki wa ardhi anaweza kupangisha ardhi yake yote au sehemu yake kwa mtu mwingine kwa kipindi maalum au kwa kipindi chote cha maisha yake au ya mpangaji au kwa kipindi ambacho ingawa hakina ukomo upangaji unaweza kusitishwa na mpangaji au mpangishaji. Hata hivyo, kipindi cha juu kabisa cha mkataba wa upangaji ni siku kumi kabla ya ukomo wa mwisho wa umiliki wa ardhi.

Kutokana na maelezo hapo juu, mkataba wako hauwezi kutolewa kwa kipindi cha zaidi ya miaka 12 na chini ya siku 10 tangu siku ulipoingia kwenye mkataba huo. Unahitaji kuutafsiri upya mkataba na kujua nia yenu wakati mnaingia. Moja ya njia ni kukubaliana kuingia mkataba mwingine mdogo ili kurekebisha makosa hayo. Kama mpangishaji hatoi ushirikiano, na kwa kutegemea kanuni ya uharamu/ubatili, mkataba wenu unaweza kutangazwa kuwa ni wa miaka 12 na chini ya siku kumi. Lakini haiwezi kuzidi kipindi hicho kwa sababu sheria hairuhusu kitu kama hicho.

Kwa kukujibu swali lako la pili, Sheria ya Ardhi inatamka kwamba iwapo mpangaji ataendelea kuwepo kwenye ardhi bila idhini ya mpangishaji wakati mkataba wa upangaji umekoma au umekwisha muda wake, masharti yote ya upangaji kwenye mkataba yataendelea kumbana mpangaji hadi pale atakapoondoka kwenye ardhi. Sheria ya ardhi pia inaeleza kwamba kupokea kodi pekee kwa kipindi ambacho mkataba umesitishwa au umekoma, hakutachukuliwa kama mwenye nyumba ameridhia mpangaji kuendelea kuwepo kwenye upangaji au kwamba ameachia haki zake dhidi ya mpangaji aliyevunja masharti, isipokuwa kama mwenye nyumba ataendelea kupokea kodi kwa kipindi cha miezi miwili kutoka kwa mpangaji ambaye yupo kwenye ardhi yake baada ya mkataba kukoma, atachukuliwa kama ameingia mkataba wa kipindi maalum wa kila mwezi. Hivyo kupokea kodi hakumaanishi kwamba mkataba wa upangaji umeongezwa.

## Kununua ardhi Dar

**Naingia mkataba wa kununua kipande cha ardhi Dar. Ninawezaje kuendelea na nifanye nini?**

*30 Aprili 2012*

Kwanza, hakikisha unafanya uchunguzi wa kutosha kuhusu ardhi unayotaka kuinunua. Anza kwanza kwa kufanya upekuzi kwa Msajili wa Hati ili kuhakikisha muuzaji ni mmiliki halali na kwamba kiwanja akijawekwa kama dhamana, zuio au vikwazo vingine vilivyowekwa kwenye ardhi unayotaka kuinunua. Pili, hakikisha unapeleka hati halisi kutoka kwa Msajili wa Hati kwa ajili ya uchunguzi wa moja kwa moja. Kuna hati feki nyingi sana mitaani na unahitaji kuwa na uhakika wa hali ya juu kwamba hati uliyonayo ni halisi. Kwa kuwa ardhi haijaendelezwa, ni muhimu kwenda kwa Msajili kujiridhisha kwamba ardhi hiyo haina umiliki wa mtu zaidi ya mmoja. Ploti nyingi zina migogoro kwa sababu ya kugawawiwa zaidi ya mara moja na kesi zipo Mahakamani.

Tatu, siyo vibaya kuongea na majirani kumtambua muuzaji wako. Hakikisha

unashughulika na muuzaji au mwanasheria wake aliyemteua. Epuka pia kulipa pesa taslimu, kwa manunuzi pesa iwekwe kwenye akaunti ya benki ya muuzaji.

Baada ya kufanya uchunguzi wa kina kama ilivyoelezwa hapo juu, utatakiwa kuandaa mkataba wa mauziano pamoja na kujaza fomu maalum za ardhi. Andaa ripoti ya tathmini ya ardhi kwa ajili ya makadirio ya kodi ya ongezeko la mtaji ambayo kwa kawaida ni asilimia 10 inayolipwa na muuzaji, labda kama mtakubaliana vinginevyo. Pia kuna ushuru wa stempu wa asilimia 1 na ada ya usajili wa ardhi ambayo ni asilimia 0.25 ya thamani ya ardhi kama ilivyothibitishwa na mthamini wa serikali, ambayo inalipwa na mnunuzi. Yote kwa yote, kama yote hapo juu yamekamilika, mchakato siyo mgumu. Ni busara kupata huduma ya mwanasheria wako.

## Dhahabu kwenye bustani yangu

**Ni nini kitatokea kama ninachimba bustani yangu nakukuta dhahabu? Majirani zangu wanasema siyo yangu. Ardhi hii ni ya kwangu, nashangaa kwa nini dhahabu isiwe yangu. Tafadhali niongozeni.**

*28 Mei 2012*

Inaonekana kama ni hadithi lakini wakati mwingine hadithi huwa za kweli. Tuchukulie unakuta dhahabu na tunatumaini kuwa utapata dhahabu kweli, dhahabu hiyo haitakuwa ya kwako. Wewe unamiliki ardhi ya juu ya uso wa dunia na hauna haki yoyote juu ya kilichopo chini ya ardhi.

Kama unahisi kwamba unaweza kupata bahati ya kukuta dhahabu, unaweza kuomba leseni ya uchimbaji madini lakini iwapo utapewa leseni hiyo ama la ni suala jingine. Tunakushauri uwasiliane na mwanasheria wako ambaye atakuongoza kupitia vifungu vya Sheria ya Ardhi pamoja na Sheria ya Madini.

## Mkopo kabla ya kuhakiki dhamana

**Kwa nia njema benki yetu ilimkopesha mteja bila kukamilisha taratibu za dhamana ya ardhi ambayo haikusajiliwa. Hatukujua kwamba mkopaji alikusudia kutoweka na kiasi hicho kikubwa cha fedha. Sasa tumegundua kwamba hati aliyotupatia kwa ajili ya usajili ni ya zamani na alishanyang'anywa lakini inaonekana ni halisi kabisa. Tufanye nini? Mali bado ipo lakini ni ya mtu mwingine.**

*13 Agosti 2012*

Ni kanuni ya 101 ya benki kwamba usitoe mkopo bila kufanya uchunguzi. Kwa kuzingatia maelezo, wewe ni mdai/mkopeshaji usiye salama ambaye licha ya kufungua mashtaka ya jinai, unaweza kumshtaki ili kurudisha pesa yako kwa kuzishika mali zake kama zipo. Inawezekana pia mtu huyu alitumia jina la kugushi na hivyo mnaweza msimpate. Uzoefu wetu unaonesha kwamba mikopo ya namna hiyo inatolewa kwa kushirikiana na maafisa wenu. Mnaweza kufanya uchunguzi wa ndani zaidi. Kwa ujumla uwezekano wa kuzipata pesa zenu ni mdogo sana labda kama kuna dhamana nyingine mnazitegemea.

Tulitegemea angalau mngechukua hati halisi na kuipeleka kwa Msajili wa Nyaraka, Ofisi ya Wizara ya Ardhi, ili kuthibitisha kabla ya kutoa mkopo lakini inaonesha hamkufanya hivyo.

## Hati ya ardhi kwa miaka 99

**Hati yangu ya ardhi inatamka kwamba itakuwa halali kwa kipindi cha miaka 990 kuanzia mwaka 2005. Kwa kuamini hilo ninaiuza kwa kuwa hii ndiyo ardhi pekee ambayo imetolewa kwa kipindi kirefu hivyo. Wanunuzi wana wasiwasi kuhusu kipindi kilichotolewa. Nifanye nini?**

*25 Februari 2013*

Kwanza kabisa hati ya ardhi haitolewi kwa kipindi cha zaidi ya miaka 99. Kwa hiyo ama una hati bandia ama kuna makosa na inapaswa kusomeka miaka 99. Tunanakili kifungu cha 20 cha Sheria ya Ardhi ambacho kinatamka hivi: (1) Hati ya umiliki wa ardhi; (a) itatolewa na Rais; (b) kwenye ardhi ya jumla au iliyotengwa; (c) kwenye ardhi iliyopimwa; (d) inayotakiwa kusajiliwa chini ya Sheria ya Usajili wa Ardhi, kwamba ni halali na, kwa kuzingatia masharti ya Sheria hiyo na Sheria hii, haijabatilishwa; (e) kwa kipindi cha mpaka miaka 99; (f) kwa malipo; (g) kwa kodi ya mwaka ambayo inaweza kufanyiwa marekebisho mara kwa mara; (h) kwa mujibu wa masharti maalum; (j) inayoweza, kwa kuzingatia masharti ya Sheria hii, kunyang'anywa; (k) inayoweza, kwa malipo stahiki ya fidia kamili, kuchukuliwa kwa malengo ya umma. (2) Hati miliki ya ardhi haimpi mmiliki haki za maji kwenye ardhi hiyo isipokuwa kama haki hizo zimetamkwa wala haitampa mmiliki wake au mwakilishi wake haki yoyote ya migodi, madini, gesi au haki ya kuondoa nchini faida, au kwa malengo yoyote ya tafiti za aina yoyote za mimea na wanyama wa asili waliopo juu ya ardhi hiyo au mabaki ya mimea au wanyama au mabaki ya akiolojia yanayopatikana kwenye ardhi hiyo. Tunashauri upate ushauri wa mwanasheria wako ili kukuongoza zaidi.

## Kuingia bila idhini na haki ya kufidiwa

**Bosi wangu aliniachia ardhi yake niilinde na yeye akahamia nchi nyingine. Hakurudi kwa kipindi cha miaka 9 na wala hajawahi kuulizia kuhusu ardhi. Nilihisi labda haitaki tena ardhi hiyo, hivyo nikajenga nyumba na kuiendeleza ardhi hiyo kitu ambacho kilinigharimu fedha nyingi. Alikuja mwaka ulioisha na kuniambia niondoke. Nilimuomba anilipe fidia ya ile nyumba kwa sababu naamini ataipangisha. Alikataa akisema kwamba hakuniomba niijenge na kama ninaweza niondoke na nyumba yangu! Ni kweli hakuniambia nijenge lakini aliitelekeza ardhi hiyo na ninafikiri nastahili kulipwa fidia. Tafadhali nishauri iwapo kuna uwezekano wa kushinda shauri hili Mahakamani.**

*11 Machi 2013*

Chini ya sheria, wewe uliajiriwa na mmiliki wa ardhi kuilinda ardhi ili mtu mwingine asiingie bila idhini. Ulipokabidhiwa ulikuwa ni mkazi halali wa ardhi uliyeidhinishwa na mmiliki, hivyo ulikuwa mvamizi mara tu ulipoamua kuichukulia ardhi hiyo kama ya kwako. Ni kweli chini ya Sheria, mtu anaweza kunyanganywa ardhi yake kama mtu mwingine anaishi kwenye ardhi hiyo akiwa hamjui mmiliki na mmiliki haingilii kuwepo kwa mtu huyo kwenye ardhi kwa kipindi cha miaka kumi na mbili mfululizo.

Lakini, kwenye suala lako, ulikuwa unamjua mmiliki wa ardhi hiyo na yeye aliacha ardhi hiyo chini ya uangalizi wako, ikiwa na maana kwamba, alikuwa anaijali sana ardhi yake kiasi cha kumtafuta mlinzi ailinde dhidi ya wavamizi. Sababu tu kwamba hajaiulizia ardhi yake kwa miaka tisa, kitu ambacho ni ngumu kuamini japo inaweza kuwa kweli, haimaanishi kwamba amepoteza haki zake kisheria kwenye ardhi hiyo. Hivyo, ulipojenga nyumba ulijenga kwa gharama zako na hasara yako mwenyewe na hakuna uwezekano mmiliki anaweza kuwajibika kukulipa fidia. Unaweza kufikiria njia nyingine za mapatano ili kumshawishi bosi wako. Wanasheria wako wanaweza kukushauri zaidi.

## Kupangilia eneo na kubadilisha matumizi ya ardhi

**Nimekuwa nikitegemea ofisi ya manispaa iniandalie mpango wa kina wa eneo langu kwa miaka mitatu lakini hawajafanya hivyo hadi sasa. Je, kuna uwezekano wa mimi**

**kupangilia eneo langu? Pia nina hati kwenye kipande kingine cha ardhi. Je, ninaweza kubadilisha matumizi ya ardhi hiyo?**

*15 Aprili 2013*

Sheria ya Mipango Mjini inatamka kwamba, mmiliki wa ardhi anaweza kuandaa mpango mahususi wa ardhi yake bila kujali uwepo wa mpango wa jumla ulioandaliwa na mamlaka ya mipango miji isipokuwa kwamba mpango mahususi ni lazima uendane na mpango wa jumla. Hivyo ni muhimu mpango wa jumla uwepo kabla ya wewe kuandaa mpango wako mahususi. Mara baada ya kuandaliwa, ni lazima upelekwe kwenye mamlaka za mji au vijiji husika ili kupata idhini kabla ya kuendelea na utekelezaji wa mpango huo. Vile vile inawezekana kubadilisha matumizi ya ardhi kwa kupeleka maombi kwenye fomu iliyoandaliwa kwa ajili ya kubadili matumizi ya ardhi kwenye mamlaka ya mji au kijiji husika. Huwezi kubadilisha matumizi ya ardhi mpaka upate idhini ya maandishi kutoka kwa mamlaka husika.

## Muuzaji kufariki kabla ya uhamisho wa umiliki wa ardhi kukamilika

**Niliingia mkataba wa mauzo ya nyumba na mtu ambaye alifariki kabla sijafanikisha kuhamisha umiliki rasmi huko Wizara ya Ardhi. Nimearifiwa kwamba kuna fomu za kuhamisha ambazo ninatakiwa kuziwasilisha lakini muuzaji hayupo hai tena kuzisaini. Ni nani ninayeweza kumuomba azisaini kwa niaba ya marehemu?**

*17 Juni 2013*

Hujatuambia kama kuna hati za uthibitisho wa wosia au hati za usimamizi wa mirathi zilizotolewa na Mahakama kwa mtu kuhusiana na mirathi ya marehemu. Kama yupo basi mtu huyo “anavaa viatu vya marehemu” na atasaini fomu husika za uhamisho. Kama hakuna msimamizi wa mirathi, basi itabidi usubiri hadi ateuliwe. Kitu kingine ni kwamba, mauzo yako yanaweza kupingwa na wanufaika kama mali hiyo ipo kwenye wosia wa marehemu. Mwanasheria wako anaweza kukuongoza zaidi.

## Serikali kunishtaki baada ya miaka 20

**Nilikuwa mfanyakazi wa Serikali na nilikuwa nikiishi kwenye nyumba ya Serikali mwanzoni mwa miaka ya 80. Nilitakiwa kulipa kodi lakini miaka hiyo hakuna aliyekuwa anafuatilia kwa hiyo sikuwahi kulipa na niliendelea kuishi hapo mpaka nilipostaafu na kuhamia kwenye nyumba yangu. Cha kushangaza, Januari mwaka huu, nimepokea barua kutoka Serikalini ikinitaka kulipa kodi hiyo pamoja na riba. Sijui chochote kuhusu sheria lakini rafiki yangu ananiambia madeni kama hayo kwenye mikataba ukomo wake ni miaka sita wakati Serikali inadai baada miaka zaidi ya 20. Je, ninaweza kulipinga hili Mahakamani? Tafadhali niongoze kwa sababu sina fedha hiyo na nimeshakuwa mzee sana.**

*17 Juni 2013*

Tafadhali elewa kwamba chini ya Sheria ya Ukomo (wa Madai/Mashtaka), kesi za mikataba ukomo wake ni miaka sita tangu haki ya kushtaki ilipoanza; hata hivyo, ukomo wa kesi ya au dhidi ya Serikali ni miaka 60 na hivyo Serikali ipo ndani ya muda, na kama ulivyokiri, Serikali ina kila haki ya kudai kodi yake pamoja na riba. Tunakusihi sana uwasiliane na taasisi husika ya Serikali ili kuona namna ya kutatua suala hili nje ya Mahakama na kuandaa ratiba ya malipo ambayo yatakuwezesha kulipa kwa awamu njia ambayo itakuwa ni bora kwako. Elewa kwamba umetumia mali ya Serikali bila kulipa pango na haki pekee ni kwa Serikali kukushtaki kwa malimbikizo ya fedha. Wanasheria wako wanaweza kukuongoza zaidi.

## Hati kwa jina la kaka

**Ninamiliki ardhi yenye thamani kubwa huko mikoani. Hata hivyo niliinunua ardhi hiyo kwa jina la kaka yangu kwa sababu nilitaka aitunze. Kaka anajua fika kwamba ploti ni yangu lakini sina uhakika kama sheria inalitambua hilo. Nimeitaja ploti hii ya ardhi kwenye wosia wangu na mke wangu ndiye mnufaika. Tafadhali niongoze.**

*2 Septemba 2013*

Ikiwa ardhi ipo kwa jina la kaka yako, kama hakuna ushahidi mwingine wowote wa maandishi, ploti hiyo ni mali yake. Unachotakiwa kukifanya ni kuingia kwenye makubaliano ambayo yanatamka wazi juu ya hicho ulichokisema hapo juu. Unaweza pia kufikiria kupata hati ya uwakilishi kutoka kwa kaka yako, ambayo ni lazima isajiliwe, ambayo inakuruhusu wewe kutenda kwa niaba yake moja kwa moja. Unaweza pia kumsainisha nyaraka za uhamisho wa ploti hiyo kama unataka kuihamisha.

Umesema kwamba umeiweka ploti hiyo kwenye wosia, kama hakuna nyaraka yoyote rasmi kuonesha kwamba wewe ndiye mmiliki halali wa ploti hiyo, wosia huo hautawaokoa wanufaika wako endapo kaka yako ataidai kwamba ni ploti yake. Wanasheria wako wanaweza kukuongoza zaidi.

## Pango baada ya kufukuzwa

**Niliingia kwenye mkataba wa upangaji na mzee fulani kwa mwaka mmoja. Nimekuwa nikimlipa mwenye nyumba huyu kodi kwa kipindi cha miezi mitatu mitatu. Cha kushangaza, baadaye mwenye nyumba ameweka masharti mengi ambayo hayakuwepo kwenye mkataba. Miongoni mwayo ni kutokupika aina fulani ya chakula kwenye nyumba. Bila taarifa yoyote, kwenye mwezi wangu wa tisa wa kukaa, aliniondoa kwa nguvu kwenye nyumba kwa kigezo kwamba nimeshindwa kutii masharti yake mapya. Kwa kuepusha shari na baada ya kuonywa na majirani kuhusu mzee huyu mwenye sura ya kishirikina, nimetafuta sehemu nyingine ambayo sasa ninaishi. Kwa bahati mbaya mwenye nyumba wangu wa kwanza aliyenifukuza ananifuatilia ili kulipa kodi ya miezi mitatu ya upangaji ingawa sikukaa kwa miezi yote 12 kutokana na kufukuzwa. Pia anadai kwamba kufukuzwa kulitokana na mimi kushindwa kutii masharti na hivyo ninatakiwa nilipe deni hilo. Mzee huyo mwenye nyumba alimtuma mwenyekiti wa Baraza la Ardhi na Nyumba kuja na kuniarifu kwamba kiasi hicho kinatakiwa kilipwe. Je, nilipe? Tafadhali niongoze.**

*23 Septemba 2013*

Kisheria, mpangaji ambaye kinyume na vigezo na masharti ya wazi ama la, ya mkataba wa upangaji, anaondolewa kwenye nyumba/ardhi yote au sehemu ya nyumba/ardhi aliyopanga, hata wakati anaondolewa, hatawajibika kulipa kodi yoyote au fedha anayodaiwa kutokana na mkataba au kutekeleza ahadi wala masharti kwa upande wa mpangaji ama ya wazi ama la, yaliyopo kwenye mkataba kuhusiana na ardhi au jengo au sehemu yake ambayo ameondolewa. Hiki ndicho kinachozungumzwa kwenye Kifungu cha 110 (1) cha Sheria ya Ardhi (Sura 113 kama ilivyorekebishwa mwaka 2002).

Tuje kwenye maelezo yako, hatuoni wajibu wako wa kulipa kodi kwenye nyumba ambayo hukai. Mkataba uliacha kufanya kazi pale ulipoondolewa. Kutokana na maelezo uliyotupatia, ni mwenye nyumba ndiye aliyevunja mkataba kwa kukuondoa kinyume na sheria. Sababu kwamba mkataba ulikuwa ni wa miezi 12 haiwezi kuibuliwa sasa, hasa ukizingatiwa kwamba ulivunjwa kabla miezi 12 kuisha hivyo hutakiwi kulipa kodi ya miezi 3 iliyobaki. Kuhusiana na kutembelewa na Mwenyekiti, tafadhali elewa kwamba

maneno ya Mwenyekiti kwamba unatakiwa kulipa hayawezi kubadili msimamo wa sheria. Mwenyekiti anaweza kuwa na maslahi na jambo hili. Mwanasheria wako anaweza kukuongoza zaidi.

# Sheria ya Kodi na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA)

Imenenwa na wahenga kuwa hapa duniani, kifo na kodi ni mambo mawili pekee mwanadamu ana uhakika nayo. Kwa kuzingatia barua tunazozipata, labda tunapaswa kuongeza “migogoro ya kodi” kwenye hiyo orodha. Sheria za kodi ni ngumu sana na mara nyingi huwa ni chanzo cha malalamiko mengi. Baadhi ya malalamiko haya hasa hutokana na mkanganyiko halisi juu ya tafsiri ya sheria ya kodi na iwapo kodi husika inapaswa kulipwa. Lakini, mara nyingi, watu na makampuni wanataka tu kukwepa wajibu wao wa kulipa kodi. Hii inaweza kuwa mbinu hatari: kwani Mamlaka ya Mapato wanayo mamlaka ya kutosha ya kuchunguza viashiria vya kukwepa kodi, ikiwa ni pamoja na haki ya kuvamia biashara yenye mwenendo mbaya katika masuala ya kodi.

## Utozaji kodi kwenye mikopo ya elimu

**Nimechaguliwa kujiunga na chuo fulani nchini Tanzania na nimepata mkopo kutoka Bodi ya Mikopo ambayo inakopesha pesa kwa wanafunzi. Bado sijapokea malipo yangu ya kwanza, napenda kujua iwapo mkopo huo unapaswa kulipiwa kodi, na kiwango gani?**

*16 Januari 2012*

Kama ni mkopo wa elimu kwa mwanafunzi wa wakati wote (full time), hutatakiwa kulipa kodi. Hilo limeelezwa kwenye aya (i) ya Nyongeza ya 2 ya Sheria ya Kodi ya Mapato. Msamaha ni kwa ajili ya ada ya mafunzo kwa mwanafunzi, kwa muda wote anaopata mafunzo kwenye taasisi ya elimu, na kama utabadilisha hadhi kwa kusoma kwa muda wa ziada (part time), unaweza kutozwa kodi kulingana na maelezo ya mabadiliko husika.

## Kulipia theluthi kabla ya kesi kusikilizwa

**Mimi ni muuza vocha za simu Morogoro. Baada ya mijadala mirefu na Mamlaka ya Mapato Morogoro, wamenifanyia makadirio makubwa ya kodi isivyostahili, na wanadai VAT kwa miamala ambayo haitozwi kodi hizo. Kwa kuangalia tu ni wazi kuwa hakuna kodi inayostahili kulipwa lakini wameendelea na kunikadiria kodi hiyo. Mkaguzi wangu wa hesabu anasema tunaweza kulazimishwa kuweka angalau theluthi ya makadirio tuliyofanyiwa ili tuweze kukata rufaa juu ya jambo hili. Hii hainiingii akilini kwani hiyo theluthi ni kubwa mno kiasi cha kuweza hata kuiua/kuifilisi biashara yangu.**

*6 Februari 2012*

Sheria ya Rufaa za Kodi inazungumzia hilo kwamba mtu yeyote anayepinga makadirio ya kodi aliyofanyiwa anaweza kupinga makadirio hayo kwa kumpatia notisi ya maandishi Kamishna Mkuu. Notisi ya kupinga iwe na maelezo fasaha yanayoeleza sababu za kupinga makadirio hayo na yapelekwe kwa Kamishna Mkuu ndani ya siku thelatini tangu siku aliyopewa makadirio hayo.

Wakati pingamizi la kodi likitolewa, na wakati maamuzi ya mwisho ya makadirio ya Kamishna Mkuu yakisubiriwa chini ya kifungu cha 13, mtu anayepinga atalipa kiwango cha kodi kisichobishaniwa au theluthi ya kodi iliyokadiriwa, kinachozidi kingine ndicho kitalipwa.

Sheria inaeleza zaidi kuwa kama Kamishna Mkuu ataridhika kwamba kuna sababu za msingi za kupunguza kiasi au za kusamehe kiasi chote, Kamishna anaweza kuelekeza kiasi pungufu kilipwe au kiasi chote kisamehewe.

Kutokana na yaliyoelezwa hapo juu, ni wazi kuwa, ni lazima ukate rufaa juu ya makadirio hayo ndani ya siku 30 na uweke theluthi au ulipe kiasi ambacho hakibishaniwi, au chochote kinachozidi kingine. Hata hivyo, sheria inampa mamlaka Kamishna kupunguza theluthi au kusamehe baada ya kuridhika kwamba kuna sababu za msingi za kufanya hivyo. Sababu za ugumu wa maisha zinaweza kusikilizwa lakini ni lazima ziwe halisi. Mshauri wako wa masuala ya kodi anaweza kukuongoza zaidi.

## Utozaji kodi kwenye pesa za msaada

**Kwa miaka mingi nimekuwa nikiichangia taasisi ya msaada jijini Dar es Salaam ambayo Mamlaka ya Mapato Tanzania inasema imesajiliwa kimakosa. Nilikuwa mchangiaji mkubwa kwa maana ya bidhaa za chakula ambazo pia ninazisambaza sokoni na ndiyo biashara yangu kuu. Kwa sasa Mamlaka ya Mapato wamezuia misaada yote ambayo nimekuwa nikiitoa kwa miaka mitatu iliyopita wakidai kwamba ninatoa kupita kiasi. Swali la pili ni kama ninahamisha mali bure, sielewi kwa nini nilipe kodi? Tanzania ni nchi pekee ambayo**

**inadai kodi kwenye jambo kama hili. Kuna njia sahihi ya kutafsiri sheria?**

*19 Machi 2012*

Sheria ya Kodi ya Mapato ya mwaka 2004 inakuruhusu kuchangia kwenye taasisi za misaada lakini imezuia kiwango ambacho unaweza kukitoa kwenye taarifa zako za faida na hasara. Sheria inatamka wazi kwamba kwa madhumuni ya kukokotoa kipato cha mtu kwa mwaka wa mapato kwenye biashara, kutakuwa na punguzo la (a) kiasi kilichochangiwa kwenye mwaka wa mapato, kwenye taasisi za misaada au miradi ya maendeleo; (b) michango yoyote inayotolewa chini ya kifungu cha 12 cha Sheria ya Mfuko wa Elimu, 2001.

Sheria inaeleza pia kwenye kifungu kidogo cha 2 cha Sheria hii kwamba kiwango cha punguzo ambacho kinatolewa hapo juu kwenye mapato ya mwaka hakitazidi asilimia mbili ya kipato cha mtu kutoka kwenye biashara.

Kwa maelezo hayo, unaweza kuona kwamba sheria inakuruhusu kuchangia na kupunguza hadi asilimia mbili ya kipato chako. Kiasi chochote kinachotolewa msaada zaidi ya asilimia mbili kinaweza kutolewa lakini hakuna punguzo la kodi.

Swali lako la pili linafurahisha sana kwa maana kwamba ghafla unaamua kutoa mali zako kwa mtu bure huku ukitegemea hakutakuwa na kodi. Nia yako inaweza kuwa njema lakini Mamlaka ya Mapato haina namna ya kupima nia njema yako kwenye msaada huo. Hakuna kipimo cha mita ambacho kinaweza kuchomekwa mahala na kuangalia dhamira ya mtu anapotoa msaada. Hivyo sheria inasema wazi kwamba kama mtu anahamisha mali kwenda kwenye taasisi au anahamisha kwa mtu mwingine kama zawadi (a) mtu huyo ataonekana amepata kiasi sawa na thamani ya soko ya mali hiyo au thamani halisi ya mali hiyo kabla ya kupata; na (b) na mtu anayepata mali hiyo atachukuliwa kama inatokana na matumizi.

Ni dhana mbaya kudhani kuwa Tanzania ndiyo nchi pekee inayotoza kodi kwenye misaada. Tulijaribu kuangalia sheria za kodi za Uganda, Kenya, Afrika Kusini, India, Uingereza na Kanada. Sheria zote kutoka kwenye nchi hizi pia wanatoza kodi na nyingine zinatoza kodi kubwa sana kwenye misaada. Hivyo, madai kwamba Tanzania ni nchi pekee inayotoza kodi za namna hii si sahihi. Kodi ni muhimu kwa maendeleo ya taifa. Kama kodi za namna hii hazitatozwa, kila mmoja atadai anahamisha bure mali zake kwa marafiki, jamaa, binamu, n.k. ili kukwepa kulipa kodi. Ni wapi sasa mstari uchorwe? Kwa muongozo zaidi onana na mshauri wako wa masuala ya kodi.

## Nimetozwa kodi kubwa na mwajiri wa pili

**Nimeajiriwa na kampuni mbili na kila kampuni inajua kwamba nina kazi sehemu mbili, ingawaje nilipanga kufanya siri kwenye hii kazi ya sasa. Hata hivyo, wakati napokea mshahara wangu kwenye kazi hii ya pili, inaonesha kwamba mwajiri wangu wa pili amenitoza kodi kwa kiwango cha asilimia 30 ya mshahara wangu wakati kodi inayotakiwa kulipwa ni asilimia 19 tu. Je, hii ni sawa kunibebesha mzigo wa ziada wa kodi? Kuna njama kati ya mwajiri wangu na Mamlaka ya Mapato.**

*16 Aprili 2012*

Siyo Mamlaka ya Mapato wala mwajiri wako wa pili ambao wamekuibia isipokuwa sheria inamtaka mwajiri wako kukutoza kama alivyofanya. Kanuni za Kodi ya Mapato (Gazeti la Serikali Na. 464 la tarehe 5 Novemba, 2004) kanuni ya 18, inaeleza kwamba kama mwajiriwa ana mwajiri zaidi ya mmoja, ana wajibu wa kuchagua miongoni mwa waajiri wake ambaye atakuwa ni mwajiri

wake wa msingi na yule wa pili. Mwajiri wa kwanza atakata kodi kwa viwango vya kawaida vilivyotolewa chini ya Sheria ya Mapato. Mwajiri wa pili atawajibika kumkata mwajiriwa mshahara kwa kiwango cha juu kama ilivyotolewa kwenye Sheria ya Mapato ambayo ni asilimia 30.

Ukumbuke pia kwamba chini ya Sheria ya Mapato, ni kosa kuficha kazi yako kwa mwajiri wako wa kwanza na yule wa pili na ukitiwa hatiani utawajibika kulipa faini.

Hata hivyo, unaweza kuomba kwa Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato kupunguziwa kiwango hicho kwa sababu Sheria inamruhusu kupunguza kiwango hicho kama atajiridhisha kwamba makato hayo yanakuletea ugumu.

Nadharia yako ya kwamba mwajiri wako na Mamlaka ya Mapato wamekula njama si sahihi.

## Matatizo lukuki ya kodi

**Najikuta nipo kwenye matatizo kadhaa ya kodi. Kwanza, niliwekeza mamilioni ya Shilingi katika kutunza mazingira kwenye kiwanda changu lakini Mamlaka ya Mapato imekataa matumizi hayo yote kwa kusema hayakuwa ya lazima. Pili, kulikuwa na kuchelewa kulipa kodi. Mamlaka ya mapato hata ilikuwa haijui kuhusu hilo na kwa hiari yangu nilikwenda kulipa lakini mwishowe nikajikuta naambulia kutozwa riba na adhabu nyingine zote. Mwisho, mkaguzi wangu ambaye alinifanyia marekebisho ya akaunti ananiambia Mamlaka ya Mapato itanijia kwa marekebisho aliyoyafanya na anahitaji pesa zaidi ili aniwekee mambo sawa. Nimechanganyikiwa. Nifanye nini?**

*14 Mei 2012*

Tunakupa pole kuhusu matatizo yako ya kodi ingawa siyo magumu kama unavyofikiria. Tunaanza na matumizi ambayo unadai yamezuiliwa na Mamlaka ya Mapato kwa pesa ulizolipa kulinda mazingira. Hujasema hasa ulikuwa unalinda nini. Sheria ya Mapato iko wazi sana na inatamka kwamba kwa madhumuni ya kupiga mahesabu ya kipato halisi cha mwaka wa mapato wa biashara yoyote, kutakuwa na punguzo kwenye maendeleo ya kilimo, tafiti na maendeleo na matumizi ya kwenye mazingira kwa kiwango kilichotumiwa na mtu katika kipindi cha mwaka wa mapato wa biashara.

Sheria ya Kodi ya Mapato pia inatafsiri matumizi ya kimazingira kwamba ni kiwango ambacho kimetumiwa na mmiliki wa ardhi kuzuia mmomonyoko wa udongo; au kuhusiana na kurekebisha hasara yoyote iliyosababishwa na uchimbaji wa maliasili kwenye uso au eneo la ardhi.

Ili kufikia maamuzi yake, Mamlaka ya Mapato inahitaji kujua kama matumizi hayo ni ya lazima na iwapo yanahusiana na biashara husika. Una haki ya kuhoji kwa nini gharama zimezuiliwa na kama hujaridhika unaweza kukata rufaa kwa Kamishna Mkuu. Iwapo ulienda Mamlaka ya Mapato kwa hiari au siyo, watu wote wanachukuliwa kuwa wanajua sheria. Huwezi kuwalalamikia Mamlaka ya Mapato kwa kukutoza faini au kukulipisha riba kwa sababu ni sheria ndiyo inayotamka hivyo. Mamlaka ya mapato haiwezi kumfuatilia kila mtu na kila utekelezaji, hilo limeachwa kwa mtu mwenyewe na ni la lazima na ni kosa kushindwa kutii. Hoja yako kwamba Mamlaka ya Mapato isingejua pia haipo kwa sababu Mamlaka huwa inafanya ukaguzi wa makampuni mbalimbali mara kwa mara. Sheria iko wazi kwamba mtu yeyote ambaye anashindwa kulipa kodi wakati au kabla ya muda ambao kodi hiyo inatakiwa kulipwa atawajibika kulipa riba kwa kila mwezi au sehemu ya mwezi ambao kodi haikulipwa na itapigwa hesabu kwa kila mwezi ambao kodi haikulipwa.

Tunarudi kwenye sehemu ya mwisho ya swali lako ambapo inaonesha ama mkaguzi

wako ameandaa taarifa za akaunti yako isivyo halali au ameficha baadhi ya maelezo ili kukupunguzia wajibu. Unaonekana unatapeliwa na mkaguzi wako ili umlipe zaidi kukuwekea mambo sawa. Tunakujibu swali lako katika sehemu mbili. Awali ya yote, kama na wewe umeshiriki kwenye udanganyifu au ufichaji huu, na wewe utakuwa umetenda kosa ambalo linaweza kukufanya ulipe faini au ufungwe. Lakini, jambo hili haliishii hapa.

Itakuwa ni vyema kwako kumtaarifu mhasibu wako juu ya vifungu vya Sheria ya Mapato ambavyo vinatamka wazi kwamba mtu yeyote ambaye kwa kujua au kwa uzembe anasaidia, anaelekeza, anaficha au anamshawishi mtu mwingine kutenda kosa chini ya Sheria hii anatenda kosa na atawajibika, akitiwa hatiani (a) kama kosa la kwanza linahusu maelezo ambayo, kama taarifa zisizo sahihi za akaunti hazikugunduliwa, na ingepelekea kulipa kodi ndogo kuliko inayostahili ya kiasi kisichozidi Shilingi 500,000, atalipa faini isiyopungua Shilingi 500,000 na isiyozidi Shilingi 2,000,000, kifungo kisichopungua mwaka mmoja au vyote kwa pamoja; na (b) katika kesi nyingine yoyote, faini isiyopungua Shilingi 100,000 na isiyozidi Shilingi 500,000.

Kulingana na maelezo ya hapo juu unaweza kuona kwamba mkaguzi wako anaweza kwenda jela. Unaweza kumkumbusha juu ya wajibu wake wa kufanya kazi kwa uaminifu na kwa weledi na kwamba naye anaweza kutiwa hatiani. Wakaguzi wengi wanasahau kuhusu vifungu hivi vya Sheria ya Mapato lakini kwa sasa Mamlaka ya Mapato inawafuatilia kwa karibu wakaguzi na wahasibu katika utekelezaji wa majukumu yao.

## Uepukaji kodi dhidi ya ukwepaji kodi

**Nilifanya biashara ya kununua mali na nilifanya manunuzi katika namna ambayo sitawajibika kulipa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT). Mamlaka ya Mapato walikuja na kuniambia nakwepa kulipa kodi. Hata hivyo nilifanya hivyo kwa kutumia mwanya uliopo kwenye kifungu cha Sheria ya Ongezeko la Thamani. Hivi ni kweli huko ni kukwepa kodi ikiwa vifungu vya sheria vinaruhusu?**

*11 Juni 2012*

Suala lako ni moja ya masuala yanayojadiliwa sana, lile la uepukaji kodi dhidi ya ukwepaji kodi. Suala la uepukaji kodi na ukwepaji kodi ni la kawaida kwenye kila nchi inayotoza kodi. Wakati mazoea haya hayawezi kuisha, yanaweza kupunguzwa. Ulichokifanya ni kutafuta upenyo kwenye sheria za kodi na ukatumia udhaifu huo kupunguza au kutokulipa kodi kwenye mali ulizonunua.

Uepukaji kodi ni mbinu/mpangilio ambao mlipa kodi analipa kodi kidogo au halipi kodi kabisa lakini bila kuvunja sheria. Uepukaji kodi ni kunufaika na mianya au mapungufu katika sheria husika. Uepukaji kodi hauna adhabu karibu kwenye kila nchi inayotoza kodi. Hata hivyo kama shughuli ni haramu au siyo halisi, haiwezi kuchukuliwa kama ni sehemu ya kupanga kodi au ni njia halali ya kuepuka wajibu wa kulipa kodi.

Kwa upande mwingine, ukwepaji kodi ni kitendo cha makusudi cha mlipa kodi kukiuka sheria za kodi ili kupunguza au kuacha kabisa wajibu wa kulipa kodi. Ukwepaji kodi ni matumizi ya njia za udanganyifu ili kupunguza au kutokutimiza wajibu wa kulipa kodi.

Kwenye suala lako, inaweza kuwa ni suala la tafsiri ambapo Mamlaka ya Mapato wanaweza kulitolea ufafanuzi. Kama hujaridhika na maamuzi ya Mamlaka ya Mapato, unaweza kukata rufaa kwenda Bodi ya Rufaa za Kodi.

Mwisho ni lazima tueleze kwamba mtu anapaswa kuwa makini sana katika upangaji wa kodi kwa sababu kuna ugumu katika kutofautisha kati ya uepukaji kodi na ukwepaji

kodi.

## Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwa kampuni ya kigeni

**Nimekuwa mshauri wa kampuni ya kigeni kuhusu mradi fulani uliopo Arusha ambapo pia nimepewa mkataba mdogo kwa upande wa Kampuni ya Kenya. Swali langu lipo kwenye masuala ya kodi kwenye shughuli hizo. Moja, je, ninaweza kuandaa ankara na kodi ya ongezeko la thamani nikaiweka ndani yake? Kama ndiyo, kampuni ya kigeni inawezaje kurudishiwa kodi ya ongezeko la thamani? Je, mteja wangu anaweza kukata kodi ya zuio kwa kazi iliyofanyika Kenya?**

*13 Agosti 2012*

Kodi ya ongezeko la thamani inatumika pia kwenye ankara zako na mteja wako ni lazima alipe ankara pamoja na kodi hiyo kwenye ada. Kwa kuwa mteja wako hajasajiliwa nchini, hawezi kurudishiwa kodi hiyo kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania. Kuhusu swali lako la pili, kodi ya zuio haimhusu mteja wako kwa sababu wewe ndiye uliyeingia mkataba mdogo kwa kazi hiyo na siyo mteja wako. Hivyo kodi ya zuio ya asilimia 15 ya thamani ya jumla ya mkataba mdogo itatumika kwenye malipo yote unayopata kwenye kampuni kutoka Kenya.

## Nani anatakiwa kusajiliwa kulipa kodi ya ongezeko la thamani (VAT)

**Nina kampuni mpya nchini Tanzania na inawezekana kabisa nisitozwe kodi ya ongezeko la thamani kwa sababu nimejikita kwenye kusafirisha bidhaa ng'ambo. Je, bado ninahitaji kujisajili kwa ajili ya kodi ya ongezeko la thamani? Je, ni ipi mipaka ya kusajiliwa kulipa kodi ya ongezeko la thamani? Nini umuhimu wa mashine za risiti za kieletroniki? Je, ni lazima nizitumie? Na vipi kama nisipozitumia?**

*10 Septemba 2012*

Kodi ya ongezeko la thamani inatozwa kwenye bidhaa au huduma nchini Tanzania zinazostahili kutozwa kodi kwa mtu ambaye anastahili kutozwa kodi hiyo kwenye biashara anayoifanya. Kifungu cha 19 cha Sheria ya Ongezeko la Thamani kinatamka kwamba mtu yeyote ambaye mauzo yake ya mwaka yanazidi, au mtu huyo ana sababu za kuamini kuwa mauzo yake ya mwaka yanazidi kiwango kilichotolewa kwenye Kanuni chini ya kifungu hiki, kabla au baada ya tarehe 1 Januari 1998 atafanya maombi ya kusajiliwa ndani ya siku thelathini tangu siku aliyotakiwa kufanya maombi hayo.

Wafanyabiashara au biashara zote ambazo mapato yake kwa mwaka yanazidi milioni 40 (au Dola za marekani 25,000) au Shilingi milioni 10 (Dola za marekani 6,259) kwa kipindi cha miezi mitatu mfululizo wanatakiwa kupeleka maombi ya usajili kwa Kamishna wa Kodi za Ndani siku 30 tangu siku waliyostahili kulipa. Baadhi ya watu na taasisi nyingine zimesamehewa kulipa kodi ya ongezeko la thamani kwa bidhaa au huduma wanazoingiza, wakati baadhi ya bidhaa zimeondolewa kodi ya ongezeko la thamani. Kwa upande wako, utatakiwa kujisajili kama unapata kiwango kilicholezwa hapo juu. Kama huna bidhaa zinazostahili kodi ya ongezeko la thamani, unaweza kuomba kurejeshewa pesa yako.

Mashine za risiti za kieletroniki (EFD) ni mashine zilizotengenezwa kwa ajili ya kutumika katika biashara ili kudhibiti usimamizi kwa ufanisi katika maeneo ya uchambuzi wa mauzo na mfumo wa udhibiti wa mali. Mashine hizi zilianzishwa kwa ajili ya wafanyabiashara waliosajiliwa kulipa kodi ya ongezeko la thamani chini ya Kanuni mpya za Kodi ya Ongezeko la Thamani (Mashine za Risiti za Kielektroniki) za mwaka 2010 ambazo zilianza kutumika tarehe 1 Oktoba 2010 na kampuni ambazo zinashindwa kutumia mashine hizi zinaweza kutozwa faini au kufungiwa biashara zao.

Zaidi, Sheria ya Fedha ya Mwaka 2012

inaongeza matakwa ya kutumia mashine za risiti za kielektroniki kwa walipa kodi wote kwa kuzingatia Mamlaka ya Mapato, isipokuwa tu wale ambao Mamlaka ya Mapato imewaondolea sharti hilo. Sheria ya Fedha pia imeleta vifungu vya makosa vilivyopo kwenye Sheria ya Mapato kwa mtu anayeshindwa kuwa nayo au kutumia mashine za risiti za kielektroniki au anashindwa kutoa risiti za kielektroniki au ankara. Adhabu ya makosa hayo baada ya kutiwa hatiani ni faini ya Shilingi milioni tatu au jela kwa kipindi kisichozidi miaka mitatu. Hivyo kama umesajiliwa kulipa kodi ya ongezeko la thamani ni lazima utumie mashine za risiti za kielektroniki. Kama hutumii unaweza kuishia jela.

## Kodi dhidi ya mapato ya nje ya Tanzania

**Mimi ni mtanzania ninayeishi Dar es Salaam. Hivi karibuni nilinunua hisa kwenye kampuni ya Afrika Kusini ambapo nilianza kupokea gawio miezi michache iliyopita. Kwa kiasi fulani Mamlaka ya Mapato wamelishtukia hilo na kwa mshangao wakanifanyia makadirio. Kivipi na kwa nini nitozwe kodi kwa uwekezaji wangu nilioufanya Afrika Kusini? Inaonekana kama Mamlaka ya Mapato wana uwezo wa kuutoza kodi ulimwengu mzima na huu ni mpango wao wa kupata pesa za haraka. Tafadhali niongoze, mimi ni masikini sana na siwezi kuhimili jambo hili.**

*1 Oktoba 2012*

Kama unavyojua, Mamlaka ya Mapato watakufikia bila kujali wewe ni tajiri au masikini, na hoja yako kwamba wewe ni masikini haina mashiko. Sheria ya Mapato ya Tanzania inatamka kwamba kama mtu ni mkazi wa Tanzania ana wajibu wa kulipa kodi ya mapato bila kujali kama kipato hicho amekipata Tanzania ama kwingineko. Kwa kuwa wewe ni mtanzania na una kipato cha ndani na nje ya nchi, vipato vyote viwili vinatakiwa kutozwa kodi Tanzania. Kifungu hiki kina maana kwamba watanzania wote wana wajibu wa kulipia kodi kwenye mapato yao, siyo tu wakiwa Tanzania lakini pia wakiwa kokote ulimwenguni.

Hata hivyo, kuna fursa ambayo unaweza kuitumia kutegemea na aina ya kipato unachopata Afrika Kusini. Ni Mkataba wa Utozaji Kodi Mara Mbili uliopo kati ya Tanzania na Afrika ya Kusini. Huu unaweza kukusaidia na kuepusha mapato yako kutoka Afrika ya Kusini kutozwa tena kodi Tanzania kama tayari yameshatozwa Afrika ya Kusini. Mshauri wako wa kodi anaweza kukuongoza zaidi.

## Utata kwenye sheria ya kodi

**Kuna sheria moja ambayo ina utata wa namna ya kukadiria kodi na namna ya kukokotoa. Je, utata wa namna hiyo unawezaje kuamuliwa? Nifanye nini kwa sababu Mamlaka ya Mapato wanautumia utata huo kwa faida yao na wanasema wengine wamelipa kwa kigezo hicho hicho? Wananitisha kunifanyia makadirio. Tafadhali niongoze.**

*5 Novemba 2012*

Kwa kawaida kama kuna utata au mkanganyiko, faida ya utata huo anapewa mlipa kodi bila kujali kama wengine wamekubali kulipa ama la. Ukweli tu kwamba wengine wamelipa haiondoi utata kwenye sheria. Kanuni za kutafsiri kifungu kinachotoza kodi ni kwamba kabla ya kumtoza mtu kodi, ni lazima ioneshwe kwamba mlipaji anaangukia kwenye kifungu kinachotoza kodi kwa maneno ya wazi yaliyotumika kwenye kifungu hicho.

Kanuni muhimu ni kwamba hakuna mtu anayeweza kutozwa kodi kwa kudhania. Kama mtu hajaelezewa kwenye sheria ya kodi, hatakiwi kutozwa kodi kabisa. Kwa upande wako, inategemea utata huo ni upi. Kwenye

sheria za kodi hakuna mwanya wa sheria kujitafsiri yenyewe. Hakuna usawa kwenye kodi na hakuna kodi ya kudhania, hakuna kitu cha kuchukulia hivi hivi, mtu anapaswa kuangalia kwa umakini lugha iliyotumika.

Unaweza kuwazuia Mamlaka ya Mapato kufanya makadirio. Hata hivyo unahitaji kupinga makadirio kwa Kamishna Mkuu na kama hujaridhika na maamuzi yake, unaweza kukata rufaa kwenda Bodi ya Rufaa za Kodi na hatimaye Mahakama ya Rufaa. Kufanyiwa makadirio siyo mwisho wa dunia. Mwanasheria wako anaweza kukuongoza zaidi.

## Kesi ya kodi katika mahakama ya rufaa

**Tuna kesi ya kodi ambayo bado inaendelea Mahakama ya Rufaa. Mamlaka ya Mapato Tanzania imefanya tena makadirio ya kodi na kuleta mahesabu yale yale ambayo yamekatiwa rufaa lakini kwa mwaka tofauti. Tumepinga maamuzi haya ya pili Bodi ya Rufaa za Kodi. Je, kuna maana yoyote ya Bodi kuendelea kusikiliza rufaa hii wakati tunasubiria hukumu ya mwisho kutoka Mahakama ya Rufaa kwenye suala hilo hilo? Je, mamlaka ya mapato inaweza kufanya makadirio kwa kitu ambacho kinapingwa?**

*19 Novemba 2012*

Tunaanza kujibu swali lako la pili la iwapo Mamlaka ya Mapato inaweza kufanya makadirio kwa masuala ambayo tafsiri yake inasubiriwa Mahakama ya Rufaa. Kwa kusoma kwetu sheria za kodi, Mamlaka ya Mapato haizuiliwi kufanya makadirio hata kama kesi iko Mahakama ya Rufaa. Hivyo hatuoni tatizo lolote kwenye hilo.

Kuhusu suala la Bodi kusikiliza maamuzi ya pili ya Mamlaka ya Mapato, tafadhali elewa kwamba kuna maamuzi ya Bodi kuhusu suala kama hilo ambapo iliahirisha kesi iliyokuwa mbele yake kwa muda usioJulaikana kusubiri maamuzi ya Mahakama ya Rufaa.

Bodi ilitamka hivi kwenye maamuzi yake, "tuna maoni kwamba ni busara na akili tu ya kawaida kwamba usikilizwaji wa rufaa hii ya pili uahirishwe hadi pale ambapo Mahakama ya Rufaa ya Tanzania itakapotoa maamuzi ya rufaa iliyopo mbele yake ambapo pande zilizoko hapa na madai yanayobishaniwa ni yale yale kama yaliyopo hapa kwenye rufaa hii. Maamuzi yoyote yatakayotolewa kule, yanakwenda kufungua njia kwa umalizaji bora wa rufaa iliyopo mbele ya Bodi hii."

Kwa kuzingatia maamuzi hayo hapo juu, unaweza kufanya maombi ili suala ambalo lipo Bodi liahirishwe likisubiri rufaa inayoendelea.

## Mamlaka ya mapato kukataa rufaa

**Nimefanyiwa makadirio makubwa sana ya kodi ya ongezeko la thamani. Kimsingi kiwango ni kikubwa sana kiasi kwamba kama nikilazimishwa kulipa inaweza kupelekea kampuni yangu kufilisika. Niliwapelekea Mamlaka ya Mapato maombi ya kupinga makadirio hayo, na pia niliomba kusamehewa kuweka dhamana ya theluthi ya kiasi nilichokadiriwa. Mamlaka ya Mapato wamekuja juu wakikataa kunipa msahama huo na mimi sina pesa ya kulipa. Nifanye nini? Ninawezaje kuhukumiwa bila kusikilizwa eti kwa sababu tu sina pesa za kuweka dhamana ili kunisaidia kupambana na kesi yangu? Tafadhali niongoze.**

*19 Novemba 2012*

Umefuata taratibu sahihi kwa kufungua maombi ya kupinga makadirio kwa Kamishna Mkuu. Pia sheria inatamka kwamba mtu anatakiwa kulipa dhamana ya theluthi ya kiasi kilichokadiriwa au kiasi ambacho hakibishaniwi, chochote kinachozidi kingine. Kwenye kesi yako unapinga kabisa kiasi ulichokadiriwa na hivyo unatakiwa kulipa theluthi ya kiasi ulichokadiriwa. Umesema Mamlaka ya Mapato haijakubali maombi

yako ya msamaha. Njia inayofuata kwako ni kupeleka maombi ya msamaha kwenye Bodi ya Rufaa za Kodi. Kama kiasi hiki cha theluthi kikikubaliwa, utagundua kwa nini msamaha huu unaweza kupatikana kupitia Bodi.

Kama sababu ni ugumu wa mzunguko wa hela, mikopo mikubwa ya benki, rekodi nzuri ya ulipaji kodi wa kipindi cha nyuma, una nafasi kubwa ya kushinda rufaa. Hali ya sasa ya kifedha ya kampuni, miongoni mwa sababu nyingine, inaweza kutumika kukusaidia kupata msamaha. Unaweza pia kujenga hoja kuwa dhima ya sera ya serikali ni kusaidia na kukuza biashara na siyo kuzikwamisha. Aidha, unaweza kuwa na hoja kwamba kama utalazimishwa kulipa kiasi kikubwa hivi cha kodi utalazimika kufunga biashara, watu watapoteza kazi na Mamlaka ya Mapato pia itapoteza mapato. Wanasheria wako wanaweza kukuongoza zaidi.

## Kikokotozi kibovu chaniweka matatizoni na Mamlaka ya Mapato

**Nilinunua kikokotozi kwa muuzaji wa mtaani kwa ajili ya biashara yangu. Nilipoongeza asilimia 18 ya kodi ya ongezeko la thamani kikokotozi kinanipa idadi ndogo. Kwa mfano, kwa mauzo ya Shilingi 100,000, nilipoongeza asilimia 18 kwenye kiasi hiki ilitakiwa isome 118,000 lakini kikokotozi hiki kinanipa namba 116,000. Nilikipeleka kwa fundi ambaye alisema kwamba kikokotozi kina matatizo na asilimia 18 ilikuwa inakokotolewa kama asilimia 16. Je, hii ni sababu nzuri kwangu kuwaeleza Mamlaka ya Mapato ambao wananikadiria upungufu wa asilimia 2 ambayo kwa sasa imefikia Shilingi milioni 150? Ninaweza kumshtaki yeyote?**

*26 Novemba 2012*

Hii ndiyo mara yetu ya kwanza kusikia kuhusu kikokotozi hicho na inatuwia vigumu kuamini. Lakini kwa hali ya sasa ambapo kuna ongezeko la bidhaa zilizo chini ya kiwango sokoni, unaweza kuwa sahihi. Kwa kuanzia, hakuna uwezekano wa Mamlaka ya Mapato kukubali hoja yako. Unapofanya mauzo ya Shilingi 100,000 hata kwa mfanyabiashara ambaye hajavuka elimu ya msingi atajua kwamba kodi ya ongezeko la thamani ni Shilingi 18,000 na siyo 16,000. Pia tunashangaa kiasi cha asilimia 2 kimeongezeka mpaka kufikia Shilingi milioni 150 ikiwa na maana kwamba umetumia kikokotozi hicho kwa muda mrefu bila kugundua tatizo.

Kuhusu nani wa kumshtaki, unaweza kumshtaki muuzaji aliyekuuzia kikokotozi hiki. Hii inaweza isikupe matokeo unayoyataka. Unaweza pia kumshtaki mtengenezaji na msambazaji wa bidhaa hiyo. Inawezekana baadhi ya vikokotozi hapa mjini vinaweza kuwa vinaongeza kodi ya ongezeko la thamani zaidi na hivyo wafanyabiashara wakawa wanajinufaisha na ziada hiyo, hivyo unapaswa pia kuripoti kwenye Tume ya Ushindani, Shirika la Viwango Tanzania pamoja na Mamlaka ya Mapato Tanzania. Tunakushauri uwasiliane na mtaalam wa masuala ya kodi ili akuongoze zaidi kwenye suala lako la kodi ya ongezeko la thamani unalokabiliana nalo.

## Serikali haiheshimu makubaliano

**Tumeingia mikataba miwili na serikali kwa ajili ya ujenzi na uendeshaji wa mradi fulani. Huu ni mradi wa muda mrefu ambao unagharimu matrilioni ya Shilingi. Mkataba unaeleza wazi wajibu, vigezo na masharti ya kutimizwa na kila upande. Mkataba ulipitia hatua za kawaida ikiwemo kuchunguzwa na Mwanasheria Mkuu kabla ya kusainiwa na Waziri. Mamlaka ya Mapato Tanzania imeanza kututoza kodi kinyume kabisa na kile tulichokubalina na serikali wakidai kwamba sheria imebadilika na wao ni watekelezaji tu. Hivyo, ni jukumu letu kuwasiliana na**

**Wizara husika ili kutatua suala hili. Wizara inatoa ahadi lakini haitekelezi. Tufanye nini? Pia tunahitaji suluhu ya haraka. Je, kipengele cha utatuzi wa mgogoro kwa njia ya usuluhishi kitatusaidia kupata nafuu ya haraka? Inakatisha tamaa sana kuona serikali haiheshimu makubaliano iliyoingia yenyewe. Kwa nini Mamlaka ya Mapato kama mkusanya kodi ambaye ni mkono wa serikali isitatue jambo hili na Wizara badala ya kumtaka mwekezaji kufanya hivyo?**

*17 Desemba 2012*

Umeibua hoja muhimu sana. Kwanza sheria inabadilika na mabadiliko hayo hayawezi kuzuiwa na mkataba wenu. Kwa kukupa mfano wa vipengele vya mabadiliko ya kodi kwenye Mikataba ya Maendeleo ya Madini (MDA) na Mikataba ya Kugawana Uzalishaji iliyoingiwa baina ya serikali na makampuni, mikataba yote hii inatamka kwamba kama kutatokea mabadiliko ya sheria za kodi, serikali itatambua uwepo wa mikataba hii ili kuhakikisha kwamba mwekezaji anabaki kwenye hali yake ya awali kama ilivyokuwa kabla ya sheria hiyo kupitishwa. Kwa mfano, kama wakati wa kuingia mkataba wa kuwekeza kwenye madini au gesi, kampuni ikafanya tathmini yake ya viwango vya kodi za kampuni kuwa ni 30%, na sasa kiwango hicho cha kodi kimepanda mpaka 40%, ama marekebisho hayo ya sheria hayataihusu kampuni au serikali itaangalia namna nyingine ya kuifidia ili kuhakikisha kwamba kampuni inawajibika kulipa 30% tu ya mwanzo. Kwa ufupi, kwa kuzingatia Mikataba ya Maendeleo ya Madini (MDA) na Mikataba ya Kugawana Uzalishaji, kampuni itawajibika kulipa kodi ya asilimia 30 tu na siyo asilimia 40 hata kama sheria imebadilika.

Kwa upande wako, inaonekana kama una hali kama hiyo ambapo aina fulani za kodi hazikuwa sehemu ya makubaliano yenu na pia hazikuwepo wakati mnafanya makubaliano. Lakini sasa kuna mabadiliko ya sheria ambazo zimeanza kutumika na Mamlaka ya Mapato inakuja kukusanya kodi hizo kwako. Swali lako ni, je, serikali inatakiwa kuheshimu makubaliano yenu? Jibu letu ni ndiyo, ni lazima iheshimu. Serikali haina hiari bila kujali kama sheria inabadilika ama la. Kama sheria mpya haisemi kuhusu kuheshimu makubaliano ya namna hiyo yaliyofikiwa kabla ya sheria mpya, maana yake ni kwamba sheria mpya moja kwa moja haitatumika kwako, na hivyo serikali itawajibika moja kwa moja kwa mujibu wa makubaliano yenu.

Kwa mazingira hayo, tunakushauri ufuatilie suala hili Wizarani na kama juhudi zote zikishindikana, utatoa notisi ya uwepo wa mgogoro kwa mujibu wa mkataba. Mwishowe mtakwenda kwenye usuluhishi ambao tunaamini kwa maelezo machache haya una kesi nzuri. Iwapo unaweza kupata nafuu ya haraka kwenye usuluhishi, hatuna uhakika ni nafuu gani hasa unaitaka. Ingawa kuna kipengele cha usuluhishi ambacho kinapinga mamlaka ya Mahakama, kama nafuu unayoitaka ni ya haraka sana na ni ya muda mfupi, Mahakama inaweza kusikiliza ombi lako.

Kwa bahati mbaya hatuwezi kujibu swali la ndani ambalo umeliibua kwamba kwa nini Mamlaka ya Mapato wasilitatue kwa kushirikiana na Wizara. Hata hivyo, ni kweli Mamlaka ya Mapato wamekuwa wakisita kutatua masuala kama hayo labda ni kwa sababu haipo kwenye mamlaka yao kufanya hivyo kwa sababu Mamlaka ya Mapato hawatoi misamaha hiyo. Hii imepelekea kilio kikubwa kwamba sheria za kodi za Tanzania siyo imara, yaani hazitabiriki, na zimejikita katika kukamua kodi kutoka kwa makampuni machache bila kuongeza wigo wa vyanzo vingine vya kodi. Unaweza kupeleka suala hili kwenye Wizara husika.

## VAT katika ununuzi wa jengo

**Nilinunua mali/bidhaa kutoka kwa mtu binafsi kwa Shilingi milioni 500. Sikulipa ushuru wa ongezeko la thamani kwa kuwa sijasajiliwa kulipa ushuru huo wala muuzaji pia. Mamlaka ya Mapato wamekuja na kunitaka kulipa VAT kwenye mauziano/biashara hiyo. Je, VAT inalipwa kwenye mauziano/biashara kama hii?**

*7 Januari 2013*

Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani kifungu cha 4 kinatoa mawanda ya kodi ya ongezeko la thamani na kinatamka kwamba kodi hiyo itatozwa kwenye bidhaa au huduma kwa Tanzania Bara zinazostahili kutozwa kodi, kwa mtu ambaye anastahili kutozwa kodi hiyo katika shughuli ya kiuchumi anayofanya. Sheria inatamka pia kwamba kodi ya ongezeko la thamani inayotozwa kwenye bidhaa au huduma italipwa na mlipa kodi mwishoni mwa kipindi cha mwaka wa fedha kilichoamriwa au wakati wowote ambao Kamishna anaweza kuagiza. Kutokusajiliwa tu kulipa kodi ya ongezeko la thamani hakumaanishi kwamba hustahili kuilipa. Hata hivyo, inaonekana kama kodi ya ongezeko la thamani haikustahili kulipwa kwenye manunuzi/biashara hii kwa kuwa muuzaji alikuwa ni mtu binafsi na uwezekano ni mkubwa kwamba mauzo hayo ya jengo hayakuwa mwendelezo wa biashara inayofanywa na muuzaji. Kama inakuwa ni mwendelezo wa biashara yake, kwa mfano, anafanya biashara kwa jina binafsi, kodi ya ongezeko la thamani ilitakiwa kulipwa. Mshauri wako juu ya mambo ya kodi anaweza kukuongoza zaidi.

## Kodi ya lipa kadiri unavyopata (PAYE) kwenye posho

**Ikiwa ninapata mshahara wa Shilingi milioni 4 lakini haujumuishi posho yangu ya chakula cha mchana ya Shilingi 300,000, posho yangu ya usafiri ya Shilingi 600,000 na posho ya ada ya ziada ya mtoto wangu ya Shilingi 250,000 kila mwezi, ni kiasi gani nilipaswa kulipa kwenye kodi ya lipia kadiri unavyopata? Je, posho pia zimejumuishwa kwenye mahesabu?**

*21 Januari 2013*

Malipo yote, yawe ya fedha taslimu au vitu halisi, yanayolipwa na mwajiri kwa mfanyakazi ni lazima yakatwe kodi ya lipia kadiri unavyopata (PAYE). Kifungu cha 7 (1) cha Sheria ya Kodi ya Mapato, 2004, kinatamka kwamba mapato yote ya mtu yanayotokana na ajira kwa mwaka wa mapato yatakuwa ni mapato na faida ya mtu kutokana na ajira ya mtu kwa mwaka wa mapato. Kuna mambo fulani ambayo hayajahusishwa kwenye kifungu hiki. Sheria pia inatamka katika Kifungu kidogo cha (2) kwamba katika kukokotoa mapato ya mtu au faida zitokanazo na ajira kwa mwaka wa mapato, malipo yafuatayo yanayotolewa kwa au kwa niaba ya mtu binafsi na mwajiri au mshiriki wa mwajiri kwa kipindi cha mwaka wa mapato yatahushisha; (a) malipo ya ujira, mshahara, malipo ya likizo, ada, kamisheni, bonasi, kiinua mgongo au posho yoyote ya safari, burudani au malipo mengine yoyote yanayohusiana na ajira au huduma inayotolewa. (b) Malipo yanayoonesha msamaha au marejesho ya matumizi ya mtu binafsi au mtu mwingine anayehusiana na mtu huyo. (c) malipo kwa mkataba wa mtu binafsi katika masharti yoyote ya ajira (d) michango na malipo ya kustaafu.

Sheria hii katika Kifungu kidogo cha (3) inaondoa mambo yafuatayo kwenye hesabu ya mapato ya mtu binafsi au faida kutoka kwenye ajira: Kiasi kilichosamehewa na malipo ya mwisho ya zuio; Huduma za kafeteria zinazotolewa bila ubaguzi; posho yoyote ya kujikimu, safari, burudani au

posho nyingine zinazohusisha urudishaji wa gharama kwa mnufaika kwa kiwango chochote alichotumia na kisichohusiana na uzalishaji wa kipato chake katika ajira au huduma inayotolewa; faida inayotokana na matumizi ya chombo cha moto ambapo mwajiri hadai kufanya makato yoyote au nafuu kuhusiana na umiliki, matengenezo au uendeshaji wa chombo cha moto.

Ingawa mhasibu wako atakuongoza zaidi katika suala hili, ni maoni yetu kwamba posho hizi, ikiwa ni pamoja na posho ya chakula, zinalipiwa kodi. Unaweza kutolipa kodi ya posho ya gari, lakini inategemea ni nani anamiliki gari hilo na iwapo mwajiri wako anadai makato katika posho husika. Hatutafanya hesabu hapa, wasiliana na mhasibu wako kwa mwongozo zaidi.

## Msamaha wa kodi

**Nilipoanzisha kiwanda changu nchini Tanzania, Wizara ya Viwanda na Biashara ilitupatia barua kwamba kwa sababu ya uwekezaji mkubwa tuliokuwa tunaufanya, tunasamehewa kulipa kodi ya mapato kwa miaka 3 ya kwanza. Tunayo barua halisi lakini Mamlaka ya Mapato (TRA) inakataa ikidai kwamba haiutambui msamaha huo. Nifanye nini? Kwa nini taasisi mbalimbali nchini Tanzania zisiratibu shughuli hizo miongoni mwao? Katika hali ya mpito, Mamlaka ya Mapato inanilazimisha kulipa kodi – ninawezaje kushughulikia jambo hili?**

*4 Machi 2013*

Mamlaka ya Mapato ipo sahihi kwenye tafsiri ya sheria. Kifungu cha 10 cha Sheria ya Kodi ya Mapato kinaeleza waziwazi kwamba (1) Waziri wa Fedha anaweza, kwa amri iliyotolewa kwenye Gazeti la Serikali, kueleza (a) kwamba kipato au tabaka/aina fulani za vipato vilivyopatikana au kutoka Jamhuri ya Muungano vitasamehewa kodi kwa kiwango kilichoainaishwa kwenye amri hiyo; au (b) kwamba msamaha wowote chini ya Jedwali la Pili itaacha kutumika ama kwa ujumla au kwa kiwango ambacho kimetajwa kwenye amri hiyo. (2) Waziri anaweza, kwa amri, katika Gazeti la Serikali, kubadilisha, kutofautiana au kuweka upya Jedwali la Pili. (3) Licha ya sheria yoyote inayokwenda kinyume, hakuna msamaha utakaotolewa kwa kodi iliyotamkwa na Sheria hii na hakuna makubaliano ambayo yataathiri au kusababisha kuathiri matumizi ya Sheria hii, isipokuwa kama ilivyoelezwa na Sheria hii au kwa njia ya marekebisho ya Sheria hii.

Kutokana na maelezo hapo juu, ni dhahiri kuwa ni Waziri wa Fedha tu ambaye hutoa msamaha na sio Wizara yoyote, na msamaha huo lazima utangazwe kwenye Gazeti la Serikali kabla ya kuanza kutumika. Barua uliyonayo kutoka Wizara ya Viwanda na Biashara haiwezi kuidhinishwa na wala haijawahi kutangazwa kwenye Gazeti. Kwa hiyo inaweza kuwa ni kama nia/pendekezo la msamaha lakini haiwezi kusimama kama msamaha wenyewe. Tunakuomba ama uwasiliane na Wizara ya Viwanda na Biashara, na / au Kituo cha Uwekezaji Tanzania ili wairasimishe barua yako kuwa msamaha. Kama hutaki kusikia hili, huwezi kuwalaumu Mamlaka ya Mapato, kwani tafsiri yao ni sahihi.

Tunakubaliana na wewe kwamba kwa kurahisisha mchakato, ingekuwa ni bora kwa Wizara na Mamlaka ya Mapato kuratibu hili kwa ajili yako - hata hivyo njia hii inaweza kuchukua muda mrefu zaidi tofauti na kama wewe binafsi ungelifuatilia. Hata hivyo, ikiwa utaweza kuwasiliana na Wizara ya Viwanda na Biashara ili iingilie kati na kuiarifu Mamlaka ya Mapato kuhusu kurasimisha mchakato wa msamaha, Mamlaka inaweza kuchelewa kukusanya kodi hizo. Kumbuka pia kuwa Mamlaka ya Mapato inaweza isikubaliane na

hilo na unaweza kuishia kulipa kodi, baada ya kupewa msamaha, kodi iliyochukuliwa inaweza kurudishwa.

## Kusamehewa ushuru wa stempu

**Niliingia mkataba wa upangaji huko London kwa ajili ya jengo langu lililoko Dar. Je, ushuru wa stempu unalipwa na nani? Je, ni muda gani wa mwisho wa kulipa ushuru wa stempu na vipi kama Mamlaka ya Mapato wakichelewesha kufanya makadirio ya ushuru wa stempu kama upo? Je, ushuru wa stempu unaweza kusamehewa nchini Tanzania?**

*22 Aprili 2013*

Kwa kuwa makubaliano yanahusu jengo, yaani mali iliyopo nchini Tanzania, haijalishi mahala mlikosainia mkataba, ushuru wa stempu bado utahusika. Kwa mujibu wa Sheria ya Ushuru wa Stempu, isipokuwa kama pande zimekubaliana vinginevyo, mpangaji ndiye anayestahili kulipa ushuru huu ambao ni asilimia 1 ya kodi ya mwaka mzima.

Kuhusu wakati gani wa kulipa ushuru wa stempu, Sheria inatamka kwamba hati zote zinazolipiwa zilizotayarishwa na mtu yeyote Tanzania Bara zitawekwa stempu ndani ya siku 30 tangu kutayarishwa: Isipokuwa (a) kama hati hiyo ikiletwa kwa afisa husika kwa ajili ya maamuzi chini ya kifungu cha 42 cha Sheria hii ndani ya siku 30, muda wa kupeleka nyaraka hiyo kwa afisa husika mpaka kumtaarifu mtu aliyeipeleka kwa afisa husika kwa maamuzi, utaondolewa katika kuhesabu siku 30 hizo; na kila risiti, waraka wa kukiri deni, hati ya malipo, hati ya kubadilishana itawekwa stempu siku ya kusainiwa au siku ya kuandaliwa yoyote itakayoanza.

Kutokana na maelezo hapo juu, kama Mamlaka ya Mapato itachelewa kukadiria ushuru wa stempu, na kama ulipeleka nyaraka hizo kwa makadirio ndani ya siku 30 tangu kuandaliwa, muda ambao Mamlaka ya Mapato itautumia kufanya makadirio hautapigiwa mahesabu. Kwa kifupi, ni lazima upeleke nyaraka kwa makadirio ndani ya siku 30 tangu siku ya kuandaliwa vinginevyo utawajibika kwa adhabu.

Kuhusu misamaha, Sheria ya Ushuru wa Stempu ina kifungu ambacho kinampa Waziri mamlaka ya kusamehe malipo ya ushuru wa stempu. Kifungu hicho kinatamka kwamba Waziri anaweza, kwa amri itakayochapishwa kwenye Gazeti la Serikali, kuondoa hati yoyote inayostahili kulipiwa, au aina yoyote, daraja au maelezo ya hati hizo, kwenye malipo ya ushuru wa stempu.

Kifungu pia kinaruhusu msamaha wa kodi kurudi nyuma pale inapoeleza kwamba pale amri chini ya kifungu kidogo (1) imeelezwa kurudi nyuma, kila hati iliyoelezwa kwenye amri au kama kesi itakavyokuwa, hati yoyote ya aina, daraja au maelezo iliyoelezwa kwenye amri, na iliyotolewa, au iliyotekelezwa wakati au baada ya tarehe iliyotolewa kwenye amri itachukuliwa kama hati isiyotozwa.

Kwenye kesi yako, isipokuwa kama kuna sababu za msingi za kwa nini usamehewe kulipa ushuru wa stempu, hakuna uwezekano kwamba utapata msamaha. Pia, kumbuka kwamba, msamaha wa ushuru wa stempu ni lazima uchapishwe kwenye Gazeti la Serikali ili uweze kuwa na nguvu ya kisheria. Mshauri wako wa kodi anaweza kukuongoza zaidi.

## Tovuti ya Mamlaka ya Mapato inapotosha

**Niliitegemea Sheria ya Kodi ya Mapato iliyopo kwenye tovuti ya Mamlaka ya Mapato na kuingia kwenye biashara ya mabilioni ya Shilingi. Cha kushangaza vifungu viwili kati ya vitatu nilivyovitegemea vimebadilishwa miezi 12 iliyopita. Kwa nini tovuti ya Mamlaka ya Mapato haijasahihishwa vizuri na ni nini ninaweza kufanya sasa kwa kuwa niliiamini ? Je, ninaweza kuishtaki Mamlaka**

**ya Mapato? Afisa mmoja wa Mamlaka ya Mapato alisema kuwa ikiwa ni kosa lao, wataheshimu kile kilicho kwenye tovuti. Tafadhali niongoze kwa sababu suala hili linaniweka kwenye wakati mgumu sana.**

*6 Mei 2013*

Makosa kwenye tovuti ya Mamlaka ya Mapato hayawezi kutumika kubadilisha sheria. Kwa mfano, kama kiwango cha kodi ya mapato katika Sheria ya Kodi ya Mapato kilichopo kwenye tovuti ya Mamlaka ya Mapato kinatajwa kuwa 25% wakati kiuhalisia ni asilimia 30, sheria haitabadilika kwa sababu ya makosa ya tovuti ya Mamlaka ya Mapato.

Kama uliingia kwenye biashara ya mabilioni ya Shilingi, angalau ungemteua mshauri wa kodi. Kushindwa kwako kufanya hivyo kumepelekea wajibu huu. Tuna mashaka iwapo makosa ya tovuti ya Mamlaka ya Mapato yanaweza kukusaidia kushinda madai dhidi ya Mamlaka ya Mapato ingawa wanasheria wako wanaweza kukuongoza zaidi. Inashauriwa pia kwamba uwasilishe rasmi suala hili kwa Mamlaka ya Mapato na usubiri majibu yao. Ni kweli baada ya kusoma swali lako na sisi pia tulipitia Sheria ya Kodi ya Mapato ambayo imewekwa kwenye tovuti ya Mamlaka ya Mapato na kuna vifungu vingi vya zamani ambavyo bado vinaonekana mle. Hili linatia aibu sana kusema kweli. Tunatumaini barua yako kwa Mamlaka ya Mapato itasaidia juu ya hili. Ni bahati mbaya sana.

## Matokeo ya kodi katika kugawana gharama kwenye kutafuta mafuta

**Tunafikiria kutoa sehemu ya kipande cha kitalu chetu cha utafiti wa mali-asili chini ya utaratibu wa kugawana mavuno/mazao ili tuweze kumpata mwekezaji awekeze fedha kwenye eneo la mkataba kwa kuwa tuna uhaba wa fedha. Tunaambiwa kuna kodi ya mapato ambayo inapaswa kulipwa kutokana na hili. Je, tunahitaji kupata idhini kutoka mamlaka yoyote kwa ajili ya jambo hili? Kwa nini tufanye hivyo? Tafadhali tuongoze.**

*20 Mei 2013*

Kwa ujumla, kodi ya faida ya mtaji inakadiriwa kama kuna kipato au pale panapodhaniwa kuwa na mtaji. Kwenye mkataba wa kugawana gharama na hasara kwenye utafiti (Fifo), kwa kawaida wewe hupati kitu zaidi ya kutawanya hasara na kuwekeza mtaji ili ukusaidie kwenye shughuli za kiutafiti.

Ingawa si rahisi kwetu kukushauri kwa kusoma tu swali hili fupi, kwa ujumla makubaliano haya hayalipiwi kodi ya faida ya mtaji kwa kuwa hakuna unachokipata kwenye eneo ambalo halijagunduliwa kitu. Takwimu ziko wazi kwamba maeneo mengi ya kiutafiti hayafanikiwi. Hata hivyo, mkataba wa kugawana gharama na hasara kwenye utafiti na namna ya kukokotoa gharama za nyuma dhidi ya gharama zijazo na asilimia utakayoitumia dhidi ya kiasi ambacho utashirikiana ikiwa utafanikiwa siku za usoni ni muhimu kuzielewa kabla hatujakuongoza.

Kuhusu idhini, mkataba wa kugawana uzalishaji (PSA) unasimamiwa na Sheria ya Utafutaji na Uzalishaji Petroli, 1980 (PEPA). Kifungu cha 54 cha PEPA kinaweka masharti mapana ya kupata idhini ya Waziri kwa hati yoyote inayotengeneza maslahi ya kisheria au usawa, au inayoathiri, au inayotengeneza leseni, inayohamishwa, inayoathiriwa au inayoshughulikiwa. Kifungu hiki kinasema isipokuwa kama Waziri akiridhia (a) kuhamisha leseni; (b) hati yoyote inayotengeneza maslahi ya kisheria au usawa, au inayoathiri, au inayotengeneza leseni, inayohamishwa, inayoathiriwa au inayoshughulikiwa ama moja kwa moja au isiyo ya moja kwa moja, kuhamisha, au hati kama ilivyotolewa kwenye aya (b), haitakuwa na nguvu ya kisheria.

Kutokana na kifungu cha hapo juu,

inawezekana idhini ya Waziri wa Nishati na Madini ikahitajika kabla ya kuendelea na makubaliano. Ni kweli mmiliki wa leseni ni Shirika la Maendeleo ya Petroli na wewe ni mzabuni chini ya makubaliano ya kugawana uzalishaji; hata hivyo mkataba wa kugawana gharama na hasara kwenye utafiti una madhara kwenye mpango kazi na hivyo inashauriwa uziarifu na upate idhini kutoka Wizara na Shirika la Maendeleo ya Petroli. Kuhusu kwa nini upate idhini, jibu ni wazi kwamba sheria inakutaka ufanye hivyo. Wanasheria wako wanaweza kukuongoza zaidi.

## Ushuru wa stempu kwenye mkataba

**Mamlaka ya Mapato inanilazimisha kulipa ushuru wa stempu kwenye mkataba nilioingia wa kununua mfumo wa kutangazia umma (PA). Wanadai ni asilimia 1 ya thamani ya mfumo, kiasi ambacho ni kikubwa sana. Mhasibu wangu anasema hailipwi. Tafadhali niongoze.**

*12 Agosti 2013*

Mhasibu wako yuko sahihi kwamba ushuru wa stempu haulipwi kwa asilimia 1 ya fedha ya manunuzi ya mfumo wa kutangazia umma (PA). Sheria ya Ushuru wa Stempu ipo wazi kwamba kila hati iliyotamkwa kwenye Jedwali la Sheria hii na ambayo (a) imeandaliwa Tanzania Bara; au (b) kama imeandaliwa nje ya Tanzania Bara, inahusiana na mali yoyote iliyopo Tanzania Bara au jambo au kitu chochote kinachotakiwa kufanyika Tanzania Bara, italipiwa ushuru wa kiasi kilichoelezwa au kupigiwa hesabu katika namna iliyoelezwa kwenye Jedwali kuhusiana na hati hiyo. Makubaliano yako siyo sehemu ya Jedwali ambayo asilimia 1 ingetumika na hivyo hakuna ushuru wa stempu unaolipwa. Unatakiwa uwaoneshe kifungu hiki maofisa wa Mamlaka ya Mapato na uwasiliane na mwanasheria wako kwa mwongozo zaidi.

## Notisi ya uwakala wa Mamlaka ya Mapato

**Mimi ni mmoja wa walipa kodi watiifu wa sheria hapa nchini. Nimepewa notisi ya uwakala na Mamlaka ya Mapato wakiwa na nia ya kukata kiasi cha Shilingi milioni 600 kutoka kwenye malipo ya msambazaji/muuzaji wetu, wakidai kwamba hajalipa ushuru wa forodha na kodi ya ongezeko la thamani. Notisi ya uwakala ni nini? Vipi kama simdai chochote msambazaji/muuzaji? Mamlaka ya Mapato wanasema kwamba ninaweza kumkata kiasi hicho baadaye, lakini kwa sasa nilipe kiasi hicho kutoka kwenye fedha zangu. Tafadhali niongoze kwa sababu nipo kwenye shinikizo na Mamlaka ya Mapato wanatishia kuniadhibu.**

*11 Novemba 2013*

Uingizaji wa bidhaa nchini unasimamiwa na Sheria ya Usimamizi wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ("EACCM"), na Mamlaka ya Mapato wana haki ya kufanya kitu kinachoitwa ukaguzi wa baada ya uingizaji uliofanywa na muingizaji/muagizaji. Inaonekana kama muuzaji wako ameagiza bidhaa ambazo Mamlaka ya Mapato baada ya kufanya ukaguzi imegundua kwamba kiwango cha chini kilitangazwa ili kujipunguzia/kukwepa kodi. Notisi ya uwakala imetolewa kwako ili kama unadaiwa na muuzaji huyo, Mamlaka ya Mapato inataka uwasilishe fedha hizo kwa Mamlaka ili kufidia wajibu wa muuzaji. Kwa kifupi ni njia ya kurudisha fedha dhidi ya aliyekuuzia na siyo wewe.

Notisi ya uwakala hapo juu inasimamiwa na kifungu cha 131 cha Sheria ya Usimamizi wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ambacho kinatamka kwamba: (1) Kamishna anaweza, kwa notisi ya maandishi iliyoelekezwa kwa mtu yeyote (ambaye katika kifungu hiki ataitwa wakala) kumteua

mtu huyo kuwa wakala wa mtu mwingine (ambaye katika kifungu hiki ataitwa mhusika mkuu) kwa lengo la kukusanya kodi iliyoiva chini ya Sheria hii kutoka kwa mhusika mkuu iwapo Kamishna ameridhika kwamba wakala (a) anadaiwa au anataka kumlipa mhusika mkuu; (b) anashikilia fedha za au kwa niaba ya mhusika mkuu; (c) anashikilia fedha za mtu mwingine anayetaka kumlipa mhusika mkuu; (d) ana mamlaka kutoka kwa mtu mwingine ya kumlipa fedha mhusika mkuu; (e) anashikilia bidhaa zinazomilikiwa na mhusika mkuu ambazo zinatakiwa kulipiwa kodi na hazijalipiwa kodi, na Kamishna kwenye notisi ataeleza kiasi cha kodi kinachotakiwa kukusanywa na wakala, ambacho hakitazidi kiasi, au thamani ya bidhaa, zilizopo au anazodaiwa wakala na mhusika mkuu. (2) Kamishna anaweza, kwa notisi ya maandishi, kumtaka mtu yeyote kumpatia Kamishna ndani ya siku 30 tangu siku ya kupata notisi hiyo, taarifa zinazoonesha idadi ya fedha au bidhaa zinazoshilikiliwa na mtu huyo ambazo ni kodi iliyoiva chini ya Sheria hii. (3) Kifungu hiki kitatumika kwa wakala aliyeteuliwa kuwa kama wakala rasmi aliyeruhusiwa kutenda kwa niaba ya mmiliki. (4) Wakala aliyeteuliwa chini ya kifungu kidogo (1) na ambaye anadai kwamba hawezi kutekeleza notisi kwa sababu yoyote atamJulaisha Kamishna kwa maandishi akieleza sababu zake za kushindwa, na Kamishna anaweza kukubali, kurekebisha au kukataa taarifa hiyo kama ataona inafaa.

Kutokana na maelezo hapo juu, wewe ni wakala tu wa mlipa kodi na huhitaji kulipa kutoka kwenye mzunguko wa fedha zako. Hivyo kama hakuna deni, au una deni ambalo linabishaniwa, unatakiwa kuitaarifu Mamlaka ya Mapato na hawawezi kukulazimisha kutoa pesa kwenye mzunguko wako. Ni deni ambalo Mamlaka ya Mapato inamdai muuzaji wako na siyo wewe. Kama una malipo/ pesa ya muuzaji, hauna budi kutekeleza notisi ya uwakala vinginevyo utatozwa faini, utawajibishwa na hata kufungwa. Wanasheria wako wanaweza kukuongoza zaidi.

## Bei bila Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT)

**Huwa ninakwenda kwenye duka fulani ambalo baadhi ya bidhaa zake zina lebo zenye bei inayojumuisha kodi ya ongezeko la thamani (VAT) na lebo katika bidhaa nyingine hazijumuishi VAT wakati zinapaswa. Inachanganya sana. Je, hakuna sheria inayosimamia jambo hili? Nifanye nini?**

*11 Novemba 2013*

Sheria yetu ya Kodi ya Ongezeko la Thamani ina kifungu maalum kinachosimamia jambo hili, inaelezwa kwa uwazi kwenye kifungu cha 63. (1) Mtu yeyote anayetoa au anayechapisha tangazo kuhusiana na uuzaji wa bidhaa au huduma, kama tangazo linataja bei ambayo bidhaa au huduma hiyo inaweza kupatikana, atataja bei yenye kodi ndani yake. (2) Kwenye kifungu hiki, "tangazo" linahusisha lebo iliyobandikwa kwenye bidhaa na alama yoyote inayooneshwa kuhusiana na bidhaa au huduma na bei zake.

Hivyo lebo zote na matangazo ni lazima viwe na bei ambayo inahusisha kodi ya ongezeko la thamani ndani yake. Hakuna hiari kwa mwenye duka. Mamlaka ya Mapato ipo, kama mtu anavyotegemea mamlaka ya kodi kuwa makini sana kuhusu utekelezaji na tunakushauri uripoti juu ya jambo hili kwa Mamlaka ya Mapato ambayo itachukua hatua za haraka.

## Mikataba ya Serikali haitambuliki na Mamlaka ya Mapato

**Kuna mkataba tuliingia na Serikali ambao ulisainiwa na Wizara ya sekta husika. Kuna masharti mengi ya mkataba ambayo Mamlaka ya Mapato inatakiwa kuyatekeleza**

**lakini inasema bayana kuwa mkataba hauna nguvu ya kisheria, hivyo tuwasiliane na Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Hatuelewi kwa nini tuzunguke wakati tumekaribishwa kuja kuwekeza nchini Tanzania. Tunaweza kuishtaki Serikali?**

*18 Novemba 2013*

Hakuna sheria nchini Tanzania ambayo inakuzuia kuishtaki Serikali. Kwa bahati mbaya, hii sio mara ya kwanza tunasikia juu ya jambo hili ambapo Wizara husika inaingia mkataba, na Mamlaka ya Mapato ya Tanzania kwa masikitiko inakataa kutekeleza yaliyomo kwenye mkataba kwa misingi kwamba hayana nguvu ya sheria za kodi.

Kwa bahati mbaya, haujatuambia ni aina gani ya mkataba, na iwapo aina hiyo ya mkataba imeruhusiwa na sheria. Kwa ujumla, na ili kuhakikisha kwamba unanufaika na misamaha ya kodi chini ya mkataba, sheria husika ya kodi ni lazima ibadilishwe na mara nyingi kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali ili kuhakikisha kwamba misamaha ya kodi chini ya mkataba ina nguvu ya sheria.

Hata hivyo mara nyingi, Mamlaka ya Mapato imekuwa ikikataa mikataba ambayo tayari ina nguvu ya sheria na kukataa huko kwa Mamlaka ya Mapato kunaweza kupingwa.

Chaguo bora kwako ni kuwasiliana na Wizara ya Fedha ambayo itaingilia kati kwa kuwasiliana na Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na Mamlaka ya Mapato ili kulitatua tatizo hili.

Tunakubaliana na wewe kwamba Mamlaka ya Mapato inatakiwa kuisaidia Serikali kwa kulisimamia jambo hili kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha, njia ambayo ni rafiki kwa mwekezaji, japo kwa bahati mbaya jambo hilo mara nyingi halifanyiki kwa haraka.

Kama hautapata mlichokubaliana na Serikali chini ya mkataba wenu, unaweza kuendelea na kipengele cha utatuzi wa mgogoro na kuendelea ama kushtaki au kuwasilisha mgogoro kwenye usuluhishi. Wanasheria wako wanaweza kukuongoza zaidi.

## Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) baada ya kuuza biashara

**Niliuza biashara yote kwa kampuni nyingine ambayo imekuwa ikiiendesha tangu wakati huo. Mshauri wetu wa kodi alituambia kwamba hakuna kodi ya ongezeko la thamani ambayo inahusika. Kwenye ukaguzi wa hivi karibuni, Mamlaka ya Mapato inadai kodi ya ongezeko la thamani inayofikia mabilioni ya Shilingi kwa sababu wakati nauza biashara niliuza mali muhimu. Mamlaka ya Mapato inadai kwamba siyo ardhi bali mali yenyewe, ndiyo iliyostahili kuthaminishwa na kulipiwa kodi ya ongezeko la thamani. Je, nifanye nini?**

*2 Desemba 2013*

Wanachokisema Mamlaka ya Mapato ni kweli kwamba kodi ya ongezeko la thamani inalipwa kwenye mali iliyojengwa na siyo kwenye ardhi, na kwenye tathmini yako ni sehemu ya mali iliyojengwa ndiyo inayolipiwa kodi ya ongezeko la thamani. Hata hivyo, kutokana na maelezo yako mafupi hapo juu, tunaamini kwamba bado Mamlaka ya Mapato haiwezi kukulipisha kodi ya ongezeko la thamani kwenye hamisho hilo, kama alivyokueleza mtaalam wako wa kodi, kwa sababu biashara hiyo iliyohamishwa bado inaendelea kufanyika.

Kifungu cha 62 cha Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani kinatamka kwamba (1) iwapo biashara au sehemu ya biashara inauzwa, kwa madhumuni ya kuamua iwapo mnunuzi anastahili kusajiliwa, mauzo ya biashara yanayotozwa kodi au sehemu inayouzwa yataongezwa kwenye mauzo ya biashara yoyote inayofanywa na mtu ambaye ananunua biashara au sehemu ya biashara

hiyo (mnunuzi). (2) Wajibu wowote isipokuwa wajibu wa kijinai wa mtu anayeuza biashara au sehemu ya biashara, wakati au kuanzia siku ya mauzo hayo, utahamia kwa mnunuzi bila kuathiri wajibu wa muuzaji na wajibu huo ni pamoja na wajibu wa (a) kutunza, kuhifadhi, au kutoa rekodi au akaunti; (b) kutoa taarifa za kodi; au (c) kulipa kodi yoyote na riba chini ya Sheria; au (d) kutekeleza mahitaji maalum yaliyotolewa kuhusiana na biashara na Kamishna. (3) Hakuna kodi itakayotozwa au kudaiwa kuhusiana na mauzo kama mnunuzi amesajiliwa. (4) Isipokuwa kama Kamishna ameamua vinginevyo na baada ya maombi ya maandishi ya pande zote mbili stahiki zozote chini ya Sheria za deni au malipo ya kodi ambayo kabla ya mauzo kufanyika yalikuwa yalipwe na muuzaji, yatalipwa na yatakuwa yanastahili kulipwa na mnunuzi, na yatakoma kulipwa na muuzaji husika. (5) Mtu yeyote anayeshindwa kumJulaisha Kamishna kuhusu mauzo ndani ya siku 30 baada ya mauzo kufanyika atakuwa ametenda kosa na akikutwa na hatia atawajibika kulipa faini isiyozidi laki moja.

Kama una uhakika biashara hiyo inaendelea kufanyika kama ilivyokuwainaendeshwa wakati wa umiliki wako, inatafsiriwa kama ni endelevu na hakuna kodi ya ongezeko la thamani inayolipwa. Kwa mfano, biashara ya hoteli inauzwa huku ikiwa endelevu, yaani inaendelea kama hoteli, hapo kodi ya ongezeko la thamani haitatozwa kwenye mauzo. Hata hivyo, kama hoteli itabadilishwa kuwa vyumba vya kawaida vya kuishi, hapo biashara haichukuliwi kuwa endelevu na kodi ya ongezeko la thamani inahusika, na hivyo kifungu cha 62 hakitaepukika.

## Kanzidata ya magari ya Mamlaka ya Mapato ni onevu

**Niliagiza gari moja kwa moja kutoka nje ambalo nililinunua kwa mnada. Niliwasilisha kwa Mamlaka ya Mapato hati ya mnada ambao ulifanyika kwa njia ya mtandao pamoja na nyaraka nyingine zote za gari, umbali uliotembewa, bei ya kununulia na mwaka wa kutengenezwa. Pia niliwasilisha nyaraka za usafirishaji ikiwemo hati ya bima lakini bado Mamlaka ya Mapato walipandisha thamani ya gari langu kwa zaidi ya mara mbili wakidai kwamba kanzidata yao ina bei ya magari. Hawakutoa sababu zaidi kwenye njia yao bubu na walikuwa wakali sana walipokuwa wakishughulikia suala langu. Kila siku niliyochelewa kuchukua mzigo wangu nilikuwa nalipa gharama za kuchelewa kuchua mzigo pamoja na gharama za uhifadhi na mwishowe nikaishia kulipia ushuru wa uingizaji pamoja na kodi ya ongezeko la thamani japo kwa kupinga ili angalau nilikomboe gari. Gari nimeshalichukua lakini nataka kuiwajibisha Mamlaka ya Mapato kwa uonevu huu. Nifanye nini?**

*9 Desemba 2013*

Katika utafiti wetu ili kujibu swali hili, tumekutana na hukumu ambayo ina hoja kama za swali lako. Katika hukumu iliyosomwa na Bodi ya Rufaa za Kodi, Bodi haikuridhika na namna ya hiki kinachoitwa kanzidata kinavyofanya kazi na mapungufu yake. Ilieleza kwamba Mamlaka ya Mapato inaweza kutumia mfumo wa kanzidata uliowekwa kwa ajili ya kuamua ushuru wa forodha wa magari yanayoingizwa, lakini kwenye mazingira yanayostahili tu, ili Mamlaka ya Mapato iepuke maamuzi yasiyo na msingi. Bodi iliamua kwa kumpendelea mlipa kodi/mrufani na zaidi ikaeleza kwamba "kila kesi inatakiwa kuangaliwa na kuamuliwa kwa mujibu wa mazingira yake, vinginevyo itakuwa ni majanga kwa walipa kodi wasio na hatia kujumuishwa kwenye kundi la wakwepa kodi na kutoza kodi zisizo za msingi." Bodi kwenye kesi sawa na yako iliweka wazi kwamba kazidata inaweza kutumika lakini

siyo katika namna ambayo inakuwa kama mtambo unaowakandamiza walipa kodi.

Sheria ya Usimamizi wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki inatoa njia mbali mbali za makadirio na njia ya kufananisha ya kanzidata ni moja ya njia za makadirio ambayo ilikosolewa sana na Bodi kwenye maamuzi yake. Yote kwa yote, na kwa kutokuionea Mamlaka ya Mapato, hakuna upungufu wa waingizaji ambao wanapunguza sana thamani ya magari ili kukwepa kulipa ushuru wa uagizaji na kodi ya ongezeko la thamani. Mtu hawezi kuilaumu mamlaka ya Mapato kwa mashaka inayolazimika kuwa nayo hasa ukizingatia kwamba thamani ya magari pia ni ya kubadilikabadilika sana.

Kwa kuwa unaamini wazi kwamba hii ni bei halisi, na inashabihiana na gari nyingine, aina, na umbali/maili ambazo gari imetembea, una kesi nzuri ya kuiwasilisha kwenye Bodi ya Rufaa za Kodi. Kwa maamuzi yenye nguvu dhidi ya Mamlaka ya Mapato kwenye uonevu dhidi ya matumizi ya jumla ya mfumo wa kanzidata wa magari, una nafasi kubwa ya kufanikiwa. Mwanasheria wako anaweza kukuongoza zaidi.

## Shughuli rasmi nchini Tanzania

**Tunataka kuyahudumia baadhi ya makampuni nchini Tanzania lakini hatutaki kusajiliwa nchini kwa kuwa tutaishia kulipa kodi mara mbili. Je, kuna njia ambayo tunaweza kufanya kazi Tanzania bila kujisajili, kwa mfano kutoa huduma tukiwa nje ya nchi? Tunataka kupunguza mzigo wa kodi. Tafadhali tuongoze.**

*16 Desemba 2013*

Hujafafanua aina ya biashara unayotaka kuifanya nchini Tanzania, lakini kwa ujumla utatakiwa kujisajili hapa ili uweze kuendelea na shughuli zako ukiwa Tanzania. Unaweza ama kusajili taasisi mpya chini ya hati ya usajili au unasajili kama tawi la kampuni ya nje na unapewa Hati ya Utekelezaji (Certificate of Compliance).

Katika mlengo wa kikodi, taasisi ya kigeni ambayo haina ofisi kuu au mahala rasmi pa kufanyia shughuli za kiutawala nchini Tanzania inachukuliwa moja kwa moja kwamba inafanya shughuli inayostahili kutozwa kodi Tanzania, ikiwa tu ina shughuli rasmi nchini. Unachukuliwa kuwepo ikiwa unapofanya biashara kupitia wakala (kuepuka kusajiliwa nchini), au unatumia, au unafunga mitambo au mashine au unafanya shughuli za usimamizi wa ujenzi, uunganishaji, au ufungaji kwenye eneo kwa zaidi ya miezi sita.

Hivyo ni lazima ieleweke kwamba kama wafanyakazi wako au wawakilishi wako watakaa nchini kwa zaidi ya siku 183 kwa mwaka, hilo pia litachangia uwepo wao au uwezekano wa uwepo wako kwa madhumuni ya kodi nchini Tanzania. Dhana ya shughuli rasmi inajaribu kutatua hichohicho unachojaribu kukipata, yaani, kutokulipa kodi yoyote nchini Tanzania. Ni lazima pia tueleze kwamba Mamlaka ya Mapato inafuatilia sana mienendo hiyo unayokusudia kukwepa kulipa kodi za ndani. Mara unapobainika kuwa na shughuli rasmi, bila kujali umesajiliwa ama la, utatakiwa kulipa kodi za ndani. Mshauri wako wa kodi anaweza kukuongoza zaidi.

## Ukwepaji Kodi ya Ongezeko la Thamani pamoja na upekuzi

**Je, Maafisa wa Mamlaka ya Mapato (TRA) wana mamlaka ya kukagua kiasi na kiwango cha ubora wa bidhaa kwenye ghala langu? Wanahisi kwamba nakwepa kulipa kodi ya ongezeko la thamani. Je, huko si kuminya/kukandamiza haki yangu ya kufanya biashara Tanzania?**

*6 Januari 2014*

Hatujui ni kwa namna gani haki yako ya kufanya biashara itaingiliwa kwa TRA

kutaka kuthibitisha kiasi na ubora wa bidhaa zako. Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani imeeleza kwa uwazi juu ya jambo hili kwenye kifungu cha 39 ya kwamba (1) Kwa madhumuni ya kutekeleza mamlaka aliyopewa chini ya Sheria hii, afisa aliyeruhusiwa anaweza, wakati wowote unaofaa, kuingia kwenye jengo lolote ambalo ana sababu za kuamini kwamba linatumika kwa au linahusiana na shughuli za biashara, ikiwa ni pamoja na jengo linalotumika kuhifadhi bidhaa au nyaraka, na atakuwa na uhuru na haki ya kuingia ndani yake, kufungua kifungashio chochote, kukagua bidhaa zozote na kufanya vitu vyote ambavyo ni muhimu katika kutekeleza majukumu yake.

Kifungu cha 36 cha Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani kinamruhusu afisa wa TRA kuchukua sampuli. Kifungu hicho kinaeleza kwamba (1) kama afisa aliyeruhusiwa atakuwa na sababu za kuamini kwamba ni lazima kufanya hivyo ili kuokoa mapato, anaweza kuchukua, kutoka kwenye bidhaa zozote zinazomilikiwa na mtu yeyote anayeuza bidhaa au anayetoa huduma, sampuli kama itakuwa ni lazima katika kuamua namna ambayo bidhaa hizo au huduma inayotokana nazo zinavyoweza kushughulikiwa kwa madhumuni ya kodi. Kama TRA itachukua sampuli, ni lazima itoe risiti inayoeleza kwamba sampuli/bidhaa hizo zimechukuliwa na kama haitarudisha ndani ya muda muafaka, TRA itawajibika kukufidia.

## Kodi kwenye mkataba wa kugawana gharama kwenye utafutaji

**Kwenye mikataba ya mafuta na gesi, iwapo kampuni itasalimisha haki zake kwenye mkataba wa kugawana uzalishaji, mkataba halisi wa kugawana gharama kwenye utafutaji, je, mapatano haya yataathirije ulipaji wa kodi ya mapato? Je, kuna kanuni maalum za kodi zinazoongoza jambo hili? Mwongozo gani unaweza kutupatia?**

*3 Machi 2014*

Bado kuna mjadala kimataifa kuhusu athari ya kodi katika makubaliano ya kugawana gharama kwenye utafutaji wa mafuta na gesi (utafutaji). Kwa bahati mbaya hakuna mwongozo maalum wa namna makubaliano hayo yanatakiwa kutozwa kodi kwa kuwa kuna aina nyingi za mikataba ya kugawana gharama kwenye utafutaji, mingine ina madhara makubwa kwenye kodi na mingine kidogo. Kwa mfano, kampuni ambayo inatoa mkataba na ambayo haina uthibitisho wa uwepo wa akiba ya haidrokaboni na inayotoa mkataba wa utafutaji itakuwa na matokeo kidogo ya kodi tofauti na kampuni ambayo imegundua uwepo wa mafuta au gesi na inauza hata kama ni kwa asilimia ndogo. Kukadiria malipo kwenye mazingira kama hayo yasiyotabirika ni kitu kisichopimika na hivyo kusababisha migogoro mingi ya kodi kote ulimwenguni.

Hivyo, ni muhimu kukumbuka kwamba ni kitu halisi na siyo muundo wake ndicho kinachoamua matumizi ya sheria za kodi ya mapato ingawa kiuhalisia, kitu halisi kwenye muamala ndicho kinachofuata muundo unaotokana nacho. Kuna mikataba mingi ya kugawana hatari za utafutaji ikiwa ni pamoja na mikataba ya kawaida, upangishaji mdogo, mkataba usiogawanya maslahi, mkataba wa drafti, mkataba unaobeba maslahi, mkataba wa faida halisi, mkataba wa kurudia, n.k.

Kuepusha utata au tafsiri zenye utata, Sheria ya Kodi ya Mapato ya Tanzania kifungu cha 131 kinaruhusu maamuzi kwa suala binafsi ambapo mlipa kodi anaweza kuiuliza Mamlaka ya Mapato kabla/mapema kuhusu matokeo ya kodi kwenye shughuli fulani. Kifungu cha 131 kinatamka kwamba, Kamishna anaweza, iwapo mtu ameomba kwa maandishi, kumpatia mtu huyo, kwa

taarifa ya maandishi iliyotolewa kwa mtu huyo, maamuzi kwa suala binafsi yanayoeleza msimamo wa Kamishna kuhusu matumizi ya Sheria hii kwa mtu huyo kuhusiana na makubaliano/shughuli anayotakakufanya au anayofanya mtu huyo.

Tunashauri uombe maamuzi binafsi kwa suala hili chini ya kifungu cha 131. Kodi nyingine ambayo timu yako ya kodi inatakiwa kuizingatia ni ile Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye shughuli hiyo. Wanasheria wako wanaweza kukuongoza zaidi.

## 1% ya ushuru wa stempu

**Sisi ni wahusika katika mkataba fulani ambao tunajua unatakiwa kubandikwa stempu na kulipa asilimia 1 ya ushuru wa stempu. Hata hivyo, waraka huu ulisainiwa nje ya nchi na hatujui iwapo tunalipa adhabu kwa sababu mkataba wenyewe ulianza kufanya kazi siku 90 baadaye na tuliuleta Tanzania kwa ajili ya usajili baada ya wiki 5. Je, tunawajibika kulipa adhabu kwa kuwa nimeambiwa kwamba adhabu ni mara 10 ya kiasi cha ushuru wa stempu unaotakiwa kulipwa?**

*10 Machi 2014*

Kama madai yako ya waraka kusainiwa nje ya nchi ni ya kweli, basi kifungu cha 26 cha Sheria ya Ushuru wa Stempu kinaelezea juu ya jambo hili; kinaeleza kwamba hati zote zinazolipiwa zilizotayarishwa na mtu yeyote Tanzania Bara zitawekwa stempu ndani ya siku 30 tangu kutayarishwa: Isipokuwa (a) kama hati hiyo ikiletwa kwa afisa husika kwa ajili ya maamuzi chini ya kifungu cha 42 cha Sheria hii ndani ya siku 30, muda wa kupeleka waraka huo kwa afisa husika mpaka kumtaarifu mtu aliyeipeleka kwa afisa husika kwa maamuzi, utaondolewa katika kuhesabu siku hizo 30; na hati ya malipo na hawala inayolipwa kwa matakwa au siku zisizozidi 30 kutoka siku ya malipo ya papo hapo au siku ya kuiwasilisha itawekwa stempu ndani ya siku 7 tangu kuwasili Tanzania bara.

Hivyo tukichukulia kwamba waraka wako siyo hawala au hati ya malipo, ushuru wa stempu unalipwa tu pale waraka huo unapowasili nchini Tanzania. Tunaamini hakuna adhabu utakayolipa.

Vile vile taarifa kuhusu adhabu ya malipo ya ushuru wa stempu kwa kiasi fulani zimetiwa chumvi/zimekuzwa. Kulingana na maelezo machache uliyotupatia, tunaweza kusema, kwa kuwa wewe mwenyewe umekubali kuwasilisha waraka huu, na haukukamatwa, hivyo malipo ya adhabu mara 10 ya ushuru wa stempu haiwezi kuwepo. Mazungumzo ya kiungwana na Mamlaka ya Mapato yanaweza kutatua jambo hili. Mwanasheria wako anaweza kukuongoza zaidi.

## Kukosekana kwa sera ya bei kati ya kampuni-ndugu

**Sisi ni kampuni ya Tanzania na kampuni yetu mama ipo Ulaya. Changamoto kubwa tunayokumbana nayo ni kukosekana kwa sheria zinazosimamia biashara kati ya kampuni-ndugu/zinazohusiana, hasa kwa sababu kanuni hizi hazipo kwa sasa. Kwa kukosekana kwa kanuni hizi, tunaweza kufanya nini? Je, kuna maamuzi ya Mahakama juu ya jambo hili?**

*26 Mei 2014*

Kwa bahati nzuri wakati tunajibu swali hili, Kanuni za Kodi ya Mapato (Biashara kati ya Kampuni-ndugu) zimechapishwa wiki chache tu zilizopita. Kanuni hizi zimekwisha chapishwa kwenye Gazeti la Serikali na Waziri wa Fedha kwa mamlaka aliyopewa chini ya vifungu vya 33 na 129 vya Sheria ya Kodi ya Mapato ya mwaka 2004, na hivi sasa zimeanza kutumika. Kama utahitaji nakala unaweza kututumia barua-pepe kupitia info@fbattorneys.com na tunaweza kukutumia kwa njia hiyo ya mtandao.

Miongoni kwa kanuni nyingine, unaweza kujielekeza kwenye Kanuni ya 4(5) ambayo inatamka kwamba mtu atatozwa faini ya asilimia 100 (kutegemea na malipo ya chini ya kodi) iwapo anakiuka kanuni hii; kanuni ya 5 inabainisha taratibu za kufuatwa katika mahusiano ya kibiashara ya kampuni-ndugu; kanuni ya 9 inazungumzia tafsiri/matumizi ya kanuni hizi yaendane na yale ya Shirika la Ushirikiano wa Kiuchumi na Maendeleo (OECD)/Umoja wa Mataifa (UN). Hata hivyo, iwapo kutakuwa na ukinzani, Sheria ya Kodi ya Mapato na Kanuni hizi vitatumika. Kanuni ya 12 inazungumzia makubaliano ya gharama za awali za uhamisho ambayo yanaweza kufanyika baada ya kupata idhini kutoka Mamlaka ya Mapato. Mshauri wako wa kodi anaweza kukuongoza zaidi.

## Mamlaka ya Mapato (TRA) inakataa msamaha wa kodi

**Sisi ni wawekezaji wa kigeni na tumepewa misamaha mingi ya kodi na Wizara inayosimamia sekta husika ili kuendelea na mradi. Kuna vilio vingi kuhusu misamaha ya kodi lakini inaonesha watu wengi wanashindwa kuelewa kwamba Tanzania ni moja ya nchi nyingi zinazojaribu kuvutia wawekezaji, na hivyo wawekezaji makini wanahitaji motisha. Matumizi mabaya ya motisha yanafanywa na wawekezaji wasio makini ambao uwekezaji wao wote unategemea misamaha na ukwepaji kodi. TRA imekataa kutambua msamaha/ motisha yetu ikidai kuwa haina uhalali. Kuna gazeti la hivi karibuni lililokuwa na makala inayosema kuwa Serikali inataka kuondoa motisha zote, habari hii pia imetutia wasiwasi. Tafadhali tushauri nini cha kufanya.**

*2 Juni 2014*

Kuna masuala mengi umeyaibua kwenye swali lako. Inaonekana umeingia mkataba na Wizara fulani. Kwa bahati mbaya hujaitaja Wizara hiyo, lakini kama ni Wizara tofauti na Wizara ya Fedha, basi uwezekano ni kwamba, ingawa kuna mkataba unaokupa motisha, motisha hizo hazijarasimishwa na Wizara ya Fedha ili TRA izitambue. Ingawa unailaumu TRA, kumbuka yenyewe ni taasisi tu ya utekelezaji na haitoi motisha hizo. Tunashauri uwasiliane na Wizara husika, ambayo itawasiliana na Wizara ya Fedha kurasimisha motisha hizo ili uweze kunufaika nazo.

Iwapo Wizara husika haitarasimisha nafuu hizo, au Wizara ya Fedha ambayo ni sehemu ya Serikali kama ilivyo Wizara husika nayo ikikataa kutoa motisha, basi unaweza kuendelea na kipengele cha usuluhishi kilichopo kwenye Mkataba wako. Ni bahati mbaya kwamba hakuna kiunganishi kati ya Wizara husika, Wizara ya Fedha na TRA ili kukuwezesha kufurahia motisha. Suala hili limepelekea malalamiko mengi kuhusu mazingira ya uwekezaji nchini Tanzania, ambapo kwenye maandishi yanaonekana ni ya kuvutia sana, lakini kiuhalisia mazingira ni kikwazo kwa wawekezaji wengi.

Kuhusu kufuta motisha, hatujui ni makala ipi ya gazeti unayoizungumzia. Hata hivyo, kufuta motisha kunaweza kufanyika kupitia sheria pekee ambayo iliruhusu upewe motisha. Hakuwezi kuwa na ufutaji wa motisha wa jumla kwa sababu itakuwa ni hatari kwa uwekezaji na wawekezaji wenyewe. Tunaamini kwamba, motisha zinaweza kufutwa, lakini zile ambazo zilitolewa kupitia mikataba ambayo Serikali iliingia lazima iheshimiwe kutegemea na mkataba ulivyoandikwa. Mikataba mingi ina vipengele vya uimara wa kodi, ambayo ina maana kwamba unaweza kuishtaki Serikali kudai fidia kutokana na usumbufu/hasara uliyoipata kwa motisha kuondolewa.

Ni lazima ukumbuke kwamba sheria haifutwi na mikataba. Tunamaanisha kwamba sheria kuhusu motisha zinaweza kubadilika, na utaishia kulipa kodi; lakini mkataba

ulioingia, kutegemea na maneno yake, bado utaendelea kuwa halali na kukuruhusu kuishtaki Serikali kudai fidia kwa hasara utakayoipata kutokana na kuondolewa motisha. Iwapo motisha itaondolewa bila kulipa fidia, fidia ambayo Serikali itailipa itazidi kodi ya ziada uliyoitoa kwa kufuta motisha hiyo. Kuna kesi nyingi kwenye nchi nyingi jirani ambapo vitendo vya Serikali vilikuwa na madhara kwa Serikali yenyewe na tuna uhakika mamlaka za nchini Tanzania zitakuwa makini juu ya jambo hili. Mshauri wako wa kodi na wanasheria wako wanaweza kukuongoza zaidi.

## Kukiuka masharti ya malipo ya kodi kwenye PSA

**Kampuni yetu imeingia kwenye Mkataba wa Kugawana Uzalishaji (PSA) na Serikali ambapo Serikali imebadilisha sharti/kipengele cha kutobadili kodi. Huu ni uvunjifu wa wazi wa masharti ya kwenye mkataba. Je, tunaweza kuishtaki Mamlaka ya Mapato (TRA) katika Mahakama ipi kwa kutokuheshimu mkataba?**

*16 Juni 2014*

Mkataba (PSA) ulikuwa baina ya Wizara ya Nishati na Madini, Shirika la Maendeleo ya Petroli (TPDC) pamoja na kampuni ya uchimbaji. TRA haikuwa sehemu ya makubaliano hayo na hivyo haiwezi kushtakiwa katika mazingira hayo.

Inawezekana mkataba una kipengele cha usuluhishi ambacho unaweza kukitumia na kudai fidia kutoka Serikalini kwa hasara na/au gharama za ziada ulizozipata kutokana na mabadiliko ya kodi. Kama mkataba hauna kipengele cha usuluhishi unaweza kuishtaki Serikali Mahakama Kuu. Hata hivyo, kabla ya kuishtaki Serikali, chini ya Sheria ya Mwenendo wa Kesi Dhidi ya Serikali unatakiwa kutoa taarifa ya siku 90. Hata hivyo, taarifa hiyo haitumiki iwapo kuna kipengele cha usuluhishi.

Zaidi ya hayo, kipengele cha kodi kwenye mkataba hakimaanishi kwamba sheria za kodi haziwezi kubadilishwa. Lakini, wakati huo huo, Serikali ni lazima iheshimu mikataba iliyoingia na haki yako ya usuluhishi au ya kuomba Mahakama kuingilia kati inabaki pale pale. Serikali pia imeridhia mikataba mbalimbali ya kimataifa ya usulihishi, na kulingana na maelezo uliyotupatia, tunaamini una kesi nzuri.

## Mamlaka ya Mapato (TRA) inanitishia kulipa theluthi

**Kuna maafisa wa TRA ambao wanatishia kuifungia biashara yangu kama sitaongea nao. Wanadai kwamba mara watakaponitaarifu wajibu wangu wa kulipa kodi, nitatakiwa kulipa kwanza theluthi ya fedha hizo ndo niweze kupinga/kukata rufaa. Wanasema kwa kuwa siwapi ushirikiano, wameniongezea mara nne zaidi ya wajibu wangu wa kodi wa awali ili nishindwe kulipa theluthi yake. Wana makusudi sana. Nifanye nini?**

*14 Julai 2014*

Kwanza kabisa, theluthi inatumika kwenye makadirio ya kodi na si vinginevyo. Kwa kawaida makadirio yanafanyika kwenye kodi za mapato na kodi za ongezeko la thamani. Hivyo, unahitaji kuangalia iwapo wajibu huo wa kodi unaingia kwenye mojawapo ya vitu hivi. Kama siyo, kwa mfano suala lako linajikita kwenye ushuru wa stempu au kodi ya zuio, haya yote siyo makadirio na kwa hiyo vifungu vinavyohusu theluthi havitumiki.

Kifungu cha 12 cha Sheria ya Rufaa za Kodi kinashughulika na jambo hili na kinaeleza kwamba (1) mtu yeyote anayepinga makadirio ya kodi aliyofanyiwa, kwa kutoa taarifa ya maandishi kwenda kwa Kamishna Mkuu, anaweza kupinga makadirio hayo. (2) Taarifa ya pingamizi itakuwa na maelezo

fasaha yanayoeleza sababu za pingamizi la makadirio hayo na yatapelekwa kwa Kamishna Mkuu ndani ya siku thelatini tangu siku ya kupewa makadirio hayo. (3) Wakati pingamizi la makadirio likitolewa, na wakati maamuzi ya mwisho ya makadirio ya Kamishna Mkuu yakisubiriwa chini ya kifungu cha 13, mtu anayepinga atalipa kiwango cha kodi kisichobishaniwa au theluthi ya kodi iliyokadiriwa, chochote kinachozidi. (4) Iwapo Kamishna Mkuu ameridhika kwamba kuna sababu za msingi za kupunguza au kusamehe masharti ya kifungu kidogo (3) anaweza kuelekeza kiasi cha chini zaidi kilipwe au kusamehe. (5) Baada ya kupata taarifa ya pingamizi, Kamishna Mkuu anaweza (a) kupokea taarifa ya pingamizi la makadirio ya kodi; au (b) kupinga kupokea taarifa ya makadirio ya kodi. (6) Kamishna Mkuu atakataa kupokea taarifa ya pingamizi la makadirio ya kodi kama (a) Taarifa haiendani na matakwa ya kifungu kidogo cha (1), (2) au (3); (b) Taarifa haielezi suala lolote la kisheria au lakiuhalisia kuhusiana na makadirio; (c) nafuu inayo ombwa haiwezi kutolewa kisheria wala kiusawa; (d) ombi limeletwa nje ya muda; au (e) pingamizi halina mashiko. (7) Iwapo Kamishna Mkuu ameridhika kwamba kwa sababu za kutokuwepo nchini, ugonjwa au sababu nyingine za msingi, mtu anayepinga makadirio ameshindwa kuleta pingamizi ndani ya muda uliowekwa, anaweza baada ya kuombwa na mtu huyo, na yeye mwenyewe kujiridhisha na matakwa ya kifungu kidogo cha (2) au, kama itakavyokuwa, kifungu kidogo cha (3), atapokea taarifa hiyo nje ya muda ulioruhusiwa na taarifa iliyopokelewa itakuwa halali kana kwamba ililetwa ndani ya muda muafaka. (8) Mtu yeyote ambaye hajaridhika na maanuzi ya Kamishna Mkuu ya kukataa kupokea taarifa ya pingamizi, anaweza, baada ya kumpatia Kamishna Mkuu kiasi cha fedha kilichokadiriwa ambacho hakibishaniwi au theluthi ya kiasi kiasi kilichokadiriwa, chochote kinachozidi kingine, pamoja na riba iliyotokana na kuchelewa kulipa wakati wa kutoa taarifa ya pingamizi, kukata rufaa kwenda Bodi dhidi ya kukataliwa na maamuzi ya Bodi iwapo Kamishna Mkuu apokee au asipokee yatakuwa ni ya mwisho.

Hivyo basi, theluthi inaweza kusamehewa kama utatoa sababu za msingi. Sababu ambazo zinaweza kukubaliwa na TRA ni pamoja na kampuni kuwa na mtaji mdogo, haijaanza kupata faida, haijaanza kuzalisha mapato, inakaribia kufilisika n.k. Mshauri wako wa kodi anaweza kukuongoza zaidi.

## Mamlaka ya Mapato kushindwa kutoa uamuzi binafsi

**Tunafanya shughuli fulani ambapo Sheria ya Kodi ya Mapato ina utata. Mshauri wetu wa kodi alisema tuombe Uamuzi Binafsi (Private Ruling) juu ya suala hili, ili TRA itoe maamuzi ya awali na hivyo kuepuka matatizo yoyote baadaye. Tuliipatia TRA taarifa zote na sasa yapata miezi 18 TRA haijajibu chochote. Mamlaka ya Mapato haijatoa sababu zozote za kutokujibu ombi letu kuhusu uamuzi binafsi. Je, ninaweza kumshtaki mshauri wangu wa kodi kwa kuchelewesha biashara? Ninaweza kufanya kitu gani zaidi?**

*11 Agosti 2014*

Mshauri wako wa kodi hajakosea chochote na tunaamini hamuwezi kumshtaki. Tunashauri muwakumbushe TRA mara ya mwisho na kama wakiendelea kukaa kimya mnaweza, ingawa inaweza kuwa ni mara ya kwanza kwa maombi kama hayo, kupeleka rufaa kwenda Bodi ya Rufaa za Kodi ambayo inaweza kuiamuru TRA kutoka maamuzi ndani ya muda fulani. Sheria ya Rufaa za Kodi inakuruhusu kufungua maombi na rufaa kama hizo mbele ya Bodi ya Rufaa za Kodi

moja kwa moja, hasa kama TRA wako kimya.

## Kuipa taarifa Mamlaka ya Mapato (TRA)

**TRA wamekuwa wakiniomba taarifa kuhusu mwenendo wa biashara zangu. Niliwapa lakini bado wamenivamia. Haki zangu ni zipi? Na je, ninaweza kuwapa TRA taarifa kwa mtindo huu? Biashara yangu ni safi – je, ninaweza kuwakatalia TRA? Je, taarifa hizi hufanywa siri?**

*18 Agosti 2014*

Sheria ya Kodi ya Mapato inawapa Maafisa wa TRA mamlaka mapana ya kufanya upekuzi wa aina hiyo. Kifungu cha 138 kinaeleza kwamba (1) Kwa malengo ya kutekeleza Sheria hii, Kamishna pamoja na afisa yeyote aliyeruhusiwa kwa maandishi na Kamishna (a) atakuwa na mamlaka (i) wakati wote wa siku kuanzia saa tatu asubuhi mpaka saa kumi na mbili jioni bila taarifa yoyote; na (ii) wakati mwingine wowote utakaoruhusiwa kwenye hati ya upekuzi iliyotolewa na hakimu wa Mahakama ya Wilaya au ya Hakimu Mkazi, kuingia kwa uhuru kwenye jengo, eneo, kupekua nyaraka au mali nyingine yoyote; (b) kutoa nakala, ikiwa ni pamoja na nakala ya kielektroniki, nakala yoyote ambayo ruhusa imepatikana chini ya aya ya (a); na (c) kukamata nyaraka yoyote ambayo, kwa maoni ya Kamishna au afisa aliyeruhusiwa, itakuwa ni ushahidi muhimu katika kutoa maamuzi juu ya kodi kuhusu mtu yeyote chini ya Sheria hii; na (d) anaweza, kama waraka haupo au nakala haijapatikana baada ya mtu mwenye nakala hiyo kuombwa, kukamata mali yoyote ambayo ruhusa imepatikana chini ya aya ya (a) ambayo Kamishna au afisa aliyeruhusiwa ana sababu za msingi za kudhani kwamba inahifadhi waraka kwenye aina yoyote.

Hivyo, TRA haihitaji kukupa taarifa yoyote ya kukuvamia, vinginevyo hakutaitwa kuvamia. Haya ni mamlaka ambayo yameelezwa kwenye sheria na huwezi kuilaumu TRA kwa kuyatekeleza. TRA isingefanya hivi kama isingegundua hali isiyokuwa ya kawaida kwenye shughuli zako. Uvamizi wa namna hii ni wa kawaida hata sehemu nyingine duniani.

Kama utawakatalia TRA, tambua kuwa wanayo mamlaka ya kuwaomba maafisa polisi kuwasaidia kwenye majukumu yao na kukataa huko siyo tu kwamba ni kinyume cha sheria bali pia unaweza kukupelekea kufungwa. Hata hivyo, kama unadai unaendesha “biashara safi” kwa nini upinge hilo?

Kuhusu usiri, sheria zetu za kodi zinaeleza jambo hili kwa ukali sana na afisa yeyote wa TRA ambaye anavujisha taarifa za siri kwa mtu asiyehusika, anaweza kutozwa faini na/au kufungwa. Kama unaamini kwamba umefanyiwa hivyo, unaweza kutoa taarifa kwa Kamishna Mkuu kwa hatua zaidi. Tunakushauri uonane na mshauri wako wa kodi akuongoze zaidi.

## Mamlaka ya Mapato (TRA) na mikataba ya madini

**Nilifurahishwa sana kuona taarifa na matangazo ya hivi karibuni ya TRA juu ya kupitia na kujadiliana upya Mikataba ya Kugawana Uzalishaji (PSAs) na Mikataba ya Maendeleo ya Madini (MDAs). Nilidhani ni wazo zuri, lakini nimebaini TRA imeondoa tangazo hilo siku chache tu baadaye. Ninaamini kwamba nchi haipati thamani halisi ya hisa zake kutoka kwenye mikataba hii. Je, TRA inaweza kujiamulia kuondoa tangazo hilo? Nimeshtushwa sana na kitendo cha TRA kukosa uzalendo kwa kusitisha jambo hili. Ninawezaje kuiwajibisha TRA?**

*15 Septemba 2014*

Hatujui kilichokushtua. TRA ni taasisi ya kodi nchini na siyo mtia saini wa PSAs na MDAs, na wala haitakuwa sehemu yake. Kazi

ya TRA ni kusimamia kodi nchini. Mikataba ya PSAs na MDAs inaingiwa na Serikali kupitia Wizara ya Nishati na Madini. Kwa PSAs kuna mtia saini mwingine ambaye ni Shirika la Maendeleo ya Petroli (TPDC).

Wakati TRA ilipotoa tangazo hilo, moja kwa moja ilikuwa inaingilia kazi ya Wizara ya Nishati na Madini. Inawezekana kuna mtu Wizarani au Serikalini aliwashtua TRA kwamba wanachokifanya ni batili na ndiyo maana waliondoa matangazo husika. Kwa bahati mbaya TRA haikusema ni kwa nini imeondoa matangazo hayo, inawezekana ilikuwa na nia ya kuepusha aibu zaidi.

Wewe umeshtushwa na kuondolewa kwa matangazo. Sisi tuna uhakika wadau wa mafuta na gesi pamoja na jamii ya wachimbaji ilishtushwa na namna TRA, kwa haraka na kutoka kusikoJulaikana, ilivyoamua kutoa tangazo hilo. Uzalendo wako unaweza kuigharimu sana nchi. Hapa chini tutakueleza kwa nini.

Tanzania ni mtia saini wa mikataba mbali mbali ya kimatafa ambayo inalinda wawekezaji dhidi ya ubinafsishaji na utaifishaji. Kimsingi, kuna sheria ya ndani, Sheria ya Uwekezaji ambayo inaeleza kwa uwazi kwenye kifungu cha 22 kwamba (1) Kwa kuzingatia kifungu kidogo cha (2) na (3) cha kifungu hiki (a) hakuna biashara itakayotaifishwa ama kuchukuliwa na Serikali, na (b) hakuna mtu anayemiliki, wote au sehemu ya mtaji wa biashara yoyote, atalazimishwa na sheria kukabidhi mali/maslahi yake kwenye mtaji kwa mtu mwingine yeyote. (2) Hakutakuwa na utaifishaji, bila kujali biashara yote au sehemu ya biashara mahali ambapo sheria hii itatumika na Serikali isipokuwa kama utaifishaji huo utafuata taratibu za kisheria ambayo zitakuwa na vifungu vya (a) malipo ya fidia kwa haki, utoshelevu na ya haraka, na (b) haki ya kwenda/kuzifikia Mahakama au haki ya usuluhishi kwa ajili ya maamuzi ya maslahi au haki za mwekezaji na kiasi cha fidia anachostahili. (3) Fidia yoyote inayostahili kulipwa chini ya kifungu hiki italipwa kwa haraka na ruhusa ya kubadilisha kwenda fedha inayobadilishika, kama inahusika, itatolewa.

Maamuzi ya upande mmoja ya kubadilisha PSAs au MDAs ni utaifishaji au ni jaribio lisilo la moja kwa moja la kutaifisha makampuni hayo. Mikataba mingi, kama siyo yote, huwa na vipengele vya usuluhishi na juhudi za TRA, au taasisi nyingine ya Serikali, kujiamulia kubadilisha mikataba kutazua mgogoro wa usuluhishi ambao unaweza kuamuliwa dhidi ya Serikali panapo usuluhishi wa kimataifa.

Iwapo Serikali itaamua kujadiliana upya juu ya mikataba hii, basi kanuni za sheria ya mikataba zitahusika, na kwamba majadiliano hayo ni lazima yafanywe kwa makubaliano, na kama makampuni hayo yatakataa kujadiliana upya au kurekebisha masharti yoyote, kitu ambacho yanaweza kukifanya, basi hayatalazimishwa kufanya majadiliano au marekebisho hayo. Pamoja na jambo hili kuleta mgogoro wa kiusuluhishi, kama makampuni hayo yatalazimishwa kufanya chochote, itachimba shimo jeusi kwenye ndoto za Tanzania kuwa kitovu cha uwekezaji.

Kwa kuzingatia swali lako, TRA ina mamlaka yote ya kuliondoa tangazo hilo, jambo ambalo tunaona ni ukomavu na ujasiri mkubwa. Iwapo unaweza kufanya chochote kwa sababu TRA imeondoa tangazo hilo, jibu ni hapana. Huna haki yoyote ya kuishtaki TRA juu ya hili na uzalendo wako ni lazima uendane na uhalisia kwa kuzingatia sheria.

## Bodi ya kodi kama mpatanishi

**Nina kesi dhidi ya TRA kwenye Bodi ya Rufaa za Kodi ("Bodi"). Tarehe ya mwisho tuliyokwenda mbele ya Bodi, mmoja wa mashahidi wetu muhimu, ambaye ni**

**mfanyakazi wa zamani wa TRA, alikataa kuja kutoa ushahidi. Wakati wa kuahirisha suala hili, Bodi ilishauri kwamba mlipa kodi akae na TRA kujaribu kutatua tofauti zao. Je, huu ni utaratibu wa kawaida?**

*22 Septemba 2014*

Chini ya kifungu cha 17, Sheria ya Rufaa za Kodi kinasema kwamba Bodi ina uwezo wa kupatanisha. Upatanishi ni njia mbadala yenye nguvu katika utatuzi wa migogoro na hutumika sana. Kifungu cha 17 kinasema (1) Bodi na Baraza vitakuwa na mamlaka (a) kuchukua ushahidi kwa kiapo; (b) kutatua malalamiko yoyote au rufaa kwa maelewano, upatanisho au usuluhishi; (c) kutoa hati za ukamataji kwa kushindwa kutii wito; (d) kuagiza malipo ya gharama kuhusiana na suala lolote lililopelekwa kwenye Bodi au Baraza; (e) kufuta jambo lolote mbele yake; (f) kuahirisha kusikilizwa kwa kesi yoyote mbele yake. (2) Bila kujali kifungu kidogo cha (1), Bodi au Baraza litakuwa na mamlaka ya kumuita na kumsikiliza shahidi yeyote na kupokea ushahidi kwa namna sawa na Mahakama ya kawaida inaposikiliza kesi za madai na vifungu vya Sheria ya Mwenendo wa Kesi za Madai, zinazohusiana na kuita mashahidi, kuchukua ushahidi kwa njia ya kiapo, na kukataa wito kwa mashahid vitatumika kuhusiana na rufaa mbele ya Bodi lakini Baraza linaweza kukataa kupokea ushahidi wowote mpya isipokuwa katika hali ambayo Mahakama Kuu ingeweza kupokea ushahidi mpya juu ya rufaa ya kwanza katika kesi ya madai.

Unaweza pia kupeleka maombi mbele ya Bodi ya kumwita shahidi afike na kama hatoweza kufanya hivyo, anaweza kukamatwa na kupelekwa mbele ya Bodi.

## Kudai nyaraka za kodi

**Kampuni yetu iliingia kwenye mkataba wa kubadili umiliki mwaka 2010, baada ya hapo tulifanyiwa ukaguzi wa mahesabu na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) mwaka 2012. Nyaraka za mkataba huo zilikabidhiwa kwa timu ya ukaguzi wa mahesabu ya TRA. Miezi miwili iliyopita tuliambiwa kurejesha/kuwapatia nyaraka zile zile tena. Je, kanuni ya kutunza nyaraka miaka mitatu haitumiki hapa nchini, na je, TRA haiko nje ya muda kuleta ombi hilo?**

*10 Novemba 2014*

Kwa kiasi fulani uko sahihi kwamba kuna kikomo cha muda, lakini ni kwa miaka isiyopungua mitano na sio mitatu. Kifungu cha 80 cha Sheria ya Kodi ya Mapato kinasimamia suala hili na kinasema kwamba, isipokuwa kama imeidhinishwa na Kamishna kwa maandishi, kila mtu anayetakiwa kulipa kodi chini ya Sheria hii atatunza katika Jamuhuri ya Muungano nyaraka (a) ambazo zitakuwa ni muhimu katika kuelezea taarifa zitakazotolewa kwenye marejesho au katika waraka mwingine wowote utakaopelekwa kwa Kamishna chini ya Sheria hii; (b) ambazo zitakuwa ni muhimu katika kutoa maamuzi sahihi ya kodi inayolipwa na mtu; na (c) kama itakavyoelekezwa na Kamishna. (2) Nyaraka zilizotajwa katika kifungu hiki zitahifadhiwa kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia mwisho wa mwaka wa mapato au miaka ya mapato husika isipokuwa kama Kamishna, kwa maandishi, ataelekeza vinginevyo. Hivyo, TRA haipo nje ya muda na labda kama kuna taarifa nyingine hujatueleza, tunapendekeza utoe ushirikiano na uwapatie nyaraka hizo.

## Mamlaka ya Mapato (TRA) inadai haisimamii sheria ya utafutaji na uzalishaji petroli (PEPA)

**Tuna mgogoro na TRA kuhusu msamaha tuliopewa chini ya Mkataba wa Kugawana Uzalishaji (PSA), na TRA inasema kwamba hilo siyo mojawapo ya mambo wanayoyasimamia na hivyo haiwezi kutoa**

**msamaha. Tufanye nini?**

*17 Novemba 2014*

Ni kweli kwamba PEPA siyo moja ya sheria inayosimamiwa na TRA. Kwa namna yoyote, TRA haitoi msamaha bali Wizara ya Fedha.

Vile vile, PSA ni mkataba ambao Serikali imeingia na unaibana Serikali, bila kujali TRA inautambua au la. Tunakushauri uwasiliane na Wizara ya Nishati na Madini kupitia TPDC na kama suala hili halijatatuliwa unaweza kutumia ama kipengele cha usuluhishi kilichopo kwenye PSA au kupeleka maombi kwenye Mahakama za ndani, kutegemea na kipengele cha utatuzi wa mgogoro kilichopo kwenye PSA. Hili ni tatizo linalojirudiarudia na moja ya makampuni ya mafuta na gesi inataka kuona jambo hili linapatiwa ufumbuzi wa kudumu kwani ni chanzo cha utata.

## Shahidi kufika kwenye mahakama ya kodi

**Kama nimeitwa kuwa shahidi kwenye kesi iliyopo kwenye Bodi ya Rufaa za Kodi, hivi sistahili kulipwa chochote, walau kifungua kinywa? Kwa nini nifanye hivyo bure? Je, ninalazimishwa kwenda?**

*29 Desemba 2014*

Sheria ya Rufaa za Kodi ina kifungu maalum juu ya jambo hili na inaeleza kwenye kifungu cha 2 kwamba (1) Bodi au Baraza linaweza kumuita mtu yeyote kufika siku iliyopanga kusikiliza shauri ili kutoa ushahidi ikiwemo kutoa waraka wowote ambao Bodi au Baraza linaamini ushahidi huo utalisaidia kwenye maamuzi yake. (2) Mtu yeyote aliyeitwa kuhudhuria na kutoa ushahidi kwenye Bodi au Baraza atalipwa posho na gharama kwa viwango vilivyowekwa na Bodi au Baraza.

Kifungu hicho kinaonesha wazi kwamba unastahili posho na gharama, lakini kwa viwango vilivyowekwa na Bodi. Kwa uelewa wetu, viwango hivyo bado havijachapishwa lakini hiyo haimaanishi kwamba hautafidiwa. Kuhusu iwapo unalazimika kwenda au la, mara suala la malipo linapokuwa limetatuliwa, tunaamini ni lazima uende.

# Kuhusu Kitabu

Maswali & Majibu na FB Attorneys ni mkusanyiko wa majibu ya maswali ya kisheria yaliyotumwa na masomaji wa safu yetu katika Gazeti la Daily News, ambalo ni moja kati ya Magazeti ya Kiingereza yanayosomwa zaidi nchini Tanzania. Toleo hili la pili linajumuisha maswali kutoka mwaka 2012 hadi 2014. Maswali husika yamechaguliwa na kuhakikiwa kwa umakini mkubwa. Kitabu hiki kimebeba maswali na mada kedekede zenye kuvutia katika nyanja kama vile Migogoro ya Biashara, Sheria ya Uhamiaji, Mali isiyohamishika (Ardhi na Majengo), Sheria ya Madini, Uhalifu wa Kibiashara/Makampuni, Sheria ya Mazingira, Sheria ya Ushuru/Kodi na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA). Waandishi wameandaa majibu husika kwa uangalifu mkubwa katika mtizamo wa kitaalam na kisheria.

ISBN 978-9976-5241-2-3

fbattorneys.co.tz

ISBN 978-9976-5241-2-3
9 789976 524123

FB ATTORNEYS